# AGANO JIPYA

FAHIRISI **(Bonyeza juu ya Sura utakayo. Jina la Kitabu ni sawa na Sura 1)**


Mathayo 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28

Marko 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16

Luka 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24

Yohana 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21

Matendo 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28

Warumi 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16

1 Wakorintho 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16

2 Wakorintho 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13

Wagalatia 2 3 4 5 6

Waefeso 2 3 4 5 6

Wafilipi 2 3 4

Wakolosai 2 3 4

1 Wathesalonike 2 3 4 5

2 Wathesalonike 2 3

1 Timotheo 2 3 4 5 6

2 Timotheo 2 3 4

Tito 2 3

Filemoni

Waebrania 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13

Yakobo 2 3 4 5

1 Petro 2 3 4 5

2 Petro 2 3

1 Yohana 2 3 4 5

2 Yohana

3 Yohana

Yuda

Ufunuo 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22

# MATHAYO

## *Utangulizi*

Mathayo alikuwa mtoza ushuru ambaye Bwana Yesu alimwita awe mwanafunzi wake mwanzoni kabisa wa huduma yake ya hadharani. Kwa hiyo mambo mengi anayoyaelezea aliyashuhudia kwa macho yake mwenyewe. Anaanza kwa kueleza kwa kirefu kuhusu kuzaliwa kwa Yesu na Bikira Maria, kubatizwa kwake na kujaribiwa kwake nyikani. Yesu alikuja akihubiri juu ya Ufalme wa Mungu ambao ni wa kila mtu anayetaka kupata uzima wa milele. Mtu anaingia katika Ufalme huu kwa kutubu dhambi na kumwamini Yesu. Mathayo ameyagawa mafundisho ya Yesu katika sehemu kubwa tano: Maadili, Kueneza Habari Njema, Mifano, Ushirika na kuja kwa Ufalme wa Mungu. Sehemu ya Mwisho ya Injili ya Mathayo inaeleza juu ya kufa na kufufuka kwa Yesu, na agizo alilotoa kwa wote wanaomwamini kueneza Habari Njema ulimwenguni kote.

## *Wazo Kuu*

Shabaha kuu ya Mathayo katika kuandika Injili hii, ilikuwa ni kuonyesha kwamba Bwana Yesu anakamilisha ahadi aliyoitoa Mungu katika Agano la Kale. Kwa sababu hii, Bwana Yesu anatambulishwa kuwa ni mwana wa Mfalme Daudi na pia mzao wa Abrahamu *(1:1).* Kadhalika Mathayo anatumia mifano mingi kutoka katika unabii uliotolewa na manabii wa Agano la Kale, kueleza maisha ya Bwana Yesu ambaye alikuja kuwa Mwokozi wa Wayahudi *(1:21),* wa watu Mataifa mengine *(4:13-16)* na hatimaye Mwokozi wa ulimwengu wote *(28:19).* Maadili yawapasayo watu wanaoingia katika Ufalme wa Mungu yanaelezwa katika Mahubiri ya Mlimani *(Sura 5-7),* ambapo wana wa Mungu wanaagizwa kukataa kufuata maadili ya dunia hii na kutafuta kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake, ndipo hayo mengineyo watakapozidishiwa*. (6:33).*

## Mgawanyo

1 Maisha na huduma ya Bwana Yesu (1:1-4:25)
2 Mahubiri ya Mlimani (5:1-7:29)
3 Mafundisho, Mifano na Mazungumzo (8:1-18:35)
4 Safari ya kwenda Yerusalemu na maonyo ya mwisho (19:1-23:39)
5 Unabii kuhusu mambo yajayo (24:1-25:46)
6 Kufa na kufufuka kwa Bwana Yesu (26:1-28:20).

### *Ukoo Wa Yesu Kristo*

**1** Habari za ukoo wa Yesu Kristo mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu:

2Abrahamu akamzaa Isaki,
Isaki akamzaa Yakobo,
Yakobo akamzaa Yuda na ndugu zake.
3Yuda akamzaa Peresi na Zera
ambao mama yao alikuwa Tamari.
Peresi akamzaa Esroni,
Esroni akamzaa Aramu,
4Aramu akamzaa Aminadabu,
Aminadabu akamzaa Nashoni,
Nashoni akamzaa Salmoni,
5Salmoni akamzaa Boazi
na mama yake Salmoni
alikuwa Rahabu.
Boazi akamzaa Obedi,
ambaye mama yake alikuwa Ruthi.
Obedi akamzaa Yese,
6Yese akamzaa Daudi
ambaye alikuwa mfalme.

Daudi akamzaa Solomoni ambaye
mama yake ni yule aliyekuwa mke
wa Uria.
7Solomoni akamzaa Rehoboamu,
Rehoboamu akamzaa Abiya,
Abiya akamzaa Asa,
8Asa akamzaa Yehoshafati,
Yehoshafati akamzaa Yoramu
[a], Yoramu akamzaa Uzia,
9Uzia akamzaa Yothamu,
Yothamu akamzaa Ahazi,
Ahazi akamzaa Hezekia,
10Hezekia akamzaa Manase,
Manase akamzaa Amoni,
Amoni akamzaa Yosia,
11wakati wa uhamisho wa Babeli, Yosia
alimzaa Yekonia na ndugu zake.

12Na baada ya uhamisho wa Babeli,
Yekonia alimzaa Shealtieli,
Shealtieli akamzaa Zerubabeli,
13Zerubabeli akamzaa Abiudi,
Abiudi akamzaa Eliakimu,
Eliakimu akamzaa Azori,
14Azori akamzaa Zadoki,
Zadoki akamzaa Akimu,
Akimu akamzaa Eliudi,
15Eliudi akamzaa Eliezari,
Eliezari akamzaa Matani,
Matani akamzaa Yakobo,

[a][8] Yoramu ndiye Yehoramu

16Yakobo akamzaa Yosefu ambaye
alikuwa mumewe Maria,
mama yake Yesu, aitwaye Kristo [b].

17Hivyo, kulikuwapo na jumla ya vizazi kumi
na vinne tangu Abrahamu mpaka Daudi, vizazi
kumi na vinne tangu Daudi hadi wakati wa
uhamisho wa Babeli na vizazi kumi na vinne
tangu wakati wa uhamisho wa Babeli hadi
Kristo.

### *Kuzaliwa Kwa Yesu Kristo*

18Basi Kuzaliwa kwake Yesu Kristo
kulikuwa hivi: Maria mama yake alikuwa
ameposwa na Yosefu, lakini kabla
hawajakutana kimwili, Maria alionekana ana
mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. 19Kwa
kuwa Yosefu, mwanaume aliyekuwa amemposa
alikuwa mtu mwadilifu, hakutaka kumwaibisha
Maria hadharani, aliazimu kumwacha kwa siri.

20Lakini mara alipoazimu kufanya jambo
hili, malaika wa Bwana akamtokea katika ndoto
na kusema., “Yosefu mwana wa Daudi,
usiogope kumchukua Maria awe mke wako,
kwa maana mimba aliyo nayo ni kwa uweza wa
Roho Mtakatifu. 21Naye atamzaa mwana , nawe
utamwita jina lake Yesu, kwa maana yeye ndiye
atakayewaokoa watu wake kutoka katika
dhambi zao.”

22Haya yote yametukia ili kutimiza lile
Bwana alilokuwa amenena kupitia nabii,
akisema: 23“Tazama, bikira atachukua mimba,
naye atamzaa mwana, nao watamwita jina lake
Imanueli,’’ maana yake, “Mungu pamoja nasi.’’

24Yosefu alipoamka kutoka usingizini,
akafanya kama vile alivyoagizwa na malaika wa
Bwana, akamchukua Maria kuwa mke wake
25Lakini hawakukutana kimwili mpaka Maria
alipojifungua mwanawe kifungua mimba
akamwita jina lake Yesu.

### *Wataalamu Wa Nyota Wafika Kumwona Mtoto Yesu*

**2** Baada ya Yesu kuzaliwa katika mji wa
Bethlehemu huko Uyahudi, wakati wa utawala
wa mfalme Herode, wataalamu wa mambo ya
nyota kutoka Mashariki walifika Yerusalemu
2wakiuliza, “Yuko wapi huyo aliyezaliwa mfalme
wa Wayahudi? Kwa maana tumeona nyota yake
ikitokea mashariki, nasi
tumekuja kumwabudu.’’

[b][16] Kristo maana yake Masiya, yaani, Mpakwa (aliyetiwa)Mafuta

3Mfalme Herode aliposikia jambo hili aliingiwa na hofu sana pamoja na watu wote wa Yerusalemu. 4Herode akawaita pamoja makuhani wakuu na waandishi wa watu, akawauliza ni mahali gani ambapo Kristo angezaliwa. 5Nao wakamwambia, "Katika Uyahudi, kwa maana hivyo ndivyo ilivyoandikwa na nabii:

6 ' "Nawe, Bethlehemu, katika nchi ya Yuda,
wewe si mdogo miongoni mwa
watawala wa Yuda,
kwa maana kutoka kwako atakuja mtawala
atakayekuwa mchungaji wa watu
wangu Israeli.' "

7Ndipo Herode akawaita wale wataalamu wa nyota kwa siri na kutaka kujua kutoka kwao uhakika kamili wa wakati ile nyota ilipoonekana. 8Kisha akawatuma waende Bethlehemu akiwaambia, "Nendeni mkamtafute kwa bidii huyo mtoto. Nanyi mara mumwonapo, mniletee habari ili na mimi niweze kwenda kumwabudu."

9Baada ya kumsikia mfalme, wale wataalamu wa nyota wakaenda zao, nayo ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, nao wakaifuata mpaka iliposimama mahali pale alipokuwa mtoto. 10Walipoiona ile nyota wakajawa na furaha kubwa mno. 11Walipoingia ndani ya ile nyumba, wakamwona mtoto pamoja na Maria mama yake, wakamsujudu na kumwabudu yule mtoto Yesu. Ndipo wakafungua hazina zao, wakamtolea zawadi za dhahabu, uvumba na manemane. 12Nao wakiisha kuonywa katika ndoto wasirudi kwa Herode, wakarudi kwenda katika nchi yao kwa njia nyingine.

### *Yosefu, Maria Na Mtoto Yesu Wakimbilia Misri*

13Walipokwisha kwenda zao, malaika wa Bwana akamtokea Yosefu katika ndoto akamwambia, "Ondoka, mchukue mtoto na mama yake mkimbilie Misri. Kaeni huko mpaka nitakapowaambia, kwa maana Herode anataka kumtafuta huyu mtoto ili amwue."

14 Kisha Yosefu akaondoka, akamchukua mtoto na mama wakati wa usiku, nao wakaenda Misri 15ambako walikaa mpaka Herode alipokufa. Hili lilikuwa, ili litimie lile lililonenwa na Bwana kwa kinywa cha nabii kusema, "Kutoka Misri nilimwita mwanangu"

16Herode alipong'amua kwamba wale wataalamu wa nyota wamemshinda kwa akili, alikasirika sana, naye akatoa amri ya kuwaua watoto wote wa kiume wenye umri wa miaka miwili kurudi chini katika mji wa Bethlehemu na sehemu zote za jirani, kufuatana na ule muda alioambiwa na wale wataalamu wa nyota. 17Ndipo lile lililonenwa na nabii Yeremia lilipotimia.

18 "Sauti ilisikika huko Rama,
kilio cha huzuni na maombolezo
makuu, Raheli akilia kwa ajili ya wanawe,
akikataa kufarijiwa, kwa
sababu hawako tena."

### *Kurudi Kutoka Misri*

19Baada ya Herode kufa, malaika wa Bwana akamtokea Yosefu katika ndoto huko Misri 20na kusema, "Ondoka, mchukue mtoto na mama mwende, mrudi katika nchi ya Israeli kwa sababu wale waliokuwa wanatafuta uhai wa mtoto wamekufa.

21 Basi Yosefu, akaondoka akamchukua mtoto na mama yake wakaenda mpaka nchi ya Israeli. 22Lakini aliposikia kwamba Arkelao alikuwa anatawala huko Uyahudi mahali pa Herode baba yake, aliogopa kwenda huko. Naye akiisha kuonywa katika ndoto, akaenda zake sehemu za Galilaya, 23akaenda, akaishi katika mji ulioitwa Nazareti, hivyo likawa limetimia lile lililonenwa na manabii, "Ataitwa Mnazarayo."

### *Yohana Mbatizaji Atayarisha Njia*

**3** Siku hizo Yohana Mbatizaji alikuja akihubiri katika nyika ya Uyahudi, akisema, 2"Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni u karibu." 3Huyu ndiye yule aliyenenwa habari zake na nabii Isaya aliposema,

"Sauti ya mtu yule aliaye huko nyikani,
'Tayarisheni njia kwa ajili ya Bwana,
yanyosheni mapito yake.' "

4Basi Yohana alivaa vazi lililotengenezwa kwa singa za ngamia akiwa na mkanda wa ngozi kiunoni mwake, chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. 5Watu walimwendea kutoka Yerusalemu, Uyahudi yote na nchi zote za kando kando ya mto Yordani. 6Nao wakaziungama dhambi zao, akawabatiza katika Mto Yordani.

7Lakini alipowaona Mafarisayo na

Masadukayo wengi wakija ili kubatizwa, aliwaambia, ‘‘Ninyi watoto wa nyoka! Ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu inayokuja? [8]Basi zaeni matunda yastahiliyo toba. [9]Wala msijidhanie mnaweza kujiambia, ‘Sisi tunaye Abrahamu, baba yetu, kwa maana nawaambia kuwa Mungu anaweza kumuinulia Abrahamu watoto kutoka katika mawe haya. [10]Hata sasa shoka limekwisha kuwekwa tayari kwenye mizizi ya mti. Kila mti usiozaa matunda mazuri, hukatwa na kutupwa motoni.

[11]“Mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba. Lakini nyuma yangu anakuja Yeye aliye na uwezo kuliko mimi, ambaye sistahili hata kuchukua viatu vyake. Yeye atawabatiza kwa [a] Roho Mtakatifu na kwa moto. [12]Chombo chake cha kupuria kiko mkononi mwake, naye atasafisha sakafu yake ya kupuria, akiikusanya ngano yake ghalani na kuyachoma makapi kwa moto usiozimika.”

### *Yesu Abatizwa*

[13]Kisha Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka mto Yordani ili Yohana ambatize. [14] Lakini Yohana akajitahidi kumzuia, akimwambia, “Mimi ninahitaji kubatizwa na Wewe, nawe waja kwangu nikubatize?’’

[15]Lakini Yesu akamjibu, “Kubali hivi sasa, kwa maana ndivyo itupasavyo kwa njia hii kuitimiza haki yote.’’ Hivyo Yohana akakubali.

[16]Naye Yesu alipokwisha kubatizwa, mara alipotoka ndani ya maji, ghafula mbingu zikamfungukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua na kutulia juu yake. [17]Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye.’’

### *Kujaribiwa Kwa Yesu*

**4** Kisha Yesu akaongozwa na Roho Mtakatifu kuingia nyikani ili akajaribiwe na Ibilisi. [2]Baada ya kufunga siku arobaini mchana na usiku, hatimaye akaona njaa. [3]Mjaribu akamjia na kumwambia, “Kama Wewe ndiye Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate.’’

[4]Lakini Yesu akajibu, “Imeandikwa, ‘Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’ ”

[5]Ndipo ibilisi akamchukua Yesu mpaka mji mtakatifu wa Yerusalemu na kumweka juu ya mnara mrefu mwembamba wa hekalu, [6]akamwambia, “Kama Wewe ndiye Mwana wa Mungu jitupe chini, kwa kuwa imeandikwa,

‘ “Atakuagizia malaika zake,
nao watakuchukua mikononi mwao
ili usije ukajikwaa mguu wako kwenye
jiwe.’ ”

[7]Yesu akamjibu, “Pia imeandikwa: ‘Usimjaribu Bwana Mungu wako.’ ”

[8]Kwa mara nyingine, ibilisi akamchukua Yesu mpaka kwenye kilele cha mlima mrefu na kumwonyesha falme zote za dunia na fahari zake, [9]kisha akamwambia, “Nitakupa hivi vyote kama ukinisujudia na kuniabudu.’’

[10]Yesu akamwambia, “Ondoka mbele yangu, Shetani! Kwa maana imeandikwa, ‘Utamwabudu Bwana Mungu wako, nawe utamtumikia Yeye peke yake.’ ”

[11]Ndipo ibilisi akamwacha, nao malaika wakaja na kumtumikia.

### *Yesu Aanza Kuhubiri*

[12]Yesu aliposikia kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa ametiwa gerezani, alirudi Galilaya. [13]Akaondoka Nazareti akaenda kuishi Kapernaumu ulioko karibu na bahari, katika mipaka ya nchi ya Zabuloni na ya Naftali, [14]ili kutimiza unabii wa nabii Isaya, kama alivyosema:

[15]“Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali,
kwenye njia ya kuelekea baharini,
ng'ambo ya Yordani,
Galilaya ya watu Mataifa,
[16]watu wale waliokaa gizani
wameona nuru kuu
nao wale waliokaa katika nchi ya uvuli
wa mauti,
nuru imewazukia.’’

[17]Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri akisema: “Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia.’’

### *Yesu Awaita Wanafunzi Wake wa Kwanza*

[18]Wakati Yesu alipokuwa anatembea kando ya bahari ya Galilaya aliwaona ndugu wawili, Simoni aitwaye Petro na Andrea ndugu yake. Walikuwa wakizitupa nyavu zao baharini kwa maana wao walikuwa wavuvi. [19]Yesu akawaambia, “Njooni, nifuateni, nami nitawafanya muwe wavuvi wa watu.’’ [20]Mara

[a][11] “Kwa” hapa ina maana “ndani ya, katika

wakaziacha nyavu zao, wakamfuata.
21 Alipoendelea mbele kutoka pale,
akawaona ndugu wengine wawili, Yakobo
mwana wa Zebedayo na Yohana nduguye,
wakiwa wamekaa kwenye mashua pamoja na
baba yao Zebedayo wakiziandaa nyavu zao.
Yesu akawaita. 22 Nao mara wakaziacha nyavu
zao, pamoja na baba yao, wakamfuata.

### *Yesu Ahubiri Na Kuponya Wagonjwa*

23 Yesu akapita katika Galilaya yote,
akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri
Habari Njema za Ufalme wa Mungu, akiponya
kila ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni
mwa watu.. 24 Kwa hiyo sifa zake zikaenea
sehemu zote za Shamu, nao watu wakamletea
wote waliokuwa na magonjwa mbalimbali na
maumivu, waliopagawa na pepo, wenye kifafa
na waliopooza, naye akawaponya. 25 Makutano
makubwa ya watu yakawa yanamjia kutoka
Galilaya, Dekapoli, Yerusalemu, Uyahudi na
kutoka ng'ambo ya Mto Yordani.

### *Sifa za Aliyebariki*

**5** Basi Yesu alipoona makutano, alipanda
mlimani akaketi chini, nao wanafunzi
wake wakamjia. 2 Ndipo akaanza kuwafundisha,
akisema:

3 "Wana heri walio masikini wa roho, maana
hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.
4 Wana heri wale wanaohuzunika,
maana hao watafarijiwa.
5 Wana heri walio wapole,
maana hao watairithi nchi.
6 Wana heri wenye njaa na kiu ya
haki, maana hao watatoshelezwa.
7 Wana heri wenye huruma,
maana hao watapata rehema.
8 Wana heri walio na moyo safi,
maana hao watamwona Mungu.
9 Wana heri walio wapatanishi,
maana hao wataitwa wana wa Mungu.
10 Wana heri wanaoteswa kwa sababu ya
haki, maana hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.

11 Mna heri ninyi watu watakapowashutumu
na kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya ya
aina zote kwa uongo kwa ajili yangu. 12 Furahini
na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kuu.

### *Chumvi na Nuru*

13 "Ninyi ni chumvi ya ulimwengu. Lakini
chumvi ikipoteza ladha yake, yawezaje
kurudishiwa ladha yake tena ? Haifai tena kwa
kitu cho chote, ila kutupwa nje ikanyagwe na
watu.
14 "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliojengwa
kilimani hauwezi kufichika. 15 Wala watu
hawawashi taa na kuifunika kwa bakuli. Badala
yake, huiweka kwenye kinara chake, nayo hutoa
mwanga kwa kila mtu aliyemo ndani ya ile
nyumba. 16 Vivyo hivyo, nuru yenu iangaze mbele
ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema
wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.

### *Kutimiza Sheria*

17 "Msidhani kwamba nimekuja kuondoa
Torati au Manabii, sikuja kuondoa bali kutimiza.
18 Kwa maana,amin, nawaambia, mpaka mbingu
na dunia zitakapopita, hakuna hata herufi moja
ndogo wala nukta itakayopotea kwa namna yo
yote kutoka kwenye Torati mpaka kila kitu kiwe
kimetimia. 19 Kwa hiyo, ye yote atakayevunja
mojawapo ya amri ndogo kuliko zote ya amri
hizi, naye akawafundisha wengine kufanya
hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika Ufalme wa
Mbinguni, lakini ye yote azitendaye na
kuzifundisha hizi amri ataitwa mkuu katika
Ufalme ya Mbinguni. 20 Kwa maana nawaambia,
haki yenu isipozidi haki ya waandishi wa sheria
na Mafarisayo, kamwe hamtaingia katika
Ufalme wa Mbinguni.

### *Kuhusu Hasira*

21 "Mmesikia walivyoambiwa watu wa
zamani kwamba, 'Usiue, ye yote atakayeua
atapasiwa hukumu.' 22 Lakini mimi nawaambia
kwamba, ye yote atakayemkasirikia ndugu yake
wa kiume au wa kike, atapasiwa hukumu. Tena,
ye yote atakayemwambia ndugu yake wa kiume
au wa kike, 'Raca' [a] , yaani kumdharau na
kumdhihaki, atapasiwa kufanyiwa baraza. Lakini
ye yote atakayesema 'We mpumbavu ulaaniwe!'
Atapasiwa hukumu ya moto wa jehanam.
23 "Kwa hiyo, kama unatoa sadaka yako
madhabahuni, ukakumbuka kuwa ndugu yako
ana kitu dhidi yako, 24 iache sadaka yako hapo
hapo, mbele ya madhabahu, uende kwanza

[a] 22 'Raca' ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni dharau na dhihaka ya hali ya juu.

ukapatane na ndugu yako wa kiume au wa kike,
kisha urudi na ukatoe sadaka yako.

**25**“Patana na mshtaki wako upesi wakati
uwapo njiani pamoja naye kwenda
mahakamani, ili mshtaki wako asije akakutia
mikononi mwa hakimu, naye hakimu akakutia
mikononi mwa walinzi, nawe ukatupwa
gerezani. **26**Amin, nakuambia, hutatoka humo
mpaka umelipa hadi senti ya mwisho”

***Kuhusu Uzinzi***

**27**“Mmesikia kwamba ilinenwa, ‘Usizini'.
**28**Lakini mimi nawaambia: kwamba ye yote
amtazamaye mwanamke kwa kumtamani,
amekwisha kuzini naye moyoni mwake. **29**Jicho
lako la kuume likikufanya utende dhambi, ling'oe
ulitupe mbali. Ni afadhali kwako kupoteza
kiungo kimoja cha mwili wako kuliko mwili wako
mzima utupwe jehanam. **30**Kama mkono wako
wa kuume ukikufanya utende dhambi, ukate
uutupe mbali. Ni afadhali kwako kupoteza
kiungo kimoja cha mwili wako kuliko mwili wako
mzima utupwe jehanam.

***Kuhusu Talaka***

**31**“Pia ilinenwa kwamba, ‘Mtu ye yote
amwachaye mkewe na ampe hati ya talaka.’
**32**Lakini mimi nawaambia, ye yote amwachaye
mkewe isipokuwa kwa kosa la uasherati,
amfanya mkewe kuwa mzinzi. Na ye yote
amwoaye yule mwanamke aliyeachwa azini.”

***Kuhusu Kuapa***

**33**“Tena mmesikia walivyoambiwa watu wa
zamani kwamba, ‘Usiape kwa uongo, bali
timizeni, nadhiri zile ulizofanya kwa Bwana’
**34**Lakini mimi nawaambia,”Msiape kabisa, ama
kwa mbingu, kwa kuwa ni kiti cha enzi cha
Mungu, **35**au kwa nchi, kwa kuwa ndipo mahali
pake pa kuwekea miguu, au kwa Yerusalemu,
kwa kuwa ndio mji wa Mfalme Mkuu. **36**Nanyi
msiape kwa vichwa vyenu kwa kuwa hamwezi
kuufanya hata unywele mmoja kuwa mweupe
au mweusi. **37**‘Ndiyo,’ yenu iwe ‘Ndiyo’ na
‘Hapana’, yenu iwe ‘Hapana.’ Lo lote zaidi ya hili
latoka kwa yule mwovu.”

***Kuhusu Kulipiza Kisasi***

**38**“Mmesikia kwamba ilinenwa, ‘Jicho kwa
jicho na jino kwa jino.’ **39**Lakini mimi nawaambia,
msishindane na mtu mwovu. Lakini kama mtu
akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie na la
pili pia, **40**Kama mtu akitaka kukushtaki na
kuchukua shati lako, mwachie achukue na koti
pia. **41**Kama mtu akikulazimisha kwenda
kilometa moja, nenda naye kilometa mbili.
**42**Mpe yeye akuombaye, wala usimgeuzie
kisogo yeye atakaye kukukopa.”

***Upendo Kwa Adui***

**43**“Mmesikia kwamba ilinenwa, ‘Mpende
jirani yako na umchukie adui yako.’ **44**Lakini
mimi ninawaambia : Wapendeni adui zenu na
waombeeni wanaowatesa ninyi, **45**ili mpate
kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa
maana Yeye huwaangazia jua lake watu waovu
na watu wema, naye huwanyeshea mvua
wenye haki na wasio haki. **46**Kama mkiwapenda
wale wanaowapenda tu, mtapata thawabu gani?
Je, hata watoza ushuru hawafanyi hivyo?
**47**Nanyi kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je,
mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata watu
wasiomjua Mungu, hawafanyi hivyo? **48**Kwa
hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa
mbinguni alivyo mkamilifu.”

***Kuwapa Wahitaji***

**6** “Angalieni msitende wema wenu mbele ya watu
ili wawaone. Kwa maana mkifanya hivyo, hamna
thawabu kutoka kwa Baba yenu
aliye mbinguni.

**2**“Hivyo mnapowapa wahitaji, msipige
panda mbele yenu kama wafanyavyo wanafiki
katika masinagogi na mitaani, ili wasifiwe na
watu. Amin, amin nawaambia wao wamekwisha
kupokea thawabu yao. **3**Lakini ninyi mtoapo
sadaka, fanyeni kwa siri, hata mkono wako wa
kushoto usijue mkono wako wa kuume
unachofanya, **4**ili sadaka yako iwe ni siri. Ndipo
Baba yako wa mbinguni, Yeye aonaye sirini
atakupa thawabu kwa wazi.

***Kuhusu Maombi***

**5**“Nanyi msalipo, msiwe kama wanafiki,
maana wao hupenda kusali wakiwa
wamesimama katika masinagogi na kando ya
barabara ili waonekane na watu. Amin, amin
nawaambieni, wao wamekwisha kupata
thawabu yao. **6**Lakini wewe unaposali, ingia
chumbani mwako, funga mlango na umwombe
Baba yako aliye sirini. Naye Baba yako aonaye
sirini atakupa thawabu yako. **7**“Nanyi mnaposali
msiseme maneno kama wafanyavyo watu
wasiomjua Mungu. Kwa maana wao hudhani
kwamba watasikiwa kwa sababu ya wingi wa
maneno yao. **8**Msiwe kama wao, kwa sababu

Baba yenu anajua kile mnachohitaji kabla hamjamwomba.''

9''Hivi basi, ndivyo iwapasavyo kuomba :

"Baba yetu uliye mbinguni,
Jina lako litukuzwe.
10Ufalme wako uje.
Mapenzi yako yafanyike hapa
duniani kama huko mbinguni.
11Utupatie leo riziki zetu za kila siku.
12Utusamehe deni zetu,
kama sisi nasi tulivyokwisha
kuwasamehe wadeni wetu.
13 Usitutie majaribuni,
bali utuokoe kutoka kwa yule mwovu,
kwa kuwa Ufalme ni Wako na nguvu
na utukufu hata milele. Amen."

14Kwa kuwa kama mkiwasamehe watu wengine wanapowakosea, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe pia na ninyi.
15Lakini msipowasamehe watu wengine makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.

### *Kuhusu Kufunga*

16"Mnapofunga, msiwe wenye huzuni kama wafanyavyo wanafiki. Maana wao hukunja nyuso zao ili kuwaonyesha wengine kwamba wamefunga. Amin, amin nawaambia wao wamekwisha kupata thawabu yao kamilifu.
17Lakini mnapofunga, jipakeni mafuta kichwani na kunawa nyuso zenu
18ili kufunga kwenu kusionekane na watu wengine ila Baba yenu aliye sirini, naye Baba yenu aonaye sirini atawapa thawabu yenu kwa wazi."

### *Akiba Ya Mbinguni*

19"Msijiwekee hazina duniani, mahali ambapo nondo na kutu huharibu, nao wevi huvunja na kuiba.
20Lakini jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambapo nondo na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji na kuiba.
21Kwa sababu mahali akiba yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa.''

### *Jicho Ni Taa Ya Mwili*

22''Jicho ni taa ya mwili. Kama jicho lako ni nyofu, mwili wako wote utakuwa na nuru.
23Lakini kama jicho lako ni ovu, mwili wako wote utajawa na giza. Kwa hiyo basi, kama nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza, hilo ni giza kuu namna gani ! "

### *Mungu Na Mali*

24''Hakuna mtu ye yote awezaye kuwatumikia mabwana wawili, kwa kuwa ama atamchukia huyu na kumpenda yule mwingine, au atashikamana sana na huyu na kumdharau huyu mwingine. Ninyi hamwezi kumtumikia Mungu na mali [a].''

### *Msiwe Na Wasiwasi*

25''Kwa hiyo nawaambia, msiwe na wasiwasi kuhusu maisha yenu: mtakula nini au mtakunywa nini, au kuhusu miili yenu, mtavaa nini. Je, maisha si zaidi ya chakula na mwili zaidi ya mavazi?
26Waangalieni ndege wa angani, wao hawapandi wala hawavuni au kuweka ghalani, lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Je, ninyi si wa thamani zaidi kuliko hao ndege?
27Ni nani miongoni mwenu ambaye kwa kujitaabisha kwake aweza kujiongezea hata saa moja zaidi katika maisha yake au kuongeza dhiraa moja [b] kwenye kimo chake ?

28''Nanyi kwa nini kujitaabisha kwa ajili ya mavazi? Fikirini maua ya shambani yameavyo. Hayafanyi kazi wala hayafumi.
29 Lakini nawaambia, hata mfalme Solomoni katika fahari yake yote hakuvikwa kama mojawapo ya hayo maua.
30 Lakini ikiwa Mungu anayavika hivi majani ya shambani, ambayo leo yapo na kesho yanatupwa motoni, je, hatawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani haba?
31Kwa hiyo msiwe na wasiwasi, mkisema, 'Tutakula nini?' Au 'Tutakunywa nini?' Au 'Tutavaa nini?'
32Kwa maana watu wasiomjua Mungu ndio wanaoshindania hayo, lakini Baba yenu wa mbinguni anafahamu kwamba mnahitaji hayo yote.
33Lakini utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake na haya yote mtaongezewa.
34Kwa hiyo msiwe na wasi wasi kuhusu kesho, kwa sababu kesho itajitaabikia yenyewe. Yatosha kwa siku masumbufu yake.''

### *Kuwahukumu Wengine*

7 "Usihukumu ili usije ukahukumiwa.
2Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea.

---

a24 Mali hapa ina maana ya 'Mammon,' ambalo ni neno la Kiaramu
au kwa Kiyunani ''Mamona'' maana yake mali, utajiri

b27 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45

3“Kwa nini unatazama kibanzi kidogo
kilichomo kwenye jicho la ndugu yako na wala
huoni boriti iliyoko kwenye jicho lako? 4Au
unawezaje kumwambia ndugu yako, ‘Acha nitoe
kibanzi kwenye jicho lako wakati kuna boriti
kwenye jicho lako mwenyewe ?’ 5Ewe mnafiki,
toa kwanza boriti kwenye jicho lako mwenyewe,
nawe ndipo utakapoona wazi ili kuondoa kibanzi
kilichoko kwenye jicho la ndugu yako.

6“Msiwape mbwa vitu vilivyo vitakatifu, wala
msitupie nguruwe lulu zenu. Kama mkifanya
hivyo, watazikanyaga kanyaga na kisha
watawageukia na kuwararua vipande vipande. ”

### *Omba, Tafuta, Bisha*

7“Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi
mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa mlango.
8Kwa maana kila aombaye hupewa, naye
atafutaye huona, naye abishaye hufunguliwa
mlango.

9“Au ni nani miongoni mwenu ambaye
mwanawe akimwomba mkate atampa jiwe?
10Au mwanawe akimwomba samaki atampa
nyoka? 11Ikiwa ninyi basi mlio waovu mnajua
jinsi ya kuwapa watoto wenu vitu vizuri, si zaidi
sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa vitu
vizuri wale wamwombao ? 12Kwa hiyo cho
chote ambacho mngetaka mtendewe na watu,
ninyi nanyi watendeeni vivyo hivyo. Kwa kuwa
hii ndiyo Torati na Manabii.’’

### *Njia Nyembamba Na Njia Pana*

13“Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba,
kwa maana lango ni pana na njia ni pana
ielekeayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa
kupitia lango hilo. 14Lakini mlango ni
mwembamba na njia ni finyo ielekayo kwenye
uzima, nao ni wachache tu waionao.’’

### *Mti na Tunda lake*

15“Jihadharini na manabii wa uongo,
wanaowajia wakiwa wamevaa mavazi ya
kondoo, lakini ndani wao ni mbwa mwitu
wakali.16Mtawatambua kwa matunda yao. Je,
watu huchuma zabibu kwenye miiba au tini
kwenye michongoma? 17Vivyo hivyo, mti
mwema huzaa matunda mazuri na mti mbaya
huzaa matunda mabaya. 18Mti mwema hauwezi
kuzaa matunda mabaya wala mti mbaya
hauwezi kuzaa matunda mazuri. 19Kila mti
usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa
motoni. 20Hivyo, kwa matunda yao,
mtawatambua.’’

### *Mwanafunzi Wa Kweli*

21“Si kila mtu aniambiaye, ‘Bwana, Bwana,’
atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni bali ni
yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye
mbinguni. 22Wengi wataniambia siku ile,
‘Bwana, Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako
na kwa jina lako kutoa pepo na kufanya miujiza
mingi? 23Ndipo nitakapowaambia wazi,
``Sikuwajua kamwe. Ondokeni kwangu, ninyi
watenda maovu!’

### *Msikiaji Na Mtendaji*

24“Kwa hiyo kila mtu ayasikiaye haya
maneno yangu na kuyatenda, ni kama mtu
mwenye busara aliyejenga nyumba yake
kwenye mwamba. 25Mvua ikanyesha, mafuriko
yakaja na upepo ukavuma ukaipiga hiyo
nyumba, lakini haikuanguka kwa sababu msingi
wake ulikuwa kwenye mwamba. 26Naye kila
anayesikia haya maneno yangu wala
asiyatende, ni kama mtu mjinga aliyejenga
nyumba yake kwenye mchanga. 27Mvua
ikanyesha, mafuriko yakaja, nao upepo
ukavuma ukaipiga hiyo nyumba, nayo
ikaanguka kwa kishindo kikubwa.’’

28Yesu alipomaliza kusema maneno haya,
makutano ya watu wakashangazwa sana na
mafundisho yake, 29kwa sababu alifundisha
kama yeye aliye na mamlaka, wala si kama
walimu wao wa sheria.

### *Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*

**8** Yesu aliposhuka kutoka mlimani, makutano
makubwa ya watu yakamfuata.
2Mtu mmoja mwenye ukoma akaja na kupiga
magoti mbele yake akasema, “Bwana, kama
ukitaka, unaweza kunitakasa.’’

3Yesu akanyoosha mkono wake akamgusa,
akamwambia, “Nataka, takasika!’’ Mara yule
mtu akatakasika ukoma wake. 4Kisha Yesu
akamwambia, “Hakikisha humwambii mtu ye
yote. Lakini nenda, ukajionyeshe kwa kuhani na
utoe sadaka aliyoamuru Mose, iwe ushuhuda
kwao kwamba umepona.’’

### *Yesu Amponya Mtumishi Wa Jemadari*

5Yesu alipoingia Kapernaumu, jemadari
mmoja alimjia, kumwomba msaada, 6akisema,
“Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani
amepooza, tena ana maumivu makali ya
kutisha.’’

7Yesu akamwambia, "Nitakuja na kumponya."

8 Lakini yule jemadari akamwambia, "Bwana, mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu. lakini sema neno tu, naye mtumishi
wangu atapona. 9Kwa kuwa mimi nami niko chini ya mamlaka, nikiwa na askari chini yangu. Nikimwambia huyu 'Nenda,' naye huenda, na mwingine nikimwambia, 'Njoo', huja. Nami nikimwambia mtumishi wangu, 'Fanya hivi,' hufanya."

10Yesu aliposikia maneno haya, akashangaa, akawaambia wale waliomfuata, "Amin, amin nawaambia, hata katika Israeli
sijaona imani kubwa namna hii. 11Ninawaambia kwamba wengi watatoka mashariki na magharibi nao wataketi karamuni pamoja na Abrahamu, Isaki na Yakobo katika Ufalme wa Mbinguni.
12Lakini warithi wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ambako kutakuwa na kulia na kusaga meno."

13Kisha Yesu akamwambia yule jemadari, "Nenda na iwe kwako sawasawa na imani yako." Naye yule mtumishi akapona saa ile ile.

### *Yesu Aponya Wengi*

14Yesu alipoingia nyumbani kwa Petro, alimkuta mama mkwe wake Petro amelala
kitandani akiwa ana homa. 15Akamgusa mkono wake na homa ikamtoka, naye akainuka na
kuanza kumhudumia. 16Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopagawa na pepo, naye akawatoa wale pepo kwa neno lake, na kuponya
wagonjwa wote. 17Haya yalifanyika ili litimie lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Isaya kwamba:

"Mwenyewe alitwaa udhaifu wetu
na alichukua magonjwa yetu."

### *Gharama ya Kumfuata Yesu*

18Yesu alipoona makutano mengi wamemzunguka, aliwaamuru wanafunzi wake
wavuke mpaka ng'ambo. 19 Kisha mwalimu mmoja wa sheria akamjia Yesu na kumwambia, "Mwalimu, mimi nitakufuata po pote uendako."

20Naye Yesu akamwambia, "Mbweha wana mashimo, nao ndege wa angani wana viota vyao, lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa chake."

21Mwanafunzi mwingine akamwambia, "Bwana, niruhusu kwanza nikamzike baba yangu."

22Lakini Yesu akamwambia, "Nifuate, nawe waache wafu wazike wafu wao."

### *Yesu Atuliza Dhoruba*

23Naye alipoingia kwenye chombo,
wanafunzi wake wakamfuata. 24Ghafula kukainuka dhoruba kali baharini hata chombo kikaanza kufunikwa na mawimbi, lakini Yesu
alikuwa amelala usingizi. 25Wanafunzi wake wakamwendea na kumwamsha, wakisema, "Bwana, tuokoe! Tunazama!"

26Naye Yesu akawaambia, 'Kwa nini mnaogopa, enyi wa imani haba?' Kisha akaondoka na kukemea dhoroba na mawimbi, nako kukawa shwari kuu.

27Wale watu wakashangaa, wakisema, "Ni mtu wa namna gani huyu? Hata upepo na mawimbi vinamtii!.

### *Wawili Wenye Pepo Waponywa*

28Walipofika ng'ambo katika nchi ya Wagerasi, watu wawili waliopagawa na pepo wakitoka makaburini walikutana naye. Watu hawa walikuwa wakali mno kiasi kwamba hakuna mtu aliyeweza kupita njia ile.
29Wakapiga kelele, "Una nini nasi, Mwana wa Mungu? Umekuja hapa kututesa kabla ya wakati ulioamuriwa?"

30Mbali kidogo kutoka pale walipokuwa, kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe wakilisha.
31Wale pepo wakamsihi Yesu, "Ukitutoa humu, turuhusu tuende kwenye lile kundi la nguruwe."

32Akawaambia, "Nendeni!" Hivyo wakatoka na kuwaingia wale nguruwe, nalo kundi lote likatelemka mbio gengeni, likaingia bahari na
kufa ndani ya maji. 33Wale waliokuwa wakiwachunga hao nguruwe wakakimbia wakaingia mjini, wakaeleza yote kuhusu yale yaliyowatokea wale waliokuwa wamepagawa na
pepo. 34 Kisha watu wote wa mji huo wakatoka kwenda kukutana na Yesu. Nao walipomwona wakamsihi aondoke kwenye nchi yao.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyepooza*

9 Yesu akaingia kwenye chombo, akavuka na
kufika katika mji wa kwao. 2Wakati huo huo
wakamletea mtu aliyepooza, akiwa amelazwa kwenye kitanda. Yesu alipoona imani yao, alimwambia yule mtu aliyepooza, "Mwanangu, jipe moyo mkuu, dhambi zako zimesamehewa."

3Kwa ajili ya jambo hili, baadhi ya walimu

wa sheria wakasema mioyoni mwao, ‘‘Huyu mtu anakufuru!’’

4 Lakini Yesu akiyafahamu mawazo yao, akawaambia, ‘‘Kwa nini mnawaza maovu mioyoni mwenu? 5 Kwa kuwa ni lipi lililo rahisi: kusema, ‘Dhambi zako zimesamehewa,’ au kusema, ‘Simama, utembee?’ 6 Lakini, ili mpate kujua kwamba Mwana wa Adamu anayo mamlaka duniani kusamehe dhambi," Ndipo akamwambia yule aliyepooza, “Simama, chukua kitanda chako na uende nyumbani kwako.’’ 7 Yule mtu akasimama, akaenda nyumbani kwake. 8 Makutano walipoyaona haya, wakajawa na hofu ya Mungu, wakamtukuza Mungu ambaye alikuwa ametoa mamlaka kama hii kwa wanadamu.

### *Kuitwa Kwa Mathayo*

9 Yesu alipokuwa akienda kutoka huko, alimwona mtu mmoja jina lake Mathayo akiwa ameketi forodhani mahali pa kutozea ushuru. Yesu akamwambia, “Nifuate.’’ Mathayo akaondoka, akamfuata.

10 Wakati Yesu alipokuwa ameketi chakulani ndani ya nyumba, watoza ushuru wengi na wenye dhambi wakaja kula pamoja naye na wanafunzi wake. 11 Mafarisayo walipoona mambo haya, wakawauliza wanafunzi Wake, “Kwa nini Mwalimu wenu anakula na watoza ushuru na ‘wenye dhambi’?’’

12 Lakini Yesu aliposikia hayo, akawaambia, “Watu wenye afya hawahitaji tabibu, lakini wale walio wagonjwa ndio wanaohitaji tabibu. 13 Nendeni mkajifunze maana ya maneno haya, ‘Nataka rehema, wala si dhabihu.’ Kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.’’

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*

14 Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji wakaja na kumwuliza Yesu, “Imekuwaje kwamba sisi na Mafarisayo tunafunga, lakini wanafunzi wako hawafungi?’’

15 Yesu akawajibu, “Je, wageni wa bwana – arusi waweza kuomboleza wakati angali pamoja nao? Wakati utafika ambapo bwana arusi ataondolewa kwao, hapo ndipo watakapofunga.

16 “Hakuna mtu anayeshonea kiraka kipya kwenye nguo kuukuu, kwa maana kile kiraka kitachanika kutoka kwenye hiyo nguo na kuchanika kwake kutakuwa kubaya zaidi ya hapo mwanzo. 17 Wala watu hawaweki divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Kama wakifanya hivyo, viriba vitapasuka na divai itamwagika. Navyo viriba vitaharibika, lakini divai mpya huwekwa kwenye viriba vipya na hivyo divai na viriba huwa salama.’’

### *Msichana Afufuliwa Na Mwanamke Aponywa*

18 Wakati Yesu akiwa anawaambia mambo haya, mara akaingia kiongozi wa sinagogi akapiga magoti mbele yake, akimwambia, ‘‘Binti yangu amekufa sasa hivi, lakini uje uweke mkono wako juu yake naye atakuwa hai.’’ 19 Yesu akaondoka akafuatana naye, wanafunzi wake pia wakaandamana naye.

20 Wakati huo huo mwanamke mmoja ambaye alikuwa na ugonjwa wa kutokwa damu kwa muda wa miaka kumi na miwili, akaja nyuma ya Yesu akagusa upindo wa vazi lake, 21 kwa maana alisema moyoni mwake, “Kama nikigusa tu vazi lake, nitaponywa.’’

22 Yesu akageuka, naye alipomwona akamwambia, “Binti, jipe moyo mkuu, imani yako imekuponya.’’ Naye yule mwanamke akapona kuanzia saa ile ile.

### *Yesu Amfufua Binti Wa Kiongozi Wa Sinagogi.*

23 Yesu alipofika nyumbani kwa yule kiongozi wa sinagogi na kuwaona waombolezaji wakipiga filimbi za maombolezo na watu wengi wakipiga kelele, 24 akawaambia, “Ondokeni! Kwa maana binti huyu hakufa, bali amelala.’’ Wakamcheka kwa dhihaka. 25 Lakini watu walipokwisha kutolewa nje, akaingia mle ndani na kumshika yule binti mkono, naye akaamka. 26 Habari hizi zikaenea katika maeneo yale yote.

### *Yesu Awaponya Vipofu*

27 Yesu alipokuwa akiondoka mahali pale, vipofu wawili wakamfuata, wakipiga kelele kwa nguvu na kusema, “Mwana wa Daudi, tuhurumie!’’

28 Alipoingia mle nyumbani wale vipofu wakamjia. Akawauliza, “Mnaamini kwamba ninaweza kufanya jambo hili?”

Wakamjibu, “Ndio Bwana.’’

29 Ndipo Yesu akagusa macho yao na kusema, “Iwe kwenu sawasawa na mnavyoamini.’’ 30 Macho yao yakafunguka. Yesu akawaonya vikali, akisema, “Angalieni mtu ye yote asijue kuhusu jambo hili.’’ 31 Lakini wao wakaenda na kueneza habari zake katika eneo lile lote.

### *Yesu Amponya Mtu Bubu*

32Walipokuwa wanatoka, mtu mmoja
aliyekuwa amepagawa na pepo na ambaye
hakuweza kuongea aliletwa kwa Yesu. 33Yule
pepo alipotolewa, yule mtu aliyekuwa bubu
akaongea. Ule umati wa watu ukastaajabu na
kusema, "Jambo kama hili kamwe halijapata
kuonekana katika Israeli."
34Lakini Mafarisayo wakasema, "Huyo
anatoa pepo kwa uwezo wa mkuu wa pepo.''

### *Watenda Kazi Ni Wachache*

35Yesu akazunguka katika miji yote na vijiji
vyote, akifundisha katika masinagogi yao ,
akihubiri Habari Njema za Ufalme na kuponya
kila ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni
mwa watu. 36Alipoona makutano aliwahurumia
kwa sababu walikuwa wanasumbuka na bila
msaada, kama kondoo wasio na mchungaji.
37Ndipo akawaambia wanafunzi wake, "Mavuno
ni mengi lakini watenda kazi ni wachache,
38Kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno, ili
apeleke watenda kazi katika shamba lake la
mavuno.''

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*

**10** Ndipo Yesu akawaita wanafunzi wake kumi
na wawili, akawapa mamlaka juu ya pepo
wachafu kuwatoa na kuponya kila
ugonjwa na maradhi ya kila aina.
2Haya ndiyo majina ya hao wanafunzi kumi
na wawili: 3wa kwanza, Simon, aitwaye Petro na
Andrea nduguye, Yakobo mwana wa Zebedayo
na Yohana nduguye, Filipo na Bartholomayo,
Tomaso na Mathayo mtoza ushuru, Yakobo
mwana wa Alfayo na Thadayo, 4 Simoni
Mkananayo na Yuda Iskariote aliyemsaliti Yesu.

### *Kutumwa Kwa Wale Kumi Na Wawili*

5Hawa kumi na wawili, Yesu aliwatuma
akawaagiza, "Msiende miongoni mwa watu
Mataifa wala msiingie mji wo wote wa
Wasamaria. 6Lakini afadhali mshike njia
kuwaendea kondoo wa nyumba ya Israeli
waliopotea. 7Wakati mnapokwenda, hubirini
mkisema, 'Ufalme wa Mbinguni umekaribia.'
8Ponyeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni
wenye ukoma, toeni pepo wachafu. Mmepata
bure, toeni bure. 9Msichukue dhahabu, wala
fedha, wala shaba kwenye vifuko vyenu.
10Msichukue mkoba wa safari, wala kanzu mbili,
wala jozi ya pili ya viatu, wala fimbo, kwa maana
mtenda kazi anastahili posho yake.
11"Mji wo wote au kijiji cho chote
mtakachoingia, tafuteni humo mtu anayestahili,
nanyi kaeni kwake mpaka mtakapoondoka.
12Mkiingia kwenye nyumba, itakieni amani.
13Kama nyumba hiyo inastahili, amani yenu na
iwe juu yake, la sivyo, amani yenu na iwarudie
ninyi. 14Kama mtu ye yote hatawakaribisha
ninyi, wala kusikiliza maneno yenu, kungu'uteni
mavumbi kutoka kwenye miguu yenu
mtakapokuwa mnatoka kwenye nyumba hiyo au
mji huo. 15Amin, amin nawaambia, itavumilika
zaidi miji ya Sodoma na Gomora katika hukumu
kuliko mji huo.

### *Mateso Yanayokuja*

16"Tazama, ninawatuma kama kondoo
katikati ya mbwa mwitu. Kwa hiyo mwe werevu
kama nyoka na wapole kama hua.
17"Jihadharini na wanadamu, kwa maana
watawapeleka katika mabaraza yao na
kuwapiga kwenye masinagogi yao, 18nanyi
mtaburutwa mbele ya watawala na
wafalme kwa ajili Yangu, ili kuwa ushuhuda
kwao na mbele ya watu Mataifa. 19Lakini
watakapowapeleka humo, msisumbuke
kufikirifikiri mtakalosema, kwa maana mtapewa
la kusema wakati huo. 20Kwa sababu si ninyi
mtakaokuwa mkinena, bali ni Roho wa Baba
yenu atakayekuwa akinena kupitia kwenu.
21"Ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe
na baba atamsaliti mtoto wake, watoto wataasi
dhidi ya wazazi wao na kuwafanya wauawe.
22Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya
Jina langu. Lakini yeye atakayevumilia hadi
mwisho ataokoka. 23Wakiwatesa katika mji
mmoja, kimbilieni mji mwingine.Amin, amin
nawaambia, hamtamaliza miji yote ya Israeli
kabla Mwana wa Adamu hajaja.
24 "Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu
wake wala mtumishi hamzidi bwana wake.
25Yatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu
wake na mtumishi kuwa kama bwana wake.
Ikiwa mkuu wa nyumba ameitwa Beelzebuli [a],
je, si zaidi sana wale wa nyumbani mwake
mwenyewe!

### *Anayestahili Kuogopwa*

26"Kwa hiyo msiwaogope hao, kwa maana
hakuna kilichofichika ambacho hakitafunuliwa,
wala hakuna siri ambayo haitajulikana.
27Ninalowaambia gizani, ninyi lisemeni mchana
peupe na lile mnalosikia likinong'onwa,

---

[a] 25 ''Beelizebubu'' au kwa Kiyunani Beezebub au Beelzebub yaani, Beelzebuli maana yake mkuu wa pepo

masikioni mwenu, lihubirini kwenye paa la
nyumba. 28Msiwaogope wale wauao mwili lakini
hawawezi kuua roho afadhali mwogopeni yeye
awezaye kuiangamiza roho na mwili katika
jehanam [b]. 29Je, shomoro wawili hawauzwi kwa
senti mbili tu? Lakini hakuna hata mmoja wao
atakayeanguka pasipo Baba yenu kujua.. 30Hata
nywele za vichwa vyenu zote zimehesabiwa.
31Hivyo msiogope, kwa maana ninyi ni wa
thamani kubwa zaidi kuliko shomoro wengi.

32"Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu,
mimi nami nitamkiri yeye mbele za Baba yangu
aliye mbinguni. 33Lakini ye yote atakayenikana
mimi mbele ya watu, mimi nami nitamkana
mbele ya Baba yangu aliye mbinguni."

### *Sikuleta Amani, Bali Upanga*

34"Msidhani kwamba nimekuja kuleta amani
duniani. Sikuja kuleta amani bali upanga.
35Kwa maana nimekuja
kumfitini mtu na babaye,
binti na mamaye,
mkwe na mama mkwe wake.
36Nao adui za mtu watakuwa ni wale watu
wa nyumbani kwake.

37"Ye yote ampendaye baba yake au mama
yake kuliko anavyonipenda mimi, hastahili kuwa
wangu. Ye yote ampendaye mwanawe au binti
yake kuliko anavyonipenda Mimi, hastahili kuwa
wangu. 38 Tena ye yote asiyeuchukua msalaba
wake na kunifuata, hastahili kuwa Wangu.
39Ayang'ang'aniaye maisha yake atayapoteza,
lakini yeye atakayeyatoa maisha yake kwa ajili
yangu atayaona."

### *Watakaopokea Thawabu*

40"Mtu ye yote atakayewapokea ninyi
atakuwa amenipokea mimi na ye yote
atakayenipokea mimi atakuwa amempokea
Yeye aliyenituma. 41Mtu ye yote anayempokea
nabii kwa kuwa ni nabii, atapokea thawabu ya
nabii na mtu anayempokea mwenye haki kwa
kuwa ni mwenye haki, atapokea thawabu ya
mwenye haki. 42 Kama ye yote akimpa hata
kikombe cha maji mmoja wa hawa wadogo kwa
kuwa ni mwanafunzi wangu, amin,
ninawaambia, hataikosa thawabu yake."

### *Yesu na Yohana Mbatizaji*

[b]28 Jehanum au Kiyunani'' ''Gehena'' maana yake
kuzimu, yaani, motoni

**11** Baada ya Yesu kumaliza kutoa maagizo kwa
wale wanafunzi wake kumi na wawili, aliondoka
hapo akaenda kufundisha na
kuhubiri katika miji yao.

2Yohana Mbatizaji aliposikia akiwa gerezani
mambo ambayo Kristo [a] alikuwa akiyafanya,
aliwatuma wanafunzi wake 3ili wakamwulize,
"Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee
mwingine?"

4Yesu akajibu, "Rudini mkamwarifu Yohana
yale mnayosikia na kuyaona: 5 Vipofu wanapata
kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma
wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu
wanafufuliwa na maskini wanahubiriwa habari
njema. 6Ana heri mtu yule asiyechukizwa kwa
ajili yangu"

7Wale wanafunzi wa Yohana walipokuwa
wanaondoka, Yesu akaanza kusema na
makutano kuhusu Yohana Mbatizaji.
Akawauliza, "Mlipokwenda kule nyikani,
mlikwenda kuona nini? Unyasi ukiyumbishwa na
upepo? 8Kama sivyo, mlitoka kwenda kuona
nini basi? Mtu aliyevaa mavazi mazuri.? Hasha,
wale wanaovaa nguo nzuri wako katika
majumba ya wafalme. 9Basi mlitoka kwenda
kuona nini? Je, ni kumwona nabii? Naam,
nawaambia, yeye ni zaidi ya nabii. 10Huyo ndiye
ambaye habari zake zimeandikwa:

" 'Tazama namtuma mjumbe mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele yako.'

11Amin, nawaambia, miongoni mwa watu
waliozaliwa na wanawake, hajatokea mtu aliye
mkuu zaidi ya Yohana Mbatizaji, lakini aliye
mdogo kabisa katika Ufalme wa Mbinguni, ni
mkuu kuliko Yohana. 12Tangu siku za Yohana
Mbatizaji hadi sasa, Ufalme wa Mungu
hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu
wauteka. 13Kwa maana manabii wote na Torati
vilitabiri mpaka wakati wa Yohana. 14Kama mko
tayari kukubali hilo, yeye Yohana ndiye yule
Eliya ambaye manabii walikuwa wamesema
angekuja. 15 Yeye aliye na sikio na
asikie.16"Lakini kizazi hiki nikifananishe na
nini?" Kinafanana na watoto waliokaa sokoni
wakiwaita wenzao na kuwaambia,

17 " 'Tuliwapigia filimbi,
lakini hamkucheza,
tuliwaimbia nyimbo za msiba

[a]2 Kristo yaani Masiya maana yake Mpakwa (Aliyetiwa) Mafuta.

lakini hamkuomboleza.’

18Kwa maana Yohana Mbatizaji alikuja hali wala
hanywi, nao wanasema, ‘Yeye ana pepo.’
19Mwana wa Adamu alikuja akila na kunywa,
nao wanasema, ‘Tazama, mlafi na mlevi, rafiki
wa watoza ushuru na wenye dhambi!’ Lakini
hekima huthibitishwa kwa haki ya matendo
yake.’’

### *Ole Wa Miji Isiyotubu*

20Ndipo Yesu akaanza kuilaumu miji
ambamo alifanya miujiza yake mingi kuliko
kwingine, kwa maana watu wake hawakutubu.
21 “Ole wako, Korazini! Ole wako Bethsaida!
Kwa maana kama miujiza iliyofanyika kwenu,
ingelifanyika Tiro na Sidoni, miji hiyo ingekuwa
imetubu tangu zamani kwa kuvaa magunia na
kujipaka majivu. 22Lakini nawaambia,
itavumilika zaidi kwa Tiro na Sidoni katika siku
ya hukumu, kuliko kwenu, 23Nawe
Kapernaumu,je, utainuliwa hadi mbinguni? La
hasha, utashushwa pande za chini sana [b] .
Miujiza iliyofanyika kwako ingefanyika huko
Sodoma, mji huo ungalikuwapo hadi leo. 24
Lakini nakuambia kwamba, itavumilika zaidi kwa
Sodoma katika siku ile ya hukumu kuliko wewe.

### *Hakuna Amjuaye Baba Ila Mwana*

25Wakati huo Yesu alisema, “Ninakuhimidi
Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa
umewaficha mambo haya wenye hekima na
wenye elimu, nawe ukawafunulia watoto
wachanga. 26Naam, Baba, kwa kuwa hivyo
ndivyo ilivyokupendeza.

27“Nimekabidhiwa vitu vyote na Baba
yangu: hakuna mtu amjuaye Mwana ila Baba,
wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana na ye
yote ambaye Mwana anapenda kumdhihirisha
Baba kwake.’’

### *Yesu Awaita Waliolemewa Na Mizigo*

28“Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika
na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.
29Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu,
kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa
moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu.
30Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo
wangu ni mwepesi.’’

b23 Pande za chini sana hapa ina maana ya neno la
Kiyunani Hades au kwa Kiyahudi Sheol, yaani, Kuzimu.

### *Bwana Wa Sabato*

**12** Wakati huo Yesu alipitia kwenye mashamba
ya ngano siku ya sabato.
Wanafunzi wake walikuwa na njaa, wakaanza
kuvunja masuke ya ngano na kuyala. 2Lakini
Mafarisayo walipoona jambo hili,
wakamwambia, “Tazama! Wanafunzi wako
wanafanya jambo lisilo halali siku ya Sabato.’’

3Yesu akawajibu, “Je, hamjasoma
alichofanya Daudi na wenzake walipokuwa na
njaa? 4 Aliingia katika nyumba ya Mungu akala
mikate iliyowekwa wakfu, yeye na wenzake,
jambo ambalo halikuwa halali kwao kufanya,
isipokuwa makuhani peke yao. 5Au hamjasoma
katika Torati kwamba siku ya Sabato makuhani
huvunja sheria ya Sabato Hekaluni lakini
hawahesabiwi kuwa na hatia? 6Nawaambia
wazi kwamba, Yeye aliye mkuu kuliko Hekalu
yupo hapa. 7Kama mngelikuwa mmejua maana
ya maneno haya, ‘Ninataka rehema, wala si
dhabihu,’ msingeliwalaumu watu wasio na hatia,
8kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana
wa Sabato.’’

### *Yesu Anamponya Mtu Aliyepooza Mkono*

9Yesu akaondoka mahali hapo, akaingia
katika sinagogi lao, 10huko alikuwepo mtu
aliyepooza mkono. Wakitafuta sababu ya
kumshtaki Yesu, wakamwuliza, “Je, ni halali
kuponya siku ya
Sabato?’’

11Yesu akawaambia, “Ni nani miongoni
mwenu, mwenye kondoo wake ambaye huyo
kondoo akitumbukia shimoni siku ya Sabato
hatamtoa? 12Mtu ana thamani kubwa kiasi
kuliko kondoo. Kwa hiyo ni halali kutenda mema
siku ya Sabato.’’

13Ndipo akamwambia yule mtu, ‘‘Nyoosha
mkono wako.’’ Akaunyoosha, nao ukaponywa
ukawa mzima kama ule mwingine. 14Lakini
Mafarisayo wakatoka nje wakafanya shauri
baya juu yake jinsi watakavyoweza kumwua
Yesu.

### *Mtumishi Aliyechaguliwa Na Mungu*

15Lakini Yesu alipoyatambua mawazo yao,
akaondoka mahali hapo. Watu wengi
wakamfuata, naye akawaponya wote,
16akiwakataza wasiseme yeye ni nani. 17Hii
ilikuwa ili litimie lile neno lililonenwa kwa kinywa
cha nabii Isaya, kusema :

18"Tazama mtumishi wangu niliyemchagua,
mpendwa wangu, ninayependezwa
naye.
Nitaweka Roho yangu juu yake,
naye atatangaza haki kwa mataifa.
19Hatagombana wala hatapiga kelele,
wala hakuna atakayesikia sauti yake njiani.
20Mwanzi uliopondeka hatauvunja,
utambi unaofuka moshi hatauzima,
mpaka atakapoifanya haki ishinde.
21"Katika jina lake mataifa wataweka
tumaini lao."

### *Yesu Na Beelzebuli*

22Kisha wakamletea mtu aliyekuwa amepagawa na pepo, naye ni kipofu na bubu, Yesu akamponya, hata akaweza kusema na kuona. 23Watu wote wakashangaa na kusema, "Je, yawezekana huyu ndiye Mwana wa Daudi?"

24Lakini Mafarisayo waliposikia jambo hili wakasema, "Mtu huyu anatoa pepo wachafu kwa uwezo wa Beelzebuli [a], mkuu wa pepo wachafu."

25Yesu alijua walichokuwa wakiwaza, akawaambia, "Kila ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe huangamia. Hali kadhalika kila mji au watu wa nyumba moja iliyogawanyika dhidi yake yenyewe haiwezi kusimama. 26Kama Shetani akimtoa Shetani, atakuwa amegawanyika yeye mwenyewe. Basi ufalme wake utawezaje kusimama? 27Nami kama natoa pepo wachafu kwa nguvu za Beelzebuli [b], watu wenu je, wao hutoa pepo wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi, wao ndio watakaowahukumu. 28Lakini kama Mimi ninatoa pepo wachafu kwa Roho wa Mungu, basi Ufalme wa Mungu umekuja juu yenu.

29"Au tena, mtu awezaje kuingia katika nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuteka nyara mali zake asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Akiisha mfunga, ndipo hakika anaweza kuteka nyara mali zake.

30"Mtu asiyekuwa pamoja nami yu kinyume nami na mtu ambaye hakusanyi pamoja nami, hutawanya. 31Kwa hiyo nawaambia, kila dhambi na kufuru watu watasamehewa, lakini mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa. 32"Mtu ye yote atakayesema neno dhidi ya Mwana wa Adamu atasamehewa, lakini ye yote anenaye neno dhidi ya Roho Mtakatifu hatasamehewa, iwe katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao.'

### *Mti Na Matunda Yake*

33"Ufanye mti kuwa mzuri nayo matunda yake yatakuwa mazuri, au ufanye mti kuwa mbaya na matunda yake yatakuwa mabaya, kwa maana mti hutambulikana kwa matunda yake. 34Enyi uzao wa nyoka! Mnawezaje kunena mambo mema, wakati ninyi ni waovu? Kwa maana kinywa cha mtu huyanena yale yaliyoujaza moyo wake. 35 Mtu mwema hutoa yaliyo mema kutoka katika hazina ya mambo mema yaliyohifadhiwa ndani yake, naye mtu mwovu hutoa yaliyo maovu kutoka katika hazina ya mambo maovu yaliyohifadhiwa ndani yake. 36Lakini nawaambia, katika siku ya hukumu watu watatoa hesabu kuhusu kila neno lisilo maana walilonena. 37Kwa maana kwa maneno yako utahesabiwa haki na kwa maneno yako utahukumiwa."

### *Ishara Ya Yona*

38Kisha baadhi ya Mafarisayo na walimu wa sheria wakamwambia, "Mwalimu, tunataka kuona ishara kutoka kwako."

39Lakini Yeye akawajibu, "Kizazi kiovu na cha uzinzi kinaomba ishara! Lakini hakitapewa ishara yo yote isipokuwa ile ishara ya nabii Yona. 40Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa ndani ya tumbo la nyangumi [c] kwa muda wa siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu, mchana na usiku. 41Siku ya hukumu watu wa Ninawi watasimama pamoja na kizazi hiki na kukihukumu, kwa maana wao walitubu katika kuhubiri kwa Yona na tazama hapa yupo yeye aliye mkuu kuliko Yona. 42Malkia wa Kusini atasimama wakati wa hukumu na kukihukumu kizazi hiki, kwa kuwa yeye alikuja kutoka miisho ya dunia ili kuisikiliza hekima ya Solomoni na hapa yupo aliye mkuu kuliko Solomoni."

### *Mafundisho Kuhusu Pepo Mchafu*

43 "Pepo mchafu amtokapo mtu, hutanga-tanga katika sehemu zisizo na maji akitafuta mahali pa kupumzika, lakini hapati. 44Ndipo husema, 'Nitarudi kwenye ile nyumba yangu nilikotoka,' Naye arudipo huikuta ile nyumba ikiwa tupu, imefagiliwa na kupangwa vizuri.

a[24] Beelizebuli au Beelizebubu maana yake: mkuu wa pepo wachafu.

b[27] Beelzebul au Beelizebubu maana yake mkuu wa pepo wachafu.

c[40] Nyangumi ni samaki mkubwa sana

45Kisha huenda na kuwaleta pepo wachafu wengine saba, wabaya zaidi kuliko yeye, nao huingia na kuishi humo. Nayo hali ya mwisho ya mtu yule huwa mbaya zaidi kuliko ile ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki cha uovu.''

### *Mama Na Ndugu Zake Yesu*

46Wakati alipokuwa akali anazungumza na makutano, mama Yake na ndugu Zake walisimama nje wakitaka kuongea naye. 47Ndipo mtu mmoja akamwambia, "Tazama mama Yako na ndugu Zako wamesimama nje, wanataka kuongea na Wewe.''

48Lakini Yeye akamjibu na kumwambia yule mtu, "Mama yangu ni nani, nao ndugu zangu ni nani?'' 49Akiwanyoshea mkono wanafunzi Wake, akasema, "Hawa hapa ndio mama Yangu nao ndugu Zangu! 50Kwa maana ye yote afanyaye mapenzi ya Baba Yangu wa mbinguni, ndiye ndugu Yangu, dada Yangu na mama yangu.''

### *Mfano Wa Mpanzi*

**13** Siku iyo hiyo Yesu akatoka nje ya nyumba akaketi kando ya bahari. 2Umati mkubwa mno wa watu ukakusanyika kumzunguka hata ikabidi aingie katika chombo na kuketi humo, nao watu wote wakawa wamesimama ukingoni mwa bahari. 3Ndipo akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema: "Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake. 4Alipokuwa akipanda, baadhi zikaanguka kando ya njia, ndege wakaja na kuzila. 5Nyingine zikaanguka sehemu yenye mawe, ambapo hapana udongo mwingi. Zikaota haraka kwa sababu udongo ulikuwa hauna kina. 6Lakini jua lilipozidi, mimea hiyo ilinyauka na kukauka kwa sababu mizizi yake haikuwa na kina. 7Mbegu nyingine zilianguka katikati ya miiba, miiba hiyo ikakua ikazisonga. 8Mbegu nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri ambapo zilitoa mazao, nyingine mara mia moja, nyingine mara sitini na nyingine mara thelathini. 9Yeye mwenye masikio ya kusikia na asikie.''

### *Sababu Ya Kufundisha Kwa Mifano*

10Wanafunzi wake wakamwendea wakamwuliza, "Kwa nini unasema na watu kwa mifano?'' 11Akawajibu, "Ninyi mmepewa kuzifahamu siri za Ufalme wa Mbinguni, lakini wao sivyo. 12Kwa maana yule aliye na kitu atapewa zaidi, naye atakuwa navyo tele, lakini yule asiye na kitu, hata kile alichonacho atanyang'anywa. 13Hii ndiyo sababu nasema nao kwa mifano:

''Ingawa wanatazama, hawaoni,
wanasikiliza, lakini hawasikii, wala
hawaelewi.

14Kwao unatimia ule unabii wa Isaya aliposema:
" 'Hakika mtasikiliza lakini hamtaelewa,
na pia mtatazama lakini hamtaona.
15Kwa maana mioyo ya watu hawa
imekuwa mizito,
hawasikii kwa masikio yao, na
wamefumba macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
wakasikia kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao,
wakageuka, nami nikawaponya.'

16"Lakini heri macho yenu, kwa sababu yanaona na heri masikio yenu kwa sababu yanasikia. 17Amin, nawaambia, manabii wengi na wenye haki walitamani kuona yale mnayoyaona, nao hawakuyaona na kusikia yale mnayosikia lakini hawakuyasikia.''

### *Maelezo Ya Mfano Wa Mbegu*

18"Sikilizeni basi maana ya ule mfano wa mpanzi: 19Mtu ye yote anaposikia neno la Ufalme, naye asilielewe, yule mwovu huja na kunyakua kile kilichopandwa moyoni mwake, hii ndiyo ile mbegu iliyopandwa kando ya njia. 20Ile mbegu iliyopandwa kwenye sehemu yenye mawe ni mtu yule ambaye hulisikia neno na mara hulipokea kwa furaha. 21Lakini kwa kuwa hana mizizi yenye kina ndani yake, lile neno hukaa kwa muda mfupi. Inapotokea dhiki au mateso kwa ajili ya hilo neno, yeye mara huchukizwa. 22 Ile mbegu iliyopandwa katika miiba ni yule mtu alisikiaye neno, lakini masumbufu ya dunia na vishawishi vya mali hulisonga lile neno na kulifanya lisizae matunda. 23Lakini ile mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri ni yule mtu ambaye hulisikia neno na kulielewa. Naye hakika hutoa matunda, akizaa mara mia, au mara sitini, au mara thelathini ya mbegu iliyopandwa.''

### *Mfano Wa Magugu*

24Yesu akawaambia mfano mwingine, akasema: ''Ufalme wa Mbinguni unaweza kufananishwa na mtu aliyepanda mbegu nzuri katika shamba lake. 25Lakini wakati kila mtu

alipokuwa amelala, adui yake akaja na kupanda
magugu katikati ya ngano, akaenda zake.
26Ngano ilipoota na kutoa masuke, magugu
nayo yakatokea.

27“Watumishi wa yule mwenye shamba
wakamjia na kumwambia, ‘Bwana, si tulipanda
mbegu nzuri shambani mwako? Basi, magugu
yametoka wapi ?

28Akawajibu, ‘Adui ndiye aliyefanya jambo
hili.’ Wale watumishi wakamwuliza, ‘Je, unataka
twende tukayang'oe? ”

29Lakini akasema, ‘Hapana, msiyang'oe,
kwa maana wakati mking’oa magugu mnaweza
mkang'oa na ngano pamoja nayo. 30Acheni
ngano na magugu vikue vyote pamoja mpaka
wakati wa mavuno. Wakati huo nitawaambia
wavunaji, wayakusanye magugu kwanza,
wayafunge matita matita ili yachomwe moto,
kisha wakusanye ngano na kuileta ghalani
mwangu.’ ”

### *Mfano Wa Mbegu ya Haradali*

31Akawaambia mfano mwingine, akasema,
“Ufalme wa Mbinguni ni kama punje ya haradali,
ambayo mtu aliichukua akaipanda shambani
mwake. 32Ingawa mbegu hiyo ni ndogo kuliko
mbegu zote, lakini inapokua ni mmea mkubwa
kuliko yote ya bustanini, nao huwa mti mkubwa,
hata ndege wa angani huja na kutengeneza
viota katika matawi yake.’’

### *Mfano Wa Chachu*

33Akawaambia mfano mwingine, ‘‘Ufalme
wa Mbinguni unafanana na chachu ambayo
mwanamke aliichukua akaichanganya katika
vipimo vitatu vya unga mpaka wote ukaumuka.’’

### Sababu Ya Yesu Kutumia Mifano

34Yesu alinena mambo haya yote kwa
makutano kwa mifano. Wala pasipo mfano
hakuwaambia lo lote. 35Hii ilikuwa ili kutimiza lile
lililonenwa kwa vinywa vya manabii kusema:

‘‘Nitakifungua kinywa changu niseme nao
kwa mifano,
nitahubiri mambo yaliyofichika tangu
kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu.’’

### *Ufafanuzi Wa Mfano Wa Magugu*

36Kisha Yesu akaagana na makutano,
akaingia nyumbani. Wanafunzi wake wakamjia
wakamwambia, ‘‘Tueleze maana ya ule mfano
wa magugu shambani.’’

37Akawaambia, “Aliyepanda mbegu nzuri ni
Mwana wa Adamu. 38Shamba ni ulimwengu na
mbegu nzuri ni wana wa Ufalme. Magugu ni
wana wa yule mwovu. 39Yule adui aliyepanda
magugu ni Ibilisi . Mavuno ni mwisho wa dunia,
nao wavunaji ni malaika.

40‘‘Kama vile magugu yang’olewavyo na
kuchomwa motoni, ndivyo itakavyokuwa wakati
wa mwisho wa dunia. 41Mwana wa Adamu
atawatuma malaika zake, nao watakusanya
kutoka katika Ufalme wake kila kitu
kinachosababisha dhambi na watenda maovu
wote· 42Nao watawatupa katika tanuru la moto
ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.
43Ndipo wenye haki watang'aa kama jua katika
Ufalme wa Baba yao. Yeye aliye na masikio , na
asikie.

### *Mfano Wa Hazina Iliyofichwa na Lulu*

44‘‘Ufalme wa Mbinguni unafanana na
hazina iliyofichwa shambani, ambayo mtu
mmoja alipoiona akaificha tena. Kisha katika
furaha yake, akaenda akauza vyote alivyokuwa
navyo, akalinunua lile shamba.’’

45‘‘Tena, Ufalme wa Mbinguni unafanana
na mfanyi biashara aliyekuwa akitafuta lulu safi.
46Alipoipata lulu moja ya thamani kubwa,
alikwenda akauza vyote alivyokuwa navyo
akainunua.

### *Mfano Wa Wavu*

47“Tena, Ufalme wa Mbinguni ni kama wavu
wa kuvulia samaki uliotupwa baharini ukavua
samaki wa kila aina. 48Ulipojaa, wavuvi
wakavuta pwani, wakaketi na kukusanya
samaki wazuri kuwaweka kwenye vyombo safi,
lakini wale samaki wabaya wakawatupa. 49Hivi
ndivyo itakavyokuwa wakati wa mwisho wa
dunia. Malaika watakuja na kuwatenganisha
watu waovu na watu wenye haki. 50Nao
watawatupa hao waovu katika tanuru la moto
ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.

51Yesu akauliza, ‘‘Je, mmeyaelewa
haya yote?"
Wakamjibu, ‘‘Ndiyo.’’

52Akawaambia, ‘‘Basi kila mwalimu wa
sheria aliyefundishwa elimu ya Ufalme wa
Mbinguni ni kama mwenye nyumba anayetoa
kutoka katika ghala yake mali mpya na mali ya
zamani.’’

### *Yesu Akataliwa Nazareti*

53Yesu alipomaliza kutoa mifano hii,

akaondoka. 54 Alipofika mjini kwao,
akawafundisha watu katika sinagogi lao. Nao
wakastaajabu, wakauliza, "Mtu huyu amepata
wapi hekima hii na uwezo huu wa kufanya
miujiza?" 55 "Huyu si yule mwana wa seremala?
Mama yake si yeye aitwaye Maria, nao ndugu
zake ni Yakobo, Yosefu, Simoni na Yuda?
56 Nao dada zake wote hawako hapa pamoja
nasi? Mtu huyu amepata wapi basi mambo haya
yote?" 57 Wakachukizwa naye.

Lakini Yesu akawaambia, "Nabii hakosi
heshima isipokuwa katika nchi yake na
nyumbani kwake."

58 Naye hakufanya miujiza mingi huko kwa
sababu ya kutokuamini kwao.

### *Yohana Mbatizaji Akatwa Kichwa*

**14** Wakati huo, mfalme Herode aliyekuwa mtawala
alisikia habari kuhusu sifa za Yesu, 2 akawaambia
watumishi wake, "Huyu ni
Yohana Mbatizaji, amefufuka kutoka kwa wafu!
Hiyo ndiyo sababu nguvu za kutenda miujiza
zinafanya kazi ndani yake."

3 Herode alikuwa amemkamata Yohana
akamfunga na kumweka gerezani kwa sababu
ya Herodia, mke wa Filipo, ndugu yake, 4 kwa
kuwa Yohana alikuwa amemwambia Herode
kwamba, "Si halali kwako kuwa na huyo
mwanamke." 5 Herode alitaka sana kumwua
Yohana, lakini akiogopa watu kwa maana
walimtambua kuwa ni nabii.

6 Katika siku ya kuadhimisha sikukuu ya
kuzaliwa kwa Herode, binti wa Herodia alicheza
mbele ya watu waliohudhuria akamfurahisha
sana Herode 7 kiasi kwamba aliahidi kwa kiapo
kumpa huyo binti lo lote atakaloomba. 8 Yeye
akiwa amefundishwa na mama yake, huyo binti
akasema, "Nipatie kichwa cha Yohana Mbatizaji
kwenye sinia." 9 Mfalme akasikitika, lakini kwa
ajili ya kile kiapo alichoapa mbele ya wageni,
akaamuru kwamba apatiwe ombi lake. 10 Hivyo
akaagiza Yohana Mbatizaji akatwe kichwa mle
gerezani. 11 Kichwa chake kikaletwa kwenye
sinia, akapewa yule binti, naye akampelekea
mama yake. 12 Wanafunzi wa Yohana wakaja na
kuuchukua mwili wake kwenda kuuzika. Kisha
wakaenda wakamwambia Yesu.

### *Yesu Alisha Watu Elfu Tano*

13 Yesu aliposikia haya yaliyokuwa
yametukia, aliondoka kwa chombo akaenda
mahali pasipo na watu ili awe peke yake. Lakini
watu walipopata habari, wakamfuata kwa miguu
kupitia nchi kavu, kutoka mijini. 14 Yesu alipofika
kando ya bahari aliona makutano makubwa ya
watu, akawahurumia na akawaponya wagonjwa
wao.

15 Ilipofika jioni, wanafunzi wake wakamjia
wakamwambia, "Mahali hapa ni nyikani, na
muda sasa umekwisha, waage makutano ili
waende zao vijijini wakajinunulie chakula."

16 Yesu akawaambia, "Hakuna sababu ya
wao kuondoka. Ninyi wapeni chakula."

17 Wakamjibu, "Tuna mikate mitano na
samaki wawili tu."

18 Akawaambia, "Nileteeni hivyo vitu hapa."
19 Akaagiza makutano wakae chini kwenye
nyasi. Akaichukua ile mikate mitano na wale
samaki wawili, akainua macho yake akatazama
mbinguni, akavibariki na kuimega ile mikate,
kisha akawapa wanafunzi wake hiyo mikate na
hao samaki,wanafunzi wakawagawia makutano.
20 Wote wakala, wakatosheka, nao wanafunzi
wake wakakusanya vipande vilivyosalia,
wakajaza vikapu kumi na viwili. 21 Idadi ya wale
watu waliokula walikuwa wanaume 5,000, bila
kuhesabu wanawake na watoto.

### *Yesu Atembea Juu Ya Maji*

22 MaraYesu akawaambia wanafunzi wake
waingie kwenye chombo watangulie kwenda
ng'ambo ya pili ya bahari, wakati Yeye
anawaaga wale makutano. 23 Baada ya
kuwaaga, akaenda zake mlimani peke yake
kuomba. Jioni ilipofika, Yesu alikuwa huko peke
Yake. 24 Wakati huo kile chombo kilikuwa
kimeshafika mbali kutoka nchi kavu
kikisukwasukwa na mawimbi kwa sababu upepo
ulikuwa wa mbisho.

25 Wakati wa zamu ya nne ya usiku [a], Yesu
akawaendea wanafunzi wake akiwa anatembea
juu ya maji. 26 Wanafunzi wake walipomwona
akitembea juu ya maji, waliingiwa na hofu kuu,
wakasema, "Ni mzimu." Wakapiga yowe kwa
kuogopa.

27 Lakini mara Yesu akasema nao,
akawaambia, "Jipeni moyo! Ni Mimi, msiogope."

28 Petro akamjibu, "Bwana, ikiwa ni Wewe,
niambie nije kwako nikitembea juu ya
maji." 29 Yesu akamwambia, "Njoo."

Basi Petro akatoka kwenyen chombo,
akatembea juu ya maji kumwelekea Yesu.
30 Lakini alipoona upepo mkali aliingiwa na hofu,
naye akaanza kuzama, huku akipiga kelele,
"Bwana, niokoe!"

---

a25 "Zamu ya nne ya usiku" ni kati ya saa 9 na saa 12 alfajiri

31Mara Yesu akanyosha mkono Wake na
kumshika, akamwambia, “Wewe mwenye imani
haba, kwa nini uliona shaka?’’

32Nao walipoingia ndani ya chombo, upepo
ukakoma. 33Ndipo wote waliokuwamo ndani ya
kile chombo wakamwabudu Yesu wakisema,
“Hakika, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu.’’

### *Yesu Awaponya Wagonjwa Genesareti*

34Walipokwisha kuvuka, wakafika nchi ya
Genesareti. 35Watu wa eneo lile
walipomtambua Yesu, walipeleka habari
sehemu zote za jirani. Watu wakawaletea
wagonjwa wao wote 36wakamsihi awaruhusu
wagonjwa waguse tu pindo la vazi Lake, nao
wote waliomgusa, wakaponywa.

### *Mapokeo Ya Wazee*

**15** Ndipo baadhi ya Mafarisayo na walimu wa
sheria wakamjia Yesu kutoka Yerusalemu na
kumwuliza, 2“Mbona wanafunzi wako wanakiuka
mapokeo ya wazee waliopita? Kwa maana wao
hawanawi mikono yao kabla
ya kula!’’

3 Yesu akawajibu, “Mbona ninyi mnavunja
amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?
4Kwa maana Mungu alisema, ‘Waheshimu baba
yako na mama yako’ na ‘Ye yote amtukanaye
baba yake au mama yake, na auawe.’ 5Lakini
ninyi mwafundisha kwamba mtu akimwambia
baba yake au mama yake, ‘Kile ambacho
ningeweza kukusaidia kimewekwa wakfu kwa
Mungu,’ basi hana tena sababu ya kumsaidia
baba yake. 6Basi kwa ajili ya mafundisho yenu
mnavunja amri ya Mungu. 7 Ninyi wanafiki!
Isaya alikuwa sawa alipotabiri juu yenu kwamba:

8“ ‘Watu hawa huniheshimu kwa midomo
yao, lakini mioyo yao iko mbali nami.
9Kuniabudu kwao ni bure,
nayo mafundisho yao ni maagizo
ya wanadamu tu.’ ”

### *Vitu Vitiavyo Unajisi*

10Yesu akaita ule umati wa watu
akawaambia, “Sikilizeni na mwelewe:
11kinachomfanya mtu kuwa najisi mbele za
Mungu si kile kiingiacho kinywani mwake, bali ni
kile kitokacho kinywani mwake.’’

12Kisha wanafunzi wake wakamjia na
kumwuliza, Je, unajua kwamba Mafarisayo
walichukizwa sana waliposikia yale uliyosema?’’

13Akawajibu, “Kila pando ambalo Baba
yangu wa mbinguni hakulipanda, litang'olewa.
14Waacheni, wao ni viongozi vipofu,
wanaoongoza vipofu. Kama kipofu
akimwongoza kipofu mwenzake, wote wawili
watatumbukia shimoni.’’

15Petro akasema, “Tuelezee maana ya huu
mfano.’’

16Yesu akawauliza, “Je, bado ninyi
hamfahamu? Je, hamfahamu 17kwamba cho
chote kiingiacho kinywani huenda tumboni na
hatimaye hutolewa nje na kuwa uchafu?
18Lakini kitokacho kinywani hutoka moyoni, na
hiki ndicho kimtiacho mtu unajisi. 19Kwa maana
ndani ya moyo hutoka mawazo mabaya, uuaji,
uzinzi, uasherati, wizi, ushahidi wa uongo na
masingizio. 20Haya ndiyo yamtiayo mtu unajisi,
lakini kula bila kunawa mikono hakumtii mtu
unajisi.”

### *Imani ya Mwanamke Mkananayo*

21Yesu aliondoka mahali pale akaenda
sehemu za Tiro na Sidoni. 22 Mwanamke mmoja
Mkananayo aliyeishi jirani na sehemu hizo akaja
kwake, akilia, akasema, “Nihurumie,Ee Bwana,
Mwana wa Daudi, binti yangu amepagawa na
pepo na anateseka sana.’’

23Lakini Yesu hakumjibu neno. Hivyo
wanafunzi wake wakamwendea na kumsihi
sana, wakisema, “Mwambie aende zake, kwa
maana anaendelea kutupigia kelele.’’

24Yesu akajibu, “Nimetumwa tu kwa ajili ya
kondoo wa Israeli waliopotea.’’

25Lakini yule mwanamke akaja, akapiga
magoti mbele ya Yesu, akasema, ‘‘Bwana,
nisaidie!’’

26Yesu akajibu, ‘‘Si haki kuchukua chakula
cha watoto na kuwatupia mbwa.’’

27Yule mwanamke akajibu, “Ndiyo, Bwana,
lakini hata mbwa hula makombo yanayoanguka
kutoka kwenye meza za bwana zao.’’

28 Ndipo Yesu akamwambia, “Mwanamke,
imani yako ni kubwa! Iwe kwako kama
unavyotaka.’’Naye binti yake akapona tangu
saa ile ile.

### *Yesu Aponya Watu Wengi*

29Yesu akaondoka na kwenda kando ya
bahari ya Galilaya. Kisha akapanda mlimani,
akaketi huko. 30Umati mkubwa wa watu
wakamjia, wakiwaleta vilema, vipofu,viwete,
bubu na wengine wengi, wakawaweka miguuni
pake, naye akawaponya.31Hao watu
wakashangaa walipoona bubu wakisema,

vilema wakipona, viwete wakitembea na vipofu wakiona, wakamtukuza Mungu wa Israeli.

### *Yesu Alisha Watu Elfu Nne*

32Kisha Yesu akawaita wanafunzi wake akawaambia, "Ninahurumia huu umati wa watu, kwa sababu sasa wamekuwa pamoja nami kwa muda wa siku tatu na hawana cho chote cha chakula, nami sipendi kuwaaga wakiwa na njaa wasije wakazimia njiani."

33Wanafunzi wake wakasema, ''Tutapata wapi mikate ya kutosha kuwalisha umati huu wa watu mkubwa namna hii, nasi tuko nyikani?''

34Yesu akawauliza, "Mnayo mikate mingapi?''

Wakamjibu, ''Tunayo mikate saba na visamaki vichache."

35Yesu akawaambia ule umati wa watu waketi chini. 36Kisha akachukua ile mikate saba na wale samaki, naye akiisha kumshukuru Mungu, akavimega na kuwapa wanafunzi wake, nao wakawapa ule umati wa watu. 37Wote wakala na kushiba. Baadaye wanafunzi wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu saba. 38Idadi ya watu walikuwa wanaume 4,000, bila kuhesabu wanawake na watoto. 39Baada ya kuaga ule umati wa watu, Yesu aliingia chomboni akaenda sehemu za Magadani [a].

### *Mafarisayo Wadai Ishara*

**16** Mafarisayo na Masadukayo wakamjia Yesu na kumjaribu kwa kumwomba awaonyeshe ishara kutoka mbinguni.

2Akawajibu akawaambia, "Ifikapo jioni, mnasema, 'Hali ya hewa itakuwa nzuri, kwa kuwa anga ni nyekundu,' 3nanyi wakati wa asubuhi mnasema, 'Leo kutakuwa na dhoruba, kwa sababu anga ni nyekundu na mawingu yametanda.' Mnajua jinsi ya kupambanua kule kuonekana kwa anga, lakini hamwezi kupambanua dalili za nyakati. 4Kizazi cha waovu na cha zinaa hutafuta ishara ya majira, lakini hakitapewa ishara yo yote isipokuwa ishara ya Yona." Yesu akawaacha, akaenda zake.

### *Chachu Ya Mafarisayo Na Masadukayo*

5Wanafunzi wake walipofika ng'ambo ya pili ya bahari, walikuwa wamesahau kuchukua

[a]39 Magadani hapa inamaanisha Magdala.

mikate. 6Yesu akawaambia, "Jihadharini, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na ya Masadukayo.''

7Wakajadiliana wao kwa wao, wakisema, "Ni kwa sababu hatukuleta mikate.''

8Yesu, akitambua mazungumzo yao, akasema, "Enyi wa imani haba! Mbona mnajadiliana miongoni mwenu kuhusu kutokuwa na mikate? 9Je, bado tu hamwelewi? Je,hamkumbuki ile mikate mitano iliyolisha watu 5,000 na ni idadi ya vikapu vingapi vya mabaki mlivyokusanya? 10Au ile mikate saba iliyolisha watu 4,000 na ni idadi ya vikapu vingapi vya mabaki mlivyokusanya? 11Inakuwaje mnashindwa kuelewa kwamba nilikuwa sisemi nanyi habari za mikate? Jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo." 12Ndipo wakaelewa kwamba alikuwa hasemi juu ya chachu ya kutengeneza mikate, bali juu ya mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo.

### *Petro Amkiri Yesu Kuwa Ni Mwana Wa Mungu*

13 Basi Yesu alipofika katika eneo la Kaisaria Filipi, akawauliza wanafunzi wake, "Watu husema Mwana wa Adamu ni nani?"

14Wakamjibu, "Baadhi ya watu husema ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya na bado wengine husema, ni Yeremia au mmojawapo wa manabii.''

15Akawauliza, ''Je, ninyi, mnasema mimi ni nani?''

16Simoni Petro akamjibu, "Wewe ndiwe Kristo [a], Mwana wa Mungu aliye hai.''

17Naye Yesu akamwambia, ''Heri wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa maana hili halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni. 18 ''Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, hata malango ya kuzimu hayataweza kulishinda. 19Nitakupa funguo za Ufalme wa Mbinguni na lo lote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa Mbinguni, lo lote utakalofungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.'' 20Kisha akawakataza wanafunzi wake wasimwambie mtu ye yote kwamba Yeye ndiye Kristo.

### *Yesu Anatabiri Juu Ya Kifo Chake*

[a]16 Kristo maana yake Masiya, yaani, Mpakwa (Aliyetiwa)Mafuta.''

21 Tangu wakati huo Yesu alianza
kuwaeleza wanafunzi wake kwamba hana budi
kwenda Yerusalemu na kupata mateso mengi
kwa mikono ya wazee, wakuu wa makuhani na
walimu wa sheria na kwamba itampasa auawe
na siku ya tatu atafufulika.

22 Petro akamchukua kando akaanza
kumkemea, akisema, "Mungu apishie hayo
mbali! Jambo hili kamwe halitakupata!!"

23 Lakini Yesu akageuka na kumwambia
Petro , "Rudi nyuma yangu, Shetani! Wewe ni
kikwazo kwangu. Moyo wako hauwazi yaliyo ya
Mungu, bali ya wanadamu."

24 Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake,
"Mtu ye yote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane
mwenyewe na auchukue msalaba wake,
anifuate. 25 Kwa maana ye yote anayetaka
kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini ye
yote atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili
yangu atayapata. 26 Kwa maana itamfaidia nini
mtu kuupata ulimwengu wote, lakini
akayapoteza maisha yake? Au mtu atatoa nini
badala ya maisha yake? 27 Kwa maana Mwana
wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake
pamoja na malaika zake, naye ndipo
atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo
yake. 28 Nawaambia kweli, baadhi yenu hapa
hawataonja mauti kabla ya kumwona Mwana wa
Adamu akija katika Ufalme wake."

### *Yesu Abadilika Sura Mlimani*

**17** Siku sita baada ya jambo hili,Yesu
akawachukua Petro, Yakobo na Yohana
ndugu yake Yakobo, na kuwaleta mpaka juu ya
mlima mrefu mahali pasipo na watu. 2 Wakiwa
huko, Yesu alibadilika sura mbele yao. Uso
wake ukang'aa kama jua na nguo zake zikawa
na weupe wa kuumiza macho. 3 Ghafula
wakawatokea mbele yao Mose
na Eliya, wakizungumza na Yesu.

4 Ndipo Petro akamwambia Yesu, "Bwana,
ni vema sisi tukae hapa. Ukitaka, nitafanya
vibanda vitatu: kimoja chako, kingine cha Mose
na kingine cha Eliya."

5 Petro alipokuwa angali ananena, ghafula,
wingu linalong'aa likawafunika na sauti ikatoka
kwenye hilo wingu ikisema, "Huyu ni mwanangu
mpendwa, ninayependezwa naye sana,
msikilizeni Yeye."

6 Wale wanafunzi, waliposikia haya,
wakaanguka chini kifudifudi, wakajawa na hofu.
7 Lakini Yesu akaja na kuwagusa, akawaambia,
"Inukeni na wala msiogope." 8 Walipoinua
macho yao, hawakumwona mtu mwingine ye
yote isipokuwa Yesu .

9 Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani,
Yesu akawaagiza, "Msimwambie mtu ye yote
maono haya mpaka Mwana wa Adamu
atakapofufuka kutoka kwa wafu."

10 Wale wanafunzi wakamwuliza, "Kwa nini
basi walimu wa sheria wanasema kwamba
lazima Eliya aje kwanza?"

11 Yesu akawajibu, "Ni kweli, Eliya lazima
aje kwanza naye atatengeneza mambo yote.
12 Lakini nawaambia, Eliya amekwisha kuja, nao
hawakumtambua, bali walimtendea kila kitu
walichotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu pia
atateswa mikononi mwao.' " 13 Ndipo wale
wanafunzi wakaelewa kuwa alikuwa
anazungumza nao habari za Yohana Mbatizaji.

### *Yesu Amponya Kijana Mwenye Pepo*

14 Walipofika penye umati wa watu, mtu
mmoja akamjia Yesu na kupiga magoti mbele
yake, akasema, 15 "Bwana, mhurumie
mwanangu. Yeye ana kifafa na anateseka sana.
Mara kwa mara huanguka kwenye moto au
kwenye maji. 16 Nilimleta kwa wanafunzi wako
lakini hawakuweza kumponya."

17 Yesu akajibu, "Enyi kizazi kisichoamini na
kilichopotoka, nitakaa nanyi hata lini, nami
nitawavumilia hadi lini? Mleteni kijana hapa
kwangu." 18 Yesu akamkemea yule pepo
mchafu, akamtoka yule kijana, naye akapona
saa ile ile

19 Kisha wanafunzi wakamwendea Yesu
wakati ambapo hakuna watu, wakamwuliza,
"Kwa nini sisi hatukuweza kumtoa?"

20 Akawajibu, "Kwa sababu ya imani yenu
ndogo. Ninawaambia kweli, mkiwa na imani
kama punje ndogo ya haradali, mtauambia
mlima huu, 'Ondoka hapa uende pale' nao
utaondoka. Wala hakutakuwa na jambo
lisilowezekana kwenu." 21 "Lakini hali kama hii
haitoki ila kwa kuomba na kufunga."

22 Siku moja walipokuwa pamoja huko
Galilaya, Yesu akawaambia, "Mwana wa
Adamu anakwenda kutiwa mikononi mwa watu.
23 Nao watamwua na siku ya tatu atafufuka."
Wanafunzi wakahuzunika sana.

### *Yesu Na Petro Watoa Kodi Ya Hekalu*

24 Baada ya Yesu na wanafunzi wake kufika
Kapernaumu, wakusanyaji wa kodi ya Hekalu

wakamjia Petro na kumwuliza, “Je, Mwalimu
wenu halipi kodi ya Hekalu [a]?’’

25Petro akajibu, “Ndiyo, Yeye hulipa.” Petro
aliporudi nyumbani, Yesu akawa wa kwanza
kulizungumzia, akamwuliza, “Unaonaje
Simoni?’’ Wafalme wa dunia hupokea ushuru na
kodi kutoka kwa nani? Je, ni kutoka kwa watoto
wao au kutoka kwa watu wengine?”

26Petro akamjibu, “Kutoka kwa watu
wengine.’’ Yesu akamwambia, “Kwa hiyo watoto
wao wamesamehewa. 27 Lakini ili tusije
tukawaudhi, nenda baharini ukatupe ndoana.
Mchukue samaki wa kwanza utakayemvua,
fungua kinywa chake nawe utakuta humo fedha,
ichukue ukalipe kodi yako na yangu.”

### *Aliye Mkuu Katika Ufalme Wa Mbinguni*

18 Wakati huo, wanafunzi wakamjia Yesu na
kumwuliza “Je, nani aliye mkuu
kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni?”

2Yesu akamwita mtoto mdogo na
kumsimamisha katikati yao. 3Naye akasema:
‘‘Amin, nawaambia, msipoongoka na kuwa
kama watoto wadogo, kamwe hamtaingia katika
Ufalme wa Mbinguni. 4Kwa hiyo mtu yeyote
ajinyenyekezaye kama huyu mtoto, ndiye aliye
mkuu kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni.

5“Ye yote amkaribishaye mtoto mdogo
kama huyu kwa jina langu, anikaribisha mimi.

### *Kujaribiwa Ili Kutenda Dhambi*

6Lakini kama mtu ye yote anamsababisha
mmojawapo wa hawa wadogo wanaoniamini
atende dhambi, ingekuwa bora kwake afungiwe
jiwe kubwa la kusagia shingoni mwake na
kutoswa katika kilindi cha bahari.

7“Ole wa ulimwengu kwa sababu ya yale
mambo yanayosababisha watu kutenda dhambi!
Mambo hayo lazima yawepo, lakini ole wake
mtu yule ambaye huyasababisha. 8Ikiwa mkono
wako au mguu wako unakusababisha utende
dhambi, ukate na uutupe mbali. Ni afadhali
kwako kuingia katika uzima ukiwa huna mkono
mmoja au mguu mmoja, kuliko kuwa na mikono
miwili au miguu miwili na kutupwa katika moto
wa milele. 9Nalo jicho lako kama
linakusababisha utende dhambi ling'oe, ulitupe
mbali. Ni afadhali kwako kuingia katika uzima
ukiwa na jicho moja, kuliko kuwa na macho
mawili lakini ukatupwa katika moto wa jehanam.

### *Mfano Wa Kondoo Aliyepotea*

10 ‘‘Angalia ili usimdharau mmojawapo wa
hawa wadogo, kwa maana nawaambia, malaika
wao mbinguni daima wanauona uso wa Baba
yangu aliye mbinguni.’’ 11Kwa maana Mwana
wa Adamu alikuja kuokoa kile kilichopotea.

12“Mwaonaje? Ikiwa mtu anao kondoo mia
moja na mmoja wao akapotea, hatawaacha
wale tisini na tisa vilimani na kwenda kumtafuta
huyo mmoja aliyepotea? 13Naye akisha mpata,
amin, nawaambia, hufurahi zaidi kwa ajili ya
huyo kondoo mmoja kuliko wale tisini na tisa
ambao hawakupotea. 14Vivyo hivyo, Baba yenu
wa mbinguni hapendi hata mmojawapo wa
hawa wadogo apotee.’’

### *Ndugu Yako Akikukosea*

15“Kama ndugu yako akikukosea, nenda
ukamwonyeshe kosa lake, kati yenu ninyi wawili
peke yenu. Kama akikusikiliza, utakuwa
umempata tena ndugu yako. 16Lakini kama
hatakusikiliza, nenda na mtu mwingine mmoja
au wawili ili kila neno lithibitishwe na ushahidi
wa mashahidi wawili au watatu. 17Kama
akikataa kuwasikiliza hao, liambie kanisa, naye
kama akikataa hata kulisikiliza kanisa, basi
mtendeeni mtu huyo kama vile ambavyo
mngemtendea asiyeamini.

18“Amin, nawaambieni, lo lote
mtakalolifunga duniani litakuwa limefungwa
mbinguni na lo lote mtakalolifungua duniani
litakuwa limefunguliwa mbinguni.

19“Tena nawaambia, ikiwa wawili wenu
watakubaliana duniani kuhusu jambo lo lote
watakaloomba, watafanyiwa na Baba yangu
aliye mbinguni. 20Kwa kuwa wanapokusanyika
pamoja watu wawili au watatu kwa jina langu,
mimi niko papo hapo pamoja nao.”

### *Kusamehe*

21Ndipo Petro akamjia Yesu na kumwuliza,
“Bwana, ndugu yangu anikosee mara ngapi
nami nimsamehe? Je, hata mara saba?”

22 Yesu akamjibu, ‘‘Sikuambii hata mara
saba, bali hata saba mara sabini.’’

### *Mfano Wa Mtumishi Asiyesamehe*

23‘‘Kwa hiyo Ufalme wa Mbinguni unaweza
kufananishwa na mfalme aliyetaka kufanya
hesabu zake za fedha na watumishi wake.
24Alipoanza kufanya hesabu zake, mtu mmoja

---

[a]24 Kodi ya hekalu hapa ilikuwa “didrachmas,’’ yaani drakamu mbili ambazo ni sawa na nusu shekeli.

aliyekuwa anadaiwa talanta 10,000 [a], aliletwa kwake. 25Kwa kuwa alikuwa hawezi kulipa deni hilo, bwana wake akaamuru kwamba auzwe, yeye, mkewe, watoto wake na vyote alivyokuwa navyo, ili lile deni lipate kulipwa.

26"Yule mtumishi akampigia magoti, akamsihi yule bwana akisema, `Naomba univumilie, nami nitakulipa deni lako lote.''
27Yule bwana wa huyo mtumishi akamwonea huruma, akafuta deni lake lote, akamwacha aende zake.

28"Lakini yule mtumishi alipokuwa anatoka nje, akakutana na mtumishi mwenzake aliyekuwa amemkopesha dinari mia moja [b]. Akamkamata, akamkaba koo akimwambia, 'Nilipe kile ninachokudai!'

29"Yule mtumishi mwenzake akapiga magoti akamsihi akisema, 'Naomba univumilie, nami nitakulipa deni lako lote.'

30"Lakini akakataa. Badala yake, alienda akamtupa gerezani hata atakapolipa hilo deni.
31"Watumishi wenzake walipoona haya yaliyotukia wakaudhika sana, nao wakaenda na kumwambia bwana wao kila kitu kilichokuwa kimetukia.

32"Yule bwana akamwita yule mtumishi akamwambia, 'Wewe mtumishi mwovu! Mimi nilikusamehe deni lako lote uliponisihi. 33Je, haikukupasa kumhurumia mtumishi mwenzako kama mimi nilivyokuhurumia wewe?' 34Kwa hasira yule bwana wake akamtia yule mtumishi mikononi mwa askari wa gereza ili ateswe mpaka atakapolipa yote aliyokuwa anadaiwa.

35"Hivi ndivyo Baba yangu wa mbinguni atakavyomfanyia kila mmoja wenu ikiwa hatamsamehe kutoka moyoni kila mmoja ndugu yake aliyemkosea.''

### *Yesu Afundisha Kuhusu Talaka*

**19** Yesu alipomaliza kusema maneno haya, aliondoka Galilaya, akaenda sehemu za Uyahudi, ng'ambo ya Mto Yordani. 2Umati mkubwa wa watu ukamfuata, naye akawaponya huko.

3Baadhi ya Mafarisayo wakamjia ili kumjaribu wakamwuliza, "Ni halali mtu kumwacha mke wake kwa sababu yo yote?''

4Akawajibu, "Je, hamkusoma kwamba hapo mwanzo Mwumba aliwaumba mtu mume na mtu mke. 5Naye akasema, 'Kwa sababu hii mtu atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja?' 6 Hivyo si wawili tena, bali ni mwili mmoja. Kwa hiyo kile alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe.''

7Wakamwuliza, "Kwa nini basi Mose aliagiza mtu kumpa mkewe hati ya talaka na kumwacha?''

8Yesu akawajibu, "Mose aliwaruhusu kuwaacha wake zenu kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu. Lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo. 9Mimi nawaambia, ye yote amwachaye mkewe isipokuwa kwa sababu ya uasherati naye akaoa mke mwingine, anazini." Naye amwoaye yule mwanamke aliyeachwa pia anazini."

10Wanafunzi wake wakamwambia, "Kama hali ndiyo hii kati ya mume na mke, ni afadhali mtu asioe!''

11Yesu akawaambia, ''Si watu wote wanaoweza kupokea neno hili, isipokuwa wale tu waliojaliwa na Mungu 12Kwa maana wengine ni matoashi kwa sababu wamezaliwa hivyo, wengine wamefanywa matoashi na wanadamu na wengine wamejifanya matoashi kwa ajili ya Ufalme wa Mbinguni. Yeye awezaye kulipokea neno hili na alipokee.''

### *Yesu Awabariki Watoto Wadogo*

13Kisha watoto wadogo wakaletwa kwa Yesu ili aweke mikono yake juu yao na awaombee. Lakini wanafunzi wake wakawakemea wale waliowaleta.

14Yesu akasema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mbinguni ni wa wale walio kama hawa. 15Naye akaweka mikono yake juu yao, akaondoka huko.

### *Kijana Tajiri*

16Mtu mmoja akamjia Yesu na kumwuliza,, "Mwalimu mwema, nifanye jambo gani jema ili nipate uzima wa milele?"

17Yesu akamjibu, "Mbona unaniita mimi mwema? Hakuna aliye mwema ila Mmoja tu, ndiye Mungu: Lakini ukitaka kuingia uzimani, zitii amri."

---

a24 Talanta moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa miaka kumi na mitano.

b28 Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja.

18Yule mtu akamwuliza,''Amri zipi?''

Yesu akamjibu, ''Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uongo, 19waheshimu baba yako na mama yako na umpende jirani yako kama nafsi yako.''

20Yule kijana akasema, ''Hizi zote nimezishika. Je, bado nimepungukiwa na nini?''

21Yesu akamwambia, ''Kama ukitaka kuwa mkamilifu, nenda, kauze vitu vyote ulivyo navyo na hizo fedha uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate.''

22Yule kijana aliposikia hayo, akaenda zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

### *Hatari Za Utajiri*

23Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Amin, amin nawaambia, itakuwa vigumu kwa mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mbinguni. 24Tena nawaambia, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu.''

25Wanafunzi wake waliposikia haya, walishangaa sana na kuuliza, "Ni nani basi awezaye kuokoka?''

26Lakini Yesu akawatazama, akawaambia, "Kwa mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa Mungu mambo yote yanawezekana.''

27Ndipo Petro akamjibu, ''Tazama, sisi tumeacha kila kitu na kukufuata, tutapata nini basi?''

28Yesu akawaambia, "Amin, amin nawaambia , wakati wa kufanywa upya vitu vyote, wakati mwana wa Adamu atakapoketi kwenye kiti chake cha utukufu cha enzi, ninyi mliomfuata pia mtaketi katika viti vya enzi kumi na viwili, mkiyahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli. 29Kila mmoja aliyeacha nyumba au ndugu zake wa kiume au wa kike au baba au mama au watoto au mashamba kwa ajili Yangu, atapokea mara mia zaidi ya hayo na naurithi uzima wa milele. 30Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho nao walio wa mwisho watakuwa wa kwanza.''

### *Mfano Wa Wafanyakazi Katika Shamba La Mizabibu*

**20** "Kwa maana Ufalme wa Mbinguni unafanana na mtu mwenye shamba aliyetoka alfajiri ili kwenda kuajiri vibarua kufanya kazi katika shamba lake la mizabibu 2Baada ya kukubaliana na hao vibarua kuwalipa ujira wa dinari moja [a] kwa siku, akawapeleka kwenye shamba lake la mizabibu.

3"Mnamo saa tatu akatoka tena, akawakuta wengine wamesimama sokoni bila kazi. 4Akawaambia, 'Ninyi nanyi nendeni mkafanye kazi katika shamba langu la mizabibu, nami nitawalipa cho chote kilicho haki yenu.' 5Kwa hiyo wakaenda.

''Akatoka tena mnamo saa sita na pia saa tisa akafanya vivyo hivyo. 6Mnamo saa kumi na moja akatoka tena akawakuta wengine bado wamesimama bila kazi. Akawauliza, 'Kwa nini mmesimama hapa kutwa nzima pasipo kufanya kazi?'

7Wakamjibu, 'Ni kwa sababu hakuna ye yote aliyetuajiri.'

Akawaambia, 'Ninyi nanyi nendeni mkafanye kazi katika shamba langu la mizabibu.'

8"Ilipofika jioni, yule mwenye shamba la mizabibu akamwambia msimamizi,'Waite hao vibarua na uwalipe ujira wao, ukianzia na wale walioajiriwa mwisho na kuishia na wale walioajiriwa kwanza.'

9Wale vibarua walioajiriwa mnamo saa kumi na moja, wakaja na kila mmoja wao akapokea dinari moja. 10Hivyo wale walioajiriwa kwanza walipofika, walidhani watalipwa zaidi. Lakini kila mmoja wao pia alipokea dinari moja. 11Walipoipokea, wakaanza kulalamika dhidi ya yule mwenye shamba, 12wakisema,'Hawa watu walioajiriwa mwisho wamefanya kazi kwa muda wa saa moja tu, nawe umewafanya sawa na sisi ambao tumestahimili taabu na joto lote la mchana kutwa?'

13"Yule mwenye shamba akamjibu mmoja wao, 'Rafiki, sijakudhulumu. Je, hukukubaliana nami kwa ujira wa kawaida wa dinari moja? 14Chukua ujira wako na uende. Mimi nimeamua kumlipa huyu mtu aliyeajiriwa mwisho kama nilivyokupa wewe. 15Je, sina haki yangu kufanya kile nitakacho na mali yangu mwenyewe ? Au unaona wivu kwa kuwa nimekuwa mkarimu?'

16''Vivyo hivyo, wa mwisho watakuwa wa kwanza na wa kwanza watakuwa wa mwisho.''

### *Yesu Atabiri Tena Kuhusu Kifo Chake*

17Basi Yesu alipokuwa anapanda kwenda Yerusalemu, aliwachukua kando wale wanafunzi wake kumi na wawili na kuwaambia,

[a] 2 Dinari moja ilikuwa mshahara wa kibarua wa siku moja.

18"Tazameni, tunapanda kwenda Yerusalemu, naye Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa viongozi wa makuhani na walimu wa sheria, nao watamhukumu kifo
19na kumtia mikononi mwa watu Mataifa ili wamdhihaki na kumpiga mijeledi na kumsulibisha msalabani, naye siku ya tatu atafufuka!"

### *Ombi La Mama Yake Yakobo na Yohana*

20Kisha mama yao wana wa Zebedayo akamjia Yesu pamoja na wanawe, naye akiwa amepiga magoti mbele yake, akamwomba Yesu amfanyie upendeleo.

21Yesu akamwuliza, "Unataka nini?"

Akajibu, "Tafadhali, wape wanangu hawa, mmoja aketi upande wako wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto katika Ufalme wako."

22Yesu akawaambia, "Ninyi hamjui mnaloomba. Je,ninyi mnaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi?"

Wakajibu, "Tunaweza."

23Yesu akawaambia, "Kwa kweli kikombe changu mtakinywea, lakini kuketi upande wangu wa kuume au wa kushoto, si langu mimi kuwapa. Nafasi hizo ni za wale ambao kwa ajili yao zimeandaliwa na Baba yangu."

24 Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia haya, waliwakasirikia hao ndugu
wawili. 25Lakini Yesu akawaita wote pamoja na kuwaambia, "Mnafahamu kuwa watawala wa watu wasiomjua Mungu huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo huonyesha mamlaka yao.
26Isiwe hivyo kwenu. Badala yake, ye yote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana
budi kuwa mtumishi wenu, 27Naye anayetaka kuwa wa kwanza miongoni mwenu ni lazima
awe mtumwa wenu, 28 kama vile ambavyo Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi"

### *Yesu Awaponya Vipofu Wawili*

29Wakati Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakiondoka Yeriko, umati mkubwa
wa watu ulimfuata. 30Vipofu wawili walikuwa wameketi kando ya barabara. Waliposikia kwamba Yesu alikuwa anapita, wakapiga kelele wakisema, "Bwana, Mwana wa Daudi, uturehemu!"

31Ule umati wa watu ukawakemea na kuwaambia wanyamaze, lakini wao wakazidi kupaza sauti wakisema, "Bwana, Mwana wa Daudi, uturehemu."

32Yesu akasimama na kuwaita, akawauliza, "Mnataka niwafanyie nini?"

33Wakamjibu, "Bwana, tunataka kuona."

34Yesu akawahurumia na kuwagusa macho yao. Mara macho yao yakapata kuona, nao wakamfuata.

### *Yesu Anaingia Yerusalemu Kwa Shangwe*

**21** Walipokuwa wanakaribia Yerusalemu, wakafika Bethfage katika Mlima wa Mizeituni, ndipo Yesu akawatuma wanafunzi wake wawili,
2akiwaambia, "Ingieni katika kijiji kilichoko mbele yenu, nanyi mtakuta punda amefungwa na mwanapunda pamoja naye. Wafungueni na
mniletee. 3Kama mtu ye yote akiwasemesha lo lote, mwambieni, 'Bwana ana haja nao, naye atawaruhusu mwalete mara.
4Haya yalitukia ili litimie lile lililonenwa na nabii, akisema:

5"Mwambieni Binti Sayuni,
'Tazama, mfalme wako anakuja kwako,
ni mnyenyekevu, naye amepanda punda,
juu ya mwanapunda, mtoto wa punda.'

6Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya kama vile Yesu alivyokuwa amewaagiza.
7Wakamleta yule punda na mwanapunda, nao wakatandika mavazi yao juu ya hao punda na
Yesu akaketi juu yake. 8Umati mkubwa wa watu wakatandika nguo zao barabarani na wengine wakakata matawi kutoka kwenye miti
wakayatandika barabarani. 9Ule umati wa watu uliomtangulia na ule uliomfuata ukapiga kelele ukisema,

"Hosana Mwana wa Daudi!"
"Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!"
"Hosana juu mbinguni!"

10Yesu alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakauliza, "Huyu ni nani?"

11Ule umati wa watu ukajibu, "Huyu ni Yesu, yule nabii kutoka Nazareti katika Galilaya."

### *Yesu Atakasa Hekalu*

12Yesu akaingia katika eneo la hekalu na kuwafukuza wote waliokuwa wakinunua na kuuza vitu hekaluni, akazipindua meza za watu waliokuwa wakibadilisha fedha na viti vya wale
waliokuwa wakiuza njiwa. 13Akawaambia,

"Imeandikwa, 'Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala,' lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi."

14 Vipofu na vilema wakamwendea kule hekaluni, naye akawaponya. 15 Lakini viongozi wa makuhani na walimu wa sheria walipoona mambo ya ajabu aliyofanya na kuwasikia watoto wakishangilia katika eneo la hekalu wakisema, "Hosana Mwana wa Daudi, walikasirika, wakamwuliza Yesu,

16 "Je, unasikia hayo hawa wanayosema?" Akawajibu,

"Naam, kwani hamkusoma,

" 'Kutoka katika vinywa vya watoto
wachanga
na wale wanaonyonya umeamuru sifa
kamili?' "

17 Akawaacha, akatoka nje ya mji, akaenda hadi Bethania, akalala huko.

### *Mtini Wanyauka*

18 Asubuhi na mapema, Yesu alipokuwa akirudi mjini, alikuwa na njaa. 19 Akiuona mtini kando ya barabara, akaukaribia lakini hakupata tunda lo lote ila majani. Ndipo akauambia, "Wewe na usizae matunda tena kamwe!" Papo hapo ule mtini ukanyauka.

20 Wanafunzi wake walipoona jambo hili wakashangaa, wakamwuliza, "Imekuwaje mtini huu kunyauka ghafula?"

21 Yesu akawajibu, "Amin, amin nawaambia, kama mkiwa na imani wala msiwe na shaka, si kwamba mtaweza kufanya tu yale yaliyofanyika kwa huu mtini, bali hata mkiuambia huu mlima, 'Ng'oka, ukatupwe baharini,' nalo litafanyika. 22 Lo lote mtakaloomba katika kusali, mkiamini, mtapokea.

### *Wahoji Kuhusu Mamlaka Ya Yesu*

23 Yesu alipoingia hekaluni, viongozi wa makuhani na wazee wa watu wakamjia alipokuwa anafundisha na kusema, "Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani, naye ni nani aliyekupa mamlaka hayo?"

24 Yesu akawajibu, "Nami nitawauliza swali moja. Kama mkinijibu, mimi nitawaambia ni kwa mamlaka gani ninafanya mambo haya. 25 Ubatizo wa Yohana, ulitoka wapi? Je, ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?"

Wakaanza kuhojiana wao kwa wao na kusema, "Tukisema ulitoka mbinguni atatuuliza, 'Mbona basi hamkumwamini?' 26 Lakini tukisema, 'Ulitoka kwa wanadamu', tunawaogopa hawa watu, maana wote wanamtambua Yohana kuwa ni nabii."

27 Kwa hiyo wakamjibu Yesu, "Sisi hatujui."

Ndipo akawaambia, "Wala mimi sitawaambia ni kwa mamlaka gani ninatenda mambo haya."

### *Mfano Wa Wana Wawili*

28 "Lakini mwaonaje? Mtu mmoja alikuwa na wana wawili. Akamwendea yule wa kwanza akamwambia, 'Mwanangu, nenda ukafanye kazi kwenye shamba la mizabibu leo.'

29 "Yule mwanawe akamjibu 'Mimi sitakwenda', baadaye akabadili mawazo yake akaenda.

30 "Kisha yule baba akamwendea yule mwanawe mwingine akamwambia vile vile. Yeye akajibu, 'Nitakwenda baba,' lakini hakwenda.

31 "Ni yupi kati yao hao wawili aliyetimiza kile alichotaka baba yake?"

Wakamjibu, "Ni yule wa kwanza."

Yesu akawaambia, "Amin, amin nawaambia, watoza ushuru na makahaba wanawatangulia kuingia katika Ufalme wa Mungu. 32 Kwa maana Yohana alikuja kwenu kuwaonyesha njia ya haki, lakini hakumsadiki, lakini watoza ushuru na makahaba wakamsadiki. Nanyi hata mlipoona hayo, baadaye hamkutubu na kumsadiki."

### *Mfano Wa Wapangaji Waovu*

33 "Sikilizeni mfano mwingine: Kulikuwa na mtu mmoja mwenye shamba ambaye alipanda mizabibu. Akajenga ukuta kulizunguka, akatengeneza shinikizo ndani yake na akajenga mnara wa ulinzi. Kisha akalikodisha hilo shamba la mizabibu kwa wakulima fulani, naye akaondoka akasafiri kwenda nchi nyingine. 34 "Wakati wa mavuno ulipokaribia, akawatuma watumishi wake kwa hao wakulima waliopangishwa ili kukusanya matunda yake.

35 "Wale wapangaji wakawakamata wale watumishi, wakampiga mmoja, wakamwua mwingine na yule wa tatu wakampiga mawe. 36 Kisha akawatuma kwao watumishi wengine, wengi kuliko wale wa kwanza, nao wale wapangaji wakawatendea vile vile. 37 "Mwisho wa yote, akamtuma mwanawe kwao, akisema, 'Watamheshimu mwanangu.'

38 "Lakini wale wapangaji walipomwona

mwanawe, wakaambiana wao kwa wao, 'Huyu ndiye mrithi. Njoni na tumwue ili tuchukue urithi wake.' 39Hivyo wakamchukua, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua.

40"Kwa hiyo, huyo mwenye shamba, atakapokuja atawafanyia nini hao wakulima?''

41Wakamjibu, "Kwa huzuni kuu atawaangamiza kabisa hao wadhalimu na kulipangisha shamba lake kwa wakulima wengine ambao watampatia fungu lake la matunda wakati wa mavuno.''

42Yesu akawaambia, "Je, hamjasoma katika maandiko kwamba:

"Lile jiwe walilolikataa waashi
 limekuwa jiwe kuu la pembeni,
Bwana ndiye aliyefanya jambo hili,
 nalo ni la ajabu machoni petu?'

43''Kwa hiyo ninawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu na watapewa watu wengine wawezao kuzaa matunda yake.'' 44"Yeye aangukaye kwenye jiwe hili atavunjika vipande vipande, lakini yule litakayemwangukia atasagika sagika kabisa.

45Viongozi wa Makuhani na Mafarisayo waliposikia mifano ya Yesu, walitambua kuwa alikuwa akiwasema wao. 46Wakatafuta njia ya kumkamata lakini wakaogopa ule umati wa watu kwa kuwa wao walimwona Yesu kuwa ni nabii.

### *Mfano Wa Karamu Ya Arusi*

**22** Yesu akasema nao tena kwa mifano, akawaambia, 2"Ufalme wa Mbinguni unaweza kufananishwa na mfalme mmoja aliyemwandalia mwanawe karamu ya arusi. 3Akawatuma watumishi wake kuwaita wale waliokuwa wamealikwa karamuni, lakini wakakataa kuja.

4''Kisha akawatuma watumishi wengine akisema, 'Waambieni wale walioalikwa kwamba karamu iko tayari kwa ajili yenu, nimekwisha kuchinja mafahali wangu na vinono. Karibuni |akaenda shambani mwake, mwingine akaenda kwenye biashara yake.

5 "Lakini hawakuzingatia, wakaenda zao, huyu shambani mwake na mwingine kwenye biashara zake. 6Wengine wao wakawakamata wale watumishi wake wakawatenda vibaya na kuwaua. 7"Yule mfalme akakasirika sana, akapeleka jeshi lake likawaangamiza wale wauaji na kuuteketeza mji wao kwa moto.

8"Kisha akawaambia watumishi wake, 'Karamu ya arusi imeshakuwa tayari, lakini wale niliowaalika hawakustahili kuja. 9Kwa hiyo nendeni katika njia panda mkamwalike karamuni ye yote mtakayemwona' 10Wale watumishi wakaenda barabarani wakawakusanya watu wote waliowaona, wema na wabaya. Ukumbi wa arusi ukajaa wageni.

11"Lakini mfalme alipoingia ndani ili kuwaona wageni, akamwona mle mtu mmoja ambaye hakuwa amevaa vazi la arusi. 12 Mfalme akamwuliza, 'Rafiki, uliingiaje humu bila vazi la arusi?' Yule mtu hakuwa na la kusema.

13Ndipo mfalme akawaambia watumishi wake, 'Mfungeni mikono na miguu mkamtupe nje, kwenye giza. Huko kutakuwa na kilio na kusaga meno.'

14Kwa maana walioitwa ni wengi, lakini walioteuliwa ni wachache.''

### *Kulipa Kodi kwa Kaisari*

15Ndipo Mafarisayo wakatoka nje wakaandaa mpango wa kumtega Yesu katika maneno yake. 16Wakatuma wanafunzi wao kwake pamoja na Maherode, wakisema, ''Mwalimu, tunajua kwamba wewe ni mtu mwadilifu na unafundisha njia ya Mungu katika kweli bila kuonyesha tofauti kwa mtu wala upendeleo. 17Tuambie basi, Wewe unaonaje? Ni halali kulipa kodi kwa Kaisari au la?''

18Lakini Yesu akijua makusudi yao mabaya akawaambia, " Enyi wanafiki, kwa nini mnajaribu kunitega ? 19Nionyesheni hiyo sarafu inayotumika kwa kulipia kodi. " Wakamletea dinari. 20 Naye akawauliza, "Sura hii na maandishi haya ni vya nani ?"

21Wakamjibu, ''Ni vya Kaisari.''

Basi Yesu akawaambia, ''Mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu.''

22Waliposikia hili, wakashangaa. Hivyo wakamwacha, wakaenda zao.

### *Ndoa Na Ufufuo*

23Siku hiyo hiyo Masadukayo, wale wasemao kwamba hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia Yesu na kumwuliza swali, wakisema, 24''Mwalimu, Mose alisema, 'Kama mtu akifa bila kuwa na watoto, ndugu yake amwoe huyo mjane ili ampatie watoto huyo nduguye aliyekufa. 25Basi palikuwa na ndugu saba miongoni mwetu. Yule wa kwanza akaoa mke, naye akafa na kwa kuwa hakuwa na watoto, akamwachia nduguye yule mjane. 26Ikatokea

vivyo hivyo kwa yule ndugu wa pili na wa tatu,
hadi wote saba. 27Hatimaye, yule mwanamke
naye akafa. 28Sasa basi, siku ile ya ufufuo, yeye
atakuwa mke wa nani miongoni mwa wale
ndugu saba, kwa kuwa wote walikuwa
wamemwoa huyo mwanamke?”

29Yesu akawajibu, “Mwapotoka kwa sababu
hamjui maandiko wala uweza wa Mungu.
30Wakati wa ufufuo watu hawataoa wala
kuolewa, bali watakuwa kama malaika wa
Mungu mbinguni. 31Lakini kuhusu ufufuo wa
wafu, hamjasoma kile Mungu alichowaambia
kwamba, 32 ‘Mimi ni Mungu wa Abrahamu,
Mungu wa Isaki na Mungu wa Yakobo?’ Yeye si
Mungu wa wafu bali ni Mungu wa walio hai.’’

33Ule umati wa watu uliposikia hayo,
ulishangaa sana kwa mafundisho yake.

### *Amri Kuu Kuliko Zote*

34Mafarisayo waliposikia kwamba Yesu
alikuwa amewanyamazisha Masadukayo,
Mafarisayo wakakusanyika pamoja. 35Mmoja
wao, mtaalam wa sheria, akamwuliza swali ili
kumjaribu, akisema, 36 “Mwalimu, ni amri ipi
katika Torati iliyo kuu kuliko zote?’’

37 Yesu akamjibu, “‘Mpende Bwana Mungu
wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako
yote na kwa akili zako zote.’ 38Hii ndio amri iliyo
kuu, tena ni ya kwanza. 39Nayo ya pili ni kama
hiyo, nayo ni hii: ‘Mpende jirani yako kama nafsi
yako.’ 40Amri hizi mbili ndizo msingi wa Torati
na manabii.’ ’’

### *Swali Kuhusu Mwana wa Daudi*

41Wakati Mafarisayo wakiwa
wamekusanyika pamoja, Yesu akawauliza,
42“Mnaonaje kuhusu Kristo [a]? Yeye ni mwana
wa nani?”

Wakamjibu, “Yeye ni mwana wa Daudi.’’

43Akawaambia, “Inakuwaje basi kwamba
Daudi akinena kwa Roho, anamwita Kristo
‘Bwana,’ kwa maana asema,

44“ ‘Bwana Mungu alimwambia Bwana wangu:
keti wewe mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako chini
ya miguu yako.’

45“Kama basi Daudi anamwita yeye ‘Bwana,’
awezaje kuwa mwanae?’’ 46Hakuna mtu
aliyeweza kumjibu Yesu neno. Tena tangu siku
hiyo hakuna aliyethubutu kumwuliza tena
maswali.

### *Yesu Awashutumu Walimu Wa Sheria Na Mafarisayo*

**23** Kisha Yesu akauambia ule umati wa watu
pamoja na wanafunzi wake:
2“Walimu wa sheria na Mafarisayo wameketi
katika kiti cha Mose, 3hivyo inawapasa kuwatii
na kufanya kila kitu wanachowaambia. Lakini
msifuate yale wanayotenda, kwa sababu
hawatendi yale wanayohubiri. 4Wao hufunga
mizigo mikubwa na kuiweka mabegani mwa
watu, lakini wao wenyewe hawako radhi hata
kuinua kidole ili kuisogeza.

5“Wao hufanya mambo yao yote ili
waonekane na watu. Vikasha vya ngozi vyenye
maandiko ya sheria na kurefusha matamvua ya
mavazi yao, 6wanapenda kukaa viti vya sehemu
za heshima karamuni na vile viti maalum sana
katika masinagogi, 7hupenda kusalimiwa
masokoni kutaka watu wawaite ‘Rabi [a]’.

8“Lakini ninyi msiitwe ‘Rabi’ kwa sababu
mnaye Bwana mmoja na ninyi nyote ni ndugu.
9Nanyi msimwite mtu ye yote ‘Baba’ hapa
duniani kwa maana mnaye Baba mmoja, naye
yuko mbinguni. 10Wala msiitwe ‘mwalimu’ kwa
maana mnaye mwalimu mmoja tu, ndiye Kristo.
11Yeye aliye mkuu kuliko ninyi nyote miongoni
mwenu atakuwa mtumishi wenu. 12Kwa kuwa
ye yote anayejikweza atashushwa, na ye yote
anayejinyenyekeza atakwezwa.

13“Lakini ole wenu, walimu wa sheria na
Mafarisayo, wanafiki! Kwa maana mnawafungia
watu milango ya Ufalme wa Mbinguni. Ninyi
wenyewe hamuingii humo, nao wale wanaotaka
kuingia mnawazuia. 14 “Ole wenu walimu wa
sheria na Mafarisayo, enyi wanafiki! Mnakula
katika nyumba za wajane, nanyi kwa kujifanya
kuwa wema, mnasali sala ndefu. Kwa hiyo
adhabu yenu itakuwa kubwa zaidi.’’

15“Ole wenu walimu wa sheria na
Mafarisayo, wanafiki! Ninyi mnasafiri baharini na
nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja ageuke na
kuwafuata ninyi, lakini baada ya kumpata,
mnamfanya mwana wa jehanamu mara mbili
kuliko ninyi!

16“Ole wenu, viongozi vipofu! Ninyi
mwasema, ‘Mtu akiapa kwa hekalu, kiapo hicho
si kitu, lakini mtu akiapa kwa dhahabu ya

a42 Kristo maana yake Masiya ,yaani Mpakwa(Aliyetiwa) Mafuta.’’

a7 Rabi maana yake bwana, mwalimu

hekalu, amefungwa kwa kiapo chake.’ 17Ninyi vipofu wapumbavu! Ni kipi kilicho kikuu zaidi, ile dhahabu au lile hekalu ambalo ndilo linaloifanya hiyo dhahabu kuwa takatifu? 18Pia mnasema, ‘Mtu akiapa kwa madhabahu, si kitu, lakini mtu akiapa kwa sadaka iliyo juu ya madhabahu, amefungwa kwa kiapo chake?’ 19Ninyi vipofu! Ni kipi kikuu zaidi, ile sadaka, au ile madhabahu ambayo ndiyo inayoifanya hiyo sadaka kuwa takatifu? 20 Kwa hiyo, mtu aapaye kwa madhabahu, huapa kwa hiyo madhabahu na vitu vyote vilivyo juu yake. 21Naye mtu aapaye kwa hekalu, huapa kwa hilo hekalu na kwa huyo akaaye ndani yake. 22Naye aapaye kwa mbingu, huapa kwa kiti cha enzi cha Mungu na kwa Yeye aketiye juu ya kiti hicho.

23“Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnatoa zaka ya mnanaa, bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu zaidi ya sheria, yaani, haki, huruma na uaminifu. Haya imewapasa kuyafanya bila kusahau hayo mengine. 24Ninyi viongozi vipofu, mnachuja kiroboto lakini mnameza ngamia!

25“Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnasafisha nje ya kikombe na kisahani, lakini ndani mmejaa unyang’anyi na kutokuwa na kiasi. 26Enyi Mafarisayo vipofu! Safisheni kwanza ndani ya kikombe na sahani, ndipo nje patakuwa safi.

27“Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Mnafanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, ambayo yanapendeza kwa nje lakini ndani yamejaa mifupa ya wafu na kila aina ya uchafu. 28Vivyo hivyo, kwa nje ninyi mnaonekana kwa watu kuwa wenye haki, lakini kwa ndani mmejaa unafiki na uovu.

29“Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Mnajenga makaburi ya manabii na kuyapamba makaburi ya wenye haki. 30Nanyi mwasema, ‘Kama tungaliishi wakati wa baba zetu, tusingalikuwa tumeshiriki katika kumwaga damu ya manabii!” 31Hivyo mnajishuhudia wenyewe kwamba ninyi ni wana wa wale waliowaua manabii. 32Haya basi, kijazeni kipimo cha dhambi ya baba zenu!

33“Ninyi nyoka, ninyi uzao wa nyoka wenye sumu! Mtaiepukaje hukumu ya jehanam? 34Kwa sababu hii tazama nawapelekea manabii na wenye hekima na walimu. Baadhi yao mtawaua na kuwasulibisha, wengine mtawapiga mijeledi katika masinagogi yenu na wengine mtawafuatia kutoka mji mmoja hadi mji mwingine. 35Hivyo ile damu ya wenye haki wote iliyomwagwa hapa duniani, tangu damu ya Abeli, ambaye alikuwa hana hatia, hadi damu ya Zekaria mwana wa Barakia, mliyemwua kati ya Patakatifu na madhabahu, itawajia juu yenu. 36Amin, nawaambieni, haya yote yatakuja juu ya kizazi hiki.’’

### *Yesu Aililia Yerusalemu*

37“Ee Yerusalemu, mnaowaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu! Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake, lakini hukutaka! 38Tazama nyumba yako imeachwa tupu na ukiwa. 39Kwa maana nawaambia, hamtaniona tena mpaka siku ile mtakaposema, ‘Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la Bwana.”

### *Kubomolewa Kwa Hekalu Kwatabiriwa*

**24** Yesu akatoka hekaluni na alipokuwa akienda zake, wanafunzi wake wakamwendea ili kumwonyesha majengo ya hekalu. 2Ndipo Yesu akawauliza, “Je, mnayaona haya yote? Amin, amin nawaambia, hakuna hata jiwe moja hapa litakalobaki juu ya jingine, kila moja litabomolewa.”

### *Ishara Za Nyakati Za Mwisho*

3Yesu alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamjia mahali pasipo na watu, wakamwuliza, “Tuambie, mambo haya yatatukia lini, nayo ni nini dalili za kuja kwako na za mwisho wa dunia?

4Yesu akawajibu, “Angalieni, mtu asiwadanganye. 5Kwa maana wengi watakuja kwa jina langu wakidai, ‘Mimi ndiye Kristo, nao watawadanganya wengi. 6Mtasikia habari za vita na matetesi ya vita,angalieni msitishike, kwa maana haya hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado. 7Taifa litainuka dhidi ya taifa na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa na njaa na matetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali. 8Haya yote yatakuwa ndio mwanzo wa utungu.

9“Ndipo mtasalitiwa, ili mteswe na kuuawa, nanyi mtachukiwa na mataifa yote kwa ajili yangu. 10Wakati huo, wengi wataacha imani yao, nao watasalitiana kila mmoja na mwenzake na kuchukiana. 11Watatokea manabii wengi wa uongo, nao watawadanganya watu wengi. 12Kwa sababu ya kuongezeka kwa uovu upendo

wa watu wengi utapoa, 13Lakini yule
atakayevumilia hadi mwisho ndiye
atakayeokoka. 14Injili ya Ufalme itahubiriwa
ulimwenguni pote, kuwa ushuhuda kwa mataifa
yote. Ndipo ule mwisho utakapokuja.

15Hivyo mtakapoona lile 'Chukizo la
Uharibifu' lililonenwa na nabii Danieli
limesimama mahali patakatifu, asomaye na
afahamu, 16Basi wale walioko Uyahudi
wakimbilie milimani. 17Ye yote aliyeko juu ya
paa la nyumba asishuke ili kuchukua cho chote
kutoka ndani ya nyumba. 18Yeye aliye
shambani na asirudi nyumbani kwenda
kuchukua vazi lake. 19Ole wa wenye mimba na
wenye watoto wachanga siku hizo! 20Ombeni ili
kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi au siku
ya Sabato. 21 Kwa maana wakati huo kutakuwa
na dhiki kuu ambayo haijapata kuwako tangu
mwanzo wa dunia mpaka sasa, wala
haitakuwako tena. 22Kama siku hizo
zisingelifupizwa, hakuna hata mtu mmoja
ambaye angeliokoka, lakini kwa ajili ya wateule
siku hizo zitafupizwa. 23Wakati huo kama mtu
ye yote akiwaambia, 'Tazama, huyu hapa ni
Kristo! Au 'Kristo yuko kule!' Msisadiki. 24Kwa
maana watatokea makristo wa uongo na
manabii wa uongo na kufanya ishara kubwa na
miujiza mingi ili kuwapotosha, hata ikiwezekana
wale wateule hasa. 25Angalieni, nimetangulia
kuwaambia mapema.

26"Kwa hiyo mtu ye yote akiwaambia, 'Yule
kule nyikani,' msiende huko. Au akisema, 'Yuko
kwenye chumba,' msisadiki. 27Kwa maana
kama vile umeme utokeavyo mashariki na
kuonekana hata magharibi, ndivyo itakavyokuwa
kuja kwake Mwana wa Adamu. 28Kwa maana
po pote ulipo mzoga, huko ndiko wakusanyikapo
tai.

### *Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*

29"Mara baada ya dhiki ya siku zile,

jua litatiwa giza,
nao mwezi hautatoa nuru yake,
nazo nyota zitaanguka kutoka angani
na nguvu za anga zitatikisika.'

30"Ndipo itakapotokea ishara ya Mwana wa
Adamu angani na makabila yote ya dunia
yataomboleza.. Nao watamwona Mwana wa
Adamu akija juu ya mawingu ya angani, katika
uwezo na utukufu mkuu. 31Naye atawatuma
malaika zake kwa sauti kuu ya tarumbeta, nao
watawakusanya wateule wake kutoka pande
zote nne za dunia, kutoka mwisho mmoja wa
mbingu hadi mwisho mwingine.

32"Jifunzeni kutokana na mtini. Matawi yake
yanapoanza kuwa laini na kuchipua majani,
fahamuni kwamba kiangazi kimekaribia. 33Hata
hivyo, mwonapo mambo hayo, jueni kwamba yu
karibu malangoni. 34 Amin, amin nawaambia,
kizazi hiki hakitapita hadi mambo haya yote
yawe yametimia. 35 Mbingu na dunia zitapita,
lakini maneno yangu hayatapita kamwe. "

### *Hakuna Ajuaye Siku Wala Saa*

36"Hakuna ajuaye siku wala saa, hata malaika
mbinguni hawajui wala Mwana, ila Baba peke
yake. 37Kama ilivyokuwa wakati wa Noa, ndivyo
itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.
38Kwa maana siku zile kabla ya gharika, watu
walikuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa,
mpaka siku ile Noa alipoingia kwenye safina,
39nao hawakujua lo lote mpaka gharika ilipokuja
ikawakumba wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa
atakapokuja Mwana wa Adamu. 40"Watu wawili
watakuwa shambani, mmoja atatwaliwa, mwingine
ataachwa. 41Wanawake wawili watakuwa
wanasaga pamoja, mmoja atatwaliwa, mwingine
ataachwa.

42"Kwa hiyo kesheni, kwa maana hamjui ni
siku gani atakapokuja Bwana wenu. 43"Lakini
fahamuni hili kwamba: Kama mwenye nyumba
angelijua ni wakati gani wa usiku ambao mwivi
anakuja, angelikesha na asingeliiacha nyumba
yake kuvunjwa. 44Kwa hiyo ninyi pia hamna
budi kuwa tayari, kwa sababu Mwana wa
Adamu atakuja saa msiyotazamia."

### *Mfano Wa Mtumishi Mwaminifu*

45"Ni nani basi aliye mtumishi mwaminifu na
mwenye busara ambaye bwana wake
amemweka kusimamia watumishi wengine
katika nyumba yake, ili awape chakula chao
kwa wakati muafaka? 46Heri mtumishi yule
ambaye bwana wake atakapokuja atamkuta
akifanya hivyo. 47 Amin, amin nawaambia,
atamweka mtumishi huyo kuwa msimamizi wa
mali yake yote. 48"Lakini kama huyo mtumishi ni
mwovu naye akasema moyoni mwake, 'Bwana
wangu atakawia muda mrefu,' 49naye kisha
akaanza kuwapiga watumishi wenzake na kula
na kunywa pamoja na walevi, 50bwana wa
mtumishi huyo atakuja siku ambayo mtumishi
huyo hamtazamii na saa ile ambayo haijui.
51Atamkata huyo mtumishi vipande vipande na

kumweka katika sehemu moja pamoja na wanafiki, mahali ambako kutakuwa ni kulia na kusaga meno."

### *Mfano Wa Wanawali Kumi*

**25** "Wakati huo, Ufalme wa Mbinguni utakuwa kama wanawali kumi waliochukua taa zao na kwenda kumlaki bwana arusi. 2 Watano wao walikuwa wapumbavu na watano walikuwa wenye busara. 3Wale wapumbavu walichukua taa zao lakini hawakuchukua mafuta ya akiba, 4lakini wale wenye busara walichukua taa zao na mafuta ya akiba kwenye vyombo. 5Bwana arusi alipokawia kuja wale wanawali wote wakasinzia na kulala.

6"Usiku wa manane pakawa na kelele: 'Tazameni, huyu hapa bwana arusi! Tokeni nje mkamlaki!'

7"Ndipo wale wanawali wote wakaamka na kuzitengeneza taa zao. 8Wale wapumbavu wakawaambia wale wenye busara, 'Tupatieni mafuta yenu kidogo, taa zetu zinazimika.'

9"Lakini wale wenye busara wakawajibu, 'Sivyo, hayatutoshi sisi na ninyi pia. Afadhali mwende kwa wauzao mkajinunulie mafuta yenu.

10"Nao walipokuwa wakienda kununua mafuta, bwana arusi akafika. Wale wanawali waliokuwa tayari, wakaingia ndani pamoja naye kwenye karamu ya arusi na mlango ukafungwa.

11"Baadaye wale wanawali wengine nao wakaja, wakaita, 'Bwana! Bwana! Tufungulie mlango!'

12"Lakini yeye bwana arusi akawajibu, 'Amin, amin nawaambia, siwajui ninyi!'

13"Kwa hiyo kesheni, kwa sababu hamjui siku wala saa."

### *Mfano wa Watumishi Watatu Walioachiwa Talanta*

14"Tena, Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu anayetaka kusafiri, akawaita watumishi wake na kuweka mali yake kwenye uangalizi wao. 15Mmoja akampa talanta tano [a] mwingine talanta mbili [b] na mwingine talanta moja [c], kila mmoja alipewa kwa kadiri ya uwezo wake. Kisha yeye akasafiri. 16"Yule aliyepewa talanta tano akaenda mara moja akafanya nazo biashara akapata talanta nyingine tano zaidi. 17Yule aliyepewa talanta mbili akafanya vivyo hivyo, akapata nyingine mbili zaidi. 18Lakini yule mtumishi aliyekuwa amepokea talanta moja,alikwenda akachimba shimo ardhini na kuificha ile fedha ya bwana wake.

19"Baada ya muda mrefu yule bwana wa wale watumishi akarudi na kufanya hesabu nao. 20Yule mtumishi aliyepokea talanta tano akaja,akaleta nyingine tano zaidi. Akasema, 'Bwana uliweka kwenye uangalizi wangu talanta tano. Tazama, nimepata faida talanta tano zaidi.'

21 "Bwana wake akamwambia, 'Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache, nitakuweka kuwa msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako!"

22"Yule mwenye talanta mbili naye akaja. Akasema, `Bwana, uliweka kwenye uangalizi wangu talanta mbili. Tazama nimepata hapa talanta mbili zaidi.'

23 Bwana wake akajibu, 'Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema na mwaminifu, umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache, nitakuweka kuwa msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako.'

24"Kisha yule mtumishi aliyepokea talanta moja akaja, akasema, 'Bwana, nilijua kwamba wewe ni mtu mgumu, unayevuna mahali usipopanda na kukusanya mahali usipotawanya mbegu. 25Kwa hiyo niliogopa, nikaenda, nikaificha talanta yako ardhini. Tazama, hii hapa ile iliyo mali yako.'

26"Bwana wake akajibu, 'Wewe mtumishi mwovu na mvivu! Ulijua kwamba ninavuna mahali nisipopanda na kukusanya mahali nisipotawanya mbegu. 27Vema basi, ingekupasa kuweka fedha yangu kwa watoa riba, nirudipo, nichukue ile iliyo yangu na faida yake?

28" 'Basi mnyang'anyeni hiyo talanta mkampe yule mwenye talanta kumi.' 29Kwa maana kila mtu mwenye kitu ataongezewa, naye atakuwa navyo tele. Lakini kwa mtu yule asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa.30"Nanyi mtupeni huyo mtumishi asiyefaa nje, kwenye giza, mahali ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.' "

### *Kondoo Na Mbuzi*

31"Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu wake na malaika wote watakatifu pamoja naye, ndipo atakapoketi juu ya kiti cha enzi cha utukufu wake. 32Mataifa yote

---

a15 Talanta tano ilikuwa na mshahara wa kibarua wa miaka 75 b15 Talanta mbili ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa miaka 30

c15 Talanta moja ilikuwa zaidi ya mshahara wa kibarua wa miaka kumi na mitano.

watakusanyika mbele zake, naye atawatenga kama mchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi.
33Atawaweka kondoo upande wake wa kuume na mbuzi upande wake wa kushoto.

34"Ndipo Mfalme atawaambia wale walioko upande wake wa kuume, 'Njoni, ninyi mliobarikiwa na Baba yangu, urithini Ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa
ulimwengu. 35Kwa maana nilikuwa na njaa mkanipa chakula, nilikuwa na kiu mkaninywesha, nilikuwa mgeni mkanikaribisha,
36nilikuwa uchi mkanivika, nilikuwa mgonjwa mkanitunza, nami nilikuwa kifungoni mkaja kunitembelea.'

37"Ndipo wale wenye haki watakapomjibu wakisema, 'Bwana, ni lini tulikuona una njaa tukakulisha au ukiwa na kiu tukakunywesha?
38Lini tulikuona ukiwa mgeni tukakukaribisha au
ukiwa uchi tukakuvika? 39Tena ni lini tulikuona ukiwa mgonjwa tukakutunza au ukiwa kifungoni tukakutembelea?'

40"Naye Mfalme atawajibu, 'Amin, amin ninawaambia, kwa jinsi mlimvyotendea mmojawapo wa hawa ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi.'

41 "Kisha atawaambia wale walio upande Wake wa kushoto, 'Ondokeni kwangu, ninyi mliolaaniwa, nendeni kwenye moto wa milele alioandaliwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake.
42Kwa maana nilikuwa na njaa hamkunipa chakula, nilikuwa na kiu hamkuninywesha,
43nilikuwa mgeni nanyi hamkunikaribisha, nilikuwa uchi hamkunivika, nilikuwa mgonjwa hamkunitunza na nilikuwa gerezani nanyi hamkuja kunitembelea.'

44"Ndipo wao pia watajibu, 'Bwana ni lini tulikuona ukiwa na njaa au kiu, au ukiwa mgeni au uchi , au ukiwa mgonjwa na kifungoni na hatukukuhudumia?'

45"Naye atawajibu, 'Amin, amin nawaambia, kwa jinsi ambavyo hamkumtendea mmojawapo wa hawa ndugu zangu walio wadogo, hamkunitendea mimi.'

46"Ndipo hawa watakapoingia kwenye adhabu ya milele, lakini wale wenye haki wataingia katika uzima wa milele."

### *Shauri Baya La Kumwua Yesu*

**26** Yesu alipomaliza kusema hayo yote,
akawaambia wanafunzi wake, 2"Mnajua kwamba baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, naye Mwana wa Adamu atasalitiwa ili asulibiwe."

3 Basi viongozi wa makuhani na wazee wa watu wakakusanyika katika jumba la utawala la kuhani mkuu, jina lake Kayafa. 4Wakafanya shauri ili kumkamata Yesu kwa siri na kumwua.
5Lakini wakasema, "Isiwe wakati wa sikukuu, la sivyo kutakuwa na ghasia miongoni mwa watu."

### *Yesu Anapakwa Mafuta Huko Bethania*

6 Wakati Yesu akiwa Bethania nyumbani mwa Simoni aliyekuwa na ukoma, 7mwanamke mmoja alimjia akiwa na chupa ya marmar yenye manukato ya thamani kubwa, akayamimina kichwani mwa Yesu alipokuwa ameketi mezani kula chakula.

8Lakini wanafunzi wake walipoona hayo wakakasirika, wakasema, "Kwa nini ubadhirifu
huu wote? 9Manukato haya yangeliuzwa kwa bei kubwa na fedha hizo wakapewa maskini."

10Yesu akijua jambo hili, akawaambia, "Mbona mnamsumbua huyu mwanamke? Yeye
amenitendea jambo zuri sana. 11Maskini mtakuwa nao siku zote, lakini mimi hamtakuwa
nami siku zote. 12Alipomiminia haya manukato kwenye mwili amefanya hivyo ili kuniandaa kwa
ajili ya maziko yangu. 13Ninawaambia kweli, mahali po pote habari njema itakapohubiriwa ulimwenguni mwote, jambo hili alilofanya litatajwa pia, kwa ukumbusho wake."

### *Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*

14Kisha mmojawapo wa wale kumi na wawili, yeye aitwaye Yuda Iskariote, alikwenda
kwa viongozi wa makuhani 15na kuuliza, "Mtanipa nini nikimtia Yesu mikononi mwenu? Wakamlipa vipande thelathini vya fedha.
16Tangu wakati huo Yuda akawa anatafuta wasaa mzuri wa kumsaliti Yesu.

### *Yesu Ala Pasaka Pamoja Na Wanafunzi*

17Siku ya kwanza ya Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu wanafunzi walimjia Yesu wakamwuliza, "Unataka tuandae wapi kwa ajili yako ili kuila Pasaka?"

18Akajibu, "Nendeni kwa mtu fulani huko mjini mkamwambie, 'Mwalimu asema hivi: saa yangu imekaribia, nitaiadhimisha Pasaka pamoja na wanafunzi wangu katika nyumba
yako.' " 19Hivyo wanafunzi wakafanya kama vile Yesu, alivyokuwa amewaelekeza, nao wakaandaa Pasaka.

20Ilipofika jioni, Yesu alikuwa ameketi
mezani pamoja na wale kumi na wawili. 21Nao
walipokuwa wakila, Yesu akasema, "Amin, amin

nawaambia, mmoja wenu atanisaliti.''

22Wakahuzunika sana, wakaanza kumwambia mmoja mmoja, ''Je, ni mimi Bwana?''

23Yesu akawaambia, ''Yule aliyechovya mkono wake katika bakuli pamoja nami, ndiye atakayenisaliti. 24Mwana wa Adamu yu aenda kama alivyoandikiwa. Lakini ole wake mtu yule amsalitie Mwana wa Adamu. Ingeliwakuwa bora kwake kama asingalizaliwa ! ''

25Kisha Yuda, yule aliyemsaliti akasema, ''Kweli si mimi, Rabi?''

Yesu akajibu, ''Naam, wewe mwenyewe umesema.''

### *Kuanzishwa Kwa Meza ya Bwana*

26Walipokuwa wanakula, Yesu akachukua mkate, akashukuru, akaumega, akawapa wanafunzi wake akisema, ''Twaeni, mle, huu ndio mwili wangu.''

27Kisha akachukua kikombe, akashukuru, akawapa akisema, ''Kunyweni nyote katika kikombe hiki. 28Hii ndiyo damu yangu ya agano, ile imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. 29 Lakini ninawaambia, tangu sasa sitakunywa tena kutoka katika uzao huu wa mzabibu, mpaka siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba yangu.''

30Walipokwisha kuimba wimbo, wakatoka kwenda mlima wa Mizeituni.

### *Yesu Atabiri Petro Kumkana*

31Kisha Yesu akawaambia, "Usiku wa leo ninyi nyote mtaniacha, kwa maana imeandikwa:

" 'Nitampiga mchungaji,
nao kondoo wa hilo
kundi watatawanyika.'

32Lakini baada ya mimi kufufuka, nitawatangulia kwenda Galilaya.''

33Petro akajibu "Hata kama wote watakuacha, kamwe mimi sitakuacha.''

34 Yesu akajibu, "Amin, amin ninakuambia, usiku huu huu, kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu.''

35Lakini Petro akasema, ''Hata kama itabidi kufa pamoja na Wewe, kamwe sitakukana.'' Nao wanafunzi wengine wote wakasema vivyo hivyo.

### *Yesu Anaomba Gethsemane*

36Kisha Yesu akaenda pamoja na wanafunzi wake mpaka kwenye bustani iitwayo Gethsemane, akawaambia, "Kaeni hapa wakati ninakwenda kule kuomba.'' 37Akamchukua Petro pamoja na wale wana wawili wa Zebedayo, naye akaanza kuhuzunika na kufadhaika. 38Kisha Yesu akawaambia, "Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe pamoja nami.''

39Akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi akaomba, akisema, "Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki na kiniepuke, lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo Wewe.''

40Kisha akarudi kwa wanafunzi wake na kuwakuta wamelala. Akamwuliza Petro, "Je, ninyi wanaume, hamkuweza kukesha pamoja nami kwa saa moja? 41''Kesheni na mwombe, msije mkaanguka majaribuni. Hakika roho iko radhi lakini mwili ni dhaifu.''

42Akaenda tena mara ya pili na kuomba, "Baba yangu, kama ikiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisikinywe, mapenzi yako yafanyike.''

43Aliporudi, akawakuta tena wamelala kwa sababu macho yao yalikuwa mazito. 44Hivyo akawaacha akaenda zake tena mara ya tatu na kuomba akisema maneno yale yale.

45Kisha akarudi kwa wanafunzi wake akawaambia, ''Bado mmelala na kupumzika? Tazameni, saa imefika ambapo Mwana wa Adamu hana budi kutiwa mikononi mwa wenye dhambi. 46Inukeni, twendeni zetu ! Huyu hapa yule anisalitiye! ''

### *Yesu Akamatwa*

47Alipokuwa bado anasema, Yuda, mmojawapo wa wale Kumi na Wawili, akafika, akiwa amefuatana na umati mkubwa wa watu wenye panga na marungu waliokuwa wametumwa na viongozi wa makuhani na wazee wa watu. 48Basi msaliti alikuwa amewapa hao watu ishara kwamba: ''Yeye nitakayembusu ndiye, mkamateni.'' 49Mara akamjia Yesu na kumsalimu, "Salaam, Rabi!'' Akambusu.

50Yesu akamwambia, "Rafiki, fanya kile ulichokuja kufanya hapa.

Kisha wale watu wakasogea mbele, wakamkamata Yesu. 51Ghafula mmoja wa wale waliokuwa na Yesu alipoona hivyo, akaushika upanga wake, akauchomoa na kumpiga mtumishi wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio.

52Ndipo Yesu akamwambia, "Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga. 53Je,

unadhani siwezi kumwomba Baba yangu naye mara moja akaniletea zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? 54Lakini je, maandiko yatatimiaje yale yasemayo kwamba ni lazima itokee hivi?"

55Wakati huo Yesu akawaambia ule umati wa watu, "Mmetoka na panga na marungu kuja kunikamata kama vile mimi ni mnyang'anyi? Siku kwa siku niliketi hekaluni nikifundisha, mbona hamkunikamata? 56Lakini haya yote yametukia ili maandiko ya manabii yapate kutimia." Ndipo wanafunzi wake wote wakamwacha na kukimbia.

### *Yesu Mbele Ya Kuhani Mkuu*

57Wale waliokuwa wamemkamata Yesu wakampeleka kwa Kayafa, Kuhani Mkuu, mahali ambapo walimu wa sheria pamoja na wazee walikuwa wamekusanyika. 58Lakini Petro akamfuata kwa mbali mpaka uani kwa Kuhani Mkuu. Akaingia ndani akaketi pamoja na walinzi ili aone litakalotukia.

59Basi viongozi wa wazee, makuhani na baraza lote wakatafuta ushahidi wa uongo dhidi ya Yesu ili wapate kumua. 60Lakini hawakupata jambo lo lote, ingawa mashahidi wengi wa uongo walijitokeza.

Hatimaye wakajitokeza mashahidi wawili wa uongo 61na kusema : "Huyu mtu alisema, 'Nina weza kulivunja hekalu la Mungu na kulijenga tena kwa siku tatu .' "

62Kisha Kuhani Mkuu akasimama na kumwambia Yesu, "Je, wewe hutajibu? Ni ushahidi wa namna gani hawa watu wauletao dhidi yako?" 63Lakini Yesu alikuwa kimya.

Ndipo Kuhani Mkuu akamwambia, "Nakuapisha mbele za Mungu aliye hai, tuambie ikiwa wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu."

64Yesu akajibu, "Wewe umenena. Lakini ninawaambia nyote, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenye Nguvu na akija juu ya mawingu ya mbinguni.''

65Ndipo Kuhani Mkuu akararua nguo zake na kusema, "Amekufuru! Kwa nini tunahitaji ushahidi zaidi? Tazama, sasa ninyi mmesikia hayo makufuru· 66 Uamuzi wenu ni nini?"

Wakajibu, ''Anastahili kufa "

67Kisha wakamtemea mate usoni na wengine wakampiga ngumi. Wengine walimpiga makofi 68na kusema, "Tutabirie, wewe Kristo! Ni nani aliyekupiga?"

### *Petro Amkana Bwana Yesu*

69Wakati huu Petro alikuwa amekaa nje uani. Mtumishi mmoja wa kike akamjia na kumwambia, "Wewe pia ulikuwa pamoja na Yesu wa Galilaya.''

70Lakini Petro akakana mbele yao wote akisema, "Sijui hilo usemalo.''

71Alipotoka nje kufika kwenye lango, mtumishi mwingine wa kike alimwona, akawaambia watu waliokuwapo, "Huyu mtu alikuwa pamoja na Yesu Mnazareti.''

72 Akakana tena kwa kiapo akisema, "Mimi simjui huyo!''

73Baada ya muda mfupi wale waliokuwa wamesimama pale wakamwendea Petro wakamwambia, "Hakika wewe ni mmoja wao kwa maana ile namna yako ya kusema ni kama yao."

74Ndipo Petro akaanza kujilaani na kuwaapia, Mimi simjui mtu huyo!''

Papo hapo jogoo akawika. 75Ndipo Petro akakumbuka lile neno alilokuwa amesema Yesu "Kabla jogoo hajawika utanikana mara tatu.'' Akaenda nje, akalia sana.

### *Yesu Aletwa Mbele Ya Pilato*

**27** Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani wote na wazee wa watu wakafanya shauri pamoja dhidi ya Yesu ili kumwua. 2Wakamfunga, wakampeleka na kumkabidhi kwa Pilato, ambaye alikuwa mtawala.

### *Yuda Ajinyonga*

3Yuda, ambaye ndiye aliyekuwa amemsaliti Yesu, alipoona kuwa Yesu amehukumiwa, akajuta na akarudisha vile vipande thelathini vya fedha alivyopewa na viongozi wa makuhani na wazee wa watu. 4Akasema, "Nimetenda dhambi, kwa maana nimeisaliti damu isiyo na hatia."

5Basi Yuda akavitupa vile vipande vya fedha ndani ya hekalu akaondoka akaenda na kujinyonga.

6Wale makuhani wakuu wakazichukua zile fedha wakasema, ''Si halali kuchanganya fedha hizi na sadaka kwa sababu hizi ni fedha zenye damu.'' 7 Kwa hiyo baada ya kushauriana, waliamua kuvitumia kununulia shamba la mfinyanzi, liwe mahali pa kuzikia wageni. 8 Hii ndiyo sababu lile shamba likaitwa, 'Shamba la Damu' hadi leo. 9Ndipo likatimia lile lililonenwa na nabii Yeremia kwamba, ''Walichukua vile

vipande thelathini vya fedha, thamani aliyopangiwa na watu wa Israeli, [10]wakanunulia shamba la mfinyanzi, kama vile Bwana alivyoniagiza.''

### *Yesu Mbele Ya Pilato*

[11]Wakati Yesu akiwa amesimama mbele ya mtawala, mtawala akamwuliza, "Wewe ndiye mfalme wa Wayahudi?''

Yesu akasema, "Wewe wasema hivyo.''

[12]Lakini viongozi wa makuhani na wazee walipomshtaki, hakujibu neno. [13]Ndipo Pilato akamwuliza, "Je, husikii ni mambo mangapi wanayokushtaki nayo?'' [14]Lakini Yesu hakumjibu hata kwa shtaka moja,kiasi kwamba mtawala alishangaa sana.

[15]Basi ilikuwa ni desturi ya mtawala kumfungua mfungwa mmoja atakayechaguliwa na umati wa watu wakati wa sikukuu. [16]Wakati huo alikuwapo mfungwa mmoja mwenye sifa mbaya, aliyeitwa Baraba. [17]Hivyo umati wa watu walipokusanyika, Pilato akawauliza, "Mnataka niwafungulie nani, Baraba au Yesu Yeye aitwaye Kristo?'' 18Kwa kuwa alitambua Yesu alikuwa amekabidhiwa kwake kwa ajili ya wivu.

[19]Pilato akiwa ameketi kwenye kiti cha hukumu, mkewe akampelekea ujumbe huu: " Usiwe na jambo lo lote juu ya huyu Mtu asiye na hatia, kwa kuwa leo nimeteseka sana katika ndoto kwa sababu Yake."

[20]Lakini viongozi wa makuhani na wazee wakaushawishi ule umati wa watu kwamba waombe Baraba afunguliwe na Yesu auawe.

[21] Mtawala akawauliza tena, "Ni yupi kati ya hawa wawili mnayetaka niwafungulie?"

Wakajibu, "Baraba''

[22]Pilato akawaambia, "Basi nifanye nini na huyu Yesu aitwaye Kristo?''

Wakajibu wote , "Msulibishe!''

[23]Pilato akauliza, "Kwa nini? Amefanya kosa gani?''

Lakini wao wakazidi kupiga kelele, "Msulibishe.''

[24]Pilato alipoona kwamba hawezi kufanya lo lote, lakini badala yake ghasia zilikuwa zinaanza, akachukua maji, akanawa mikono yake mbele ya ule umati wa watu, akasema. "Sina hatia juu ya damu ya mtu huyu. Hili ni jukumu lenu!"

[25]Watu wote wakajibu, ''Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu!''

[26]Basi akawafungulia Baraba, na baada ya kumchapa Yesu mijeledi, akamtoa ili asulibiwe.

### *Askari Wamdhihaki Yesu*

[27]Kisha askari wa mtawala wakampeleka Yesu kwenye Praitorio [a] na wakakusanya kikosi kizima cha askari kumzunguka. [28] Wakamvua nguo Zake na kumvika vazi la rangi nyekundu, kisha [29]wakasokota taji ya miiba wakaiweka kichwani pake. Wakamwekea fimbo katika mkono wake wa kuume, wakapiga magoti mbele zake na kumdhihaki wakisema "Salaam, mfalme wa Wayahudi!'' 30Wakamtemea mate, wakachukua ile fimbo wakampiga kichwani tena na tena. 31Baada ya kumdhihaki, wakamvua lile vazi , wakamvika tena nguo Zake. Kisha wakampeleka ili kumsulibisha.

### *Yesu Asulibishwa*

[32]Walipokuwa wakienda, wakakutana na mtu mmoja kutoka Kirene, jina lake Simoni, nao wakamlazimisha kuubeba ule msalaba.
[33]Wakafika mahali paitwapo Golgotha, (ambayo maana yake ni, Mahali pa Fuvu la Kichwa),
[34]wakampa Yesu divai iliyochanganywa na nyongo ili anywe, lakini alipoionja, akakataa kuinywa. [35]Walipokwisha kumsulibisha wakagawana mavazi Yake kwa kuyapigia kura, ili litimie lile neno lililonenwa na nabii, 'Waligawa nguo zangu miongoni mwao na vazi langu wakalipigia kura. [36]Kisha wakaketi, wakamchunga. [37]Juu ya kichwa chake, kwenye msalaba, wakaandika shtaka lake: 'HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI.'
[38]Wanyang'anyi wawili walisulibiwa pamoja naye, mmoja kuume Kwake na mwingine kushoto Kwake. [39]Watu waliokuwa wakipita njiani wakamvurumishia matukano huku wakatikisa vichwa vyao [40]na kusema, "Wewe ambaye utalivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe basi! Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani.''

[41]Vivyo hivyo, viongozi wa , makuhani, walimu wa sheria na wazee wakamdhihaki wakisema, [42] "Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe!. Yeye ni Mfalme wa Israeli! Ashuke sasa kutoka msalabani, tutamwamini.
[43]Anamwamini Mungu, basi Mungu na amwokoe sasa kama anamtaka, kwa maana alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.' " [44]Hata

---

a[27]Praitoria maana yake makao makuu ya mtawala. Jumba la kifalme lilokuwa linakaliwa na Pontio Pilato huko Yerusalemu, palipokuwa na kiti cha hukumu

wale wanyang'anyi waliosulibiwa pamoja naye wakamtukana vivyo hivyo.

### *Kifo Cha Yesu*

45Tangu saa sita hadi saa tisa giza lilifunika nchi yote. 46Ilipofika saa tisa Yesu akapaza sauti akalia, "Eloi, Eloi lama sabakthani?'' Maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?''

47Baadhi ya wale watu waliokuwa wamesimama pale waliposikia haya, wakasema ''Anamwita Eliya,''

48Ghafula mmoja wao akaenda mbio na kuleta sifongo akaichovya kwenye siki, akaiweka kwenye mwanzi akampa Yesu ili
anywe. 49Wengine wakasema, "Mwacheni na tuone kama Eliya atakuja kumwokoa.''

50Yesu alipolia tena kwa sauti kuu, akakata roho.

51Wakati huo huo pazia la hekalu likachanika vipande viwili, kuanzia juu hadi chini. Dunia ikatetemeka na miamba ikapasuka.
52Makaburi yakafunguka na miili ya watakatifu
waliokuwa wamekufa ikafufuka. 53Wakatoka makaburini na baada ya Yesu kufufuka waliingia kwenye Mji Mtakatifu na kuwatokea watu wengi.

54Basi yule jemadari na wale waliokuwa pamoja naye wakimlinda Yesu walipoona lile tetemeko na yale yote yaliyokuwa yametukia, wakaogopa wakasema, "Hakika huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu!''

55Walikuwako wanawake huko, wakiangalia kwa mbali. Hawa walikuwa wamemfuata Yesu tangu Galilaya ili kushughulika na mahitaji yake.
56Miongoni mwao walikuwapo Maria Magdalena, Maria mama yake Yakobo na Yosefu na mama yao wana wa Zebedayo.

### *Maziko Ya Yesu*

57Ilipofika jioni, alifika mtu mmoja tajiri kutoka Arimathea aitwaye Yosefu, ambaye pia
alikuwa mwanafunzi wa Yesu. 58Akamwendea Pilato, kumwomba mwili wa Yesu. Pilato
akaamuru apewe. 59Yosefu akauchukua mwili wa Yesu, akauviringishia nguo ya kitani safi
nyeupe 60 na kuuzika kwenye kaburi lake mwenyewe jipya alilokuwa amelichonga kwenye
mwamba. 61Maria Magdalene na yule Maria mwingine walikuwapo mahali pale, wakiwa wameketi mkabala na kaburi. Kisha akavingirisha jiwe kubwa mlangoni mwa kaburi na akaenda zake.

### *Walinzi Pale Kaburini*

62Kesho yake, yaani siku iliyofuata ile ya Maandalizi ya Sabato, viongozi wa makuhani na
Mafarisayo wakamwendea Pilato 63na kusema, "Bwana, tumekumbuka kwamba yule mdanganyifu kabla hajafa alisema, 'Baada ya
siku tatu nitafufuka.' 64Kwa hiyo uamuru kaburi lilindwe kwa uthabiti mpaka baada ya siku tatu. La sivyo, wanafunzi wake wanaweza kuja kuuiba mwili wake na kuwaambia watu kwamba amefufuka kutoka kwa wafu. Udanganyifu huu wa mwisho utakuwa mbaya kuliko ule wa kwanza."

65Pilato akawaambia, "Ninyi mnao askari Walinzi. Nendeni, liwekeeni ulinzi kadiri
mwezavyo". 66Kwa hiyo wakaenda na walinzi ili kulilinda kaburi kwa uthabiti, wakatia mhuri kwenye lile jiwe na kuweka ulinzi.

### *Yesu Afufuka*

**28** Baada ya Sabato, alfajiri mapema siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalene na yule Maria mwingine walikwenda kulitazama kaburi.

2Ghafula pakawa na tetemeko kubwa la ardhi, kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni akaenda penye kaburi
akalivingirisha lile jiwe na kulikalia. 3Sura ya huyo malaika ilikuwa kama umeme na mavazi
yake yalikuwa meupe kama theluji. 4Wale walinzi wa kaburi walimwogopa sana, wakatetemeka hata wakawa kama wafu.

5Yule malaika akawaambia wale wanawake, "Msiogope.kwa maana ninajua kuwa mnamtafuta
Yesu aliyesulibiwa. 6Hayupo hapa, kwa kuwa amefufuka, kama vile alivyosema. Njoni
mpatazame mahali alipokuwa amelazwa. 7Kisha nendeni upesi mkawaambie wanafunzi Wake kwamba, 'Amefufuka kutoka kwa wafu, naye awatangulia kwenda Galilaya. Huko ndiko mtakakomwona. Sasa nimekwisha kuwaambia."

8Hivyo wale wanawake wakaondoka pale kaburini, wakiwa wamejawa na hofu lakini wenye furaha nyingi, wakaenda mbio ili kuwaeleza wanafunzi Wake habari hizo.
9Ghafula Yesu akakutana nao, akasema, "Salaam!" Wale wanawake wakamkaribia wakaishika miguu Yake, wakamwabudu.
10Ndipo Yesu akawaambia, "Msiogope. Nendeni mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona.''

### *Taarifa Ya Walinzi*

11Wakati wale wanawake wakiwa njiani
wakienda, baadhi ya wale askari waliokuwa
wakilinda kaburi walienda mjini na kuwaeleza
viongozi wa makuhani kila kitu kilichokuwa
kimetukia. 12Baada ya viongozi wa makuhani
kukutana na wazee na kutunga hila, waliwapa
wale askari kiasi kikubwa cha fedha
13wakiwaambia, “Inawapasa mseme,
‘Wanafunzi Wake walikuja wakati wa usiku na
kumwiba sisi tulipokuwa tumelala.’ 14Kama
habari hizi zikimfikia mtawala, sisi
tutamwondolea mashaka nanyi hamtapata tatizo
lo lote. 15Kwa hiyo wale askari wakazipokea
hizo fedha nao wakafanya kama
walivyoelekezwa. Habari hii imeenea miongoni
mwa Wayahudi mpaka leo.

### *Yesu Awatuma Wanafunzi Wake*

16Basi wale wanafunzi kumi na mmoja
wakaenda hadi Galilaya kwenye ule mlima
ambao Yesu alikuwa amewaagiza.
17Walipomwona, wakamwabudu, lakini baadhi
yao wakaona shaka. 18Yesu akawajia na
kusema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na
duniani. 19Kwa sababu hii, enendeni
ulimwenguni mkawafanye mataifa yote kuwa
wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la
Mwana na la Roho Mtakatifu, 20nanyi
wafundisheni kuyashika mambo yote
niliyowaamuru ninyi. Hakika Mimi niko pamoja
nanyi sikuzote, hadi mwisho wa nyakati.’’ Amen.

# MARKO

### *Utangulizi:*

Marko ambaye aliitwa Yohana Marko alifuatana na Mtume Paulo katika safari zake za kitume.Huyu ndiye anayetajwa na mababa wa kanisa Papiass, Irenio na Klement wa Aleksandria kuwa mshirika wa karibu sana wa Mtume Petro.Uhusiano huu wa karibu na Petro umeonyeshwa katika*(1Pet..5:13),* pale ambapo Petro anamtaja Marko kama “mwanawe.” Hatimaye aliishi Rumi ambako aliandika kumbukumbu za Mtume Petro. Kwa hiyo Injili ya Marko inawakilisha maneno ya mtu aliyeshuhudia kwa macho yake mwenyewe juu ya maisha ya Yesu yanayoelezwa katika Injili hii.

Yohana Marko ni mtoto wa Maria ambaye nyumbani kwao kulikuwa Yerusalemu, ambako kunaonekana kuwa kituo kikuu cha Ukristo *(Mdo. 12: 12).* Marko alisafiri na Barnaba ambaye ni mjomba wake mpendwa *(Mdo. 4:36 -37 )* kwenda Antiokia ya Syria*(Mdo 12:25)* ambako walifuatana na Paulo kwenye safari yake ya kwanza ya kitume.Marko hata hivyo aliwaacha Barnaba na Paulo huko Kipro na kurudi Yerusalemu *(Mdo 13:13)*. Baadaye Barnaba na Marko walielekea Kipro wakati Paulo akienda Asia.
Miaka kumi baadaye *( 60 B.K)* Marko alikuwa pamoja na Paulo huko Rumi *(2Tim.4:11; Kol.4:10.)*

Shabaha ya Marko ilikuwa ni kukusanya pamoja ujumbe wote wa Injili. Kwa sababu hii, Injili ya Marko inakazia zaidi matendo ya Yesu kuliko maneno Yake. Pia Injili hii inatumia nafasi kubwa kueleza matukio ya juma la mwisho la maisha ya Bwana Yesu. Marko anaanza kwa kueleza habari za huduma ya Bwana Yesu hadharani na juu ya kuhubiri Kwake kuhusu Habari Njema ya Ufalme wa Mungu. Kisha anatoa unabii wazi kuhusu matazamio ya kifo cha Bwana Yesu *(Mk. 8:31;9:31;10:33-34,45).* Hatimaye anaeleza jinsi Bwana Yesu alivyosulibiwa msalabani kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, kufufuka Kwake kutoka kwa wafu, kuonekana Kwake na wanafunzi Wake baada ya kufufuka, maneno na maagizo Yake ya mwisho na kupaa Kwake kwenda mbinguni.

### *Tarehe*

Inawezekana ni katika wakati huu wa uhai wa Petro, au muda mfupi tu baada ya kifo chake *(55-65 B.K.),* ambao Marko aliandika Injili hii yenye kuchukua jina lake.

### *Wazo Kuu*

Marko anamdhihirisha Bwana Yesu kuwa ni Mtumishi wa Mungu, Mtu wa vitendo, aliyekuja kutimiza mapenzi ya Mungu. Marko anaonyesha waziwazi huduma ya Yesu na utendaji Wake wa miujiza, uponyaji Wake, mamlaka Yake juu ya pepo wachafu na nguvu Zake, Bwana Yesu alithibitishwa kuwa si mtumishi wa kawaida bali kwamba kwa hakika alikuwa Mwana wa Mungu. Ufufuo wa Yesu ulithibitisha yale yote aliyotenda na sasa tunangojea kurudi Kwake kwa utukufu, kutoka mbinguni. Marko aliandika Injili hii ili pia kuwatia moyo Wakristo walioishi Rumi wakati wa mateso.

### *Mgawanyo*

- Yohana Mbatizaji na ubatizo wa Bwana Yesu (1:1-13)
- Huduma ya Yesu Galilaya (1:14-9:50)
- Safari ya kwenda Yerusalemu na kuingia mjini (10:1-11:25[26])
- Matatizo mjini Yerusalemu (11:27-12:44)
- Unabii kuhusu mambo yajayo (13:1 -37)
- Kufa kwa Yesu na kufufuka kwake. (14:1-16:8[9-20]).

### *Mahubiri Ya Yohana Mbatizaji*

1 Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa
Mungu.

2Kama ilivyoandikwa katika nabii Isaya,

"Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele
yako, yeye
atakayeitengeneza njia yako."
3"Sauti ya mtu aliaye nyikani.
'Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni
mapito Yake.' "
'Itengenezeni njia ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.' "

4Yohana alikuja, akibatiza huko nyikani, akihubiri
ubatizo wa toba kwa ajili ya ondoleo la dhambi.
5Watu kutoka Uyahudi wote na sehemu zote za
Yerusalemu walikuwa wakimwendea, naye
akawabatiza katika mto Yordani, wakitubu dhambi
zao. 6Yohana alivaa mavazi yaliyotengenezwa
kwa singa za ngamia na mkanda wa ngozi kiunoni
mwake. Chakula chake kilikuwa nzige na asali ya
mwitu. 7Naye alihubiri akisema, "Baada yangu
atakuja Yeye aliye na uwezo kuliko mimi, ambaye
sistahili hata kuinama na kulegeza ukanda wa
viatu vyake. 8Mimi nawabatiza kwa maji, lakini
Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu."

### *Ubatizo Wa Yesu*

9Wakati huo Yesu akaja kutoka Nazareti ya
Galilaya, naye akabatizwa na Yohana katika Mto
Yordani. 10Yesu alipokuwa akitoka ndani ya maji,
aliona mbingu zikifunguka na Roho akishuka juu
Yake kama huwa. 11Nayo sauti kutoka mbinguni
ikasema, "Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa
Wangu, ambaye nimependezwa Nawe."

### *Majaribu Ya Yesu*

12Wakati huo huo, Roho akamwongoza Yesu
kwenda nyikani, 13naye akawa huko nyikani kwa
muda wa siku arobaini, akijaribiwa na Shetani.
Alikaa na wanyama wa mwituni na malaika
wakimhudumia.

### *Yesu Aanza Kuhubiri*

14Baada ya Yohana kukamatwa na kutiwa
gerezani, Yesu aliingia Galilaya akaanza kuhubiri
Habari Njema za Mungu, 15akisema, "Wakati
umewadia, Ufalme wa Mungu umekaribia. Tubuni
na kuiamini Habari Njema."

### *Yesu Awaita Wanafunzi Wanne*

16Yesu alipokuwa akitembea kando-kando ya
Bahari ya Galilaya alimwona Simoni na Andrea
nduguye wakizitupa nyavu zao baharini, kwa
kuwa hawa wawili walikuwa wavuvi. 17Yesu
akawaambia, "Njoni nifuateni, nami nitawafanya
kuwa wavuvi wa watu." 18Mara wakaacha nyavu
zao, wakamfuata Yesu.

19Alipokwenda mbele kidogo, akamwona
Yakobo mwana wa Zebedayo na Yohana
nduguye, wakiwa kwenye mashua yao
wakizitengeneza nyavu zao. 20Papo hapo
akawaita, nao wakamwacha Zebedayo baba yao
kwenye mashua pamoja na watumishi wa
kuajiriwa, nao wakamfuata Yesu.

### *Yesu Amtoa Pepo Mchafu*

21Wakaenda mpaka Kapernaumu. Ilipofika
siku ya Sabato, mara Yesu akaingia kwenye
sinagogi akaanza kufundisha. 22Watu
wakashangaa sana mafundisho yake, kwa maana
aliwafundisha kama Yeye aliye na mamlaka, wala
si kama walimu wa sheria. 23Wakati huo huo,
palikuwa na mtu kwenye sinagogi lao aliyekuwa
amepagawa na pepo mchafu, 24naye alikuwa
akapiga kelele akisema, "Tuna nini nawe, Yesu
wa Nazarethi? Je, umekuja kutuangamiza?
Nakujua Wewe ni nani, Wewe ndiwe Mtakatifu wa
Mungu!"

25Lakini Yesu akamkemea, akamwambia,
"Nyamaza kimya! Nawe Umtoke!" 26 Yule pepo
mchafu akamtikisa-tikisa sana huyo mtu kwa
nguvu akipiga kelele kwa sauti kubwa, kasha
akamtoka.

27Watu wote wakashangaa, hata kuulizana
wao kwa wao, "Haya ni mambo gani? Ni
mafundisho mapya, tena yenye mamlaka!
Anaamuru hata pepo wachafu nao wanamtii!"
28Sifa Zake zikaanza kuenea kwa upesi katika
eneo lote la karibu na Galilaya.

### *Yesu Amponya Mama Mkwe Wa Simoni*

29Mara walipotoka katika sinagogi,
walikwenda pamoja na Yakobo na Yohana hadi
nyumbani kwa Simoni na Andrea. 30Mama mkwe
wake Simoni alikuwa kitandani, ana homa, nao
wakamweleza Yesu habari zake. 31 Hivyo Yesu
akamwendea, akamshika mkono na kumwinua.

Hivyo homa ikamwacha, naye akaanza
kuwahudumia.

### *Yesu Aponya Wengi*

32Jioni ile baada ya jua kutua, watu
wakamletea Yesu wagonjwa wote na
waliopagawa na pepo wachafu. 33Mji wote
ukakusanyika mbele ya nyumba hiyo. 34 Yesu
akawaponya watu wengi waliokuwa na magonjwa
ya aina mbalimbali. Akawatoa pepo wachafu
wengi, lakini hakuwaacha hao pepo wachafu
waseme kwa sababu walimjua kuwa Yeye ni nani.

### *Yesu Aondoka Kapernaumu Na Kwenda Galilaya*

35Mapema sana alfajiri kulipokuwa bado
kungali giza, Yesu akamka, akaondoka, akaenda
mahali pa faragha,ili kuomba. 36Simoni na
wenzake wakaenda kumtafuta, 37nao
walipomwona, wakamwambia, “Kila mtu
anakutafuta!”

38Yesu akawajibu, “Twendeni mahali pengine
kwenye vijiji vya jirani, ili niweze kuhubiri huko
nako, kwa sababu hicho ndicho nilichokuja
kukifanya. 39Kwa hiyo akazunguka Galilaya kote,
akihubiri katika masinagogi yao na kutoa pepo
wachafu.

### *Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*

40Mtu mmoja mwenye ukoma alimjia
akamwomba akipiga magoti akamwambia Yesu,
“Ukitaka, waweza kunitakasa.”

41Yesu akiwa amejawa na huruma, akanyosha
mkono Wake akamgusa, akamwambia, “Nataka
takasika!” 42Mara ukoma ukamtoka, naye
akatakasika. 43Baada ya Yesu kumwonya vikali,
akamruhusu aende zake 44akimwambia, “Hakikisha
humwambii mtu ye yote habari hizi, bali nenda
ukajionyeshe kwa kuhani na ukatoe sadaka kwa ajili
ya kutakasika kwako kama alivyoamuru Mose kuwa
ushuhuda kwao.” 45Lakini yule mtu akaenda
akaanza kutangaza habari za kuponywa kwake
waziwazi. Kwa hiyo Yesu hakuweza tena kuingia
katika miji waziwazi isipokuwa alikaa sehemu zisizo
na watu. Lakini bado watu wakamfuata huko kutoka
kila upande.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyepooza*

**2** Baada ya siku kadhaa Yesu alirudi
Kapernaumu, watu wakasikia kwamba
amerudi nyumbani. 2Hivyo watu wengi
wakakusanyika hata hapakubaki nafasi yo yote
hata mlangoni! Naye akawahubiria neno. 3Ndipo
baadhi ya watu wakaja wakamletea Yesu mtu
aliyepooza, akiwa amebebwa na watu wanne.
4Kwa kuwa walikuwa hawawezi kumfikisha kwa
Yesu kwa ajili ya umati wa watu, walitoboa tundu
kwenye paa mahali pale alipokuwa Yesu,
wakamshusha yule aliyepooza kwa kitanda.
5Yesu alipoona imani yao, alimwambia yule
aliyepooza, ‘‘Mwanangu, dhambi zako
zimesamehewa. ”

6Basi baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa
wameketi huko wakawaza mioyoni mwao, 7‘‘Kwa
nini mtu huyu anasema hivi? Huyu anakufuru! Ni
nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa
Mungu peke Yake?

8Mara moja Yesu akatambua kile
walichokuwa wanawaza mioyoni mwao, naye
akawaambia, ”Kwa nini mnawaza hivyo mioyoni
mwenu? 9Ni jambo gani lililo rahisi, kumwambia
huyu aliyepooza, ‘‘Umesamehewa dhambi zako,
au kusema, ‘Inuka, uchukue kitanda chako
uende?’ 10Lakini ili mpate kujua ya kwamba
Mwana wa Adamu anao uwezo duniani wa
kusamehe dhambi,” Yesu akamwambia yule
aliyepooza, 11‘‘Nakuambia, inuka, chukua kitanda
chako uende nyumbani kwako.” 12Yule mtu
aliyekuwa amepooza akainuka, akachukua
kitanda chake akatembea machoni pao wote!
Jambo hili likawashangaza wote, wakamtukuza
Mungu, wakisema, ‘‘Hatujapata kuona jambo
kama hili kamwe!”

### *Yesu Amwita Lawi (Mathayo)*

13Yesu akaenda tena kando -kando ya bahari
ya Galilaya. Umati mkubwa wa watu ukamfuata,
naye akaanza kuwafundisha. 14Alipokuwa
akitembea, akamwona Lawi mwana wa Alfayo
ameketi forodhani mahali pa kukusanyia kodi,
akamwambia, ‘‘Nifuate.” Lawi akaondoka,
akamfuata Yesu.

15Yesu alipokuwa akila chakula nyumbani
mwa Lawi, watoza ushuru wengi pamoja na
wenye dhambi walikuwa wakila pamoja naye na
wanafunzi Wake, kwa maana kulikuwa na watu
wengi waliokuwa wakimfuata. 16Baadhi ya walimu
wa sheria na Mafarisayo walipomwona akila
pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi,
wakawauliza wanafunzi Wake, ‘‘Mbona Yesu

anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?”.

17Yesu aliposikia haya akawaambia, “Walio
wazima hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa.
Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.”

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*

18Basi wanafunzi wa Yohana pamoja na
Mafarisayo walikuwa wakifunga. Baadhi ya watu
wakamjia Yesu na kumwuliza, “Mbona wanafunzi
wa Yohana na wa Mafarisayo hufunga lakini
wanafunzi Wako hawafungi?”

19Yesu akawajibu, “Wageni wa bwana arusi
wawezaje kufunga wakati bwana arusi akiwa
pamoja nao? Maadam bwana arusi yuko pamoja
nao, hawawezi kufunga. 20Lakini wakati utakuja
ambapo bwana arusi ataondolewa kwao, siku hiyo
ndipo watakapofunga.

21 ‘‘Hakuna mtu ashonaye kiraka cha nguo
mpya kwenye nguo iliyochakaa. Akifanya hivyo,
kile kiraka kipya kilichoshonewa kwenye nguo
iliyochakaa huondoka, nayo ile nguo huchanika
zaidi. 22Wala hakuna mtu awekaye divai mpya
kwenye viriba vikuukuu. Akifanya hivyo, ile divai
mpya itavipasua hivyo viriba, kwa hiyo divai
itamwagika na viriba vitaharibika. Divai mpya
huwekwa kwenye viriba vipya.”

### *Bwana Wa Sabato*

23Siku moja ya Sabato, Yesu pamoja na
wanafunzi Wake, walikuwa wakipita katikati ya
mashamba ya nafaka. Walipokuwa wakipita
wanafunzi Wake wakaanza kuvunja masuke.
24Mafarisayo wakamwambia, “Tazama, mbona
wanafanya jambo ambalo si halali kufanywa siku
ya Sabato?”

25Yesu akawajibu, Je, hamjasoma kamwe
alivyofanya Daudi wakati yeye na wenzake
walipokuwa na njaa na uhitaji wa chakula?
26Daudi aliingia katika nyumba ya Mungu wakati
Abiathari akiwa kuhani mkuu, akaila ile mikate ya
Wonyesho, ambayo ilikuwa hairuhusiwi mtu ye
yote kuila isipokuwa makuhani, naye akawapa
wenzake.”

27Kisha Yesu akawaambia, ‘‘Sabato ilifanyika
kwa ajili ya mwanadamu, lakini si mwanadamu
kwa ajili ya Sabato. 28Hivyo, Mwana wa Adamu
ndiye Bwana wa Sabato.”

### *Yesu Amponya Mtu Mwenye Mkono Uliopooza*

**3** Yesu akaingia tena ndani ya sinagogi na huko
palikuwa na mtu mwenye mkono uliopooza.
2Wakawa wanamwangalia ili waone kama
atamponya siku ya Sabato wapate sababu ya
kumshtaki. 3Yesu akamwambia yule mwenye
mkono uliopooza, ‘‘Njoo hapa mbele.”

4Kisha Yesu akawauliza, ‘‘Je ni lipi lililo halali
siku ya Sabato, kufanya jema au baya ”, kuokoa
maisha au kuua?” Lakini wao wakanyamaza
kimya.

5Yesu akawatazama pande zote kwa hasira,
akahuzunika sana kwa ajili ya ugumu wa mioyo
yao. Akamwambia yule mtu mwenye mkono
uliopooza, ‘‘Nyosha mkono wako.’’ Akaunyosha,
nao ukapona kabisa! 6Kisha Mafarisayo wakatoka
nje, mara wakaanza kufanya shauri la kumwua
Yesu wakiwa na kundi la wafuasi wa Herode.

### *Umati Wa Watu Wamfuata Yesu*

7Yesu pamoja na wanafunzi Wake
wakaondoka huko wakaenda baharini, nao umati
mkubwa wa watu kutoka Galilaya ukamfuata.
8Waliposikia mambo yote aliyokuwa akiyafanya,
umati mkubwa wa watu ukamjia kutoka Uyahudi,
Yerusalemu, Idumaya, Ng’ambo ya Yordani
pamoja na wale wa sehemu za karibu na Tiro na
Sidoni. 9Kwa sababu ya umati mkubwa wa watu,
aliwaambia wanafunzi Wake waweke tayari
mashua ndogo kwa ajili Yake, ili kuwazuia watu
kumsonga. 10Kwa kuwa alikuwa amewaponya
wagonjwa wengi, wale wenye magonjwa walikuwa
wanasukamana ili wapate kumgusa. 11Kila mara
pepo wachafu walipomwona, walianguka chini
mbele Yake na kupiga kelele wakisema, “Wewe
ndiwe Mwana wa Mungu.” 12Lakini aliwaonya
wasimseme Yeye ni nani.

### *Yesu Achagua Mitume Kumi Na Wawili*

13Yesu akapanda mlimani na kuwaita wale
aliowataka, nao wakamjia. 14Akawachagua kumi
na wawili ambao pia aliwaita mitume, ili wapate
kuwa pamoja naye na ili apate kuwatuma kwenda
kuhubiri 15na kuwa na mamlaka ya kutoa pepo
wachafu. 16Hawa ndio wale kumi na wawili
aliowachagua: Simoni (ambaye alimwita Petro),
17Yakobo mwana wa Zebedayo na Yohana
nduguye (ambao aliwaita Boanerge, maana yake
Wana wa Ngurumo), 18Andrea, Filipo,
Bartholomayo, Mathayo, Thomaso, Yakobo,
mwana wa Alfayo, Thadayo, Simoni Mkananayo

na [19]Yuda Iskariote, ambaye ndiye aliyemsaliti
Yesu.

### *Yesu Na Beelzebuli*

[20]Ndipo Yesu aliporudi nyumbani, umati wa
watu ukakusanyika tena, kiasi kwamba Yeye na
wanafunzi Wake hawakuweza kula chakula.
[21]Ndugu Zake walipopata habari wakaja ili
kumchukua kwa maana watu walikuwa wakisema,
“Amerukwa na akili.”

[22]Walimu wa sheria waliotelemka kutoka
Yerusalemu walisema, “Amepagawa na
Beelzebuli! Kwa kutumia mkuu wa pepo wachafu,
anatoa pepo wachafu.”

[23]Basi Yesu akawaita na kuzungumza nao
kwa mifano akasema: “Shetani awezaje kumtoa
Shetani? [24]Kama ufalme ukigawanyika wenyewe
kwa wenyewe, ufalme huo hauwezi kusimama.
[25]Nayo nyumba kama ikigawanyika yenyewe kwa
yenyewe, nyumba hiyo haiwezi kusimama.
[26]Naye Shetani kama akijipinga mwenyewe akiwa
amegawanyika, hawezi kusimama bali mwisho
wake umewadia. [27]Hakuna mtu ye yote awezaye
kuingia kwenye nyumba ya mtu mwenye nguvu na
kuteka nyara mali zake asipomfunga kwanza yule
mwenye nguvu, ndipo awezapo kuteka nyara.
[28]“Amin, amin nawaambia, dhambi zote na
makufuru yote ya wanadamu watasamehewa.
[29]Lakini ye yote anayemkufuru Roho Mtakatifu
hatasamehewa kamwe, atakuwa na hatia ya
dhambi ya milele”.

[30]Yesu alisema hivi kwa sababu walikuwa
wanasema, “Ana pepo mchafu.”

### *Mama Na Ndugu Zake Yesu*

[31]Kisha wakaja ndugu zake Yesu pamoja na
mama yake. Wakiwa wamesimama nje,
wakamtuma mtu kumwita. [32] Umati wa watu
ulikuwa umeketi kumzunguka wakamwambia,
“Mama Yako na ndugu Zako wako nje,
wanakutafuta.”

[33]Akawauliza, ‘‘Mama yangu na ndugu zangu
ni nani?’’

[34]Kisha akawatazama wale watu waliokuwa
wameketi kumzunguka pande zote, akasema,
‘‘Hawa ndio mama zangu na ndugu zangu. [35]Mtu
ye yote anayetenda mapenzi ya Mungu huyo
ndiye ndugu yangu, dada Yangu na mama
Yangu.’’

### *Mfano Wa Mpanzi*

**4** Yesu akaanza kufundisha tena kando ya
bahari. Umati wa watu uliokuwa
umemkusanyikia kumzunguka ulikuwa mkubwa
kiasi kwamba ilimbidi Yesu aingie kwenye
mashua iliyokuwa baharini na kuketi humo.
[2]Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, naye
katika mafundisho yake akasema: [3]“Sikilizeni!
Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake.
[4]Alipokuwa akipanda, mbegu nyingine zilianguka
kando ya njia, ndege wakaja na wakazila.
[5]Nyingine zilianguka kwenye ardhi yenye
mwamba ambako hakukuwa na udongo wa
kutosha. Zikaota haraka, kwa kuwa udongo
ulikuwa haba. [6]Jua lilipozidi, mimea ikanyauka na
kukauka kwa kuwa mizizi yake ilikuwa haina kina.
[7]Mbegu nyingine zilianguka kwenye miiba, miiba
hiyo ikakua ikaisonga hiyo mimea hivyo haikutoa
mazao. [8]Mbegu nyingine zilianguka kwenye
udongo mzuri, zikaota vizuri na kukua, zikatoa
mazao, moja thelathini, nyingine sitini na nyingine
mia moja.”

[9]Kisha Yesu akasema, “Mwenye masikio ya
kusikia na asikie.”

### *Sababu Za Mifano*

[10]Alipokuwa peke Yake, wale waliokuwepo
pamoja na wanafunzi wake kumi na wawili,
wakamwuliza kuhusu mifano Yake. [11]Naye
akawaambia, ” Ninyi mmepewa kujua siri ya
Ufalme wa Mungu, lakini kwa wale walioko nje,
kila kitu husemwa kwao kwa mifano [12] ili,

‘Daima waone lakini wasitambue,
daima wasikie lakini wasielewe.
Wasije wakageuka,
wakatubu na kusamehewa.’ ”

### *Yesu Afafanua Maana Ya Mfano Wa Mbegu*

[13]Kisha Yesu akawauliza, “Hamwelewi
maana ya mfano huu? Basi mtaelewaje mifano
mingine? [14]Yule mpanzi hupanda neno. [15]Hawa
ndio wale walio kando ya njia, ambako neno
lilipandwa. Walisikiapo neno, Shetani huja mara
na kulichukua lile neno lililopandwa ndani yao.
[16]Nazo hizi ni zile mbegu zilizoanguka kwenye
udongo wenye miamba, wanapolisikia neno, mara
hulipokea kwa furaha. [17]Basi kwa kuwa hawana
mizizi, hudumu kwa muda mfupi tu, kisha dhiki au
mateso yanapoinuka kwa ajili ya lile neno, wao

mara huiacha imani. 18Lakini wengine, kama mbegu iliyopandwa kwenye miiba, hulisikia lile neno, 19lakini masumbufu ya maisha haya, udanganyifu wa mali na tamaa ya mambo mengine huja na kulisonga lile neno na kulifanya lisizae. 20Wengine, kama mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri, hulisikia lile neno, wakalipokea na kutoa mazao: Wengine thelathini, wengine sitini na wengine mara mia moja ya ile iliyopandwa."

### *Mfano Wa Taa*

21Akawaambia, "Je, taa huwashwa na kufunikwa chini ya kikapu au mvunguni mwa kitanda? Je, haiwashwi na kuwekwa juu ya kinara chake? 22Kwa kuwa hakuna kilichofichika ambacho hakitafunuliwa, wala hakuna jambo lo lote la siri ambalo halitaletwa nuruni. 23Mwenye masikio ya kusikia na asikie."

24Naye akawaambia, "Iweni waangalifu na yale mnayosikia. Kipimo mnachotumia kuwapimia wengine ndicho kitakachotumiwa kuwapimia ninyi, hata na zaidi. 25Kwa maana aliye na kitu ataongezewa na yeye asiye na kitu hata kile alicho nacho atanyang'anywa."

### *Mfano Wa Mbegu Inayoota*

26Pia akawaambia, "Ufalme wa Mungu unafanana na mtu apandaye mbegu shambani. 27Akiisha kuzipanda, usiku hulala na mchana huamka, nazo mbegu huota na kukua pasipo yeye kujua inavyokua. 28Udongo huifanya iote kuwa mche, halafu suke, kisha nafaka kamili kwenye suke. 29Lakini nafaka inapokuwa imekomaa, mara mkulima huingia shambani na mundu wa kuvunia maana mavuno yamekuwa tayari."

### *Mfano Wa Mbegu Ya Haradali*

30Akawaambia tena, ``Tuufananishe Ufalme wa Mungu na nini? Au tutumie mfano gani ili kuueleza? 31Uko kama punje ya haradali, ambayo ni mbegu ndogo sana kuliko mbegu zote zinazopandwa ardhini. 32Lakini ikishaota, hukua ikawa mmea mkubwa kuliko yote katika bustani, ikawa na matawi makubwa hata ndege wa angani kujenga viota kwenye matawi yake."

33Kwa mifano mingine mingi kama hii Yesu alinena nao neno Lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikiza. 34Hakusema nao neno lo lote pasipo mifano. Lakini alipokuwa na wanafunzi Wake, aliwafafanulia kila kitu.

### *Yesu Atuliza Dhoruba*

35Siku hiyo, ilipokaribia jioni, aliwaambia wanafunzi Wake, "Tuvuke na twende mpaka ng'ambo.'' 36Wakiuacha ule umati wa watu nyuma, walimchukua vile vile kama alivyokuwa kwenye mashua. Palikuwa pia na mashua nyingine nyingi pamoja naye. 37Kukawa na dhoruba kali, nayo mawimbi yakaipiga ile mashua hata ikawa karibu kujaa maji. 38 Wanafunzi Wake wakamwamsha, wakamwambia, "Mwalimu, hujali kama tunazama?"

39Akaamka, akaukemea ule upepo, akayaambia yale mawimbi, "Uwe kimya! Tulia!" Ule upepo ukatulia, kukawa shwari kabisa.

40Yesu akawaambia wanafunzi Wake, "Kwa nini mnaogopa hivyo? Je, bado hamna imani?"

41Nao wakawa wameogopa sana, wakaulizana,''Ni nani huyu ambaye hata upepo na mawimbi vinamtii?"

### *Yesu Amponya Mtu Mwenye Pepo*

**5** Wakafika upande wa pili wa bahari wakaingia katika nchi ya Wagerasi. 2Yesu alipotoka kwenye mashua, mara mtu mmoja mwenye pepo mchafu akatoka makaburini akakutana naye. 3Mtu huyu aliishi makaburini, wala hakuna aliyeweza kumzuia hata kwa kumfunga minyororo, 4kwa kuwa mara kwa mara alikuwa amefungwa kwa minyororo mikononi na miguuni, akaikata hiyo minyororo na kuzivunja zile pingu miguuni mwake. Hapakuwa na mtu ye yote aliyekuwa na nguvu za kumzuia. 5Usiku na mchana alikuwa makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikatakata kwa mawe.

6Alipomwona Yesu kwa mbali, alimkimbilia akapiga magoti mbele Yake. 7Akapiga kelele kwa nguvu akisema, "Una nini nami, Yesu Mwana wa Mungu Aliye Juu? Ninakuapisha kwa Mungu, usinitese! " 8Kwa kuwa Yesu alikuwa amemwambia,''Mtoke mtu huyu wewe pepo mchafu!"

9Yesu akamwuliza, ''Jina lako ni nani?''

Akamjibu, ''Jina langu ni Legioni[a], kwa kuwa tuko wengi. " 10Akamwomba sana Yesu asiwapeleke nje ya nchi ile.

---

a9 Legioni hapa maana yake ni Jeshi.

11Kundi kubwa la nguruwe lilikuwa karibu likilisha kando ya kilima. 12Wale pepo wakamsihi Yesu wakisema, ‘‘Tuamuru twende kwenye wale nguruwe, turuhusu tuwaingie.” 13Basi Yesu akawaruhusu, nao wale pepo wakatoka wakawaingia hao nguruwe. Lile kundi lilikuwa na nguruwe wapata 2,000, likatelemkia kasi gengeni nao wakazama baharini.

14Wale waliokuwa wakichunga hao nguruwe wakakimbilia mjini na vijijini kueleza yaliyotukia. Watu wakatoka kwenda kuona hayo yaliyokuwa yametukia. 15Walipofika kwa Yesu, wakamwona yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu Legioni, akiwa ameketi hapo, amevaa nguo na pia akiwa na akili zake timamu. Wakaogopa. 16Wale walioyaona mambo haya wakawaeleza watu wengine yaliyomtokea yule aliyekuwa na pepo wachafu na lile kundi la nguruwe. 17Basi watu wakaanza kumwomba Yesu aondoke katika nchi yao.

18Yesu alipokuwa anaingia kwenye mashua, yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu akamsihi Yesu waende pamoja. 19Yesu hakumruhusu, bali alimwambia, ‘‘Nenda nyumbani kwa jamaa yako ukawaeleze mambo makuu aliyokutendea Bwana na jinsi alivyokuhurumia.” 20Yule mtu akaenda zake akaanza kutangaza katika Dekapoli jinsi Yesu alivyomtendea, nao watu wote wakastaajabu.

### *Mwanamke Aponywa*

21Yesu alipokwisha kuvuka tena na kufika ng’ambo, umati mkubwa wa watu ukamzunguka, Yeye akiwa kando ya bahari. 22Kisha mmoja wa viongozi wa sinagogi aliyeitwa Yairo, akafika pale, naye alipomwona Yesu akapiga magoti miguuni pake, 23akamsihi akisema, “Binti yangu mdogo ni mgonjwa mahututi. Tafadhali njoo uweke mikono Yako juu yake ili apate kupona na kuishi.” 24Hivyo Yesu akaongozana naye.

Umati mkubwa wa watu ukamfuata, watu wakawa wanamsonga. 25Hapo palikuwa na mwanamke aliyekuwa amesumbuliwa na tatizo la kutokwa damu kwa miaka kumi na miwili. 26Mwanamke huyu alikuwa ameteseka sana kwa mikono ya matabibu wengi na kutumia kila kitu alichokuwa nacho lakini badala ya kupona hali yake ilizidi kuwa mbaya. 27Alikuwa amesikia habari za Yesu naye akaja kwa nyuma yake kwenye umati wa watu, akaligusa vazi Lake,28maana alisema moyoni mwake, “Kama nikiweza kuligusa vazi Lake tu, nitapona.” 29Mara kutoka damu kwake kukakoma, naye akajisikia mwilini mwake amepona kabisa.

30Ghafula Yesu akatambua kuwa nguvu zimemtoka. Akaugeukia ule umati wa watu na kuuliza, “Ni nani aliyenigusa?”

31 Wanafunzi Wake wakamjibu, “Unaona jinsi umati wa watu unavyokusonga, wawezaje kuuliza, ‘Ni nani aliyenigusa?’ ’’

32Lakini Yesu akaangalia pande zote ili aone ni nani aliyemgusa. 33Yule mwanamke, akijua kilichomtokea, akaja, akaanguka miguuni pake akitetemeka kwa hofu, akamweleza ukweli wote. 34Yesu akamwambia, ‘‘Binti, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani, upone kabisa ugonjwa wako. ”

### *Yesu Amfufua Binti Yairo*

35Alipokuwa bado anaongea, watu wakafika kutoka nyumbani kwa Yairo wakamwambia, “Binti yako amekufa. Kwa nini kuendelea kumsumbua Mwalimu?’’

36Kwa kusikia hayo waliyosema, Yesu akamwambia huyo kiongozi wa sinagogi, “Usiogope. Amini tu.”

37Hakumruhusu mtu mwingine ye yote amfuate isipokuwa Petro, Yakobo na Yohana nduguye Yakobo. 38Walipofika nyumbani kwa yule kiongozi wa sinagogi, Yesu akaona ghasia, watu wakilia na kuomboleza kwa sauti kubwa. 39Alipokwisha kuingia ndani, akawaambia, “Kwa nini mnafanya ghasia na kulia? Mtoto hajafa bali amelala tu.” 40Wale watu wakamcheka kwa dharau.

Lakini Yeye akawatoa wote nje, akawachukua baba na mama wa yule mtoto pamoja na wale wanafunzi aliokuwa nao. Wakaingia ndani mpaka pale alipokuwa yule mtoto. 41 Akamshika mtoto mkono akamwambia, ‘‘Talitha, Cumi[b].” (Maana yake, ‘‘Msichana ninakuambia amka!”) 42Mara yule msichana akasimama, akaanza kutembea. Alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili. Walipoona haya, wakastaajabu sana. 43 Yesu akawaagiza kwa ukali wasimweleze mtu ye yote jambo hili, naye akawaambia wampe yule msichana chakula.

---

[b] 41 ‘Talitha Cumi’ ni lugha ya Kiaramu ambayo maana yake ni “Msichana amka!”

### *Nabii Hana Heshima Kwao*

6 Yesu akaondoka huko na kwenda mji wa kwao,
akiwa amefuatana na wanafunzi Wake. 2Ilipofika
siku ya Sabato, akaanza kufundisha katika
sinagogi na wengi waliomsikia
wakashangaa.
Wakauliza, "Mtu huyu ameyapata wapi
mambo haya yote?. Tazama ni hekima ya namna
gani hii aliyopewa? Tazama matendo ya miujiza
ayafanyayo kwa mikono Yake! 3Huyu si yule
seremala, mtoto wa Maria? Nao ndugu zake si
Yakobo, Yose, Yuda na Simoni? Dada zake wote
si tuko nao hapa petu?" Nao wakachukizwa sana
kwa ajili Yake wakakataa kumwamini.
4Yesu akawaambia, "Nabii hakosi heshima
isipokuwa katika mji wake mwenyewe na
miongoni mwa jamaa na ndugu zake."
5Hakufanya miujiza yo yote huko isipokuwa
kuweka mikono Yake juu ya wagonjwa wachache
na kuwaponya. 6Naye akashangazwa sana kwa
jinsi wasivyokuwa na imani.

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*

Kisha Yesu akawa anakwenda huku na huko
kutoka kijiji kimoja hadi kingine akifundisha.
7Akawaita wale kumi na wawili, akawatuma wawili
wawili na kuwapa mamlaka juu ya pepo wachafu
wawatoe.
8Akawaagiza wasichukue cho chote kwa ajili
ya safari isipokuwa fimbo tu. Wasichukue mkate,
wala mkoba, wala fedha kwenye mikanda yao,
9bali wavae viatu, lakini wasivae nguo ya ziada.
10Akawaambia, "Mkiingia kwenye nyumba yo
yote, kaeni humo hadi mtakapoondoka katika mji
huo. 11Kama mahali po pote hawatawakaribisha
wala kuwasikiliza, mtakapoondoka huko,
kung'uteni mavumbi yaliyoko miguuni mwenu, ili
kuwa ushuhuda dhidi yao."
12Kwa hiyo wakatoka na kuhubiri kwamba
inawapasa watu watubu, waache dhambi.
13Wakatoa pepo wachafu wengi, wakawapaka
wagonjwa wengi mafuta na kuwaponya.

### *Yohana Mbatizaji Akatwa Kichwa*

14Mfalme Herode akasikia habari hizi, kwa
maana Jina la Yesu lilikuwa limejulikana kila
mahali. Watu wengine walikuwa wakisema,
"Yohana Mbatizaji amefufuka kutoka kwa wafu
ndiyo maana uwezo wa kutenda miujiza unafanya
kazi ndani Yake! ".
15Wengine wakasema, "Yeye ni Eliya."
Nao wengine wakasema, "Yeye ni nabii,
kama mmojawapo wa wale manabii wa zamani."
16Lakini Herode aliposikia habari hizi,
akasema, "Huyo ni Yohana Mbatizaji, niliyemkata
kichwa, amefufuka!"
17Kwa kuwa Herode alikuwa ameagiza
kwamba Yohana Mbatizaji akamatwe, afungwe na
kutiwa gerezani. Alifanya hivi kwa sababu ya
Herodia, mke wa Filipo ndugu yake, ambaye
alikuwa amemwoa. 18Yohana alikuwa
amemwambia Herode, "Si halali wewe kumwoa
mke wa ndugu yako." 19Kwa hiyo Herodia alikuwa
amemwekea Yohana kinyongo akataka kumwua.
Lakini hakuweza, 20kwa sababu Herode
alimwogopa Yohana akijua kwamba ni mtu
mwenye haki na mtakatifu, akawa anamlinda.
Herode alifadhaika sana alipomsikia Yohana,
lakini bado alipenda kumsikiliza.
21Hatimaye Herodia alipata wasaa aliokuwa
akiutafuta. Mfalme Herode wakati wa Sikukuu
yake ya kuzaliwa alifanya karamu kubwa,
akawaalika maafisa wake wakuu, majemadari wa
jeshi na watu mashuhuri wa Galilaya. 22Binti yake
Herodia alipoingia na kucheza, akamfurahisha
Herode pamoja na wageni wake walioalikwa
chakulani.
Mfalme Herode akamwambia yule binti,
"Niombe kitu cho chote utakacho, nami nitakupa."
23Tena akamwahidi kwa kiapo akamwambia,
"Cho chote utakachoomba nitakupa, hata kama ni
nusu ya ufalme wangu."
24Yule binti akatoka nje akaenda kumwuliza
mama yake, "Niombe nini?"
Mama yake akajibu, "Omba kichwa cha
Yohana Mbatizaji."
25Yule binti akarudi haraka kwa mfalme
akamwambia, "Nataka unipe sasa hivi kichwa cha
Yohana Mbatizaji kwenye sinia."
26Mfalme akasikitika sana, lakini kwa sababu
alikuwa ameapa mbele ya wageni wake hakutaka
kumkatalia. 27Mara mfalme akatuma askari
mmojawapo wa walinzi wake kukileta kichwa cha
Yohana. Akaenda na kumkata Yohana kichwa
humo gerezani, 28 akakileta kichwa chake kwenye
sinia na kumpa yule msichana, naye yule
msichana akampa mama yake. 29Wanafunzi
wake walipopata habari hizi, wakaja kuuchukua
mwili wake, wakauzika kaburini.

### *Yesu Awalisha Watu 5,000*

30 Wale wanafunzi wa Yesu wakamkusanyikia na kumpa taarifa ya mambo yote waliyokuwa wamefanya na kufundisha. 31 Basi kwa kuwa watu wengi mno walikuwa wakija na kutoka, hata wakawa hawana nafasi ya kula, Yesu akawaambia wanafunzi Wake, "Twendeni peke yetu mahali pa faragha, mpate kupumzika."

32 Hivyo wakaondoka kwa mashua peke yao wakaenda mahali pa faragha pasipo na watu. 33 Lakini watu wengi waliowaona wakiondoka, wakawatambua, nao wakawatangulia haraka kwa miguu kutoka katika miji yote nao wakatangulia kufika. 34 Yesu alipofika nchi kavu na kuuona huo umati wa watu, aliwaonea huruma kwa maana walikuwa kama kondoo wasiokuwa na mchungaji. Kwa hiyo akaanza kuwafundisha mambo mengi.

35 Mchana ulipokuwa umeendelea sana, wanafunzi Wake wakamwendea, wakamwambia, "Mahali hapa ni mbali na pasipo na watu, nazo saa zimekwenda sana. 36 Waage watu ili waweze kwenda sehemu za mashambani na vijiji vya jirani, wakajinunulie chakula.

37 Lakini Yesu akawajibu, "Wapeni ninyi chakula.''

Wakamwambia, "Je, twende tukanunue mikate ya dinari 200[a] ili tuwape watu hawa wale?''

38 Akawauliza, "Kuna mikate mingapi? Nendeni mkaangalie.''

Walipokwisha kuona wakarudi, wakamwambia, "Kuna mikate mitano na samaki wawili.''

39 Kisha Yesu akawaamuru wawaketishe watu makundi makundi kwenye majani, 40 nao wakaketi kwenye makundi ya watu mia mia na wengine hamsini hamsini. 41 Yesu akaichukua ile mikate mitano na wale samaki wawili akatazama mbinguni, akashukuru, kisha akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi Wake ili wawagawie wale watu wote. Pia akawagawia wote wale samaki wawili. 42 Watu wote wakala, wakashiba. 43 Wanafunzi Wake wakakusanya vipande vilivyosalia vya mikate na samaki, wakajaza vikapu kumi na viwili. 44 Idadi ya wanaume waliokula walikuwa 5,000.

### *Yesu Atembea Juu Ya Maji*

45 Mara Yesu akawataka wanafunzi Wake waingie kwenye mashua watangulie kwenda Bethsaida, wakati Yeye anauaga ule umati wa watu. 46 Baada ya kuwaaga wale watu, akaenda mlimani kuomba.

47 Ilipofika jioni, ile mashua ilikuwa imefika katikati ya bahari na Yesu alikuwa peke yake katika nchi kavu. 48 Akawaona wanafunzi Wake wanahangaika na kupiga makasia kwa nguvu, kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho.Karibu na mapambazuko, Yesu akawaendea wanafunzi Wake, akitembea juu ya maji. Alikuwa karibu kuwapita, 49 lakini walipomwona akitembea juu ya maji, wakadhani ni mzimu, wakapiga yowe, 50 kwa sababu wote walipomwona waliogopa.

Mara Yesu akasema nao, akawaambia, "Jipeni moyo! Ni Mimi, msiogope!" 51 Akapanda kwenye mashua yao na ule upepo ukakoma! Wakashangaa kabisa. 52 Kwa kuwa walikuwa hawajaelewa kuhusu ile mikate, mioyo yao ilikuwa migumu.

53 Walipokwisha kuvuka, wakafika Genezareti, wakatia nanga. 54 Mara waliposhuka kutoka katika mashua yao, watu wakamtambua Yesu, 55 wakaenda katika vijiji vyote upesi, wakawabeba wagonjwa kwenye mikeka ili kuwapeleka mahali po pote waliposikia kuwa Yesu yupo. 56 Kila mahali Yesu alipokwenda, iwe vijijini, mijini na mashambani, watu waliwaweka wagonjwa wao masokoni, wakamwomba awaruhusu hao wagonjwa waguse japo upindo wa vazi Lake. Nao wote waliomgusa, waliponywa.

### *Kilicho Safi Na Kilicho Najisi*

**7** Mafarisayo na baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa wametoka Yerusalemu wakakusanyika mbele ya Yesu. 2 Wakawaona baadhi ya wanafunzi Wake wakila chakula kwa mikono iliyo najisi, yaani, bila kunawa kama ilivyotakiwa na sheria ya dini ya Wayahudi. 3 Kwa kuwa Mafarisayo na Wayahudi wote hawali chakula pasipo kunawa kwa kufuata desturi za wazee wao. 4 Wanapotoka sokoni hawawezi kula pasipo kunawa. Pia kuna desturi nyingine nyingi wanazofuata kama vile jinsi ya kuosha vikombe, vyungu na vyombo vya shaba.

---

[a] 37 Dinari 200 – dinari moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua kwa siku.Hivyo dinari 200 ni sawa na mshahara wa siku 200.

5Kwa hiyo wale Mafarisayo na walimu wa
sheria wakamwuliza Yesu, “Mbona wanafunzi
wako hawafuati desturi za wazee wetu na badala
yake wanakula kwa mikono najisi?’’
6Yesu akawajibu, “Nabii Isaya alisema ukweli
alipotabiri juu yenu, ninyi wanafiki, kama
ilivyoandikwa:

“ ‘Watu hawa wananiheshimu kwa midomo
yao,
lakini mioyoni mwao wako mbali nami.
7Huniabudu bure,
wakifundisha mapokeo ya wanadamu.’ ’’

8Ninyi mmeziacha amri za Mungu na kushika
desturi za watu.’’
9Naye akawaambia, “Ninyi mnayo njia nzuri ya
kukataa amri za Mungu ili mpate kuzishika desturi
zenu! 10Kwa mfano, Mose alisema, ‘Waheshimu
baba yako na mama yako’ na ‘Ye yote
amtukanaye baba yake au mama yake auawe.’
11Lakini ninyi mwasema mtu akimwambia baba
yake au mama yake kuwa, “Msaada ambao
ningekupa ni Korbani,” yaani, umetengwa kama
sadaka kwa Mungu, 12basi hawajibiki tena
kumsaidia baba yake au mama yake. 13Kwa njia
hiyo ninyi mnabatilisha neno la Mungu kwa
taratibu zenu mlizojiwekea. Nanyi mnafanya
mambo mengi ya jinsi hiyo.”
14Yesu akaita tena ule umati wa watu
akawaambia, “Nisikilizeni, kila mmoja wenu na
mwelewe jambo hili. 15Hakuna kitu
kinachomwingia mtu kimtiacho unajisi, lakini kile
kimtokacho ndicho kimtiacho unajisi. 16Kama mtu
ye yote ana masikio ya kusikia na asikie.”
17Akiisha kuuacha ule umati wa watu na
kuingia ndani, wanafunzi Wake wakamwuliza
maana ya mfano ule. 18Akawajibu, “Hata nanyi
hamwelewi? Hamtambui kwamba kitu
kimwingiacho mtu hakimtii unajisi? 19Mtu akila kitu
hakiingii moyoni mwake bali tumboni na baadaye
hutolewa nje ya mwili wake. (Kwa kusema hivi,
Yesu alivihalalisha vyakula vyote kuwa ni safi.”)
20Akaendelea kusema, “Kile kimtokacho mtu
ndicho kimtiacho unajisi. 21Kwa maana kutoka
ndani ya moyo wa mtu hutoka: Mawazo mabaya,
uasherati, 22wizi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya,
uovu, udanganyifu, ufisadi, wivu,matukano, kiburi
na upumbavu. 23Maovu haya yote hutoka ndani ya
mtu nayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi.’’

### *Imani Ya Mwanamke Msirofoinike*

24Ndipo Yesu akaondoka hapo akaenda
sehemu za Tiro. Akaingia katika nyumba moja,
naye hakutaka mtu ye yote ajue kwamba yuko
humo. Lakini hakuweza kujificha. 25Lakini
mwanamke mmoja ambaye binti yake mdogo
alikuwa na pepo mchafu, akaja na kumpigia
magoti miguuni pake. 26Basi huyo mwanamke
hakuwa Myahudi, bali wa asili ya Kisirofoinike[a].
Akamsihi Yesu amtoe binti yake huyo pepo
mchafu.
27Yesu akamwambia, “Waache watoto
washibe kwanza, kwa maana si vema kuchukua
chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.’’
28Lakini yule mwanamke akamjibu, “Bwana,
hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya
chakula cha watoto.’’
29Ndipo Yesu akamjibu, “Kwa sababu ya jibu
lako, endenda zako nyumbani, yule pepo machafu
amemtoka binti yako.”
30Akaenda zake nyumbani akamkuta binti
yake amelala kitandani, yule pepo mchafu akiwa
amemtoka.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyekuwa Kiziwi Na Bubu*

31Kisha Yesu akaondoka sehemu za Tiro,
akapita katikati ya Sidoni, hadi Bahari ya Galilaya
na kuingia eneo la Dekapoli. 32 Huko, watu
wakamletea Yesu mtu mmoja kiziwi, ambaye pia
alikuwa na kigugumizi, wakamwomba awekee
mkono Wake juu ya huyo mtu na amponye.
33Baada ya Yesu akampeleka yule kiziwi
kando mbali na watu, Yesu akatia vidole vyake
masikioni mwa yule mtu. Kisha akatema mate na
kuugusa ulimi wa yule mtu. 34Ndipo Yesu
akatazama mbinguni, akavuta hewa ndani kwa
nguvu akamwambia, “Efatha!” yaani, “Funguka!”
35Mara masikio yake yakafunguka na ulimi wake
ukaachiwa akaanza kuongea sawasawa.
36Yesu akawaamuru wasimwambie mtu ye
yote habari hizi. Lakini kadiri alivyowazuia, ndivyo
walivyozidi kutangaza kwa bidii. 37Walistaajabu
mno. Wakasema, “Amefanya mambo yote vizuri
mno! Amewawezesha viziwi wasikie na bubu
waseme!”

[a]26 “Asili ya Kisirofoinike” ni watu waliokuwa na asili ya Kifoinike lakini kutoka Syria ili kuwatofautisha na Wafoinike wa Libya.

### *Yesu Alisha Watu 4000*

**8** Katika siku hizo, umati mkubwa wa watu ulikusanyika tena. Kwa kuwa walikuwa hawana chakula, Yesu akawaita wanafunzi wake akawaambia, 2"Ninauhurumia huu umati wa watu, kwa sababu sasa wamekuwa nami kwa muda wa siku tatu na hawana chakula. 3 Nikiwaaga waende nyumbani bila kula, watazimia njiani kwa sababu baadhi yao wametoka mbali. ."

4Wanafunzi wake wakamjibu, "Lakini hapa nyikani tutapata wapi mikate ya kutosha kuwalisha?"

5Yesu akawauliza, "Mna mikate mingapi?" Wakajibu, "Tuna mikate saba."

6Akawaambia watu waketi chini. Akiisha kuichukua mikate saba na kushukuru, akaimega na kuwapa wanafunzi wake ili wawagawie watu. Wanafunzi wake wakafanya hivyo. 7Walikuwa pia na visamaki vichache, Yesu akavibariki, akawaamuru wanafunzi wake wawagawie watu. 8Wale watu walikula na kutosheka, baadaye wanafunzi wakakusanya vipande vilivyosalia wakajaza vikapu saba. 9Watu waliokula walikuwa wapata 4000. Akiisha kuwaaga, 10aliingia kwenye mashua pamoja na wanafunzi wake akaenda sehemu za Dalmanutha.

11 Mafarisayo wakaja, wakaanza kumhoji Yesu. Ili kumtega, wakamwomba awaonyeshe ishara kutoka mbinguni. 12Akahuzunika moyoni, akawaambia, "Kwa nini kizazi hiki kinataka ishara? Amin, nawaambieni, hakitapewa ishara yo yote." 13Kisha akawaacha, akarudi kwenye mashua, akavuka hadi ng'ambo .

### *Chachu Ya Mafarisayo Na Ya Herode*

14Wanafunzi walikuwa wamesahau kuleta mikate ya kutosha. Walikuwa na mkate mmoja tu kwenye mashua. 15Yesu akawaonya: "Jihadharini na chachu ya Mafarisayo na ya Herode."

16Wakaanza kujadiliana wao kwa wao wakasema, "Anasema hivi kwa kuwa hatukuleta mikate."

17Yesu akifahamu majadiliano yao, akawauliza: "Mbona mnazungumzia kuhusu kutokuwa na mikate? Bado hamtambui wala kuelewa? Je, mbona mioyo yenu ni migumu kiasi hicho? 18Mna macho lakini mnashindwa kuona, mna masikio lakini mnashindwa kusikia? Je, hamkumbuki? 19Nilipoimega ilemikate mitano kuwalisha watu elfu tano, mlikusanya vikapu vingapi vilivyojaa vya masazo?"

Wakamjibu, "Kumi na viwili."

20"Je ? nilipomega ile mikate saba kuwalisha watu 4,000, mlikusanya vikapu vingapi vilivyojaa vya masazo?"

Wakamjibu, "Saba."

21Ndipo akawaambia, Akawauliza, "Je, bado tu hamwelewi?"

### *Yesu Amponya Kipofu Huko Bethsaida*

22Wakafika Bethsaida na baadhi ya watu wakamleta mtu mmoja kipofu mmoja wakamsihi Yesu amguse. 23Yesu akamshika mkono huyo kipofu akampeleka nje ya kijiji. Baada ya kuyatemea mate macho ya yule kipofu na kumwekea mikono, Yesu akamwuliza, "Unaona cho chote?"

24 Yule kipofu akaangalia, akasema, "Ninaona watu, wanaonekana kama miti inayotembea."

25 Yesu akamwekea tena mikono machoni. Kisha macho yake yakafunguka, kuona kwake kukarejea kuona kila kitu kwa udhahiri. 26Yesu akamwaga aende nyumbani kwake, akimwambia, "Hata kijijini usiingie. "

### *Petro Amkiri Yesu Kuwa Ndiye Kristo*

27Yesu na wanafunzi wake wakaondoka kwenda katika vijiji vya Kaisaria Filipi. Walipokuwa njiani Yesu akawauliza, "Watu husema mimi ni nani?"

28Wakamjibu, "Baadhi husema wewe ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya na wengine husema wewe ni mmojawapo wa manabii."

29Akawauliza, "Je, ninyi, mnasema mimi ni nani?"

Petro akajibu, "Wewe ndiye Kristo."

30Akawaonya wasimwambie mtu ye yote habari zake.

### *Yesu Atabiri Juu Ya Kifo Chake*

31 Ndipo akaanza kuwafundisha wanafunzi wake kuwa Mwana wa Adamu atapata mateso mengi na kukataliwa na wazee, viongozi wa makuhani, na walimu wa sheria na kwamba atauawa na baada ya siku tatu atafufuka. 32Aliyasema haya wazi wazi, ndipo Petro akamchukua kando akaanza kumkemea.

33 Lakini Yesu alipogeuka na kuwaangalia
wanafunzi wake, akamkemea Petro, akasema,
“Rudi nyuma yangu Shetani! Wewe huwazi yaliyo
ya Mungu bali ya wanadamu.’’

34 Ndipo akauita ule umati wa watu pamoja na
wanafunzi wake, akasema, “Mtu ye yote akitaka
kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue
msalaba wake, anifuate. 35 Kwa maana mtu yeyote
anayetaka kuiokoa nafsi ataipoteza, lakini yeye
ayapotezaye maisha yake kwa ajili yangu na kwa
ajili ya Injili ataiokoa. 36 Mtu atafaidiwa nini kama
akiupata ulimwengu wote lakini akaipoteza nafsi
yake? 37 Au mtu atatoa nini apate tena maisha
yake? 38 Mtu ye yote anayenionea aibu mimi na
maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na cha
dhambi, Mwana wa Adamu, atamwonea aibu wakati
nitakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja
na malaika watakatifu.’’

**9** Yesu akaendelea kuwaambia, ‘‘Amin, amin
nawaambia, kuna watu waliosimama hapa ambao
hawataonja mauti kabla ya kuuona Ufalme
wa Mungu ukija katika nguvu.’’

### *Yesu Ageuka Sura*

2 Baada ya siku sita, Yesu akawachukua
petro, Yakobo na Yohana akawapeleka juu ya
mlima mrefu, mahali walipokuwa faraghani. Huko,
Yesu akageuka sura mbele yao. 3 Mavazi Yake
yakawa na weupe wa kuzima macho, meupe
kuliko ambavyo mtu ye yote duniani angaliweza
kuyang’arisha. 4 Mose na Eliya wakawatokea,
wakawa wanazungumza na Yesu.

5 Petro akamwambia Yesu, ‘‘Mwalimu, ni vizuri
sisi tukae hapa. Turuhusu tujenge vibanda vitatu :
Kimoja chako, kimoja cha Mose na kingine cha
Eliya.” 6 Petro hakujua aseme nini kwa maana
yeye na wenzake walikuwa wameogopa sana.

7 Ndipo pakatokea wingu, likawafunika, nayo
sauti kutoka katika lile wingu ikasema, “Huyu ni
Mwanangu, nimpendaye, msikilizeni Yeye.’’

8 Mara walipotazama huku na huku,
hawakuona tena mtu mwingine ye yote pamoja
nao isipokuwa Yesu.

9 Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani,
Yesu akawakataza wasimwambie mtu ye yote
mambo waliyoona, mpaka Mwana wa Adamu
atakapofufuka kutoka kwa wafu. 10 Wakalihifadhi
jambo hilo wao wenyewe, lakini wakawa
wanajiuliza ‘‘huku kufufuka kwa wafu’’ maana
yake nini.

11 Wakamwuliza, “Kwa nini walimu wa sheria
husema kwamba ni lazima Eliya aje kwanza?’’

12 Yesu akawajibu, “Ni kweli, Eliya yuaja
kwanza, ili kurudisha upya mambo yote. Mbona
basi imeandikwa kwamba Mwana wa Adamu ni
lazima ateseke sana na kudharauliwa? 13 Lakini
ninawaambia, Eliya amekwisha kuja nao
wakamtendea walivyopenda, kama ilivyoandikwa
kumhusu yeye.’’

### *Kuponywa Kwa Mvulana Mwenye Pepo Mchafu*

14 Walipowafikia wale wanafunzi wengine,
wakawakuta wamezungukwa na umati mkubwa
wa watu na baadhi ya walimu wa sheria
wakibishana nao. 15 Mara wale watu walipomwona
Yesu, wakastaajabu sana, wakamkimbilia, ili
kumsalimu.

16 Akawauliza wanafunzi Wake, “Mnabishana
nao kuhusu nini?’’

17 Mtu mmoja miongoni mwa ule umati wa
watu akajibu, “Mwalimu, nilimleta kwako
mwanangu ambaye ana pepo mchafu ambaye
ana mfanya asiweze kuongea. 18 Kila mara huyo
pepo mchafu ampagaapo mwanangu,
humwangusha chini na kumfanya atokwe povu
mdomoni na kusaga meno, kisha mwili wake
hukauka. Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe
huyo pepo mchafu, lakini hawakuweza.’’

19 Yesu akawaambia, “Enyi kizazi kisicho na
imani! Nitakuwa pamoja nanyi mpaka lini?
Nitachukuliana nanyi mpaka lini? Mleteni huyo
mvulana kwangu.”

20 Nao wakamleta yule mvulana. Yule pepo
mchafu alipomwona Yesu, mara akamtia yule
mvulana kifafa, akaanguka, akagaagaa chini huku
akitokwa na povu kinywani.

21 Yesu akamwuliza baba yake, “Mwanao
amekuwa akitokewa na hali hii tangu lini?’’

Akamjibu, “Tangu utoto wake. 22 Mara kwa
mara huyo pepo mchafu amekuwa akimwangusha
kwenye moto au kwenye maji ili kumwangamiza.
Lakini kama unaweza kufanya jambo lo lote,
tafadhali tuhurumie utusaidie.’’

23 Yesu akamwambia, “Kama ukiweza kuamini,
yote yawezekana kwake yeye aaminiye.’’ 24 Mara
baba yake yule mvulana akapiga kelele akisema,
“Ninaamini. Nisaidie kutokuamini kwangu!’’ 25 Yesu
alipoona kwamba umati wa watu

unakusanyika pamoja mbio, akamkemea yule pepo mchafu, akimwambia, ''Wewe pepo bubu na kiziwi, nakuamuru umtoke wala usimwingie tena!"

26Yule pepo mchafu akiisha kupiga kelele, akamtia kifafa kwa nguvu, akamtoka. Yule mvulana alikuwa kama maiti, hivyo watu wengi
wakasema, ''Amekufa.'' 27Lakini Yesu akamshika
mkono akamwinua, naye akasimama.

28Baada ya Yesu kuingia ndani ya nyumba, wanafunzi Wake wakamwuliza wakiwa peke yao, ''Mbona sisi hatukuweza kumtoa huyo pepo mchafu?''

29Yesu akawajibu, ''Hali hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba na kufunga.''

### *Yesu Atabiri Tena Kifo Chake Na Ufufuo*

30Wakaondoka huko, wakapitia Galilaya. Yesu hakutaka mtu ye yote afahamu mahali
walipo 31kwa maana alikuwa anawafundisha
wanafunzi Wake. Akawaambia, "Mwana wa Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu nao watamwua, naye siku tatu baada ya kuuawa
atafufuka.'' 32Lakini wao hawakuelewa kile
alichokuwa akisema nao waliogopa kumwuliza.

### *Mabishano Kuhusu Aliye Mkuu Zaidi Wote*

33Basi wakafika Kapernaumu na baada ya kuingia nyumbani akawauliza, "Mlikuwa
mnabishana nini kule njiani?'' 34Lakini
hawakumjibu, kwa sababu njiani walikuwa wakibishana kuhusu nani miongoni mwa aliyekuwa mkuu zaidi ya wote.

35Akaketi, akawaita wote kumi na wawili akawaambia: 'Kama mtu ye yote akitaka kuwa wa kwanza hana budi kuwa wa mwisho na mtumishi wa wote.'

36Kisha akamchukua mtoto mdogo akamsimamisha katikati yao, akamkumbatia,
akawaambia, 37"Mtu ye yote amkaribishaye
mmoja wa hawa watoto wadogo, kwa Jina Langu anikaribisha Mimi. Naye ananikaribishaye Mimi, amkaribisha Baba yangu aliyenituma."

### *Ye Yote Asiye Kinyume Nasi Yuko Upande Wetu*

38Yohana akamwambia, "Mwalimu, tumemwona mtu akitoa pepo wachafu kwa Jina Lako nasi tukamkataza kwa sababu yeye si mmoja wetu.''

39Yesu akasema, "Msimkataze, hakuna ye
yote atendaye miujiza kwa Jina Langu ambaye baada ya kitambo kidogo aweza kunena lo lote
baya dhidi Yangu. 40Kwa maana ye yote asiye
kinyume chetu yuko upande wetu. 41Amin, amin
nawaambia, ye yote awapaye ninyi kikombe cha maji kwa Jina Langu kwa sababu ni mali ya Kristo, hakika hataikosa thawabu yake."

### *Kusababisha Kutenda dhambi*

42"Kama mtu ye yote akimsababisha mmojawapo wa wadogo hawa wanaoniamini kutenda dhambi, ingekuwa afadhali mtu huyo afungiwe shingoni mwake jiwe kubwa la kusagia
na kutoswa baharini. 43Kama mkono wako
ukikusababisha kutenda dhambi, ukate. Ni afadhali kuingia katika uzima ukiwa na mkono mmoja kuliko kuwa na mikono miwili ukaingia jehanam mahali ambako moto hauzimiki.
[44Mahali ambako funza wake hawafi wala moto
wake hauzimiki.] 45Kama mguu wako
ukikusababisha kutenda dhambi, ukate. Ni afadhali kuingia katika uzima ukiwa kilema kuliko kuwa na miguu miwili ukaingia jehanam mahali
ambako moto hauzimiki. [46Mahali ambako funza
wake hawafi wala moto hauzimiki.] 47Nalo jicho
lako litakusababisha kutenda dhambi, ling'oe. Ni afadhali kuwa chongo ukaingia katika Ufalme wa Mungu kuliko kuwa na macho mawili na ukatupwa
jehanam. 48Mahali ambako

" 'funza wake hawafi, wala
moto hauzimiki.'

49Kila mmoja atatiwa chumvi kwa moto.

50"Chumvi ni nzuri, lakini ikipoteza ladha yake utaifanyaje ili iweze kukolea tena? Mwe na chumvi ndani yenu, mkaishi kwa amani, kila mmoja na mwenzake."

### *Mafundisho Kuhusu Talaka*

**10** Yesu akaondoka huko akavuka Mto wa Yordani, akaenda sehemu ya Uyahudi. Umati mkubwa wa watu ukamjia tena na kama ilivyokuwa desturi Yake akawafundisha.

2Baadhi ya Mafarisayo wakaja ili kumjaribu kwa kumwuliza, "Je, ni halali mtu kumwacha mke wake?"

3Yesu akawajibu, "Je, Mose aliwaamuru nini?"

4Wakajibu, "Mose aliruhusu kwamba mume anaweza kumwandikia mkewe hati ya talaka na

kumwacha."

5Yesu akawaambia, "Mose aliwaandikia sheria hiyo kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu. 6Lakini tangu mwanzo wa uumbaji, 'Mungu aliwaumba mume na mke. 7Kwa sababu hii mwanaume atamwacha baba yake na mama yake na kuambatana na mkewe na hao wawili, watakuwa mwili mmoja.' 8Kwa hiyo hawatakuwa wawili tena bali mwili mmoja. 9Basi, alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe"

10Walipokuwa tena ndani ya nyumba, wanafunzi Wake wakamwuliza kuhusu jambo hili. 11Akawajibu, "Mtu ye yote anayemwacha mkewe na kuoa mke mwingine, azini naye. 12Naye mwanamke anayemwacha mumewe na kuolewa na mume mwingine, anazini pia."

### *Yesu Anawabariki Watoto Wadogo*

13Watu walikuwa wakimletea Yesu watoto wadogo ili awaguse lakini wanafunzi Wake wakawakemea. 14Yesu alipoona yaliyokuwa yakitukia akachukizwa, akawaambia wanafunzi Wake, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa watu kama hawa. 15 Amin, amin nawaambia, mtu ye yote asiyeukubali Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo, hatauingia kamwe." 16Akawachukua watoto mikononi mwake, akawakumbatia, akaweka mikono Yake juu yao, akawabariki."

### *Kijana Tajiri*

17Yesu alipokuwa anaondoka, mtu mmoja akamkimbilia, akapiga magoti mbele Yake, akamwuliza, "Mwalimu mwema, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?''

18Yesu akamwambia, "Mbona unaniita mwema? Hakuna aliye mwema isipokuwa Mungu peke Yake. 19Unazijua amri: 'Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, usidanganye, waheshimu baba yako na mama yako.' "

20Akamjibu, "Mwalimu, amri hizi zote nimezishika tangu nikiwa mtoto.''

21Yesu akamtazama na kumpenda, akamwambia, "Umepungukiwa na kitu kimoja, nenda ukauze kila kitu ulicho nacho uwape maskini hizo fedha, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate."

22Yule mtu aliposikia hayo, akasikitika sana, akaondoka kwa huzuni kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

23Yesu akatazama pande zote, akawaambia wanafunzi Wake, "Itakuwa vigumu sana kwa wenye mali kuingia kwenye Ufalme wa Mungu!''

24Wanafunzi Wake wakashangazwa sana na maneno hayo. Lakini Yesu akawaambia tena, "Wanangu, tazama jinsi ilivyo vigumu kwa wale wanaotumainia mali kuingia katika Ufalme wa Mungu. 25Ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko tajiri[a] kuingia katika Ufalme wa Mungu.''

26Wanafunzi Wake wakashangaa mno. Wakaulizana wao kwa wao, "Ni nani basi awezaye kuokolewa?''

27Yesu akawatazama, akawaambia, "Kwa mwanadamu hili haliwezekani, lakini kwa Mungu sivyo. Yote kwa Mungu yanawezekana.''

28Petro akaanza kumwambia, "Tazama, tumeacha kila kitu na kukufuata Wewe!"

29Yesu akasema, "Amin, nawaambia, hakuna mtu ye yote aliyeacha nyumba, ndugu waume,au ndugu wake, mama, baba, watoto au mashamba kwa ajili Yangu na kwa ajili ya Injili, 30ambaye hatalipwa mara mia katika ulimwengu huu, nyumba, ndugu waume, ndugu wake, mama, baba, watoto, mashamba pamoja na mateso kisha uzima wa milele katika ulimwengu ujao. 31Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho na wa mwisho watakuwa wa kwanza.''

### *Yesu Atabiri Mara Ya Tatu Kufa Na Kufufuka Kwake*

32Walikuwa njiani wakipanda kwenda Yerusalemu na Yesu alikuwa ametangulia. Wanafunzi Wake walishangaa, nao watu waliowafuata walijawa na hofu. Yesu akawachukua tena wale wanafunzi Wake kumi na wawili kando na kuwaambia yatakayompata. 33Akasema, "Tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana wa Adamu atasalitiwa kwa viongozi wa makuhani na walimu wa sheria. Wao watamhukumu kifo na kumtia mikononi mwa kwa watu Mataifa, 34ambao watamdhihaki, watamtemea mate, watampiga na kumwua. Siku tatu baada ya kifo Chake atafufuka."

### *Ombi La Yakobo Na Yohana*

---

[a] 24Tajiri hapa ina maana wale wanaotumainia mali

35Kisha Yakobo na Yohana, wana wa
Zebedayo, wakaja mbele alikokuwa na
kumwambia, “Mwalimu, tunataka utufanyie lo lote
tutakalokuomba.”
36Naye akawaambia, “Je, mwataka
niwafanyie jambo gani?”
37Wakamwambia, “Tupe kukaa mmoja
upande Wako wa kuume na mwingine upande
wako wa kushoto katika utukufu Wako.”
38Lakini Yesu akawaambia, “Hamjui
mnaloliomba. Je, mnaweza kukinywea kikombe
ninyweacho Mimi, au kubatizwa ubatizo
nibatizwao Mimi?”
39Wakajibu, “Tunaweza.”
Kisha Yesu akawaambia, “Kikombe
nikinyweacho mtakinywea na ubatizo nibatizwao
mtabatizwa, 40lakini kuketi mkono wangu wa
kuume au wa kushoto si juu Yangu mimi kuwapa.
Nafasi hizi ni kwa ajili ya wale walioandaliwa.”
41Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia
hayo wakaanza kuwakasirikia Yakobo na Yohana.
42Yesu akawaita wanafunzi Wake pamoja
akawaambia, “Mnafahamu kuwa watawala wa
watu Mataifa huwatawala watu kwa nguvu, nao
wenye vyeo huwaonyesha mamlaka yao. 43Lakini
sivyo kwenu. Badala yake ye yete anayetaka
kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa
mtumishi wenu 44na ye yote anayetaka kuwa wa
kwanza, hana budi kuwa mtumwa wa wote.
45Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja
kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai Wake
kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi.”

### *Yesu Amponya Kipofu Bartimayo*

46Kisha wakafika Yeriko. Wakati Yesu na
wanafunzi Wake alipokuwa akiondoka mjini
pamoja na umati mkubwa wa watu, kipofu mmoja,
jina lake Bartimayo, mwana wa Timayo, alikuwa
ameketi kando ya njia akiomba msaada.
47Aliposikia kuwa ni Yesu wa Nazareti aliyekuwa
anapita, akaanza kupaza sauti akisema, “Yesu,
Mwana wa Daudi, unihurumie!”
48Watu wengi wakamkemea, wakamwambia
akae kimya, lakini yeye akazidi kupaza sauti
akisema, “Mwana wa Daudi, unihurumie!”
49Yesu akasimama na kusema, “Mwiteni.”
Hivyo wakamwita yule mtu kipofu
wakamwambia, “Jipe moyo! Inuka, anakuita.”
50Akiwa analivua lile joho lake, alisimama na
kumwendea Yesu.
51Yesu akamwuliza, “Unataka nikufanyie
nini?”
Yule kipofu akajibu, “Mwalimu, nataka kuona.”
52Yesu akamwambia, “Nenda zako, imani yako
imekuponya.” Mara akapata kuona,
akamfuata Yesu njiani.

### *Yesu Aingia Yerusalemu Kwa Shangwe*

11 Walipokaribia Yerusalemu, wakafika
Bethfage na Bethania katika Mlima wa Mizeituni,
Yesu akawatuma wawili wa wanafunzi Wake,
2akiwaambia, “Nendeni kwenye kijiji kilichoko
mbele yenu na mara mwingiapo kijijini, mtakuta
mwana punda amefungwa, ambaye hajapandwa
na mtu ye yote. Mfungueni, mkamlete hapa.
3Kama mtu ye yote akiwauliza, ‘Mbona
mnamfungua?’ Mwambieni, ‘Bwana anamhitaji
na atamrudisha hapa baada ya muda
mfupi.’ ”
4Wakaenda, wakamkuta mwana punda
amefungwa kando ya barabara, karibu na mlango
wa nyumba. 5Walipokuwa wanamfungua, watu
waliokuwa wamesimama karibu wakawauliza,
“Mna maana gani mnapomfungua huyo mwana
punda?” 6Wakawajibu kama vile Yesu alivyokuwa
amewaagiza, nao wale watu wakawaruhusu.
7Kisha wakamleta huyo mwana punda kwa Yesu
na kutandika mavazi yao juu yake, naye
akampanda. 8Watu wengi wakatandaza mavazi
yao barabarani na wengine wakatandaza matawi
waliyokuwa wamekata mashambani. 9Kisha wale
waliokuwa wametangulia mbele na wale
waliokuwa wakifuata nyuma wakapaza sauti,
wakisema,

“Hosana!

Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!

10Umebarikiwa Ufalme unaokuja wa
baba yetu Daudi!

Hosana kwake Yeye Aliye Juu!”

11Yesu akaingia Yerusalemu na kwenda
hekaluni. Akaangalia kila kitu kilichokuwemo,
lakini kwa kuwa ilishakuwa jioni, akaenda Zake
Bethania pamoja na wale kumi na wawili.

### *Yesu Alaani Mtini Usiozaa*

12Kesho yake walipokuwa wakitoka Bethania,
Yesu alikuwa na njaa. 13 Alipouona mtini kwa
mbali, akaenda ili aone kama ulikuwa na
matunda. Alipoufikia, akakuta una majani tu, kwa
kuwa hayakuwa majira ya tini. 14Yesu akauambia
ule mti, ‘‘Tangu leo mtu ye yote na asile matunda
kutoka kwako tena.’’ Wanafunzi Wake walimsikia
akisema hayo.

### *Yesu Atakasa Hekaluni*

15Walipofika Yerusalemu, Yesu akaingia
hekaluni akaanza kuwafukuza wale waliokuwa
wananunua na kuuza humo ndani. Akapindua
meza za wale waliokuwa wakibadilisha fedha na
viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa, 16Wala
hakumruhusu mtu ye yote kuchukua bidhaa
kupitia ukumbi wa hekalu. 17Naye alipokuwa
akiwafundisha, akasema, “Je, haikuandikwa
kuwa:

“ ‘Nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala kwa
mataifa yote?’

Lakini ninyi mmeifanya kuwa ‘pango la
wanyang’anyi.’ ”

18Viongozi wa makuhani na walimu wa sheria
wakapata habari hizi, nao wakaanza kutafuta njia
ya kumwua, kwa kuwa walikuwa wakimwogopa,
kwa sababu umati wote wa watu walikuwa
wanashangazwa mafundisho Yake.

19Ilipofika jioni, Yesu na wanafunzi Wake
wakatoka nje ya mji.

### *Mtini Ulionyauka*

20Asubuhi yake, walipokuwa wakipita,
wakauona ule mtini umenyauka kutoka juu hadi
kwenye mizizi yake. 21Petro akakumbuka na
kumwambia Yesu, “Mwalimu, tazama! Ule mtini
ulioulaani umenyauka!’’

22Yesu akawajibu akawaambia, “Mwaminini
Mungu. 23Amin, amin nawaambia, mtu ye yote
atakayeuambia mlima huu ‘Ng’oka ukatupwe
baharini,’ wala asione shaka moyoni mwake, bali
aamini kwamba hayo asemayo yametukia,
yatakuwa yake. 24Kwa sababu hiyo nawaambia,
yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba
mmeyapokea nayo yatakuwa yenu. 25Nanyi kila
msimamapo kusali, sameheni, mkiwa na neno na
mtu ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe
na ninyi makosa yenu. 26Lakini kama ninyi
msiposamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni
hatawasamehe ninyi makosa yenu.’’

### *Wauliza Kuhusu Mamlaka Ya Yesu.*

27Wakafika tena Yerusalemu, wakati Yesu
akitembea hekaluni, viongozi wa makuhani,
walimu wa sheria pamoja na wazee wakamjia.
28Wakamwuliza, “Unafanya mambo haya kwa
mamlaka gani? Naye ni nani aliyekupa mamlaka
ya kufanya hayo?”

29Yesu akawajibu, ‘‘Nitawauliza swali mmoja.
Nijibuni, nami pia nitawaeleza ni kwa mamlaka gani
ninafanya mambo haya. 30 Niambieni, ubatizo wa
Yohana ulitoka mbinguni au kwa wanadamu? ”
31Wakasemezana wao kwa wao, wakisema, ‘‘Kama
tukisema, ‘ulitoka mbinguni,’ atatuuliza, ‘Mbona
hamkumwamini?’ 32Lakini tukisema, ‘ulitoka kwa
wanadamu,’ ’’ waliwaogopa watu kwa sababu kila
mtu aliamini kwamba Yohana
Mbatizaji alikuwa kweli nabii.
33Kwa hiyo wakamjibu Yesu, “Hatujui.’’

Naye Yesu akawaambia, ”Wala Mimi pia
sitawaambia ni kwa mamlaka gani ninafanya
mambo haya. ”

### *Mfano Wa Wapangaji Waovu*

**12** Yesu akaanza kusema nao kwa mifano,
akawaambia: ‘‘Mtu mmoja alipanda shamba la
mizabibu. Akajenga ukuta kulizunguka, akachimba
shimo ndani yake kwa ajili ya shinikizo la
kusindikia divai, akajenga mnara wa ulinzi.
Akalikodisha shamba hilo kwa wakulima, kisha
akasafiri kwenda nchi nyingine. 2 Wakati wa
mavuno ulipofika, mwenye shamba akamtuma
mtumishi wake kwa hao wakulima ili kuchukua
sehemu yake ya mavuno kutoka kwa hao
wapangaji. 3Lakini wale wakulima walimkamata
yule mtumishi, wakampiga, wakamfukuza mikono
mitupu. 4 Kisha yule mwenye shamba akamtuma
mtumishi mwingine kwao, wale wakulima
wakampiga kichwani na kumfanyia mambo ya
aibu. 5Kisha akatuma mtumishi mwingine, huyu
wakamwua. Akatuma wengine wengi, baadhi yao
wale wakulima wakawapiga na wengine
wakawaua.

6‘‘Mwenye shamba alikuwa amebakiwa na
mmoja wa kumtuma, huyu ni mwanawe
mpendwa. Hatimaye akamtuma akisema,
‘Watamheshimu mwanangu.’

7‘‘Lakini wale wapangaji wakasemezana wao

kwa wao, wakisema, 'Huyu ndiye mrithi, njoni tumwue, nao urithi utakuwa wetu.' 8Hivyo wakamkamata, wakamwua na kumtupa nje ya lile shamba la mizabibu.

9 "Mnadhani yule mwenye shamba atafanya nini? Atakuja na kuwaua hao wapangaji, kisha atawapa wapangaji wengine hilo shamba la mizabibu. 10Je, hamjasoma maandiko haya:

" 'Jiwe lile walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni,
11Bwana amefanya jambo hili,
nalo ni ajabu machoni petu?' "

12Walipotambua kuwa amesema mfano huu kwa ajili yao wakataka kumkamata, lakini wakaogopa ule umati wa watu. Wakamwacha wakaondoka, wakaenda zao.

### *Swali Kuhusu Kulipa Kodi*

13Baadaye wakawatuma baadhi ya Mafarisayo na Maherode ili kuja kumtega Yesu katika yale anayosema. 14Wakamjia, wakamwambia, "Mwalimu, tunajua ya kuwa Wewe ni mtu mwadilifu. Wewe huyumbishwi na wanadamu, kwa kuwa hujali kwamba wao ni nani. Lakini Wewe hulifundisha neno la Mungu sawasawa na kweli. Je, ni haki kumlipa Kaisari kodi au la? 15Je, tulipe kodi au tusilipe?"

Lakini Yesu alijua unafiki wao. Akawauliza "Mbona mnajaribu kunitega? Nileteeni hiyo dinari[a] niione." 16 Wakamletea hiyo sarafu. Naye akawauliza, "Picha hii ni ya nani na maandishi haya ni ya nani?"

Wakamjibu, "Ni ya Kaisari."

17Ndipo Yesu akawaambia, "Mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari na kilicho cha Mungu mpeni Mungu."

Nao wakamstaajabia sana.

### *Ndoa Wakati Wa Ufufuo*

18Kisha Masadukayo, wale wasemao kuwa hakuna ufufuo wakamjia Yesu, 19wakasema, "Mwalimu, Mose alituandikia kuwa kama ndugu wa mtu akifa na kumwacha mkewe bila mtoto, basi ndugu yake atamwoa huyo mjane ili amzalie ndugu yake watoto. 20Basi walikuwapo ndugu saba. Yule wa kwanza akaoa na akafa pasipo kuwa na mtoto ye yote. 21Wa pili akamwoa yule mjane, lakini naye akafa bila kuacha mtoto ye yote. Ikawa vivyo hivyo kwa yule wa tatu. 22Hakuna hata mmojawapo wa hao ndugu wote saba aliyeacha mtoto. Hatimaye naye yule mwanamke akafa. 23Kwa hiyo wakati wa ufufuo, watakapofufuka wote, huyo atakuwa mke wa nani maana aliolewa na ndugu wote saba?"

24Yesu akawajibu, "Je, hampotoki kwa sababu hamjui maandiko wala uweza wa Mungu? 25Wafu watakapofufuka, hawataoa wala kuolewa, watakuwa kama malaika wa mbinguni. 26Basi kuhusu ufufuo wa wafu: Je, hamjasoma katika kitabu cha Mose jinsi Mungu alivyosema na Mose kutoka katika kile kichaka akisema, 'Mimi, ni Mungu wa Abrahamu na Mungu wa Isaki na Mungu wa Yakobo?' 27Mungu si Mungu wa wafu, bali ni Mungu wa walio hai. Kwa hiyo mmekosea kabisa."

### *Amri Iliyo Kuu*

28Mwalimu mmoja wa sheria akaja akawasikia wakijadiliana. Akiona kwamba Yesu amewajibu vema, naye akamwuliza, "Katika amri zote, ni ipi iliyo kuu?"

29Yesu akajibu, "Amri iliyo kuu ndiyo hii, 'Sikiza Ee Israeli, Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. 30Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.' 31Ya pili ndiyo hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi."

32 Yule mwalimu wa sheria akamwambia Yesu, "Mwalimu, umejibu vema kwamba Mungu ni mmoja wala hakuna mwingine ila Yeye. 33Kumpenda Mungu kwa moyo wote na kwa akili zote na kwa nguvu zote na kumpenda jirani kama mtu anavyojipenda mwenyewe ni bora zaidi kuliko kutoa sadaka ya kuteketezwa na dhabihu."

34Yesu alipoona kwamba amejibu kwa busara, akamwambia, "Wewe hauko mbali na Ufalme wa Mungu." Tangu wakati huo, hakuna mtu ye yote aliyethubutu kumwuliza maswali tena.

### *Kristo Ni Mwana Wa Nani?*

35Wakati Yesu alipokuwa akifundisha hekaluni, akauliza, "Imekuwaje walimu wa sheria wanasema kwamba Kristo ni Mwana wa Daudi? 36Kwa maana Daudi mwenyewe akinena kwa

[a]15Dinari ni sarafu ya fedha iliyokuwa inatumik a wakati huo, sawa na mshahara wa kibarua wa siku moja

kuongozwa na Roho Mtakatifu alisema:

" 'BWANA alimwambia Bwana wangu:
Keti mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako.' "

37Kwa hiyo Daudi mwenyewe anamwita 'Bwana',
awezaje basi Yeye kuwa mwanawe?" Ule umati
wote wa watu wakamsikiliza kwa furaha.

### *Yesu Awatahadharisha Watu Kuhusu Walimu Wa Sheria*

38Alipokuwa akifundisha, Yesu alisema,
"Jihadharini na walimu wa sheria. Wao hupenda
kutembea wakiwa wamevaa mavazi marefu na
kusalimiwa kwa heshima masokoni. 39Pia wao
hupenda kukaa viti vya mbele katika masinagogi
na kupewa nafasi za heshima katika karamu.
40Wao hula nyumba za wajane na ili waonekane
kuwa wema wanasali sala ndefu. Watapata
hukumu iliyo kuu sana."

### *Sadaka Ya Mjane*

41Kisha Yesu akaketi mkabala na sehemu
sadaka zilikokuwa zinawekwa na kuangalia umati
wa watu wakati wakitoa fedha zao kwenye hazina
ya hekalu. Matajiri wengi wakaweka kiasi kikubwa
cha fedha. 42Lakini mjane mmoja maskini akaja
na kuweka sarafu mbili ndogo za shaba zenye
thamani ya senti mbili.''

43Yesu akawaita wanafunzi Wake
akawaambia, "Amin, amin nawaambia,, huyu
mjane maskini ametoa zaidi katika hazina kuliko
wengine wote. 44Wengine wote wametoa
kutokana na ziada ya mali zao, lakini huyu mjane
kutokana na umaskini wake, ametoa kila kitu
alichokuwa nacho, hata kile alichohitaji ili kuishi."

### *Dalili Za Siku Za Mwisho*

**13** Wakati Yesu alipokuwa akitoka hekaluni,
mmojawapo wa wanafunzi Wake
akamwambia, "Mwalimu!,Tazama jinsi mawe haya
yalivyo makubwa na majengo haya yalivyo
mazuri!''

2Ndipo Yesu akajibu akasema, ''Je, unayaona
majengo haya yalivyo makubwa? Hakuna hata
jiwe moja litakalobaki juu ya jingine, yote
yatabomolewa.''

3Yesu alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa
Mizeituni mkabala na hekalu, Petro, Yakobo,
Yohana na Andrea wakamwuliza faraghani,
4"Tafadhali tuambie, mambo haya yatatukia lini?
Nayo ni nini ishara ya wakati hayo yote
yanapokaribia kutimia?''

5Yesu akawaambia: "Jihadharini mtu ye yote
asiwadanganye. 6Wengi watakuja kwa Jina Langu
wakidai, 'Mimi ndiye', nao watawadanganya
wengi. 7Msikiapo habari za vita na uvumi juu ya
vita, msiwe na hofu. Mambo haya hayana budi
kutukia, lakini ule mwisho bado. 8Taifa litainuka
dhidi ya taifa na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa
na matetemeko sehemu mbalimbali na njaa. Huu
ndio mwanzo wa utungu.

### *Mateso Yatabiriwa*

9"Lakini ninyi jihadharini. Kwa maana
watawapeleka mahakamani na kuwapiga mijeledi
katika masinagogi. Mtashtakiwa mbele ya
watawala na wafalme kwa ajili Yangu, ili kuwa
ushuhuda kwao. 10Nayo Habari Njema lazima
ihubiriwe kwanza kwa mataifa yote kabla ule
mwisho haujaja. 11Mtakapokamatwa na
kushtakiwa, msisumbuke kuhusu mtakalosema.
Semeni tu lo lote mtakalopewa wakati huo, kwa
kuwa si ninyi msemao bali ni Roho Mtakatifu.

12"Ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe,
baba atamsaliti mwawe. Watoto watawaasi
wazazi wao na kusababisha wauawe. 13Watu
wote watawachukia kwa ajili ya Jina Langu,lakini
atakayevumilia hata mwisho ataokoka.

### *Chukizo La Uharibifu*

14"Mtakapoona chukizo la uharibifu limesimama
mahali pasipolipasa (asomaye na afahamu), basi
wale walioko Uyahudi na wakimbilie milimani.
15Yeye aliyeko juu ya dari ya nyumba asishuke au
kuingia ndani ili kuchukua kitu cho chote. 16Aliye
shambani asirudi nyumbani kuchukua vazi lake. 17
Ole wao wenye mimba na wale wanaonyonyesha
watoto siku hizo! 18Ombeni mambo haya yasitokee
wakati wa baridi. 19Kwa maana siku hizo itakuwako
dhiki kuu ambayo haijapata kuwako tangu mwanzo
wa uumbaji, hapo Mungu alipoumba ulimwengu
mpaka leo na wala haitakuwako tena kamwe.
20Kama Bwana asingelifupiza siku hizo, kamwe
asingeliokoka mtu ye yote, lakini kwa ajili ya
wateule, wale aliowachagua, amezifupiza siku hizo.
21"Wakati huo mtu ye yote akiwaambia, 'Tazama,
Kristo

huyu hapa!' au, 'Tazama, yuko kule,' msiamini.
22Kwa maana watatokea makristo wa uongo na
manabii wa uongo nao watafanya ishara na
maajabu ili kuwapotosha, ikiwezekana hata wale
wateule. 23Hivyo jihadharini, nimekwisha
kuwaambia mambo haya yote mapema kabla
hayajatukia."

### *Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*

24"Lakini katika siku hizo, baada ya hiyo dhiki,

" 'jua litatiwa giza
na mwezi hautatoa nuru yake,
25nyota zitaanguka kutoka angani,
nazo nguvu za anga zitatikisika.'

26"Ndipo watu wote watakapomwona Mwana
wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na
utukufu. 27Naye atawatuma malaika Wake
wawakusanye wateule Wake kutoka pande zote
nne za dunia, kutoka miisho ya dunia hadi miisho
ya mbingu.

### *Somo Kuhusu Mtini*

28"Basi jifunzeni somo hili kutokana na mtini:
Mara mwonapo matawi yake yakishipua na kutoa
majani, mnajua kwamba wakati wa kiangazi
umekaribia. 29 Vivyo hivyo, myaonapo mambo
haya yakitukia, tambueni kwamba Kristo yu karibu
malangoni. 30Amin, amin nawaambia, kizazi hiki
hakitapita hadi mambo haya yote yametukia.
31Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno Yangu
hayatapita kamwe.

### *Hakuna Ajuaye Siku Wala Saa*

32"Lakini kwa habari ya siku ile na saa
hakuna ye yote ajuaye,hata malaika walioko
mbinguni wala hata Mwana hajui, ila Baba peke
Yake. 33Jiharadharini! Kesheni! Kwa maana
hamjui wakati ule utakapowadia. 34Ni kama mtu
anayesafiri akiiacha nyumba yake na kuwaachia
watumishi wake kuiangalia, kila mtu na kazi yake,
kisha akamwambia yule bawabu aliye mlangoni
akeshe.

35"Basi kesheni kwa sababu hamjui ni lini
mwenye nyumba atakaporudi, iwapo ni jioni, au
kwamba ni usiku wa manane, au alfajiri awikapo
jogoo, au wakati wa mapambazuko. 36Kama akija
ghafula, asije akawakuta mmelala. 37Lile
ninalowaambia ninyi, nawaambia watu wote:
'Kesheni.' "

### *Shauri La Kumwua Yesu*

**14** Zilikuwa zimebaki siku mbili tu kabla ya
Sikukuu ya Pasaka na Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu. Viongozi wa makuhani na walimu wa
sheria walikuwa wakitafuta njia ya kumkamata
Yesu kwa hila na kumwua, 2kwa kuwa walisema,
"Tusilifanye jambo hili wakati wa Sikukuu, maana
watu wanaweza wakafanya
ghasia."

### *Yesu Kupakwa Mafuta Huko Bethania*

3Yesu alipokuwa huko Bethania nyumbani
kwa Simoni aliyekuwa na ukoma, wakati
alipokuwa ameketi mezani akila chakula cha jioni,
mwanamke mmoja aliingia akiwa na chupa ya
marmar yenye manukato ya nardo[a] safi ya
thamani kubwa. Akaivunja hiyo chupa, akamiminia
hayo manukato kichwani mwa Yesu.

4Baadhi ya watu waliokuwapo pale walikuwa
wakisemezana wao kwa wao, "Kwa nini ubadhirifu
huu wa manukato? 5Mafuta haya yangeweza
kuuzwa kwa zaidi ya dinari 300[b] na fedha hizo
wakapewa maskini." Wakamkemea vikali huyo
mwanamke.

6Lakini Yesu akawaambia, "Kwa nini
mnamsumbua? Mwacheni! Amenitendea jambo la
kupendeza. 7Maskini mnao pamoja nanyi siku
zote na mnaweza kuwasaidia wakati wo wote
mnaotaka. Lakini Mimi hamko nami daima. 8Huyu
mwanamke amenitendea lile aliloweza. Ameutia
mwili wangu manukato kuniandaa kwa maziko
Yangu. 9Amin, amin nawaambia, mahali po pote
duniani ambapo Injili itahubiriwa, jambo hili
alilotenda huyu mwanamke litatajwa kwa
ukumbusho wake. "

### *Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*

10Kisha Yuda Iskariote, mmoja wa wale
wanafunzi kumi na wawili wa Bwana Yesu,
akaenda kwa viongozi wa makuhani ili kumsaliti
Yesu kwao. 11Walifurahi sana kusikia jambo hili
na wakaahidi kumpa fedha. Hivyo yeye akawa
anatafuta wasaa mzuri wa kumtia Yesu mikononi
mwao.

---

**a**[3] Nardo ni aina ya manukato yaliyokuwa yanatengenezwa kutokana na mimea yenye mizizi inayotoa harufu nzuri.

**b**[5] Dinari 300 ni sawa na mshahara wa kibarua kwa siku 300. Dinari moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa siku moja.

### *Yesu Ala Pasaka Na Wanafunzi Wake*

12Siku ya kwanza ya Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu, siku ambayo kwa desturi kondoo wa Pasaka huchinjwa, wanafunzi wa Yesu wakamwuliza, "Unataka tuende wapi ili tukuandalie mahali pa kula Pasaka?"

13Basi akawatuma wawili miongoni mwa wanafunzi Wake, akawaambia, "Nendeni mjini, huko mtakutana na mwanamume amebeba mtungi wa maji. Mfuateni.
14Mwambieni mwenye nyumba ile atakayoingia, 'Mwalimu anauliza, kiko wapi chumba changu kwa ajili ya wageni ambamo nitakula Pasaka pamoja na wanafunzi Wangu?'
15Atawaonyesha chumba kikubwa ghorofani, kilichopambwa tena kilicho tayari. Tuandalieni humo."

16 Wale wanafunzi wakaondoka na kwenda mjini, nao wakakuta kila kitu kama alivyowaambia. Hivyo wakaandaa chakula cha Pasaka.

17Ilipofika jioni, Yesu akaja pamoja na wale wanafunzi wake kumi na wawili.
18 Walipokwisha kuketi kwenye nafasi zao, wakati wakila Yesu akawaambia, ''Amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti, yaani, yeye anayekula pamoja nami.''

19Wakaanza kuhuzunika na kumwambia mmoja baada ya mwingine, "Je, ni mimi Bwana?"

20Akawajibu, "Ni mmoja miongoni mwenu ninyi kumi na wawili, yule anayechovya mkate kwenye bakuli pamoja nami.
21Kwa kuwa Mwana wa Adamu yu aenda Zake kama vile alivyoandikiwa. Lakini ole wake mtu yule amsalitiye Mwana wa Adamu! Ingelikuwa heri kama asingelizaliwa."

### *Kuanzishwa Kwa MezaYa Bwana*

22Walipokuwa wakila, Yesu akachukua mkate, akashukuru, akaumega na kuwapa wanafunzi Wake akisema, "Kuleni, huu ndio mwili Wangu.''

23Kisha akachukua kikombe, akashukuru, akawapa wanafunzi Wake, wote wakanywa kutoka humo.

24Akawaambia, "Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi.
25Amin nawaambia, sitakunywa tena uzao wa mzabibu mpaka siku ile nitakapokunywa mpya katika Ufalme wa Mungu.''

26Walipokwisha kuimba wimbo, wakatoka wakaenda kwenye Mlima wa Mizeituni.

### *Yesu Atabiri Kuwa Petro Atamkana*

27Yesu akawaambia, "Ninyi nyote mtaniacha, kwa maana imeandikwa:

'Nitampiga mchungaji,
nao kondoo watatawanyika.'

28Lakini baada ya kufufuka, nitawatangulia kwenda Galilaya."

29Petro akasema, "Hata kama wengine wote watakuacha, mimi sitakuacha.''

30 Yesu akamwambia, "Amin, nakwambia, leo, usiku huu huu, kabla jogoo hajawika mara mbili, utanikana mara tatu.''

31 Lakini Petro akasisitiza akasema, ''Hata kama inanipasa kufa pamoja nawe, sitakukana.'' Nao wale wanafunzi wengine wote wakasema vivyo hivyo.

### *Yesu Akiomba Bustanini Gethsemane*

32Wakaenda mahali paitwapo Gethsemane, Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kaeni hapa wakati ninakwenda kule kuomba.''
33Kisha akawachukua pamoja naye Petro, Yakobo na Yohana. Naye akaanza kuhuzunika sana na kutaabika.
34Akawaambia, "Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe."

35Akaenda mbele kidogo, akajitupa chini kifudifudi akaomba akisema, kama ikiwezekana saa hiyo ya mateso imwepuke.
36Akasema, "Aba[c], Baba, mambo yote yawezekana Kwako. Niondolee kikombe hiki, lakini si kama nitakavyo Mimi, bali mapenzi Yako yatimizwe.''

37Akarudi kwa wanafunzi Wake akawakuta wamelala, naye akamwambia Petro, "Simoni, umelala? Je, hukuweza kukesha hata kwa saa moja?
38Kesheni na kuomba msije mkaingia majaribuni. Roho iko radhi lakini mwili ni dhaifu.''

39Akaenda tena kuomba akisema maneno yale yale.
40Aliporudi kwa wanafunzi Wake, akawakuta tena wamelala, kwa sababu macho yao yalikuwa mazito. Nao hawakujua la kumwambia.

41Akaja mara ya tatu, akawaambia, ''Bado mmelala na kupumzika? Imetosha! Saa imewadia. Tazama, Mwana wa Adamu anasalitiwa mikononi

---

c36 Aba ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni baba.Ni mtoto wa kuzaa tu ndiye ambaye angeweza kulitumia kwa baba yake

mwa wenye dhambi. 42Amkeni ! Twendeni zetu ! Tazameni, msaliti Wangu yu aja!"

### *Yesu Akamatwa*

43Yesu alipokuwa bado anazungumza, Yuda, mmoja wa wale wanafunzi kumi na wawili, akatokea akiwa pamoja na umati wa watu wenye panga na marungu, waliokuwa wametumwa na viongozi makuhani, walimu wa sheria na wazee.

44Basi Yuda, yule msaliti, alikuwa amewapa ishara wale watu kuwa: "Yule nitakayembusu, ndiye, mkamateni na mchukueni akiwa chini ya ulinzi.'' 45Kwa hiyo Yuda alipofika, akamwendea Yesu akamwambia, "Rabi'' [d] na kumbusu. 46Wale watu wakamkamata Yesu, wakamweka chini ya ulinzi. 47Ndipo mmoja wa wale waliokuwa wamesimama karibu akachomoa upanga wake na kumpiga mtumishi wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio.

48Kisha Yesu akawaambia, "Mmekuja mkiwa na panga na marungu kana kwamba Mimi ni mnyang'anyi ? 49Siku zote nilikuwa pamoja nanyi nikifundisha hekaluni, wala hamkunikamata. Lakini maandiko na yatimie." 50Ndipo wanafunzi Wake wote wakamwacha, wakakimbia.

51Kijana mmoja, ambaye hakuwa amevaa kitu isipokuwa alijitanda nguo ya kitani, alikuwa akimfuata Yesu. Wakamkamata, 52akakimbia uchi, akaliacha vazi lake.

### *Yesu Mbele Ya Baraza*

53Wakampeleka Yesu kwa Kuhani Mkuu, nao viongozi wa makuhani, wazee na walimu wa sheria wakakusanyika pamoja. 54Petro akamfuata kwa mbali, mpaka kwenye ua wa Kuhani Mkuu. Huko akaketi pamoja na walinzi, akiota moto.

55Viongozi wa makuhani na wajumbe wote wa Baraza[e] walikuwa wanatafuta ushahidi dhidi ya Yesu ili wapate kumwua, lakini hawakupata. 56Wengi wakatoa ushahidi wa uongo dhidi Yake, lakini maelezo yao hayakukubaliana.

57Ndipo wengine wakasimama wakatoa ushahidi wa uongo dhidi Yake, wakisema, 58''Sisi tulimsikia akisema, 'Mimi nitalibomoa hekalu hili lililojengwa na wanadamu na katika siku tatu nitajenga jingine ambalo halikujengwa na wanadamu.' '' 59Lakini hata hivyo, ushahidi wao haukukubaliana.

60Kuhani Mkuu akasimama mbele ya hilo Baraza akamwuliza Yesu, "Je, Wewe huwezi kujibu mashtaka haya ambayo watu hawa wameleta juu Yako?" 61 Lakini Yesu akakaa kimya, hakusema neno lo lote.

Kuhani Mkuu akamwuliza tena, "Je, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Mbarikiwa?"

62Yesu akajibu, "Mimi ndimi, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenye Nguvu, akija na mawingu ya mbinguni."

63Kuhani Mkuu akararua mavazi yake, akasema, "Tuna haja gani tena ya mashahidi zaidi? 64 Ninyi mmemsikia hayo makufuru. Uamuzi wenu ni nini?"

Wote wakamhukumu kwamba anastahili kifo. 65Kisha baadhi ya watu wakaanza kumtemea mate, wakamfunga kitambaa machoni, wakampiga kwa ngumi na kumwambia, "Tabiri ni nani aliyekupiga!'' Walinzi wakamchukua na kumpiga makofi.

### *Petro Amkana Yesu*

66Petro alipokuwa bado yuko chini kwenye ua wa jumba la kifalme tazama akaja mmoja wa watumishi wa kike wa Kuhani Mkuu. 67Alipomwona Petro akiota moto, akamtazama sana, akamwambia,

"Wewe pia ulikuwa pamoja na Yesu Mnazareti."

68Lakini Petro akakana, akasema, "Sijui wala sielewi unalosema." Naye akaondoka kuelekea kwenye njia ya kuingilia.

69Yule mtumishi wa kike alipomwona hapo mahali, akawaambia tena wale waliokuwa wamesimama hapo, "Huyu mtu ni mmoja wao.'' 70Lakini Petro akakana tena.

Baada ya muda kidogo wale waliokuwa wamesimama hapo karibu na Petro wakamwambia, ''Hakika wewe ni mmoja wao, kwa maana wewe pia ni Mgalilaya!'' 71Petro akaanza kulaani na kuapa, akawaambia, ''Simjui huyu mtu mnayemsema habari Zake.''

72Papo hapo jogoo akawika mara ya pili. Ndipo Petro akakumbuka lile neno Yesu alilokuwa

---

d45 "Rabi" hapa ni neno la Kiebrenia ambalo maana yake ni daktari, mwalimu, au Bwana.Walikuwa na madaraja matatu: La chini kabisa "rab" (bwana), la pili "rabbi" (bwana wangu), la juu kabisa (mkuu wangu,bwana wangu)

e55 Baraza hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la uatawala la Kiyahudi,lililoundwa na wazee 70 pamoja na Kuhani Mkuu

amemwambia, “Kabla jogoo hajawika mara mbili,
utanikana mara tatu.’’ Akalia sana.

### *Yesu Mbele Ya Pilato*

**15** Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani,
pamoja na wazee, walimu wa sheria na Baraza
lote, wakafikia uamuzi.
Wakamfunga Yesu, wakamchukua na kumkabidhi
kwa Pilato.

2Pilato akamwuliza, “Je, Wewe ndiye Mfalme
wa Wayahudi?”

Yesu akajibu,” Wewe umesema.”

3Viongozi wa makuhani wakamshtaki kwa
mambo mengi. 4Pilato akamwuliza tena, “Je, huna
la kujibu? Tazama ni mashtaka mangapi
wanayaleta juu yako.’’

5Lakini Yesu hakuendelea kujibu, hivyo Pilato
akashangaa.

### *Pilato Amtoa Yesu Ili Akasulibiwe*

6Ilikuwa desturi wakati wa Sikukuu ya Pasaka
kumfungulia mfungwa ye yote ambaye watu
wangemtaka. 7Wakati huo, mtu mmoja aitwaye
Baraba alikuwa amefungwa gerezani pamoja na
waasi wengine waliokuwa wamesababisha mauaji
wakati wa maasi yaliyotokea dhidi ya Serikali.8Ule
umati wa watu ukamjia Pilato na kumwomba
awafanyie kama ilivyokuwa desturi yake.

9 Pilato akawauliza, “Mnataka niwafungulie
huyu Mfalme wa Wayahudi?’’ 10Kwa maana yeye
alitambua kuwa viongozi wa makuhani walikuwa
wamemtia Yesu mikononi mwake kwa ajili ya
wivu. 11Lakini viongozi wa makuhani
wakauchochea ule uamati wa watu wamwombe
awafungulie Baraba badala Yake.

12Pilato akawauliza tena, “Basi mnataka
nifanye nini na huyu mtu mnayemwita Mfalme wa
Wayahudi?’’

13Wakapiga kelele, “Msulibishe!’’

14Akawauliza, “Kwa nini? Amefanya kosa
gani?’’

Lakini wao wakapiga kelele kwa nguvu zaidi,
wakisema, ‘‘Msulibishe!’’

15 Pilato akitaka kuuridhisha ule umati wa
watu, akawafungulia Baraba, naye baada ya
kuamuru Yesu achapwe mijeledi, akamtoa ili
asulibishwe.

### *Maaskari Wamdhihaki Yesu*

16Maaskari wakampeleka Yesu hadi kwenye
ukumbi wa ndani wa jumba la kifalme, ndio
Praitoria[a], wakakusanya kikosi kizima cha
maaskari. 17Wakamvalisha Yesu joho la
zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamvisha
kichwani. 18Wakaanza kumsalimu kwa dhihaka,
“Salamu, Mfalme wa Wayahudi!’’ 19Wakampiga
kwa fimbo ya mwanzi tena na tena kichwani na
kumtemea mate. Wakapiga magoti mbele Yake
wakasujudia kwa kumdhihaki. 20Walipokwisha
kumdhihaki, wakamvua lile joho la zambarau,
wakamvika zile nguo Zake mwenyewe. Kisha
wakamtoa nje ili wakamsulibishe.

### *Kusulibiwa Kwa Yesu*

21Mtu mmoja kutoka Kirene, jina lake Simoni,
baba yao Aleksanda na Rufo, alikuwa anapita
zake kuingia mjini kutoka shamba,
wakamlazimisha aubebe ule msalaba wa Yesu.
22Kisha wakampeleka Yesu mpaka mahali
palipoitwa Golgota, (ambayo, maana yake ni
Mahali pa Fuvu la Kichwa). 23Nao wakampa divai
ilichanganywa na manemane, lakini hakuiinywa.
24Basi wakamsulibisha, nazo nguo Zake
wakagawana miongoni mwao kwa kuzipigia kura
ili kuamua ni nini kila mtu atakachochukua.

25Ilikuwa yapata saa tatu asubuhi
walipomsulibisha. 26Tangazo likaandikwa la
mashtaka dhidi Yake lenye maneno haya:
“MFALME WA WAYAHUDI.” 27Pamoja naye
walisulibiwa wanyag’anyi wawili mmoja upande
Wake wa kuume na mwingine upande wa
kushoto. 28Nayo maandiko yakatimizwa, yale
yasemayo, “Alihesabiwa pamoja na watenda
dhambi.” 29Watu waliokuwa wakipita karibu
wakamtukana na kutikisa vichwa vyao kwa mzaha
wakisema, “Aha! Wewe ambaye ungelibomoa
hekalu na kulijenga kwa siku tatu, 30basi ujiokoe
mwenyewe na ushuke kutoka msalabani.”

31Vivyo hivyo viongozi wa makuhani pamoja
na walimu wa sheria wakamdhihaki miongoni
mwao wakisema, “Yeye aliwaokoa wengine, lakini
hawezi kujiokoa mwenyewe! 32Basi huyu Kristo,
huyu Mfalme wa Wayahudi, ashuke sasa kutoka
msalabani, ili tupate kuona na kuamini.” Wale
waliosulibiwa pamoja naye pia wakamtukana.

---

a16 Praitoria maana yake makao makuu ya mtawala. Jumba la kifalme lilokuwa linakaliwa na Pontio Pilato huko Yerusalemu, palipokuwa na kiti cha hukumu

### *Kifo Cha Yesu Msalabani*

33Ilipofika saa sita, giza lilifunika nchi yote
mpaka saa tisa. 34Mnamo saa tisa Yesu akalia
kwa sauti kuu, akasema, ''Eloi, Eloi lama
Sabakthani?'' Maana yake, "Mungu Wangu,
Mungu Wangu, mbona umeniacha?''

35Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama
karibu waliposikia maneno hayo, wakasema,
''Msikieni anamwita Eliya.''

36Mtu mmoja akaenda mbio, akachovya
sifongo kwenye siki, akaiweka kwenye mwanzi,
akampa Yesu ili anywe akisema, "Basi mwacheni,
hebu tuone kama Eliya atakuja kumshusha kutoka
hapo msalabani''

37Kisha Yesu akatoa sauti kuu, akakata roho.

38Pazia la hekalu likachanika vipande viwili
kuanzia juu hadi chini. 39Basi yule jemadari,
aliyekuwa amesimama hapo mbele ya msalaba
wa Yesu, aliposikia ile sauti Yake na kuona jinsi
alivyokata roho, akasema, "Hakika mtu huyu
alikuwa Mwana wa Mungu!''

40Walikuwapo pia wanawake waliokuwa
wakiangalia kwa mbali, ambao miongoni mwao
alikuwa Maria Magdalene, Maria mama yao
Yakobo mdogo na Yose, pia na Salome. 41Hawa
walifuatana na Yesu na kumhudumia alipokuwa
Galilaya. Pia walikuwapo wanawake wengine
wengi waliokuwa wamekuja pamoja naye
Yerusalemu.

### *Maziko Ya Yesu*

42Ilipofika jioni, kwa kuwa ilikuwa Siku ya
Maandalizo, siku moja kabla ya Sabato, 43Yosefu
wa Arimathaya mtu aliyeheshimiwa katika Baraza,
ambaye yeye mwenyewe alikuwa anautarajia
Ufalme wa Mungu, akamwendea Pilato kwa ujasiri
na kumwomba huo mwili wa Yesu. 44Pilato
alikuwa akijiuliza kama Yesu alikuwa amekwisha
kufa. Akamwita yule jemadari, akamwuliza iwapo
Yesu alikuwa amekwisha kufa. 45Baada ya kupata
habari kutoka kwa yule jemadari kwamba kweli
amekwisha kufa, Pilato akampa Yosefu ruhusa ya
kuuchukua huo mwili. 46Hivyo Yosefu akanunua
kitambaa cha kitani safi, akaushusha mwili wa
Yesu kutoka msalabani, akauviringishia kile
kitambaa cha kitani na akamweka ndani ya kaburi
lililochongwa kwenye mwamba. Kisha
akalivingirisha jiwe kwenye ingilio la kaburi.
47Maria Magdalene na Maria mamaye Yose
walipaona mahali pale alipolazwa.

### *Kufufuka Kwa Yesu*

16 Sabato ilipomalizika, Maria Magdalene,
Maria mama yake Yakobo na Salome walinunua
manukato ili wakaupake mwili wa Yesu. 2Asubuhi
na mapema, siku ya kwanza ya juma, mara tu
baada ya kuchomoza jua walikwenda kaburini.
3Njiani wakawa wanaulizana wao kwa wao, "Ni nani
atakayetuvingirishia lile
jiwe kutoka kwenye ingilio la kaburi?''

4Lakini walipotazama, wakaona lile jiwe,
ambalo lilikuwa kubwa sana, limekwisha
kuvingirishwa kutoka pale penye ingilio la kaburi.
5Walipokuwa wakiingia mle kaburini, wakamwona
kijana mmoja aliyevaa joho jeupe akiwa ameketi
upande wa kuume, nao wakastaajabu.

6Yule malaika akawaambia, "Msistaajabu.
Mnamtafuta Yesu Mnazareti aliyesulibiwa.
Amefufuka! Hayuko hapa. Patazameni mahali
walipomlaza. 7Lakini nendeni mkawaambie
wanafunzi Wake pamoja na Petro, kwamba
'Anawatangulia kwenda Galilaya, huko ndiko
mtakakomwona, kama alivyowaambia.' "

8Hivyo wakatoka wakakimbia kutoka mle
kaburini, kwani hofu kuu na mshangao ulikuwa
umewapata, nao hawakumwambia mtu ye yote
neno lo lote.

### *Yesu Anamtokea Maria Magdalene*

9Yesu alipofufuka alfajiri na mapema siku ya
kwanza ya juma alimtokea kwanza Maria
Magdalene, yule ambaye alikuwa amemtoa pepo
wachafu saba. 10Maria akaenda akawaambia
wale waliokuwa wakifuatana na Yesu, ambao
walikuwa wanaomboleza na kulia. 11Lakini
waliposikia kwamba Yesu yu hai na kwamba
Maria alikuwa amemwona, hawakusadiki.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Wawili*

12Baadaye Yesu akawatokea wawili miongoni
mwa wanafunzi Wake walipokuwa wakienda
shambani akiwa katika sura nyingine. 13Nao
wakarudi na kuwaambia wenzao. Lakini
hawakuwasadiki wao pia.

### *Yesu Awaagiza Wale Wanafunzi Kumi Na Mmoja*

14 Baadaye Yesu akawatokea wale wanafunzi
Wake kumi na mmoja, walipokuwa wakila
chakula. Akawakemea kwa kutokuamini kwao na

kwa ugumu wa mioyo yao kwa sababu
hawakuwasadiki wale waliomwona baada ya
kufufuka.

15 Akawaambia, “Enendeni ulimwenguni
mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. 16 Ye yote
aaminiye na kubatizwa ataokoka. Lakini ye yote
asiyeamini atahukumiwa. 17 “Nazo ishara hizi
zitafuatana na wale waaminio: Kwa Jina Langu
watatoa pepo wachafu, watasema kwa lugha
mpya, 18 watashika nyoka kwa mikono yao na
hata wakinywa kitu cho chote cha kuua,
hakitawadhuru kamwe, wataweka mikono yao juu
ya wagonjwa, nao watapona.”

### *Yesu Apaa Kwenda Mbinguni*

19 Baada ya Bwana Yesu kusema nao,
alichukuliwa juu mbinguni na kuketi mkono wa
kuume wa Mungu. 20 Kisha wanafunzi Wake
wakatoka, wakahubiri kila mahali, naye Bwana
akatenda kazi pamoja nao na kulithibitisha neno
Lake kwa ishara zilizofuatana nalo.Amen.

## LUKA

### *Utangulizi*

Luka alikuwa tabibu aliyefuatana na Mtume Paulo katika safari zake za kitume. Injili hii ndiyo ndefu kuliko zote. Aliandika kwa msomi mmoja wa Kiyunani aliyeitwa Theofilo *(1:3).*Utangulizi wa Injili ya Luka na Matendo ya Mitume zinaunganisha vitabu hivi viwili pamoja .Vyote vinaandikiwa mtu mmoja , yaani, Theofilo, ambaye maana ya jina lake ni "mpenzi wa Mungu." Utangulizi wa Matendo unarejea juu ya "mambo yale ya kwanza "kuhusiana na yale Yesu aliyoanza kufanya na kufundisha."

Utambulisho wa Luka kama mwandishi unaonekana katika *Mdo.16:10* anapotumia neno "tulijiandaa," linaloashiria kwamba alikuwa akishirikiana na Paulo katika safari zake za kitume na kuandika habari za shughuli zake na matukio yote.Lugha na mtindo wa uandishi wa Injili ya Luka na Matendo unaonyesha kuwa yeye ni mtu mtaalamu mwenye uwezo mkubwa wa kuandika kwa ufasaha, aliye na elimu ya juu, mwenye asili na mtazamo wa Kiyunani.

Kuna uwezekano mkubwa kwamba Luka alikuwa Mmataifa kutoka Antiokia ya Syria aliyeokoka, ambaye aliungana na Paulo huko Troa katika safari yake ya pili ya kitume. Wakati Paulo akiwa kifungoni sehemu mbalimbali, si kwamba Luka alishughulika na kuhubiri tu, bali pia alitumia muda mwingi kujifunza na kuchunguza kwa undani maisha ya Kristo. Ingawa kuna kazi nyingine nyingi kuhusu Kristo, Luka alitaka kutoa mpangilio na mtiririko wa matukio kama mwana historia ambaye alikuwa na habari za kina na mwenye uwezo wa kuandika na kutoa habari za kuaminika alizozipata kwa wale walioona kwa macho yao wenyewe.

Shabaha yake ilikuwa ni kudhihirisha kwamba Yesu alikuwa Mungu na pia mwanadamu aliyeleta mapinduzi katika historia, "*aliyekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea(19:10).*" Kwa sababu hii, Luka alichambua ushahidi wake kwa uangalifu na kutoa tarehe maalum kwa matukio anayoyaandika. Anaanza kwa kuelezea juu ya kuzaliwa kwa Yesu na Bikira Maria, akitoa maelezo ya ndani ambayo hayapo katika Injili nyingine. Huduma ya Yesu inaelezwa, ikifuatiwa na maelezo marefu kuhusu safari ya Yesu kwenda Yerusalemu. Baada ya kifo cha Yesu, kufufuka kutoka kwa wafu na kupaa Kwake mbinguni, wanafunzi wanabaki wakingoja ahadi ya Baba, yaani, kujazwa nguvu ya Roho Mtakatifu kutoka mbinguni.

### *Wazo Kuu*

Luka anaeleza asili na kusudi la Injili hii *(1:3).*Anamdhihirisha Yesu kuwa ni Mungu-Mwanadamu ambaye asili ya ubinadamu anaotajwa nao unaanzia kwa Adamu kwani Yeye anatajwa kama mwana wa Daudi*(3:23-38).* Yesu ndiye mwanadamu aliye kamili kabisa katika historia, naye Luka anamthibitisha kuwa ndiye anayewezesha mambo yote kuwepo kwa kuwa ana Uungu mmoja na Mungu Baba Yake. Yesu ni mkuu kuliko wanadamu wote kwa kuwa Yeye alikuwa Mungu-Mwanadamu, yaani, Mungu aliyefanyika mwili, akafanyika mwanadamu mkamilifu na asiye na damu ya Adamu ya anguko. Mafundisho Yake, matendo Yake, miujiza Yake, hata kifo Chake na kufufuka Kwake kutoka kwa wafu kulidhihirisha Uungu Wake. Kwa sababu hii inatupasa kumwamini na kumpokea ili awe Mwokozi na Bwana wetu.

### *Mwandishi*

Luka tabibu. Luka anatajwa hasa na Paulo katika *Kol. 4:14* na katika *Flm.1:24* wakati Paulo akiwa amefungwa huko Rumi (*ona pia 2Tim.4:11).* Mtazamo wa ushahidi wa kitabibu katika *8:43* unamthibitisha Luka kuwa ndiye yule "tabibu mpenzi" katika *Kol.4: 14.*

### *Tarehe*

Huenda Injili hii iliandikwa kama 60 B.K.

### *Mgawanyo*

- Kuzaliwa kwa Yesu na ujana wake (1:1-2:52)
- Kubatizwa na kujaribiwa kwa Yesu (3:14-4:13)
- Huduma ya Yesu Galilaya (4:14-9:50)
- Safari ya Yesu kwenda Yerusalemu (9:51-19:27)
- Huduma ya Yesu Yerusalemu (19:28-20:47)
- Unabii kuhusu mambo yajayo (21:1-38)
- Kifo cha Yesu na kufufuka kwake (22:1-24:53)

1 Kwa kuwa, watu wengi wamekaa ili
kuandika habari za mambo yaliyotukia katikati
yetu, 2kama vile yalivyokabidhiwa kwetu na wale
ambao walikuwa mashahidi walioona na
watumishi wa Bwana, 3mimi nami baada ya
kuchunguza kila kitu kwa uangalifu kuanzia
mwanzo, niliamua kukuandikia habari za
mambo hayo ewe mtukufu Theofilo, 4ili upate
kujua ule ukweli kuhusu yale uliyofundishwa.

### *Kuzaliwa Kwa Yohana Mbatizaji Kwatabiriwa*

5Wakati wa Herode mfalme wa Uyahudi
palikuwa na kuhani mmoja jina lake Zekaria,
ambaye aliyekuwa wa ukoo wa kikuhani wa
Abiya. Elizabeti mkewe alikuwa pia mzao wa
Aroni. 6Zekaria na Elizabeti mkewe wote
walikuwa watu wanyofu mbele za Mungu,
wakizishika amri zote za Bwana na maagizo
yote bila lawama. 7Lakini walikuwa hawana
watoto, kwa sababu Elizabeti alikuwa tasa, nao
wote wawili walikuwa wazee sana.

8Siku moja Zekaria ilipokuwa zamu ya
kikundi chake, yeye akifanya kazi ya ukuhani
hekaluni mbele za Mungu, 9alichaguliwa kwa
kura kwa kufuata desturi za ukuhani, kuingia
hekaluni mwa Bwana ili kufukiza uvumba. 10Nao
wakati wa kufukiza uvumba ulipowadia, wale
wote waliokuwa wamekusanyika ili kuabudu
walikuwa nje wakiomba.

11Ndipo malaika wa Bwana akamtokea
Zekaria, akiwa amesimama upande wa kuume
wa madhabahu ya kufukizia uvumba. 12Zekaria
alipomwona huyo malaika, akafadhaika sana
akajawa na hofu. 13Lakini malaika
akamwambia, "Usiogope, Zekaria, kwa maana
Mungu amesikia maombi yako. Mkeo Elizabeti
atakuzalia mtoto wa kiume, nawe utamwita jina
lake Yohana. 14Yeye atakuwa furaha na
shangwe kwako, nao watu wengi watashangilia
kwa sababu ya kuzaliwa kwake. 15Kwa kuwa
atakuwa mkuu mbele za Bwana, kamwe
hataonja mvinyo wala kinywaji cho chote cha
kulevya, naye atajazwa Roho Mtakatifu hata
kabla ya kuzaliwa kwake. 16Naye atawavuta
watu wengi warudi kwa Bwana Mungu wao.
17Nao waasi warejee katika hekima ya wenye
haki na kuliweka tayari taifa lililoandaliwa kwa
ajili ya Bwana.

18Zekaria akamwuliza malaika, "Jambo hilo
linawezekanaje? Mimi ni mzee na mke wangu
pia ana umri mkubwa."

19Malaika akamjibu, akamwambia, "Mimi ni
Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu, nami
nimetumwa kwako ili nikuambie habari hizi
njema. 20Basi sasa kwa kuwa hujaamini
maneno yangu ambayo yatatimizwa kwa wakati
wake, utakuwa bubu hadi siku ile mambo haya
yatakapotukia."

21Wakati huo watu walikuwa wanamngojea
Zekaria nje huku wakishangaa kukawia kwake
mle hekaluni. Alipotoka akawa hawezi kusema
nao, wao wakatambua kuwa ameona maono
ndani ya hekalu. Lakini kwa kuwa alikuwa bubu,
aliendelea akawaashiria kwa mikono.

23Muda wake wa kuhudumu hekaluni
ulipomalizika, akarudi nyumbani kwake.
24Baada ya muda si mrefu Elizabeti mkewe
akapata mimba, naye akajitenga kwa miezi
mitano.
25akasema, "Hili ndilo Bwana alilonitendea
aliponiangalia kwa upendeleo na kuniondolea
aibu yangu mbele ya watu."

### *Kuzaliwa Kwa Yesu Kwatabiriwa*

26Mwezi wa sita baada ya Elizabeti kupata
mimba, Mungu alimtuma malaika Gabrieli
aende Galilaya katika mji wa Nazareti, 27 kwa
mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na
mtu mmoja jina lake Yosefu wa nyumba ya
Daudi. Jina la huyu mwanamwali bikira ni Maria.
28Naye malaika akaja kwake akamwambia:
"Salamu, wewe uliyebarikiwa, Bwana yu pamoja
nawe!"

29 Maria akafadhaishwa sana na maneno
haya, akajiuliza moyoni, "Salamu hii ni ya
namna gani?" 30Ndipo malaika akamwambia,
"Usiogope, Maria, umepata upendeleo kwa
Mungu. 31Tazama, utachukua mimba, nawe
utamzaa mtoto mwanamume na utamwita jina
lake Yesu. 32Yeye atakuwa mkuu, naye ataitwa
Mwana wa Aliye Juu. Bwana Mungu atampa kiti
cha enzi cha Daudi baba yake. 33Ataimiliki
nyumba ya Yakobo milele na ufalme Wake
hautakuwa na mwisho."

34Maria akamwuliza huyo malaika,
"Maadam mimi ni bikira, jambo hili
litawezekanaje?"

35Malaika akamjibu, "Roho Mtakatifu
atakujilia juu yako, nazo nguvu Zake Yeye Aliye
Juu zitakufunika kama kivuli, kwa hiyo mtoto
atakayezaliwa atakuwa mtakatifu, naye ataitwa
Mwana wa Mungu. 36Tazama, jamaa yako
Elizabeti amechukua mimba katika uzee wake
na huu ni mwezi wake wa sita, yeye aliyeitwa
tasa. 37Kwa maana kwa Mungu hakuna
lisilowezekana."

38Maria akasema, “Tazama, mimi ni mtumisi
wa Bwana na iwe kwangu kama ulivyosema.”
Kisha malaika akaondoka akamwacha.

### *Mariamu Aenda Kumtembelea Elizabeti*

39Wakati huo Maria akajiandaa
akaharakisha kwenda katika mji mmoja kwenye
vilima ya Uyahudi. 40Akaingia nyumbani kwa
Zekaria na kumsalimu Elizabeti. 41Naye
Elizabeti aliposikia salamu ya Maria, mtoto
aliyekuwa tumboni mwake akaruka. Elizabeti
akajazwa na Roho Mtakatifu, 42akapaza sauti
kwa nguvu akasema, “Umebarikiwa wewe
miongoni mwa wanawake, naye mtoto
utakayemzaa amebarikiwa. 43Lakini ni kwa nini
mimi nimepata upendeleo kiasi hiki, hata mama
wa Bwana wangu afike kwangu? 44Mara tu
niliposikia sauti ya salamu yako, mtoto aliyeko
tumboni mwangu aliruka kwa furaha.
45Amebarikiwa yeye aliye amini kwamba lile
Bwana alilomwambia litatimizwa.”

### *Wimbo Wa Maria Wa Sifa*

46Naye Maria akasema:

“Moyo wangu wamwadhimisha Bwana,
47nayo roho yangu inamfurahia Mungu Mwokozi
wangu,
48kwa kuwa ameangalia kwa fadhili unyonge
wa mtumishi wake,
hakika tangu sasa vizazi vyote
vitaniita mbarikiwa,
49kwa maana, Yeye Mwenye Nguvu,
amenitendea mambo ya ajabu,
Mtakatifu ndilo Jjina Lake.
50Rehema Zake huwaendea wale
wamchao, kutoka kizazi hadi kizazi.
51Kwa kuwa ametenda mambo ya ajabu
kwa mkono Wake,
amewatawanya wale wenye kiburi ndani ya
mioyo yao.
52Amewashusha watawala toka kwenye
viti vyao vya enzi,
lakini amewainua wanyenyekevu.
53Amewashibisha wenye njaa kwa vitu vizuri
na matajiri amewafukuza mikono mitupu.
54Amemsaidia mtumishi Wake Israeli,
amekumbuka ahadi Yake ya kumrehemu
55kama alivyowaahidi baba zetu
Abrahamu na uzao wake milele.”

56Maria akakaa na Elizabeti karibu miezi
mitatu, kisha akarudi nyumbani kwake.

### *Kuzaliwa Kwa Yohana Mbatizaji*

57Ulipowadia wakati wa Elizabeti kujifungua,
alizaa mtoto mwanaume. 58Majirani zake na jamii
zake wakasikia jinsi Bwana alivyomfanyia rehema
kuu, nao wakafurahi pamoja naye.
59Siku ya nane wakaja kumtahiri motto,
wakataka kumpa yule mtoto jina la Zekaria baba
yake. 60Lakini mama yake akakataa na kusema,
“Hapana! Jina lake ataitwa Yohana.”
61Wakamwambia, “Hakuna mtu ye yote
katika jamaa yako mwenye jina kama hilo.”
62Basi wakamfanyia Zekaria baba yake
ishara ili kujua kwamba yeye angependa kumpa
mtoto jina gani. 63Akaomba wampe kibao cha
kuandikia na kwa mshangao wa kila mtu
akaandika: “Jina lake ni Yohana.” 64Papo hapo
kinywa chake kikafunguliwa na ulimi wake
ukaachiwa, akawa anaongea akimsifu Mungu.
65Majirani wote wakajawa na hofu ya Mungu na
katika nchi yote ya vilima ya Uyahudi watu
walikuwa wakinena juu ya mambo haya yote.
66Kila aliyesikia habari hizi alishangaa akauliza,
“Je, mtoto huyu atakuwa mtu wa namna gani?”
Maana mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye.

### *Unabii Wa Zekaria*

67Zekaria, baba yake, akajazwa na Roho
Mtakatifu, naye akatoa unabii akisema:

68“Ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli,
kwa kuwa amewajilia Watu wake na
kuwakomboa.
69Naye ametusimamishia pembe[a] ya wokovu
katika nyumba ya Daudi mtumishi Wake,
70kama alivyonena kwa vinywa vya
manabii wake watakatifu
tangu zamani,
71kwamba atatuokoa kutoka kwa adui
zetu na kutoka mikononi mwao wote
watuchukiao,
72ili kuonyesha rehema kwa baba zetu
na kukumbuka agano lake takatifu,
73kiapo alichomwapia baba yetu Abrahamu:
74kutuokoa kutoka mkononi mwa adui zetu,
tupate kumtumikia Yeye pasipo hofu
75katika utakatifu na haki mbele
Zake, siku zetu zote.

76Nawe mtoto wangu, utaitwa nabii wa Aliye

---

[a] 69 “Pembe” hapa ina maanisha “nguvu.”

Juu,
kwa kuwa utamtangulia Bwana na kuandaa
njia kwa ajili Yake,
77kuwajulisha watu Wake juu ya wokovu
utakaopatikana kwa kusamehewa dhambi
zao,
78kwa ajili ya wingi wa rehema za Mungu
wetu, nuru itokayo juu itatuzukia
79ili kuwaangazia wale waishio gizani
na katika uvuli wa mauti,
kuiongoza miguu yetu katika njia ya amani."

80Yule mtoto akakua na kuongezeka nguvu
katika roho, akaishi nyikani hadi siku ile
alipojionyesha hadharani kwa Waisraeli.

### *Kuzaliwa Kwa Yesu*

**2** Siku zile Kaisari Augusto alitoa amri kwamba
watu wote waandikishwe katika ulimwengu wa
Kirumi. 2(Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyofanyika
wakati Krenio alipokuwa mtawala wa Shamu[a]).
3Kila mtu alikwenda
kuandikishwa katika mji wake alikozaliwa.
4Hivyo Yosefu akapanda kutoka mji wa
Nazareti ulioko Galilaya kwenda Uyahudi,
mpaka Bethlehemu mji wa Daudi, kwa sababu
yeye alikuwa wa ukoo na wa nyumba ya Daudi.
5Alikwenda huko kujiandikisha pamoja na Maria,
ambaye alikuwa amemposa naye alikuwa mja
mzito. 6Wakiwa Bethlehemu, wakati wa Maria
wa kujifungua ukawa umetimia, 7naye akamzaa
mwanawe, kifungua mimba. Akamfunika nguo
za kitoto na kumlaza katika hori ya kulia
ng'ombe, kwa sababu hapakuwa na nafasi
katika nyumba ya wageni.

### *Wachungaji Na Malaika*

8Katika eneo lile walikuwako wachungaji
waliokuwa wakikaa mashambani, wakilinda
makundi yao ya kondoo usiku. 9Ghafula tazama,
malaika wa Bwana akawatokea, nao utukufu wa
Bwana ukawang'aria kotekote, wakaingiwa na
hofu. 10Lakini malaika akawaambia: "Msiogope.
Kwa maana tazama nawaletea habari njema za
furaha itakayokuwa kwa watu wote. 11Leo katika
mji wa Daudi kwa ajili yenu amezaliwa Mwokozi,
ndiye Kristo Bwana. 12Hii ndiyo itakayokuwa
ishara kwenu: Mtamkuta mtoto mchanga
amefunikwa nguo za kitoto na kulazwa katika
hori ya kulia ng'ombe."

13Ghafula pakawa na jeshi kubwa la
mbinguni pamoja na huyo malaika wakimsifu
Mungu wakisema,

14"Atukuzwe Mungu juu mbinguni na
duniani iwe amani kwa watu
aliowaridhia."

15Hao malaika walipokwisha kuondoka na
kwenda zao mbinguni, wale wachungaji
wakasemezana wao kwa wao wakisema,
"Twendeni Bethlehemu tukaone mambo haya
ya ajabu yaliyotukia, ambayo Bwana
ametuambia habari zake."
16Hivyo wakaenda haraka Bethlehemu,
wakawakuta Maria na Yosefu na yule mtoto
mchanga akiwa amelala katika hori la kulia
ng'ombe. 17Walipomwona yule mtoto,
wakawaeleza yale waliyokuwa wameambiwa
kuhusu huyu mtoto. 18Nao wote waliosikia
habari hizi wakastaajabia yale waliyoambiwa na
wale wachungaji wa kondoo. 19Lakini Maria
akayaweka mambo haya yote moyoni mwake
na kuyatafakari. 20Wale wachungaji wakarudi,
huku wakimtukuza Mungu na kumsifu kwa ajili
ya mambo yote waliyokuwa wameambiwa na
kuyaona.
21Hata zilipotimia siku nane, ulikuwa ndio
wakati wa kumtahiri mtoto, akaitwa Yesu, jina
alilokuwa amepewa na malaika kabla
hajatungwa mimba.

### *Yesu Apelekwa Hekaluni*

22Ulipotimia wakati wa utakaso wake Maria,
kwa mujibu wa Sheria ya Mose, Yosefu na
Maria walimpeleka mtoto Yerusalemu, ili
kumweka wakfu kwa Bwana 23(kama
ilivyoandikwa katika Sheria ya Bwana kwamba,
"Kila mtoto wa kiume kifungua mimba atawekwa
wakfu kwa Bwana"), 24pia kutoa dhabihu
kulingana na yale yaliyonenwa, katika Sheria ya
Bwana: "Hua wawili au makinda mawili ya
njiwa."
25Basi alikuwako huko Yerusalemu mtu
mmoja jina lake Simeoni, ambaye alikuwa
mwenye haki na mcha Mungu, akitarajia faraja
ya Israeli na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake.
26Roho Mtakatifu alikuwa amemfunulia kuwa
hatakufa kabla hajamwona Kristo[b] wa Bwana.
27Simeoni akiwa ameongozwa na Roho

[a]2Shamu hapa ina maanisha Syria

[b]26 "Kristo ni neno la Kiyunani, yaani, Masiya maana yake Mpakwa (Aliyetiwa) Mafuta.

Mtakatifu, alikwenda hekaluni. Wazazi
walipomleta mtoto Yesu ili kumfanyia kama
ilivyokuwa desturi ya Sheria, 28ndipo Simeoni
akampokea mtoto mikononi mwake
na kumsifu Mungu, akisema:

29"Bwana Mungu Mwenyezi, kama ulivyoahidi,
sasa wamruhusu mtumishi wako
aende zake kwa amani.
30Kwa maana macho yangu yameuona
wokovu Wako,
31ulioweka tayari machoni pa watu wote,
32nuru kwa ajili ya ufunuo kwa watu Mataifa
na kwa ajilin ya utukufu kwa watu wako
Israeli."

33Naye Yosefu na mama yake mtoto
wakastaajabu kwa yale yaliyokuwa yamesemwa
kumhusu huyo mtoto. 34Kisha Simeoni
akawabariki, akamwambia Maria mama yake,
"Mtoto huyu amewekwa kwa makusudi ya
kuanguka na kuinuka kwa wengi katika Israeli.
Atakuwa ishara ambayo watu watanena dhidi
yake, 35 ili mawazo ya mioyo mingi yadhihirike
na upanga utauchoma moyo wako.

36Tena alikuwako hekaluni nabii mmoja
mwanamke mzee sana, jina lake Ana binti
Fanueli, wa kabila la Asheri. Alikuwa mzee
sana, naye alikuwa ameolewa na kuishi na
mume kwa miaka saba tu, kisha mumewe
akafa. 37Hivyo alikuwa mjane na umri wake
ulikuwa miaka thamanini na minne. Yeye
hakuondoka humo hekaluni usiku wala mchana
bali alikuwa akimwabudu Mungu, akifunga na
kuomba. 38Wakati uo huo, Ana alikuja akaanza
kusifu akimshukuru Mungu na kusema habari za
huyo mtoto kwa watu wote waliokuwa
wakitarajia ukombozi wa Yerusalemu.

39Yosefu na Maria walipokuwa
wamekamilisha mambo yote yaliyotakiwa na
Sheria ya Bwana, walirudi mjini kwao Nazareti
huko Galilaya. 40Naye mtoto Yesu akakua na
kuongezeka nguvu akiwa amejaa hekima na
neema ya Mungu ilikuwa juu Yake.

### *Kijana Yesu Hekaluni*

41Kila mwaka Yosefu na Maria mama yake
Yesu walikuwa na desturi ya kwenda
Yerusalemu kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka.
42Yesu alipokuwa na umri wa miaka kumi na
miwili, walipanda kwenda kwenye Sikukuu hiyo
kama ilivyokuwa desturi. 43Baada ya Sikukuu
kumalizika, wakati Yosefu na Maria mama Yake
walipokuwa wakirudi nyumbani, Yesu alibaki
Yerusalemu lakini hawakutambua. 44Wao
wakidhani kuwa yuko miongoni mwa wasafiri,
walienda mwendo wa kutwa nzima. Ndipo
wakaanza kumtafuta miongoni mwa jamaa zao na
marafiki. 45Walipomkosa walirudi Yerusalemu ili
kumtafuta. 46Baada ya siku tatu wakamkuta ndani
ya hekalu, akiwa ameketi katikati ya walimu wa
Sheria, akiwasikiliza na kuwauliza maswali.
47Wote waliomsikia walistaajabishwa na uwezo
Wake mkubwa wa kuelewa na majibu aliyoyatoa.
48Yosefu na Maria mama yake walipomwona
walishangaa. Mama Yake akamwuliza,
"Mwanangu, mbona umetufanyia hivi? Tazama,
mimi na baba yako tumekuwa tukikutafuta kwa
wasiwasi mkubwa kila mahali.''

49Yesu akawaambia, "Kwa nini kunitafuta?
Hamkujua kwamba imenipasa kuwa katika
nyumba ya Baba Yangu?"
50Lakini wao hawakuelewa maana ya lile
alilowaambia.

51Ndipo akashuka pamoja nao hadi
Nazareti, naye alikuwa mtii kwao. Lakini Mama
Yake akayaweka moyoni mwake mambo haya
yote. 52Naye Yesu akakua katika hekima na
kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.

### *Yohana Mbatizaji Aanza Kuhubiri*

**3** Katika mwaka wa kumi na tano wa
utawala wa Kaisari Tiberio, Pontio Pilato alikuwa
mtawala wa Uyahudi. Herode alikuwa mfalme wa
Galilaya na Filipo ndugu yake alikuwa mfalme
wa Iturea na nchi ya Trakoniti. Naye Lisania
alikuwa mfalme wa Abilene. 2Anasi na Kayafa
walikuwa makuhani wakuu. Wakati huo ndipo
neno la Mungu likamjia Yohana, mwana wa
Zekaria huko nyikani. 3Akaenda katika nchi yote
kandokando ya Mto Yordani, akihubiri ubatizo wa
toba kwa ajili ya msamaha wa dhambi. 4Kama
ilivyoandikwa katika kitabu
cha nabii Isaya:

"Sauti ya mtu aliyae nyikani,
'Itengenezeni njia ya Bwana,
yanyosheni mapito Yake,
5kila bonde litajazwa,
kila mlima na kilima kitasawazishwa.
Njia zilizopinda zitanyooshwa,
zilizoparuza zitasawazishwa
6na watu wote watauona Wokovu wa
Mungu.' "

7Yohana akauambia ule umati wa watu

uliokuwa unakuja ili kubatizwa naye, “Enyi uzao
wa nyoka! Ni nani aliyewaonya mwikimbie
ghadhabu ijayo? [8]Zaeni matunda yafananayo
na toba yenu. Wala msianze kusema mioyoni
mwenu kuwa ninyi ni uzao wa Abrahamu. Kwa
maana nawaambia, Mungu anaweza
kumwinulia Abrahamu watoto kutoka katika
mawe haya. [9]Hata sasa shoka limekwisha
wekwa tayari kwenye shina la kila mti, basi kila
mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na
kutupwa motoni.”

[10]Ule umati wa watu ukamwuliza,
“Inatupasa tufanyeje basi?”

[11]Yohana akawaambia, “Aliye na kanzu
mbili amgawie asiye nayo, naye aliye na
chakula na afanye vivyo hivyo.”

[12]Watoza ushuru nao wakaja ili wabatizwe,
wakamwuliza, “Bwana na sisi inatupasa
tufanyeje?”

[13]Akawaambia, “Msichukue zaidi ya
kiwango mlichopangiwa.”

[14]Askari nao wakamwuliza, “Je, nasi
inatupasa tufanye nini?”

Akawaambia, “Msimdhulumu mtu wala
msimshtaki mtu kwa uongo, bali mridhike na
mishahara yenu.”

[15]Watu walikuwa na matazamio makubwa.
Wakawa wanajiuliza mioyoni mwao iwapo
Yohana angeweza kuwa ndiye Kristo. [16]Yohana
akawajibu akawaambia, ‘‘Mimi nawabatiza kwa
maji[a] Lakini atakuja aliye na nguvu kuliko mimi
ambaye sistahili hata kufungua kamba ya viatu
vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na
kwa moto. [17]Pepeto lake liko mkononi, tayari
kusafisha sakafu yake ya kupuria na kuikusanya
ngano ghalani, lakini makapi atayateketeza kwa
moto usiozimika.” [18]Basi, kwa maonyo mengine
mengi Yohana aliwahubiri watu Habari Njema.

[19]Lakini Yohana alipomkemea Mfalme
Herode kuhusu uhusiano wake na Herodia mke
wa ndugu yake na maovu mengine aliyokuwa
amefanya, [20]Herode akijumlisha haya yote,
akamfunga Yohana gerezani.

### *Kubatizwa Kwa Bwana Yesu*

[21]Baada ya watu wote kubatizwa, Yesu
naye akabatizwa. Naye alipokuwa akiomba,
mbingu zilifunguka. [22]Roho Mtakatifu akashuka
juu Yake kwa umbo kama la hua na sauti ikaja
kutoka mbinguni ikisema: “Wewe ni Mwanangu
mpendwa wangu, ninayependezwa nawe sana.”

### *Ukoo Wa Bwana Yesu*

[23]Yesu alikuwa na umri wa miaka thelathini
alipoanza huduma Yake. Alikuwa akidhaniwa
kuwa mwana wa Yosefu,

Yosefu alikuwa mwana wa Eli, [24]Eli
alikuwa mwana wa Mathati,
Mathati alikuwa mwana wa Lawi,
Lawi alikuwa mwana Melki, Melki
alikuwa mwana wa Yanai,
Yanai alikuwa mwana wa Yosefu,
[25]Yosefu alikuwa mwana wa Matathia,
Matathia alikuwa mwana wa Amosi,
Amosi alikuwa mwana wa Nahumu,
Nahumu alikuwa mwana wa Esli, Esli
alikuwa mwana wa Nagai, [26]Nagai
alikuwa mwana wa Maathi, Maathi
alikuwa mwana wa Matathia,
Matathia alikuwa mwana Semeini,
Semeini alikuwa mwana wa Yoseki,
Yoseki alikuwa mwana wa Yoda,
[27]Yoda alikuwa mwana wa Yoanani,
Yoanani alikuwa mwana wa Resa, Resa
alikuwa mwana wa Zerubabeli,
Zerubabeli alikuwa mwana wa
Shealtieli, Shealtieli alikuwa mwana wa
Neri, [28]Neri alikuwa mwana wa Melki,
Melki alikuwa mwana wa Adi, Adi
alikuwa mwana wa Kosamu,
Kosamu alikuwa mwana wa Elmadamu,
Elmadamu alikuwa mwana wa Eri,
[29]Eri alikuwa mwana wa Yoshua, Yoshua
alikuwa mwana wa Eliezeri, Eliezeri
alikuwa mwana wa Yorimu, Yorimu
alikuwa mwana wa Mathati, Mathati
alikuwa mwana wa Lawi, [30]Lawi
alikuwa mwana wa Simeoni, Simeoni
alikuwa mwana wa Yuda, Yuda
alikuwa mwana wa Yosefu, Yosefu
alikuwa mwana wa Yonamu,
Yonamu alikuwa mwana wa Eliakimu,
Eliakimu alikuwa mwana wa Melea,
[31]Melea alikuwa mwana ma Mena, Mena
alikuwa mwana wa Matatha, Matatha
alikuwa mwana wa Nathani, Nathani
alikuwa mwana wa Daudi, [32]Daudi
alikuwa mwana wa Yese, Yese
alikuwa mwana wa Obedi, Obedi
alikuwa mwana wa Boazi, Boazi
alikuwa mwana wa Salmoni,
Salmoni alikuwa mwana wa Nashoni,
[33]Nashoni alikuwa mwana wa Aminadabu,
Aminadabu alikuwa mwana wa Aramu,

a[16] “Kwa maji” hapa tafsiri nyingine zinasema “ndani ya maji”

Aramu alikuwa mwana wa Hesroni,
Hesroni alikuwa mwana wa Peresi,
Peresi alikuwa mwana wa Yuda,
34Yuda alikuwa mwana wa Yakobo,
Yakobo alikuwa mwana wa Isaki,
Isaki alikuwa mwana wa Abrahamu,
Abrahamu alikuwa mwana wa Tera,
Tera alikuwa mwana wa Nahori,
35Nahori alikuwa mwana wa Serugi,
Serugi alikuwa mwana wa Reu,
Reu alikuwa mwana wa Pelegi,
Pelegi alikuwa mwana wa Eberi,
Eberi alikuwa mwana wa Sala,
36Sala alikuwa mwana wa Kenani,
Kenani alikuwa mwana wa Arfaksadi,
Arfaksadi alikuwa mwana wa Shemu,
Shemu alikuwa mwana wa Noa, Noa
alikuwa mwana wa Lameki,
37Lameki alikuwa mwana wa Methusela,
Methusela alikuwa mwana wa Enoki,
Enoki alikuwa mwana wa Yaredi,
Yaredi alikuwa mwana wa Mahalaleli,
Mahalaleli alikuwa mwana wa Kenani,
38Kenani alikuwa mwana wa Enoshi,
Enoshi alikuwa mwana wa Sethi,
Sethi alikuwa mwana wa Adamu,
Adamu alikuwa mwana wa Mungu.

### *Yesu Ajaribiwa Na Shetani*

**4** Yesu, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, akarudi
kutoka Yordani akaongozwa na Roho Mtakatifu hadi
jangwani, 2mahali ambako kwa siku arobaini alikuwa
akijaribiwa na Ibilisi. Kwa siku zote hizo hakula cho
chote, hivyo
baada ya muda huo akaona njaa.

3Ibilisi akamwambia, "Ikiwa Wewe ni Mwana
wa Mungu, amuru jiwe hili liwe mkate."

4Yesu akajibu akamwambia, "Imeandikwa:
'Mtu haishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno la
Mungu.' "

5Ibilisi akampeleka hadi juu ya mlima mrefu
akamwonyesha milki zote za dunia kwa mara
moja. 6Akamwambia, "Nitakupa mamlaka juu ya
milki hizi na fahari zake zote, kwa maana
zimekabidhiwa mikononi mwangu nami
ninaweza kumpa ye yote ninayetaka. 7Hivyo
ikiwa utanisujudia na kuniabudu, vyote vitakuwa
vyako."

8Yesu akamjibu, "Imeandikwa: 'Mwabudu
Bwana Mungu wako na umtumikie Yeye peke
yake.' "

9Kisha Ibilisi akampeleka mpaka
Yerusalemu, akamweka juu ya mnara mrefu
mwembamba wa hekalu, akamwambia, "Kama
Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini
kutoka hapa, 10kwa maana imeandikwa:

" 'Atakuagizia malaika zake wakulinde,
11nao watakuchukua mikononi mwao
usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.' "

12Yesu akamjibu, "Imesemwa, 'Usimjaribu
Bwana Mungu wako.' "

13Ibilisi alipomaliza kila jaribu, akamwacha
Yesu mpaka wakati mwingine ufaao.

### *Mwanzo Wa Huduma Ya Galilaya*

14Kisha Yesu akarudi mpaka Galilaya, akiwa
amejaa nguvu za Roho Mtakatifu, nazo habari
Zake zikaenea katika sehemu zote za nchi za
kandokando. 15Akaanza kufundisha kwenye
masinagogi yao na kila mmoja akamsifu.

### *Kukataliwa Kwa Yesu*

16Yesu akaenda Nazareti, hapo alipolelewa
na siku ya Sabato alikwenda katika sinagogi
kama ilivyokuwa desturi Yake. Akasimama ili
asome, 17naye akapewa kitabu cha nabii Isaya,
akakifungua na kukuta mahali palipoandikwa:

18"Roho wa Bwana yu juu Yangu,
kwa sababu amenitia mafuta
kuwaletea maskini habari njema.
Amenituma kuwatangazia wafungwa
kufunguliwa kwao na
vipofu kupata kuona tena,
kuwaweka huru wanaoonewa
19na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubalika."

20Kisha akakifunga kitabu, akamrudishia
mtumishi na akaketi. Watu wote waliokuwamo
katika sinagogi wakamkazia macho. 21Ndipo
akaanza kwa kuwaambia, "Leo maandiko haya
yametimia mkiwa mnasikia."

22Wote waliokuwako wakamsifu na
kuyastaajabia maneno Yake yaliyojaa neema,
wakaulizana, "Je, huyu si mwana wa Yosefu?"

23Yesu akawaambia, "Bila shaka mtatumia
mithali hii, 'Tabibu, jiponye mwenyewe! Nanyi
mtasema, 'Mambo yale tuliyosikia kwamba
uliyafanya huko Kapernaumu, yafanye na hapa
kwenye mji Wako.' "

24Yesu akasema, Amin, nawaambia,
hakuna nabii anayekubalika kwenye mji wake
mwenyewe. 25Lakini ukweli ni kwamba palikuwa
na wajane wengi katika Israeli wakati wa Eliya,

mbingu zilipofungwa kwa miaka mitatu na miezi sita pakawa na njaa kuu katika nchi nzima. 26Lakini Eliya hakutumwa hata kwa mmoja wao, bali kwa mjane mmoja wa Sarepta katika nchi ya Sidoni. 27Pia palikuwa na wengi wenye ukoma katika Israeli katika siku za nabii Elisha, lakini hakuna hata mmoja wao aliyetakaswa, isipokuwa Naamani mtu wa Shamu[a].”

28Watu wote katika sinagogi waliposikia maneno haya, wakakasirika sana. 29Wakasimama, wakamtoa nje ya mji, wakamchukua hadi kwenye kilele cha mlima mahali ambapo mji huo ulikuwa umejengwa, ili wamtupe chini kutoka kwenye mtelemko mkali. 30Lakini Yeye akapita papo hapo katikati ya huo umati wa watu akaenda Zake.

### *Yesu Atoa Pepo Mchafu*

31Kisha akashuka kwenda Kapernaumu, mji wa Galilaya na katika za siku za Sabato akawa anafundisha. 32Wakashangazwa sana na mafundisho Yake, maana maneno Yake yalikuwa na mamlaka.

33Ndani ya sinagogi palikuwa na mtu aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu, akapiga kelele kwa nguvu akisema, 34 “Tuache! Tuna nini nawe Yesu wa Nazareti? Je, umekuja kutuangamiza? Ninakujua Wewe ni nani. Wewe ni Mtakatifu wa Mungu.”

35Basi Yesu akamkemea yule pepo mchafu, akisema, “Nyamaza na umtoke!’’ Yule pepo mchafu akamwangusha chini yule mtu mbele yao wote, akatoka pasipo kumdhuru. 36Watu wote wakashangaa wakaambiana, ‘‘Mafundisho haya ni ya namna gani? Kwa mamlaka na nguvu, anawaamuru pepo wachafu, nao wanatoka!” 37 Habari Zake zikaanza kuenea kila mahali katika sehemu ile.

### *Yesu Awaponya Wengi*

38Yesu akatoka kwenye sinagogi akaenda nyumbani kwa Simoni. Basi huko alimkuta mkwewe Simoni ana homa kali, nao wakamwomba Yesu amsaidie. 39Hivyo Yesu akamwinamia na kukemea ile homa, nayo ikamwacha. Akaamka saa ile ile akaanza kuwahudumia.

40Jua lilipokuwa linatua, watu wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbalimbali wakawaleta kwa Yesu, naye akaweka mikono Yake juu ya kila mgonjwa, akawaponya. 41Pepo wachafu pia wakawatoka watu wengi, nao walipokuwa wakitoka wakapiga kelele wakisema: “Wewe ni Mwana wa Mungu!” Lakini Yesu akawakemea na kuwazuia wasiseme, kwa maana walimjua kuwa Yeye ni Kristo.

42Kesho yake, kulipopambazuka, Yesu alikwenda mahali pa faragha. Watu wengi wakawa wanamtafuta kila mahali, nao walipomwona wakajaribu kumzuia asiondoke. 43Lakini Yeye akawaambia, “Imenipasa kuhubiri Habari Njema za Ufalme wa Mungu katika miji mingine pia, kwa maana kwa kusudi hili nilitumwa.” 44Naye aliendelea kuhubiri katika masinagogi ya Uyahudi.

### *Kuitwa Kwa Wanafunzi Wa Kwanza*

**5** Siku moja Yesu alipokuwa amesimama karibu na Ziwa la Genesareti, watu wengi wakiwa wanasongana kumzunguka ili wapate kusikia neno la Mungu, 2akaona mashua mbili ukiongoni mwa ziwa, zikiwa zimeachwa hapo na wavuvi waliokuwa wanaosha nyavu zao. 3Akaingia katika mojawapo ya hizo mashua ambayo ilikuwa ya Simoni, akamwomba aisogeze ndani ya maji kidogo kutoka pwani. Kisha akaketi na kufundisha watu akiwa mle ndani ya mashua.

4Alipomaliza kunena, akamwambia Simoni, “Sasa peleka mashua hadi kilindini kisha mshushe nyavu zenu mkavue samaki.”

5Simoni akamjibu, “Bwana, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha na hatukuvua cho chote. Lakini, kwa neno lako nitazishusha nyavu.”

6Nao walipozishusha nyavu zao, wakavua samaki wengi sana, nyavu zao zikajaa zikaanza kukatika. 7Wakawaashiria wavuvi wenzao kwenye ile mashua nyingine ili waje kuwasaidia. Wakaja, wakajaza mashua zote mbili samaki hata zikaanza kuzama.

8Simoni Petro alipoona haya yaliyotukia alianguka miguuni mwa Yesu na kumwambia, “Bwana, ondoka kwangu, mimi ni mtu mwenye dhambi!” 9Kwa kuwa yeye na wavuvi wenzake walikuwa wameshangazwa sana na wingi wa samaki waliokuwa wamepata, 10vivyo hivyo wenzake Simoni, yaani, Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo walishangazwa pia.

Ndipo Yesu akamwambia Simoni, “Usiogope, tangu sasa utakuwa mvuvi wa watu.” 11Hivyo wakasogeza mashua zao mpaka ufuoni mwa bahari, wakaacha kila kitu na kumfuata Yesu.

---

a 27 Shamu hapa inamaanisha Syria

### *Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*

12Ikawa siku moja Yesu alipokuwa katika mji frulani, mtu mmoja mwenye ukoma mwili mzima akamjia. Alipomwona Yesu, alianguka chini mpaka uso wake ukagusa ardhi na kumsihi akisema, “Bwana, ukitaka waweza kunitakasa.”

13Yesu akanyosha mkono Wake akamgusa yule mtu, akamwambia, “Nataka, takasika!” Naye mara ukoma ukapona.

14Yesu akamwagiza akisema, “Usimwambie mtu ye yote, bali nenda ukajionyeshe kwa kuhani na ukatoe dhabihu alizoagiza Mose ili kuwa ushuhuda kwao.”

15Lakini habari zake Yesu zikazidi sana kuenea kotekote kuliko wakati mwingine wo wote, makutano makubwa ya watu yalikuwa yakikusanyika ili kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao. 16Lakini mara kwa mara Yesu alijitenga nao ili kwenda mahali pa faragha kuomba.

### *Yesu Amponya Mwenye Kupooza*

17Siku moja Yesu alipokuwa akifundisha, Mafarisayo na walimu wa sheria, waliokuwa wametoka kila kijiji cha Galilaya na kutoka Uyahudi na Yerusalemu, walikuwa wameketi huko. Nao uweza wa Bwana ulikuwa juu Yake kuponya wagonjwa. 18Wakaja watu wamembeba mgonjwa aliyepooza kwenye mkeka. Wakajaribu kumwingiza ndani ili wamweke mbele ya Yesu. 19Walipokuwa hawawezi kufanya hivyo kwa sababu ya umati wa watu, wakapanda juu ya paa, wakaondoa baadhi ya vigae, wakapata nafasi ya kumtelemsha yule mgonjwa kwa mkeka wake katikati ya ule umati pale pale mbele ya Yesu.

20Yesu alipoiona imani yao, akamwambia yule mgonjwa, “Rafiki, dhambi zako zimesamehewa.”

21Mafarisayo na wale walimu wa sheria wakaanza kuuliza, “Ni nani mtu huyu anayesema maneno ya makufuru? Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke Yake?”

22Yesu akijua mawazo yao akawauliza, “Kwa nini mnawaza haya mioyoni mwenu? 23Je, ni lipi lililo rahisi zaidi, kumwambia huyu, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema, ‘Simama uende?’ 24Lakini ili mpate kujua ya kuwa Mwana wa Adamu anayo mamlaka duniani ya kusamehe dhambi,” Akamwambia yule aliyepooza, “Nakuambia, Simama, chukua mkeka wako uende nyumbani kwako.” 25Mara yule mtu aliyekuwa amepooza akasimama mbele yao wote, akachukua mkeka wake akaenda zake nyumbani, huku akimtukuza Mungu. 26Kila mmoja akashangaa na kumtukuza Mungu. Wakajawa na hofu ya Mungu, wakasema, “Leo tumeona mambo ya ajabu.”

### *Yesu Amwita Lawi*

27Baada ya haya Yesu alitoka na kumwona mtoza ushuru mmoja jina lake Lawi akiwa amekaa forodhani, mahali pake pa kukusanyia kodi, akamwambia, “Nifuate.” 28Naye Lawi akaacha kila kitu, akaondoka, akamfuata.

29Kisha Lawi akamfanyia Yesu karamu kubwa nyumbani kwake, nao umati mkubwa wa watoza ushuru na watu wengine walikuwa wakila pamoja nao. 30Lakini Mafarisayo na walimu wa sheria ambao walikuwa wa madhehebu yao wakawalalamikia wanafunzi wa Yesu, wakisema, “Mbona mnakula na kunywa pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?”

31Yesu akawajibu, “Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa. 32Sikuja kuwaita wenye haki bali wenye dhambi wapate kutubu.”

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*

33Wakamwambia Yesu, “Wanafunzi wa Yohana na wa Mafarisayo mara kwa mara hufunga na kuomba, lakini wanafunzi Wako wanaendelea kula na kunywa.”

34Yesu akawajibu, “Je, mnaweza kuwafanya wageni wa bwana arusi kufunga wakati akiwa pamoja nao? 35Lakini wakati utafika ambapo bwana arusi ataondolewa kwao, ndipo watakapofunga.”

36Yesu akawapa mfano huu, akawaambia: “Hakuna mtu achanaye kiraka kutoka kwenye nguo mpya na kukishonea kwenye nguo kuukuu. Akifanya hivyo atakuwa amechana nguo mpya na kile kiraka hakitaendana na ile nguo kuukuu. 37Hakuna mtu awekaye divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Akifanya hivyo, hiyo divai mpya itapasua hivyo viriba nayo yote itamwagika. 38Divai mpya lazima iwekwe kwenye viriba vipya. 39Wala hakuna mtu anayependelea divai mpya baada ya kunywa divai ya zamani, husema, ‘Ile ya zamani ni nzuri zaidi.’ ”

### *Bwana Wa Sabato*

**6** Ikawa siku moja ya Sababo Yesu alikuwa
akipita katika mashamba ya nafaka, wanafunzi
Wake wakawa wakivunja masuke ya nafaka,
wakayafikicha kwa mikono yao na kula punje zake.
2Baadhi ya Mafarisayo wakawauliza, "Mbona
mnafanya mambo
ambayo ni kinyume na sheria siku ya Sabato?"
3Yesu akawajibu, "Je, ninyi hamkusoma
jinsi alivyofanya Daudi wakati yeye na wenzake
walipokuwa na njaa? 4Aliingia ndani ya nyumba
ya Mungu, akaichukua ile mikate ya Wonyesho
ambayo huliwa na makuhani peke yao. Naye pia
akawapa wenzake wakala!" 5Yesu akawaambia,
"Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato."

6Ikawa siku nyingine ya Sabato Yesu
aliingia ndani ya sinagogi akawa anafundisha,
huko palikuwa na mtu ambaye mkono wake wa
kuume ulikuwa umepooza. 7Mafarisayo na
walimu wa sheria walikuwa wakitafuta sababu
ya kumshtaki Yesu, hivyo wakawa
wanamwangalia kwa karibu ili waone kama
ataponya katika siku ya Sabato. 8Lakini Yesu
alijua mawazo yao, hivyo akamwambia yule
mwenye mkono uliopooza, "Ondoka." Hivyo yule
mtu akaondoka, akasimama mbele yao wote.
9Ndipo Yesu akawaambia wale walimu wa
sheria na Mafarisayo, akisema, "Nawauliza
ninyi, ni lipi lililo halali siku ya Sabato, kutenda
mema au kutenda mabaya? Kuokoa maisha au
kuyaangamiza?"
10 Akawatazama watu wote waliokuwepo,
kisha akamwambia yule aliyepooza mkono,
"Nyosha mkono wako!" Akaunyosha na mkono
wake ukawa tena mzima kabisa. 11Wale wakuu
wakakasirika sana, wakashauriana wao kwa
wao, ni nini watakachomtendea Yesu.

### *Yesu Achagua Mitume Kumi Na Wawili*

12Ikawa katika siku hizo Yesu alikwenda
mlimani kuomba, akakesha usiku kucha
akimwomba Mungu. 13Kulipopambazuka
akawaita wanafunzi Wake, naye akachagua
kumi na wawili, ambao pia aliwaita mitume:
14Simoni aliyemwita Petro, Andrea nduguye,
Yakobo, Yohana, Filipo, Bartholomayo,
15Mathayo, Thomasi. Yakobo mwana wa Alfayo,
Simoni aliyeitwa Zelote, 16Yuda mwana wa
Yakobo na Yuda Iskariote, ambaye ndiye
aliyemsaliti Yesu.

### *Yesu Aponya Wengi*

17Akashuka pamoja nao akasimama mahali
penye uwanja tambarare. Hapo palikuwa na
idadi kubwa ya wanafunzi Wake na umati
mkubwa wa watu kutoka sehemu zote za
Uyahudi, Yerusalemu na kutoka pwani ya Tiro
na Sidoni, 18waliokuwa wamekuja kumsikiliza
na kuponywa magonjwa yao. Wale waliokuwa
wakiteswa na pepo wachafu akawaponya.
19Watu wote walikuwa wanajitahidi kumgusa
kwa sababu nguvu zilikuwa zikimtoka na
kuwaponya wote.

20Akawatazama wanafunzi wake akasema:

"Mmebarikiwa ninyi mlio maskini,
kwa sababu Ufalme wa Mbingini
ni wenu.
21Mmebarikiwa ninyi mlio na njaa sasa,
kwa sababu mtashibishwa.
Mmebarikiwa ninyi mnaolia sasa,
kwa sababu mtacheka.
22Mmebarikiwa ninyi watu watakapowachukia,
watakapowatenga na kuwatukana
na kulikataa jina lenu kama neno
ovu, kwa ajili ya Mwana wa Adamu.

23Furahini na kurukaruka kwa shangwe kwa
sababu thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa
kuwa hivyo ndivyo baba zao walivyowatenda
manabii.

24"Lakini ole wenu ninyi mlio matajiri,
kwa sababu mmekwisha kupata
faraja yenu.
25Ole wenu ninyi mlioshiba sasa,
maana mtaona njaa.
Ole wenu ninyi mnaocheka sasa,
maana mtaomboleza na kulia.
26Ole wenu watu watakapowasifu,
kwani ndivyo baba zao walivyowasifu
manabii wa uongo."

### *Wapendeni Adui Zenu*

27"Lakini nawaambia wale wanaonisikia,
wapendeni adui zenu. Watendeeni mema
wanaowachukia. 28Wabarikini wale
wanaowalaani, waombeeni wale wanao
watendea mabaya. 29Kama mtu akikupiga
shavu moja mgeuzie na la pili. Mtu
akikunyang'anya koti lako, usimzuie kuchukua
joho pia. 30Mpe kila akuombaye na kama mtu
akichukua mali yako usitake akurudishie.
31Watendeeni wengine kama ambavyo
mngetaka wawatendee ninyi.
32"Kama mkiwapenda tu wale

wanaowapenda, mwapata sifa gani? Hata wenye dhambi huwapenda wale wawapendao. 33Tena mkiwatendea mema wale tu wanaowatendea ninyi mema mwapata sifa gani? Hata “wenye dhambi” hufanya vivyo hivyo. 34Tena mnapowakopesha wale tu mnaotegemea wawalipe, mwapata sifa gani? Hata “wenye dhambi” huwakopesha wenye dhambi wenzao wakitarajia kulipwa mali yao yote. 35 Lakini wapendeni adui zenu, watendeeni mema, wakopesheni bila kutegemea kurudishiwa mlichokopesha. Ndipo thawabu yenu itakapokuwa kubwa, nanyi mtakuwa wana wa Aliye Juu, kwa sababu Yeye ni mwema kwa watu wasio na shukrani na waovu. 36Iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma.

### *Kuwahukumu Wengine*

37“Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa. Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni, nanyi mtasamehewa. 38Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa. Kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa.”

39Pia akawapa mfano akasema, “Je, kipofu aweza kumwongoza kipofu? Je, wote wawili hawatatumbukia shimoni? 40 Mwanafunzi hamzidi mwalimu wake, ila yule aliyehitimu aweza kuwa kama mwalimu wake.

41“Mbona unatazama kibanzi kilichoko ndani ya jicho la mwenzako nawe huoni boriti iliyoko ndani ya jicho lako? 42Utawezaje kumwambia ndugu yako, ‘Ndugu yangu, niache nikitoe hicho kibanzi kilichoko ndani ya jicho lako’, wakati wewe mwenyewe huoni boriti iliyoko ndani ya jicho lako? Ewe mnafiki, ondoa kwanza boriti ndani ya jicho lako, ndipo utakapoweza kuona dhahiri jinsi ya kuondoa kibanzi kilichoko ndani ya jicho la ndugu yako.

43“Hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya wala hakuna mti mbaya uzaao matunda mazuri. 44Kila mti hujulikana kwa matunda yake. Kwa maana watu hawachumi tini kwenye miiba wala zabibu kwenye michongoma. 45Vivyo hivyo mtu mwema hutoa mambo mema kutoka kwenye hazina ya moyo wake, naye mtu mwovu hutoa mambo mabaya kutoka kwenye hazina ya moyo wake. Kwa kuwa mtu hunena kwa kinywa chake yale yaliyoujaza moyo wake.

### *Mjenzi Mwenye Busara Na Mpumbavu*

46“Kwa nini mnaniita, ‘Bwana, Bwana,’ nanyi hamfanyi ninayowaambia? 47Nitawaonyesha jinsi alivyo mtu yule anayekuja kwangu na kusikia maneno Yangu na kuyatenda. 48Yeye ni kama mtu anayejenga nyumba, akachimba chini sana na kuweka msingi kwenye mwamba. Mafuriko yalipokuja, maji ya ghafula yakaipiga ile nyumba lakini haikutikisika, kwa sababu ilikuwa imejengwa vizuri juu ya mwamba. 49Lakini yeye ayasikiaye maneno Yangu na asiyatende ni kama mtu aliyejenga nyumba juu ya mchanga bila kuweka msingi. Mafuriko yalipoikumba nyumba ile, ikaanguka mara na kubomoka kabisa.”

### *Yesu Amponya Mtumishi Wa Jemadari*

**7** Baada ya Yesu kumaliza kusema haya yote watu wakiwa wanamsikiliza, akaingia Kapernaumu. 2Mtumishi wa jemadari mmoja wa Kirumi, ambaye bwana wake alimthamini sana, alikuwa mgonjwa sana karibu ya kufa. 3Jemadari huyo aliposikia habari za Yesu, aliwatuma wazee wa Kiyahudi Kwake, wakamwomba aje kumponya mtumishi wa huyo jemadari. 4Wale wazee walipofika kwa Yesu, wakamsihi sana amsaidie yule jemadari wakisema, “Mtu huyu anastahili Wewe umfanyie jambo hili, 5kwa sababu analipenda taifa letu tena ametujengea sinagogi.” 6Hivyo Yesu akaongozana nao,

lakini alipokuwa hayuko mbali na nyumbani, yule jemadari akatuma rafiki zake kumwambia Yesu, “Bwana, usijisumbue kwani mimi sistahili Wewe kuingia chini ya dari yangu. 7Ndiyo maana sikujiona ninastahili hata kuja kwako. Lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu atapona. 8Kwa kuwa mimi mwenyewe ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, nikiwa na askari chini yangu. Nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ yeye huenda na huyu, ‘Njoo,’ yeye huja. Nikimwambia mtumishi wangu, ‘Fanya hili,’ yeye hufanya.”

9Yesu aliposikia maneno haya alimshangaa sana, akaugeukia ule umati wa watu uliokuwa unamfuata, akawaambia, “Sijaona imani kubwa namna hii hata katika Israeli.” 10Nao wale watu waliokuwa wametumwa kwa Yesu waliporudi nyumbani walimkuta yule mtumishi amepona.

### *Yesu Amfufua Mwana Wa Mjane*

11Baadaye kidogo, Yesu alikwenda katika mji mmoja ulioitwa Naini. Nao wanafunzi Wake

na umati mkubwa wa watu walikwenda pamoja
naye. **12**Alipokaribia lango la mji, alikutana na
watu waliokuwa wamebeba maiti wakitoka nje
ya mji. Huyu aliyekufa alikuwa mwana pekee wa
mwanamke mjane. Umati mkubwa wa watu wa
mji ule ulikuwa pamoja na huyo mwanamke.
**13**Bwana Yesu alipomwona yule mjane, moyo
Wake ulimhurumia, akamwambia, “Usilie.”

**14**Kisha akasogea mbele akaligusa lile
jeneza na wale waliokuwa wamelibeba
wakasimama kimya. Akasema, “Kijana,
nakuambia inuka.” **15**Yule aliyekuwa amekufa
akaketi akaanza kuongea, naye Yesu
akamkabidhi kwa mama yake.

**16**Watu wote wakajawa na hofu ya Mungu,
nao wakamtukuza Mungu wakisema, “Nabii
mkuu ametokea miongoni mwetu, Mungu
amekuja kuwakomboa watu Wake.” **17**Habari
hizi za mambo aliyofanya Yesu zikaenea
Uyahudi wote na sehemu zote za jirani.

### *Yesu Na Yohana Mbatizaji*

**18**Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji
wakamweleza Yohana mambo haya yote. Hivyo
Yohana akawaita wanafunzi wake wawili **19**na
kuwatuma kwa Bwana ili kumwuliza, “Je, Wewe
ndiye yule ajaye, au tumtazamie mwingine?’”

**20**Wale watu walipofika kwa Yesu
wakamwambia, ‘‘Yohana Mbatizaji ametutuma
tukuulize, ‘Je, Wewe ndiye yule ajaye au
tumtazamie mwingine?’ ”

**21**Wakati huo huo, Yesu aliwaponya wengi
waliokuwa na magonjwa, maradhi na pepo
wachafu, pia akawafungua vipofu wengi macho
wakaona. **22**Hivyo akawajibu wale wajumbe,
“Rudini mkamwambie Yohana yote mliyoyaona
na kuyasikia. Vipofu wanaona, viwete
wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa,
viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa na maskini
wahubiriwa Habari Njema. **23**Amebarikiwa mtu
yule asiyechukizwa nami.”

**24**Wanafunzi wa Yohana walipoondoka, Yesu
akaanza kuuambia ule umati wa watu kuhusu
Yohana: “Mlipokwenda nyikani mlikwenda kuona
nini? Je, ni unyasi ukipeperushwa na upepo?
**25**Kama sivyo, mlikwenda kuona nini basi? Mtu
aliyevaa mavazi ya fahari? La hasha, watu
wanaovaa mavazi ya fahari na kuishi maisha ya
anasa hukaa katika majumba ya kifalme. **26**Lakini
mlikwenda kuona nini? Mlikwenda kumwona
nabii? Naam! Nawaambia, tena zaidi ya nabii.
**27**Huyu ndiye ambaye habari zake zimeandikwa:

“Tazama, namtuma mjumbe wangu
akutangulie, atakayeandaa njia mbele
yako.”

**28**Nawaambia, miongoni mwa wale waliozaliwa
na mwanamke hakuna aliye mkuu kuliko
Yohana, lakini yeye aliye mdogo kabisa katika
Ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko Yohana.”

(**29**Watu wote hata watoza ushuru
waliposikia maneno ya Yesu, walikubali
kwamba mpango wa Mungu ni mwema, maana
walikuwa wamebatizwa na Yohana. **30**Lakini
Mafarisayo na wataalamu wa sheria walikataa
mpango wa Mungu kwao kwa kutokukubali
kubatizwa na Yohana.)

**31**Yesu akawauliza, “Niwafananishe na nini
watu wa kizazi hiki? Wanafanana na nini?
**32**Wao ni kama watoto waliokaa sokoni
wakiitana wao kwa wao wakisema:

“ ‘Tuliwapigia filimbi,
lakini hamkucheza,
tuliwaimbia nyimbo za
maombolezo, lakini hamkulia.’

**33**Kwa maana Yohana Mbatizaji alikuwa hali
mkate wala hanywi divai, ninyi mkasema, ‘Ana
pepo mchafu,’ **34**Mwana wa Adamu alikuja akila
na kunywa, nanyi mnasema: ‘Mtazameni huyu
mlafi na mlevi, rafiki wa watoza ushuru na
wenye dhambi.’ **35**Nayo hekima imethibitishwa
kuwa kweli na watoto wake wote.”

### *Yesu Apakwa Mafuta Na Mwanamke Mwenye Dhambi*

**36**Basi Farisayo mmoja alimwalika Yesu
nyumbani kwake kwa chakula. Hivyo Yesu
akaenda nyumbani mwa yule Farisayo na kukaa
katika nafasi Yake mezani. **37**Naye mwanamke
mmoja kwenye ule mji, ambaye alikuwa mwenye
dhambi, alipojua kwamba Yesu alikuwa akila
chakula nyumbani kwa yule Farisayo, akaleta
chupa ya marmar yenye manukato. **38**Yule
mwanamke akiwa amesimama nyuma ya miguu
ya Yesu alilia. Akailowanisha miguu yake kwa
machozi yake, kisha akaifuta kwa nywele zake
akaibusu na kuimiminia manukato.

**39**Yule Farisayo aliyemwalika Yesu alipoona
yanayotendeka, akawaza moyoni mwake,
“Kama huyu mtu angekuwa nabii, angejua
kwamba ni nani anayemgusa na kwamba yeye
ni mwanamke wa namna gani na ya kuwa huyu
mwanamke ni mwenye dhambi.”

40Yesu akanena akamwambia, “Simoni,
nina jambo la kukuambia.”
Simoni akajibu, “Mwalimu Sema.”
41“Palikuwa na mtu mmoja aliyewakopesha
watu wawili fedha: Mmoja alidaiwa dinari 500[a]
na mwingine dinari hamsini. 42Wote wawili
walipokuwa hawawezi kulipa, aliyafuta madeni
yao wote wawili. Sasa ni yupi kati yao
atakayempenda yule aliyewasamehe zaidi?”
43Simoni akajibu, “Nadhani ni yule
aliyesamehewa deni kubwa zaidi.”
Naye Yesu akamwambia, “Umehukumu kwa
sahihi.”
44Kisha akamgeukia yule mwanamke
akamwambia Simoni, “Je, unamwona
mwanamke huyu? Niliingia nyumbani mwako,
hukunipa maji ya kunawa miguu yangu, lakini
huyu ameninawisha miguu kwa machozi yake
na kunifuta kwa nywele zake. 45Hukunisalimu
kwa busu, lakini huyu mwanamke hajaacha
kuibusu miguu yangu tangu nilipoingia.
46Hukunipaka mafuta kichwani mwangu, lakini
yeye ameipaka miguu yangu manukato. 47Kwa
hiyo, nakuambia, dhambi zake zilizokuwa nyingi
zimesamehewa, kwani ameonyesha upendo
mwingi. Lakini yule aliyesamehewa kidogo,
hupenda kidogo.”
48Kisha akamwambia yule mwanamke,
“Dhambi zako simesamehewa.”
49Lakini wale waliokuwa wameketi pamoja
naye chakulani wakaanza kusemezana wao
kwa wao, “Huyu ni nani ambaye hata
anasamehe dhambi?”
50Yesu akamwambia yule mwanamke,
“Imani yako imekuokoa, nenda kwa amani.”

### *Mfano Wa Mpanzi*

**8** Baada ya haya Yesu alikwenda akawa
anazunguka katika miji na vijiji akihubiri Habari
Njema za Ufalme wa Mungu. Wale
wanafunzi Wake kumi na wawili walikuwa
pamoja naye, 2pia baadhi ya wanawake
waliokuwa wametolewa pepo wachafu na
kuponywa magonjwa miongoni mwao alikuwepo
Maria Magdalene, aliyetolewa pepo wachafu
saba, 3 Yoana mkewe Kuza, msimamizi wa
nyumba ya watu wa nyumbani mwa Herode,
Susana na wengine wengi waliokuwa
wakimhudumia kwa mali zao.
4 Wakati umati mkubwa wa watu ulipokuwa
ukija kwa Yesu kutoka mji hadi mji, akawaambia
mfano huu: 5“Mpanzi alitoka kwenda kusia
mbegu zake. Alipokuwa akitawanya mbegu,
nyingine zilianguka kando ya njia,
zikakanyagwa-kanyagwa na ndege wa angani
wakazila. 6Mbegu nyingine zilianguka penye
miamba, nazo zilipoota, hiyo mimea ikakauka
kwa kukosa unyevu. 7Nazo mbegu nyingine
zilianguka kwenye miiba, ile miiba ikakua
pamoja nazo na kusonga hiyo mimea ikafa.
8Mbegu nyingine zilianguka penye udongo
mzuri. Zikaota na kuzaa mara mia zaidi ya
mbegu alizopanda.”
Baada ya kusema haya, Yesu akapaza
sauti akasema, “Mwenye masikio ya kusikia na
asikie.”
9Wanafunzi Wake wakamuliza maana ya
mfano huu. 10 Naye akasema, “Ninyi mmejaliwa
kufahamu siri za Ufalme wa Mungu, lakini kwa
wengine nazungumza kwa mifano,

‘Ili ingawa wanaona, wasione,
Ingawa wanasikia, wasielewe.’ ”

11“Maana ya mfano huu ni hii: Mbegu ni
neno la Mungu. 12Zile zilizoanguka kando ya
njia, ni wale ambao husikia neno na ibilisi huja
na kuliondoa kutoka mioyoni mwao, ili wasije
wakaamini na kuokoka. 13Zile za kwenye
mwamba ni wale ambao hulipokea neno kwa
furaha wanapolisikia, lakini hawana mizizi.
Wanaamini kwa kitambo klidogo, lakini wakati
wa kujaribiwa huiacha imani. 14Zile mbegu
zilizoanguka kwenye miiba ni mfano wa wale
wanaosikia, lakini wanapoendelea husongwa na
masumbufu ya maisha haya, utajiri na anasa,
nao hawakui. 15Lakini zile mbegu kwenye
udongo mzuri ni mfano wa wale ambao hulisikia
neno la Mungu na kulishika kwa moyo mnyofu
na wa utii, nao kwa kuvumilia kwingi huzaa
matunda.

### *Mfano Wa Taa*

16 “Hakuna mtu awashaye taa na kuificha
ndani ya gudulia au kuiweka mvunguni mwa
kitanda. Badala yake, huiweka juu ya kinara, ili
wale waingiao ndani waone mwanga. 17Kwa
maana hakuna jambo lo lote lililofichika ambalo
halitafichuliwa, wala lo lote lililositirika ambalo
halitajulikana na kuwekwa wazi. 18Kwa hiyo,
iweni waangalifu mnavyosikia. Kwa maana ye
yote aliye na kitu atazidishiwa na ye yote asiye
nacho, hata kile anachodhani anacho
atanyang’anywa.’’

a[41] Dinari 500 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 500.
Kwani mshahara wa kibarua ulikuwa dinari moja kwa siku.

### *Ndugu Za Yesu Na Mama Yake*

19Wakati mmoja mama yake Yesu na ndugu
zake walikuja kumwona, lakini hawakuweza
kumfikia kwa sababu ya msongamano wa watu.
20Mtu mmoja akamwambia, “Mama Yako na
ndugu Zako wako nje wanataka kukuona.”

21Yesu akamjibu, “Mama Yangu na ndugu
Zangu ni wale wote wanaolisikia neno la Mungu
na kulitii.”

### *Yesu Atuliza Dhoruba*

22Siku moja Yesu alipanda ndani ya mashua
pamoja na wanafunzi Wake, akawaambia,
“Twendeni tuvuke mpaka ng’ambo ya ziwa.”
23Hivyo wakaondoka, akalala usingizi. Dhoruba
kali ikatokea mle ziwani, hata mashua ikawa
inajaa maji, nao walikuwa katika hatari kubwa.

24Wanafunzi Wake wakamwendea na
kumwamsha, wakipiga kelele, wakisema,
‘‘Bwana, Bwana, tunaangamia!”

Yeye akaamka akaukemea ule upepo na
yale mawimbi, vikakoma, pakawa shwari.
25Akawauliza wanafunzi Wake, “Imani yenu iko
wapi?”

Kwa woga na mshangao wakaulizana,
“Huyu ni mtu wa namna gani ambaye anaamuru
hata upepo na maji navyo vikamtii?”

### *Yesu Amponya Mtu Mwenye Pepo Mchafu*

26Basi wakafika katika nchi ya Wagerasi,
ambayo iko upande wa pili wa ziwa kutoka
Galilaya, 27Yesu aliposhuka katika mashua na
kukanyaga pwani, alikutana na mtu mmoja wa
mji ule aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu,
naye kwa muda mrefu alikuwa havai nguo wala
kuishi nyumbaini, bali makaburini.
28Alipomwona Yesu alipiga kelele, akajitupa
chini mbele Yake na kusema kwa sauti kuu,
“Nina nini nawe, Yesu Mwana wa Mungu Aliye
Juu? Nakuomba, usinitese!’’ 29Wakati huo Yesu
alikuwa amemwamuru yule pepo mchafu
amtoke huyo mtu. Mara nyingi huyo pepo
mchafu alimpagaa na hata alipofungwa kwa
minyororo mikono na miguu na kuwekwa chini
ya ulinzi alikata hiyo minyororo na kupelekwa na
huyo pepo mchafu kwenda nyikani.

30Yesu akamwuliza, “Jina lako ni nani?”

Akamjibu, “Legioni”, maana yake, “Jeshi,”
kwa kuwa alikuwa ameingiwa na pepo wachafu
wengi mno. 31Wale pepo wachafu wakamsihi
sana asiwaamru kwenda shimoni[a].

32Palikuwa na kundi kubwa la nguruwe
hapo karibu wakilisha kandokando ya kilima.
Wale pepo wachafu wakamsihi Yesu
awaruhusu wawaingie hao nguruwe, naye
akawaruhusu. 33Wale pepo wachafu
walipomtoka yule mtu, wakawaingia wale
nguruwe, nalo kundi lote likatelemkia gengeni
likatumbukia ziwani na kuzama.

34 Wale watu waliokuwa wakichunga lile
kundi la nguruwe walipoona yaliyotukia,
wakakimbia, wakaeneza habari hizi mjini na
mashambani. 35Nao watu wakatoka kwenda
kujionea wenyewe yaliyotukia. Walipofika hapo
alipokuwa Yesu wakamkuta yule mtu aliyetokwa
na pepo wachafu amekaa karibu na Yesu,
akiwa amevaa nguo na mwenye akili timamu!
Wakaogopa sana. 36Wale walioona mambo
hayo wakawaeleza wenzao jinsi yule mtu
aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu
alivyoponywa. 37Ndipo watu wote wa nchi ile ya
Wagerasi wakamwomba Yesu aondoke kwao,
kwa sababu walikuwa wamejawa na hofu. Basi
akaingia katika mashua akaondoka Zake.

38Yule mtu aliyetokwa na pepo wachafu
akamsihi Yesu afuatane naye, lakini Yesu
akamwaga, akamwambia: 39‘‘Rudi nyumbani
ukawaeleze mambo makuu Mungu
aliyokutendea.” Kwa hiyo yule mtu akaenda,
akatangaza katika mji wote mambo makuu
Yesu aliyomtendea.

### *Msichana Afufuliwa Na Mwanamke Aponywa*

40Basi Yesu aliporudi, umati mkubwa wa
watu ukampokea kwa furaha, kwani walikuwa
wakimngojea. 41Kisha mtu mmoja jina lake
Yairo, kiongozi wa sinagogi, akaja na kuanguka
miguuni mwa Yesu, akimwomba afike nyumbani
kwake, 42kwa kuwa binti yake wa pekee,
mwenye umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa
anakufa.

Yesu alipokuwa akienda, umati wa watu
ukamsonga sana. 43Katika umati huo alikuwepo
mwanamke mmoja aliyekuwa anatokwa damu
kwa muda wa miaka kumi na miwili, tena
alikuwa amegharimia yote aliyokuwa nayo kwa
ajili ya matibabu wala hakuna ye yote aliyeweza
kumponya. 44Huyo mwanamke akaja kwa
nyuma na kugusa upindo wa vazi la Yesu, mara
kutokwa damu kwake kukakoma.

45Yesu akauliza, “Ni nani aliyenigusa?”

---

[a]31 “Shimoni” hapa ina maana ya ‘shimo lisilo na mwisho,’ yaani, kuzimu hasa makao ya pepo wachafu.

Watu wote walipokana, Petro akasema,
“Bwana, huu umati wa watu unakusonga na
kukusukuma kila upande.”

46Lakini Yesu akasema, “Kuna mtu
aliyenigusa, kwa maana nimetambua kuwa
nguvu zimenitoka.”

47Yule mwanamke alipofahamu ya kuwa
hawezi kuendelea kujificha, alikuja akitetemeka,
akaanguka miguuni mwa Yesu, akaeleza mbele
ya watu wote kwa nini alimgusa na jinsi
alivyoponywa mara. 48Basi Yesu akamwambia,
“Binti, imani yako imekuponya. Nenda kwa
amani.”

49Yesu alipokuwa bado anasema, akaja
mtumishi kutoka nyumbani kwa Yairo, yule
kiongozi wa sinagogi, kumwambia, “Binti yako
amekwisha kufa. Usiendelee kumsumbua
Mwalimu.’’

50Yesu aliposikia jambo hili, akamwambia
Yairo, “Usiogope, amini tu, naye binti yako
atapona.”

51Walipofika nyumbani kwa Yairo,
hakumruhusu mtu ye yote aingie ndani pamoja
naye isipokuwa Petro, Yakobo na Yohana, baba
na mama wa yule binti. 52Wakati ule ule watu
wote walikuwa wakilia na kuomboleza kwa ajili
ya huyo binti. Yesu akawaambia, “Acheni kulia.
Huyu binti hajafa ila amelala.”

53 Wao wakamcheka kwa dharau, wakijua
kuwa amekwisha kufa. 54Yesu akamshika yule
binti mkono na kuita, “Binti, amka!” 55Roho yake
ikamrudia, naye akainuka mara. Akaamuru
apewe kitu cho chote cha kula. 56Wazazi wake
wakastaajabu sana, lakini Yesu akawakataza
wasimwambie mtu ye yote juu ya yale
yaliyotukia.

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*

**9** Yesu akiisha kuwaita wale kumi na wawili
pamoja, aliwapa mamalaka na uwezo wa kutoa
pepo wachafu wote na kuponya magonjwa
yote, 2 kisha akawatuma waende wakahubiri
Ufalme wa Mungu na kuponya wagonjwa.
3Akawaagiza akisema, “Msichukue cho chote
safarini, wala fimbo, wala mkoba, wala chakula,
wala fedha, wala msichukue kanzu ya ziada.
4Katika nyumba yo yote mwingiayo, kaeni
humo hadi mtakapoondoka katika mji huo.
5Kama watu wasipowakaribisha, mnapoondoka
katika mji wao, kung’uteni mavumbi miguuni
mwenu kuwa ushuhuda dhidi yao.’’ 6Hivyo
wale wanafunzi wakaondoka wakaenda
kutoka kijiji hadi kijiji, wakihubiri
Habari Njema na kuponya wagonjwa kila
mahali.

7Basi Herode mtawala wa Galilaya akasikia
habari za yote yaliyotendeka, naye akafadhaika
kwa kuwa baadhi ya watu walikuwa wakisema,
“Yohana Mbatizaji amefufuka.” 8Wengine
wakasema, “Eliya ametutokea” na wengine
wakasema kwamba, “Mmoja wa manabii wa
kale amefufuka.” 9Herode akasema, “Yohana
nilimkata kichwa. Lakini ni nani basi huyu
ambaye ninasikia habari Zake kuhusu mambo
kama haya?”. Akatamani sana kumwona.

### *Yesu Awalisha Watu 5,000*

10Wale mitume Wake waliporudi,
wakamweleza Yesu yote waliyofanya.
Akawachukua akaenda nao faraghani mpaka
mji mmoja uitwao Bethsaida. 11Lakini umati wa
watu ulipofahamu alikokwenda, wakamfuata.
Akawakaribisha na kunena nao kuhusu Ufalme
wa Mungu na kuwaponya wale wote waliokuwa
wanahitaji uponyaji.

12Ilipokaribia jioni, wale mitume kumi na
wawili wakamjia Yesu na kumwambia, “Uage
umati huu wa watu waondoke ili waweze
kwenda kwenye vijiji vya karibu na sehemu za
jirani, ili kupata chakula na mahali pa kulala kwa
maana hapa tuko nyikani.”

13 Yesu akawajibu, “Ninyi wapeni chakula.”

Wao wakasema, “Hatuna zaidi ya mikate
mitano na samaki wawili, labda tuende
tukanunue chakula cha kuwatosha watu wote
hawa.” 14Kwa kuwa walikuwako wanaume
wapatao 5,000.

Yesu akawaambia wanafunzi Wake,
“Waketisheni katika makundi ya watu hamsini
hamsini.” 15Wakafanya hivyo, wakawaketisha
wote. 16Yesu akaichukua ile mikate mitano na
wale samaki wawili, akatazama mbinguni,
akavibariki na kuvimega, kisha akawapa
wanafunzi wake waugawie ule umati wa watu.
17Wote wakala, wakashiba. Nao wanafunzi
wakakusanya vipande vilivyobaki, vikajaa
vikapu kumi na viwili.

### *Petro Amkiri Bwana Yesu Kuwa Ndiye Kristo*

18Wakati mmoja, Yesu alipokuwa akiomba
faraghani, nao wanafunzi Wake wakiwa pamoja
naye, akawauliza, “Watu husema mimi ni nani?”

19Wakamjibu, “Wengine husema Wewe ni
Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya na
wengine husema, Wewe ni mmoja wa nabii wa
kale aliyefufuka kutoka kwa wafu.”

20Kisha akawauliza, “Je, ninyi mnasema
Mimi ni nani?”

Petro akajibu, “Wewe ndiwe Kristo wa
Mungu.”

21Yesu akawakataza wasimwambie mtu ye
yote jambo hilo. 22Yesu akasema, “Imempasa
Mwana wa Adamu kupata mateso mengi na
kukataliwa na wazee, viongozi wa makuhani na
walimu wa sheria, naye atauawa na siku ya tatu
atafufuka.”

23Kisha akawaambia wote, “Ye yote
anayetaka kunifuata ni lazima ajikane
mwenyewe, achukue msalaba wake kila siku na
anifuate. 24Kwa maana ye yote
atakayekuyaponya maisha yake atayapoteza,
lakini ye yote atakayepoteza maisha yake kwa
ajili Yangu atayaokoa. 25Je, itamfaidia nini mtu
kuupata ulimwengu wote, lakini akayapoteza
maisha yake? 26Kama mtu ye yote akinionea
aibu Mimi na maneno Yangu, Mwana wa Adamu
atamwonea aibu mtu huyo atakapokuja katika
utukufu Wake na katika utukufu wa Baba na wa
malaika watakatifu. 27Amin, amin nawaambia,
wako baadhi ya watu waliosimama hapa ambao
hawataonja mauti mpaka watakapouona Ufalme
wa Mungu.’’

### *Bwana Yesu Abadilika Sura*

28 Yapata siku nane baada ya Yesu kusema
hayo, aliwachukua Petro, Yakobo na Yohana
akaenda nao mlimani kuomba. 29Alipokuwa
akiomba, mwonekano wa sura yake ukabadilika,
mavazi Yake yakameta-meta kama mwanga wa
umeme wa radi. 30Ghafula wakawaona watu
wawili, Mose na Eliya wakizungumza naye.
31Walionekana katika utukufu wakizungumza na
Yesu kuhusu kifo Chake ambacho kingetokea
huko Yerusalemu. 32Petro na wenzake
waliokuwa wamelala usingizi mzito walipoamka,
wakaona utukufu wa Yesu na wale watu wawili
waliokuwa wamesimama pamoja naye. 33Mose
na Eliya, walipokuwa wanaondoka, Petro
akamwambia Yesu, “Bwana, ni vizuri tukae
hapa! Tutajenga vibanda vitatu, kimoja Chako,
kingine cha Mose na kingine cha Eliya.” Lakini
Petro alikuwa hajui asemacho.

34Alipokuwa bado anazungumza, pakatokea
wingu likawafunika, nao wakaogopa walipoingia
mle kwenye wingu. 35 Sauti ikatoka kwenye lile
wingu ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa
Wangu, msikilizeni Yeye.” 36Baada ya Sauti hiyo
kusema, walimkuta Yesu akiwa peke Yake. Wale
wanafunzi wakalihifadhi jambo hili wala
kwa wakati huo hawakumwambia mtu ye yote
yale waliyokuwa wameyaona.

### *Kuponywa Kwa Kijana Mwenye Pepo Mchafu*

37Kesho yake, waliposhuka kutoka mlimani,
alikutana na umati mkubwa wa watu. 38Mtu
mmoja miongoni mwa ule umati wa watu
ukapiga kelele, akasema, “Mwalimu, naomba
umwangalie mwanangu, ndiye mtoto wangu wa
pekee. 39 Mara kwa mara pepo mchafu
humpagaa na kumfanya apige kelele, kisha
humwangusha na kumtia kifafa akatokwa na
povu kinywani. Huyo pepo chafu anamtesa
sana na hamwachii ila mara chache.
40Niliwaomba wanafunzi Wako wamtoe huyo
pepo mchafu lakini hawakuweza.”

41Yesu akajibu akawaambia, “Enyi kizazi
kisichoamini na kilichopotoka, nitakaa nanyi na
kuwavumilia mpaka lini? Mlete mwanao hapa.”

42Hata yule mtoto alipokuwa akija, yule
pepo mchafu akamwangusha, akamtia kifafa.
Lakini Yesu akamkemea yule pepo mchafu
amtoke, akamponya yule mtoto, akamrudisha
kwa baba yake. 43Watu wote wakastaajabia
uweza mkuu wa Mungu.

Wakati bado watu wanastaajabia hayo yote
aliyokuwa akiyafanya Yesu, Yeye akawaambia
wanafunzi Wake: 44“Sikilizeni kwa bidii haya
nitakayowaambia sasa: “Mwana wa Adamu
atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu.”
45Lakini wao hawakuelewa alimaanisha nini.
Maana ya maneno hayo ilifichika kwao, hivyo
hawakuyaelewa, nao wakaogopa kumwuliza
maana yake.

### *Ni Nani Atakayekuwa Mkubwa Kuliko Wote*

46Kukazuka mabishano miongoni mwa
wanafunzi kuhusu ni nani miongoni mwao
atakayekuwa mkuu kuliko wote. 47Lakini Yesu
akayatambua mawazo yao, akamchukua mtoto
mdogo, akamsimamisha kando Yake. 48Kisha
akawaambia, “Ye yote atakayemkaribisha mtoto
huyu mdogo kwa Jina langu, atakuwa
amenikaribisha Mimi na ye yote
atakayenikaribisha Mimi, atakuwa
amemkaribisha Yeye aliyenituma, kwa maana
yeye aliye mdogo miongoni mwenu, ndiye aliye
mkuu kuliko wote.”

49Yohana akasema, “Bwana, tumemwona
mtu akitoa pepo wachafu kwa Jina lako
tukamzuia, kwa sababu yeye si mmoja wetu.”

50Yesu akasema, “Msimzuie, kwa sababu
ye yote ambaye si kinyume nanyi, yu upande

wenu.”

### *Yesu Akataliwa Samaria*

51Wakati ulipokaribia wa Yeye kuchukuliwa
mbinguni, alikaza uso Wake kwenda
Yerusalemu. 52Akatuma watu wamtangulie, nao
wakaenda katika kijiji kimoja cha Samaria
kumwandalia kila kitu, 53lakini watu wa kijiji kile
hawakumkaribisha kwa sababu alikuwa
anakwenda Zake Yerusalemu. 54Wanafunzi
Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona
hayo, wakasema: “Bwana, unataka tuagize
moto kutoka mbinguni ili uwaangamize?”
55Yesu akageuka na kuwakemea, 56nao
wakaenda kijiji kingine.

### *Gharama Ya Kumfuata Yesu*

57Walipokuwa njiani wakienda, mtu mmoja
akamwambia Yesu, “Nitakufuata ko kote
uendako.”

58Yesu akamjibu, “Mbweha wana mapango
na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana
wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa
Chake.”

59Yesu akamwambia mtu mwingine,
“Nifuate.”

Mtu huyo akamjibu, “Bwana, niache kwanza
nikamzike baba yangu.”

60Yesu akamwambia, “Waache wafu
wawazike wafu wao, bali wewe nenda
ukautangaze Ufalme wa Mungu.”

61Mtu mwingine akamwambia, “Bwana,
nitakufuata lakini naomba kwanza nikaage
jamaa yangu.”

62Yesu akamwambia, “Mtu ye yote atiaye
mkono wake kulima, kisha akatazama nyuma,
hafai kwa Ufalme wa Mungu.”

### *Yesu Awatuma Wale Sabini Na Wawili*

**10** Baada ya hayo, Yesu akawachagua wengine
sabini na wawili, akawatuma wawili wawili katika kila
mji na kila sehemu
aliyokusudia kwenda Yeye mwenyewe.
2Akawaambia, “Mavuno ni mengi, lakini
watenda kazi ni wachache. Kwa hiyo mwombeni
Bwana wa mavuno, awapeleke watenda kazi
katika shamba lake. 3Haya, nendeni.
Ninawatuma kama kondoo katikati ya mbwa
mwitu. 4Msichukue mkoba wala mfuko, wala
viatu na msimsalimu mtu ye yote njiani.

5“Mkiingia katika nyumba yo yote kwanza
semeni, ‘Amani iwe kwenu.’ 6Kama kuna mtu
wa amani humo, basi amani yenu itakuwa juu
yake, la sivyo itawarudia. 7Kaeni katika nyumba
hiyo, mkila na kunywa kile watakachowapa, kwa
sababu kila mtenda kazi anastahili malipo yake.
Msihamehame kutoka nyumba hadi nyumba.

8“Mkienda katika mji na watu wake
wakawakaribisha, kuleni cho chote kiwekwacho
mbele yenu, 9waponyeni wagonjwa waliomo na
waambieni: ‘Ufalme wa Mungu umekaribia.’
10Lakini mkiingia katika mji, nao
hawakuwakaribisha, tokeni mwende katika
barabara zake mkaseme: 11 ‘Hata mavumbi ya
mji wenu yaliyoshikamana na miguu yetu,
tunayakung’uta dhidi yenu. Lakini mjue kwamba
Ufalme wa Mungu umekaribia.’ 12Ninawaambia,
hukumu ya Mungu katika Sodoma itavumilika
zaidi kuliko ya mji ule.

### *Ole Wa Miji Isiyotubu*

13“Ole wako Korazini! Ole wake Bethsaida!
Kwa kuwa miujiza iliyofanyika kwako
ingefanyika Tiro na Sidoni, ingekuwa imetubu
zamani, kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu.
14Lakini itavumilika zaidi Tiro na Sidoni katika
hukumu kuliko kwenu. 15Nawe, Kapernaumu,
je, utainuliwa hadi mbinguni? La hasha,
utashushwa mpaka kuzimu.”

16“Yeye awasikilizaye ninyi, anisikiliza Mimi,
naye awakataaye ninyi, amenikataa Mimi. Lakini
yeye anikataaye Mimi amkataa Yeye
aliyenituma.”

17Wale sabini na wawili wakarudi kwa
furaha na kusema, “Bwana, hata pepo wachafu
wanatutii kwa Jina Lako.”

18Yesu akawaambia, “Nilimwona Shetani
akianguka kutoka mbinguni kama umeme wa
radi. 19Tazama nimewapa mamlaka ya
kukanyaga nyoka na ng’e na juu ya nguvu zote
za adui, wala hakuna kitu cho chote
kitakachowadhuru kwa namna yo yote. 20Basi
msifurahi kwa kuwa pepo wachafu wanawatii,
bali furahini kwa kuwa majina yenu
yameandikwa mbinguni.”

### *Yesu Anashangilia*

21Saa ile ile, Yesu akashangilia katika Roho
Mtakatifu akasema, “Nakushukuru Baba, Bwana
wa mbingu na nchi, kwa sababu mambo haya
umewaficha wenye hekima na wenye akili,
nawe umewafunulia watoto wadogo. Naam,
Baba, kwa kuwa hayo ndiyo yaliyokuwa
mapenzi Yako.

22“Vitu vyote vimekabidhiwa mikononi
Mwangu na Baba. Wala hakuna amjuaye

Mwana ila Baba, wala amjuaye Baba ila Mwana
na ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia.”
23 Basi Yesu akawageukia wanafunzi Wake
akanena nao faraghani, akawaambia,
“Yamebarikiwa macho yanayoona yale mambo
mnayoyaona. 24 Kwa maana nawaambia,
manabii wengi na wafalme walitamani kuona
mnayoyaona, lakini hawakuyaona, pia kusikia
mnayoyasikia, lakini hawakuyasikia.”

### *Mfano Wa Msamaria Mwema*

25 Wakati huo mtaalam mmoja wa sheria
alisimama ili kumjaribu Yesu, akamwuliza,
“Mwalimu, nifanye nini ili nipate kurithi uzima wa
milele?”
26 Yesu akamjibu, “Imeandikwaje katika
Torati? Kwani unasoma nini humo?”
27 Akajibu, “ ‘Mpende Bwana Mungu wako
kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa
nguvu zako zote na kwa akili zako zote, tena
mpende jirani yako kama unavyojipenda
mwenyewe.’ ”
28 Yesu akamwambia, “Umejibu vema.
Fanya hivyo nawe utaishi.”
29 Lakini yule mtaalam wa sheria akitaka
kuonyesha kuwa mwenye haki, akamwuliza
Yesu, “Jirani yangu ni nani?”
30 Yesu akamjibu akasema, “Mtu mmoja
alikuwa akitelemka kutoka Yerusalemu kwenda
Yeriko, naye akaangukia mikononi mwa
wanyang’anyi, wakampiga, wakaondoka,
wakamwacha karibu ya kufa. 31 Kwa bahati nzuri
kuhani mmoja alikuwa anapitia njia ile,
alipomwona huyo mtu, akapita upande
mwingine wa barabara, akamwacha hapo hapo.
32 Vivyo hivyo Mlawi mmoja naye alipofika
mahali pale, alimwona, akapita upande
mwingine wa barabara, akamwcha hapo hapo.
33 “Lakini Msamaria mmoja aliyekuwa akisafiri
kupitia njia hiyo alipomwona, alimhurumia,
34 akamwendea, akasafisha majeraha yake kwa
divai na mafuta, kisha akayafunga. Ndipo
akampandisha kwenye punda wake akamleta
mpaka kwenye nyumba ya kulala wageni na
kumtunza. 35 Kesho yake, yule Msamaria
akachukua dinari mbili [a] akampa yule mwenye
nyumba ya wageni na kusema, ‘Mtunze, nami
nirudipo nitakulipa gharama yo yote ya ziada
uliyotumia kwa ajili yake.

[a] 35 Dinari mbili ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 2.
Kwani mshahara wa kibarua ulikuwa dinari moja kwa siku.

36 “Ni yupi basi miongoni mwa hawa watatu,
wewe unadhani ni jirani yake yule mtu
aliyeangukia mikononi mwa wanyang’anyi?”
37 Yule mtaalam wa sheria akajibu, “Ni yule
aliyemhurumia.”
Ndipo Yesu akamwambia, “Nenda,
ukafanye vivyo hivyo.”

### *Yesu Awatembelea Martha Na Maria*

38 Ikawa Yesu na wanafunzi Wake
walipokuwa wakienda Yerusalemu, akaingia
kwenye kijiji kimoja ambapo mwanamke mmoja
aliyeitwa Martha alimkaribisha nyumbani kwake.
39 Martha alikuwa na mdogo wake aliyeitwa
Maria, ambaye yeye aliketi chini miguuni mwa
Yesu akisikiliza yale aliyokuwa akisema.
40 Lakini Martha alikuwa akihangaika na
maandalizi yote yaliyokuwa yafanyike. Martha
akaja kwa Yesu na kumwuliza, “Bwana, hujali
kwamba ndugu yangu ameniachia kazi zote
mwenyewe? Basi mwambie anisaidie.”
41 Lakini Bwana akamjibu, “Martha,Martha,
mbona unasumbuka na kuhangaika na mengi?
42 Lakini kunahitajika kitu kimoja tu. Maria
amechagua kile kilicho bora, wala hakuna mtu
atakayemwondolea.”

### *Yesu Afundisha Wanafunzi Wake Kuomba*

**11** Siku moja, Yesu alikuwa mahali fulani akiomba.
Alipomaliza kuomba, mmoja wa wanafunzi Wake
akamwambia, “Bwana,
tufundishe kuomba, kama vile Yohana
alivyowafundisha wanafunzi wake.”
2 Akawaambia, “Mnapoomba, semeni hivi :

“ ‘Baba yetu uliye mbinguni,
Jina Lako litukuzwe,
Ufalme Wako uje.
3 Utupatie kila siku riziki zetu.
4 Utusamehe dhambi zetu,
kwa kuwa na sisi huwasamehe
wote wanaotukosea.
Wala usitutie majaribuni, bali utuokoe
kutoka kwa yule mwovu.’ ”

5 Kisha akawaambia, “Ni nani miongoni
mwenu mwenye rafiki yake, naye akamwendea
usiku wa manane na kumwambia, ‘Rafiki,
nikopeshe mikate mitatu. 6 Kwa sababu rafiki
yangu amekuja kutoka safarini, nami sina kitu
cha kumpa.’
7 “Kisha yule aliyeko ndani amjibu,
‘Usinisumbue. Mlango umefungwa, nami na

watoto wangu tumelala. Siwezi kuamka nikupe
cho chote.’ 8Nawaambia, ingawa huyo mtu
hataamka na kumpa hiyo mikate kwa sababu ni
rafiki yake, lakini kwa sababu ya kuendelea
kwake kuomba, ataamka na kumpa kiasi
anachohitaji.

9Kwa hiyo nawaambia, “Ombeni nanyi
mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, bisheni, nanyi
mtafunguliwa mlango. 10Kwa kuwa kila
aombaye hupewa, naye kila atafutaye hupata na
kila abishaye hufunguliwa mlango.

11Je, kuna ye yote miongoni mwenu,
ambaye mtoto wake akimwomba samaki,
atampa nyoka badala ya samaki? 12Au mtoto
akimwomba yai atampa ng’e? 13 Basi ikiwa ninyi
mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vitu
vizuri, si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni
atawapa Roho Mtakatifu wale wamwombao?”

### *Yesu Na Beelzebuli*

14Basi Yesu alikuwa anamtoa pepo mchafu
kutoka kwa mtu aliyekuwa bubu. Yule pepo
mchafu alipomtoka yule mtu aliyekuwa bubu,
akaanza kuongea, nao umati wa watu
ukashangaa. 15Lakini wengine wakasema,
“Anatoa pepo wachafu kwa uwezo wa
Beelzebuli, yule mkuu wa pepo wachafu wote.”
16Wengine ili kumjaribu wakataka awaonyeshe
ishara kutoka mbinguni.

17Yesu akijua mawazo yao, akawaambia,
“Kila ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe
huangamia, nayo nyumba iliyogawanyika dhidi
yake yenyewe huanguka. 18Kama Shetani
amegawanyika mwenyewe ufalme wake
utasimamaje? Nawaambia haya kwa sababu
ninyi mnadai ya kuwa Mimi ninatoa pepo
wachafu kwa uwezo wa Beelzebuli. 19Kama
Mimi ninatoa pepo wachafu kwa nguvu za
Beelzebuli, wafuasi wenu je, wao hutoa pepo
wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi, wao
watakuwa mahakimu wenu. 20 Lakini ikiwa
ninatoa pepo wachafu kwa kidole cha Mungu,
basi Ufalme wa Mungu umewajia.

21“Mtu mwenye nguvu aliyejifunga silaha,
anapoilinda nyumba yake, mali yake iko salama.
22Lakini mtu mwenye nguvu zaidi kuliko yeye
amshambuliapo na kumshinda, humnyang’anya
silaha zake zote alizozitegemea na kuchukua
nyara.

23 “Mtu ye yote ambaye hayuko pamoja
nami, yu kinyume changu na mtu ye yote
asiyekusanya pamoja nami, hutapanya.

### *Kurudi Kwa Pepo Mchafu*

24“Pepo mchafu amtokapo mtu,
huzungukazunguka sehemu zisizo na maji
akitafuta mahali pa kupumzika, lakini asipopata
mahali po pote husema, ‘Nitarudi kwenye
nyumba yangu nilikotoka.’ 25 Arudipo na kuikuta
ile nyumba imefagiliwa na kupambwa vizuri,
26ndipo huenda na kuchukua pepo wachafu
wengine saba wabaya kuliko yeye mwenyewe,
huingia na kukaa humo. Nayo hali ya mwisho ya
yule mtu huwa ni mbaya kuliko ile ya kwanza.’’

27Ikawa Yesu alipokuwa akisema hayo,
mwanamke mmoja katikati ya ule umati wa watu
akapaza sauti akasema, “Limebarikiwa tumbo
lililokuzaa na matiti uliyonyonya!”

28Yesu akajibu, “Wamebarikiwa zaidi wale
wanaolisikia neno la Mungu na kulitii.”

### *Ishara Ya Yona*

29Umati wa watu ulipokuwa unazidi
kuongezeka, Yesu akaendelea kufundisha
akisema, “Hiki ni kizazi kiovu. Kinatafuta ishara
lakini hakitapewa ishara yo yote isipokuwa ile ya
Yona. 30Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa
ishara kwa watu wa Ninawi, ndivyo Mwana wa
Adamu atakavyokuwa ishara kwa kizazi cha
sasa. 31 Siku ya hukumu, Malkia wa Kusini
atainuka pamoja na watu wa kizazi hiki
akiwahukumu kwa sababu yeye alisafiri kutoka
mbali kuja kusikiliza hekima ya Solomoni. Lakini
sasa, Yeye aliye mkuu kuliko Solomoni yuko
hapa. 32Siku ile ya hukumu, watu wa Ninawi
watasimama pamoja na kizazi hiki na
kukihukumu kwa sababu wao walitubu
walipomsikia Yona akihubiri. Lakini sasa, Yeye
aliye mkuu kuliko Yona yuko hapa.

### *Taa Ya Mwili*

33“Hakuna mtu ye yote awashaye taa na
kuiweka mahali palipofichika au kuifunikia chini
ya bakuli. Badala yake huiweka juu ya kinara
chake, ili watu wote wanaoingia waone nuru.
34Jicho lako ni taa ya mwili wako. Kama jicho
lako ni zima, mwili wako wote umejaa nuru.
Lakini kama jicho ni bovu, mwili wako wote
umejaa giza. 35Kwa hiyo, hakikisha kwamba
nuru iliyoko ndani yako isiwe giza. 36Basi ikiwa
mwili wako wote umejaa nuru, bila sehemu yake
yo yote kuwa gizani, basi utakuwa na nuru
kama vile taa ikuangazavyo kwa nuru yake.’’

### *Yesu Awashutumu Mafarisayo Na Wanasheria*

37Yesu alipomaliza kuzungumza, Farisayo mmoja alimkaribisha nyumbani kwake kwa chakula. Yesu akaingia na kuketi katika sehemu Yake mezani. 38Yule Farisayo akashangaa kwamba Yesu hakunawa kwanza kabla ya kula.

39Ndipo Bwana akamwambia, "Enyi Mafarisayo, mnasafisha kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani mmejaa choyo na uovu. 40Enyi wapumbavu! Hamjui kuwa Yeye aliyetengeneza nje ndiye aliyetengeneza na ndani pia? 41 Basi toeni sadaka vile mlivyo navyo na tazama, vitu vyote vitakuwa safi kwenu.

42"Lakini ole wenu, Mafarisayo, kwa maana mnampa Mungu zaka za mnanaa, mchicha na kila aina ya mboga, lakini mnapuza haki na upendo wa Mungu. Iliwapasa kutoa matoleo hayo, wala msisahau kufanya hayo mengine.

43"Ole wenu Mafarisayo, kwa sababu ninyi mnapenda kuketi viti vya mbele katika masinagogi na kusalimiwa kwa heshima masokoni.

44"Ole wenu, kwa sababu ninyi ni kama makaburi yasiyokuwa na alama, ambayo watu huyakanyaga pasipo kujua."

45Mtaalam mmoja wa sheria akamjibu, akasema, "Mwalimu, unaposema mambo haya, unatutukana na sisi pia."

46Yesu akamjibu, "Nanyi wataalam wa sheria, ole wenu, kwa sababu mnawatwika watu mizigo mizito ambayo hawawezi kubeba, wala ninyi wenyewe hamwinui hata kidole kimoja kuwasaidia.

47"Ole wenu, kwa sababu ninyi mnawajengea makaburi manabii waliouawa na
baba zenu. 48Hivyo ninyi ni mashahidi na mnathibitisha kile baba zenu walichofanya, wao waliwaua manabii, nanyi mnawatengenezea
makaburi. 49Kwa sababu ya jambo hili, Mungu katika hekima Yake alisema, 'Tazama, nitatuma kwao manabii na mitume, nao watawauwa
baadhi yao na wengine watawatesa.' 50Kwa hiyo kizazi hiki kitawajibika kwa ajili ya damu ile ya manabii iliyomwagwa tangu kuwekwa misingi
ya ulimwengu, 51tangu damu ya Abeli mpaka damu ya Zekaria, aliyeuawa kati ya madhabahu na mahali patakatifu. Naam, nawaambia, kizazi hiki kitawajibika kwa haya yote.

52"Ole wenu ninyi wataalam wa sheria, kwa sababu mmeuondoa ufunguo wa maarifa. Ninyi wenyewe hamkuingia na wale waliokuwa wanaingia mkawazuia.''

53Yesu alipoondoka huko, walimu wa sheria na Mafarisayo wakaanza kumpinga vikali na
kumsonga kwa maswali, 54wakivizia kumkamata kwa kitu atakachosema ili wamshtaki.

### *Maonyo Dhidi Ya Unafiki*

**12** Wakati huo, umati mkubwa wa watu kwa maelfu, walipokuwa wamekusanyika, hata wakawa wanakanyagana, Yesu akaanza kuzungumza kwanza na wanafunzi Wake, akawaambia: "Jihadharini na chachu ya Mafarisayo, yaani, unafiki wao.
2"Hakuna jambo lo lote lililositirika ambalo halitafunuliwa au lililofichwa ambalo
halitajulikana. 3 Kwa hiyo, lo lote mlilosema gizani litasikiwa nuruni na kile mlichonong'ona masikioni mkiwa kwenye vyumba vya ndani, kitatangazwa juu ya paa.

4 "Nawaambieni rariki zangu, msiwaogope wale wauao mwili na baada ya hilo hawawezi
kufanya lo lote zaidi. 5Lakini nitawaambia nani wa kumwogopa: "Mwogopeni yule ambaye baada ya kuua mwili, ana mamlaka ya kuwatupa motoni. Naam, nawaambia
mwogopeni huyo! 6Mnajua kwamba shomoro watano huuzwa kwa senti mbili? Lakini Mungu
hamsahau hata mmoja wao. 7Naam, hata idadi ya nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa. Kwa hiyo msiogope, ninyi ni wa thamani kuliko mashomoro wengi.

8"Ninawaambia kwamba, ye yote atakayenikiri mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri mbele za malaika wa Mungu.
9Lakini yeye atakayenikana mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkana mbele ya
malaika wa Mungu. 10Naye kila atakaye nena neno baya dhidi ya Mwana wa Adamu atasamehewa, lakini ye yote atakayemkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa.

11"Watakapowapeleka katika masinagogi mbele ya watawala na wenye mamlaka, msiwe na wasiwasi kuhusu namna mtakavyojitetea au
mtakavyosema: 12Kwa maana Roho Mtakatifu atawafundisha wakati uo huo mnachopaswa kusema."

### *Mfaano Wa Tajiri Mpumbavu*

13Mtu mmoja katika umati wa watu akamwambia Yesu, "Mwalimu, mwambie ndugu yangu tugawane naye urithi wetu."

14Lakini Yesu akamwambia, "Rafiki, ni nani aliyeniweka Mimi kuwa hakimu wenu au
msuluhishi juu yenu?" 15Ndipo Yesu akawaambia, "Jihadharini! Jilindeni na aina zote za choyo. Kwa maana maisha ya mtu

hayatokani na wingi wa mali alizo nazo.”

16 Kisha akawaambia mfano huu: “Shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana. 17 Akawaza moyoni mwake, ‘Nifanye nini? Sina mahali pa kuhifadhi mavuno yangu.’

18 “Ndipo huyo tajiri akasema, ‘Nitafanya hivi: Nitabomoa ghala zangu za nafaka na kujenga nyingine kubwa zaidi na huko nitayahifadhi mavuno yangu yote na vitu vyangu. 19 Nami nitaiambia nafsi yangu, ‘Nafsi, unavyo vitu vingi vizuri ulivyojiwekea miaka mingi. Pumzika, ule, unywe, ufurahi.’ ”

20 “Lakini Mungu akamwambia, ‘Mpumbavu wewe! Usiku huu huu uhai wako unatakiwa. Sasa hivyo vitu ulivyojiwekea akiba vitakuwa vya nani?’

21 “Hivyo ndivyo ilivyo kwa wale wanaojiwekea vitu lakini hawajitajirishi kwa Mungu.’’

### *Msiwe Na Wasiwasi*

22 Kisha Yesu akawaambia wanafunzi Wake: “Kwa hiyo ninawaambia, msisumbukie maisha yenu, kwamba mtakula nini, au miili yenu kwamba mtavaa nini. 23 Maisha ni zaidi ya chakula na mwili ni zaidi ya mavazi. 24 Fikirini ndege! Wao hawapandi wala hawavuni, hawana ghala wala po pote pa kuhifadhi nafaka, lakini Mungu huwalisha. Ninyi ni bora kuliko ndege! 25 Ni nani miongoni mwenu ambaye kwa kusumbuka anaweza kujiongeza maisha yake hata kwa saa moja? 26 Kama hamwezi kufanya jambo dogo kama hilo, kwa nini basi kuyasumbukia hayo mengine?

27 “Angalieni maua jinsi yameavyo: Hayafumi wala hayasokoti, lakini ninawaambia, hata Solomoni katika fahari yake yote, hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya hayo. 28 Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya shambani ambayo leo yapo kesho yanatupwa motoni, si zaidi sana atawavika ninyi enyi wa imani haba! 29 Wala msisumbuke mioyoni mwenu mtakula nini au mtakunywa nini. Msiwe na wasiwasi juu ya haya. 30 Watu wasiomjua Mungu husumbuka sana kuhusu vitu hivi vyote. Naye Baba yenu wa mbinguni anajua kuwa mnavihitaji. 31 Bali utafuteni Ufalme wa Mungu na vitu hivyo vyote atawapatia pia.

### *Utajiri Wa Mbinguni*

32 “Msiogope enyi kundi dogo, kwa maana Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi Ufalme. 33 Uzeni mali zenu mkawape maskini. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, mkajiwekee hazina mbinguni isiyokwisha, mahali ambapo mwivi hakaribii wala nondo haharibu. 34 Kwa maana hazina yako ilipo, ndipo na moyo wako utakapokuwa pia.

### *Kukesha*

35 “Iweni tayari mkiwa mmevikwa kwa ajili ya huduma na taa zenu zikiwa zinawaka, 36 kama watumishi wanaomngojea bwana wao arudi kutoka kewnye karamu ya arusini, ili ajapo na kugonga mlango waweze kumfungulia mara. 37 Heri wale watumishi ambao bwana wao atakapokuja atawakuta wakiwa wanakesha. Amin, nawaambia, atajifunga mkanda wake na kuwaketisha ili wale, naye atakuja na kuwahudumia. 38 Itakuwa heri kwa watumwa hao ikiwa bwana wao atakapokuja atawakuta wamekesha hata kama atakuja mnamo usiku wa manane, au karibu na mapambazuko. 39 Lakini fahamuni jambo hili kwamba: Kama mwenye nyumba angalijua ni saa ipi mwivi atakapo kuja, asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. 40 Ninyi nanyi imewapasa kuwa tayari saa zote, kwa maana Mwana wa Adamu atakuja saa ambayo hamumtarajii.”

### *Mtumishi Mwaminifu Na Asiye Mwaminifu*

41 Ndipo Petro akamwuliza, “Bwana, mfano huu unatuambia sisi peke yetu au watu wote?”

42 Yesu akamjibu, “Ni yupi basi wakili mwaminifu na mwenye busara ambaye bwana wake atamfanya msimamizi juu ya nyumba yake yote, naye awape watumishi wengine chakula chao wakati unaofaa? 43 Itakuwa ni furaha kwa mtumishi yule ambaye bwana wake atakaporudi atamkuta akifanya hivyo. 44 Amin nawaambia, atampa mamlaka juu ya vyote alivyo navyo. 45 Lakini ikiwa yule mtumishi atawaza moyoni mwake, ‘Bwana wangu anakawia kurudi,’ akaanza kuwapiga wale watumishi wa kiume na wa kike na kula na kunywa na kulewa, 46 bwana wake yule mtumwa atakuja siku asiyodhani, na saa asiyoijua. Huyo bwana wake atamkata vipande vipande na kumwekea fungu lake pamoja na wale wasio waaminifu.

47 “Yule mtumishi anayefahamu vema mapenzi ya bwana wake na asijiandae wala kufanya kama apendavyo bwana wake, atapigwa kwa mapigo mengi. 48 Lakini ye yote ambaye hakujua laini akafanya yale yastahilio kupigwa atapigwa kidogo.Ye yote aliyepewa vitu vingi, atadaiwa vingi na ye yote aliyekabidhiwa

vingi kwake vitatakiwa vingi.

### *Sikuleta Amani Bali Mafarakano*

49“Nimekuja kuleta moto duniani, laiti kama
ungekuwa tayari umewashwa! 50Lakini ninao
ubatizo ambao lazima nibatizwe, nayo dhiki
Yangu ni kuu mpaka ubatizo huo ukamilike!
51Mnadhani nimekuja kuleta amani duniani? La,
nawaamba sivyo, nimekuja kuleta mafarakano.
52Kuanzia sasa, kutakuwa na watu watano
katika nyumba moja, watatu dhidi ya wawili na
wawili dhidi ya watatu. 53Watafarakana baba
dhidi ya mwanawe na mwana dhidi ya babaye,
mama dhidi ya bintiye na binti dhidi ya mamaye,
mama mkwe dhidi ya mkwewe. Naye mkwe
dhidi ya mama mkwe wake.”

### *Kutambua Majira*

54Pia Yesu akauambia ule umati wa watu,
“Mwonapo wingu likitokea magharibi, mara
mwasema, ‘Mvua itanyesha,’ nayo hunyesha.
55Nanyi mwonapo upepo wa kusini ukivuma,
ninyi husema, ‘Kutakuwa na joto’ na huwa hivyo.
56Enyi wanafiki! Mnajua jinsi ya kutambua
kuonekana kwa dunia na anga. Inakuwaje basi
kwamba mnashindwa kutambua wakati huu wa
sasa?
57“Kwa nini hamwamui wenyewe lililo haki?
58Uwapo njiani na adui yako kwenda kwa
hakimu, jitahidi kupatana naye mkiwa njiani. La
sivyo, atakupeleka kwa hakimu, naye hakimu
atakukabidhi kwa afisa, naye afisa atakutupa
gerezani. 59Nawaambia, hautatoka humo hadi
ulipe senti ya mwisho.’’

### *Tubu La Sivyo Utaangamia.*

**13** Wakati huo huo, kulikuwa na watu
waliomwambia Yesu habari za Wagalilaya
ambao Pilato aliwaua na damu ya hao watu
akaichanganya na dhabihu yao waliyokuwa
wanatoa 2 Yesu akawauliza, “Mnadhani
kwamba hawa Wagalilaya ambao walikufa kifo
cha namna hiyo wao walikuwa na dhambi
kuwazidi Wagalilaya wengine wote? 3La hasha!
Ninyi nanyi msipotubu, mtaangamia vivyo
hivyo. 4Au wale watu kumi na wanane waliokufa
walipoangukiwa na mnara huko Siloamu,
mnadhani wao walikuwa waovu kuliko watu
wote waliokuwa wanaishi Yerusalemu?
5Nawaambia, la hasha! Ninyi nanyi msipotubu,
wote mtaangamia vivyo hivyo.”

### *Mfano Wa Mti Usiozaa Matunda*

6Kisha Yesu akawaambia mfano huu: “Mtu
mmoja alikuwa na mtini uliopandwa katika
shamba lake la mizabibu, akaja ili kutafuta tini
kwenye mti huo, lakini hakupata hata moja.
7Hivyo akamwambia mtunza shamba: ‘Tazama,
kwa muda wa miaka mitatu sasa nimekuwa
nikija kutafuta matunda kwenye mtini huu, nami
sikupata hata moja. Ukate! Kwa nini uendelee
kuharibu ardhi?’
8Yule mtunza shamba akamjibu, “ ‘Bwana,
uache tena kwa mwaka mmoja zaidi, nami
nitaupalilia na kuuwekea mbolea. 9Kama ukizaa
matunda mwaka ujao, vema, la sivyo ukate.’ ”

### *Yesu Amponya Mwanamke Kilema Siku Ya Sabato*

10Basi Yesu alikuwa akifundisha katika
sinagogi mojawapo siku ya Sabato. 11Wakati uo
huo akaja mwanamke mmoja aliyekuwa na pepo
mchafu, naye alikuwa amepinda mgongo kwa
muda wa miaka kumi na minane, wala alikuwa
hawezi kunyoka wima. 12Yesu alipomwona,
akamwita akamwambia, “Mwanamke, uwe huru,
umepona ugonjwa wako.” 13Yesu alipomwekea
mikono Yake, mara akasimama wima akaanza
kumtukuza Mungu.
14Lakini mkuu wa sinagogi, akakasirika kwa
sababu Yesu alikuwa ameponya mtu siku ya
Sabato. Kwa hiyo mkuu wa sinagogi
akaendelea kuuambia ule umati wa watu, “Kuna
siku sita ambazo watu wanapaswa kufanya
kazi, katika siku hizo, njoni mponywe, lakini si
kuja kuponywa siku ya Sabato.”
15Lakini Bwana akamjibu, “Enyi wanafiki!
Je, kila mmoja wenu humfungulii ng’ombe wake
au punda wake kutoka zizini akampeleka
kumnywesha maji siku ya Sabato? 16Je, huyu
mwanamke, ambaye ni binti wa Abrahamu,
aliyeteswa na Shetani akiwa amemfunga kwa
miaka yote hii kumi na minane, hakustahili
kufunguliwa kutoka katika kifungo hicho siku ya
Sabato?”
17Aliposema haya, wapinzani Wake
wakaaibika, lakini watu wakafurahi kwa ajili ya
mambo ya ajabu aliyoyafanya.

### *Mfano Wa Punje Ya Haradali*

18Kisha Yesu akauliza, “Ufalme wa Mungu
unafanana na nini? Nitaufananisha na nini?
19Umefanana na punje ya haradali ambayo ni
ndogo sana, ambayo mtu aliichukua na
kuipanda katika shamba lake. Nayo ikakua,
ikawa mti na ndege wa angani wakatengeneza

viota vyao kwenye matawi yake.”

### *Mfano Wa Chachu*

20Yesu akauliza tena, “Nitaufananisha
Ufalme wa Mungu na nini? Unafanana na
chachu ambayo mwanamke aliichukua na
kuichanganya kwenye vipimo vitatu vya unga
hadi wote ukawa umeumuka.”

### *Mlango Mwembamba*

22Yesu akapita katika miji na vijiji
akifundisha wakati akisafiri kwenda Yerusalemu.
23Mtu mmoja akamwuliza, “Bwana, ni watu
wachache tu watakaookolewa?”

24Yesu akawaambia, “Jitahidini kuingia kwa
kupitia mlango mwembamba, kwa maana,
nawaambia, wengi watajaribu kuingia lakini
hawataweza. 25Wakati mwenye nyumba
atakapoondoka na kufunga mlango, mtasimama
nje mkigonga mlango na kusema, ‘Bwana,
utufungulie mlango.’

“Lakini yeye atawajibu, ‘Siwajua ninyi wala
mtokako.’

26“Ndipo mtamjibu, ‘Tulikula na kunywa
pamoja nawe, tena ulifundisha katika barabara
zetu.’

27“Lakini Yeye atawajibu, ‘Siwajui ninyi wala
mtokako. Ondokeni kwangu ninyi watenda
maovu!’

28“Ndipo kutakuwako kilio na kusaga meno,
mtakapomwona Abrahamu, Isaki na Yakobo na
manabii wote wakiwa katika Ufalme wa Mungu,
lakini ninyi mkiwa mmetupwa nje. 29Watu
watakuja kutoka mashariki na magharibi,
kaskazini na kusini, nao wataketi kwenye
sehemu walizoandaliwa karamuni katika Ufalme
wa Mungu. 30Tazama wako walio wa mwiho
watakaokuwa wa kwanza, nao wa kwanza
watakaokuwa wa mwsho.”

### *Yesu Aomboleza Kwa Ajili Ya Yerusalemu*

31Wakati huo huo baadhi ya Mafarisayo
wakamwendea Yesu na kumwambia, “Ondoka
hapa uende mahali pengine kwa maana Herode
anataka kukuua.”

32Yesu akawajibu, “Nendeni mkamwambie
yule mbweha, ‘Ninafukuza pepo wachafu na
kuponya wagonjwa leo na kesho, nami siku ya
tatu nitaikamilisha kazi Yangu. 33Sina budi
kuendelea na safari yangu leo, kesho na kesho
kutwa, kwa maana haiwezekani nabii kufa
mahali pengine isipokuwa Yerusalemu.

34“Ewe Yerusalemu, Yerusalemu, wewe
uwauaye manabii na kuwapiga mawe wale
waliotumwa kwako! Mara ngapi nimetamani
kuwakusanya watoto wako pamoja kama kuku
akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa
zake, lakini hamkutaka! 35Tazama nyumba yenu
inaachwa ukiwa, ninawaambia hamtaniona tena
mpaka wakati ule mtakaposema, “Amebarikiwa
Yeye ajaye katika Jina la Bwana.’ ”

### *Yesu Nyumbani Mwa Farisayo*

**14** Ikawa siku moja Yesu alipokuwa
amekwenda kula chakula kwa mmoja wa viongozi
wa Mafarisayo siku ya Sabato, watu walikuwa
wakimchunguza kwa bidii. 2Papo hapo mbele Yake
palikuwa na mtu mmoja mwenye ugonjwa wa
kuvimba mwili. 3Yesu akawauliza wale Mafarisayo
na walimu wa sheria, “Je, ni halali kuponya watu
siku ya Sabato au la?” 4Wakakaa kimya. Hivyo
Yesu akamshika yule mgonjwa mkono na
kumponya, akamruhusu
aende zake.

5Kisha akawauliza, “Kama mmoja wenu
angekuwa na mtoto au ng’ombe wake
aliyetumbukia katika kisima siku ya Sabato, je,
hamtamvuta mara moja na kumtoa?” 6Nao
hawakuwa na la kusema.

### *Unyenyekevu Na Ukarimu*

7Alipoona jinsi wageni walivyokuwa
wanachagua mahali pa heshima wakati wa kula,
akawaambia mfano huu: 8“Mtu akikualika
arusini, usikae mahali pa mgeni wa heshima
kwa kuwa inawezekana amealikwa mtu
mheshimiwa kuliko wewe. 9Kama mkifanya
hivyo yule aliyewaalika ninyi wawili atakuja na
kukuambia, ‘Mpishe huyu mtu kiti chako.’ Ndipo
kwa aibu utalazimika kukaa katika nafasi ya
chini kabisa. 10 Badala yake, unapoalikwa,
chagua nafasi ya chini, ili yule mwenyeji wako
atakapokuona atakuja na kukuambia, ‘Rafiki
yangu, nenda kwenye nafasi iliyo bora zaidi.’
Kwa jinsi hii utakuwa umepewa heshima mbele
ya wageni wenzako wote. 11Kwa maana kila
mtu ajikwezaye atashushwa, naye ajishushaye
atakwezwa.”

12Kisha Yesu akamwambia yule
aliyewaalika, “Uandaapo karamu ya chakula
cha mchana au cha jioni, usialike rafiki zako au
ndugu zako au jamaa zako au majirani zako
walio matajiri tu, ukifanya hivyo, wao nao
wanaweza kukualika kwao, nawe ukawa
umelipwa kile ulichofanya na kupata thawabu
yako. 13Bali ufanyapo karamu, waalike maskini,

vilema na vipofu, 14nawe utabarikiwa kwa
sababu hawa hawana uwezo wa kukulipa.
Mungu atakulipa wakati wa ufufuo wa wenye
haki."

### *Mfano Wa Karamu Kuu*

15Mmoja wa wale waliokuwa pamoja naye
mezani aliposikia hivi akamwambia Yesu,
"Amebarikiwa mtu yule atakayekula katika
karamu ya Ufalme wa Mungu!"

16Yesu akamjibu, "Mtu mmoja alikuwa
anaandaa karamu kubwa, akaalika watu wengi.
17Wakati wa karamu ulipofika akamtuma
mtumishi wake akawaambie wale walioalikwa,
'Karibuni, kila kitu ni tayari sasa.'

18"Lakini wote, kila mmoja, wakaanza kutoa
udhuru: Wa kwanza akasema, 'Nimenunua
shamba, lazima niende kuliona. Tafadhali niwie
radhi.'

19"Mwingine akasema, 'Ndipo tu nimenunua
jozi tano za ng'ombe wa kulimia, nami
ninakwenda kuwajaribu, tafadhali niwie radhi.'
20Naye mwingine akasema, 'Nimeoa mke, kwa
hiyo siwezi kuja.'

21 "Yule mtumishi akarudi, akampa bwana
wake taarifa. Ndipo yule mwenye nyumba
akakasirika, akamwagiza yule mtumishi wake
akisema, 'Nenda upesi kwenye mitaa na
vichochoro vya mjini uwalete maskini, vilema,
vipofu na viwete.'

22"Yule mtumishi akamwambia, 'Bwana,
yale uliyoniagiza nimefanya, lakini bado ipo
nafasi'

23"Ndipo yule bwana akamwambia mtumishi
wake, 'Nenda kwenye barabara na vijia vilivyoko
nje ya mji na uwalazimishe watu waingie ili
nyumba yangu ipate kujaa. 24Kwa maana
nawaambia, hakuna hata mmoja wa wale
walioalikwa atakayeionja karamu yangu.' "

### *Gharama Ya Kuwa Mwanafunzi*

25Umati mkubwa wa watu ulikuwa ukisafiri
pamoja na Yesu, naye akageuka, akawaambia,
26"Mtu ye yote anayekuja kwangu hawezi kuwa
mwanafunzi wangu kama hatanipenda mimi
zaidi ya baba yake na mama yake, mke wake
na watoto, ndugu zake na dada zake, naam,
hata maisha yake mwenyewe. 27Ye yote
asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata
hawezi kuwa mwanafunzi wangu.

28"Ni nani miongoni mwenu ambaye kama
anataka kujenga nyumba, hakai kwanza chini na
kufanya makisio ya gharama aone kama ana
fedha za kutosha kukamilisha? 29La sivyo,
akiisha kuweka msingi naye akiwa hana uwezo
wa kuikamilisha, wote waionao wataanza
kumdhihaki, 30Wakisema, 'Mtu huyu alianza
kujenga lakini hakuweza kukamilisha.'

31"Au ni mfalme gani atokaye kwenda
kupigana vita na mfalme mwingine, ambaye
hakai chini kwanza na kufikiri iwapo akiwa na
jeshi la watu elfu kumi ataweza kupigana na
yule anayekuja na jeshi la watu elfu ishirini?
32Kama hawezi, basi wakati yule mwingine
akiwa bado yuko mbali, yeye hutuma ujumbe
wa watu na kuomba masharti ya amani. 33Vivyo
hivyo, ye yote miongoni mwenu ambaye hawezi
kuacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa
mwanafunzi Wangu.

### *Chumvi Isiyofaa*

34"Chumvi ni kitu kizuri, lakini chumvi ikiwa
imepoteza ladha yake, inawezaje kurudishiwa
tena ladha yake? 35Haifai ardhi wala kwa lundo
la mbolea, bali hutupwa nje.

"Mwenye masikio ya kusikia na asikie."

### *Mfano Wa Kondoo Aliyepotea*

**15** Basi watoza ushuru na wenye dhambi wote
walikuwa wanakusanyika ili wapate kumsikiliza
Yesu. 2Lakini Mafarisayo na
walimu wa sheria wakanung'unika wakisema,
"Huyu mtu anawakaribisha wenye dhambi na
kula nao."

3Ndipo Yesu akawaambia mfano huu:
4"Ikiwa mmoja wenu ana kondoo mia moja naye
akapoteza mmoja wao, je, hawaachi wale tisini
na tisa nyikani na kwenda kumtafuta huyo
aliyepotea mpaka ampate? 5Naye akiisha
kumpata, kwa furaha humbeba mabegani
mwake 6na kwenda nyumbani. Kisha huwaita
rafiki zake na majirani na kuwaambia, 'Furahini
pamoja nami, nimempata kondoo wangu
aliyepotea.' 7Nawaambieni, vivyo hivyo
kutakuwa na furaha zaidi mbinguni kwa sababu
ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa
wenye haki tisini na tisa ambao hawana haja ya
kutubu."

### *Mfano Wa Sarafu Iliyopotea*

8"Au ikiwa mwanamke ana sarafu za fedha
kumi, naye akapoteza moja, je, hawashi taa na
kufagia nyumba na kuitafuta kwa bidii mpaka
aipate? 9 Naye akisha kuipata, huwaita rafiki
zake na majirani na kuwaambia, 'Furahini
pamoja nami, nimeipata ile sarafu yangu ya

fedha iliyopotea.’ 10Vivyo hivyo, nawaambia,
kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu juu ya
mwenye dhambi mmoja atubuye.”

### *Mfano Wa Mwana Mpotevu*

11Yesu akaendelea kusema: “Kulikuwa na
mtu mmoja aliyekuwa na wana wawili. 12Yule
mdogo akamwambia baba yake, ‘Baba, nipe
urithi wangu.’ Hivyo akawagawia wanawe mali
yake.

13“Baada ya muda mfupi, yule mdogo
akakusanya vitu vyote alivyokwa navyo,
akaenda nchi ya mbali na huko akaitapanya
mali yake kwa maisha ya anasa. 14Baada ya
kutumia kila kitu alichokuwa nacho, kukawa na
njaa kali katika nchi ile yote, naye akawa hana
cho chote. 15Kwa hiyo akaenda akaajiriwa na
mwenyeji mmoja wa nchi ile ambaye alimpeleka
shambani kwake kulisha nguruwe. 16Akatamani
kujishibisha kwa maganda waliyokula wale
nguruwe, wala hakuna mtu aliyempa cho chote.

17“Lakini alipozingatia moyoni mwake,
akasema, ‘Ni watumishi wangapi walioajiriwa na
baba yangu ambao wana chakula cha
kuwatosha na kusaza, bali mimi hapa nakufa
kwa njaa! 18Nitaondoka na kurudi kwa baba
yangu na kumwambia, ‘Baba, nimetenda
dhambi mbele za Mungu na mbele yako.
19Sistahili tena kuitwa mwanao, nifanye kama
mmoja wa watumishi wako.’ 20Basi akaondoka,
akaenda kwa baba yake.

“Lakini alipokuwa bado yuko mbali, baba yake akamwona, moyo wake ukajawa na huruma. Akamkimbilia mwanawe, akamkumbatia na kumbusu.

21“Yule mtoto akamwambia baba yake, ‘Baba, nimekosa mbele za Mungu na mbele yako. Sistahili kuitwa mwanao tena.’

22“Lakini baba yake akawaambia watumishi,
‘Leteni upesi joho lililo bora sana, mkamvike
pete kidoleni mwake na viatu miguuni mwake.
23Leteni ndama aliyenona, mkamchinje ili tuwe
na karamu, tule na kufurahi. 24Kwa maana huyu
mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai
tena, alikuwa amepotea na sasa amepatikana!’
Nao wakaanza kufanya tafrija.

25“Wakati huo, yule mwana mkubwa alikuwa
shambani. Alipokaribia nyumbani, akasikia sauti
ya nyimbo na watu wakicheza. 26Akamwita mmoja
wa watumishi na kumwuliza, ‘Kuna nini?’
27Akamwambia, ‘Mdogo wako amekuja, naye
baba yako amemchinja ndama aliyenona kwa
sababu mwanawe amerudi nyumbani akiwa
salama na mzima.’

28Yule mwana mkubwa akakasirika,
akakataa kuingia ndani. Basi baba yake akatoka
nje na kumbembeleza. 29 Lakini yeye akamjibu
baba yake, ‘Tazama! Miaka yote hii
nimekutumikia na hata siku moja sijaacha kutii
amri zako, lakini hujanipa hata mwana mbuzi ili
nifurahi na rafiki zangu. 30Lakini huyu mwanao
ambaye ametapanya mali yako kwa makahaba
aliporudi nyumbani, wewe umemchinjia ndama
aliyenona!’

31“Baba yake akamjibu, “ ‘Mwanangu,
umekuwa nami sikuzote na vyote nilivyo navyo
ni vyako. 32Lakini ilitubidi tufurahi na kushangilia
kwa sababu huyu mdogo wako alikuwa
amekufa na sasa yu hai, alikuwa amepotea
naye amepatikana.’ ”

### *Mfano Wa Msimamizi Mjanja*

**16** Yesu akawaambia wanafunzi Wake, “Palikuwa
na tajiri mmoja na msimamizi wake. Ilisemekana
kwamba huyo msimamizi
alikuwa anatumia vibaya mali ya tajiri yake.
2Hivyo huyo tajiri akamwita na kumwuliza, ‘Ni
mambo gani haya ninayoyasikia kukuhusu? Toa
taarifa ya usimamizi wako, kwa sababu huwezi
kuendelea kuwa msimamizi.’

3“Yule msimamizi akawaza moyoni mwake,
‘Nitafanya nini sasa? Bwana wangu ananiondoa
katika kazi yangu. Sina nguvu za kulima, nami
ninaona aibu kuombaomba. 4Najua
nitakalofanya ili nikiachishwa kazi yangu hapa,
watu wanikaribishe nyumbani kwao.’

5“Kwa hiyo akawaita wadeni wote wa bwana wake, mmoja mmoja. Akamwuliza wa kwanza, ‘Deni lako kwa bwana wangu ni kiasi gani?’

6“Akajibu, ‘Galoni 500[a] za mafuta ya mizeituni.’

“Msimamizi akamwambia, ‘Chukua hati ya deni lako, ibadilishe upesi, uandike galoni 400.’

7“Kisha akamwuliza wa pili, ‘Wewe deni lako ni kiasi gani?’

“Akajibu, ‘Vipimo mia moja[b] vya ngano.’ “Yule msimamizi akamwambia, ‘Chukua hati yako, andika vipimo themanini!’

8“Yule bwana akamsifu yule msimamizi kwa jinsi alivyotumia ujanja. Kwa maana watu wa dunia hii wana ujanja zaidi wanapojishughulisha na mambo ya dunia kuliko watu wa nuru.

a6 Galoni 500 hapa ni sawa na lita 2,500.Galoni moja ni kama lita 5

b7 Vipimo 100 ni kama magunia 100

9Nawaambia tumieni mali ya dunia kujipatia
marafiki, ili itakapokwisha mkaribishwe katika
makao ya milele.

10"Ye yote aliye mwaminifu katika mambo
madogo, pia ni mwaminifu hata katika mambo
makubwa, naye mtu ambaye si mwaminifu
katika mambo madogo pia si mwaminifu katika
mambo makubwa. 11Ikiwa hamkuwa waaminifu
katika mali ya udhalimu, ni nani
atakayewaaminia mali ya kweli? 12Nanyi kama
hamkuwa waaminifu na mali ya mtu mwingine,
ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?

13"Hakuna mtumishi awezaye kuwatumikia
mabwana wawili. Ama atamchukia mmoja na
kumpenda mwingine au atamheshimu mmoja na
kumdharau mwingine. Hamwezi kumtumikia
Mungu pamoja na mali[a]."

14Mafarisayo, ambao walikuwa wapenda
fedha, waliyasikia hayo yote na wakamcheka
kwa dharau. 15 Yesu akawaambia, "Ninyi
mnajifanya kuwa wenye haki mbele za
wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu.
Kwa maana vile vitu ambavyo wanadamu
wanavithamini sana, kwa Mungu ni machukizo.

### *Sheria Na Ufalme Wa Mungu*

16"Torati na manabii vilitumiwa mpaka kuja
kwa Yohana Mbatizaji. Tangu wakati huo habari
njema za Ufalme wa Mungu zinahubiriwa na kila
mmoja hujiingiza kwa nguvu. 17Lakini ni rahisi
zaidi mbingu na nchi kupita kuliko hata herufi
moja kuondoka katika Sheria.

18"Mtu ye yote ampaye mkewe talaka na
kumwoa mwanamke mwingine azini, naye
mwanaume amwoaye mwanamke aliyetalikiwa
azini.

### *Tajiri Na Lazaro*

19"Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyevaa
nguo za rangi ya zambarau na kitani safi,
ambaye aliishi kwa anasa, kila siku. 20Hapo
penye mlango wake aliishi maskini mmoja, jina
lake Lazaro, mwenye vidonda mwili mzima.
21Huyo Lazaro alitamani kujishibisha kwa
makombo yaliyoanguka kutoka mezani kwa yule
tajiri. Hata mbwa walikuwa wakija na kulamba
vidonda vyake.

22"Wakati ukafika yule maskini akafa, nao
malaika wakamchukua akae pamoja na
Abrahamu. Yule tajiri naye akafa na akazikwa.

23Kule kuzimu alipokuwa akiteseka, alitazama
juu, akamwona Abrahamu kwa mbali, naye
Lazaro alikuwa karibu yake. 24Hivyo yule tajiri
akamwita, 'Baba Abrahamu, nihurumie na
umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake
ndani ya maji aupoze ulimi wangu, kwa sababu
nina maumivu makuu kwenye moto huu.'

25"Lakini Abrahamu akamjibu, 'Mwanangu,
kumbuka kwamba wakati wa uhai wako ulipata
mambo mazuri, lakini Lazaro alipata mambo
mabaya. Lakini sasa anafarijiwa hapa na wewe
uko katika maumivu makuu. 26Zaidi ya hayo kati
yetu na ninyi huko, kumewekwa shimo kubwa,
ili wale wanaotaka kutoka huku kuja huko
wasiweze, wala mtu ye yote asiweze kuvuka
kutoka huko kuja kwetu.'

27"Akasema, 'Basi, nakuomba, umtume
Lazaro aende nyumbani kwa baba yangu,
28maana ninao ndugu watano. Awaonye, ili
wasije nao wakafika mahali hapa pa mateso.

29 "Abrahamu akamjibu, 'Ndugu zako wana
Mose na Manabii, wawasikilize hao.'

30" 'Yule tajiri akasema, 'Hapana, baba
Abrahamu, lakini mtu kutoka kwa wafu
akiwaendea, watatubu.'

31"Abrahamu akamwambia, 'Kama
wasipowasikiliza Mose na manabii, hawataweza
kushawishiwa hata kama atafufuka mtu kutoka
kwa wafu.' "

### *Yesu Afundisha Kuhusu Majaribu, Dhambi Na Imani*

17 Yesu akawaambia wanafunzi Wake,
"Mambo yasababishayo watu watende dhambi
hayana budi kutukia. Lakini ole wake mtu yule
anayeyasababisha. 2Ingekuwa heri kama mtu
huyo angefungiwa jiwe zito la kusagia shingoni na
kutoswa baharini kuliko kumfanya mmoja wa hawa
wadogo atende dhambi. 3Kwa
hiyo, jilindeni.

"Kama ndugu yako akikukosea mwonye,
naye akitubu, msamehe. 4Kama akikukosea
mara saba kwa siku moja na mara saba kwa
siku moja akaja kwako akisema, 'Ninatubu',
msamehe."

### *Imani*

5Wanafunzi Wake wakamwambia Bwana,
"Tuongezee imani."

6Yesu akawajibu, "Kama mngekuwa na
imani ndogo kama punje ya haradali,
mngeweza kuuambia mti huu wa mkuyu,
'Ng'oka ukaote baharini,' Nao ungewatii.

[a] 13 Neno "Mali" hapa ni neno linalotokana na neno la Kiyunani *"mammon"* linalotokana na Kiaramu, '*mamon, mamona*,' yaani, 'mali, utajiri.'

### *Wajibu Wa Mtumishi*

7“Ikiwa mmoja wenu ana mtumishi anayelima shambani au anayechunga kondoo, je, mtumishi huyo arudipo atamwambia, ‘Karibu hapa keti ule chakula?’ 8Je, badala yake, hutamwambia, ‘Niandalie chakula, nile, jifunge unitumikie ninapokula na kunywa, baadaye waweza kula na kunywa?’ 9Je, huyo mtu utamshukuru mtumishi huyo kwa kutimiza yale aliyoamriwa? 10Vivyo hivyo nanyi mkiisha kufanya mliyoagizwa, semeni, ‘Sisi tu watumishi tusiostahili, tumefanya tu yale tuliyopaswa kufanya.’ ”

### *Yesu Atakasa Wakoma Kumi*

11Yesu alipokuwa njiani akienda Yerusalemu, alipitia mpakani mwa Samaria na Galilaya. 12Alipokuwa akiingia kwenye kijiji kimoja, watu kumi waliokuwa na ukoma wakakutana naye. Wakasimama mbali, 13wakapaza sauti, wakasema, “Yesu, Bwana, tuhurumie!’’

14Alipowaona akawaambia, “Nendeni mkajionyeshe kwa makuhani.” Nao walipokuwa njiani wakienda, wakatakasika.

15Mmoja wao alipoona kwamba amepona, akarudi kwa Yesu, akimsifu Mungu kwa sauti kuu. 16Akajitupa miguuni mwa Yesu akamshukuru. Yeye alikuwa Msamaria.

17Yesu akauliza, “Je,hawakuponywa wote kumi? Wako wapi wale wengine tisa? 18Hakuna hata mmoja aliyeonekana kurudi ili kumshukuru Mungu isipokuwa huyu mgeni?” 19 Yesu akamwambia, “Inuka na uende zako, imani yako imekuponya.”

### *Kuja Kwa Ufalme Wa Mungu*

20Yesu alipoulizwa na Mafarisayo Ufalme wa Mungu utakuja lini, Yeye akawajibu, “Ufalme wa Mungu hauji kwa kuchunguza kwa bidii, 21wala watu hawatasema, ‘Huu hapa’ au ‘Ule kule,’ kwa maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu.”

22Kisha Yesu akawaambia wanafunzi Wake, “Wakati utafika ambapo mtatamani kuiona moja ya siku ya Mwana wa Adamu, lakini hamtaiona. 23Watu watawaambia, ‘Yule kule!’ Au, ‘Huyu hapa!’ Msiwakimbilie. 24Kwa maana Mwana wa Adamu katika siku Yake atakuwa kama umeme wa radi, umulikao katika anga kuanzia mwisho mmoja hadi mwingine. 25Lakini kwanza itampasa kuteseka katika mambo mengi na kukataliwa na kizazi hiki.

26“Kama ilivyokuwa siku za Noa, ndivyo itakavyokuwa katika siku za Mwana wa Adamu. 27Wakati huo wa Noa watu walikuwa wakila, wakinywa, wakioa na kuolewa mpaka siku ile Noa alipoingia katika safina, gharika ikaja na kuwaangamiza wote.

28 “Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Lutu: Watu walikuwa wakila na kuinywa, wakinunua na kuuza, wakilima na kujenga. 29Lakini siku ile Lutu alipoondoka Sodoma, ikanyesha mvua ya moto na kiberiti kutoka mbinguni ukawaangamiza wote.

30“Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile Mwana wa Adamu atakapofunuliwa. 31Siku hiyo, mtu ye yote aliyeko kwenye dari ya nyumba yake, vitu vyake vikiwa ndani ya hiyo nyumba asishuke kuvichukua. Vivyo hivyo mtu aliyeko shambani asirudi nyumbani kuchukua cho chote. 32Mkumbukeni mke wa Lutu! 33 Mtu ye yote anayejaribu kuyaokoa maisha yake atayapoteza na ye yote atakayeyapoteza maisha yake atayaokoa. 34 Nawaambia, usiku huo watu wawili watakuwa wamelala kitanda kimoja, mmoja atachukuliwa, mwingine ataachwa. 35Wanawake wawili watakuwa wanasaga nafaka pamoja, mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa.” 36Wanaume wawili watakuwa wanafanya kazi pamoja shambani, mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa.”

37Kisha wakamwuliza, “Haya yatatukia wapi Bwana?”

Akawaambia, “Pale ulipo mzoga, ndipo tai watakapokusanyika.”

### *Mfano Wa Mjane Asiyekata Tamaa*

**18** Kisha Yesu akawapa wanafunzi W ake mfano ili kuwaonyesha kuwa yawapasa kuomba pasipo kukata tamaa. 2Akawaambia, “Katika mji mmoja alikuwapo hakimu ambaye hakumwogopa Mungu wala kumjali mtu. 3Katika mji huo alikuwako mjane mmoja ambaye alikuwa akija kwake mara kwa mara akimwomba, ‘Tafadhali nipatie haki kati yangu na adui yangu.’

4“Kwa muda mrefu yule hakimu alikataa. Lakini hatimaye akasema moyoni mwake, ‘Japokuwa simwogopi Mungu wala simjali mwanadamu, 5lakini kwa kuwa huyu mjane ananisumbuasumbua, nitahakikisha amepata haki yake ili asiendelee kunichosha kwa kunijia mara kwa mara!’ ”

6Bwana akasema, “Sikilizeni asemavyo

huyu hakimu dhalimu. 7Je, Mungu
hatawatendea haki wateule Wake wanaomlilia
mchana na usiku? Je, atakawia kuwasaidia?
8Ninawaambia, atawapatia haki upesi. Lakini je,
Mwana wa Adamu atakapokuja ataikuta imani
duniani?"

### *Mfano Wa Farisayo Na Mtoza Ushuru*

9Yesu akatoa mfano huu kwa wale
waliojiona kuwa wao ni wenye haki na
kuwadharau wengine. 10"Watu wawili
walikwenda hekaluni kusali, mmoja wao alikuwa
Farisayo na mwingine alikuwa mtoza ushuru.
11Yule Farisayo, akiwa amesimama peke yake,
akasali hivi: 'Mungu, ninakushukuru kwa sababu
mimi si kama watu wengine: Wanyang'anyi,
wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza
ushuru. 12Mimi nafunga mara mbili kwa juma,
natoa sehemu ya kumi ya mapato yangu.'

13"Lakini yule mtoza ushuru akasimama mbali, hakuthubutu hata kuinua uso wake kutazama mbinguni, bali alijipiga piga kifuani na kusema: 'Mungu, nihurumie, mimi mwenye dhambi.'

14"Nawaambia, huyu mtoza ushuru alirudi nyumbani akiwa amehesabiwa haki mbele za Mungu zaidi ya yule Farisayo. Kwa maana ye yote ajikwezaye atashushwa na ye yote ajishushaye atakwezwa."

### *Yesu Awabariki Watoto Wadogo*

15Watu walikuwa wakimletea Yesu pia
watoto wachanga ili awaguse. Wanafunzi Wake
walipoona hivyo, wakawakemea. 16Lakini Yesu
akawaita wale watoto waje kwake, akasema,
"Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala
msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa
watu walio kama hawa watoto. 17Amin,
nawaambia, ye yote ambaye hataupokea
Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo,
hatauingia kamwe."

### *Mtawala Tajiri*

18Mtawala mmoja akamwuliza Yesu, "Mwalimu mwema, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?"

19Yesu akamjibu, "Mbona unaniita mwema?
Hakuna mtu ye yote aliye mwema ila Mungu
peke Yake. 20Unazifahamu amri: 'Usizini, usiue,
usiibe, usishuhudie uongo, waheshimu baba
yako na mama yako.' "

21 Akajibu, "Amri zote hizi nimezishika tangu ujana wangu."

22Yesu aliposikia haya, akamwambia, "Bado kuna jambo moja ulilopungukiwa. Nenda ukauze kila kitu ulicho nacho, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate."

23Aliposikia jambo hili, alisikitika sana kwa
maana alikuwa mtu mwenye mali nyingi. 24
Yesu akamtazama akasema, "Tazama ni jinsi
gani ilivyo vigumu kwa tajiri kuingia katika
Ufalme wa Mungu! 25Hakika ni rahisi zaidi kwa
ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko
tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu."

26Wale waliosikia haya wakauliza, "Kama ni vigumu hivyo, ni nani basi awezaye kuokoka?"

27Yesu akajibu, "Yasiyowezekana kwa wanadamu kwa Mungu yawezekana."

28Ndipo Petro akasema, "Tazama, tumeacha vyote tulivyokuwanavyo tukakufuata!"

29Yesu akajibu, "Amin nawaambia, hakuna
hata mmoja aliyeacha nyumba yake, au mke,
au ndugu, au wazazi au watoto kwa ajili ya
Ufalme wa Mungu 30 ambaye hatapewa mara
nyingi zaidi ya hivyo katika maisha haya na
hatimaye kupata uzima wa milele ujao.''

### *Yesu Kwa Mara Ya Tatu Atabiri Kifo Chake*

31Yesu akawachukua wale wanafunzi Wake
kumi na wawili kando na kuwaambia,
"Tunapanda kwenda Yerusalemu na kila kitu
kilichoandikwa na manabii kumhusu Mwana wa
Adamu kitatimizwa. 32Kwa kuwa atatiwa
mikononi mwa watu wasiomjua Mungu, nao
watamdhihaki, watamtukana na kumtemea
mate, watampiga mijeledi na kumwua. 33Siku ya
tatu atafufuka."

34 Wanafunzi Wake hawakuelewa mambo haya, kwa kuwa maana yake ilikuwa imefichika kwao, nao hawakujua Yesu alikuwa anazungumzia nini.

### *Yesu Amponya Kipofu Karibu Na Yeriko*

35Yesu alipokuwa anakaribia Yeriko, kipofu
mmoja alikuwa ameketi kando ya njia akiomba
msaada. 36Kipofu huyo aliposikia umati wa watu
ukipita, akauliza, "Kuna nini?" 37Wakamwambia,
"Yesu wa Nazareti anapita."

38Akapaza sauti, akasema, "Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu!"

39Wale waliokuwa wametangulia mbele wakamkemea wakamwambia akae kimya. Lakini yeye akapaza sauti zaidi, "Mwana wa Daudi, unirehemu!"

40Yesu akasimama, akawaamuru huyo mtu
aletwe kwake. Alipokaribia, Yesu akamwuliza,
41“Unataka nikufanyie nini?”

Akajibu, “Bwana, nataka kuona.”

42 Yesu akamwambia, “Basi upate kuona,
imani yako imekuponya.” 43Akapata kuona saa
ile ile, akamfuata Yesu, huku akimsifu Mungu.
Watu wote walipoona mambo hayo, nao
wakamsifu Mungu.

### *Zakayo Mtoza Ushuru*

**19** Yesu akaingia Yeriko, naye alikuwa
anapita katikati ya huo mji. 2 Tazama, palikuwa
na mtu mmoja mkuu wa watoza ushuru naye
alikuwa tajiri, jina lake Zakayo. 3Yeye alikuwa
akijitahidi kumwona Yesu ni mtu wa namna
gani. Lakini kutokana na umati mkubwa wa
watu hakuweza kwa sababu alikuwa mfupi wa
kimo. 4Kwa hiyo akatangulia mbio mbele ya
umati wa watu akapanda juu ya mkuyu ili
amwone Yesu, kwa sababu angeipitia
njia ile.

5Yesu alipofika pale chini ya huo mkuyu,
akatazama juu, akamwambia, “Zakayo, shuka
upesi, kwa maana leo nitakuwa mgeni nyumbani
kwako!” 6Hivyo Zakayo akashuka upesi,
akamkaribisha Yesu nyumbani kwake kwa
furaha kubwa.

7Watu wote walioona, wakaanza
kunung’unika wakisema, “Amekwenda kuwa
mgeni wa ‘mtu mwenye dhambi.’ ”

8Lakini Zakayo akasimama na kumwambia
Bwana, “Tazama, Bwana! Sasa hivi nusu ya
mali yangu ninawapa maskini, nami kama
nimemdhulumu mtu ye yote kitu cho chote,
nitamrudishia mara nne ya hicho kiwango.”

9Ndipo Yesu akamwambia, “Leo, wokovu
umeingia nyumbani humu kwa sababu, huyo
naye, ni mwana wa Abrahamu. 10Kwa maana
Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa
kile kilichopotea.”

### *Mfano Wa Fedha*

11Walipokuwa wanasikiliza haya, Yesu
akaendelea kuwaambia mfano, kwa sababu
alikuwa anakaribia Yerusalemu na watu
walikuwa wakidhani ya kuwa Ufalme wa Mungu
ulikuwa unakuja saa iyo hiyo. 12Hivyo
akawaambia: “Mtu mmoja mwenye cheo
kikubwa, alisafiri kwenda nchi ya mbali ili
akapokee madaraka ya kuwa mfalme, kisha
arudi. 13Hivyo akawaita kumi miongoni mwa
watumishi wake akawapa kila mmoja fungu la
fedha. Akawaambia, ‘Fanyeni biashara na fedha
hizi mpaka nitakaporudi.’

14“Lakini raia wa nchi yake walimchukia
wakapeleka ujumbe na kusema, ‘Hatutaki huyu
mtu awe mfalme wetu.’

15“Hata hivyo alirudi akiwa amekwisha
kupokea mamalaka ya ufalme, akawaita wale
watumishi wake aliokuwa amewaachia fedha, ili
afahamu ni faida kiasi gani kila mmoja wao
aliyopata kwa kufanya biashiara.

16“Wa kwanza akaja na kusema, ‘Bwana,
kutokana na fedha uliyoniachia nimepata faida
mara kumi zaidi.’

17“Yule bwana akamjibu, ‘Umefanya vizuri
mtumishi mwema! Kwa sababu umekuwa
mwaminifu katika wajibu mdogo sana, nakupa
mamlaka juu ya miji kumi.’

18 “Wa pili naye akaja, akasema, ‘Bwana,
fedha yako imeleta faida mara tano zaidi.’

19“Bwana wake akajibu, ‘Nakupa mamlaka
juu ya miji mitano.’

20“Kisha akaja yule mtumishi mwingine
akasema, ‘Bwana, hii hapa fedha yako.
Niliitunza vizuri kwenye kitambaa.
21Nilikuogopa, kwa sababu wewe ni mtu
mgumu. Unachukua ambapo hukuweka kitu na
unavuna mahali ambapo hukupanda kitu.’

22“Bwana wake akamjibu, ‘Nitakuhukumu
kwa maneno yako mwenyewe, wewe mtumishi
mwovu! Kama ulifahamu kwamba mimi ni mtu
mgumu, nichukuaye mahali ambapo sikuweka
kitu na kuvuna mahali ambapo sikupanda,
23kwa nini basi hukuweka fedha zangu kwa
watoa riba ili nitakaporudi, nichukue iliyo yangu
na riba yake?’

24“Ndipo akawaambia wale waliokuwa
wamesimama karibu, ‘Mnyang’anyeni fungu
lake la fedha mkampe yule mwenye kumi.’

25“Wakamwambia, ‘Bwana, mbona tayari
anayo mafungu kumi?’

26“Akawajibu, ‘Nawaambia kwamba, kila
aliye na kitu, ataongezewa, naye yule
asiyetumia alicho nacho atanyang’anywa hata
kile alicho nacho, 27lakini wale adui zangu
ambao hawakutaka mimi niwe mfalme juu yao,
waleteni hapa mkawaue mbele yangu.’ ”

### *Yesu Aingia Yerusalemu Kwa Ushindi*

28Baada ya Yesu kusema haya, alitangulia
kupanda kwenda Yerusalemu. 29Naye alipokaribia
Bethfage na Bethania kwenye Mlima uitwao wa
Mizeituni, aliwatuma wanafunzi Wake wawili
akawaambia, 30“Nendeni katika

kijiji kile kilicho mbele yenu, mtakapokuwa mnaingia kijijini, mtamkuta mwana-punda ambaye hajapandwa na mtu bado, akiwa amefungwa hapo. Mfungueni, mumlete hapa. 31Kama mtu akiwauliza, 'Mbona mnamfungua?' Mwambieni, 'Bwana anamhitaji.' "

32Wale waliotumwa wakaenda, wakakuta kila kitu kama vile Yesu alivyokuwa amewaambia. 33Walipokuwa wanamfungua yule mwana-punda, wenyewe wakawauliza, "Mbona mnamfungua huyo mwana-punda?"

34Wale wanafunzi wakajibu, "Bwana anamhitaji."

35Wakamleta kwa Yesu, nao baada ya kutandika mavazi yao juu ya huyo mwana-punda, wakampandisha Yesu juu yake. 36Alipokuwa akienda akiwa amempanda, watu wakatandaza nguo zao barabarani.

37Alipokaribia mahali yanapoanzia matelemko ya Mlima wa Mizeituni, umati wote wa wafuasi Wake wakaanza kumsifu Mungu kwa furaha kwa sauti kuu kwa ajili ya matendo yote ya miujiza waliyoyaona.

38Wakasema:

"Amebarikiwa Mfalme ajaye kwa Jina la
Bwana!"

"Amani mbinguni na Utukufu Kwake
Aliye Juu."

39Baadhi ya Mafarisayo waliokuwemo miongoni mwa ule umati wa watu wakamwambia, "Mwalimu, waamuru wanafunzi Wako wanyamaze."

40 Yesu akawajibu, "Nawaambia ninyi, kama hawa wakinyamaza, mawe yatapiga kelele."

### *Yesu Anaulilia Mji Wa Yerusalemu*

41Alipokaribia Yerusalemu na kuuona mji, aliulilia, 42akisema, "Laiti ungalijua hata wewe leo yale ambayo yangeleta amani, lakini sasa yamefichika machoni pako. 43Hakika siku zinakujia, ambazo adui zako watakuzingira, watakuzunguka pande zote na kukuzuilia ndani. 44Watakuponda chini, wewe na watoto walioko ndani ya kuta zako. Nao hawataacha hata jiwe moja juu ya jingine, kwa sababu hukutambua wakati wa kujiliwa kwako."

### *Yesu Atakasa Hekaluni*

45Ndipo akaingia hekaluni akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza vitu humo. 46Naye akaawaambia, "Imeandikwa, 'Nyumba Yangu itakuwa nyumba ya sala, lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.' "

47Kila siku alikuwa akifundisha hekaluni. Lakini viongzi wa makuhani, walimu wa sheria na viongozi wa watu walikuwa wakitafuta njia ili kumwua. 48Lakini hawakupata nafasi kwa sababu watu wote walimfuata wakiyasikiliza maneno Yake kwa usikivu mwingi.

### *Wahoji Kuhusu Mamlaka Ya Yesu*

**20** Siku moja, Yesu alipokuwa akifundisha watu hekaluni na kuhubiri habari njema, viongozi wa makuhani, walimu wa sheria, pamoja na wazee wakamjia. 2Wakamwuliza, "Tuambie, unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Ni nani aliyekupa mamlaka haya?"

3Akawajibu, "Nami nitawauliza swali. 4Je, ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?"

5Wakasemezana wao kwa wao wakisema, "Kama tukisema, ulitoka mbinguni, atatuuliza, 'Mbona hamkumwamini?' 6Lakini tukisema, ulitoka kwa 'wanadamu', watu wote watatupiga mawe kwa sababu wanaamini kwamba Yohana alikuwa nabii."

7Basi wakajibu, "Hatujui ulikotoka."

8Yesu akawaambia, "Wala mimi sitawaambia ni kwa mamlaka gani ninafanya mambo haya."

### *Mfano Wa Wapangaji Waovu*

9 Akaendelea kuwaambia watu mfano huu: "Mtu mmoja alipanda shamba lake la mizabibu, akalikodisha kwa wakulima fulani, kisha akasafiri kwa muda mrefu. 10Wakati wa mavuno akamtuma mtumishi wake kwa hao wakulima aliowakodishia ili wampatie sehemu ya mavuno ya shamba la mizabibu. Lakini wale wakulima waliokodisha wakampiga na kumfukuza mikono mitupu. 11Akamtuma mtimishi mwingine, huyo naye wakampiga, wakamfanyia mambo ya aibu na kumfukuza. 12Bado akamtuma na mwingine wa tatu, huyu pia wakamjeruhi na kumtupa nje ya shamba.

13"Basi yule mwenye shamba la mizabibu akasema, 'Nifanye nini? Nitamtuma mwanangu mpendwa, huenda yeye watamheshimu.'

14"Lakini wale wakulima waliokodisha shamba walipomwona wakasemezana wao kwa wao na kusema, 'Huyu ndiye mrithi, basi na tumwue ili urithi uwe wetu.' 15Kwa hiyo

wakamtoa nje ya shamba la mizaibu, wakamwua."

"Sasa basi yule mwenye shamba la mizabibu atawafanyia nini wakulima hawa
waliokodisha shamba? 16Atakuja na kuwaua
hao wapangaji na kuwapa wapangaji wengine hilo shamba la mizabibu."

Watu waliposikia hayo wakasema, "Mungu apishie mbali jambo hili lisitokee!"

17Lakini Yesu akawakazia macho akasema, "Basi ni nini maana ya yale yaliyoandikwa:

" 'Jiwe lile walilolikataa waashi,
limekuwa jiwe kuu la pembeni?'

18Kila mtu aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika vipande vipande na ye yote litakayemwangukia litamsagasaga awe unga."

19Walimu wa sheria na viongozi wa makuhani wakatafuta njia ya kumkamata mara moja kwa sababu walifahamu kwamba ametoa mfano huo kwa ajili yao. Lakini waliwaogopa watu.

### *Kumlipa Kaisari Kodi*

20Kwa hiyo wakawa wanamchunguza na kutuma wapelelezi waliojifanya kuwa waaminifu ili wapate kumtega kwa maneno asemayo ili wamtie katika uwezo na mamlaka ya mtawala.
21Hivyo wale wapelelezi wakamwuliza, "Mwalimu, tunajua unasema na kufundisha yaliyo kweli wala humpendelei mtu, bali wafundisha njia ya Mungu kwa kufuata ukweli.
22Je, ni halali sisi kumlipa Kaisari kodi au la?"

23Lakini Yesu akatambua hila yao, kwa hiyo akawaambia, "Kwa nini ninyi mnanijaribu?"
24Nionyesheni dinari. Je, picha hii na maandishi haya yaliyoko juu yake ni ya nani?"

25Wakamjibu, "Ni ya Kaisari."

Akawaambia, "Basi mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari na Mungu mpeni kilicho cha Mungu."

26Wakashindwa kumkamata kwa yale aliyokuwa amesema hadharani. Nao wakashangazwa mno na majibu Yake, wakanyamaza kimya.

### *Ufufuo Na Ndoa*

27Baadhi ya Masadukayo, wale wasemao kwamba hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia
Yesu na kumwuliza, 28"Mwalimu, Mose alituandikia kwamba kama ndugu wa mtu akifa na kuacha mkewe bila mtoto, basi huyo mtu inampasa amwoa huyo mjane ili amzalie ndugu
yake watoto. 29Basi walikuwepo ndugu saba, wa kwanza akaoa, akafa bila kuzaa mtoto.
30Kisha yule wa pili akamwoa huyo mjane, naye
kafa bila mototo. 31Naye wa tatu pia, vivyo hivyo ndugu wote saba wakawa wamemwoa huyo mwanamke na wote wakafa pasipo kupata
mtoto. 32Mwishowe, huyo mwanamke mjane
naye akafa. 33Sasa basi, siku ya ufufuo huyo mwanamke atakuwa mke wa nani? Maana aliolewa na ndugu wote saba.''

34Yesu akawajibu, "Katika maisha haya
watu huoa na kuolewa. 35Lakini wale ambao wamehesabiwa kwamba wanastahili kupata nafasi katika ulimwengu ule na katika ufufuo wa
wafu, hawaoi wala hawaolewi. 36Hawa hawawezi kufa tena, kwa maana wao ni kama malaika. Wao ni watoto wa Mungu, kwa sababu
ni watoto wa ufufuo. 37Hata Mose alidhihirisha kuwa wafu wanafufuka, kwa habari ya kile kichaka kilichokuwa kikiwaka moto bila keteketea, alipomwita Bwana 'Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaki na Mungu wa
Yakobo.' 38Yeye Mungu si Mungu wa wafu bali wa walio hai, kwa kuwa Kwake wote ni hai."

39Baadhi ya walimu wa sheria wakasema, "Mwalimu, umesema sawasawa kabisa!"
40Baada ya hayo hakuna mtu aliyethubutu kumwuliza maswali zaid..

### *Kristo Ni Mwana Wa Nani?*

41Kisha Yesu akawaambia, "Imekuwaje basi wao husema Kristo ni Mwana wa Daudi?
42Daudi mwenyewe anasema katika Kitabu cha Zaburi,

' "BWANA alimwambia Bwana wangu:
"Keti mkono wangu wa kuume
43mpaka niwaweke adui
zako chini ya miguu yako.' "

44Ikiwa Daudi anamwita Yeye 'Bwana,' basi, atakuwaje Mwanawe?"

### *Yesu Awashutumu Walimu Wa Sheria*

45Wakati watu wote walipokuwa wanamsikiliza, Yesu akawaambia wanafunzi
Wake, 46 "Jihadharini na walimu wa sheria. Wao hupenda kutembea wakiwa wamevaa majoho marefu na kusalimiwa kwa heshima masokoni. Hukaa kwenye viti maalum katika masinagogi na kukaa kwenye sehemu za wageni wa heshima
katika karamu. 47Wanakula nyumba za

wajane na ili waonekane mbele ya watu husali
sala ndefu. Watu kama hawa watapata hukumu
iliyo kuu.

### *Sadaka Ya Mjane*

**21** Yesu alipoinua macho yake, aliwaona
matajiri wakiweka sadaka zao kwenye sanduku
la hazina ya hekalu. 2Akamwona pia mwanamke
mmoja mjane maskini, akiweka humo sarafu
mbili za shaba. 3 Yesu akasema, "Amin, amin
nawaambia, huyu mjane maskini ameweka
humo sadaka kubwa zaidi kuliko wengine
wote. 4Hawa watu wengine wote wametoa
sadaka kwa Mungu kutokana na wingi wa mali
zao, lakini huyu mjane ametoa kutokana na
umaskini wake vyote alivyokuwa
navyo kwa ajili ya maisha yake."

### *Dalili Za Siku Za Mwisho*

5Baadhi ya wanafunzi Wake wakawa
wanamwonyesha jinsi hekalu lilivyopambwa kwa
mawe mazuri na kwa vitu vilivyotolewa kuwa
sadaka kwa Mungu. Lakini Yesu akawaambia,
6"Kuhusu haya mnayoyaona hapa saa, wakati
utafika ambapo hakuna jiwe moja litakalosalia
juu ya jiwe jingine, kila moja litabomolewa."

7Wakamwuliza, "Mwalimu, mambo haya
yatatukia lini? Ni dalili gani zitaonyesha kwamba
yanakaribia kutendeka?"

8Yesu akawajibu, "Jihadharini msije
mkadanganywa. Maana wengi watakuja kwa
Jina langu, wakidai kwamba, 'Mimi ndiye,' nao
'Wakati umekaribia.' Msiwafuate. 9Lakini
msikiapo habari za vita na machafuko,
msiogope. Kwa maana hayo ni lazima yatokee
kwanza, ila ule mwisho hautakuja wakati huo."

10Kisha akawaambia: "Taifa litainuka dhidi
ya taifa jingine na ufalme mmoja dhidi ya ufalme
mwingie. 11Kutakuwa na matetemeko ya ardhi
katika sehemu mbalimbali, njaa kali na
magonjwa ya kuambukiza. Kutakuwa na
matukio ya kutisha na ishara kuu kutoka
mbinguni.

### *Mateso*

12"Lakini kabla yote hayajatokea,
watawakamata ninyi na kuwatesa. Watawatia
mikononi mwa wakuu wa masinagogi na
kufungwa magerezani; nayi mtapelekwa mbele
ya wafalme na watawala kwa ajili ya Jina langu.
13Hii itawapa nafasi ya kushuhudia. 14 Lakini
msiwe na wasiwasi kwamba mtasema nini kabla
ya mashtaka. 15Kwa maana nitawapa maneno
na hekima ambayo hakuna hata adui yenu
mmoja atakayeweza kushindana nayo wala
kuipinga. 16Mtasalitiwa hata na wazazi, ndugu,
jamaa na marafiki na baadhi yenu watawaua.
17Mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina
langu. 18Lakini hapatakuwa na unywele mmoja
wa kichwa chenu utakaoangamia. 19Kwa
kuvumilia mtaokoa roho zenu.

### *Kuharibiwa Kwa Yerusalemu Kwatabiriwa*

20"Mtakapoona mji wa Yerusalemu
umezungukwa na majeshi, basi fahamuni
kwamba kuharibiwa kwake kumekaribia.
21Wakati huo, wale walio Uyahudi wakimbilie
milimani, walio mjini Yerusalemu watoke humo
na wale walioko mashambani wasiingie mjini.
22Kwa sababu huu utakuwa ni wakati wa
adhabu ili kutimiza yaliyoandikwa. 23Ole wao
wenye mimba na watakaoukuwa
wananyonyesha katika siku hizo! Kutakuwa na
dhiki kuu katika nchi na ghadhabu juu ya hawa
watu 24Wataanguka kwa makali ya upanga,
wengine watachukuliwa kuwa mateka katika
mataifa yote, nao Yerusalemu utakanyagwa na
watu Mataifa mpaka muda wa hao watu Mataifa
utimie.

### *Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*

25"Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi na
nyota. Hapa duniani, mataifa yatakuwa katika
dhiki na fadhaa kutokana na ngurumo na
misukosuko ya bahari. 26Watu watazimia roho
kutokana na hofu kuu na kuyaona yale mambo
yanayotokea duniani, kwa maana nguvu za vitu
vya angani zitatikisika. 27Wakati huo ndipo
watakapomwona Mwana wa Adamu akija
mawinguni pamoja na uweza na utukufu mkuu.
28Mambo haya yatakapoanza kutendeka,
simameni na mkaviinue vichwa vyenu, kwa
sababu ukombozi wenu umekaribia."

29Akawaambia mfano huu: "Uangalieni mtini
na miti mingine yote. 30Unapochipua majani, ninyi
wenyewe mnaweza kuona na kutambua ya kuwa
wakati wa kiangazi umekaribia. 31Vivyo hivyo,
mnapoyaona mambo haya yakitukia, mwajua
kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia.

32"Amin, amin nawaambia, kizazi hiki
hakika hakitapita hadi mambo haya yote
yatimie. 33Mbingu na nchi zitapita, lakini
maneno Yangu hayatapita kamwe."

### *Siku Ya Mwisho Itakuja Ghafula*

34“Jihadharini mioyo yenu isije ikalemewa na
anasa, ulevi na fadhaa za maisha haya, nayo siku
ile ikawakuta ninyi bila kutazamia kama vile mtego
unasavyo. 35Kwa maana kama vile mtego
unasavyo, ndivyo siku hiyo itakavyowapata
wanadamu wote waishio katika uso wa dunia yote.
36Kesheni daima na mwombe ili mweze kuokoka
na yale yote yatakayotokea na kusimama mbele
ya Mwana wa Adamu.”

37Kila siku Yesu alikuwa akifundisha
hekaluni na jioni ilipofika, alikwenda Zake
kwenye Mlima wa Mizeituni na kukaa huko usiku
kucha. 38Nao watu wote walikuja asubuhi na
mapema hekaluni ili kumsikiliza.

### *Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*

**22** Wakati huu Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, iitwayo Pasaka, ilikuwa imekaribia.
2Viongozi wa makuhani na walimu wa sheria
walikuwa wanatafuta njia ya kumwua Yesu, kwa
sababu waliwaogopa watu. 3Shetani
akamwingia Yuda, aliyeitwa Iskariote, mmoja wa
wale Kumi na Wawili. 4Yuda akaenda kwa
viongozi wa makuhani na kwa maafisa wa
walinzi wa hekalu kuzungumza nao jinsi
ambavyo angeweza kumsaliti Yesu. Wakafurahi
na wakakubaliana kumpa fedha. 6Naye
akakubali, akaanza kutafuta wasaa mzuri wa
kumsaliti Yesu kwao wakati ambapo hakuna
umati wa watu.

### *Maandalizi Ya Pasaka*

7Basi ikawadia siku ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, siku ambayo Mwana-Kondoo wa
Pasaka huchinjwa. 8Hivyo Yesu akawatuma
Petro na Yohana, akisema, “Nendeni
mkatuandalie chakula cha Pasaka ili tuweze
kuila.”

9Wakamwuliza, “Unataka tukuandalie wapi
Pasaka?”

10Yesu akawaambia, “Sikilizeni,
mtakapokuwa mmeingia mjini, mtakutana na
mwanaume mmoja aliyebeba mtungi wa maji,
mfuateni mpaka kwenye nyumba atakayoingia,
11nanyi mwambieni mwenye nyumba, ‘Mwalimu
anauliza, kiko wapi chumba cha wageni,
ambamo mimi na wanafunzi Wangu tutakula
Pasaka?’ 12Atawaonyesha chumba kikubwa
ghorofani, ambacho kina samani zote kikiwa
kimepambwa vizuri. Tuandalieni humo.”

13Wakaenda, wakakuta kila kitu kama Yesu
alivyokuwa amewaambia. Kwa hiyo wakaandaa
Pasaka.

### *Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

14Wakati ulipowadia, Yesu akaketi mezani
pamoja na wanafunzi Wake. 15Kisha
akawaambia, “Nimetamani sana kuila Pasaka
hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa Kwangu.
16Kwa maana, nawaambia, sitaila tena Pasaka
mpaka itakapotimizwa katika Ufalme wa
Mungu.”

17Akiisha kukichukua kikombe, akashukuru,
akasema, “Chukueni hiki mnywe wote. 18Kwa
maana, nawaambia kwamba, tangu sasa
sitakunywa tena divai hadi Ufalme wa Mungu
utakapokuja.”

19Kisha akachukua mkate, akashukuru,
akaumega, akawapa akisema, “Huu ni mwili
Wangu unaotolewa kwa ajili yenu, fanyeni hivi
kwa ukumbusho Wangu.”

20Vivyo hivyo baada ya kula, akachukua kile
kikombe akasema, “Kikombe hiki ni agano jipya
katika damu Yangu, imwagikayo kwa ajili yenu.
21Lakini mkono wake huyo atakaenisaliti uko hapa
mezani pamoja nami. 22Mwana wa Adamu
anakwenda Zake kama ilivyokusudiwa, lakini ole
wake mtu huyo atakayenisaliti.” 23 Wakaanza
kuulizana wao kwa wao, ni nani miongoni mwetu
anayeweza kufanya jambo hilo?

### *Mabishano Kuhusu Ukuu*

24Pia yakazuka mabishano katikati ya
wanafunzi kwamba ni nani anayeonekana kuwa
mkuu wa wote miongoni mwao. 25Yesu
akawaambia, “Wafalme na watu wakuu
wasiomjua Mungu huwatawala watu wao kwa
nguvu na wenye mamlaka juu yao huitwa
‘Wafadhili.’ 26Lakini ninyi msifanane nao. Bali
yeye aliye mkuu kuliko wote miongoni mwenu,
inampasa kuwa kama yeye aliye mdogo wa
wote, naye atawalaye na awe kama yeye
ahudumuye. 27Kwani ni nani aliye mkuu? Ni
yule aketiye mezani au ni yule ahudumiaye? Si
ni yule aliyekaa mezani? Lakini Mimi niko
miongoni mwenu kama yule ahudumiaye.
28“Ninyi mmekuwa pamoja nami katika majaribu
Yangu. 29Nami kama Baba Yangu alivyonipa
ufalme, kadhalika mimi nami ninawapa ninyi,
30ili mpate kula na kunywa mezani pangu katika
karamu ya Ufalme Wangu na kukaa katika viti
vya enzi, mkihukumu makabila kumi na mawili
ya Israeli.

### *Yesu Atabiri Kuwa Petro Atamkana*

31Yesu akasema, “Simoni, Simoni, sikiliza,

Shetani ameomba kuwapepeta ninyi wote kama
ngano. 32Lakini nimekuombea wewe Simoni ili
imani yako isishindwe, nawe ukiisha kunirudia,
uwaimarishe ndugu zako."

33Petro akajibu, "Bwana, niko tayari kwenda
pamoja nawe gerezani na hata kifoni."

34 Yesu akamjibu, "Ninakwambia Petro,
kabla jogoo hajawika usiku huu wa leo,
utanikana mara tatu kwamba hunijui Mimi."

### *Mfuko, Mkoba Na Upanga*

35Kisha Yesu akawauliza, "Nilipowatuma
bila mfuko, wala mkoba, wala viatu,
mlipungukiwa na kitu cho chote?"

Wakajibu, "La, hatukupungukiwa na kitu cho
chote."

36Akawaambia, "Lakini sasa, aliye na mfuko
na auchukue na aliye na mkoba vivyo hivyo.
Naye asiye na upanga, auze joho lake anunue
mmoja. 37Kwa sababu, nawaambia, andiko hili
lazima litimizwe juu Yangu, kwamba,
"Alihesabiwa pamoja na wahalifu, kwa kweli
yaliyoandikwa kunihusu Mimi hayana budi
kutimizwa."

38Wanafunzi Wake wakamwambia, "Bwana,
tazama hapa kuna panga mbili."

Akawajibu, "Inatosha."

### *Yesu Aomba Kwenye Mlima Wa Mizeituni*

39Yesu akatoka akaenda kwenye Mlima wa
Mizeituni kama ilivyokuwa kawaida Yake, nao
wanafunzi Wake wakamfuata. 40Walipofika
huko, akawaambia wanafunzi Wake, "Ombeni
msije mkaangukia majaribuni." 41Akajitenga
nao, kama umbali wa kutupa jiwe, akapiga
magoti, akaomba, 42akisema, "Baba, kama ni
mapenzi Yako, niondolee kikombe hiki, lakini si
kama Mimi nipendavyo, bali mapenzi Yako
yatendeke." 43Malaika kutoka mbinguni
akamtokea, akamtia nguvu. 44Naye akiwa katika
maumivu makuu, akaomba kwa bidii, nalo jasho
Lake likawa kama matone ya damu
yakidondoka ardhini.

45 Baada ya kuomba, akawarudia
wanafunzi Wake akawakuta wamelala, wakiwa
wamechoka kutokana na huzuni. 46Naye
akawauliza, "Mbona mmelala? Amkeni mwombe
ili msiangukie majaribuni."

### *Yesu Akamatwa*

47Wakati Yesu alipokuwa bado
anazungumza, umati mkubwa wa watu ukaja,
ukiongozwa na Yuda, ambaye alikuwa mmoja
wa wale Wanafunzi Kumi na Wawili.
Akamkaribia Yesu ili ambusu. 48Lakini Yesu
akamwambia, "Yuda, je, unamsaliti Mwana wa
Adamu kwa busu?"

49Wafuasi wa Yesu walipoona yale
yaliyokuwa yanakaribia kutokea, wakasema,
"Bwana, tutumie panga zetu?" 50Mmoja wao
akampiga mtumishi wa Kuhani Mkuu kwa
upanga, akamkata sikio la kuume.

51Lakini Yesu akasema, "Acheni!" Akaligusa
lile sikio la yule mtu na kumponya.

52Kisha Yesu akawaambia viongozi wa
makuhani, maafisa wa walinzi wa hekalu na
wazee waliokuwa wamekuja, "Mmekuja na
panga na marungu, kana kwamba Mimi ni
mnyang'anyi? 53Siku kwa siku nilikuwa pamoja
nanyi hekaluni lakini hamkunikamata. Lakini hii
ni saa yenu, wakati giza linatawala!"

### *Petro Amkana Yesu*

54Kisha wakamkamata Yesu, wakamchukua
wakaenda naye mpaka nyumbani kwa Kuhani
Mkuu. Lakini Petro akafuata kwa mbali.
55Walipokwisha kuwasha moto katikati ya ua na
kuketi pamoja, Petro naye akaketi pamoja nao.
56Mtumishi wa kike mmoja akamwona Petro
ameketi pale kwenye mwanga wa moto.
Akamwangalia kwa uangalifu na kusema, "Huyu
mtu pia alikuwa pamoja na Yesu!"

57Lakini Petro akakana akasema, "Ewe
mwanamke, hata simjui!!"

58Baadaye kidogo mtu mwingine, kwa
kumwona Petro, akasema, "Wewe pia ni mmoja
wao!"

59Baada ya muda wa kama saa moja hivi,
mtu mwingine akazidi kusisitiza, "Kwa hakika
huyu mtu naye alikuwa pamoja na Yesu, kwa
maana yeye pia ni Mgalilaya."

60Petro akajibu, "Wewe mtu, mimi sijui
unalosema!" Wakati uo huo, akiwa bado
anazungumza, jogoo akawika. 61Naye Bwana
akageuka akamtazama Petro. Ndipo Petro
akakumbuka yale maneno ambayo Bwana
alimwambia, "Kabla jogoo hajawika leo,
utanikana mara tatu." 62Akatoka nje, akalia
sana.

### *Walinzi Wamdhihaki Yesu Na Kumpiga*

63Wale watu waliokuwa wanamlinda Yesu
wakaanza kumdhihaki na kumpiga.
64Wakamfunga kitambaa machoni na
kumwuliza, "Tabiri!" Tuambie ni nani
aliyekupiga?" 65Wakaendelea kumtukana kwa

matusi mengi.

### *Yesu Apelekwa Mbele Ya Baraza*

66 Kulipopambazuka baraza[a] la wazee wa watu, viongozi wa makuhani na walimu wa sheria, wakakutana pamoja, naye Yesu akaletwa mbele yao. 67Wakamwambia, "Kama Wewe ndiye Kristo, tuambie."

Yesu akawajibu, "Hata nikiwaambia hamtaamini. 68Nami nikiwauliza swali, hamtanijibu. 69Lakini kuanzia sasa, Mwana wa Adamu ataketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenye Nguvu."

70Wote wakauliza, "Wewe basi ndiwe Mwana wa Mungu?"

Yeye akawajibu, "Ninyi mmesema kwamba Mimi ndiye."

71Kisha wakasema, "Kwani tunahitaji ushahidi gani zaidi? Tumesikia wenyewe kutoka kinywani Mwake."

### *Yesu Apelekwa Kwa Pilato*

23 Kisha umati wote wa watu wakainuka na kumpeleka Yesu kwa Pilato. 2Nao wakaanza kumshtaki wakisema: "Tumemwona huyu mtu akipotosha taifa letu, akiwazuia watu wasilipe kodi kwa Kaisari na kujiita kuwa Yeye ni Kristo, mfalme."

3Basi Pilato akamwuliza Yesu, "Wewe ndiye mfalme wa Wayahudi?"

Yesu akajibu, "Wewe wasema."

4Pilato akawaambia viongozi wa makuhani na watu wote waliokuwapo, "Sioni sababu ya kutosha kumshtaki mtu huyu!"

5Lakini wao wakakazana kusema, "Anawachochea watu kwa mafundisho Yake katika Uyahudi yote, tangu Galilaya alikoanzia, hadi sehemu hii!"

### *Yesu Apelekwa Kwa Herode*

6Pilato aliposikia hayo akauliza, 'Huyu mtu ni Mgalilaya?" 7Alipofahamu kwamba Yesu alikuwa chini ya mamlaka ya Herode, akampeleka kwa Herode, ambaye wakati huo alikuwa pia Yerusalemu.

8Herode alipomwona Yesu alifurahi sana, kwa sababu kwa muda mrefu alikuwa amesikia mambo mengi kumhusu Yeye. Pia alitarajia kumwona akifanya miujiza kadha wa kadha. 9Pilato akamwuliza maswali mengi, lakini Yesu hakumjibu lo lote. 10Wakati huo viongozi wa makuhani na walimu wa sheria walikuwepo wakitoa mashtaka yao kwa nguvu sana. 11Herode na maaskari wake wakamdhihaki Yesu na kumfanyia mzaha. Wakamvika vazi zuri sana, wakamrudisha kwa Pilato. 12 Siku hiyo, Herode na Pilato wakawa marafiki, kabla ya jambo hili walikuwa na uadui kati yao.

### *Yesu Ahukumiwa Kifo*

13Basi Pilato akawaita pamoja viongozi wa makuhani, viongozi wengine na watu, 14akawaambia, "Ninyi mlimleta huyu mtu kwangu kuwa ni mtu anayewachochea watu ili waasi. Nimemhoji mbele yenu nami nimeona hakuna msingi wo wote wa mashtaka yenu dhidi Yake. 15Wala Herode hakumwona na kosa lo lote, ndiyo sababu amemrudisha kwetu. Kama mnavyoona, mtu huyu hakufanya jambo lo lote linalostahili kifo. 16Kwa hiyo nitaamuru apigwe mijeledi na kumwachia." (17Kwa kuwa ilikuwa lazima kuwafungulia mfungwa mmoja wakati wa Sikukuu).

18Ndipo watu wote wakapiga kelele kwa pamoja, "Mwondoe mtu huyo! Tufungulie Baraba!" (19 Baraba alikuwa amefungwa gerezani kwa sababu ya maasi yaliyokuwa yametokea mjini na kwa ajili ya mauaji).

20Pilato akitaka kumwachilia Yesu, akasema nao tena. 21Lakini wao wakaendelea kupiga kelele wakisema, "Msulibishe! Msulibishe! Msulibishe!"

22Kwa mara ya tatu Pilato akawaambia, "Kwani amefanya kosa gani huyu mtu? Sikuona Kwake sababu yo yote inayostahili adhabu ya kifo. Kwa hiyo nitaamuru apigwe mijeledi na kisha nitamwachia."

23Lakini watu wakazidi kupiga kelele kwa nguvu wakidai kwamba Yesu asulibiwe. Hivyo, kelele zao zikashinda. 24Kwa hiyo Pilato akatoa hukumu kwamba madai yao yatimizwe. 25Akamfungua yule mtu aliyekuwa amefungwa gerezani kwa kuhusika katika uasi dhidi ya serikali na mauaji. Akamkabidhi Yesu mikononi mwao, wamfanyie watakavyo.

### *Kusulibiwa Kwa Yesu*

26Walipokuwa wakienda naye, wakamkamata mtu mmoja aitwaye Simoni mweyeji wa Kirene, aliyekuwa anatoka shambani. Wakambebesha msalaba, wakamlazimisha auchukue nyuma ya Yesu. 27Idadi kubwa ya watu wakamfuata Yesu, wakiwamo wanawake waliokuwa wakimlilia na kumwombolezea. 28Yesu akawageukia,

[a]66 Baraza hapa maana yake "Sanhedrin"

akawaambia, "Enyi binti za Yerusalemu,
msinililie Mimi bali jililieni ninyi wenyewe na
watoto wanu. 29Kwa maana wakati utafika
mtakaposema, 'Wamebarikiwa wanawake tasa,
ambao matumbo yao hayakuzaa wala matiti yao
hayakunyonyesha!'

30"Ndipo wataiambia milima,
'Tuangukieni' na vilima, 'Tufunikeni!'

31Kwa maana kama wamefanya hivi kwa mti
mbichi, kwa mti mkavu itakuwaje?"
32Watu wengine wawili wahalifu
walipelekwa pamoja na Yesu ili wakasulibiwe.
33Walipofika mahali paitwapo "Fuvu La Kichwa,"
hapo ndipo walipomsulibisha Yesu pamoja na
hao wahalifu, mmoja upande Wake wa kuume
na mwingine upande Wake wa kushoto. 34Yesu
akasema, "Baba, wasamehe, kwa maana
hawajui walitendalo!" Wakagawana nguo Zake
kwa kupiga kura.
35Watu wakasimama hapo wakimwangalia,
nao viongozi wa Wayahudi wakamdhihaki
wakisema, "Aliokoa wengine! Ajiokoe
mwenyewe basi, kama Yeye ndiye Kristo wa
Mungu, Mteule wake."
36Askari nao wakaja, wakamdhihaki,
wakamletea siki ili anywe. 37Nao
wakamwambia, "Kama Wewe ni Mfalme wa
Wayahudi, jiokoe mwenyewe."
38Maandishi haya yaliwekwa kwenye
msalaba juu ya kichwa Chake: "HUYU NDIYE
MFALME WA WAYAHUDI."
39Mmoja wa wale wahalifu waliosulibiwa
pamoja naye akamtukana, akasema: "Wewe si
ndiye Kristo? Jiokoe ili utuokoe na sisi."
40Lakini yule mhalifu mwingine akamkemea
mwenzake, akasema, "Je, wewe humwogopi
Mungu, wakati uko kwenye adhabu hiyo hiyo?
41Sisi tumehukumiwa kwa haki kwa kuwa
tunapata tunayostahili kwa ajili ya matendo yetu.
Lakini huyu mtu hajafanya kosa lo lote."
42Kisha akasema, "Bwana Yesu,
unikumbuke utakapokuja katika Ufalme Wako."
43Yesu akamjibu, "Amin, nakuambia, leo hii
utakuwa pamoja nami Paradiso[a]"

### *Kifo Cha Yesu*

44Ilikuwa kama saa sita mchana, kukawa na
giza katika nchi yote mpaka saa tisa, 45kwa
sababu jua liliacha kutoa nuru. Pazia la hekalu
likachanika vipande viwili. 46Yesu akapaza sauti
Yake akasema, "Baba, mikononi mwako
naikabidhi roho Yangu." Baada ya kusema
haya, akakata roho.
47Yule jemadari alipoona yaliyotukia,
akamsifu Mungu akasema, "Hakika, mtu huyu
alikuwa mwenye haki." 48Watu wote waliokuwa
wamekusanyika hapo kushuhudia tukio hili
walipoyaona hayo, wakapigapiga vifua vyao
kwa huzuni na kwenda zao. 49Lakini wale wote
waliomfahamu, pamoja na wale wanawake
waliokuwa wamemfuata kutoka Galilaya,
walisimama kwa mbali wakiyatazama mambo
haya.

### *Maziko Ya Yesu*

50Basi kulikuwa na mtu mmoja mwema na
mwenye haki jina lake Yosefu.Yeye alikuwa
mjube wa Baraza[b] la Wayahudi, 51 lakini yeye
hakuwa amekubaliana na maamuzi na vitendo
vya viongozi wenzake. Huyu alikuwa mweyeji
wa Arimathaya huko Uyahudi, naye alikuwa
unaungojea Ufalme wa Mungu kwa matarajio
makubwa. 52Yosefu alikwenda kwa Pilato
akaomba apewe mwili wa Yesu. 53Akaushusha
kutoka msalabani, akauzungushia kitani safi na
kuuweka katika kaburi lililochongwa kwenye
mwamba, ambalo lilikuwa hajazikiwa mtu
mwingine ye yote. 54Ilikuwa siku ya Maandalio,
nayo Sabato ilikuwa karibu kuanza.
55Wale wanawake waliokuwa wamekuja
pamoja na Yesu wakimfuata kutoka
Galilaya,wakamfuata Yosefu, wakaliona kaburi
na jinsi mwili wa Yesu ulivyolazwa. 56Kisha
wakarudi nyumbani, wakaandaa manukato na
marhamu ya kuupaka huo mwili. Lakini
wakapumzika siku ya Sabato kama
ilivyoamriwa.

### *Kufufuka Kwa Yesu*

Mnamo siku ya kwanza ya juma, alfajiri
**24** na mapema, wale wanawake
walichukua yale manukato waliyokuwa
wameyaandaa na kwenda kaburini. 2Wakakuta
lile jiwe limefingirishwa kutoka kwenye kaburi,
3lakini walipoingia ndani, hawakuuona mwili wa
Bwana Yesu. 4Walipokuwa wanashangaa juu
ya jambo hili, ghafula watu wawili waliokuwa
wamevaa mavazi yanayong'aa kama umeme

---

**a**[43] Paradiso maana yake bustani nzuri , hapa ina maana mahali zinapokwenda roho za wacha Mungu, yaani, watakatifu

**b**[50] Baraza hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la uatawala la Kiyahudi,lililoundwa na wazee 70 pamoja na Kuhani Mkuu

wa radi, wakasimama karibu nao. **5**Wale
wanawake, wakiwa na hofu, wakainamisha nyuso
zao mpaka chini. Lakini wale watu wakawaambia,
“Kwa nini mnamtafuta aliye hai miongoni mwa
wafu? **6**Hayuko hapa, amefufuka! Kumbukeni
alivyowaambia alipokuwa bado yuko pamoja nanyi
huko Galilaya kwamba: **7**‘Ilikuwa lazima Mwana
wa Adamu atiwe mikononi mwa watu wenye
dhambi, waovu, asulibiwe na siku ya tatu afufuke.’
” **8**Ndipo wakayakumbuka maneno ya Yesu.

**9**Waliporudi kutoka huko kaburini,
wakawaeleza wale wanafunzi kumi na mmoja
pamoja na wengine wote mambo haya yote.
**10**Basi hawa walikuwa Maria Magdalene, Yoana
na Maria mama yake Yakobo, pamoja na
wengine waliofuatana nao. **11**Lakini wale
waliosikia hawakuwasadiki hao wanawake, kwa
sababu maneno yao yalionekana kama upuzi.
**12**Petro, hata hivyo, akainuka na kukimbilia kule
kaburini. Alipoinama kuchungulia, akaona vile
vitambaa vya kitani, ila hakuona kitu kingine.
Naye akaenda zake akijiuliza nini kilichotokea.

### *Njiani Kwenda Emau*

**13**Ikawa siku iyo hiyo, wanafunzi wawili wa
Yesu walikuwa njiani wakienda kijiji cha Emau,
yapata maili saba[a] kutoka Yerusalemu.
**14**Walikuwa wakizungumza wao kwa wao
kuhusu mambo yote yaliyotukia. **15**Walipokuwa
wakizungumza na kujadiliana, Yesu mwenyewe
akaja akatembea pamoja nao, **16**lakini macho
yao yakazuiliwa wasimtambue.

**17**Akawauliza, “Ni mambo gani haya
mnayozungumza wakati mnatembea?”

Wakasimama, nyuso zao zikionyesha
huzuni. **18**Mmoja wao, aliyeitwa Kleopa,
akamwuliza, “Je, Wewe ndiye peke yako mgeni
huku Yerusalemu ambaye hufahamu mambo
yaliyotukia humo siku hizi?”

**19**Akawauliza, “Mambo gani?”

Wakamjibu, “Mambo ya Yesu wa Nazareti.
Yeye alikuwa nabii, mwenye uwezo mkuu katika
maneno Yake na matendo Yake, mbele za
Mungu na mbele ya wanadamu wote.
**20**Viongozi wa makuhani na viongozi wetu
walimtoa ahukumiwe kufa, nao wakamsulibisha.
**21**Lakini tulikuwa tumetegemea kwamba Yeye
ndiye angeliikomboa Israeli. Zaidi ya hayo, leo ni
siku ya tatu tangu mambo haya yatokee.
**22**Isitoshe, baadhi ya wanawake katika kundi
letu wametushtusha. Walikwenda kaburini leo
alfajiri, **23**lakini hawakuukuta mwili Wake.
Walirudi wakasema wameona maono ya
malaika ambao waliwaambia kwamba Yesu yu
hai. **24**Kisha baadhi ya wenzetu walikwenda
kaburini wakalikuta kama vile wale wanawake
walivyosema, lakini Yeye hawakumwona.”

**25**Yesu akawaambia, “Ninyi ni wajinga kiasi
gani, nanyi ni wazito mioyoni mwenu kuamini
mambo yote yaliyonenwa na manabii! **26**Je,
haikumpasa Kristo kuteswa kwa njia hiyo na
kisha aingie katika utukufu Wake?” **27**Naye
akianzia na Mose na manabii wote,
akawafafanulia jinsi maandiko yalivyosema
kumhusu Yeye.

**28**Nao wakakaribia kile kijiji walichokuwa
wakienda, Yesu akawa kama anaendelea
mbele. **29**Lakini wao wakamsihi sana akae nao,
wakisema, “Kaa hapa nasi, kwa maana sasa ni
jioni na usiku unaingia.’’ Basi akaingia ndani
kukaa nao.

**30**Alipokuwa mezani pamoja nao,
akachukua mkate, akashukuru, akaumega,
akaanza kuwagawia. **31**Ndipo macho yao
yakafumbuliwa, nao wakamtambua, naye
akatoweka machoni pao. Hawakumwona tena.
**32**Wakaulizana wao kwa wao, “Je, mioyo yetu
haikuwakawaka kwa furaha ndani yetu
alipokuwa anazungumza nasi njiani na
kutufafanulia Maandiko?”

**33**Wakaondoka mara, wakarudi Yerusalemu.
Wakawakuta wale wanafunzi kumi na mmoja na
wale waliokuwa pamoja nao, wamekusanyika
**34**wakisema, “Ni kweli Bwana amefufuka, naye
amemtokea Simoni.” **35**Kisha wale wanafunzi
wawili wakaeleza yaliyotukia njiani na jinsi
walivyomtambua Yesu alipoumega mkate.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Wake*

**36** Wakati walipokuwa bado wanazungumza
hayo, Yesu mwenyewe akasimama katikati yao
akasema, “Amani iwe nanyi.”

**37**Wakashtuka na kuogopa wakidhani
kwamba wameona mzuka. **38** Lakini Yesu
akawauliza, “Kwa nini mnaogopa? Kwa nini
mna shaka mioyoni mwenu? **39**Tazameni
mikono Yangu na miguu Yangu, mwone kuwa ni
mimi hasa. Niguseni mwone, kwa maana mzuka
hauna nyama na mifupa, kama mnionavyo
kuwa nayo.’’

**40**Aliposema haya, akawaonyesha mikono
na miguuu Yake. **41**Wakashindwa kuamini kwa
ajili ya furaha na mshangao waliokuwa nao.
Akawauliza, “Mna chakula cho chote hapa?”

[a] **13** Maili saba ni kama kilomita 11.2

42Wakampa kipande cha samaki aliyeokwa,
43nayeakakichukua na kukila mbele yao.

44Akawaambia, "Haya ndiyo yale
niliyowaambia nilipokuwa bado niko pamoja
nanyi, kwamba yote yaliyoandikwa kunihusu
Mimi katika Torati ya Mose, manabii na Zaburi
hayana budi kutimizwa."

45Ndipo akafungua fahamu zao ili waweze
kuyaelewa Maandiko. 46Akawaambia, "Haya
ndiyo yaliyoandikwa: Kristo atateswa na siku ya
tatu atafufuka kutoka kwa wafu. 47Toba na
msamaha wa dhambi utatangazwa kupitia Jina
Lake, kuanzia Yerusalemu. 48Ninyi ni mashahidi
wa mambo haya.

### *Kuahadiwa Kwa Roho Mtakatifu*

49 Tazama nawaletea juu yenu ahadi ya
Baba Yangu, lakini kaeni humu Yerusalemu
mpaka mtakapovikwa uwezo utokao juu."

### *Kupaa Kwa Yesu Mbinguni*

50Akiisha kuwaongoza mpaka kwenye
viunga vya Bethania, akainua mikono Yake juu
na kuwabariki. 51Alipokuwa anawabariki,
akawaacha, akachukuliwa mbinguni. 52Kisha
wakamwabudu na kurudi Yerusalemu wakiwa
wamejawa na furaha kuu. 53Nao wakadumu
ndani ya hekalu wakimtukuza Mungu. Amen.

**YOHANA**

### *Utangulizi*

Miongoni mwa Injili zote nne, Injili ya Yohana ni ya aina ya pekee.Ingawa kwa ujumla inaonyesha maisha ya Yesu na huduma Yake, iko tofauti sana katika mpangilio na mfumo ukilinganisha na zile nyingine tatu.Injili hii haina mifano, ina miujiza miwili tu iliyoandikwa katika zile Injili nyigine zinazofanana (Mathayo, Marko na Luka) na mingine mitano ambayo ni Yohana peke yake anayeieleza.

Mtume Yohana aliandika Injili hii miaka mingi baada ya kufa na kufufuka kwa Yesu. Kusudi la kuiandika ilikuwa kwamba wale wanaoisoma wamwamini Yesu Kristo na kwa njia hiyo wapate uzima wa milele *(Yohana 20:31).* Yohana anaanza na utangulizi wa pekee ambao haumo katika Injili nyingine. Anaeleza juu ya kuwapo kwa Yesu pamoja na Baba kabla ya kitu cho chote kuumbwa. Kwa njia hii anaonyesha wazi kwamba Yesu hakuwa tu mwanadamu wa pekee bali ana asili ya Mungu. Katika Injili hii tunapata habari za baadhi ya miujiza ya Yesu na mafundisho Yake ambayo hayakutajwa katika Injili nyingine. Sehemu kubwa *(Yohana 14-17 )* inaeleza mafundisho ambayo Yesu aliwapa wanafunzi wake kabla ya kifo chake. Sehemu maalumu inaeleza jinsi Yesu alivyojidhihirisha kwa wanafunzi wake baada ya kufa na kufufuka kwake.

### *Wazo Kuu*

Injili ya Yohana inatilia mkazo zaidi Uungu wa Kristo. Pia inatueleza kwa undani zaidi ishara ambazo Injili nyingine zinaziita miujiza, ili msomaji aweze kuamini kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu na kwamba kwa kuamini apate uzima wa milele.*(20;30-31).*Zile ishara ambazo mwandishi anazielezea zinatoa uthibitisho wa uweza wa Yesu Kristo wa kiungu na maana hasa ya maisha Yake pale ambapo mwanadamu hana uwezo.Neno "amini" linaonekana mara tisini na nane.Yesu anatambulishwa kama ***NENO*** katika Injili hii, pia anaitwa Nuru, Kweli, Upendo, Mchungaji Mwema, Mlango, Ufufuo na Uzima, Mkate wa Mbinguni na majina mengine.

Ule ukweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu umerudiwa mara kwa mara. Wakati huo huo ubinadamu wa Yesu unaonyeshwa katika hali Zake za kuchoka, kuhuzunika, kulia, nk

### *Mwandishi*

Yohana ndiye mwandishi wa Injili hii,kwani huyu ndiye yule mwanafunzi mpendwa (*13:23)* aliyekuwa na Yesu kila mahali na ambaye ndiye aliyeegama kifuani mwa Yesu wakati wa chakula cha mwisho na wanafunzi Wake.Matukio ya Yohana kuwa na upendo na uhusiano wa karibu sana na Yesu umetajwa mara nyingi.Huyu ndiye Yohana mwana wa Zebedayo.Yohana alikuwa Mgalilaya mvuvi *(Mk.1:19-20.)* Yesu alipomwita. Yohana na Yakobo nduguye waliungana na Andrea na Petro katika uanafunzi wa Yesu. Mama yake Yohana alikuwa Salome dada yake Maria mamaye Yesu *(ona Mat.27:56; Mk.15:40; Yh.29:25)*

### *Tarehe*

Karibu na mwisho wa karne ya kwanza kama 90 B.K.

### *Mahali*

Nyumbani kwa Yohana kulikuwa Efeso na ambako ndiko alikozikwa. Kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa kwamba Injli hii iliandikiwa Efeso.

### *Mgawanyo*

- Mwanzo unaonyesha kuwa Yesu ni Mungu (1:1-14)
- Huduma ya Yesu kabla ya kwenda Galilaya (1:15-4:54)
- Huduma ya Yesu huko Galilaya na upinzani uliomkabili huko Yerusalemu (5:1-10:42)
- Kufufuliwa kwa Lazaro (11:1-57)
- Kukamilishwa kwa huduma ya Bwana Yesu (12:1-13:38)
- Mafundisho ya mwisho ya Bwana Yesu (14:1-17:26)
- Kufa kwa Yesu na kufufuka kwake (18:1-20:10)
- Kuonekana kwa Yesu baada ya kufufuka (20:11-21:25)

### *Neno Alifanyika Mwili*

**1** Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno
alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa
Mungu. 2Tangu mwanzo huyo
Neno alikuwa pamoja na Mungu.

3Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala
pasipo Yeye hakuna cho chote kilichoumbwa
ambacho kimeumbwa. 4Ndani Yake ndimo
ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya
watu. 5Nuru hung'aa gizani nalo giza
halikuishinda.

6Alikuja mtu mmoja aliyetumwa kutoka kwa
Mungu, jina lake Yohana. 7Alikuja kama shahidi
apate kuishuhudia hiyo nuru, ili kwa kupitia yeye
watu wote waweze kuamini. 8Yeye mwenyewe
hakuwa ile nuru, bali alikuja kuishuhudia hiyo
nuru. 9Nuru halisi, imwangaziayo kila mtu
ilikuwa inakuja ulimwenguni.

10Alikuwepo ulimwenguni na ingawa
ulimwengu uliumbwa kwa Yeye,
haukumtambua. 11Alikuja kwa walio Wake,
lakini wao hawakumpokea. 12Bali wote
waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika
watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina
Lake. 13Hawa watoto wamezaliwa si kwa damu
wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya
mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu.

14Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni
mwetu, nasi takauona utukufu Wake, utukufu
kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba,
amejaa neema na kweli.

15Yohana alishuhudia habari Zake, akapiga
kelele akisema, "Huyu ndiye yule niliyewaambia
kwamba, 'Yeye ajaye baada yangu ni mkuu
kuliko mimi, kwa kuwa alikuwako kabla yangu.' "
16Kutokana na ukamilifu Wake, sisi sote
tumepokea neema juu ya neema. 17Kwa kuwa
torati ilitolewa kwa mkono wa Mose, lakini
neema na kweli imekuja kupitia Yesu Kristo.
18Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu
wakati wo wote, ila ni Mungu Mwana pekee,
aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye
amemdhihirisha.

### *Ushuhuda Wa Yohana Mbatizaji*

19Huu ndio ushuhuda wa Yohana wakati
Wayahudi walipotuma makuhani na Walawi
kutoka Yerusalemu kumwuliza, "Wewe ni nani?"
20Yohana alikiri waziwazi pasipo kuficha
akasema, "Mimi si Kristo[a]."

21 Wakamwuliza, "Wewe ni nani basi? Je,
wewe ni Eliya?"

Yeye akajibu, "Hapana, mimi
siye." "Je, wewe ni yule Nabii?"
Akajibu, "Hapana."

22Ndipo wakasema, "Basi tuambie wewe ni
nani ili tupate jibu la kuwapelekea wale
waliotutuma. Wewe wasemaje juu yako
mwenyewe?"

23Akawajibu kwa maneno ya Nabii Isaya,
akisema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani,
'Inyosheni njia ya Bwana.' "

24Basi walikuwa wametumwa watu kutoka
kwa Mafarisayo 25wakamwuliza, "Kama wewe
si Kristo, wala si Eliya na wala si yule Nabii, kwa
nini basi unabatiza?"

26Yohana akawajibu, "Mimi ninabatiza kwa
maji[b], lakini katikati yenu yupo mtu msiyemjua.
27Yeye ajaye baada yangu, sistahili hata
kufungua kamba ya viatu vyake."

28Mambo haya yote yalitukia huko
Bethania, ng'ambo ya Mto Yordani, mahali
Yohana alipokuwa akibatiza.

### *Yesu Mwana Kondoo Wa Mungu*

29Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu
akimjia akasema, "Tazama, Mwana Kondoo wa
Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!
30Huyu ndiye Yule niliyewaambia ya kwamba,
'Yuaja mtu nyuma yangu ambaye ni mkuu
kuliko mimi kwa maana alikuwapo kabla yangu.'
31Mimi mwenyewe sikumfahamu, lakini sababu
ya kuja nikibatiza kwa maji ni ili Yeye apate
kufunuliwa kwa Israeli."

32Kisha Yohana akatoa ushuhuda huu:
"Nilimwona Roho akishuka kutoka mbinguni
kama hua, akakaa juu Yake. 33Mimi
nisingemtambua, lakini Yeye aliyenituma
nibatize kwa maji alikuwa ameniambia, 'Yule
mtu utakayemwona Roho akimshukia na kukaa
juu Yake, huyo ndiye atakayebatiza kwa Roho
Mtakatifu.' 34Mimi mwenyewe nimeona jambo
hili na ninashuhudia kuwa huyu ndiye Mwana
wa Mungu."

### *Wanafunzi Wa Kwanza Wa Yesu*

35Siku iliyofuata, Yohana alikuwako huko
tena pamoja na wanafunzi wake wawili.
36Alipomwona Yesu akipita, akasema,
"Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu!"

37Wale wanafunzi wawili walipomsikia
Yohana akisema haya, wakamfuata Yesu.
38Yesu akageuka, akawaona wakimfuata
akawauliza, "Mnataka nini?"

---

**a**20 Kristo, yaani, Masiya- maana yake Mpakwa (Aliyetiwa)Mafuta

**b**26 "Kwa maji" hapa tafsiri zingine zinasema "ndani ya maji"

Wakamwambia, "Rabi,'' (maana yake Mwalimu), "Unaishi wapi?''

39Yesu akawajibu, "Njoni, nanyi mtapaona!'' Hivyo wakaenda na kupaona mahali alipokuwa anaishi, wakakaa naye siku ile, kwa kuwa ilikuwa yapata saa kumi.

40Andrea nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa wale wawili waliosikia yale Yohana aliyokuwa amesema, naye ndiye aliyemfuata Yesu. 41Kitu cha kwanza Andrea alichofanya ni kumtafuta Simoni nduguye na kumwambia, "Tumemwona Masiya" (yaani, Kristo). 42Naye akamleta kwa Yesu.

Yesu akamwangalia na kusema, "Wewe ni Simoni mwana wa Yohana, utaitwa Kefa'' (ambalo limetafsiriwa Petro[c]).

***Yesu Awaita Filipo Na Nathanaeli***

43Siku iliyofuata Yesu aliamua kwenda Galilaya. Akamkuta Filipo, akamwambia, "Nifuate."

44Basi Filipo alikuwa mwenyeji wa Bethsaida, mji alikotoka Andrea na Petro. 45Filipo naye akamkuta Nathanaeli na kumwambia, "Tumemwona Yeye ambaye Mose aliandika habari Zake katika Torati na ambaye pia manabii waliandika kumhusu, yaani, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yosefu."

46Nathanaeli akauliza, ''Nazareti! Je, kitu cho chote chema chaweza kutoka Nazareti?" Filipo akamwambia, "Njoo uone."

47Yesu alipomwona Nathanaeli anakaribia, akanena habari zake akasema, "Tazama huyu ni Mwisraeli kweli kweli, hana hila ndani yake.''

48Nathanaeli akamwuliza, "Umenifahamuje?"

Yesu akamjibu, "Nilikuona ulipokuwa bado uko chini ya mtini, kabla hata Filipo hajakuita.''

49Nathanaeli akamwambia, ''Mwalimu, Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli!''

50Yesu akamwambia, "Unaamini kwa kuwa nilikuambia nilikuona ulipokuwa bado uko chini ya mtini? Basi utaona mambo makuu zaidi kuliko hilo.'' 51Ndipo akawaambia, "Amin, amin nawaambia, ninyi mtaona mbingu ikifunguka na malaika wa Mungu wakipanda na kushuka juu ya Mwana wa Adamu.''

***Arusi Huko Kana***

c42 Petro kwa Kiyunani au Kefa kwa Kiaramu maana yake ni kipande cha mwamba

**2** Siku ya tatu kulikuwa na arusi katika mji wa Kana ya Galilaya, naye mama yake Yesu alikuwako huko. 2Yesu pamoja na wanafunzi wake walikuwa wamealikwa arusini pia. 3Divai ilipokwisha, mama yake Yesu akamwambia, "Wameishiwa na divai."

4Yesu akamwambia, ''Mwanamke, nina nini nawe? Saa Yangu haijawadia.''

5Mama Yake akawaambia wale watumishi, ''Lo lote atakalowaambia, fanyeni.''

6Basi ilikuwapo huko mitungi sita iliyotengenezwa kwa mawe kwa ajili ya kujitakasa kwa desturi ya Kiyahudi, kila mtungi ungeweza kuchukua vipipa viwili au vitatu[a].

7Yesu akawaambia wale watumishi, "Ijazeni hiyo mitungi maji.'' Nao wakaijaza ile mitungi mpaka juu.

8Kisha akawaambia, "Sasa choteni hayo maji kidogo, mpelekeeni mkuu wa meza.''

Hivyo wakachota, wakampelekea. 9Yule mkuu wa meza akayaonja yale maji ambayo yalikuwa yamebadilika kuwa divai. Hakujua divai hiyo ilikotoka ingawa wale watumishi waliochota yale maji wao walifahamu. Basi akamwita bwana arusi kando 10akamwambia, "Watu wote hutoa kwanza divai nzuri, kisha huleta ile divai hafifu wageni wakisha kunywa vya kutosha, lakini wewe umeiweka ile nzuri kupita zote mpaka sasa."

11Huu, ndio uliokuwa muujiza wa kwanza Yesu aliofanya huko Kana ya Galilaya. Hivyo Yesu alidhihirisha utukufu Wake na wanafunzi wake wakamwamini.

***Yesu Atakasa Hekalu***

12 Baada ya hayo, Yesu pamoja na mama Yake, ndugu Zake na wanafunzi Wake, walishuka mpaka Kapernaumu wakakaa huko siku chache.

13Ilipokaribia wakati wa Pasaka ya Wayahudi, Yesu alipanda kwenda Yerusalemu. 14Huko hekaluni aliwakuta watu wakiuza ng'ombe, kondoo na njiwa. Nao wabadilisha fedha wakiwa wameketi kwenye meza zao. 15Akatengeneza mjeledi kutokana na kamba, akawafukuza wote kutoka kwenye eneo la hekalu pamoja na kondoo na ng'ombe. Akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadilisha fedha na kuzimwaga fedha zao. 16Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa, "Waondoeni hapa! Mnathubutuje kuifanya

a6 Kipipa kimoja kidogo chenye ujazo wa lita 40.Hivyo kila mtungi ulikuwa na ujazo wa 80 au 120

nyumba ya Baba yangu kuwa mahali pa biashara?''

17Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa imeandikwa: "Wivu wa nyumba Yako utanila.''

18Ndipo Wayahudi wakamwuliza, "Unaweza kutuonyesha ishara gani ili kuthibitisha mamlaka uliyo nayo ya kufanya mambo haya?''

19Yesu akawajibu, "Libomoeni hili hekalu, nami nitalijenga tena kwa siku tatu!''

20Wale Wayahudi wakamjibu, "Hekalu hili
lilijengwa kwa muda wa miaka arobaini na sita,
nawe wasema utalijenga kwa siku tatu?''
21Lakini Yeye, 'hekalu' alilozungumzia ni mwili
Wake. 22Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu,
wanafunzi Wake wakakumbuka yale aliyokuwa amesema. Ndipo wakayaamini Maandiko na yale maneno Yesu aliyokuwa amesema.

23Ikawa Yesu alipokuwa Yerusalemu
kwenye Sikukuu ya Pasaka, watu wengi waliona
ishara na miujiza alizokuwa akifanya,
wakamwamini. 24Lakini Yesu hakujiaminisha
kwao kwa sababu aliwajua wanadamu wote.
25Hakuhitaji ushuhuda wa mtu ye yote kuhusu mtu kwa kuwa alijua yote yaliyokuwa moyoni mwa mtu.

### *Nikodemo Amwendea Yesu Usiku*

**3** Basi palikuwa na mtu mmoja Farisayo, jina lake Nikodemo, mmoja wa Baraza la Wayahudi[a]
lililotawala. 2Huyu alimjia Yesu usiku
akamwambia, "Rabi, tunajua kuwa Wewe ni mwalimu uliyetumwa na Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya miujiza hii uifanyayo Wewe, kama Mungu hayuko pamoja naye.''

3Yesu akamjibu, "Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili.''

4Nikodemo akauliza, "Awezeje mtu kuzaliwa wakati akiwa mzee?" ''Hakika hawezi kuingia mara ya pili kwenye tumbo la mama yake ili azaliwe!"

5Yesu akamwambia, ''Amin, amin
nakuambia, hakuna mtu ye yote anayeweza kuingia katika Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho. 6Mwili huzaa
mwili, lakini Roho huzaa roho. 7Kwa hiyo
usishangae ninapokuambia huna budi 'kuzaliwa
mara ya pili'. 8Upepo huvuma po pote
upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi ukafahamu utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na Roho.''

9Nikodemo akamwuliza, ''Mambo haya yanawezekanaje?''

10Yesu akamwambia, ''Wewe ni mwalimu mashuhuri wa Waisraeli, nawe huelewi mambo
haya? 11Amin, amin, ninakwambia, sisi
tunazungumza lile tunalolijua na tunashuhudia lile tulililoliona. Lakini ninyi watu hamkubali
ushuhuda wetu. 12 Nimewaambia mambo ya
duniani, nanyi hamkuniamini, mtaniaminije basi nitakapowaambia mambo ya mbinguni?
13Hakuna mtu ye yote aliyekwenda mbinguni isipokuwa Yeye aliyeshuka kutoka mbinguni,
yaani, Mwana wa Adamu. 14Kama vile Mose
alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa
juu. 15Ili kila mtu amwaminiye awe na uzima wa
milele.

16''Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na
uzima wa milele. 17Kwa maana Mungu
hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu, bali kwa Yeye ulimwengu upate kuokolewa.
18Ye yote amwaminiye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakumwamini Mwana pekee wa Mungu.
19Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko
nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. 20Kwa
kuwa kila atendaye maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili matendo yake maovu
yasifichuliwe. 21Lakini wale watendao yaliyo
mema huja kwenye nuru, kusudi ionekane wazi kwamba matendo yao yametendeka katika Mungu.''

### *Ushuhuda Wa Yohana Mbatizaji Kuhusu Yesu*

22Baada ya haya, Yesu na wanafunzi wake walikwenda katika nchi ya Uyahudi, nao wakakaa
huko kwa muda na kubatiza. 23Yohana naye
alikuwa akibatiza huko Ainoni karibu na Salimu kwa sababu huko kulikuwa na maji tele. Watu
wazima wakamjia huko ili kubatizwa. 24(Hii ilikuwa
kabla Yohana hajatiwa gerezani). 25Mashindano
yakazuka kati ya baadhi ya wanafunzi wa Yohana na Myahudi mmoja kuhusu suala la desturi ya
kunawa. 26Wakamwendea Yohana
wakamwambia, "Rabi, yule mtu aliyekuwa pamoja nawe ng'mbo ya

[a1] Baraza la Wayahudi, yaani "Sanhedrin" lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la utawala ambalo lilikuwa na wazee 70 pamoja na Kuhani Mkuu.

pili ya Mto Yordani, yule uliyeshuhudia habari
zake, sasa anabatiza na kila mtu anamwendea!”
27Yohana akawajibu, “Hakuna mtu ye yote
awezaye kupata kitu cho chote isipokuwa kile tu
alichopewa kutoka mbinguni. 28Ninyi wenyewe
ni mashahidi wangu kwamba nilisema, ‘Mimi si
Kristo, ila nimetumwa nimtangulie’. 29Bibi arusi
ni wa bwana arusi. Lakini rafiki yake bwana
arusi anayesimama karibu naye na kusikiliza
kutoka kwake, hufurahi sana aisikiapo sauti ya
bwana arusi. Kwa sababu hii furaha yangu
imekamilika. 30Yeye hana budi kuwa mkuu zaidi
na mimi nizidi kuwa mdogo.’’

### *Yeye Aliyetoka Mbinguni*

31“Yeye ajaye kutoka juu yu juu ya yote,
yeye aliye wa duniani ni wa dunia, naye
huzungumza mambo ya duniani. Yeye aliyekuja
kutoka mbinguni, yu juu ya yote. 32Yeye
hushuhudia yale aliyoyaona na kuyasikia, lakini
hakuna ye yote anayekubali ushuhuda Wake.
33Lakini ye yote anayekubali huo ushuhuda
anathibitisha kwamba, Mungu ni kweli. 34Yeye
aliyetumwa na Mungu husema maneno ya
Mungu, kwa kuwa Mungu humtoa Roho pasipo
kipimo. 35Baba anampenda Mwana, naye
ametia vitu vyote mikononi Mwake. 36Ye yote
anayemwamini Mwana ana uzima wa milele,
lakini yeye asiyemwamini Mwana hatauona
uzima, bali ghadhabu ya Mungu itakuwa juu
yake.’’

### *Yesu Azungumza Na Mwanamke Msamaria*

**4** Mafarisayo wakasikia kwamba Yesu alikuwa
anapata na kubatiza wanafunzi wengi zaidi kuliko
Yohana, 2ingawa kwa kweli si Yesu mwenyewe
aliyekuwa akibatiza, ila ni wanafunzi Wake.
3Bwana alipojua mambo haya,
aliondoka Uyahudi akarudi tena Galilaya. 4Wakati
huo ilimbidi apitie Samaria. 5Akafika
kwenye mji mmoja wa Samaria uitwao Sikari,
karibu na lile shamba ambalo Yakobo alimpa
mwanawe Yosefu. 6Huko ndiko kulikokuwa na
kile kisima cha Yakobo. Naye Yesu alikuwa
amechoka kwa kuwa alikuwa ametoka safarini.
Akaketi karibu na hicho kisima. Ilikuwa yapata
saa sita mchana.
7 Mwanamke mmoja Msamaria akaja kuteka
maji, Yesu akamwambia, “Naomba maji
ninywe.’’ 8(Wakati huo wanafunzi Wake
walikuwa wamekwenda mjini kununua chakula.)
9Yule mwanamke akamjibu, ‘‘Wewe ni
Myahudi na mimi ni Msamaria. Yawezekanaje
uniombe nikupe maji ya kunywa?’’ Wayahudi
walikuwa hawashirikiani kabisa na Wasamaria.
10Yesu akajibu akamwambia, ‘‘Kama
ungelijua karama ya Mungu, naye ni nani
anayekuambia, Nipe maji ninywe, wewe
ungelimwomba Yeye, naye angelikupa maji
yaliyo hai.’’
11Yule mwanamke akamjibu, “Bwana,
Wewe huna chombo cha kutekea maji na kisima
hiki ni kirefu. Hayo maji ya uzima utayapata
wapi? 12Kwani Wewe ni mkuu kuliko baba yetu
Yakobo ambaye alitupatia kisima hiki, ambacho
yeye pamoja na watoto wake na mifugo yake
walikitumia?’’
13Yesu akamjibu, “Kila mtu anayekunywa
maji ya kisima hiki, ataona kiu tena. 14Lakini ye
yote anywaye maji nitakayompa, hataona kiu
kamwe. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake
chemchemi ya maji yakibubujika uzima wa
milele.’’
15Yule mwanamke akamwambia, “Bwana,
tafadhali nipe maji hayo ili nisipate kiu tena na
wala nisije tena hapa kuteka maji!”
16Yesu akamjibu, “Nenda ukamwite
mumeo, uje naye hapa.’’
17Yule mwanamke akajibu, “Sina mume.’’
Yesu akamwambia, “Umesema kweli kuwa
huna mume. 18Kwa maana umeshakuwa na
wanaume watano na mwanamume unayeishi
naye sasa si mume wako!’’
19Yule mwanamke akasema, “Bwana,
naona bila shaka Wewe ni nabii. 20Baba zetu
waliabudu kwenye mlima huu, lakini ninyi
Wayahudi mnasema ni lazima tukaabudu huko
Yerusalemu.’’
21Yesu akamjibu, “Mwanamke, niamini,
wakati unakuja ambapo hamtamwabudu Baba
katika mlima huu, wala huko Yerusalemu.
22Ninyi Wasamaria mnaabudu msichokijua. Sisi
Wayahudi tunamwabudu Mungu tunayemjua
kwa sababu wokovu unatoka kwa Wayahudi.
23Lakini saa yaja, tena ipo, ambapo wale
waabuduo halisi, watamwabudu Baba katika
roho na kweli. Watu wanaoabudu namna hii,
ndio Baba anawatafuta. 24Mungu ni Roho na
wote wanaomwabudu imewapasa kumwabudu
katika roho na kweli.’’
25Yule mwanamke akamwambia,
“Ninafahamu kwamba Masiya, aitwaye Kristo,
anakuja. Yeye akija, atatueleza mambo yote.’’
26Yesu akamwambia, “Mimi
ninayezungumza nawe, ndiye Masiya.’’
27Wakati huo wanafunzi wake wakarudi,

wakashangaa sana kumwona akizungumza na mwanamke. Lakini hakuna aliyemwuliza, “Unataka nini kwake?’’ Au “Kwa nini unazungumza naye?’’

**28**Yule mwanamke akaacha mtungi wake, akarudi mjini akawaambia watu, **29**“Njoni mkamwone mtu aliyeniambia kila kitu nilichotenda! Je, yawezekana huyu ndiye Masiya?’’ **30**Basi wakamiminika watu kutoka mjini wakamwendea Yesu.

**31**Wakati huo wanafunzi wake walikuwa wakimsihi, “Rabi, kula angalau cho chote.’’

**32**Lakini Yeye akawajibu, “Mimi ninacho chakula ambacho ninyi hamkifahamu.’’

**33**Basi wanafunzi wakaanza kuulizana, “Kuna mtu ambaye amemletea chakula?’’ **34**Lakini Yesu akawajibu, “Chakula changu ni kufanya mapenzi ya Mungu ambaye amenituma na kuikamilisha kazi yake. **35**Je, ninyi hamsemi, ‘Bado miezi minne tuvune?’ Inueni macho yenu myaangalie mashamba jinsi mazao yalivyo tayari kuvunwa! **36**Mvunaji tayari anapokea mshahara wake, naye anakusanya mazao kwa ajili ya uzima wa milele.Ili yeye apandaye na yeye avunae wafurahi pamoja. **37**Hivyo kule kusema, ‘Mmoja hupanda na mwingine huvuna,’ ni kweli kabisa. **38**Niliwatuma mkavune mazao ambayo hamkupanda, wengine walifanya kazi ngumu, nanyi mmevuna faida ya taabu yao.’’

### *Wasamaria Wengi Waamini*

**39**Wasamaria wengi kutoka katika mji ule wakamwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke alipowaambia kwamba, “Ameniambia kila jambo nililotenda.’’ **40**Hivyo wale Wasamaria walipomjia, wakamsihi akae kwao. Naye akakaa huko siku mbili. **41**Kwa sababu ya neno Lake, watu wengi wakaamini.

**42**Wakamwambia yule mwanamke, “Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu, bali kwa kuwa tumemsikia sisi wenyewe. Tumejua hakika kweli ya kwamba huyu ndiye Kristo, Mwokozi wa ulimwengu.’’

### *Yesu Amponya Mwana Wa Afisa*

**43**Bada ya zile siku mbili, Yesu aliondoka kwenda Galilaya. **44**(Basi Yesu mwenyewe alikuwa amesema kwamba nabii hapati heshima katika nchi yake mwenyewe.) **45**Alipofika Galilaya, Wagalilaya walimkaribisha, kwani walikuwa wameona yale aliyoyatenda huko Yerusalemu wakati wa Sikukuu ya Pasaka. Kwa maana wao pia walikuwa wamehudhuria kwenye hiyo Sikukuu.

**46**HivyoYesu akaja tena mpaka Kana ya Galilaya, kule alikokuwa amebadili maji kuwa divai. Huko kulikuwako na mtu mmoja afisa wa kifalme, ambaye mwanawe alikuwa mgonjwa huko Kapernaumu. **47**Huyo mtu aliposikia kwamba Yesu alikuwa amewasili Galilaya kutoka Uyahudi, alimwendea na kumwomba ili aje kumponya mwanawe, aliyekuwa mgonjwa karibu ya kufa.

**48**Yesu akamwambia, “Ninyi watu msipoona ishara na miujiza kamwe hamtaamini.’’

**49**Yule afisa wa kifalme akamwambia, “Bwana, tafadhali shuka kabla mwanangu hajafa.’’

**50**Yesu akamjibu, “Enenda zako, mwanao yu hai.’’

Yule afisa akaamini yale maneno Yesu aliyomwambia, akaondoka akaenda zake. **51**Alipokuwa bado yuko njiani, akakutana na watumishi wake wakamwambia kwamba mwanawe yu mzima. **52** Akawauliza saa ambayo alianza kupata nafuu. Wakamwambia, “Jana yapata saa saba, homa ilimwacha.’’

**53** Ndipo baba wa huyo mtoto akakumbuka kuwa huo ndio wakati ambapo Yesu alikuwa amemwambia, “Mwanao yu hai.’’ Kwa hiyo yeye, pamoja na wote wa nyumbani mwake wakamwamini Yesu.

**54**Hii ilikuwa ishara ya pili ambayo Yesu alifanya aliporudi Galilaya kutoka Uyahudi.

### *Yesu Amponya Mtu Penye Bwawa La Bethzatha*

**5** Baada ya haya, kulikuwa na Sikukuu ya Wayahudi, naye Yesu akapanda kwenda Yerusalemu. **2**Huko Yerusalemu, karibu na mlango uitwao Mlango wa Kondoo, palikuwa na bwawa moja lililoitwa kwa Kiebrania Bethzatha[a], ambalo lilikuwa limezungukwa na kumbi tano. **3**Hapa palikuwa na idadi kubwa ya wasiojiweza, yaani, vipofu, viwete, na waliopooza, wakingojea maji yatibuliwe, [**4**kwa maana malaika alikuwa akishuka wakati fulani, akayatibua maji na yule aliyekuwa wa kwanza kuingia ndani baada ya maji kutibuliwa alipona ugonjwa wo wote aliokuwa nao.] **5**Mtu mmoja alikuwako huko ambaye alikuwa ameugua kwa miaka thelathini na minane. **6**Yesu alipomwona

---

[a] 2 Bethzatha ni neno la Kiebrania,ambalo maana yanke ni nyumba ya “mizeituni”Mahali pengine limetajwa kama Bethesda kwa Kiaramu,yaani, nyumba ya “huruma” na pengine kama Bethsaida,yaani,nyumba ya “uvuvi.”

akiwa amelala hapo, naye akijua kuwa
amekuwako hapo kwa muda mrefu,
akamwambia, “Je, wataka kuponywa?’’

7Yule mgonjwa akamjibu, “Bwana, mimi
sina mtu wa kuniingiza bwawani maji
yanapotibuliwa. Nami ninapotaka kutumbukia
bwawani, mtu mwingine huingia kabla yangu.’’

8Yesu akamwambia, “Simama, chukua
mkeka wako na uende.’’ 9Mara yule mtu
akapona, akachukua mkeka wake, akaanza
kutembea.

Basi siku hiyo ilikuwa siku ya Sabato. 10Kwa
hiyo Wayahudi wakamwambia yule mtu
aliyeponywa, “Leo ni Sabato, ni kinyume cha
sheria wewe kubeba mkeka wako.’’

11Yeye akawajibu, “Yule mtu aliyeniponya
aliniambia, ‘Chukua mkeka wako na uende.’ ’’

12Wakamwuliza, “Ni mtu gani huyo
aliyekuambia uchukue mkeka wako uende?’’

13Basi yule mtu aliyeponywa hakufahamu ni
nani aliyemponya, kwa sababu Yesu alikuwa
amejiondoa katika ule umati wa watu uliokuwa
hapo.

14Baadaye Yesu akamkuta yule mtu
aliyemponya ndani ya hekaluni na kumwambia,
“Tazama umeponywa, usitenda dhambi tena. La
sivyo, lisije likakupata jambo baya zaidi.’’ 15Yule
mtu akaenda, akawaambia wale Wayahudi
kuwa ni Yesu aliyemponya.

### *Uzima Kupitia Mwana*

16Kwa hiyo Wayahudi wakaanza
kumsumbua, kwa sababu alikuwa anafanya
mambo kama hayo siku ya Sabato. 17Yesu
akawajibu, “Baba yangu anafanya kazi yake
daima hata siku hii ya leo, nami pia ninafanya
kazi.’’ 18Maneno haya yaliwaudhi sana viongozi
wa Wayahudi. Wakajaribu kila njia wapate jinsi
ya kumwua, kwani si kwamba alivunja Sabato
tu, bali alikuwa akimwita Mungu Baba Yake,
hivyo kujifanya sawa na Mungu.

### *Mamlaka Ya Mwana Wa Mungu*

19Yesu akawaambia, Amin, amin
nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo
lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile
analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lo
lote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya hivyo
hivyo. 20Baba ampenda Mwana na
kumwonyesha yale ambayo Yeye Baba
mwenyewe anayafanya, naye atamwonyesha
kazi kuu kuliko hizi ili mpate kushangaa.
21Hakika kama vile Baba awafufuavyo wafu na
kuwapa uzima, vivyo hivyo Mwana huwapa
uzima wale anaopenda. 22Wala Baba
hamhukumu mtu ye yote, lakini hukumu yote
amempa Mwana, 23ili wote wamheshimu
Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Ye
yote asiyemheshimu Mwana, hamheshimu
Baba aliyemtuma.

24‘‘Amin, amin, ninawaambia, ye yote
anayesikia maneno Yangu na kumwamini Yeye
aliyenituma, anao uzima wa milele, naye
hatahukumiwa, bali amepita kutoka mautini, na
kuingia uzimani. 25Amin, amin, nawaambia, saa
yaja, nayo saa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya
Mwana wa Mungu, nao watakaoisikia watakuwa
hai. 26Kama vile Baba alivyo na uzima ndani
Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na
uzima ndani Yake. 27Naye amempa Mwanawe
mamlaka ya kuhukumu kwa kuwa Yeye ni
Mwana wa Adamu.

28“Msishangae kusikia haya, kwa maana
saa inakuja ambapo wale walio makaburini
wataisikia sauti Yake. 29Nao watatoka nje, wale
waliotenda mema watafufuka wapate uzima na
wale waliotenda maovu, watafufuka
wahukumiwe.

### *Shuhuda Kuhusu Yesu*

30Mimi siwezi kufanya jambo lo lote peke
Yangu. Ninavyosikia ndivyo ninavyohukumu,
nayo hukumu Yangu ni ya haki kwa kuwa
sitafuti kufanya mapenzi Yangu mwenyewe, bali
mapenzi Yake Yeye aliyenituma.’’

31“Kama ningejishuhudia Mimi mwenyewe,
ushuhuda Wangu si kweli. 32Lakini yuko
mwingine anishuhudiaye na ninajua kwamba
ushuhuda Wake ni wa kweli.

33“Mlituma wajumbe kwa Yohana, naye
akashuhudia juu ya kweli. 34Si kwamba
naukubali ushuhuda wa mwanadamu, la, bali
ninalitaja hili kusudi ninyi mpate kuokolewa.
35Yohana alikuwa taa iliyowaka na kutoa nuru,
nanyi kwa muda mlichagua kuifurahia nuru
yake.

36“Lakini ninao ushuhuda mkuu zaidi kuliko
wa Yohana. Kazi zile nizifanyazo, zinashuhudia
juu yangu, zile ambazo Baba amenituma
nizikamilishe, naam, ishara hizi ninazofanya,
zinashuhudia kuwa Baba ndiye aliyenituma.
37Naye Baba mwenyewe ameshuhudia juu
Yangu. Hamjapata kamwe kuisikia sauti Yake
wala kuona umbo Lake, 38wala hamna neno
Lake ndani yenu, kwa sababu hamkumwamini
Yeye aliyetumwa naye. 39Ninyi mnachunguza

Maandiko mkidhani ya kuwa ndani yake mna uzima wa milele, maandiko haya ndiyo yanayonishuhudia Mimi. 40Lakini mnakataa kuja Kwangu ili mpate uzima.

41“Mimi sitafuti kutukuzwa na wanadamu. 42Lakini ninajua kwamba hamna upendo wa Mungu mioyoni mwenu. 43Mimi nimekuja kwa Jina la Baba Yangu, nanyi hamnipokei, lakini mtu mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea. 44Ninyi mwawezaje kuamini ikiwa mnapeana utukufu ninyi kwa ninyi, lakini hamna bidii kupata utukufu utokao kwa Mungu?

45“Lakini msidhani kuwa mimi nitawashtaki mbele za Baba, mshtaki wenu ni Mose, ambaye mmemwekea tumaini lenu. 46 Kama mngelimwamini Mose, mngeliniamini na Mimi kwa maana aliandika habari Zangu. 47Lakini ikiwa hamwamini aliyoandika Mose, mtaaminije ninayoyasema?’’

### *Yesu Alisha Watu 5,000*

**6** Baada ya haya, Yesu alikwenda ng'ambo ya Bahari ya Galilaya, ambayo pia huitwa Bahari ya Tiberia. 2Umati mkubwa wa watu uliendelea kumfuata, kwa sababu waliona ishara nyingi za miujiza alizofanya kwa wagonjwa. 3Kisha Yesu akapanda mlimani akaketi huko pamoja na wanafunzi Wake. 4Pasaka ya Wayahudi ilikuwa imekaribia.

5Yesu alipotazama na kuuona ule umati mkubwa wa watu ukimjia, akamwambia Filipo, “Tutanunua wapi mikate ili watu hawa wale?” 6Aliuliza swali hili kumpima, kwa maana alishajua la kufanya.

7Filipo akamjibu, “Hata fedha kiasi cha dinari mia mbili[a], hazitoshi kununua mikate ya kuwapa watu hawa kila mtu apate kidogo.’’

8Mmoja wa wanafunzi wake, aitwaye Andrea, ndugu yake Simoni Petro, akamwambia, 9 “Hapa kuna mvulana mmoja mwenye mikate mitano ya shayiri na samaki wawili wadogo. Lakini hivi vitatosha nini kwa umati wote huu?’’

10Yesu akasema, “Waketisheni watu chini.’’ Palikuwa na majani mengi katika eneo lile, nao watu wakaketi, palikuwa na wanaume 5,000. 11Ndipo Yesu akachukua ile mikate, akamshukuru Mungu na kuwagawia wale watu waliokuwa wamekaa kwa kiasi walichohitaji. Akafanya vivyo hivyo na wale samaki. Kila mtu akapata kadri alivyotaka.

[a]7 Dinari 200 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 200.Mshahara wa kibarua ulikuwa dinari moja kwa siku

12Watu wote walipokwisha kula na kushiba, akawaambia wanafunzi wake, “Kusanyeni vipande vilivyobaki vya ile mikate, kisipotee cho chote.’’ 13Hivyo wakavikusanya wakajaza vikapu kumi na viwili kwa vipande vilivyobaki vya ile mikate mitano na samaki wale wawili wadogo.

14Baada ya watu kuona mwujiza ule Yesu aliofanya, walianza kusema, “Hakika huyu ndiye Nabii ajaye ulimwenguni!’’ 15 Yesu akijua kwamba walitaka kuja kumfanya awe mfalme wao, kwa nguvu, akajitenga nao akaenda milimani peke Yake.

### *Yesu Atembea Juu Ya Maji*

16Ilipofika jioni, wanafunzi wake walitelemka kwenda baharini. 17Wakaingia kwenye mashua, wakaanza kuvuka bahari kwenda Kapernaumu. Wakati huu kulikuwa tayari giza na Yesu alikuwa hajajumuika nao. 18Bahari ikachafuka kwa sababu upepo mkali ulikuwa unavuma. 19Wanafunzi walipokuwa wamekwenda mwendo wa karibu maili tatu au nne[b], walimwona Yesu akitembea juu ya maji akikaribia mashua, wakaogopa sana. 20Lakini Yesu akawaambia, “Ni mimi, msiogope.’’ 21Ndipo kwa furaha wakamkaribisha kwenye mashua, na mara wakafika walikokuwa wanakwenda.

### *Watu Wanamtafuta Yesu*

22Siku iliyofuata, wale watu waliokuwa wamebaki ng'ambo ya pili waliona kwamba palikuwepo na mashua moja tu na kwamba Yesu hakuwa ameondoka pamoja na wanafunzi Wake, ila walikuwa wameondoka peke yao. 23Lakini zikaja mashua nyingine kutoka Tiberia zikafika karibu na mahali pale walipokula mikate baada ya Yesu kumshukuru Mungu. 24Mara wale watu wakatambua kwamba Yesu hakuwepo hapo, wala wanafunzi wake. Wakaingia kwenye mashua hizo, wakaenda Kapernaumu ili kumtafuta Yesu.

### *Yesu Ni Mkate Wa Uzima*

25Walipomkuta Yesu ng'ambo ya bahari wakamwuliza, “Rabi, umefika lini huku?’’

26Yesu akawajibu, “Amin, amin nawaambia, ninyi hamnitafuti kwa kuwa mliona ishara na miujiza, bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba. 27Msishughulikie chakula kiharibikacho, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele, ambacho Mwana wa Adamu

[b]19 Maili tatu au nne ni kama kilomita 5 au 6

atawapa. Yeye ndiye ambaye Mungu Baba
amemtia muhuri.''

28Ndipo wakamwuliza, "Tufanye nini ili
tupate kuitenda kazi ya Mungu?"

29Yesu akawajibu, "Kazi ya Mungu ndiyo hii:
Mwaminini Yeye aliyetumwa Naye.''

30Hivyo wakamwuliza, "Utafanya ishara gani
ya mwujiza, ili tuione tukuamini? Utafanya
jambo gani? 31Baba zetu walikula mana
jangwani, kama ilivyoandikwa, 'Aliwapa mikate
kutoka mbinguni ili wale.' "

32Yesu akawaambia, "Amin, amin,
nawaambia, si Mose aliyewapa mikate kutoka
mbinguni, bali Baba Yangu ndiye anawapa
mkate wa kweli kutoka mbinguni. 33Kwa maana
mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka
mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.''

34Wakamwambia, "Bwana, kuanzia sasa
tupatie huo mkate sikuzote.''

35Yesu akawaambia, "Mimi ndimi mkate wa
uzima. Yeye ajaye Kwangu, hataona njaa
kamwe na yeye aniaminiye, hataona kiu kamwe.
36Lakini kama nilivyowaambia, mmeniona lakini
bado hamwamini. 37Wale wote anipao Baba
watakuja Kwangu na ye yote ajaye Kwangu,
sitamfukuzia nje kamwe. 38 Kwa kuwa
nimeshuka kutoka mbinguni si ili kufanya
mapenzi Wangu, bali mapenzi yake Yeye
aliyenituma. 39Haya ndiyo mapenzi yake Yeye
aliyenituma, kwamba, nisimpoteze hata mmoja
wa wale alionipa, bali niwafufue siku ya mwisho.
40Kwa maana mapenzi ya Baba yangu ni
kwamba kila mmoja amtazamaye, Mwana na
kumwamini awe na uzima wa milele, nami
nitawafufua siku ya mwisho.''

41 Wayahudi wakaanza kunung'unika kwa
kuwa alisema, "Mimi ndimi mkate ulioshuka
kutoka mbinguni.'' 42Wakasema, "Huyu si Yesu,
mwana wa Yosefu, ambaye baba yake na
mama yake tunawajua? Anawezaje basi sasa
kusema, ''Nimeshuka kutoka mbinguni?''

43Hivyo Yesu akawaambia, "Acheni
kunung'unikiana ninyi kwa ninyi. 44Hakuna mtu
awezaye kuja kwangu kama asipovutwa na Baba
aliyenituma, nami nitamfufua siku ya mwisho.
45Imeandikwa katika manabii, 'Wote
watafundishwa na Mungu.' Ye yote amsikilizaye
Baba na kujifunza kutoka Kwake, huyo huja
Kwangu. 46Hakuna mtu ye yote aliyemwona Baba
isipokuwa Yeye atokaye kwa Mungu, Yeye ndiye
peke yake aliyemwona Baba. 47Amin, amin,
nawambia, yeye anayeamini anao uzima wa
milele. 48Mimi ni mkate wa uzima.
49Baba zenu walikula mana jangwani, lakini
wakafa. 50Lakini hapa kuna mkate utokao
mbinguni, ambao mtu ye yote akiula, hatakufa.
51Mimi ni mkate wa uzima ule uliotoka
mbinguni. Mtu ye yote akiula mkate huu, ataishi
milele. Mkate huu ni mwili wangu, ambao
nitautoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.''

52Ndipo Wayahudi wakaanza kuhojiana
vikali wao kwa wao wakisema, "Mtu huyu
awezaje kutupatia mwili wake tuule?''

53Hivyo Yesu akawaambia, "Amin, amin,
nawaambia, msipoula mwili wa Mwana wa
Adamu na kuinywa damu Yake, hamna uzima
ndani yenu. 54Mtu ye yote aulaye mwili wangu
na kunywa damu yangu, anao uzima wa milele.
Nami nitamfufua siku ya mwisho. 55Kwa maana
mwili wangu ni chakula cha kweli na damu
yangu ni kinywaji cha kweli. 56Ye yote alaye
mwili wangu na kunywa damu yangu, atakaa
ndani yangu nami nitakaa ndani yake. 57 Kama
vile Baba aliye hai alivyonituma Mimi, na kama
nami ninavyoishi kwa sababu ya Baba, hivyo
anilaye mimi ataishi kwa sababu yangu. 58Huu
ndio mkate ushukao kutoka mbinguni, si kama
ule mkate baba zenu waliokula nao wakafa.
Lakini yeye aulaye mkate huu ataishi milele.''
59Yesu alisema maneno haya alipokuwa
akifundisha katika sinagogi huko Kapernaumu.

### *Wafuasi Wengi Wamwacha Yesu*

60Wengi wa wafuasi Wake waliposikia
jambo hili wakasema, "Mafundisho haya ni
magumu. Ni nani awezaye kuyapokea?''

61Yesu alipojua kwamba wafuasi Wake
wananung'unika kuhusu mafundisho Yake,
akawaambia, "Je, jambo hili limewaudhi?
62Ingekuwaje basi kama mngemwona Mwana
wa Adamu akipaa kwenda Zake huko alipokuwa
kwanza? 63Roho ndiye atiaye uzima, mwili
haufai kitu. Maneno haya niliyowaambia ni
Roho tena ni uzima. 64Lakini baadhi yenu
hamwamini.'' Kwa maana Yesu alifahamu tangu
mwanzo wale ambao hawangemwamini
miongoni mwao na yule ambaye angemsaliti.
65Akaendelea kusema, ''Hii ndiyo sababu
niliwaambia kwamba hakuna mtu awezaye kuja
kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba Yangu.''

66Tangu wakati huo wafuasi Wake wengi
wakarejea nyuma wakaacha kumfuata.

67 Hivyo Yesu akawauliza wale wanafunzi
Wake kumi na wawili, ''Je, ninyi pia mnataka
kuondoka?''

68Simoni Petro akamjibu, ''Bwana, tuondoke

twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. 69Tunaamini na kujua kuwa Wewe ndiwe Kristo[c] Mwana wa Mungu aliye hai.''

70Ndipo Yesu akajibu, ''Je, sikuwachagua ninyi kumi na wawili? Lakini mmoja wenu ni ibilisi.'' 71(Hapa alikuwa anasema juu ya Yuda, mwana wa Simoni Iskariote. Ingawa alikuwa mmoja wa wale kumi na wawili, ndiye ambaye baadaye angemsaliti Yesu.)

### *Kutokuamini Kwa Ndugu Zake Yesu*

**7** Baada ya mambo haya, Yesu alikwenda sehemu mbalimbali za Galilaya. Hakutaka kwenda Uyahudi kwa sababu Wayahudi huko walitaka kumwua. 2Sikukuu ya Vibanda ya Wayahudi ilikuwa imekaribia. 3Hivyo ndugu zake Yesu wakamwambia, "Ondoka hapa uende Uyahudi ili wanafunzi Wako wapate kuona miujiza unayofanya. 4 Mtu anayetaka kujulikana hafanyi mambo yake kwa siri. Kama unafanya mambo haya jionyeshe kwa ulimwengu.'' 5Hata ndugu zake mwenyewe hawakumwamini. 6Yesu akawaambia, "Wakati wangu bado haujawadia, lakini wakati wenu upo sikuzote. 7Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi, lakini unanichukia Mimi kwa sababu ninawashuhudia kwamba matendo yao ni maovu. 8Ninyi nendeni kwenye Sikukuu, lakini mimi sitahudhuria Sikukuu hii kwa sababu wakati wangu haujawadia.'' 9Akiisha kusema hayo, akabaki Galilaya.

### *Yesu Kwenye Sikukuu Ya Vibanda*

10Lakini ndugu zake walipokwisha kuondoka kwenda kwenye Sikukuu, Yeye pia alikwenda lakini kwa siri. 11Wayahudi walikuwa wakimtafuta huko kwenye Sikukuu na kuulizana, "Yuko wapi huyu Mtu?''

12Kulikuwa na minong'ono iliyoenea kumhusu Yesu katika umati wa watu, wakati wengine wakisema, "Ni Mtu mwema,'' wengine walikuwa wakisema, "La, Yeye anawadanganya watu.'' 13Lakini hakuna mtu ye yote aliyemsema waziwazi kumhusu kwa sababu ya kuwaogopa Wayahudi.

### *Yesu Afundisha Kwenye Sikukuu***.**

14Ilipokaribia katikati ya Sikukuu, Yesu alipanda kwenda hekaluni na kuanza kufundisha. 15Wayahudi wakastaajabia mafundisho Yake wakasema, "Mtu huyu amepataje kujua mambo haya bila kufundishwa?''

16Ndipo Yesu akawajibu, "Mafundisho Yangu si Yangu mwenyewe, bali yanatoka kwake Yeye aliyenituma. 17Mtu ye yote akipenda kufanya mapenzi ya Mungu, atajua kama mafundisho Yangu yanatoka kwa Mungu au ninasema kwa ajili yangu mwenyewe. 18Wale wanenao kwa ajili yao wenyewe hufanya hivyo kwa kutaka utukufu wao wenyewe. Lakini Yeye atafutaye utukufu wa yule aliyemtuma ni wa kweli, wala hakuna uongo ndani yake. 19Je, Mose hakuwapa ninyi sheria? Lakini hakuna hata mmoja wenu anayeishika hiyo sheria. Kwa nini mnataka kuniua?''

20Ule umati wa watu ukamjibu, "Wewe una pepo mchafu! Ni nani anayetaka kukuua?''

21Yesu akawajibu, "Nimefanya muujiza mmoja na nyote mkastaajabu. 22Lakini kwa kuwa Mose aliwaamuru tohara (ingawa kwa kweli haikutoka kwa Mose bali kwa baba zenu wakuu,) mnamtahiri mtoto hata siku ya Sabato. 23Ikiwa mtoto aweza kutahiriwa siku ya Sabato kusudi sheria ya Mose isivunjwe, kwa nini mnanikasirikia kwa kumponya mtu mzima siku ya Sabato? 24Acheni kuhukumu mambo kwa jinsi mnavyoona tu, bali hukumuni kwa haki.''

### *Je, Yesu Ndiye Kristo?*

25Ndipo baadhi ya watu wa Yerusalemu wakawa wanasema, "Tazameni, huyu si yule mtu wanayetaka kumwua? 26Mbona yuko hapa anazungumza hadharani na wala hawamwambii neno lo lote? Je, inawezekana viongozi wanafahamu kuwa huyu ndiye Kristo? 27Tunafahamu huyu mtu anakotoka, lakini Kristo atakapokuja, hakuna ye yote atakayejua atokako.''

28Ndipo Yesu, akaendelea kufundisha hekaluni, akisema, ''Ninyi mnanifahamu na kujua nitokako. Mimi sikuja kwa ajili Yangu mwenyewe, bali Yeye aliyenituma ni wa kweli na ninyi hamumjui. 29 Mimi namjua kwa kuwa nimetoka Kwake, naye ndiye aliyenituma.''

30Ndipo wakatafuta kumkamata, lakini hakuna mtu ye yote aliyethubutu kumshika kwa sababu saa yake ilikuwa bado haijawadia. 31Nao watu wengi wakamwamini, wakasema, "Je, Kristo atakapokuja, atafanya miujiza mikuu zaidi kuliko aliyoifanya Mtu huyu?''

### *Maaskari Wanatumwa Kumkamata Yesu*

32Mafarisayo wakasikia watu wakinong'ona

[c]69 Kristo maana yake Masiya, yaani, Mpakwa (Aliyetiwa) Mafuta

mambo kama hayo kuhusu Yesu, ndipo wao
pamoja na viongozi wa makuhani, wakatuma
walinzi wa hekalu waende kumkamata.

33 Yesu akasema, "Mimi bado niko pamoja
nanyi kwa kitambo kidogo, kisha nitarudi Kwake
Yeye aliyenituma. 34Mtanitafuta, lakini
hamtaniona, nami niliko, ninyi hamwezi kuja.''

35Wayahudi wakaulizana wao kwa wao,
"Huyu mtu anataka kwenda wapi ambako
hatuwezi kumfuata? Je, anataka kwenda kwa
Wayunani ambako baadhi ya watu wetu
wametawanyikia, akawafundishe Wayunani?
36Yeye ana maana gani anaposema,
'Mtanitafuta lakini hamtaniona na huko
nitakapokuwa ninyi hamwezi kuja?' ''

### *Mito Ya Maji Ya Uzima*

37Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile
kuu, wakati Yesu akiwa amesimama huko,
akapaza sauti Yake akasema, "Kama mtu ye
yote anaona kiu na aje Kwangu anywe. 38Ye
yote aniaminiye Mimi, kama maandiko
yasemavyo, vijito vya maji ya uzima vitatiririka
ndani mwake.'' 39Yesu aliposema haya
alimaanisha Roho Mtakatifu ambaye wote
waliomwamini wangempokea, kwani mpaka
wakati huo, Roho alikuwa hajatolewa, kwa kuwa
Yesu alikuwa bado hajatukuzwa.

### *Mgawanyiko Miongoni Mwa watu.*

40Waliposikia maneno hayo, baadhi ya watu
miongoni mwa ule umati wakasema, "Hakika
huyu ndiye yule Nabii.''

41Wengine wakasema, "Huyu ndiye Kristo!''
Lakini wengine wakauliza, "Je, Kristo kwao ni
Galilaya? 42Je, Maandiko hayasemi kwamba
Kristo atakuja kutoka katika jamaa ya Daudi na
kutoka Bethlehemu, mji alioishi Daudi?'' 43Kwa
hiyo watu wakagawanyika kwa ajili ya Yesu.
44Baadhi yao walitaka kumkamata, lakini
hakuna aliyethubutu kumgusa.

### *Kutokuamini Kwa Viongozi Wa Wayahudi*

45Hatimaye wale walinzi wa hekalu wakarudi
kwa viongozi wa makuhani na Mafarisayo
waliokuwa wamewatuma ili kumkamata Yesu,
wakaulizwa, "Mbona hamkumkamata?''

46Wale walinzi wakajibu, "Kamwe hajanena
mtu ye yote kama Yeye anenavyo.''

47Mafarisayo wakajibu, "Je, nanyi pia
mmedanganyika? 48Je, kuna kiongozi ye yote
au mmoja wa Mafarisayo ambaye
amemwamini? 49Lakini huu umati wa watu
wasiojua Sheria ya Mose, wamelaaniwa.''

50Ndipo Nikodemo, yule aliyekuwa
amemwendea Yesu siku moja usiku, ambaye
alikuwa mmoja wao akauliza, 51"Je, sheria zetu
zinaturuhusu kumhukumu mtu kabla ya
kumsikiliza na kufahamu alilotenda?''

52Wakamjibu, "Je, wewe pia unatoka
Galilaya? Chunguza nawe utaona kwamba
hakuna nabii atokae Galilaya!'' [53Kisha
wakaondoka, kila mtu akarudi nyumbani kwake].

### *Mwanamke Aliyefumaniwa Akizini*

**8** Lakini Yesu akaenda katika Mlima wa Mizeituni.
2Alfajiri na mapema Yesu akaja tena hekaluni, watu
wote wakakusanyika,
akakaa akaanza kuwafundisha. 3Walimu wa
sheria na Mafarisayo wakamleta mwanamke
mmoja aliyefumaniwa akizini. Wakamsimamisha
katikati ya umati wa watu wote. 4Wakamwambia
Yesu, "Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa
akizini. 5Katika sheria, Mose alituamuru
kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii,
mpaka wafe. Sasa Wewe wasemaje?''
6Walimwuliza swali hili kama mtego ili wapate
sababu ya kumshtaki.

Lakini Yesu akainama akaanza kuandika
ardhini kwa kidole Chake. 7Walipoendelea
kumwulizauliza akainuka, akawaambia, "Kama
kuna mtu ye yote miongoni mwenu ambaye
hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia
jiwe.'' 8Akainama tena na kuandika ardhini.

9Waliposikia haya, wakaanza kuondoka
mmoja mmoja, wakianzia wazee, hadi Yesu
akabaki peke Yake na yule mwanamke akiwa
amesimama mbele Yake. 10Yesu akainuka na
kumwambia, "Wako wapi wale waliokuwa
wanakuhukumu kuwa mwenye hatia?''

11Yule mwanamke akajibu, "Hakuna hata
mmoja Bwana.''

Yesu akamwambia, "Hata Mimi
sikuhukumu. Nenda zako, kuanzia sasa
usitende dhambi tena.''

### *Yesu Nuru Ya Ulimwengu*

12Kisha Yesu akasema nao tena
akawaambia, "Mimi ni nuru ya ulimwengu. Mtu
ye yote akinifuata hatatembea gizani kamwe,
bali atakuwa na nuru ya uzima."

13 Mafarisayo wakamwambia, "Ushuhuda
Wako haukubaliki kwa kuwa unajishuhudia
mwenyewe.''

14Yesu akawajibu, "Hata kama najishuhudia
mwenyewe, ushuhuda Wangu ni kweli kwa

sababu najua nilikotoka na ninakokwenda.
Lakini ninyi hamjui nilikotoka wala
ninakokwenda. 15Ninyi mnahukumu kwa kufuata
vipimo vya kibinadamu, Mimi simhukumu mtu ye
yote. 16Lakini hata kama nikihukumu, hukumu
zangu ni sahihi kwa sababu sitoi hukumu yangu,
bali Mimi pamoja na Baba aliyenituma.
17Imeandikwa katika Sheria yenu kwamba,
ushahidi wa watu wawili ni thabiti. 18Mimi
najishuhudia mwenyewe, naye Baba
aliyenituma hunishuhudia''.

19Ndipo wakamwuliza, "Huyo Baba yako
yuko wapi?"

Yesu akawajibu, "Ninyi hamnifahamu Mimi
ni nani, wala hamumfahamu Baba yangu. Kama
mngenifahamu Mimi, mngemfahamu pia na
Baba Yangu." 20Yesu alisema maneno haya
alipokuwa akifundisha katika chumba cha
hazina hekaluni. Lakini hakuna mtu
aliyemkamata kwa kuwa saa Yake ilikuwa
haijawadia. Yesu akasema, 'Niendako Mimi
ninyi hamwezi kufika.'

### *Yesu Atabiri Kifo chake Mwenyewe*

21 Yesu akawaambia tena, "Ninaenda
zangu, nanyi mtanitafuta, lakini mtakufa katika
dhambi zenu. Niendako ninyi hamwezi kuja.''

22Ndipo wale Wayahudi wakasema, "Je,
atajiua? Je, hii ndiyo sababu amesema,
'Niendako Mimi ninyi hamwezi kuja?'

23Akawaambia, ''Ninyi mmetoka chini, mimi
nimetoka juu. Ninyi ni wa ulimwengu huu, mimi
si wa ulimwengu huu. 24Niliwaambia kuwa
mtakufa katika dhambi zenu, kwa maana
msipoamini ya kwamba 'Mimi Ndiye,' mtakufa
katika dhambi zenu.''

25Wakamwuliza, "Wewe ni nani?''

Naye Yesu akawajibu, ''Mimi ndiye yule
ambaye nimekuwa nikiwaambia tangu mwanzo.
26Nina mambo mengi ya kusema juu yenu na
mengi ya kuwahukumu. Lakini Yeye aliyenituma
ni wa kweli, nami nanena na ulimwengu
niliyoyasikia kutoka Kwake''

27Hawakuelewa kuwa alikuwa akiwaambia juu
ya Baba Yake wa Mbinguni. 28Kisha Yesu
akawaambia, "Mtakapokwisha kumwinua juu
Mwana wa Adamu, ndipo mtakapojua kuwa, 'Mimi
ndiye Yule niliyesema na kwamba Mimi sitendi
jambo lo lote peke Yangu bali ninasema yale tu
ambayo Baba Yangu amenifundisha. 29Yeye
aliyenituma yu pamoja nami, hajaniacha, kwa
kuwa sikuzote nafanya mapenzi Yake.'' 30Wengi
waliomsikia Yesu akisema maneno
haya wakamwamini.

### *Wanafunzi Wa Kweli*

31Kisha Yesu akawaambia wale Wayahudi
waliomwamini, "Kama mkidumu katika maneno
Yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli.
32Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka
huru.''

33Wao wakamjibu, "Sisi tu wazao wa
Abrahamu, nasi hatujawa watumwa wa mtu ye
yote. Wawezaje kusema kwamba tutawekwa
huru?''

34Yesu akajibu, ''Amin, amin, nawaambia,
kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.
35Mtumwa hakai nyumbani anakotumika
sikuzote, lakini mwana hukaa nyumbani daima.
36Hivyo Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru
kweli kweli. 37Ninajua ya kuwa ninyi ni wazao
wa Abrahamu, lakini mnatafuta wasaa wa
kuniua kwa sababu ndani yenu hamna nafasi ya
neno Langu. 38Ninasema yale niliyoyaona
mbele za Baba yangu, nanyi inawapa kufanya
yale mliyosikia kutoka kwa baba yenu.''

### *Yesu Na Abrahamu*

39Wakajibu, ''Baba yetu ni Abrahamu.''

Yesu akawaambia, ''Kama mngekuwa
wazao wa Abrahamu mngefanya mambo yale
aliyofanya Abrahamu. 40Lakini sasa ninyi
mnatafuta kuniua, mtu ambaye nimewaambia
kweli ile niliyosikia kutoka kwa Mungu, Abrahamu
hakufanya jambo la namna hii. 41Ninyi mnafanya
mambo afanyayo baba yenu''.

Wakamjibu, ''Sisi si watoto wa haramu,
tunaye Baba mmoja ndiye Mungu.''

42Yesu akawaambia, ''Kama Mungu
angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa
maana nilitoka kwa Mungu na sasa niko hapa.
Sikuja kwa ajili Yangu mwenyewe, ila Yeye
alinituma. 43 Kwa nini hamwelewi
ninayowaambia? Ni kwa sababu hamwezi
kusikia nisemacho. 44Ninyi ni watoto wa baba
yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya
baba yenu. Yeye alikuwa mwuaji tangu
mwanzo, wala hakushikana na kweli maana
hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo
husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana
yeye ni mwongo na baba wa huo uongo.
45Lakini kwa sababu nimewaambia kweli
hamkuniamini! 46 Je, kuna ye yote miongoni
mwenu awezaye kunithibitisha kuwa mwenye
dhambi? Kama nawaambia yaliyo kweli, mbona
hamniamini? 47Yeye atokaye kwa Mungu

husikia kile Mungu asemacho. Sababu ya ninyi
kutosikia ni kwa kuwa hamtokani na Mungu.''

### *Maelezo Ya Yesu Kuhusu Yeye Mwenyewe*

48Wayahudi wakamjibu Yesu, "Je, hatuko
sahihi tunaposema ya kwamba Wewe ni
Msamaria na ya kwamba una pepo mchafu?"

49Yesu akawajibu, "Mimi sina pepo mchafu,
bali ninamheshimu Baba Yangu, nanyi
mnanidharau. 50Lakini Mimi sitafuti utukufu
Wangu mwenyewe, bali yuko anayetaka
kunitukuza, naye ndiye mwamuzi. 51Amin, amin,
nawaambia, mtu ye yote akilitii Neno Langu
hataona mauti milele.''

52Ndipo Wayahudi wakamwambia, ''Sasa
tumejua kwamba una pepo mchafu. Ikiwa
Abrahamu alikufa na vivyo hivyo manabii, nawe
unasema 'Mtu akitii Neno Langu hatakufa?'
53Je, Wewe ni mkuu kuliko baba yetu Abrahamu
ambaye alikufa na manabii ambao nao pia
walikufa? Hivi Wewe unajifanya kuwa nani?''

54Yesu akawajibu, "Kama nikijitukuza
utukufu wangu hauna maana. Baba yangu, huyo
ambaye ninyi mnadai kuwa ni Mungu wenu,
ndiye anitukuzaye Mimi. 55Ingawa hamkumjua,
Mimi ninamjua. Kama ningesema simjui,
ningekuwa mwongo kama ninyi, lakini Mimi
ninamjua na ninalitii Neno Lake. 56Baba yenu
Abrahamu alishangilia kwamba angaliiona siku
Yangu, naye akaiona na akafurahi.''

57Wayahudi wakamwambia, "Wewe
hujatimiza hata miaka hamsini, Wewe wasema
umemwona Abrahamu?''

58Yesu akawaambia, ''Amin, amin,
nawaambia, kabla Abrahamu hajakuwako, 'Mimi
niko.' '' 59Ndipo wakaokota mawe ili kumpiga,
lakini Yesu akajificha, naye akatoka hekaluni.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyezaliwa Kipofu*

**9** Yesu alipokuwa akipita, akamwona mtu
aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa.
2Wanafunzi Wake wakamwuliza, "Rabi, ni nani
aliyetenda dhambi, ni huyu mtu au wazazi wake
hata azaliwe kipofu?''

3Yesu akawajibu, "Huyu mtu wala wazazi
wake hawakutenda dhambi. Alizaliwa kipofu ili
kazi za Mungu zidhihirishwe katika maisha yake.
4Yanipasa kuzifanya kazi zake Yeye aliyenituma
wakati bado ni mchana, kwa kuwa usiku waja
ambapo hakuna mtu awezaye kufanya kazi.
5Wakati niko ulimwenguni, Mimi ni nuru ya
ulimwengu.''

6Baada ya kusema haya, akatema mate
ardhini, akatengeneza tope kwa mate na
kumpaka yule mtu kipofu machoni. 7Kisha
akamwambia, "Nenda ukanawe katika bwawa la
Siloamu." (Siloamu, maana yake ni aliyetumwa.)
Ndipo yule kipofu akaenda, akanawa, naye
akarudi akiwa anaona.

8Majirani zake na wale wote waliokuwa
wamemwona hapo awali akiombaomba
wakaanza kuuliza, "Je, huyu si yule aliyekuwa
akiketi akiombaomba?" 9Wengine wakasema,
"Ndiye."

Wengine wakasema, "Siye, bali
wamefanana.''

Lakini yeye akawaambia, "Mimi ndiye''.

10Wakamwuliza, "Basi macho yako
yalifumbuliwaje?''

11Yeye akawajibu, "Yule mtu aitwaye Yesu
alitengeneza tope, akanipaka machoni mwangu,
naye akaniambia nenda ukanawe katika Bwawa
la Siloamu, ndipo nikanawa nami nikapata
kuona!''

12Wale wakamwuliza, "Yeye huyo mtu yuko
wapi?''

Akawajibu, "Sijui.''

### *Mafarisayo Wachunguza Kuponywa Kwa Kipofu*

13Wakamleta kwa Mafarisayo yule mtu
aliyekuwa kipofu hapo awali. 14Basi siku hiyo
Yesu alipotengeneza tope na kuyafungua
macho ya huyo mtu ilikuwa Sabato.
15Mafarisayo nao wakaanza kumwuliza
alivyopata kuponywa. Naye akawaambia,
"Alinipaka tope kwenye macho yangu, nikanawa
na sasa ninaona.''

16Baadhi ya Mafarisayo wakasema, ''Huyu
mtu hatoki kwa Mungu, kwa sababu hashiki
Sabato.''

Lakini wengine wakasema, "Awezaje mtu
mwenye dhambi kufanya miujiza kama hii?''
Wakagawanyika.

17Hivyo wakamwambia tena yule mtu
aliyekuwa kipofu, "Wewe ndiwe uliyefunguliwa
macho, wasemaje kuhusu mtu huyo?'' Maana
macho yako ndiyo yaliyofunguliwa.

Yeye akawajibu, "Yeye ni nabii.''

18Wale Wayahudi hawakuamini ya kuwa mtu
huyo alikuwa kipofu, akapata kuona, mpaka
walipowaita wazazi wake. 19Wakawauliza, "Je,
huyu ni mtoto wenu, ambaye mnasema alizaliwa
kipofu? Imekuwaje basi sasa anaona?''

20Wazazi wake wakajibu, "Tunajua ya kuwa
huyu ni mtoto wetu na ya kuwa alizaliwa kipofu.

[21]Lakini sisi hatujui ni kwa jinsi gani kwamba
sasa anaona, wala hatujui ni nani aliyemfungua
macho yake. Mwulizeni, yeye ni mtu mzima na
anaweza kujieleza mwenyewe.'' [22]Wazazi wake
walisema hivi kwa sababu waliwaogopa
Wayahudi kwani walikuwa wamekubaliana kuwa
mtu ye yote atakayemkiri Yesu kuwa ndiye
Kristo atafukuzwa kutoka katika sinagogi. [23]Kwa
hiyo wazazi wake wakasema, "Yeye ni mtu
mzima. Mwulizeni.''

[24]Hivyo kwa mara ya pili wakamwita yule
aliyekuwa kipofu, nao wakamwambia, "Mpe
Mungu utukufu! Sisi tunafahamu kuwa mtu huyu
aliyekuponya ni mwenye dhambi.''

[25]Akawajibu, "Mimi sijui kama Yeye ni
mwenye dhambi. Lakini jambo moja ninalojua,
nilikuwa kipofu na sasa ninaona.''

[26]Wakamwuliza, "Alikufanyia nini?
Aliyafumbuaje macho yako?''

[27]Akawajibu, "Tayari nimekwisha
kuwaambia, nanyi hamtaki kunisikiza. Mbona
mnataka kusikia tena? Je, ninyi nanyi mnataka
kuwa wanafunzi Wake?''

[28]Ndipo wakamtukana na kusema, "Wewe
ndiwe mwanafunzi Wake, Sisi ni wanafunzi wa
Mose. [29]Tunajua kwamba Mungu alisema na
Mose, lakini kwa habari ya mtu huyu hatujui
atokako.''

[30]Yule mtu akawajibu, ''Hili ni jambo la
ajabu! Hamjui anakotoka, naye amenifungua
macho yangu! [31] Tunajua ya kuwa Mungu
hawasikilizi wenye dhambi, lakini huwasikiliza
wote wanaomcha na kumtii. [32] Tangu kuumbwa
kwa ulimwengu hatujasikia kwamba mtu
amemponya ye yote aliyekuwa kipofu. [33]Kama
huyu mtu hakutoka kwa Mungu, asingeweza
kufanya lo lote.''

[34]Wao wakamjibu, ''Wewe ulizaliwa katika
dhambi kabisa, nawe unajaribu kutufundisha?''
Wakamfukuzia nje.

### *Upofu Wa Kiroho*

[35]Yesu aliposikia kuwa wamemfukuzia nje
yule mtu aliyemfumbua macho, alimkuta
akamwuliza, "Je, unamwamini Mwana wa
Adamu?''

[36]Yule mtu akamjibu, "Yeye ni nani ili nipate
kumwamini, niambie ili nipate kumwamini.''

[37]Yesu akamjibu, "Umekwisha kumwona,
naye anayezungumza nawe Ndiye.''

[38] Yule mtu akasema, "Bwana, naamini.''
Naye akamwabudu.

[39]Yesu akasema, "Nimekuja ulimwenguni
humu kwa ajili ya kuhukumu, ili wale walio
vipofu wapate kuona, nao wale wanaoona,
wawe vipofu.''

[40]Baadhi ya Mafarisayo waliokuwa karibu
naye wakamsikia na kumwambia, "Je, kweli sisi
ni vipofu?''

[41] Yesu akawajibu, "Kama mngekuwa
vipofu kweli, msingekuwa na hatia ya dhambi,
lakini kwa kuwa mnasema, 'Tunaona,' basi mna
hatia.''

### *Mchungaji Mwema*

**10** "Amin, amin, nawaambia, yeye asiyeingia
katika zizi la kondoo kwa kupitia kwenye lango,
lakini akwea kuingia ndani
kwa njia nyingine, ni mwivi na mnyang'anyi.
[2]Yeye anayeingia kwa kupitia kwenye lango
ndiye mchungaji wa kondoo. [3]Mlinzi
humfungulia lango na kondoo huisikia sauti
yake. Huwaita kondoo wake kwa majina yao na
kuwatoa nje ya zizi. [4] Akiisha kuwatoa wote nje,
hutangulia mbele yao na kondoo humfuata kwa
kuwa wanaijua sauti yake. [5]Lakini kondoo
hawatamfuata mgeni bali watamkimbia, kwa
sababu hawaijui sauti ya mgeni.'' [6]Yesu alitumia
mfano huu, lakini wao hawakuelewa hayo
aliyokuwa akiwaambia.

[7]Kwa hiyo Yesu akasema nao tena
akawaambia, "Amin, amin, nawaambia, Mimi
ndimi lango la kondoo. [8]Wote walionitangulia ni
wevi na wanyang'anyi, lakini kondoo
hawakuwasikia. [9]Mimi ndimi lango, ye yote
anayeingia zizini kwa kupitia Kwangu ataokoka,
ataingia na kutoka, naye atapata malisho.
[10]Mwivi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi
nimekuja ili wapate uzima kisha wawe nao tele.

[11]''Mimi ndimi Mchungaji Mwema.
Mchungaji Mwema huutoa uhai Wake kwa ajili
ya kondoo. [12]Mtu wa kuajiriwa ambaye kondoo
si mali yake, amwonapo mbwa mwitu anakuja,
hukimbia na kuwaacha kondoo na mbwa mwitu
hulishambulia kundi na kulitawanya. [13]Yeye
hukimbia kwa sababu ameajiriwa wala hawajali
kondoo.

[14]''Mimi ndimi Mchungaji Mwema:
Ninawajua kondoo Wangu nao kondoo Wangu
wananijua. [15]Kama vile Baba anavyonijua Mimi,
nami ninavyomjua Baba, nami nautoa uhai
Wangu kwa ajili ya kondoo. [16]Ninao kondoo
wengine ambao si wa zizi hili, inanipasa
kuwaleta, nao wataisikia sauti yangu, hivyo
patakuwa na kundi moja na mchungaji mmoja.
[17]Baba Yangu ananipenda kwa kuwa ninautoa

uhai wangu ili niupate tena. 18Hakuna mtu aniondoleaye uhai wangu, bali ninautoa kwa hiari yangu mwenyewe. Ninao uwezo wa kuutoa uhai wangu na pia ninao uwezo wa kuutwaa tena. Amri hii nimepewa na Baba yangu.''

19Kwa maneno haya Wayahudi waligawanyika. 20Wengi wao wakasema, "Huyu amepagawa na pepo mchafu, naye amechanganyikiwa.''

21Wengine wakasema, "Haya si maneno ya mtu mwenye pepo mchafu. Je, pepo mchafu aweza kufungua macho ya kipofu?''

### *Yesu Akataliwa Na Wayahudi*

22Wakati huo ulikuwa Sikukuu ya kuwekwa wakfu hekalu, nao ulikuwa wakati wa majira ya baridi. 23Naye Yesu alikuwa akitembea ndani ya hekalu katika ukumbi wa Solomoni. 24Wayahudi wakamkusanyikia wakamwuliza, "Utatuweka katika hali ya mashaka mpaka lini? Kama Wewe ndiye Kristo tuambie waziwazi.''

25Yesu akawajibu, "Nimewaambia, lakini hamwamini. Mambo ninayoyatenda kwa jina la Baba yangu yananishuhudia. 26Lakini hamwamini, kwa sababu ninyi si wa kundi la kondoo Wangu. 27Kondoo Wangu huisikia sauti Yangu nami nawajua, nao hunifuata, 28nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka katika mikono Yangu. 29Baba Yangu aliyenipa hawa ni Mkuu kuliko wote na hakuna awezaye kuwapokonya kutoka mikononi Mwake. 30Mimi na Baba Yangu tu Umoja.''

31Kwa mara nyingine Wayahudi wakainua mawe ili wampige nayo, 32lakini Yesu akawaambia, "Nimewaonyesha miujuza mingi mikubwa kutoka kwa Baba Yangu. Ni ipi katika hiyo mnataka kunipiga mawe?"

33Wayahudi wakamjibu, "Hutukupigi mawe kwa sababu ya mambo mema uliyotenda, bali ni kwa kuwa umekufuru. Wewe ingawa ni mwanadamu unajifanya kuwa Mungu.''

34 Yesu akawajibu, ''Je, haikuandikwa katika Torati ya kwamba, 'Nimesema kuwa, ninyi ndinyi miungu?' 35Kama aliwaita 'miungu', wale ambao neno la Mungu liliwafikia, nayo Maandiko hayawezi kutanguka. 36Je, mwawezaje kusema kwamba, Yule ambaye Baba amemweka wakfu na kumtuma ulimwenguni anakufuru kwa sababu nilisema 'Mimi ni Mwana wa Mungu?' 37Ikiwa sifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini, 38lakini ikiwa nazifanya kazi za Mungu, hata kama hamniamini Mimi ziamininі hizo kazi, ili mpate kujua na kuelewa kwamba Baba yu ndani Yangu, nami ndani Yake.'' 39Ndipo wakajaribu kumkamata kwa mara nyingine, lakini akaponyoka kutoka mikononi mwao.

40Akaenda tena ng'ambo ya Mto Yordani mpaka mahali pale ambapo Yohana alikuwa akibatiza hapo awali, naye akakaa huko. 41Watu wengi wakamjia, nao wakawa wakisema, ''Yohana hakufanya mwujiza wo wote, lakini kila jambo alilosema kumhusu huyu Mtu ni kweli.'' 42Nao wengi wakamwamini Yesu huko.

### *Kifo Cha Lazaro*

**11** Basi mtu mmoja jina lake Lazaro alikuwa mgonjwa. Yeye alikuwa akiishi Bethania kijiji cha Maria na Martha dada zake. 2Huyu Maria, ambaye Lazaro kaka yake alikuwa mgonjwa, ndiye yule ambaye alimpaka Bwana mafuta na kuifuta miguu Yake kwa nywele zake. 3Hivyo hawa dada wawili walituma ujumbe kwa Yesu kumwambia, "Bwana, yule umpendaye ni mgonjwa.''

4Lakini Yesu aliposikia hayo, akasema, ''Ugonjwa huu hautaleta mauti bali umetokea ili kudhihirisha utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu apate atukuzwe kutokana na ugonjwa huu.'' 5Pamoja na hivyo, ingawa Yesu aliwapenda Martha, Maria na Lazaro ndugu yao, 6baada ya kusikia kwamba Lazaro ni mgonjwa, aliendelea kukawia huko alikokuwa kwa siku mbili zaidi.

7Ndipo akawaambia wanafunzi Wake, "Haya na turudi Uyahudi.''

8Wanafunzi Wake wakamwambia, "Rabi, Wayahudi walikuwa wanataka kukupiga mawe, nawe unataka kurudi huko?''

9Yesu akawajibu, "Si kuna saa kumi na mbili za mchana katika siku moja? Wala watembeao mchana hawawezi kujikwaa kwa maana wanaona nuru ya ulimwengu huu. 10Lakini wale watembeao usiku hujikwaa kwa sababu hakuna nuru ndani yao.''

11Baada ya kusema haya, Yesu akawaambia, "Rafiki yetu Lazaro amelala, lakini nakwenda kumwamsha.''

12Wanafunzi wakamwambia, "Bwana, kama amelala usingizi ataamka.'' 13Hata hivyo, Yesu alikuwa anazungumzia kuwa Lazaro amekufa, lakini wanafunzi wake hawakuelewa, walidhani kwamba anasema Lazaro amelala usingizi tu.

14Kwa hiyo Yesu akawaambia waziwazi, "Lazaro amekufa. 15Hata hivyo nafurahi kwa

kuwa sikuwepo huko kabla ya Lazaro kufa, ili mpate kuamini. Lakini sasa twendeni kwake.''

16Thomasi aliyeitwa Pacha akawaambia wanafunzi wenzake, "Sisi nasi twendeni tukafe pamoja naye.''

### *Yesu Ndiye Ufufuo Na Uzima*

17Yesu alipowasili huko alikuta Lazaro amekwisha kuwako kaburini siku nne. 18Basi Bethania ulikuwa karibu na Yerusalemu umbali wakaribu wa maili mbili[a], 19 Wayahudi wengi walikuwa wamekuja kuwafariji Martha na Maria kwa ajili ya kufiwa na ndugu yao. 20 Martha aliposikia kwambaYesu anakuja, alitoka kwend kumlaki,ila Maria alibaki nyumbani.

21Martha akamwambia Yesu, ''Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu hangalikufa. 22Lakini sasa ninajua kuwa cho chote utakachomwomba Mungu, atakupa.''

23Yesu akamwambia, ''Ndugu yako atafufuka.''

24Martha akamjibu, ''Ninajua ya kuwa atafufuka wakati wa ufufuo wa wafu siku ya mwisho.''

25Yesu akamwambia, "Mimi ndiye huo ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye Mimi, hata akifa atakuwa anaishi 26na ye yote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je, unasadiki haya?''

27Martha akamwambia, "Ndiyo Bwana, ninaamini ya kuwa Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, Yeye ajaye ulimwenguni.''

### *Yesu Alia*

28Baada ya kusema haya Martha alikwenda, akamwita Maria dada yake faraghani na kumwambia, "Mwalimu yuko hapa anakuita.'' 29Maria aliposikia hivyo, akaondoka upesi akaenda mpaka alipokuwa Yesu. 30 Yesu alikuwa hajaingia kijijini, bali alikuwa bado yuko mahali pale alipokutana na Martha. 31Wale Wayahudi waliokuwa pamoja na Maria nyumbani wakimfariji walipoona ameondoka haraka na kutoka nje, walimfuata wakidhani ya kwamba alikuwa anakwenda kule kaburini kulilia huko.

32Maria alipofika mahali pale Yesu alipokuwa, alipiga magoti miguuni Pake na kusema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu hangalikufa.''

33Yesu alipomwona Maria akilia na wale Wayahudi waliokuja pamoja naye pia wakilia, Yesu alisikia uchungu moyoni, akafadhaika sana. 34Akauliza, "Mmemweka wapi?''

Wakamwambia, "Bwana, njoo upaone.''

35Yesu akalia machozi.

36Ndipo Wayahudi wakasema, "Tazama jinsi alivyompenda Lazaro!''

37Lakini wengine wakasema, "Je, yule aliyefungua macho ya kipofu, hakuweza kumfanya na huyu asife?''

### *Yesu Amfufua Lazaro*

38Yesu kwa mara nyingine akiwa amefadhaika sana, akafika penye kaburi. Hilo kaburi lilikuwa pango ambalo jiwe lilikuwa limewekwa penye ingilio lake. 39 Yesu akasema, "Liondoeni hilo jiwe.'' Martha ndugu yake yule aliyekuwa amekufa akasema,

"Lakini Bwana, wakati huu atakuwa ananuka kwani amekwisha kuwako kaburini siku nne''.

40Yesu akamwambia, "Sikukuambia kwamba kama ukiamini utauona utukufu wa Mungu?''

41Kwa hiyo wakaliondoa lile jiwe kutoka penye kaburi. Yesu akainua macho Yake juu akasema, "Baba, ninakushukuru kwa kuwa wanisikia. 42Ninajua ya kuwa Wewe hunisikia sikuzote, lakini nimesema haya kwa ajili ya umati huu uliosimama hapa, ili wapate kuamini ya kuwa Wewe umenituma.''

43Baada ya kusema haya, Yesu akapaaza sauti Yake akaita, ''Lazaro, njoo huku!'' 44Yule aliyekuwa amekufa akatoka nje, mikono yake na miguu yake ikiwa imeviringishiwa vitambaa vya kitani na leso usoni pake.

Yesu akawaambia, "Mfungueni, mwacheni aende zake.''

### *Shauri La Kumwua Yesu*

45Hivyo Wayahudi wengi waliokuwa wamekuja kumfariji Maria, walipoona yale Yesu aliyoyatenda wakamwamini. 46Lakini baadhi yao wakaenda kwa Mafarisayo na kuwaambia mambo Yesu aliyoyafanya. 47 Kwa hiyo viongozi wa makuhani na Mafarisayo wakaita mkutano wa baraza, wakaulizana,

"Tufanyeje? Huyu mtu anafanya ishara nyingi. 48Kama tukimwacha aendelee hivi, kila mtu atamwamini, nao Warumi watakuja na kupaharibu mahali petu patakatifu na taifa letu.''

49Mmoja wao, aliyeitwa Kayafa, ambaye alikuwa Kuhani Mkuu mwaka huo akasema, "Ninyi hamjui kitu cho chote! 50Hamjui kwamba

---

a18 Maili mbili ni kama kilomita tatu.

ni afadhali mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, kuliko taifa lote liangamie?''

51Hakusema haya kutokana na mawazo yake mwenyewe bali kama Kuhani Mkuu mwaka huo, alitabiri kuwa Yesu angelikufa kwa ajili ya Wayahudi, 52wala si kwa ajili ya Wayahudi peke yao, bali pia kwa ajili ya watoto wa Mungu waliotawanyika, ili kuwaleta pamoja na kuwafanya wawe wamoja. 53Hivyo tangu siku hiyo wakawa wanafanya mipango ili wamwue Yesu.

54Kwa hiyo Yesu akawa hatembei hadharani miongoni mwa Wayahudi, bali alijitenga akaenda sehemu iliyo karibu na jangwa kwenye kijiji kiitwacho Efraimu. Akakaa huko na wanafunzi Wake.

55Basi Pasaka ya Wayahudi ilipokuwa imekaribia, watu wengi walitoka vijijini wakaenda Yerusalemu kabla ya Pasaka ili wakajitakase. 56Watu wakawa wanamtafuta Yesu, nao waliposimama kwenye eneo la hekalu waliulizana, Je, Mtu huyu hatakuja kamwe kwenye Sikukuu? 57Viongozi wa makuhani na Mafarisayo walikuwa wametoa amri kuwa ye yote atakayejua mahali Yesu aliko, lazima atoe taarifa ili wapate kumkamata.

### *Maria Ampaka Yesu Mafuta Huko Bethania*

**12** Siku sita kabla ya Pasaka, Yesu alikwenda Bethania mahali ambako Lazaro aliyekuwa amefufuliwa na Yesu alikuwa anaishi. 2Wakaandaa karamu kwa heshima ya Yesu. Martha akawahudumia wakati Lazaro alikuwa miongoni mwa waliokaa mezani pamoja na Yesu. 3Kisha Maria akachukua chupa ya painti moja[a] yenye manukato ya nardo[b] safi ya thamani kubwa akayamimina miguuni mwa Yesu na kuifuta kwa nywele zake. Nyumba nzima ikajaa harufu nzuri ya manukato.

4Ndipo Yuda Iskariote mwana wa Simoni, mmoja wa wale wanafunzi ambaye ndiye atakayemsaliti Yesu, akasema, 5"Kwa nini manukato haya hayakuuzwa kwa dinari 300[c] na fedha hizo wakapewa maskini?" 6Yuda alisema hivi si kwa kuwa aliwajali maskini, bali kwa kuwa alikuwa mwivi, kwa kwani ndiye aliyekuwa akitunza mfuko wa fedha akawa anaiba kile kilichowekwa humo.

7Yesu akasema, "Mwacheni. Aliyanunua manukato hayo ili ayaweke kwa ajili ya siku ya maziko Yangu. 8Maskini mnao siku zote lakini mimi hamko pamoja nami siku zote."

### *Shauri La kumwua Lazaro*

9Umati mkubwa wa Wayahudi walipojua kwamba Yesu alikuwa huko Bethania, walikuja si tu kwa ajili ya Yesu, lakini pia kumwona Lazaro ambaye Yesu alikuwa amemfufua.10Kwa hiyo viongozi wa makuhani wakafanya mpango wa kumwua Lazaro pia, 11kwa kuwa kutokana na habari za kufufuliwa kwake Wayahudi wengi walikuwa wanamwendea Yesu na kumwamini.

### *Kuingia KwaYesu Yerusalemu Kwa Ushindi.*

12Siku iliyofuata umati mkubwa uolikuwa umekuja kwenye Sikukuu walisikia kwamba Yesu angekuja Yerusalemu. 13 Basi wakachukua matawi ya mitende wakatoka kwenda kumlaki, huku wakipaza sauti wakisema,

"Hosana!
Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina
la Bwana!
Amebarikiwa Mfalme wa Israeli!''

14Yesu akamkuta mwana-punda akampanda, kama ilivyoandikwa,

15"Usiogope, Ewe binti Sayuni,
tazama, Mfalme wako anakuja,
amepanda mwana-punda!''

16Wanafunzi wake Yesu mwanzoni hawakuelewa mambo haya, lakini Yesu alipotukuzwa, ndipo walipokumbuka kuwa mambo haya yalikuwa yameandikwa kwa ajili Yake na alitendewa Yeye.

17Wale waliokuwepo wakati Yesu alipomwita Lazaro kutoka kaburini na kumfufua kutoka kwa wafu, walindelea kushuhudia. 18Ni kwa sababu pia walikuwa wamesikia kwamba alikuwa ametenda mwujiza huu ndiyo maana umati wa watu ukaenda kumlaki. 19Hivyo Mafarisayo walipoona hayo wakaambiana, "Mnaona, hamwezi kufanya lo lote. Angalieni, ulimwengu wote unamfuata Yeye!''

### *Yesu Anatabiri Kifo Chake*

20Basi palikuwapo Wayunani fulani miongoni mwa wale waliokuwa wamekwenda kuabudu wakati wa Sikukuu. 21Hawa wakamjia

a[3] Painti moja hapa ni kama nusu lita

b[3] Nardo ni aina ya manukato yaliyokuwa anatengenezwa kutokana na mimea yenye mizizi inayotoa harufu nzuri.

c[5] Dinari 300 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 300, yaani, mshahara wa kibarua ulikuwa dinari moja kwa siku

Filipo, ambaye alikuwa mwenyeji wa Bethsaida huko Galilaya, wakiwa na ombi, wakamwambia, "Tungependa kumwona Yesu." 22Filipo akaenda akamweleza Andrea, nao wote wawili wakamwambia Yesu.

23Yesu akawajibu, "Saa imewadia ya Mwana wa Adamu kutukuzwa. 24Amin, amin, nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu nyingi. 25Mtu ye yote anayependa maisha yake atayapoteza, naye ayachukiaye maisha yake katika ulimwengu huu atayaokoa hata uzima wa milele. 26Mtu ye yote akinitumikia lazima anifuate, nami mahali nilipo ndipo mtumishi wangu atakapokuwa. Mtu akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu.

27"Sasa roho yangu imefadhaika sana. Niseme nini? 'Baba, niokoe na saa hii.' Lakini, ni kwa kusudi hili nimeufikia wakati huu. 28Baba, litukuze Jina Lako."

Ndipo ikaja sauti kutoka mbinguni, "Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena." 29Ule umati wa watu uliokuwa mahali pale uliisikia nao ukasema, "Hiyo ni sauti ya radi", wengine wakasema, "Malaika ameongea naye."

30Yesu akawaambia, "Sauti hii imesikika, kwa faida yenu, wala si kwa faida Yangu. 31Sasa ni saa ya hukumu kwa ajili ya ulimwengu huu, sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. 32Lakini Mimi, nikiinuliwa kutoka katika nchi, nitawavuta watu wote waje Kwangu". 33Yesu aliyasema haya akionyesha ni kifo gani atakachokufa.

34Ule umati wa watu ukapiga kelele ukasema, "Tumesikia kwamba 'Kristo adumu milele, Wewe wawezaje kusema, 'Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu'? Huyu 'Mwana wa Adamu ni nani'?"

35Ndipo Yesu akawaambia, "Bado kitambo kidogo nuru ingalipo pamoja nanyi. Enendeni maadam mna nuru, msije mkakumbwa na giza. Mtu anayetembea gizani hajui anakokwenda. 36Wekeni tumaini lenu katika nuru hiyo ili mpate kuwa wana wa nuru". Baada ya kusema haya, Yesu aliondoka, akajificha wasimwone.

### *Wayahudi Waendelea Kutokuamini*

37Hata baada ya Yesu kufanya miujiza hii yote mbele yao, bado hawakumwamini. 38Hii ilikuwa ili kutimiza lile neno la nabii Isaya lililosema:

"Bwana, ni nani aliyesadiki ujumbe wetu
na mkono wa Bwana amefunuliwa
nani?

39 Kwa hivyo hawakuamini, kwa sababu Isaya anasema mahali pengine:

40"Amewafanya vipofu
na kuifanya mioyo yao kuwa migumu,
ili wasiweze kuona kwa macho yao,
wala kuelewa kwa mioyo yao,
wasije wakageuka, nami nikawaponya."

41Isaya alisema haya alipoona utukufu wa Yesu na kunena habari Zake.

42Lakini wengi miongoni mwa viongozi wa Wayahudi walimwamini, lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakukiri waziwazi kwa maana waliogopa kufukuzwa katika masinagogi. 43Wao walipenda sifa za wanadamu kuliko sifa zitokazo kwa Mungu.

### *Amwaminiye Yesu Hatabaki Gizani*

44Yesu akapaza sauti akasema, "Ye yote aniaminiye, haniamini Mimi peke Yangu, bali Yeye aliyenituma. 45Ye yote anionaye Mimi, amemwona Yeye aliyenituma. 46Mimi nimekuja kama nuru ulimwenguni, ili kwamba kila mtu aniaminiye asibaki gizani.

47"Mimi simhukumu mtu ye yote anayesikia maneno Yangu na asiyatii, kwa maana sikuja kuuhukumu ulimwengu, bali kuuokoa. 48 Yuko amhukumuye yeye anikataaye Mimi na kutokuyapokea maneno Yangu, yaani, yale maneno niliyosema yenyewe yatamhukumu siku ya mwisho. 49Kwa maana sisemi kwa ajili Yangu mwenyewe, bali Baba aliyenituma aliniamuru ni nini cha kusema na jinsi ya kukisema. 50Nami ninajua amri Zake huongoza hadi kwenye uzima wa milele. Hivyo lo lote nisemalo, ndilo lile Baba aliloniambia niseme."

### *Yesu Awanawisha Wanafunzi Wake Miguu*

**13** Ilikuwa mara tu kabla ya Sikukuu ya Pasaka. Yesu alijua ya kuwa wakati Wake wa kuondoka ulimwenguni ili kurudi kwa Baba umewadia. Alikuwa amewapenda watu Wake waliokuwa ulimwenguni, naam, aliwapenda hadi kipimo cha mwisho.

2Wakati alipokuwa akila chakula cha jioni na wanafunzi Wake, ibilisi alikuwa amekwisha kutia ndani ya moyo wa Yuda Iskariote, mwana wa Simoni, wazo la kumsaliti Yesu. 3Yesu akijua ya

kwamba Baba ameweka vitu vyote chini ya
mamlaka Yake na kwamba Yeye alitoka kwa
Mungu na alikuwa anarudi kwa Mungu, 4hivyo
aliondoka chakulani, akavua vazi Lake la nje,
akajifunga kitambaa kiunoni. 5Kisha akamimina
maji kwenye sinia na kuanza kuwanawisha
wanafunzi Wake miguu na kuikausha kwa kile
kitambaa alichokuwa amejifunga kiunoni.

6Alipomfikia Simoni Petro, Petro
akamwambia, ‘‘Bwana, je, Wewe utaninawisha
mimi miguu?’’

7Yesu akamjibu, ‘‘Hivi sasa hutambui lile
ninalofanya, lakini baadaye utaelewa’’.

8Petro akamwambia, ‘‘La, Wewe
hutaninawisha miguu kamwe’’.

Yesu akamjibu, ‘‘Kama nisipokunawisha,
wewe huna sehemu nami’’.

9Ndipo Simoni Petro akajibu, ‘‘Usininawishe
miguu peke yake, bali pamoja na mikono na
kichwa pia!’’

10Yesu akamjibu, ‘‘Mtu aliyekwisha kuoga
anahitaji kunawa miguu tu, kwani mwili wake
wote ni safi. Ninyi ni safi, ingawa si kila mmoja
wenu.’’ 11Kwa kuwa Yeye alijua ni nani ambaye
angemsaliti, ndiyo sababu akasema, ‘Si kila
mmoja aliyekuwa safi.’

12Alipomaliza kuwanawisha miguu yao,
alivaa tena mavazi Yake, akarudi alikokuwa
ameketi, akawauliza, ‘‘Je, mmeelewa
nililowafanyia? 13Ninyi mnaniita Mimi ‘Mwalimu’
na ‘Bwana’, hii ni sawa, maana ndivyo nilivyo.
14Kwa hiyo, ikiwa Mimi niliye Bwana wenu na
Mwalimu wenu nimewanawisha ninyi miguu, pia
hamna budi kunawishana miguu ninyi kwa ninyi.
15Mimi nimewawekea kielelezo kwamba
imewapasa kutenda kama vile nilivyowatendea
ninyi. 16Amin, amin, nawaambia, mtumishi si
mkuu kuliko bwana wake, wala anayetumwa si
mkuu kuliko yule aliyemtuma. 17Sasa kwa kuwa
mmejua mambo haya, heri yenu ninyi kama
mkiyatenda.

18‘‘Sisemi kuhusu ninyi nyote. Ninawajua
wale niliowachagua. Lakini ni ili maandiko
yapate kutimia, ‘Yeye aliyekula chakula changu,
ameinua kisigino chake dhidi yangu.’

19‘‘Ninawaambia mambo haya kabla
hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini ya
kuwa Mimi ndiye. 20Amin, amin, nawaambia, ye
yote anayempokea yule niliyemtuma, anipokea
Mimi, naye anipokeaye Mimi ampokea Yeye
aliyenituma Mimi.’’

### *Yesu Anatabiri Kusalitiwa Kwake*

21Baada ya kusema haya, Yesu alifadhaika
sana moyoni, akasema, ‘‘Amin, amin,
nawaambia, mmoja wenu atanisaliti.’’

22 Wanafunzi Wake wakatazamana bila
kujua kuwa alikuwa anamsema nani. 23Mmoja
wa wanafunzi Wake, ambaye Yesu alimpenda
sana alikuwa ameegama kifuana mwa Yesu.
24Simoni Petro akampungia mkono yule
mwanafunzi akamwambia, ‘‘Mwulize
anamaanisha ni nani.’’

25Yule mwanafunzi akiwa amemwegemea
Yesu akamwuliza, ‘‘Bwana tuambie ni nani?’’

26Yesu akajibu, ‘‘Ni yule nitakayempa hiki
kipande cha mkate baada ya kukichovya
kwenye bakuli.’’ Hivyo baada ya kukichovya kile
kipande cha mkate, akampa Yuda, mwana wa
Simoni Iskariote. 27Mara tu baada ya kukipokea
kile kipande cha mkate, Shetani akamwingia.

Yesu akamwambia Yuda, ‘‘Lile unalotaka
kulitenda litende haraka.’’ 28Hakuna hata mmoja
wa wale waliokuwa ameketi nao chakulani
aliyeelewa kwa nini Yesu alimwambia hivyo.
29Kwa kuwa Yuda alikuwa mtunza fedha,
wengine walifikiri Yesu alikuwa amemwambia
akanunue vitu vilivyohitajika kwa ajili ya
Sikukuu, au kuwapa maskini cho chote. 30Mara
tu baada ya kupokea ule mkate, Yuda akatoka
nje. Wakati huo ulikuwa ni usiku.

### *Yesu Atabiri Petro Kumkana*

31Baada ya Yuda kutoka nje, Yesu
akasema, ‘‘Sasa Mwana wa Adamu
ametukuzwa, naye Mungu ametukuzwa ndani
Yake. 32Ikiwa Mungu ametukuzwa ndani ya
Mwana, Mungu atamtukuza Mwana ndani Yake
mwenyewe naye atamtukuza mara.

33 ‘‘Watoto wangu, Mimi bado niko pamoja
nanyi kwa kitambo kidogo. Mtanifafuta na kama
vile nilivyowaambia Wayahudi, vivyo hivyo sasa
nawaambia na ninyi. Niendako, ninyi hamwezi
kuja.

34‘‘Amri mpya nawapa: Mpendane kama
Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi
mpendane. 35Kama mkipendana ninyi kwa
ninyi, kwa njia hii, watu wote watajua kuwa ninyi
ni wanafunzi Wangu’’

36Simoni Petro akamwuliza, “Bwana,
unakwenda wapi?’’

Yesu akamjibu, ‘‘Ninakokwenda huwezi
kunifuata sasa, lakini utanifuata baadaye.’’

37Petro akamwuliza tena, “Bwana, kwa nini
siwezi kukufuata sasa? Mimi niko tayari kuutoa
uhai wangu kwa ajili Yako.’’

[38]Yesu akamjibu, ''Je, ni kweli uko tayari kuutoa uhai wako kwa ajili Yangu? Amin, amin, nakuambia, kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu.''

### *Yesu Ndiye Njia Ya Kwenda Kwa Baba*

**14** Yesu akawaambia, "Msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi pia. [2]Nyumbani mwa Baba Yangu kuna makao mengi. Kama sivyo, ningeliwaambia. Nakwenda kuwaandalia makao. [3]Nami nikienda na kuwaandalia makao, nitarudi tena na kuwachukua mkae pamoja nami, ili mahali nilipo, nanyi mpate kuwepo. [4]Ninyi mnajua njia ya kufika ninakokwenda.''

[5]Thomasi akamwambia, "Bwana, sisi hatujui unakokwenda, tutaijuaje njia?''

[6]Yesu akawaambia, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu. [7]Kama mngenijua Mimi, mngemjua na Baba pia. Tangu sasa mnamjua Baba Yangu tena mmemwona.

[8]Filipo akamwambia, ''Bwana, tuonyeshe Baba yako yatosha.''

[9]Yesu akamjibu, "Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema, 'Tuonyeshe Baba?' [10]Je, huamini ya kuwa Mimi niko ndani ya Baba, naye Baba yuko ndani Yangu? Maneno ninayowaambia siyasemi kwa ajili Yangu mwenyewe, bali Baba akaaye ndani Yangu ndiye atendaye hizi kazi. [11]Nisadiki Mimi kwamba niko ndani ya Baba na Baba yuko ndani Yangu, la sivyo, niaminini kwa sababu ya zile kazi nizitendazo. [12]Amin, amin, nawaambia, ye yote aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya, naam na kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa sababu Mimi ninakwenda kwa Baba. [13]Nanyi mkiomba lo lote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa katika Mwana. [14]Kama mkiniomba lo lote kwa Jina Langu nitalifanya.''

### *Yesu Ahaidi Roho Mtakatifu*

[15]''Kama mnanipenda, mtazishika amri Zangu. [16]Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi milele. [17]Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi naye anakaa ndani yenu. [18]Sitawaacha ninyi yatima, naja kwenu. [19]Bado kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, ila ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai. [20]Wakati huo mtajua ya kuwa Mimi niko ndani ya Baba na ninyi mko ndani Yangu na Mimi niko ndani yenu. [21] Ye yote mwenye amri Zangu na kuzishika ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.''

[22]Ndipo Yuda, siyo Iskariote, akamwambia, ''Bwana, itakuwaje kwamba utajidhihirisha kwetu na si kwa ulimwengu?''

[23]Yesu akamjibu, ''Mtu ye yote akinipenda atalishika Neno Langu na Baba Yangu atampenda, Nasi tutakuja kwake na kufanya makao Yetu kwake. [24]Mtu ye yote asiyenipenda hayashiki maneno Yangu na maneno niliyowapa si Yangu bali ni ya Baba aliyenituma.

[25]''Nimewaambia mambo haya yote wakati nikiwa bado niko pamoja nanyi. [26]Lakini huyo Msaidizi, yaani, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwenu kwa Jina Langu, atawafundisha mambo yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia. [27]Amani nawaachia, amani yangu nawapa, amani hii niwapayo si kama ile ulimwengu utoayo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiogope.

[28]''Mlinisikia nikisema, 'Ninakwenda Zangu, lakini nitarudi tena.' Kama kweli mngelinipenda mngelifurahi kwa kuwa nakwenda kwa Baba, kwani Baba ni mkuu kuliko Mimi. [29] Nimewaambia mambo haya kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini. [30]Sitasema nanyi zaidi, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu anakuja, naye hana kitu Kwangu, [31]lakini ulimwengu upate kujua kuwa ninampenda Baba, nami hufanya vile vile kama Baba alivyoniamuru.

''Haya inukeni twendeni zetu.

### *Yesu Mzabibu Wa Kweli*

**15** ''Mimi ndimi mzabibu wa kweli na Baba Yangu ndiye mkulima. [2]Kila tawi ndani Yangu lisilozaa matunda, Baba Yangu hulikata, nalo kila tawi lizaalo, Yeye hulipogolea ili lipate kuzaa matunda zaidi. [3]Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililonena nanyi. [4]Kaeni ndani Yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda lisipokaa ndani ya mzabibu, vivyo hivyo ninyi msipokaa ndani Yangu hamwezi kuzaa matunda.

[5]''Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi. Akaaye

ndani Yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana, maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya jambo lo lote. 6 Mtu ye yote asipokaa ndani Yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka. Matawi kama hayo hukusanywa na kutupwa motoni, yakateketea. 7Ninyi mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lo lote mtakalo, nanyi mtatendewa. 8Kwa hiyo Baba Yangu hutukuzwa, kwa vile mzaavyo matunda mengi, nanyi mtakuwa wanafunzi Wangu.

9"Kama vile Baba alivyonipenda Mimi, hivyo ndivyo Mimi nilivyowapenda ninyi. Basi kaeni katika pendo Langu. 10 Mkizishika amri Zangu mtakaa katika pendo Langu, kama Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake. 11Nimewaambia mambo haya ili furaha Yangu iwe ndani yenu na furaha yenu iwe kamili. 12Amri Yangu ndiyo hii: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi. 13Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. 14Ninyi ni rafiki Zangu mkifanya ninayowaamuru. 15Siwaiti ninyi watumishi tena, kwa sababu watumishi hawajui bwana wao analofanya, bali nimewaita ninyi rafiki, kwa maana nimewajulisha mambo yote niliyoyasikia kutoka kwa Baba Yangu. 16Si ninyi mlionichagua, bali Mimi ndiye niliyewachagua ninyi na kuwaweka mwende mkazae matunda na matunda yenu yapate kudumu, ili lo lote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, awape. 17Amri Yangu ndiyo hii, Mpendane.

### *Ulimwengu Wawachukia Wanafunzi*

18"Kama ulimwengu ukiwachukia ninyi, kumbukeni kwamba ulinichukia Mimi kabla yenu. 19Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungeliwapenda kama vile unavyowapenda walio wake. Kwa sababu ninyi si wa ulimwengu, lakini Mimi nimewachagua kutoka katika ulimwengu, hii ndiyo sababu ulimwengu unawachukia. 20'Kumbukeni lile neno nililowaambia, 'Hakuna mtumishi aliye mkuu kuliko bwana wake.' Kama wamenitesa Mimi, nanyi pia watawatesa, kama wamelishika neno langu, watalishika na neno lenu pia. 21Watawatendea ninyi haya yote kwa ajili ya Jina Langu, kwa sababu hawamjui Yeye aliyenituma. 22Kama sikuja na kusema nao wasingalikuwa na hatia ya dhambi. Lakini sasa hawana udhuru kwa ajili ya dhambi zao. 23Ye yote anayenichukia Mimi, anamchukia pia na Baba Yangu. 24Kama sikuwa nimefanya miujiza ambayo haijapata kufanywa na mtu mwingine ye yote, wasingalikuwa na hatia ya dhambi. Lakini sasa wameiona miujiza hii na bado wakatuchukia Mimi na Baba Yangu. 25Lakini hii ni kutimiza lile neno lililoandikwa kwenye Torati kwamba 'Walinichukia pasipo sababu.'

26"Lakini atakapokuja huyo Msaidizi nitakayemtuma kwenu kutoka kwa Baba, yaani, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, Yeye atanishuhudia Mimi. 27Ninyi nanyi itawapasa kushuhudia kwa sababu mmekuwa pamoja Nami tangu mwanzo.

**16** "Nimewaambia mambo haya yote ili msije mkaiacha imani. 2Watawatenga na masinagogi. Naam, saa yaja ambayo mtu ye yote atakayewaua atadhani kwa kufanya hivyo anamtumikia Mungu. 3Nao watawatenda haya kwa sababu hawamjui Baba wala Mimi. 4Lakini nimewaambia ninyi mambo haya, ili saa hiyo ikiwadia mpate kumkumbuka ya kuwa nilikuwa nimewaambia. Sikuwaambia mambo haya tangu mwanzo kwa sababu nilikuwa pamoja nanyi.

### *Kazi Ya Roho Mtakatifu*

5"Sasa Mimi ninakwenda Kwake Yeye aliyenituma, lakini hakuna hata aniulizaye, 'Unakwenda wapi?' 6Kwa sababu nimewaambia mambo haya, mioyo yenu imejawa na huzuni. 7Lakini amin nawaambia, yafaa Mimi niondoke kwa kuwa nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu, lakini nikienda nitamtuma kwenu. 8Naye atakapokuja, atauthibitishia ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu. 9Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini Mimi, 10kwa habari ya haki, kwa sababu ninakwenda kwa Baba, nanyi hamtaniona tena, 11kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.

12"Bado ninayo mambo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili sasa. 13Atakapokuja huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie katika kweli yote. Yeye hatanena kwa ajili Yake mwenyewe, bali atanena yale yote atakayosikia, naye atawaonyesha mambo yajayo. 14Atanitukuza Mimi, kwa maana atayachukua yaliyo Yangu na kuwajulisha ninyi. 15Vyote alivyo navyo Baba ni vyangu. Ndiyo maana nimesema Roho atachukua yaliyo Yangu na kuwajulisha ninyi.

### *Huzuni Itageuka Kuwa Furaha*

16“Bado kitambo kidogo nanyi hamtaniona
na tena bado kitambo kidogo nanyi mtaniona.”

17Baadhi ya wanafunzi wakaulizana, “Ana
maana gani asemapo, ‘Bado kitambo kidogo
nanyi hamtaniona na tena bado kitambo kidogo
nanyi mtaniona? Naye ana maana gani
asemapo, ‘Kwa sababu ninakwenda kwa Baba?’
” 18Wakaendelea kuulizana, “Ana maana gani
asemapo, ‘Kitambo kidogo?’ Hatuelewi hilo
analosema.”

19Yesu akatambua kuwa walitaka
kumwuliza juu ya hilo, hivyo akawaambia, “Je,
mnaulizana nina maana gani niliposema, ‘Bado
kitambo kidogo nanyi hamtaniona na tena bado
kitambo kidogo nanyi mtaniona?’ 20Amin, amin,
nawaambia, ninyi mtalia na kuomboleza, lakini
ulimwengu utafurahi. Ninyi mtahuzunika, lakini
huzuni yenu itageuka kuwa furaha.
21Mwanamke anapokuwa na utungu wa kuzaa
huwa na maumivu kwa sababu saa yake
imewadia. Lakini mtoto akiisha kuzaliwa, yule
mwanamke husahau maumivu hayo kwa
sababu ya furaha ya kuzaliwa mtoto
ulimwenguni. 22Hivyo ninyi mna maumivu sasa,
lakini nitawaona tena, nayo mioyo yenu itafurahi
na furaha yenu hakuna awaondoleaye. 23 Katika
siku hiyo hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin,
nawaambia, kama mkimwomba Baba jambo lo
lote kwa Jina Langu, Yeye atawapa. 24Mpaka
sasa hamjaomba jambo lo lote kwa Jina Langu.
Ombeni nanyi mtapewa, ili furaha yenu ipate
kuwa kamili.”

### *Amani Kwa Wanafunzi*

25“Nimewaambia mambo haya kwa
mafumbo. Saa yaja ambapo sitazungumza
nanyi tena kwa mafumbo bali nitawaeleza
waziwazi kuhusu Baba. 26Siku hiyo mtaomba
kwa Jina Langu. Wala sitawaambia kwamba
nitamwomba Baba kwa ajili yenu, 27kwa maana
Baba mwenyewe anawapenda, kwa sababu
mmenipenda Mimi na mmeamini kwamba
nimetoka kwa Mungu. 28Nilitoka kwa Baba na
kuja ulimwenguni, sasa naondoka ulimwenguni
na kurudi kwa Baba.”

29Ndipo wanafunzi Wake wakasema, “Sasa
unazungumza waziwazi, wala si kwa mafumbo.
30Sasa tumejua kwamba Wewe unajua mambo
yote, wala hakuna haja ya mtu kukuuliza
maswali. Kwa jambo hili tunaamini kwamba
ulitoka kwa Mungu.”

31Yesu akawajibu, “Je, sasa mnaamini?
32Saa inakuja, naam, imekwisha kuwadia,
mtakapotawanyika kila mmoja kwenda
nyumbani kwake na kuniacha peke Yangu.
Lakini Mimi si peke Yangu kwa sababu Baba yu
pamoja nami. 33Nimewaambia mambo haya, ili
mpate kuwa na amani mkiwa ndani Yangu.
Ulimwenguni mtapata dhiki. Lakini jipeni moyo,
kwa maana Mimi nimeushinda ulimwengu.”

### *Yesu Awaombea Wanafunzi Wake*

**17** Baada ya Yesu kusema haya, alitazama
kuelekea mbinguni akawaombea na
kusema :

“Baba, saa imewadia, umtukuze
Mwanao, ili Mwanao apate kukutukuza
Wewe. 2 Kwa kuwa umempa mamlaka juu
ya wote wenye mwili ili awape uzima wa
milele wale uliompa. 3Nao uzima wa milele
ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa
pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.
4Nimekutukuza Wewe duniani kwa kuitimiza
ile kazi uliyonipa niifanye. 5Hivyo sasa,
Baba, unitukuze mbele Zako kwa ule
utukufu niliokuwa nao pamoja na Wewe
kabla ulimwengu haujakuwako.

6“Nimewajulisha Jina Lako wale
ulionipa kutoka katika ulimwengu. Walikuwa
Wako, ukanipa Mimi, nao wamelitii Neno
Lako. 7Sasa wamejua ya kuwa vyote
ulivyonipa vimetoka Kwako, 8kwa kuwa
maneno yale ulionipa nimewapa wao, nao
wameyapokea na kujua kwamba kweli
nimetoka Kwako, nao wameamini kuwa
Wewe ulinituma. 9Ninawaombea wao.Mimi
siuombei ulimwengu, bali nawaombea wale
ulionipa kwa sababu wao ni Wako. 10Wote
walio Wangu ni Wako na walio Wako ni
Wangu, nami nimetukuzwa ndani yao.
11Mimi sasa simo tena ulimwenguni, lakini
wao bado wamo ulimwenguni, nami naja
Kwako. Baba Mtakatifu, uwalinde kwa
uweza wa Jina Lako ulilonipa, ili wawe na
umoja kama sisi tulivyo wamoja.
12Nilipokuwa pamoja nao, niliwalinda,
wakawa salama kwa lile Jina ulilonipa.
Hakuna hata mmoja aliyepotea, isipokuwa
yule aliyekusudiwa, ili Maandiko yapate
kutimia.

13“Lakini sasa naja Kwako, nami
ninasema mambo haya wakati bado nikiwa
ulimwenguni, ili wawe na furaha Yangu
kamili ndani yao. 14Nimewapa Neno Lako,

nao ulimwengu umewachukia kwa kuwa wao si wa ulimwengu kama Mimi nisivyo wa ulimwengu huu. 15Siombi kwamba uwaondoe ulimwenguni, bali uwalinde na yule mwovu. 16Wao si wa ulimwengu huu, kama vile Mimi nisivyo wa ulimwengu. 17Uwatakase kwa ile kweli, Neno Lako ndilo kweli. 18Kama vile ulivyonituma Mimi ulimwenguni, nami nawatuma vivyo hivyo. 19Kwa ajili yao najiweka wakfu ili wao nao wapate kutakaswa katika ile kweli.

### *Yesu Awaombea Wote Wamwaminio*

20"Siwaombei hawa peke yao, bali nawaombea pia wale wote watakaoniamini kupitia neno lao 21ili wawe na umoja kama vile Wewe Baba ulivyo ndani Yangu na Mimi nilivyo ndani Yako, wao nao wawe ndani yetu, ili ulimwengu upate kuamini ya kuwa Wewe ndiye uliyenituma Mimi. 22Utukufu ule ulionipa nimewapa wao, ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo wamoja. 23 Mimi ndani Yako na Wewe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja na ulimwengu upate kujua ya kuwa umenituma, nami nimewapenda wao kama unavyonipenda Mimi.

24"Baba, shauku Yangu ni kwamba, wale ulionipa wawe pamoja nami pale nilipo, ili waweze kuuona utukufu Wangu,yaani, utukufu ule ulionipa kwa kuwa ulinipenda hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

25"Baba Mwenye Haki, ingawa ulimwengu haukujui, Mimi ninakujua, nao wanajua ya kuwa umenituma. 26Nimekufanya Jina Lako lijulikane kwao nami nitaendelea kufanya lijulikane, ili kwamba upendo ule unaonipenda Mimi uwe ndani yao na Mimi mwenyewe nipate kuwa ndani yao.''

### *Yesu Akamatwa*

**18** Yesu alipomaliza kuomba, akaondoka na wanafunzi Wake wakavuka Bonde la Kidroni. Upande wa pili palikuwa na bustani, Yeye na wanafunzi Wake wakaingia humo.

2Basi Yuda, yule aliyemsaliti alipafahamu mahali hapo kwani Yesu alikuwa akikutana humo na wanafunzi Wake mara kwa mara. 3Hivyo Yuda akaja bustanini, akiongoza kikosi cha maaskari wa Kirumi na baadhi ya maafisa kutoka kwa viongozi wa makuhani na Mafarisayo, wakiwa wamechukua taa, mienge na silaha.

4Yesu akijua yale yote yatakayompata, akajitokeza mbele yao akawauliza, ''Mnamtafuta nani?''

5Wao wakamjibu, ''Yesu wa Nazareti.''

Yesu akawajibu, "Mimi ndiye.'' Yuda, yule aliyemsaliti alikuwa amesimama pamoja nao. 6Yesu alipowaambia, 'Mimi ndiye,' walirudi nyuma na kuanguka chini!

7Akawauliza tena, "Mnamtafuta nani?''

Nao wakamjibu, ''Yesu wa Nazareti.''

8Yesu akawaambia, ''Nimekwisha kuwaambia kuwa, Mimi ndiye, kwa hiyo kama mnanitafuta Mimi waacheni hawa watu waende zao.'' 9Hii ilikuwa ili litimie lile neno alilosema, ''Sikumpoteza hata mmoja miongoni mwa wale ulionipa.''

10Simoni Petro aliyekuwa na upanga akaufuta na kumkata sikio la kuume mtumishi wa Kuhani Mkuu. Jina la mtumishi huyo aliitwa Malko.

11Yesu akamwambia Petro, ''Rudisha upanga wako kwenye ala yake. Je, hainipasi kukinywea kikombe alichonipa Baba?''

### *Yesu Mbele Ya Kuhani Mkuu*

12Hivyo wale maaskari wakiwa pamoja na majemadari wao na maafisa wa Wayahudi, wakamkamata Yesu na kumfunga. 13Kwanza wakampeleka kwa Anasi, mkwewe Kayafa, aliyekuwa Kuhani Mkuu mwaka ule. 14Kayafa ndiye aliyekuwa amewashauri Wayahudi kwamba imempasa mtu mmoja kufa kwa ajili ya watu.

### *Petro Anamkana Yesu*

15Simoni Petro pamoja na mwanafunzi mwingine walikuwa wakimfuata Yesu. Huyu mwanafunzi mwingine alikuwa anafahamika kwa Kuhani Mkuu, hivyo aliingia ndani ya ukumbi pamoja na Yesu. 16Lakini Petro alisimama nje karibu na lango, ndipo yule mwanafunzi mwingine akazungumza na msichana aliyekuwa analinda lango, akamruhusu Petro aingie ndani.

17 Yule msichana akamwuliza Petro, ''Je, wewe pia si mmoja wa wanafunzi wa mtu huyu?''

Petro akajibu, "Mimi sio.''

18Wale watumishi na maaskari walikuwa wamesimama wakiota moto wa makaa kwa sababu palikuwa na baridi, Petro naye alikuwa

amesimama pamoja nao akiota moto.

### *Kuhani Mkuu Amhoji Yesu*

19 Wakati huo Kuhani Mkuu akawa
anamwuliza Yesu kuhusu wanafunzi Wake na
mafundisho Yake.

20 Yesu akamjibu, "Nimekuwa nikizungumza
waziwazi mbele ya watu wote. Sikuzote
nimefundisha katika masinagogi na hekaluni
mahali ambapo Wayahudi wote hukusanyika.
Sikusema jambo lo lote kwa siri.
21 Mbona
unaniuliza Mimi maswali? Waulize wale
walionisikia yale niliyowambia. Wao wanajua
niliyosema.''

22 Alipomaliza kusema hayo, mmoja wa
maaskari aliyekuwa amesimama karibu naye,
akampiga Yesu kofi usoni, kisha akasema, "Je,
hivyo ndivyo unavyomjibu Kuhani Mkuu?''

23 Yesu akamjibu akasema, "Kama
nimesema jambo baya, shuhudia huo ubaya
niliousema. Lakini kama nimesema yaliyo kweli,
mbona umenipiga?''
24 Ndipo Anasi akampeleka
Yesu kwa Kuhani Mkuu Kayafa, akiwa bado
amefungwa.

### *Petro Amkana Yesu Tena*

25 Wakati huo Simoni Petro alikuwa
amesimama akiota moto. Baadhi ya wale
waliokuwepo wakamwuliza, "Je, wewe si mmoja
wa wanafunzi Wake?''

Petro akakana, akasema, "Mimi sio.''

26 Mmoja wa watumishi wa Kuhani Mkuu,
ndugu yake yule mtu ambaye Petro alikuwa
amemkata sikio, akamwuliza, "Je, mimi
sikukuona kule bustanini ukiwa na Yesu?''
27 Kwa mara nyingine tena Petro akakana, naye
jogoo akawika wakati uo huo.

### *Yesu Apelekwa Kwa Pilato*

28 Ndipo Wayahudi wakamchukua Yesu
kutoka kwa Kayafa na kumpeleka kwenye
jumba la kifalme la mtawala wa Kirumi[a]. Wakati
huo ilikuwa ni alfajiri, ili kuepuka kuwa najisi kwa
taratibu za ibada, Wayahudi hawakuingia ndani
kwa sababu ya sheria za Kiyahudi.
Wangehesabiwa kuwa najisi kama wangeingia
nyumbani mwa mtu asiye Myahudi na
wasingeruhusiwa kushiriki katika Sikukuu ya
Pasaka.
29 Hivyo Pilato akatoka nje walikokuwa
akawauliza, ''Mmeleta mashtaka gani kumhusu
Mtu huyu?''

30 Wao wakamjibu, ''Kama huyu Mtu
hakuwa mhalifu tusingemleta kwako.''

31 Pilato akawaambia, "Basi mchukueni ninyi
mkamhukumu kwa kufuata sheria zenu.''

Wayahudi wakamjibu, ''Sisi haturuhusiwi
kutoa hukumu ya kifo kwa mtu ye yote.''
32 Walisema hivyo ili yale maneno aliyosema
Yesu kuhusu kifo atakachokufa yapate kutimia.

33 Kwa hiyo Pilato akaingia ndani akamwita
Yesu, akamwuliza, ''Wewe ndiye mfalme wa
Wayahudi?''

34 Yesu akamjibu, ''Je, unauliza swali hili
kutokana na mawazo yako mwenyewe au
uliambiwa na watu kunihusu Mimi?''

35 Pilato akamjibu, ''Mimi si Myahudi, ama
sivyo? Taifa lako mwenyewe na viongozi wa
makuhani wamekukabidhi kwangu. Umefanya
kosa gani?''

36 Yesu akajibu, ''Ufalme Wangu si wa
ulimwengu huu. Ufalme Wangu ungekuwa wa
ulimwengu huu wafuasi Wangu wangenipigania
ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini
kama ilivyo Ufalme Wangu hautoki hapa
ulimwenguni.''

37 Pilato akamwuliza, "Kwa hiyo Wewe ni
mfalme?'' Yesu akajibu, "Wewe wasema
kwamba mimi ni mfalme. Kwa kusudi hili
nilizaliwa na kwa ajili ya hili nilikuja ulimwenguni
ili niishuhudie kweli. Mtu ye yote aliye wa kweli
husikia sauti yangu.''

38 Pilato akamwuliza Yesu, "Kweli ni nini?''
Baada ya kusema haya Pilato akaenda nje tena
akawaambia wale viongozi wa Wayahudi
waliomshtaki Yesu, "Sioni kosa lo lote alilotenda
Mtu huyu.
39 Lakini ninyi mna desturi yenu
kwamba wakati wa Pasaka nimwachie huru
mfungwa mmoja mnayemtaka. Je, mnataka
niwafungulie huyu 'Mfalme wa Wayahudi?' "

40 Wao wakapiga kelele wakisema, "Si huyu
mtu bali tufungulie Baraba!'' Basi Baraba
alikuwa mnyang'anyi.

### *Yesu Ahukumiwa Kusulibiwa*

**19** Ndipo Pilato akamtoa Yesu akaamuru apigwe
mijeledi.
2 Askari wakasokota taji ya miiba
wakamvika Yesu kichwani.
Wakamvalisha joho la zambarau.
3 Wakawa
wanapanda pale alipo tena na tena, wakisema,
"Salamu! Mfalme wa Wayahudi!'' Huku
wakimpiga makofi usoni.

4 Pilato akatoka tena nje akawaambia wale
waliokusanyika, "Tazameni, namkabidhi Yesu
kwenu kuwajulisha kwamba mimi sikumwona

---

[a] 28 Jumba la kifalme la mtawala wa Kirumi lilikuwa linaitwa "Praitorio"

ana hatia.'' 5Kwa hiyo Yesu akatoka nje akiwa amevaa ile taji ya miiba na lile vazi la zambarau. Pilato akawaambia, "Tazameni, huyu hapa huyo mtu!''

6Wale viongozi wa makuhani na maafisa walipomwona, wakapiga kelele wakisema, "Msulibishe! Msulibishe!''

Pilato akawaambia, "Mchukueni ninyi mkamsulibishe, mimi sioni hatia juu yake.''

7Wayahudi wakamjibu, ''Sisi tunayo sheria na kutokana na sheria hiyo, hana budi kufa kwa sababu Yeye alijiita Mwana wa Mungu.''

8Pilato aliposikia haya, akaogopa zaidi. 9Akaingia tena ukumbini akamwuliza Yesu, "Wewe umetoka wapi?'' Lakini Yesu hakumjibu. 10Pilato akamwambia, "Wewe unakataa kuongea na mimi?'' Hujui ya kuwa nina mamlaka ya kukuachia huru au kukusulibisha?''

11Ndipo Yesu akamwambia, "Wewe hungekuwa na mamlaka yo yote juu Yangu kama hungepewa kutoka juu. Kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako ana hatia ya dhambi iliyo kubwa zaidi.''

12Tangu wakati huo, Pilato akajitahidi kutafuta njia ya kumfungua Yesu, lakini Wayahudi wakazidi kupiga kelele wakisema, "Ukimwachia huyu mtu, wewe si rafiki wa Kaisari. Mtu ye yote anayedai kuwa mfalme anampinga Kaisari.''

13Pilato aliposikia maneno haya akamtoa Yesu nje tena akaketi katika kiti chake cha hukumu, mahali palipoitwa Sakafu ya Jiwe, kwa Kiebrania paliitwa Gabatha[a]. 14Basi ilikuwa siku ya Maandalio ya Pasaka, yapata kama saa sita hivi.

Pilato akawaambia Wayahudi, "Huyu hapa Mfalme wenu!''

15Wao wakapiga kelele, "Mwondoe! Mwondoe! Msulibishe!''

Pilato akawauliza, "Je, nimsulibishe Mfalme wenu?''

Wale viongozi wa makuhani wakamjibu, "Sisi hatuna mfalme mwingine ila Kaisari.''

16Ndipo Pilato akamkabidhi Yesu kwao ili wamsulibishe.

### *Kusulibiwa Kwa Yesu*

Kwa hiyo maaskari wakamchukua Yesu. 17Yesu akiwa ameubeba msalaba Wake, akatoka kuelekea mahali palipoitwa, 'Fuvu la Kichwa,' au ambapo kwa Kiebrania ni Golgotha. 18Hapo ndipo walipomsulibisha. Pamoja naye walisulibisha watu wengine wawili, mmoja upande wa kushoto na mwingine upande wa kuume wa Yesu.

19Pilato akaamuru tangazo liandikwe na liwekwe juu kwenye msalaba wa Yesu: "YESU WA NAZARETI, MFALME WA WAYAHUDI.'' 20Kwa kuwa mahali hapo aliposulibiwa palikuwa karibu na mjini, Wayahudi wengi walisoma maandishi haya yaliyokuwa yameandikwa kwa lugha za Kiebrania, Kiyunani na Kilatini. 21Viongozi wa makuhani wa Wayahudi wakapinga, wakamwambia Pilato, "Usiandike, 'Mfalme wa Wayahudi,' bali andika kwamba, Mtu huyu alisema, Mimi ni Mfalme wa Wayahudi.''

22Pilato akawajibu, "Nilichokwisha kuandika, nimeandika!''

### *Mavazi Ya Yesu Yagawanywa*

23Maaskari walipokwisha kumsulibisha Yesu, walichukua nguo Zake wakazigawa mafungu manne, kila askari fungu lake. Ila walikubaliana wasilichane lile vazi Lake kwa maana lilikuwa halina mshono bali limefumwa tangu juu hadi chini. 24Wakaambiana, "Tusilichane ila tulipigie kura ili kuamua ni nani alichukue.''

Hili lilitukia ili Maandiko yapate kutimizwa yale aliyosema,

> "Waligawana nguo zangu na
> mavazi yangu wakayapigia kura.''

Hayo ndiyo waliyoyafanya wale maaskari.

25Wakati huo huo karibu na msalaba wa Yesu walikuwa wamesimama: Maria mama yake, Maria dada wa mamaye, yaani, mke wa Klopa na Maria Magdalene. 26Yesu alipomwona mama Yake mahali pale pamoja na yule mwanafunzi aliyempenda wamesimama karibu, akamwambia mama Yake, "Mwanamke, huyo hapo ndiye mwanao," 27Kisha akamwambia yule mwanafunzi, "Nawe huyo hapo ndiye mama yako.'' Tangu wakati huo yule mwanafunzi akamchukua mama yake Yesu nyumbani kwake.

### *Kifo Cha Yesu*

28Baada ya haya, Yesu hali akijua kuwa mambo yote yamemalizika, alisema ili kutimiza Maandiko, "Naona kiu." 29Hapo palikuwa na bakuli lililojaa siki. Kwa hiyo wakachovya

[a]13 Gabatha ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni "sakafu ya jiwe ", mahali pa wazi, palipoinuliwa ambako palitumika kama mahakama

sifongo kwenye hiyo siki, wakaiweka kwenye
ufito wa mti wa hisopo, wakampelekea
mdomoni. 30Baada ya kuionja hiyo siki, Yesu
akasema, "Imekwisha.'' Akainamisha kichwa
chake, akakata roho.

### *Yesu Achomwa Mkuki Ubavuni*

31Kwa kuwa ilikuwa siku ya Maandalio ya
Pasaka, Wayahudi hawakutaka miili ibaki
msalabani siku ya Sabato, hasa kwa kuwa hiyo
Sabato ingekuwa Sikukuu. Wakamwomba Pilato
aamuru miguu ya wale waliosulibiwa ivunjwe ili
wafe haraka miili iondolewe kwenye misalaba.
32Kwa hiyo maaskari wakaenda wakavunja
miguu ya mtu wa kwanza aliyesulibiwa pamoja
na Yesu na yule mwingine pia. 33Lakini
walipomkaribia Yesu, wakaona ya kuwa
amekwisha kufa, hivyo hawakuvunja miguu
Yake. 34Badala yake mmoja wa wale maaskari
akamchoma mkuki ubavuni na mara pakatoka
damu na maji. 35Mtu aliyeona mambo hayo
ndiye aliyetoa ushuhuda, nao ushuhuda wake ni
kweli. Anajua kuwa anasema kweli, naye
anashuhudia ili pia nanyi mpate kuamini. 36Kwa
maana mambo haya yalitukia ili Maandiko
yapate kutimia, yale yasemayo, "Hakuna hata
mfupa Wake mmoja utakaovunjwa.'' 37Tena
Maandiko mengine yanasema, "Watamtazama
Yeye waliyemchoma kwa mkuki.''

### *Maziko Ya Yesu.*

38Baada ya mambo haya, Yosefu wa
Arimathaya, aliyekuwa mfuasi wa Yesu, ingawa
kwa siri kwa sababu ya kuwaogopa Wayahudi,
alimwomba Pilato ruhusa ili kuuchukua mwili wa
Yesu. Pilato alimruhusu, hivyo akaja,
akauchukua. 39Naye Nikodemo, yule ambaye
kwanza alimwendea Yesu usiku, akaja, akaleta
mchanganyiko wa manemane na manukato,
yenye uzito wa zaidi ya kilo thelathini[b].
40Wakauchukua mwili wa Yesu,
wakauviringishia sanda ya kitani safi pamoja na
yale manukato, kama ilivyokuwa desturi ya
Wayahudi. 41Basi palikuwa na bustani karibu na
mahali pale aliposulibiwa, nako ndani ya ile
bustani palikuwa na kaburi jipya, ambalo
hajazikiwa mtu bado. 42Kwa hiyo, kwa kuwa
ilikuwa siku ya Wayahudi ya Maandalio, nalo
kaburi hilo lilikuwa karibu, wakamzika Yesu
humo.

### *Kufufuka Kwa Yesu*

20 Alfajiri na mapema siku ya kwanza ya
juma, kulipokuwa kungali giza bado,
Maria Magdalene alikwenda kaburini na kukuta
lile jiwe limeondolewa penye ingilio. 2 Hivyo
akaja kwa Simoni Petro pamoja na yule
mwanafunzi mwingine ambaye Yesu alimpenda
akikimbia na kusema, "Wamemwondoa Bwana
kaburini na hatujui walikomweka!"

3Petro na yule mwanafunzi mwingine
wakaondoka mara kuelekea kaburini. 4Wote
wawili walikuwa wanakimbia, lakini yule
mwanafunzi mwingine akakimbia mbio zaidi
kuliko Petro, akatangulia kufika kaburini.
5Alipofika, akainama na kuchungulia mle
kaburini, akaona vile vitambaa vya kitani
vilivyokuwa sanda mle ndani, lakini hakuingia.
6Ndipo Simoni Petro akaja, akimfuata nyuma
akaenda moja kwa moja hadi ndani ya kaburi.
Naye akaona vile vitambaa vya ile sanda vikiwa
pale chini 7na kile kitambaa kilichokuwa
kichwani mwa Yesu. Kitambaa hicho kilikuwa
kimekunjwa mahali pa peke yake, mbali na vile
vitambaa vya kitani vya ile sanda. 8Kisha yule
mwanafunzi aliyetangulia kufika kaburini naye
akaingia ndani, akaona, akaamini, 9(kwa kuwa
mpaka wakati huo walikuwa bado hawajaelewa
yale maandiko kwamba ilikuwa lazima Yesu
afufuke kutoka kwa wafu.)

10Kisha hao wanafunzi wakaondoka
wakarudi nyumbani kwao.

### *Yesu Anamtokea Maria Magdalene*

11Lakini Maria Magdalene akasimama nje
ya kaburi akilia. Alipokuwa akilia, akainama,
kuchungulia mle kaburini, 12naye akaona
malaika wawili wamevaa mavazi meupe,
wameketi pale mwili wa Yesu ulipokuwa
umelazwa, mmoja upande wa kichwani na
mwingine upande wa miguuni.

13Wakamwuliza Maria, ''Mwanamke, mbona
unalia?''

Akawaambia, "Nalia kwa kuwa
wamemchukua Bwana wangu na sijui
walikomweka.'' 14Baada ya kusema hayo,
akageuka, akamwona Yesu amesimama, lakini
hakumtambua.

15Yesu akamwambia, ''Mwanamke, mbona
unalia? Unamtafuta nani?''

Maria akidhani ya kuwa aliyekuwa
anaongea naye ni mtunza bustani, kwa hiyo
akamwambia, ''Bwana, kama ni wewe
umemchukua, tafadhali nionyeshe ulikomweka,

---

[b]39 Zaidi ya kilo 30 hapa tafsiri nyingine zinasema "ratli 100 na nyingine ratli 75," ambazo ni kama kilo 34

nami nitamchukua.’’

16 Yesu akamwita, ‘‘Maria!’’

Ndipo Maria akamgeukia Yesu na kusema naye kwa Kiebrania, ‘‘Rabboni!’’ (maana yake Mwalimu.)

17 Yesu akamwambia, ‘‘Usinishike, kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini nenda kwa ndugu zangu ukawaambie, ‘Ninapaa kwenda kwa Baba yangu ambaye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu ambaye ni Mungu wenu.’ ’’

18 Kwa hiyo Maria Magdalene akaenda kuwatangazia wanafunzi wa Yesu akisema, ‘‘Nimemwona Bwana!’’ Naye akawaambia kwamba amemweleza mambo hayo yote.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Wake*

19 Ikawa jioni ya ile siku ya kwanza ya juma,
wanafunzi Wake walipokuwa pamoja, milango
ikiwa imefungwa kwa kuwaogopa Wayahudi,
Yesu aliwatokea, akasimama katikati yao,
akasema, “Amani iwe nanyi.’’ 20 Baada ya
kusema haya, akawaonyesha mikono Yake na
ubavu Wake. Wanafunzi Wake wakafurahi sana
walipomwona Bwana.

21 Yesu akawaambia tena, “Amani iwe
nanyi! Kama vile Baba alivyonituma Mimi, Mimi
nami nawatuma ninyi.’’ 22 Naye alipokwisha
kusema haya, akawavuvia, akawaambia,
“Pokeeni Roho Mtakatifu. 23 Mkimwondolea mtu
ye yote dhambi zake, zitaondolewa na ye yote
mtakayemfungia dhambi zake, zitafungiwa.’’

### *Yesu Anamtokea Thomasi*

24 Lakini Thomasi, aliyeitwa Didimasi, yaani,
Pacha, mmoja wa wale kumi na wawili, hakuwa
pamoja nao Yesu alipokuja. 25 Hivyo wale
wanafunzi wengine wakamwambia,
‘’Tumemwona Bwana.’’

Lakini yeye akawaambia, ‘‘Nisipoona zile alama za misumari mikononi mwake na kuweka kidole changu kwenye hizo alama za misumari na mkono wangu ubavuni Mwake, sitaamini.’’

26 Baada ya siku nane, wanafunzi Wake
walikuwa tena pamoja ndani ya nyumba, naye
Thomasi alikuwa pamoja nao. Ndipo Yesu akaja
milango ikiwa imefungwa na kusimama katikati
yao akasema, “Amani iwe nanyi.’’ 27 Kisha
akamwambia Thomasi, “Weka kidole chako
hapa na uone mikono Yangu, nyosha mkono
wako uguse ubavuni Mwangu. Usiwe na shaka,
bali uamini tu.’’

28 Thomasi akamwambia, “Bwana wangu na Mungu wangu!’’

29 Yesu akamwambia, “Umeamini kwa kuwa umeniona? Wamebarikiwa wale ambao hawajaona lakini wameamini.’’

### *Kusudi La Kitabu Hiki*

30 Yesu alifanya miujiza mingine mingi
mbele za wanafunzi Wake, ambayo
haikuandikwa katika kitabu hiki. 31 Lakini haya
yameandikwa ili mweze kuamini ya kuwa Yesu
ndiye Kristo[a], Mwana wa Mungu na kwa
kumwamini mpate uzima katika Jina Lake.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Saba*

**21** Baada ya haya Yesu akawatokea tena
wanafunzi Wake kando ya Bahari ya Tiberia.
Yeye alijionyesha kwao hivi: 2 Simoni Petro,
Thomasi aitwaye Didimasi, yaani Pacha,
Nathanaeli wa Kana ya Galilaya, wana wa
Zebedayo na wanafunzi wengine wawili
walikuwa pamoja. 3 Simoni Petro akawaambia
wenzake, “Mimi nakwenda kuvua samaki.’’ Nao
wakamwambia, ‘‘Tutakwenda pamoja nawe.’’
Wakatoka, wakaingia ndani ya mashua, lakini
usiku ule hawakupata cho chote.

4 Mara baada ya kupambazuka, Yesu akasimama ufuoni, lakini wanafunzi hawakumtambua kwamba alikuwa Yesu.

5 Yesu akawaambia, “Wanangu, je, mna samaki wo wote?’’

Wakamjibu, “La.’’

6 Akawaambia, “Shusheni nyavu upande wa kuume wa mashua yenu nanyi mtapata samaki.’’ Wakashusha nyavu na tazama wakapata samaki wengi mno hata wakashindwa kuvutia zile nyavu zilizojaa samaki ndani ya mashua.

7 Yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu
akamwambia Petro, “Huyu ni Bwana!’’ Simoni
Petro aliposikia haya, akajifunga nguo yake kwa
kuwa alikuwa uchi, naye akajitosa baharini.
8 Wale wanafunzi wengine wakaja kwa ile
mashua huku wakikokota ule wavu uliyojaa
samaki, maana hawakuwa mbali na nchi kavu,
ilikuwa yapata dhiraa 200 [a]. 9 Walipofika pwani,
wakaona moto wa makaa na samaki wakiokwa
juu yake na mikate.

10 Yesu akawaambia, “Leteni baadhi ya hao samaki mliovua sasa hivi.’’

11 Simoni Petro akapanda kwenye mashua na kuukokota ule wavu pwani. Ulikuwa umejaa samaki wakubwa 153. Ingawa samaki walikuwa

---

**a**31 Kristo maana yake Masiya,yaani, Mpakwa (Aliyetiwa) Mafuta **a**8 Dhiraa 200 ni kama mita 90

wengi kiasi hicho, ule wavu haukuchanika.
[12]Yesu akawaambia, "Njoni mpate kifungua
kinywa." Hakuna hata mmoja wao aliyethubutu
kumwuliza, "Wewe ni nani?" Kwa sababu
walijua ya kuwa ni Bwana. [13]Yesu akaja,
akachukua ule mkate, akawapa na vivyo hivyo
akawagawia pia wale samaki. [14]Hii ilikuwa mara
ya tatu Yesu kuwatokea wanafunzi Wake tangu
afufuke kutoka kwa wafu.

### *Yesu Amwuliza Petro Kama Anampenda*

[15]Walipokwisha kula, Yesu akamwuliza
Simoni Petro, "Je, Simoni mwana wa Yohana,
unanipenda kweli kuliko hawa?"

Yeye akamjibu, "Ndiyo, Bwana Wewe
unajua ya kuwa ninakupenda."

Yesu akamwambia, "Lisha wana-kondoo
Wangu."

[16]Yesu akamwambia tena, "Simoni, mwana
wa Yohana, wanipenda?"

Petro akamjibu, "Ndiyo Bwana, Wewe
unajua ya kuwa ninakupenda."

Yesu akamwambia, "Chunga kondoo
Zangu."

[17]Kwa mara ya tatu Yesu akamwuliza Petro,
"Simoni mwana wa Yohana, unanipenda?"

Petro akahuzunika sana kwa kuwa Yesu
alimwuliza mara ya tatu, 'Unanipenda?'
Akamjibu, "Bwana, Wewe unajua yote, unajua
ya kuwa ninakupenda."

Yesu akamwambia, "Lisha kondoo Zangu.
[18]Amin, amin, nakuambia, ulipokuwa kijana
ulivaa na kwenda unakotaka, lakini
utakapokuwa mzee utanyosha mikono yako na
mtu mwingine atakuvika na kukupeleka
usipotaka kwenda." [19]Yesu alisema haya ili
kuashiria ni kifo cha aina gani Petro
atakachomtukuza nacho Mungu. Kisha Yesu
akamwambia Petro, "Nifuate!"

[20]Petro akageuka akamwona yule
mwanafunzi aliyependwa na Yesu akiwafuata.
(Huyu ndiye yule mwanafunzi aliyeegema
kifuani mwa Yesu walipokula naye chakula cha
mwisho na kuuliza, 'Bwana, ni nani
atakayekusaliti?') [21]Petro alipomwona huyo
mwanafunzi, akamwuliza Yesu, "Bwana na huyu
je?"

[22]Yesu akamjibu, "Ikiwa nataka aishi mpaka
nitakaporudi, inakuhusu nini? Wewe inakupasa
unifuate!" [23]Kwa sababu ya maneno haya ya
Yesu, uvumi ukaenea miongoni mwa ndugu
kwamba huyu mwanafunzi hangekufa. Lakini
Yesu hakusema kuwa hangekufa. Yeye alisema
tu kwamba, "Ikiwa nataka aishi mpaka
nitakaporudi, inakuhusu nini?"

[24]Huyu ndiye yule mwanafunzi
anayeshuhudia mambo haya na ndiye ambaye
ameandika habari hizi. Nasi tunajua ya kuwa
ushuhuda wake ni kweli.

[25]Lakini kuna mambo mengine mengi
ambayo Yesu alifanya, kama yote
yangeliandikwa, nadhani hata ulimwengu wote
usingekuwa na nafasi ya kutosha kuweka vitabu
vyote ambavyo vingeandikwa. Amen.

# Matendo ya Mitume

### *Utangulizi*

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinatoa historia ya msingi ya kuenea kwa Ukristo katika miongo mitatu mara baada ya kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. Ingawa kuna injili nne zinazoelezea juu ya maisha ya Yesu Kristo, kuna kitabu kimoja tu katika Agano Jipya kinachofuatilia kupanuka kwa kanisa la kwanza. Kitabu hiki cha Matendo kimeelezewa kama egemeo la Agano Jipya. Kitabu hiki ni moja ya vitabu viwili vinavyokubaliwa kuwa mwandishi ni Theoflo.Kitabu cha kwanza ambacho ni Injili ya Luka, kinamfahamisha msomaji kuhusu maisha na kazi ya Kristo. Kitabu hiki cha pili kinajihusisha na huduma ya wafuasi wa Kristo. Kusudi la mwandishi ni kutoa maelezo juu ya kuanza kwa ukristo na jinsi Mungu alivyodhihirisha nafsi Yake mwenyewe katika mwili wa Yesu Kristo kwa kupitia Kanisa.Luka anajaribu kuonyesha hali ambayo Kanisa la kwanza lilikabiliwa nayo wakati wa kuenea kwake katika utawala wa Rumi.

Umahiri wake wa historia unamsaidia kutumia misamiati sahihi kwa maafisa wa Kirumi katika kitabu chake chote ambacho kinatambuliwa kama kazi ya utafiti wa msomi au ya ujuzi wa binafsi.Kutokana na hilo, mwandishi anahesabiwa kama mwana historia aliye sahihi zaidi.

Po pote ambako elimu ya mambo ya kale au uhakika wa uandishi unapopatikana kitabu hiki cha Matendo kimeonekana kuwa chanzo muhimu cha kumbukumbu.

Luka anathibitisha katika kitabu hiki kwamba kazi ambayo Bwana Yesu aliianzisha alipokuwa duniani anaendelea kuifanya katika kanisa lake kwa njia ya Roho Mtakatifu. Katika kuenea kwa Ukristo, mkazo mkubwa umewekwa kwa Roho Mtakatifu katika kitabu chote. Ingawa wanafunzi wa Yesu wanatajwa katika sura za mwanzoni, wengi wa wale Kumi na Wawili hawatajwi tena baadaye. Petro ndiye anayeonekana sana wakati wa kuanza kwa kanisa huko Yerusalemu, naye anakuwa kimya hadi wakati wa baraza huko Yerusalemu. Kama vile kituo cha Ukristo kilivyohama kwenda Antiokia, Paulo alijitokeza kama kiongozi mkuu, hivyo sehemu ya mwisho ya kitabu hiki imetoa nafasi kubwa kwa Paulo na utume wake. Kitabu kinaishia ghafula na Paulo kama mfungwa anayehubiri Habari Njema (Injili) huko Rumi.

Ujumbe wa kanisa la kwanza umepewa umuhimu mkubwa katika kitabu cha Matendo. Anaanza kwa kueleza jinsi wanafunzi wa Yesu walivyojazwa na nguvu za Roho Mtakatifu wa Mungu, wakaanza kuhubiri kwa ujasiri na watu 3,000 wakaokolewa kwa siku moja *(2:41).* Kisha anaeleza maisha ya Kanisa la Yerusalemu, kuenezwa kwa Injili Samaria, matendo ya mtume Petro na kuteswa kwa waamini wa kwanza. Baada ya hapo anaeleza juu ya kazi ya mtume Paulo miongoni mwa watu wa mataifa mengine (ambao si Waisraeli). Anaeleza kwa kirefu kuhusu safari tatu za Mtume Paulo kueneza injili na anamalizia na safari ya Paulo huko Rumi.

### *Wazo Kuu*

Kitabu cha Matendo ya Mitume kiliandikwa kwa madhumuni ya kueleza jinsi Injili ilivyoenezwa kutoka kwa Wayahudi na kuwafikia watu wa mataifa mengine *(1:8).* Habari Njema kuhusu kufa na kufufuka kwa Yesu ilikuwa ndiyo kiini cha msingi wa imani ya Ukristo. Imani hii isingeweza kuzuiliwa ikae katika sehemu moja tu ya dunia, bali ilikusudiwa na Mungu iwafikie watu wote duniani. Kwa sababu hii Mungu aliwawezesha watu Wake kuieneza Injili kila mahali kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye aliwatia nguvu, Mungu mwenyewe akitenda kazi pamoja nao akilithibitisha lile Neno kwa ishara, miujiza na maajabu mengi.

Kule kuenea kwa Kanisa kutoka kwa Wayahudi kwenda kwa mataifa mengine, kulisababisha shinikizo kutoka kwa Wayahudi walioamini kutaka watu wa mataifa mengine wafuate mapokeo ya Kiyahudi, kitu kilichopelekea kufanyika kwa baraza huko Yerusalemu (*Mdo.15*). Hili baraza liliamua kuweka msimamo kwamba watu Mataifa wasilazimishwe kufuata mapokeo wala desturi za Kiyahudi. Hivyo uamuzi ulikuwa *(Mdo15:28-29) "Kwa maana imempendeza Roho Mtakatifu na sisi tusiwatwike mzigo wo wote mkubwa zaidi ya mambo haya yafuatayo ambayo ni ya lazima: Kwamba mjiepushe na kitu cho chote kilichotolewa sadaka kwa sanamu, kunywa damu, nyama ya wanyama walionyongwa na mjiepushe na uasherati. Mkiyaepuka mambo haya mtakuwa mmefanya vyema."* Uwezo wa Mungu juu ya vitu vyote unadhihirika kwa jinsi Injili inavyowabadilisha watu wasioamini wakawa watu wapya na jinsi Roho Mtakatifu alivyowaimarisha Wakristo wakastahimili wakati wa mateso. Ingawa wengi walipoteza maisha yao ( hata Petro na Paulo walikufa wakiitetea Injili), lakini walipata ushindi wa kweli na uzima wa milele ndani ya Yesu Kristo.

### *Mwandishi*

Luka

### *Tarehe*

Kama 63 B.K.

### *Mgawanyo*

- Kanisa la kwanza (1:1-5:42).
- Mateso na kuenea kwa Injili (6 :1-9:31).
- Matendo ya Petro (9:32-12:25).
- Safari ya kwanza ya Paulo kueneza Injili (13:1-14:28).
- Mkutano wa Yerusalemu (15:1-41).
- Safari ya pili ya Paulo kueneza Injili (16:1-18:22).
- Safari ya tatu ya Paulo kueneza Injili (18:23-21:14).
- Kukamatwa kwa Paulo na safari yake kwenda Rumi (21:15-28:31).

## *Ahadi Ya Roho Mtakatifu*

**1** Katika kitabu changu cha kwanza nilikuandikia mpendwa Theofilo, kuhusu mambo yote Yesu aliyofanya na kufundisha tangu mwanzo, **2** hadi siku ile alipochukuliwa kwenda mbinguni, baada ya kuwapa maelekezo kwa njia Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua. **3**Baada ya mateso Yake, alijionyesha kwao na kuwathibitishia kwa njia nyingi kwamba yeye yu hai. Katika muda wa siku arobaini baada ya kufufuka kwake aliwatokea na kunena kuhusu Ufalme wa Mungu. **4**Wakati mmoja alipokuwa pamoja nao, aliwapa amri hii, "Msitoke humu Yerusalemu, bali ingojeni ahadi ya Baba, ambayo mmenisikia nikisema habari Zake. **5**Yohana aliwabatiza kwa maji, lakini baada ya siku hizi chache mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu.''

## *Kupaa Kwa Yesu Kwenda Mbinguni*

**6**Mitume walipokuwa wamekusanyika pamoja, wakamwuliza Yesu, "Bwana, je, huu ndio wakati wa kuwarudishia Israeli ufalme?''

**7**Yesu akawaambia, "Si juu yenu kujua nyakati na majira ambayo Baba ameyaweka katika mamlaka Yake mwenyewe. **8**Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na Samaria, hadi miisho ya dunia.''

**9**Baada ya kusema mambo haya, walipokuwa wanatazama, akachukuliwa juu mbinguni mbele ya macho yao na wingu likampokea wasimwone tena.

**10**Walipokuwa bado wakikaza macho yao kuelekea juu alipokuwa akienda Zake Mbinguni, tazama ghafula, wanaume wawili waliovaa mavazi meupe wakasimama karibu nao, **11**wakasema, "Enyi watu wa Galilaya, mbona mnasimama mkitazama juu mbinguni?Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda Mbinguni, atarudi tena jinsi iyo hiyo mliyomwona akienda Zake Mbinguni.''

## *Mathiya Achaguliwa Badala Ya Yuda*

**12**Ndipo waliporudi Yerusalemu kutoka Mlima wa Mizeituni, uliokuwa karibu na Yerusalemu, umbali wa mwendo wa Sabato[a] kutoka mjini. **13**Walipowasili mjini Yerusalemu, walikwenda ghorofani kwenye chumba walichokuwa wakiishi. Wale waliokuwepo walikuwa: Petro, Yohana, Yakobo, Andrea, Filipo, Thomasi, Bartholomayo, Mathayo, Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni Zelote[b] na Yuda mwana wa Yakobo. **14**Hawa wote waliungana pamoja katika maombi. Pamoja nao walikuwapo wanawake kadha wa kadha na Maria mama Yake Yesu pamoja na ndugu Zake Yesu.

**15**Katika siku hizo Petro akasimama katikati ya waamini, (jumla yao wote walikuwa watu wapatao 120,) akasema, **16**"Ndugu zangu, ilibidi maandiko yatimie yale ambayo Roho Mtakatifu alitabiri kupitia kwa Daudi kumhusu Yuda aliyewaongoza wale waliomkamata Yesu. **17**Yuda alikuwa mmoja wetu, kwa maana na yeye alichaguliwa ashiriki katika huduma hii.''

**18** (Basi Yuda alinunua shamba kwa zile fedha za uovu alizopata, akiwa huko shambani akaanguka, akapasuka na matumbo yote yakatoka nje. **19**Kila mtu huko Yerusalemu akasikia habari hizi, kwa hiyo wakapaita mahali hapo kwa lugha yao, Akeldama, yaani, Shamba la Damu.)

**20**"Kama vile ilivyoandikwa katika kitabu cha Zaburi,

" 'Mahali pake na pawe ukiwa
wala asiwepo mtu atakayekaa humo
na mtu mwingine aichukue nafasi yake.'

## *Mathiya Achaguliwa*

**21**Kwa hiyo inatubidi tumchague mtu mwingine miongoni mwa wale ambao wamekuwa pamoja nasi wakati wote Bwana Yesu alipoingia na kutoka katikati yenu, **22**kuanzia ubatizo wa Yohana mpaka siku aliyochukuliwa kutoka kwetu kwenda Mbinguni. Kwa kuwa mmoja wao inabidi awe shahidi pamoja nasi wa ufufuo Wake."

**23**Wakapendekeza majina ya watu wawili: Yosefu, aitwaye Barsaba (ambaye pia alijulikana kama Yusto) na Mathiya. **24**Kisha wakaomba, wakasema, "Bwana, Wewe waujua moyo wa kila mtu. Tuonyeshe ni yupi kati ya hawa wawili uliyemchagua **25**ili achukue nafasi ya huduma ya utume ambayo Yuda aliacha ili aende mahali pake mwenyewe.'' **26**Kisha wakawapigia kura, nayo kura ikamwangukia Mathiya, naye akaongezwa kwenye wale mitume kumi na mmoja.

---

a[12] Mwendo wa Sabato hapa ina maana umbali wa kama kilomita 1.1,yaani, (mita 1,100)

b[13] Zelote hapa ina maana alikuwa mwanachama wa Wazelote, ambacho kilikuwa kikundi cha kizalendo cha Kiyahudi cha kupinga jeuri ya Warumi.

### *Kushuka Kwa Roho Mtakatifu*

**2** Ilipowadia siku ya Pentekoste, walikuwa wote
mahali pamoja. 2 Ghafula sauti kama mvumo
mkubwa wa upepo uliotoka mbinguni, ukaijaza
nyumba yote walimokuwa wameketi. 3 Zikatokea
ndimi kama za moto zilizogawanyika na kukaa
juu ya kila mmoja wao. 4 Wote wakajazwa na
Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha
nyingine, kama Roho
alivyowajalia.

5 Basi walikuwepo Yerusalemu Wayahudi
wanaomcha Mungu kutoka kila taifa chini ya
mbingu. 6 Waliposikia sauti hii, umati wa watu
ulikusanyika pamoja wakistaajabu, kwa sababu
kila mmoja wao aliwasikia wakisema kwa lugha
yake mwenyewe. 7 Wakiwa wameshangaa na
kustaajabu wakauliza, "Je, hawa wote
wanaozungumza si Wagalilaya? 8 Imekuwaje basi
kila mmoja wetu anawasikia wakinena kwa lugha
yake ya kuzaliwa? 9 Warparathi, Wamedi,
Waelami, wakazi wa Mesopotamia, Uyahudini,
Kapadokia, Ponto na Asia, 10 Frigia, Pamfilia, Misri
na pande za Libya karibu na Kirene na wageni
kutoka Rumi, 11 (Wayahudi na waongofu, Wakrete
na Waarabu sote tunawasikia watu hawa
wakisema katika lugha zetu wenyewe, mambo
makuu ya ajabu ya Mungu.'' 12 Wakiwa
wameshangaa na kufadhaika wakaulizana, "Ni nini
maana ya mambo haya?''

13 Lakini wengine wakawadhihaki
wakasema, "Hawa wamelewa mvinyo!"

### *Petro Ahutubia Umati*

14 Ndipo Petro akasimama pamoja na wale
mitume kumi na moja, akainua sauti yake na
kuhutubia ule umati wa watu, akasema:
"Wayahudi wenzangu na ninyi nyote mkaao
Yerusalemu, jueni jambo hili mkanisikilize.
15 Hakika watu hawa hawakulewa kama
mnavyodhania, kwa kuwa sasa ni saa tatu
asubuhi! 16 Hawa hawakulewa, ila jambo hili ni
lile lililotabiriwa na nabii Yoeli akisema,

17 " 'Katika siku za mwisho, asema Bwana,
nitamimina Roho wangu juu ya wote
wenye mwili.
Wana wenu na binti zetu watatabiri,
vijana wenu wataona maono
na wazee wenu wataota ndoto.
18 Hata juu ya watumishi
wangu nitamwaga Roho
wangu, nao watatabiri".
19 Nami nitaonyesha maajabu mbinguni juu
na ishara duniani chini,
moto na mvuke wa moshi
mnene. 20 Jua litakuwa giza
na mwezi utakuwa mwekundu kama damu,
kabla ya kuja siku ile kuu ya Bwana iliyo
tukufu.
21 Lakini ye yote atakayeliita jina la
Bwana, ataokolewa.'

22 "Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya
nisemayo: Yesu wa Nazareti alikuwa mtu
aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza,
maajabu na ishara, ambayo Mungu alitenda
miongoni mwenu kwa kupitia yeye, kama ninyi
wenyewe mjuavyo. 23 Huyu mtu akiisha
kutolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa
kwa kujua kwake Mungu tangu zamani, ninyi,
kwa mikono ya watu wabaya, mlimwua kwa
kumgongemea msalabani. 24 Lakini Mungu
alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea
uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana
yeye kushikiliwa na nguvu za mauti. 25 Kwa
maana Daudi asema kumhusu yeye:

" 'Nalimwona Bwana mbele yangu
siku zote.
Kwa sababu yuko mkono wangu wa
kuume,
sitatikisika.
26 Kwa hiyo moyo wangu unafurahia na
ulimi wangu unashangilia,
mwili wangu nao utaishi kwa tumaini.
27 Kwa maana hutaniacha kaburini,
wala hutamwacha aliye Mtakatifu
wako kuona uharibifu.
28 Umenionyesha njia za uzima,
utanijaza na furaha mbele zako.'

29 "Ndugu zangu Waisraeli, nataka
niwaambie kwa uhakika kwamba baba yetu
Daudi alikufa na kuzikwa, nalo kaburi lake lipo
hapa mpaka leo. 30 Lakini alikuwa nabii na alijua
ya kuwa Mungu alikuwa amemwahidi kwa kiapo
kwamba angemweka mmoja wa wazao wake
penye kiti chake cha enzi. 31 Daudi akiona
mambo yaliyoko mbele, akanena juu ya
kufufuka kwa Kristo, kwamba hakuachwa
kaburini, wala mwili wake haukuona uharibifu.
32 Mungu alimfufua huyu Yesu na sisi sote ni
mashahidi wa jambo hilo. 33 "Basi ikiwa yeye
ametukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu,
amepokea kutoka kwa Baba ahadi ya Roho
Mtakatifu, naye amemimina kile mnachoona

sasa na kusikia. 34Kwa kuwa Daudi hakupaa kwenda mbinguni, lakini anasema,

" 'BWANA alimwambia Bwana wangu: Kaa
wewe upande wangu wa kuume,
35mpaka nitakapowafanya adui zako
kuwa chini ya miguu yako.' "

36"Kwa hiyo Israeli wote na wajue jambo hili kwa uhakika kwamba: Mungu amemfanya huyu Yesu, ambaye ninyi mlimsulibisha, kuwa Bwana na Kristo.''

### *Ongezeko La Waamini*

37Watu waliposikia maneno haya yakawachoma mioyo yao, wakawauliza Petro na wale mitume wengine, "Ndugu zetu tufanye nini?''

38Petro akawajibu, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu abatizwe kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu. nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. 39Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu na kwa wale wote walio mbali na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu atamwita amjie.''

40Petro akawaonya kwa maneno mengine mengi na kuwasihi akisema, "Jiepusheni na kizazi hiki kilichopotoka." 41Wale wote waliopokea ujumbe wa Petro kwa furaha wakabatizwa na siku ile waliongezeka watu wapatao 3,000.

### *Ushirika Wa Waamini*

42Nao wakawa wanadumu katika mafundisho ya mitume, katika ushirika, katika kumega mkate na katika kusali. 43Kila mtu akaingiwa na hofu ya Mungu, nayo miujiza mingi na ishara zikafanywa na mitume. 44Walioamini wote walikuwa mahali pamoja nao, walikuwa na kila kitu shirika. 45Waliuza mali zao na vitu walivyokuwa navyo, wakamgawia kila mtu kwa kadiri alivyokuwa anahitaji. 46Siku zote kwa moyo mmoja walikutana ndani ya ukumbi wa hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, wakila chakula chao kwa furaha na moyo mweupe, 47wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Kila siku Bwana akaliongeza kanisa kwa wale watu waliokuwa wakiokolewa.

### *Petro Amponya Mlemavu Kwa Jina La Yesu*

**3** Siku moja Petro na Yohana walikuwa wanapanda kwenda hekaluni kusali yapata saa tisa alasiri. 2Basi palikuwa na mtu mmoja aliyekuwa kiwete tangu kuzaliwa. Alichukuliwa na kuwekwa kwenye lango la hekalu liitwalo Zuri, kila siku ili aombe msaada kwa watu wanaoingia hekaluni. 3Huyu mtu akiwaona Petro na Yohana wakikaribia kuingia hekaluni, aliwaomba wampe sadaka. 4Wakamkazia macho, kisha Petro akamwambia, "Tutazame sisi.'' 5Hivyo yule mtu akawatazama, akitazamia kupata kitu kutoka kwao.

6 Ndipo Petro akamwambia, "Sina fedha wala dhahabu, lakini kile nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu wa Nazareti simama, uende.'' 7Petro akamshika yule mtu kwa mkono wa kuume akamwinua, mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikapata nguvu. 8Akaruka juu na kusimama, akaanza kutembea. Kisha akaingia Hekaluni pamoja na Petro na Yohana, huku akitembea na kurukaruka na kumsifu Mungu. 9Watu wote walipomwona akitembea na kumsifu Mungu, 10wakamtambua kuwa ni yule mtu aliyekuwa akiketi nje ya hekalu penye lango liitwalo Zuri akiomba msaada, nao wakajawa na mshangao, wakastaajabu juu ya yale yaliyomtukia.

### *Petro Anashuhudia Kuwa Yesu Anaponya*

11Yule mtu kiwete aliyeponywa alipokuwa akiambatana na Petro na Yohana, watu wote walishangaa mno, wakaja wanawakimbilia mpaka kwenye ukumbi wa Solomoni. 12Petro alipoona watu wamekusanyika akawaambia, "Enyi waume wa Israeli, kwa nini mnastaajabu kuhusu jambo hili? Mbona mnatukazia macho kwa mshangao kana kwamba ni kwa uwezo wetu au utakatifu wetu tumefanya mtu huyu kutembea? 13Mungu wa Abrahamu na Isaki na Yakobo, Mungu wa baba zetu amemtukuza Mwanawe Yesu ambaye ninyi mlimtoa ahukumiwe kifo na mkamkana mbele ya Pilato ingawa Yeye alikuwa ameamua kumwachia aende zake. 14Ninyi mlimkataa huyo Mtakatifu na Mwenye Haki mkaomba mpewe yule mwuaji. 15Hivyo mkamwua aliye chanzo cha uzima, lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu. Sisi tu mashahidi wa mambo haya. 16Kwa imani katika Jina la Yesu, huyu mtu mnayemwona na kumfahamu limemtia nguvu. Ni kwa Jina la Yesu na imani ile itokayo Kwake ambayo imemponya kabisa huyu mtu, kama ninyi wote mnavyoona.

17"Sasa, Ndugu zangu, najua ya kuwa ninyi mlitenda bila kujua, kama walivyofanya viongozi

wenu. 18Lakini kwa njia hii Mungu alitimiza kile ambacho alikuwa ametabiri kwa vinywa vya manabii Wake wote, kwamba Kristo atateswa.
19Tubuni basi mkamgeukie Mungu, ili dhambi zenu zifutwe, ili zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwepo kwake Bwana.
20Kwamba apate kumtuma Kristo, ambaye amewekwa kwa ajili yenu, yaani Yesu,
21ambaye ilimpasa mbingu zimpokee mpaka wakati wa kufanywa upya kila kitu, kama Mungu alivyosema kwa vinywa vya manabii wake wote watakatifu kabla ya mwanzo wa ulimwengu.
22Kwa maana Mose alisema, 'Bwana Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu, itawapasa kumtii huyo kwa kila jambo atakalowaambia. 23Mtu ye yote ambaye hatamsikiliza huyo nabii, atakataliwa mbali kabisa na watu wake.'

24"Naam, manabii wote tangu Samweli na wale waliofuata baada yake, wote walionena walitabiri kuhusu siku hizi. 25Ninyi ndio wana wa manabii na wa agano ambayo Mungu alifanya baba zenu, akimwambia Abrahamu, 'Katika wewe, jamaa zote za duniani watabarikiwa.'
26Mungu alipomfufua Mwanawe Yesu, alimtuma kwenu kwanza, ili awabariki kwa kumgeuza kila mmoja wenu kutoka katika njia yake mbaya."

### *Petro Na Yohana Mbele Ya Baraza*[a]

**4** Wakati Petro na Yohana walipokuwa wakisema na watu, makuhani, mkuu wa walinzi wa hekalu na Masudakayo wakawajia wakiwa
2wamekasirika sana kwa sababu hao mitume walikuwa wanawafundisha watu na kuhubiri kwamba katika Yesu kuna ufufuo wa wafu. 3
Wakawakamata Petro na Yohana na kuwatia gerezani mpaka kesho yake kwa kuwa ilikuwa jioni. 4Lakini wengi wale waliosikia lile neno waliamini, idadi yao ilikuwa yapata wanaume 5,000.

5Siku ya pili yake viongozi wa Kiyahudi, wazee na waandishi wa sheria wakakusanyika Yerusalemu, 6walikuwepo Kuhani Mkuu Anasi, Kayafa, Yohana, Iskanda na wengi wa jamaa ya Kuhani Mkuu. 7Wakiisha kuwasimamisha Petro na Yohana katikati yao, wakawauliza, "Ni kwa uwezo gani au kwa jina la nani mmefanya jambo hili?"

8Petro akiwa amejaa Roho Mtakatifu akajibu, "Enyi watawala na wazee wa watu,
9kama leo tukihojiwa kwa habari ya mambo mema aliyotendewa yule kiwete na kuulizwa jinsi alivyoponywa, 10ijulikane kwenu nyote na kwa watu wote wa Israeli kwamba: Ni kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu, kwa uwezo wa Yesu, kwamba mtu huyu anasimama mbele yenu akiwa mzima kabisa. 11Huyu Yesu ndiye

'lile jiwe ambalo ninyi wajenzi mlilikataa,
ambalo limekuwa jiwe kuu la pembeni.'

12Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna Jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."

### *Ujasiri Wa Petro Na Yohana Washangaza Watu*

13Wale viongozi na wazee walipoona ujasiri wa Petro na Yohana na kujua ya kuwa walikuwa watu wa kawaida, wasio na elimu, walishangaa sana, wakatambua kwamba hawa watu walikuwa na Yesu. 14 Lakini kwa kuwa walikuwa wanamwona yule kiwete aliyeponywa amesimama pale pamoja nao, hawakuweza kusema lo lote kuwapinga. 15Wakawaamuru watoke nje ya baraza wakati wakisemezana jambo hilo wao kwa wao. 16Wakaulizana, "Tuwafanyie nini watu hawa? Hatuwezi kukanusha mwujiza huu mkubwa walioufanya ambao ni dhahiri kwa kila mtu Yerusalemu.
17Lakini ili kuzuia jambo hili lisiendelee kuenea zaidi miongoni mwa watu, ni lazima tuwaonye watu hawa ili wasiseme tena na mtu ye yote kwa Jina la Yesu." 18Kisha wakawaita tena ndani na kuwaamuru wasiseme wala kufundisha kamwe kwa hili Jina la Yesu.

### *Imetupasa Kumtii Mungu Kuliko Wanadamu*

19Lakini Petro na Yohana wakajibu, "Amueni ninyi wenyewe iwapo ni haki mbele za Mungu kuwatii ninyi kuliko Mungu. 20Lakini sisi hatuwezi kuacha kusema yale tuliyoyaona na kuyasikia." 21Baada ya vitisho vingi, wakawaacha waende zao. Hawakuona njia yo yote ya kuwaadhibu, kwa sababu ya watu, kwa kuwa watu wote walikuwa wakimsifu Mungu kwa kile kilichokuwa kimetukia.
22Kwa kuwa umri wa yule mtu aliyekuwa ameponywa kwa mwujiza ulikuwa zaidi ya miaka arobaini.

**a** Baraza hapa ina maana "Sanhedrin", ambalo ndilo lililokuwa baraza la juu kabisa la utawla la Kiyahudi, lililokuwa na wazee 70 pamoja na Kuhani Mkuu.

### *Maombi Ya Waamin*

23Mara Petro na Yohana waliopoachiliwa,
walirudi kwa waamini wenzao wakawaeleza
waliyoambiwa na makuhani wakuu na wazee.
24Watu hao waliposikia hayo, wakainua sauti
zao wakamwomba Mungu kwa pamoja
wakasema, "Bwana Mwenyezi, uliyeumba
mbingu na nchi na bahari na kila vitu vyote
vilivyomo, 25Wewe ulisema kwa Roho Mtakatifu
kupitia kwa kinywa cha baba yetu Daudi,
mtumishi Wako, ukasema:

" 'Mbona mataifa wanaghadhibika,
na mataifa yanawaza ubatili?
6Wafalme wa dunia wamejipanga
na watawala wanakusanyika pamoja dhidi ya Bwana
na dhidi ya Kristo wake.'

27Ni kweli Herode na Pontio Pilato pamoja na
watu Mataifa na Waisraeli, walikusanyika katika
mji huu dhidi ya Mwanao Yesu uliyemtia mafuta.
28Wao wakafanya yale ambayo uweza wako na
mapenzi yako yalikuwa yamekusudia yatokee
tangu zamani. 29Sasa, Bwana angalia vitisho
vyao na utuwezeshe sisi watumishi Wako
kulinena neno Lako kwa ujasiri mkuu. 30Nyosha
mkono Wako ili kuponya wagonjwa na kutenda
ishara na miujiza kwa Jina la Mwanao Mtakatifu
Yesu."

31Walipokwisha kuomba, mahali pale
walipokuwa wamekutanika pakatikiswa, nao
wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakanena
neno la Mungu kwa ujasiri.

### *Walioamini Washirikiana Mali Zao*

32Wale walioamini wote walikuwa na moyo
mmoja na nia moja. Wala hakuna hata mmoja
aliyesema cho chote alichokuwa nacho ni mali
yake mwenyewe, lakini walishirikiana kila kitu
walichokuwa nacho. 33Mitume wakatoa
ushuhuda wa kufufuka kwa Bwana Yesu kwa
nguvu nyingi na neema ya Mungu ilikuwa juu
yao wote. 34Wala hapakuwepo mtu ye yote
miongoni mwao aliyekuwa mhitaji, kwa sababu
mara kwa mara wale waliokuwa na mashamba
na nyumba waliviuza, wakaleta thamani ya vitu
vilivyouzwa, 35wakaiweka miguuni kwa wale
mitume, kila mtu akagawiwa kadiri ya mahitaji
yake.

36Yosefu, Mlawi kutoka Kipro, ambaye
mitume walimwita Barnaba, maana yake Mwana
wa Faraja, 37aliuza shamba alilokuwa nalo,
akaleta hizo fedha alizopata na kuziweka
miguuni pa mitume.

### *Anania Na Safira*

**5** Lakini mtu mmoja jina lake Anania pamoja na
mkewe Safira waliuza kiwanja. 2 Mkewe akijua
kikamilifu alificha sehemu ya fedha alizopata,
akaleta kiasi kilichobaki na kukiweka
miguuni mwa mitume.

3Petro akamwuliza, "Anania, mbona
Shetani ameujaza moyo wako ili kumwambia
uongo Roho Mtakatifu, ukaficha sehemu ya
fedha ulizopata kutokana na kiwanja? 4Je, kabla
hujauza hicho kiwanja si kilikuwa mali yako?
Hata baada ya kukiuza, fedha ulizopata si
zilikuwa kwenye uwezo wako? Kwa nini basi
umewaza hila hii moyoni mwako kufanya jambo
kama hili? Wewe hukumwambia uongo
mwanadamu bali Mungu."

5 Anania aliposikia maneno haya
akaanguka chini na kufa. Hofu kuu ikawapata
wote waliosikia jambo lililokuwa limetukia.
6Vijana wakaja, wakaufunga mwili wake,
wakamchukua nje kumzika.

7 Saa tatu baadaye mkewe Anania
akaingia, naye hana habari ya mambo
yaliyotukia. 8Petro akamwuliza, "Niambie, je,
mliuza kiwanja kwa thamani hii?" Akajibu,
"Ndiyo, tuliuza kwa thamani hiyo."

9Ndipo Petro akamwambia, "Imekuwaje
mkakubaliana kumjaribu Roho Mtakatifu wa
Bwana? Tazama! Nyayo za vijana waliomzika
mumeo iko mlangoni, wewe nawe
watakuchukua nje."

10Saa ile ile akaanguka chini miguuni
mwake na kufa, wale vijana waliingia,
wakamkuta amekufa, wakamchukua wakamzika
kando ya mumewe. 11Hofu kuu ikalipata kanisa
lote pamoja na watu wote waliosikia juu ya
matukio haya.

### *Mitume Waponya Wengi*

12Mitume wakafanya ishara nyingi na miujiza
miongoni mwa watu. Nao wale wote walioamini
walikuwa wakikusanyika katika ukumbi wa
Solomoni kwa nia moja. 13Hakuna mtu mwingine
aliyethubutu kuambatana nao ijapokuwa
waliheshimiwa sana na watu. 14Lakini walioamini
wengi wakaongezeka kwa Bwana, idadi kubwa ya
wanaume na wanawake. 15Hata wakawa
wanawaleta wagonjwa na kuwalaza kwenye
magodoro na kwenye vitanda barabarani ili
yamkini Petro akipita kivuli chake

kiwaguse baadhi yao. 16Pia watu wakakusanyika kutoka katika miji iliyokuwa karibu na Yerusalemu, wakileta wagonjwa na watu walioteswa na pepo wachafu, hao wote wakaponywa.

### *Mitume Washtakiwa*

17Kisha Kuhani Mkuu na wenzake wote waliokuwa pamoja naye, (ambao ni wa kundi la Masadukayo,) wakiwa wamejawa na wivu, 18wakawakamata mitume na kuwatia gerezani. 19Lakini wakati wa usiku malaika wa Bwana akaja akafungua milango ya gereza akawatoa nje akawaambia, 20 "Nendeni, mkasimame hekaluni mkawaambie watu maneno yote ya uzima huu mpya.''

21Waliposikia haya wakaenda hekaluni alfajiri wakaendelea kufundisha watu.

Kuhani Mkuu na wale waliokuwa pamoja nao walipowasili, alikusanya baraza na wazee wote wa Israeli wakatuma wale mitume waletwe kutoka gerezani. 22Lakini wale walinzi wa hekalu walipokwenda gerezani hawakuwakuta wale mitume mle. Kwa hiyo wakarudi na kutoa habari. 23Wakasema, "Tumekuta milango ya gereza imefungwa sawasawa na maaskari wa gereza wamesimama nje ya mlango, lakini tulipofungua milango hakuwepo mtu ye yote ndani.'' 24Basi mkuu wa walinzi wa hekalu, viongozi na makuhani waliposikia haya, wakafadhaika na kushangaa sana kwa ajili yao kwamba jambo hili litakuwaje.

25Ndipo mtu mmoja akaja akawaambia, "Tazameni watu wale mliowatia gerezani wako hekaluni wakiwafundisha watu.'' 26Ndipo yule mkuu wa walinzi wa hekalu wakaenda pamoja na maaskari wakawaleta wale mitume, lakini bila ghasia kwa sababu waliogopa kupigwa mawe na watu.

27Wakiisha kuwaleta hao mitume wakawaamuru kusimama mbele ya baraza. Kuhani Mkuu akawahoji. 28"Tuliwaonya kwa nguvu msifundishe kwa jina hili, lakini ninyi mmeijaza Yerusalemu yote mafundisho yenu na tena mmekusudia kuleta damu ya mtu huyu juu yetu.''

29Petro na wale mitume wengine wakajibu, "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. 30Mungu wa baba zetu aliyemfufua Yesu ambaye ninyi mlimwua kwa kumtundika kwenye msalaba. 31 Mungu alimtukuza akamweka mkono wake wa kuume kuwa kiongozi na Mwokozi ili awape Israeli toba na msamaha wa dhambi. 32Nasi tu mashahidi wa mambo haya, vivyo hivyo na Roho Mtakatifu ambaye na Mungu amewapa wale wanaomtii.''

33Wale wajumbe wa baraza la wazee waliposikia haya, walijawa na ghadhabu, wakataka kuwaua wale mitume. 34Lakini Farisayo mmoja, jina lake Gamalieli, aliyekuwa mwalimu wa sheria, aliyeheshimiwa na watu wote, akasimama mbele ya baraza akaamuru wale mitume watolewe nje kwa muda. 35Ndipo alipowaambia wajumbe wa baraza, "Enyi watu wa Israeli, fikirini kwa uangalifu yale mnayotaka kuwatendea watu hawa. 36Kwa maana wakati uliopita aliinuka mtu mmoja jina lake Theuda ambaye alijidai kuwa yeye ni mtu maarufu, akapata wafuasi wapatao 400 walioambatana naye. Lakini aliuawa na wafuasi wake wote wakatawanyika na kupotea. 37Baada yake alitokea Yuda Mgalilaya wakati ule wa kuandikwa orodha ya watu akaongoza kundi la watu kuasi. Yeye naye aliuawa, nao wafuasi wake wakatawanyika. 38Kwa hiyo, kwa shauri hili, nawashauri habari ya jambo hili, jiepusheni na watu hawa. Waacheni waende zao! Kwa maana kama kusudi lao na shughuli yao imetokana na mwanadamu haitafanikiwa. 39Lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamtaweza kuwazuia watu hawa, badala yake mtajikuta mnapigana dhidi ya Mungu"

40Wakapokea ushauri wa Gamalieli. Wakawaita mitume ndani, wakaamuru wachapwe mijeledi, kisha wakawaagiza wasinene tena kwa jina la Yesu, nao wakawaachia waende zao.

41Wale mitume walitoka nje ya baraza, wakiwa wamejaa furaha kwa sababu wamehesabiwa kustahili kupata aibu kwa ajili ya jina la Yesu. 42Hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema kwamba Yesu ndiye Kristo kila siku hekaluni na nyumba kwa nyumba.

### *Saba Wachaguliwa Kuhudumia*

**6** Basi ikawa katika siku hizo, wakati idadi ya wanafunzi ilipokuwa ikiongezeka sana palitokea manung'uniko kati ya Wayahudi wa Kiyunani, dhidi ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahaulika katika mgawanyo wa chakula wa kila siku. 2Wale mitume kumi na wawili wakakusanya wanafunzi wote pamoja, wakasema, "Haitakuwa vema sisi kuacha huduma ya neno la Mungu ili kutumika mezani. 3Kwa hiyo ndugu, chagueni watu saba miongoni

mwenu, watu wenye sifa njema, waliojawa na Roho Mtakatifu na hekima, ambao tunaweza kuwakabidhi kazi hii, 4wakati sisi tutatumia muda wetu mrefu kuomba na kulihudumia lile neno.''

5Yale waliyosema yakawapendeza watu wote, nao wakawachagua Stefano, mtu aliyejawa na imani na Roho Mtakatifu pamoja na Filipo, Prokoro, Nikanori, Timoni, Parmena na Nikolao mwongofu wa kutoka Antiokia. 6Wakawaleta watu hawa mbele ya mitume, nao wakawaombea na kuwawekea mikono juu yao.

7Neno la Mungu likazidi kuenea, idadi ya wanafunzi ikazidi kuongezeka sana katika Yerusalemu hata makuhani wengi wakamwamini Yesu.

### *Kukamatwa Kwa Stefano*

8Stefano, akiwa amejawa na neema na nguvu za Mungu, alifanya ishara na miujiza mikubwa miongoni mwa watu. 9Lakini baadhi ya watu wa sinagogi lililoitwa la 'Watu Huru,' (kama lilivyokuwa linaitwa), la Wakirene, Waiskanderia na wengine kutoka Kilikia na Asia, wakasimama na kujadiliana na Stefano. 10Lakini hawakuweza kushindana na hekima na Roho ambaye kwayo alisema.

11 Ndipo wakawashawishi watu fulani kwa siri ili waseme, "Tumemsikia Stefano akisema maneno ya kufuru dhidi ya Mose na dhidi ya Mungu.''

### *Stefano Afikishwa Mbele ya Baraza*

12Wakawachochea watu, wazee na waalimu wa sheria nao wakamkamata Stefano wakamfikisha mbele ya baraza. 13Wakaweka mashahidi wa uongo ambao walishuhudia wakisema, "Mtu huyu kamwe haachi kusema dhidi ya mahali hapa patakatifu na dhidi ya torati. 14Kwa maana tumemsikia akisema kwamba huyu Yesu wa Nazareti atapaharibu mahali patakatifu na kubadili desturi zote tulizopewa na Mose.''

15Watu wote waliokuwa wameketi katika baraza wakimkazia macho Stefano, wakaona uso wake unang'aa kama uso wa malaika.

### *Hotuba ya Stefano*

**7** Ndipo kuhani mkuu alimwuliza Stefano, "Je, mashtaka haya ni ya kweli?"

2Stefano akajibu, "Ndugu zangu na baba zangu, nisikilizeni! Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu Abrahamu, alipokuwa bado yuko Mesopotamia, kabla hajaishi Harani, 3akamwambia, 'Ondoka katika nchi yako na kutoka kwa jamii yako uende katika nchi nitakayokuonyesha.'

4"Hivyo aliondoka katika nchi ya Wakaldayo akaenda kukaa Harani. Baada ya kifo cha baba yake, Mungu akamtoa huko akamleta katika nchi hii ambayo mnaishi sasa. 5Mungu hakumpa urithi wo wote katika nchi hii, hakumpa hata mahali pa kuweka wayo mmoja. Bali Mungu alimwahidi kuwa yeye na uzao wake baada yake wangeirithi hii nchi, ingawa wakati huo Ibrahimu hakuwa na mtoto. 6Mungu akasema naye hivi, 'Wazao wako watakuwa wageni kwenye nchi ambayo si yao, nao watafanywa watumwa na kutendewa vibaya miaka 400.' 7Mungu akasema, 'Lakini mimi nitaliadhibu taifa lile watakalolitumikia kama watumwa na baadaye watatoka katika nchi hiyo na kuniabudu mahali hapa.' 8Ndipo akampa Abrahamu agano la tohara. Naye Abrahamu akamzaa Isaki na kumtahiri siku ya nane baada ya kuzaliwa kwake. Baadaye Isaki akamzaa Yakobo, naye Yakobo akawazaa wale wazee wetu wakuu kumi na wawili.

9"Kwa sababu wazee wetu wakuu walimwonea wivu Yosefu ndugu yao, walimwuza kama mtumwa huko Misri. Lakini Mungu alikuwa pamoja naye. 10Akamwokoa kutoka katika mateso yote yaliyompata, tena akampa kibali na hekima aliposimama mbele ya Farao, Mfalme wa Misri, ambaye alimweka kuwa mtawala juu ya Misri na juu ya jumba lote la kifalme.

11"Basi kukawa na njaa katika nchi yote ya Misri na Kanaani, ikasababisha dhiki kubwa, nao baba zetu wakawa hawana chakula. 12Lakini Yakobo aliposikia kwamba kuna nafaka huko Misri, aliwatuma baba zetu, wakaenda huko kwa mara yao ya kwanza. 13Walipokwenda mara ya pili, Yosefu alijitambulisha kwa ndugu zake, nao ndugu zake Yosefu wakajulishwa kwa Farao. 14 Ndipo Yosefu akatuma wamlete Yakobo baba yake kutoka Misri pamoja na jamaa yake yote, jumla yao walikuwa watu sabini na watano. 15 Hivyo Yakobo akaenda Misri ambako yeye na baba zetu walifia. 16Miili yao ilirudishwa Shekemu na kuzikwa katika kaburi ambalo Abrahamu alinunua kutoka kwa wana wa Hamori kwa kiasi Fulani cha fedha.

17"Lakini wakati ulipokuwa unakaribia wa kutimizwa kwa ile ahadi ambayo Mungu alikuwa

amempa Abrahamu, watu wetu walizidi na kuongezeka. 18 Ndipo mfalme mwingine ambaye hakujua lo lote kuhusu Yosefu, akatawala Misri. 19Huyu mfalme akawatendea watu wetu kwa hila na kuwatesa baba zetu kwa kuwalazimisha wawatupe watoto wao wachanga ili wafe.

20 “Wakati huo Mose alizaliwa, naye alikuwa mtoto mzuri sana machoni pa Mungu. Akalelewa nyumbani kwa wazazi wake kwa muda wa miezi mitatu. 21 Waliposhindwa kumficha zaidi, wakamweka nje mtoni na binti Farao akamchukua akamtunza kama mtoto wake mwenyewe. 22Mose akafundishwa hekima yote ya Wamisri, akawa mtu hodari kwa maneno na matendo.

23“Mose alipokuwa na umri wa miaka arobaini aliamua kuwatembelea ndugu zake Waisraeli. 24Aliona mmoja wao akionewa na Mmisri, akamtetea yule aliyeonewa, akampiga yule Mmisri akamwua kulipiza kisasi. 25Mose alidhani wangeelewa kwamba Mungu akimtumia ili kuwaokoa, lakini wao hawakuelewa. 26Siku iliyofuata Mose aliwakuta Waisraeli wawili wakigombana, akajaribu kuwapatanisha kwa kuwaambia, ‘Enyi watu, ninyi ni ndugu, mbona mnataka kuumizana?’

27“Lakini yule mtu aliyekuwa akimwonea mwenzake akamsukuma Mose kando, akamwuliza, ‘Ni nani alikuweka uwe mtawala na mwamuzi juu yetu? 28Je, unataka kuniua kama ulivyomwua yule Mmisri jana?’ 29Mose aliposikia maneno haya, alikimbilia huko Midiani alikokaa kama mgeni, naye akapata. watoto wawili wa kiume.

30“Basi baada ya miaka arobaini kupita, malaika wa Mungu akamtokea Mose jangwani karibu na Mlima Sinai katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto. 31Alipoona mambo haya, alishangaa yale maono. Aliposogea ili aangalie kwa karibu, akaisikia sauti ya Bwana, ikisema: 32 ‘Mimi ndimi Mungu wa baba zako, Mungu wa Abrahamu, Isaki na Yakobo.’ Mose alitetemeka kwa hofu na hakuthubutu kutazama.

33“Ndipo Bwana akamwambia, ‘Vua viatu vyako kwa maana hapo uliposimama ni mahali patakatifu. 34 Hakika nimeona mateso ya watu wangu huko Misri. Nimesikia kilio chao cha uchungu, nami nimeshuka ili niwaokoe. Basi sasa njoo, nami nitakutuma Misri.’

35“Huyu ndiye Mose yule waliyemkataa wakisema, ‘Ni nani aliyekufanya uwe mtawala na mwamuzi juu yetu?’ Alikuwa ametumwa na Mungu mwenyewe kuwa mtawala na mkombozi wao, kwa njia ya yule malaika aliyemtokea katika kile kichaka. 36Aliwaongoza wana wa Israeli kutoka Misri, baada ya kufanya ishara na maajabu mengi huko Misri, katika bahari ya Shamu na katika jangwa kwa muda wa miaka arobaini.

37“Huyu ndiye yule Mose aliyewaambia Waisraeli, ‘Mungu atawainulia nabii kutoka miongoni mwa ndugu zenu.’ 38Huyu ndiye yule Mose aliyekuwa katika kusanyiko huko jangwani pamoja na baba zetu na yule malaika aliyesema naye kwenye Mlima Sinai pamoja na baba zetu, naye akapokea maneno yaliyo hai ili atupatie.

39“Lakini baba zetu walikataa kumtii Mose, badala yake wakamkataa na kuielekeza mioyo yao Misri tena. 40Wakamwambia Aroni, “Tufanyie miungu watakaotuongoza, kwa maana mtu huyu Mose aliyetutoa Misri hatujui yaliyompata.’ 41Huu ndio wakati walipotengeneza sanamu katika umbo la ndama, wakailetea sadaka kufanya maadhimisho kwa ajili ya kile kitu walichotengeneza kwa mikono yao wenyewe. 42Ndipo Mungu akageuka, akawaacha waabudu jeshi lote la mbinguni kama ilivyoandikwa katika kitabu cha manabii:

“ ‘Je, mlinitolea Mimi dhabihu na sadaka
kwa kipindi cha miaka arobaini kule
jangwani, enyi nyumba ya Israeli?
43La, ninyi mlichukua hema ya Moleki
na ya mungu wenu Refani,
vinyago mlivyotengeneza ili kuviabudu. Kwa
hiyo nitawapeleka mbali kuliko Babeli.’ 44“Baba
zetu walikuwa na ile Hema ya Ushuhuda
huko jangwani. Lilikuwa limetengenezwa
kama Mungu alivyokuwa amemwelekeza
Mose, kulingana na kielelezo alichoona.
45Baba zetu wakiisha kulipokea hema kwa
kupokezana wakiongozwa na Yoshua katika
milki ya nchi kutoka kwa yale mataifa ambayo
Mungu aliyafukuza mbele yao. Ilidumu mpaka
wakati wa Daudi, 46 ambaye alipendwa na
Mungu, naye akaomba atafute maskani katika
nyumba ya Yakobo. 47Lakini ilikuwa
Solomoni ndiye aliyemjengea Mungu
nyumba.

48“Hata hivyo Mungu Aliye Mkuu sana hakai kwenye nyumba zilizojengwa kwa mikono na wanadamu. Kama nabii alivyosema:

49“ ‘Mbingu ni kiti changu cha Enzi
na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu.

Mtanijengea nyumba ya namna gani?”
asema Bwana.
Au mahali pangu pa kupumzikia
patakuwa wapi?
50Je, mikono yangu haikuumba vitu hivi vyote?’

51“Ninyi watu wenye shingo ngumu, wasio
tahiriwa mioyo wala masikio, daima hamwachi
kumpinga Roho Mtakatifu, kama walivyofanya
baba zetu. 52Je, kuna nabii gani ambaye baba
zetu hawakumtesa? Waliwaua wale waliotabiri
habari za kuja kwake yule Mwenye Haki, nanyi
sasa mmekuwa wasaliti wake na wauaji. 53Ninyi
ndio mlipokea sheria zilizoletwa kwenu na
malaika, lakini hamkuzitii.’’

### *Stefano Apigwa Mawe*

54Waliposikia haya wakaghadhibika,
wakamsagia Stefano meno. 55Lakini yeye
Stefano akiwa amejazwa Roho Mtakatifu,
alikaza macho mbinguni, akaona utukufu wa
Mungu, naye Yesu akiwa amesimama mkono
wa kuume wa Mungu. 56Akasema, “Tazameni!
Naona mbingu zimefunguka na Mwana wa
Adamu amesimama upande wa kuume wa
Mungu.’’

57Lakini wao wakapiga kelele kwa sauti
kubwa, wakaziba masikio yao, wakamrukia kwa
nia moja. 58Wakamtupa nje ya mji, wakampiga
kwa mawe. Nao mashahidi wakaweka nguo zao
miguuni mwa kijana mmoja aitwae Sauli.

59Walipokuwa wakimpiga mawe, Stefano
aliomba, “Bwana Yesu, pokea roho yangu”
60Kisha akapiga magoti, akalia kwa sauti kubwa
akasema, “Bwana usiwahesabie dhambi hii.’’
Baada ya kusema haya, akalala.

**8** Naye Sauli alikuwepo pale akipendezwa na
kuuawa kwa Stefano.

### *Kanisa Lateswa Na Kutawanyika*

Siku ile kukatukia mateso makuu dhidi ya
kanisa huko Yerusalemu, waamini wote
isipokuwa mitume wakatawanyika, wakakimbilia
Uyahudi na Samaria. 2Watu wacha Mungu
wakamzika Stefano na kumwombelezea sana.
3Lakini kwa habari ya Sauli alikuwa analiharibu
kanisa, akiingia nyumba kwa nyumba,
akiwaburuta wanawake, wanaume na kuwatia
gerezani.

### *Filipo Ahubiri Injili Samaria*

4Kwa hiyo wale waliotawanyika wakalihubiri
neno la Mungu kila mahali walipokwenda.
5Filipo akateremkia mji mmoja wa Samaria
akawahubiria habari za Kristo. 6Watu
walipomsikia Filipo na kuona ishara na miujiza
aliyofanya, wakasikiliza kwa bidii yale
aliyosema. 7Pepo wachafu wakawa wakiwatoka
watu wengi, huku wakipiga kelele na wengi
waliopooza na viwete, wakaponywa. 8Hivyo
pakawa na furaha kuu katika mji huo.

### *Simoni Mchawi*

9Basi mtu mmoja jina lake Simoni alikuwa
amefanya uchawi kwa muda mrefu katika mji
huo akishangaza watu wote wa Samaria.
Alijitapa kwamba yeye ni mtu mkuu, 10watu
wote wakubwa kwa wadogo wakamsikiliza na
kumaka wakisema “Mtu huyu ndiye ile nguvu ya
kiungu ijulikanayo kama ‘Uweza Mkuu’.”
11Wakamfuata kwa sababu kwa muda mrefu
alikuwa amewashangaza kwa uchawi wake.
12Lakini watu walipomwamini Filipo akihubiri
habari njema ya ufalme wa Mungu na jina la
Yesu Kristo, wakabatizwa wanaume na
wanawake. 13Simoni naye akaamini na
akabatizwa. Akamfuata Filipo kila mahali,
akistaajabishwa na ishara kuu na miujiza
aliyoiona.

14Basi mitume waliokuwa Yerusalemu
waliposikia kuwa Samaria walipokea neno la
Mungu, wakawatuma Petro na Yohana waende
huko. 15Nao walipofika wakawaombea ili
wampokee Roho Mtakatifu, 16kwa sababu Roho
Mtakatifu alikuwa bado hajawashukia hata
mmoja ila wamebatizwa tu katika jina la Bwana
Yesu. 17Ndipo Petro na Yohana wakaweka
mikono yao juu ya wale waliobatizwa, nao
wakapokea Roho Mtakatifu.

18 Simoni alipoona kuwa watu wanapokea
Roho Mtakatifu mitume walipoweka mikono juu
yao, akawapa fedha 19akisema, “Nipeni na mimi
uwezo huu ili kila mtu nitakayeweka mikono
yangu juu yake apate kupokea Roho Mtakatifu.”

20Petro akamjibu, “Fedha yako na iangamie
pamoja nawe, kwa sababu ulidhani unaweza
kununua karama ya Mungu kwa fedha! 21Wewe
huna sehemu wala fungu katika huduma hii kwa
kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu.
22Kwa hiyo tubia uovu huu wako na umwombe
Mungu, ili yamkini aweze kusamehe mawazo
uliyo nayo moyoni mwako. 23 Kwa maana
ninaona kwamba wewe umejawa na uchungu
na ni mfungwa wa dhambi,”

24Ndipo Simoni akajibu, “Niombeeni kwa
Bwana, ili hayo mliyosema lo lote lisinitukie.”

[25]Nao walipokwisha kutoa ushuhuda na kuhubiri neno la Bwana, wakarudi Yerusalemu wakihubiri injili katika vijiji vingi vya Samaria.

### *Filipo Na Towashi wa Kushi*

[26]Basi Malaika wa Bwana akamwambia Filipo, "Nenda upande wa kusini kwenye ile barabara itokayo Yerusalemu kuelekea Gaza ambayo ni jangwa." [27]Hivyo akaondoka na kwenda. Akiwa njiani akakutana na Towashi wa Kushi, aliyekuwa afisa mkuu, mwenye mamlaka juu ya hazina zote za Kandake, Malkia wa Kushi. Huyu Towashi alikuwa amekwenda Yerusalemu ili kuabudu, [28]naye akiwa njiani kurudi nyumbani alikuwa ameketi garini mwake akisoma kitabu cha nabii Isaya. [29]Roho Mtakatifu akamwambia Filipo, "Nenda kwenye lile gari ukae karibu na ushikamane nalo.''

[30]Ndipo Filipo akakimbilia na kumsikia yule mtu anasoma kitabu cha nabii Isaya. Filipo akamwuliza, "Je, yanakuelea hayo usemayo?"

[31]Yule towashi akasema, "Nitawezaje kuelewa mtu asiponifafanulia?" Hivyo akamkaribisha Filipo ili apande na kuketi pamoja naye.

[32]Huyu Towashi alikuwa anasoma fungu hili la maandiko:

"Aliongozwa kama kondoo aendae
machinjoni,
kama mwana-kondoo anyamazavyo
mbele yake yeye akamtaye
manyoya,
hivyo hakukifungua kinywa chake.
[33]Katika kufedheheshwa kwake alinyimwa haki
yake.
Nani awezaye kueleza juu ya kizazi chake?
Kwa maana maisha yake yameondolewa
kutoka duniani.''

[34]Yule Towashi akamwuliza Filipo, "Tafadhali niambie, nabii huyu anena kwa habari zake mwenyewe au habari za mtu mwingine?" [35]Ndipo Filipo akaanza kutumia fungu lile la maandiko akamweleza habari njema za Yesu.

[36]Walipokuwa wakiendelea na safari wakafika mahali palipokuwa na maji, yule towashi akamwambia Filipo, "Tazama, hapa kuna maji. Kitu gani kitanizuia nisibatizwe?" ([37]Filipo akamwambia, "Kama ukiamini kwa moyo wako wote unaweza kubatizwa." Akajibu, "Naamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu)." [38]Naye akaamuru lile gari lisimamishwe. Wakatelemka kwenye maji wote wawili, yule towashi na Filipo, naye akambatiza. [39]Nao walipopanda kutoka kwenye maji, ghafula Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, naye towashi hakumwona tena, lakini akaenda zake akifurahi. [40]Filipo akajikuta yuko Azoto, akasafiri akihubiri injili katika miji yote mpaka alipofika Kaisaria.

### *Kuongoka Kwa Sauli*

**9** Wakati ule ule, Sauli alikuwa bado anazidisha vitisho vya kuua wanafunzi wa Bwana, akamwendea Kuhani Mkuu, [2]naye akamwomba Kuhani Mkuu ampe barua ya kwenda kwenye masinagogi huko Dameski, ili akimkuta mtu ye yote wa "Njia Ile", akiwa mwanaume au mwanamke, aweze kuwafunga na kuwaleta Yerusalemu. [3]Basi katika safari yake, alipokuwa akikaribia Dameski, ghafula nuru kutoka mbinguni ikamwangaza kote kote. [4]Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, "Sauli, Sauli, mbona unanitesa?"

[5]Sauli akajibu, "U nani wewe, Bwana?"

Ile sauti ikajibu, "Mimi ni Yesu unayemtesa". [6]"Sasa inuka uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda."

[7]Watu wale waliokuwa wakisafiri pamoja na Sauli wakasimama bila kuwa na la kusema, kwa sababu walisikia sauti lakini hawakumwona aliyekuwa akizungumza. [8]Sauli akainuka kutoka pale chini na alipojaribu kufungua macho yake hakuweza kuona kitu cho chote. Basi wakamshika mkono wakamwongoza mpaka Dameski. [9]Naye kwa muda wa siku tatu alikuwa kipofu naye hakula wala kunywa cho chote.

[10]Huko Dameski alikuwepo mwanafunzi mmoja jina lake Anania. Bwana alimwita katika maono, "Anania!"

akajibu, "Mimi hapa Bwana."

[11]Bwana akamwambia, "Ondoka uende katika barabara iitwayo Nyofu ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu kutoka Tarso, jina lake Sauli wakati huu anaomba, [12]katika maono amemwona mtu aitwaye Anania akija na kuweka mikono juu yake ili apate kuona tena."

[13]Anania akajibu, "Bwana, nimesikia kutoka kwa watu wengi habari nyingi kuhusu mtu huyu na madhara yote aliyowatendea watakatifu wako huko Yerusalemu. [14]Naye amekuja hapa Dameski akiwa na mamlaka kutoka kwa viongozi wa makuhani ili awakamate wote wanaotaja jina lako."

15Lakini Bwana akamwambia Anania, "Nenda! Mtu huyu ni chombo changu kiteule nilichokichagua apate kulichukua jina langu kwa watu Mataifa na wafalme wao na mbele ya watu wa Israeli. 16 Nami nitamwonyesha jinsi impasavyo kuteseka kwa ajili ya jina langu."

17Kisha Anania akaenda, akaingia mle nyumbani. Akaweka mikono yake juu ya Sauli akasema, "Ndugu Sauli, Bwana Yesu aliyekutokea njiani amenituma kwako ili upate kuona tena na ujazwe Roho Mtakatifu." 18Ghafula vitu kama magamba vikaanguka kutoka machoni mwa Sauli, akapata kuona tena. Akasimama, akabatizwa. 19 Kisha akala chakula, akapata nguvu tena. Sauli akakaa siku kadhaa pamoja na wanafunzi huko Dameski.

### *Sauli Ahubiri Dameski*

20Papo hapo akaanza kuhubiri kwenye masinagogi kwamba "Yesu Kristo ni mwana wa Mungu" 21Watu wote waliomsikia Sauli walishangaa na kuuliza, "Huyu si yule mtu aliyesababisha maangamizi makuu miongoni mwa watu waliolitaja jina hili na si amekuja hapa kwa kusudi la kuwakamata na kuwapeleka wakiwa wamefungwa mbele ya viongozi wa makuhani?" 22Sauli akazidi kuwa na nguvu na kuwashangaza Wayahudi walioishi Dameski kwa kuthibitisha kuwa Yesu ndiye Mesiya.

23Baada ya siku nyingi kupita, Wayahudi walifanya shauri kumwua Sauli. 24Lakini shauri lao likajulikana kwa Sauli. Wayahudi walikuwa wakilinda malango yote ya mjini, mchana na usiku ili wapate kumwua. 25Lakini wafuasi wake wakamchukua usiku wakamshusha kwa kapu kupitia mahali penye nafasi ukutani.

### *Sauli Huko Yerusalemu*

26Sauli alipofika Yerusalemu akajaribu kujiunga na wanafunzi lakini wote walimwogopa, kwa maana hawakuamini kwamba kweli naye alikuwa mwanafunzi. 27Lakini Barnaba akamchukua, akampeleka kwa wale mitume, akawaeleza jinsi Sauli akiwa njiani alivyomwona Bwana na jinsi Bwana alivyosema naye na jinsi alivyohubiri kwa ujasiri kwa jina la Yesu huko Dameski. 28Kwa hiyo Sauli akakaa nao akishirikiana nao na akihubiri wazi wazi kwa jina laYesu kila mahali huko Yerusalemu. 29Alinena na kuhojiana na Wayahudi wenye asili ya Kiyunani lakini wao walijaribu kumwua. 30Wale ndugu walipopata habari wakampeleka hadi Kaisaria, wakamsafirisha kwenda Tarso.

31Ndipo kanisa katika Uyahudi wote, Galilaya na Samaria likafurahia wakati wa amani. Likatiwa nguvu na likaendelea kudumu katika kumcha Bwana na kwa faraja ya Roho Mtakatifu, idadi yake ikazidi kuongezeka.

### *Kuponywa Kwa Ainea*

32 Petro alipokuwa akisafiri sehemu mbali mbali alikwenda kuwatembelea watakatifu walioishi huko Lida. 33Huko alimkuta mtu mmoja aitwaye Ainea, ambaye alikuwa amepooza na kwa muda wa maika minane alikuwa hajaondoka kitandani. 34Petro akamwambia, "Ainea, Yesu Kristo anakuponya, inuka utandike kitanda chako." Mara Ainea akainuka. 35Watu wote wa Lida na Sharoni walipomwona Ainea akitembea wakamgeukia Bwana.

### *Petro Amfufua Dorkasi*

36Huko Yafa palikuwa na mwanafunzi jina lake Tabitha ambalo kwa Kiyunani ni Dorkasi, maana ya paa. Huyu alikuwa mkarimu sana, akitenda mema na kuwasaidia maskini. 37Wakati huo akaugua akafa, wakiisha kuuosha mwili wake wakauweka katika chumba cha ghorofani. 38Kwa kuwa Yafa hapakuwa mbali sana na Lida, wanafunzi waliposikia kwamba Petro yuko huko waliwatuma watu wawili kwake ili kumwomba, "Tafadhali njoo huku pasipo kukawia."

39Kwa hiyo Petro akainuka akaenda nao, naye alipowasili, wakampeleka hadi kwenye chumba cha ghorofani alipokuwa amelazwa. Wajane wengi walisimama karibu naye wakilia na kuonyesha majoho na nguo nyingine ambazo Dorkasi alikuwa amewashonea alipokuwa pamoja nao.

40 Petro akawatoa wote nje ya kile chumba, kisha akapiga magoti akaomba, akaugeukia ule mwili akasema, "Tabitha, inuka." Akafumbua macho yake na alipomwona Petro, akaketi. 41Petro akamshika mkono akamwinua, ndipo akawaita wale watakatifu na wajane akawakabidhi kwao akiwa hai. 42Habari hizi zikajulikana sehemu zote za Yafa na watu wengi wakamwamini Bwana. 43Petro akakaa Yafa kwa siku nyingi akiishi na Simoni mtengenezaji ngozi.

### *Mungu Ajibu Maombi Ya Kornelio*

#### *Kornelio Amwita Petro*

**10** Katika mji wa Kaisaria palikuwa na mtu jina lake Kornelio, ambaye alikuwa jemadari wa kile kilichojulikana kama kikosi cha Kiitalia. 2Yeye alikuwa mcha Mungu pamoja na wote wa nyumbani mwake, aliwapa watu sadaka nyingi na kumwomba Mungu daima. 3Siku moja alasiri, yapata saa tisa, aliona maono wazi wazi malaika wa Mungu akimjia na kumwambia, "Kornelio!"

4Kornelio akamkazia macho kwa hofu akasema, "Kuna nini, Bwana?"

Malaika akamwambia, "Sala zako na sadaka zako kwa wahitaji zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu. 5Sasa tuma watu waende Yafa wakamwite mtu mmoja jina lake Simoni aitwaye Petro. 6Yeye anaishi na Simoni mtengenezaji ngozi ambaye nyumba yake iko kando ya bahari."

7Yule malaika aliyekuwa akizungumza naye alipoondoka, Kornelio akawaita watumishi wake wawili pamoja na askari mmoja mcha Mungu aliyekuwa mmoja wa wale waliomtumikia. 8Akawaambia mambo yote yaliyotukia, kisha akawatuma waende Yafa.

### *Maono Ya Petro*

9Siku ya pili yake, walipokuwa wameukaribia mji, wakati wa adhuhuri, Petro alipanda juu ghorofani kuomba. 10Alipokuwa akiomba akaona njaa, akatamani kupata chakula. Lakini wakati walipokuwa wakiandaa akalala usingizi mzito sana. 11 Akaona mbingu zimefunguka na kitu kama nguo kubwa ikishushwa kwa ncha zake nne. 12Ndani yake walikuwepo aina zote za wanyama wenye miguu minne, nao watambaao na ndege wa angani. 13Ndipo sauti ikamwambia "Petro, ondoka, uchinje na ule."

14Petro akajibu, "La Bwana! Sijakula kamwe kitu cho chote kilicho najisi."

15Ile sauti ikasema naye tena mara ya pili, "Usikiite najisi kitu cho chote alichokitakasa Bwana."

16Jambo hili likatukia mara tatu na ghafula ile nguo ikarudishwa mbinguni.

17Wakati Petro akiwa bado anajiuliza kuhusu maana ya maono haya, wale watu waliokuwa wametumwa na Kornelio wakauliza nyumba ya Simoni mtengenezaji ngozi wakawa wamesimama mbele ya lango. 18Wakabisha hodi na kuuliza kama Simoni aliyeitwa Petro alikuwa anaishi hapo.

19Wakati Petro akiwa anafikiria juu ya yale maono, Roho Mtakatifu akamwambia, "Simoni, wako watu watatu wanaokutafuta. 20Ondoka na ushuke, usisite kwenda nao kwa kuwa mimi nimewatuma."

21Petro akashuka na kuwaambia wale watu waliokuwa wametumwa kutoka kwa Kornelio, "Mimi ndiye mnayenitafuta. Mmekuja kwa sababu gani?"

22Wale watu wakamjibu, "Tumetumwa na Kamanda Kornelio ambaye ni mtu mwema anayemcha Mungu na kusifiwa na Wayahudi wote. Yeye ameagizwa na malaika wa Mungu akukaribishe nyumbani kwake, ili asikilize maneno utakayomwambia." 23Basi Petro akawakaribisha wakafuatana naye ndani akawapa pa kulala. Kesho yake aliondoka na kwenda pamoja na baadhi ya ndugu kutoka Yafa.

### *Petro Nyumbani Mwa Kornelio*

24Siku iliyofuata wakawasili Kaisaria. Kornelio alikuwa akiwangoja pamoja na jamaa yake na marafiki zake wa karibu. 25Petro alipokuwa akiingia ndani, Kornelio alikuja kumlaki, akaanguka miguuni pake kwa heshima. 26Lakini Petro akamwinua akamwambia, "Simama, mimi ni mwanadamu tu."

27Petro alipokuwa akizungumza naye akaingia ndani na kukuta watu wengi wamekusanyika. 28Akawaambia, "Mnajua kabisa kwamba ni kinyume cha sheria yetu Myahudi kuchangamana na mtu Mmataifa au kumtembelea. Lakini Mungu amenionyesha kwamba nisimwite mtu ye yote kuwa najisi au asiye safi. 29Ndiyo sababu ulipotuma niitwe nilikuja bila kupinga lo lote. Basi sasa naomba unieleze kwa nini umeniita?"

30Kornelio akajibu, "Siku nne zilizopita, nilikuwa nyumbani nikisali saa kama hii, saa tisa alasiri. Ghafula mtu mwenye nguo za kumetameta akasimama mbele yangu, 31akasema, 'Kornelio, maombi yako yamefikiwa na sadaka zako zimekumbukwa mbele za Mungu'. 32Basi tuma watu waende Yafa wakaulize mtu mmoja Simoni aitwaye Petro, yeye ni mgeni katika nyumba ya Simoni mtengenezaji ngozi, ambaye nyumba yake iko kando ya bahari.' 33Nilituma watu kwako mara moja, nawe umefanya vema kuja. Basi sasa sisi sote tuko hapa mbele za Mungu kuyasikiliza yote ambayo Bwana amekuamuru kutuambia".

### *Hotuba Ya Petro*

**34**“Ndipo Petro akafumbua kinywa chake akasema, “Mungu hana upendeleo, **35**Lakini katika kila taifa ,kila mtu amchaye na kutenda yaliyo haki hukubaliwa naye. **36**Ninyi mnajua ule ujumbe uliotumwa kwa Israeli, ukitangaza habari njema ya amani kwa Yesu Kristo. Yeye ni Bwana wa wote. **37**Mnajua yale yaliyotukia katika Uyahudi wote kuanzia Galilaya baada ya mahubiri ya Yohana Mbatizaji: **38**Jinsi Mungu alivyomtia Yesu wa Nazareti mafuta katika Roho Mtakatifu na jinsi alivyokwenda huku na huko akitenda mema na kuponya wote waliokuwa wameonewa na nguvu za Shetani, kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye.

**39**“Sisi ni mashahidi wa mambo yote aliyoyafanya katika Uyahudi na Yerusalemu. Wakamwua kwa kumtundika msalabani. **40**Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu siku ya tatu na akamwezesha kuonekana na watu. **41**Hakuonekana kwa watu wote, lakini kwetu sisi tuliochaguliwa na Mungu kuwa mashahidi, ambao tulikula na kunywa naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu. **42** Naye alituamuru kuhubiri kwa watu wote na kushuhudia kwamba yeye ndiye aliyetiwa mafuta na Mungu kuwa hakimu wa walio hai na wafu. **43** Manabii wote walishuhudia juu yake kwamba kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika jina lake.”

### *Mataifa Wapokea Roho Mtakatifu*

**44** Wakati Petro akiwa anasema maneno hayo, Roho Mtakatifu aliwashukia wote waliokuwa wakisikiliza ule ujumbe. **45**Wale wa tohara waliomini waliokuwa wamekuja pamoja na Petro walishangaa kuona kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu kimemwagwa juu ya watu Mataifa. **46**Kwa kuwa waliwasikia wakinena kwa lugha mpya na kumwadhimisha Mungu.

Ndipo Petro akasema, **47**“Je, kuna mtu ye yote anayeweza kuzuia watu hawa wasibatizwe kwa maji? Wamempokea Roho Mtakatifu kama sisi tulivyompokea.” **48**Kwa hiyo akaamuru wabatizwe kwa jina la Yesu Kristo. Wakamsihi Petro akae nao kwa siku chache.

### *Petro Aeleza Alivyotumwa Kwa Watu Mataifa*

**11** Mitume na ndugu walioamini waliokuwa huko Uyahudi wakasikia kuwa watu Mataifa nao wamepokea neno la Mungu. **2** Hivyo Petro alipopanda Yerusalemu, wale wa tohara waliokuwa wameamini wakamshutumu, **3**wakisema, “Kwa nini ulikwenda kwa watu wasiotahiriwa na kula pamoja nao?”

**4**Ndipo Petro akaanza kuwaeleza kuhusu mambo yote yalivyotokea hatua kwa hatua akisema, **5**“Nilikuwa katika mji wa Yafa nikiomba, nami katika usingizi mzito nikaona maono. Kulikuwa na kitu kama nguo kubwa ikishuka kutoka mbinguni, ikishushwa kwa ncha zake nne, nayo ikanikaribia. **6** Nilipoangalia ndani yake kwa karibu niliona wanyama wenye miguu minne, wanyama wa mwitu, watambaao na ndege wa angani. **7**Ndipo nikasikia sauti ikiniambia ‘Petro, ondoka uchinje ule’.

**8**“Nikajibu, ‘La hasha Bwana! Kitu cho chote kilicho najisi hakijaingia kinywani mwangu’.

**9**“Sauti ikasema kutoka mbinguni mara ya pili, ‘Usikiite najisi kitu cho chote Mungu alichokitakasa.’ **10**Jambo hili lilitokea mara tatu, ndipo kile kitu kikavutwa tena mbinguni.

**11**“Wakati ule ule watu watatu, waliokuwa wametumwa kutoka Kaisaria waliwasili katika nyumba niliyokuwa nikikaa. **12**Roho Mtakatifu akaniambia niende nao bila kuwa na ubaguzi kati yao na sisi. Hawa ndugu sita pia walifuatana nami, nasi tukaingia nyumbani mwa huyo Kornelio. **13** Akatuambia jinsi alivyoona malaika aliyekuwa amesimama katika nyumba yake na kusema, ‘Tuma watu waende Yafa wakamlete Simoni aitwaye Petro. **14**Yeye atakupa ujumbe ambao kwa huo wewe na wa nyumbani mwako wote mtaokoka.’

**15**“Nami nilipoanza kusema, Roho Mtakatifu akashuka juu yao kama vile alivyotushukia sisi hapo mwanzo. **16**Nami nikakumbuka neno la Bwana alivyosema, ‘Yohana alibatiza kwa maji, lakini ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu.’ **17**Basi ikiwa Mungu aliwapa hawa watu kipawa kile kile alichotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu, mimi ni nani hata nifikirie kuwa ningeweza kumpinga Mungu?”

**18** Waliposikia haya hawakuwa na la kupinga zaidi. Nao wakamwadhimisha Mungu wakisema, “Basi, Mungu amewapa hata watu Mataifa toba iletayo uzima wa milele.”

### *Kanisa Huko Antiokia*

**19**Basi wale waliotawanyika kwa ajili ya mateso yaliyotokana na kifo cha Stefano, wakasafiri hadi Foinike na Kipro na Antiokia. Nao hawakusema neno na mtu ye yote isipokuwa Wayahudi. **20**Lakini baadhi yao walikuwapo watu wa Kipro na Kirene, ambao

walipokuja Antiokia walinena na Wayunani pia wakimhubiri Bwana Yesu. 21Mkono wa Bwana ulikuwa pamoja nao, nayo idadi kubwa ya watu wakaamini na kumgeukia Bwana.

22Habari hizi zilipofika masikioni mwa kanisa huko Yerusalemu, wakamtuma Barnaba aende Antiokia. 23Alipofika na kuona madhihirisho ya neema ya Mungu, akafurahi na kuwatia moyo waendelee kuwa waaminifu kwa Bwana kwa mioyo yao yote. 24Barnaba alikuwa mtu mwema, aliyejaa Roho Mtakatifu, mwenye imani, nayo idadi kubwa ya watu wakaongezeka kwa Bwana.

25 Kisha Barnaba akaenda Tarso kumtafuta Sauli, 26naye alipompata akamleta Antiokia. Hivyo kwa mwaka mzima Barnaba na Sauli wakakutana na kanisa na kufundisha idadi kubwa ya watu. Ilikuwa ni katika kanisa la Antiokia kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa ‘Wakristo.’

27Wakati huo manabii walishuka toka Yerusalemu hadi Antiokia. 28Mmoja wao, jina lake Agabo, akasimama akatabiri kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itaenea ulimwengu nzima. Njaa hiyo ilitokea wakati wa utawala wa Klaudio. 29Mitume wakaamua kwamba kila mtu, kulingana na uwezo wake alio nao, atoe msaada kwa ajili ya ndugu wanaoishi Uyahudi. 30Wakafanya hivyo, misaada yao ikapelekwa kwa wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli.

### *Yakobo Auawa, Petro Atiwa Gerezani*

**12** Ilikuwa wakati kama huu Mfalme Herode Agripa aliwakamata baadhi ya watu wa kanisa. 2Akaamuru Yakobo, ndugu yake Yohana, auawe kwa upanga. 3Alipoona jambo hilo limewapendeza Wayahudi, akaendelea, akamkamata pia Petro. Hii ilitokea wakati wa Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu. 4Baada ya kumkamata alimtia gerezani, chini ya ulinzi wa vikundi vinne vya askari, vyenye askari wanne kila kimoja. Herode alikuwa amekusudia kumtoa na kumfanyia mashtaka mbele ya watu baada ya Pasaka.

5Kwa hiyo Petro akawekwa gerezani, lakini kanisa lilikuwa likimwombea kwa Mungu kwa bidii.

6Usiku ule kabla ya siku ambayo Herode Agripa alikuwa amekusudia kumtoa na kumfanyia mashtaka Petro alikuwa amelala kati ya askari wawili, akiwa amefungwa kwa minyororo miwili. Nao walinzi wa zamu walikuwa wakilinda penye lango la gereza. 7Ghafula malaika wa Bwana akatokea na nuru ikamulika mle ndani ya gereza. Yule malaika akampiga Petro ubavuni na kumwamsha, akisema, “Ondoka upesi!” Mara ile minyororo ikaanguka kutoka mikononi mwa Petro.

8 Yule malaika akamwambia, “Vaa nguo zako na viatu vyako.” Petro akafanya hivyo. Kisha akamwambia, “Jifunge vazi lako na unifuate.” 9Petro alitoka mle gerezani akiwa amefuatana na yule malaika. Hakujua wakati huo kuwa yailyokuwa yakitukia yalikuwa kweli. Alidhani kuwa anaona maono. 10Wakapita lindo la kwanza na la pili, ndipo wakafika kwenye lango la chuma linaloelekea mjini. Lango likawafungukia lenyewe, nao wakapita hapo wakatoka nje. Baada ya kutembea umbali wa barabara moja, ghafula yule malaika akamwacha Petro.

11Ndipo Petro akarudiwa na fahamu, akasema, “Sasa ninajua bila shaka yo yote kuwa Bwana amemtuma malaika wake na kuniokoa kutoka katika makucha ya Herode Agripa na kutoka katika matazamio yote ya Wayahudi.’’

12Mara Petro alipotambua hili alikwenda nyumbani kwa Maria, mama yake Yohana aliyeitwa pia Marko, ambako watu wengi walikuwa wamekutana kwa maombi. 13Petro alipobisha hodi kwenye lango la nje, mtumishi wa kike jina lake Roda, akaja kumfungulia. 14Alipoitambua sauti ya Petro, alifurahi mno akarudi bila kufungua na kuwaeleza kwamba, “Petro yuko langoni!”

15Wakamwambia yule mtumishi wa kike, “Umerukwa na akili.” Alipozidi kusisitiza kuwa ni kweli, wakasema, “Lazima awe ni malaika wake.”

16Lakini Petro aliendelea kugonga langoni, nao walipofungua lango na kumwona Petro, walistaajabu sana. 17Yeye akawaashiria kwa mkono wake wanyamaze kimya, akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa gerezani. Naye akaongeza kusema, “Waelezeni Yakobo na ndugu wengine habari hizi.” Kisha akaondoka akaenda sehemu nyingine.

18Kulipokucha kukawa na fadhaa kubwa miongoni mwa wale maaskari kuhusu yaliyomtukia Petro. 19Baada ya Herode kuamuru atafutwe kila mahali na bila kumpata, aliwahoji wale askari walinzi kisha akatoa amri wauawe. Basi Herode Agripa akatoka Uyahudi akaenda Kaisaria, akakaa huko kwa muda.

### *Kifo Cha Herode Agripa*

20 Basi Herode Agripa alikuwa amekasirishwa sana na watu wa Tiro na Sidoni. Hivyo watu wa miji hiyo miwili wakaungana pamoja wakatafuta kukutana naye. Wakiisha kuungwa mkono na Blasto, mtumishi maalum wa Mfalme Herode Agripa aliyeaminika, wakaomba mapatano ya amani maana nchi zao zilitegemea nchi ya huyo mfalme kwa mahitaji yao ya chakula.

21 Katika siku iliyochaguliwa Herode Agripa akavaa mavazi yake ya kifalme, akaketi kwenye kiti chake cha enzi na kuwahutubia watu. 22 Watu waliokuwa wamekusanyika wakapiga kelele, wakisema, “Hii si sauti ya mwanadamu, bali ni ya Mungu.” 23 Ghafula, kwa kuwa Herode Agripa hakumpa Mungu utukufu, malaika akampiga, akaliwa na chango akafa.

24 Lakini neno la Mungu likaendelea mbele na kuenea, nao wengi wakaambatana nalo.

25 Barnaba na Sauli walipomaliza ile huduma yao iliyowapeleka, wakarudi Yerusalemu wakiwa pamoja na Yohana aitwaye Marko.

### *Safari Ya Kwanza Ya Paulo ya Kitume*

#### *Barnaba Na Sauli Wanatumwa*

**13** Katika kanisa huko Antiokia ya Shamu walikuwako manabii na walimu, yaani: Barnaba, Simeoni aitwaye Nigeri, Luko Mkirene, Manaeni aliyekuwa amelelewa pamoja na mfalme Herode Agripa na Sauli. 2 Walipokuwa wakimwabudu Bwana na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, “Nitengeeni Sauli na Barnaba kwa kazi ile maalumu niliyowaitia.” 3 Ndipo baada ya kufunga na kuomba, wakawawekea mikono yao.

### *Barnaba Na Sauli Waenda Kipro*

4 Hivyo, wakiwa wametumwa na Roho Mtakatifu, wakashuka kwenda Seleukia na kutoka huko wakasafiri baharini mpaka kisiwa cha Kipro. 5 Walipowasili katika mji wa Salami, wakahubiri neno la Mungu katika sinagogi la Wayahudi. Pia walikuwa na Yohana Marko kuwa msaidizi wao.

6 Walipokwisha kupita katika nchi zote hizo wakafika Pafo, ambapo walikutana na Myahudi mmoja mchawi aliyekuwa nabii wa uongo, jina lake Bar-Yesu. 7 Mtu huyu alikuwa pamoja na Sergio Paulo, mtu mwenye hekima aliyekuwa msaidizi wa mwakilishi wa mtawala wa kile kisiwa, Serigio Paulo akawaita Sauli na Barnaba akitaka kusikia neno la Mungu. 8 Lakini Elima yule mchawi (hii ndiyo maana ya jina lake,) aliwapinga Barnaba na Sauli na kujaribu kumpotosha yule mkuu wa kile kisiwa aiache imani. 9 Ndipo Sauli, ambaye pia aliitwa Paulo, akiwa amejawa na Roho Mtakatifu, akamkazia macho yule Elima mchawi, 10 akamwambia, “Ewe mwana wa ibilisi, wewe ni adui wa kila kilicho haki! Umejaa kila aina ya udanganyifu na ulaghai. Je, hutaacha kuzipotosha njia za Bwana zilizonyooka? 11 Nawe sasa sikiliza, mkono wa Bwana u dhidi yako. Utakuwa kipofu, wala hutaona jua kwa muda.

Mara ukungu na giza vikamfunika, naye akaenda huko na huko akitafuta mtu wa kumshika mkono ili amwonyeshe njia. 12 Yule mkuu wa kile kisiwa alipoona yaliyotukia, akaamini kwa sababu alistaajabishwa na mafundisho kuhusu Bwana.

### *Paulo Na Barnaba Huko Antiokia Ya Pisidia*

13 Kisha Paulo na wenzanke wakasafiri toka Pafo wakafika Perge huko Pamfilia. Lakini, Yohana Marko akawaacha huko akarejea Yerusalemu. 14 Kutoka Perge wakaendelea hadi Antiokia ya Pisidia. Siku ya Sabato wakaingia ndani ya sinagogi wakaketi. 15 Baada ya kusomwa Torati na vitabu vya manabii, viongozi wa lile sinagogi wakawatumia ujumbe wakisema, “Ndugu, kama mna neno la kuwasaidia watu hawa, tafadhali lisemeni.”

16 Paulo akasimama akawapungia mkono na kusema, “Enyi wanaume wa Israeli na ninyi nyote mnaomcha Mungu. 17 Mungu wa watu hawa wa Israeli aliwachagua baba zetu, akawafanya kustawi walipokuwa huko Misri, kwa uwezo mwingi akawaongoza na kuwatoa katika nchi ile. 18 Kwa muda wa miaka arobaini alivumilia matendo yao walipokuwa jangwani. 19 Naye baada ya kuyaangamiza mataifa saba waliokuwa wakiishi katika nchi ya Kanaani, akawapa Waisraeli nchi yao iwe urithi wao. 20 Haya yote yalichukua kama muda wa miaka 450.

“Baada ya haya, Mungu akawapa waamuzi mpaka wakati wa nabii Samweli. 21 Ndipo watu wakaomba wapewe mfalme, naye Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi wa kabila la Benyamini, aliyetawala kwa miaka arobaini. 22 Baada ya kumwondoa Sauli katika ufalme, akawainulia Daudi kuwa mfalme wao. Ambaye pia alimshuhudia, akisema, ‘Nimemwona Daudi mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo

wangu, atakayetimiza mapenzi yangu yote.’
23“Kutoka katika uzao wa mtu huyu, Mungu
amewaletea Israeli Mwokozi Yesu, kama
alivyoahidi. 24 Kabla ya kuja kwa Yesu, Yohana
alihubiri toba na ubatizo kwa watu wote wa
Israeli. 25Yohana alipokuwa anakamilisha kazi
yake, alisema: ‘Ninyi mnadhani mimi ni nani?
Mimi si yeye. La hasha, lakini yeye yuaja baada
yangu, ambaye mimi sistahili kufungua kamba
ya viatu vya miguu yake?’

26“Ndugu zangu, wana wa Abrahamu nanyi
mnaomcha Mungu, ujumbe wa huu wokovu ni
kwa ajili yetu. 27Kwa sababu wakaao
Yerusalumu na viongozi wao hawakumtambua
wala kuelewa maneno ya manabii yasomwayo
kila Sabato, bali waliyatimiza maneno hayo kwa
kumhukumu yeye. 28Ijapokuwa hawakupata
sababu yo yote ya kumhukumu kifo,
walimwomba Pilato aamuru auawe.
29Walipokwisha kufanya yale yote
yaliyoandikwa kumhusu, walimshusha kutoka
msalabani na kumzika kaburini. 30Lakini Mungu
alimfufua kutoka katika wafu. 31Naye kwa siku
nyingi akawatokea wale waliokuwa pamoja
kuanzia Galilaya hadi Yerusalemu. Nao sasa
wamekuwa mashahidi wake kwa watu wetu.

32“Nasi tunawaletea habari njema kwamba
yale Mungu aliyowaahidi baba zetu 33sasa
ameyatimiza kwetu, sisi watoto wao kwa
kumfufua Yesu, kama ilivyoandikwa katika
Zaburi ya pili,

“ ‘Wewe ni mwanangu,
leo nimekuzaa.’

34Kwa kuwa Mungu alimfufua kutoka kwa wafu
asioze kamwe, alitamka maneno haya:

“ ‘Nitakupa wewe baraka takatifu zilizo za
hakika
nilizomwahidi Daudi.’

35Kama ilivyosemwa mahali pengine katika
Zaburi,

“Hutamwacha Mtakatifu wako aone
uharibifu.’

36“Kwa maana Daudi akiisha kulitumikia
kusudi la Mungu katika kizazi chake, akalala,
akazikwa pamoja na baba zake na mwili wake
ukaoza. 37Lakini yule ambaye Mungu alimfufua
kutoka kwa wafu hakuona uharibifu.

38“Kwa hiyo ndugu zangu, nataka ninyi mjue
kwamba kwa kupitia huyu Yesu msamaha wa
dhambi unatangazwa kwenu. 39Kwa kumpitia
yeye, kila mtu amwaminiye anahesabiwa haki kwa
kila kitu ambacho asingeweza kuhesabiwa haki
kwa sheria ya Mose. 40Kwa hiyo jihadharini ili yale
waliyosema manabii yasiwapate:

41“ ‘Angalieni, enye wenye dhihaka!
Mkastaajabu, mkaangamie,
kwa maana nitatenda jambo wakati wenu
ambalo hamtasadiki
hata kama mtu akiwaambia.’ ”

42Paulo na Barnaba walipokuwa wakitoka
nje ya sinagogi, watu wakamwomba
wazungumze tena mambo hayo Sabato
nyingine inayofuata. 43Baada ya kusanyiko la
Sinagogi kutawanyika, wengi wa Wayahudi na
waongofu wa dini ya Kiyahudi wakawafuata
Paulo na Barnaba, nao wakazungumza na
kuwahimiza wadumu katika neema ya Mungu.

44Sabato iliyofuata karibu watu wote wa mji
ule walikuja kusikiliza neno la Mungu. 45Lakini
Wayahudi walipoona ule umati mkubwa wa
watu walijawa na wivu na kunena maneno ya
kashfa kuhusu yale Paulo aliyokuwa akisema.

46Ndipo Paulo na Barnaba wakawajibu kwa
ujasiri, wakisema, “Ilitupasa kunena nanyi neno
la Mungu kwanza. Lakini kwa kuwa mmelikataa,
mkajihukumu wenyewe kuwa hamstahili uzima
wa milele, sasa tunawageukia watu Mataifa.
47Kwa maana hili ndilo Bwana alilotuamuru:

“ ‘Nimewafanya ninyi kuwa nuru kwa
watu Mataifa,
ili mpate kuuleta wokovu hadi miisho ya
dunia.’ ”

48Watu Mataifa waliposikia haya wakafurahi
na kulitukuza neno la Bwana, nao wote
waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele
wakaamini.

49Neno la Bwana likaenea katika eneo lile
lote. 50Lakini Wayahudi wakawachochea
wanawake wenye kumcha Mungu, wenye vyeo
pamoja na watu maarufu katika mji,
wakachochea mateso dhidi ya Paulo na
Barnaba na kuwafukuza kutoka kwenye eneo
lao. 51Hivyo Paulo na Barnaba wakakung’uta
mavumbi kutoka kwenye miguu yao ili
kuwapinga, nao wakaenda Ikonio. 52Wanafunzi
wakajawa na furaha na Roho Mtakatifu.

### *Paulo Na Barnaba Huko Ikonio*

**14** Huko Ikonio Paulo na Barnaba waliingia pamoja
katika sinagogi la Wayahudi kama kawaida yao. Huko
wakahubiri kwa uwezo
mkubwa kiasi kwamba Wayahudi pamoja na
watu Mataifa wakaamini. 2Lakini wale Wayahudi
walikataa kuamini, wakawachochea watu
Mataifa, wakatia chuki ndani ya mioyo yao dhidi
ya wale walioamini. 3Hivyo Paulo na Barnaba
wakakaa huko kwa muda wa kutosha wakihubiri
kwa ujasiri juu ya Bwana, ambaye alithibitisha
ujumbe wa neema yake kwa kuwawezesha
kufanya ishara na miujiza. 4Lakini watu wa mji
ule waligawanyika, wengine wakakubaliana na
Wayahudi na wengine na mitume. 5Watu
Mataifa na Wayahudi wakajiunga na baadhi ya
viongozi, wakafanya mpango wa kuwatendea
mitume mabaya na kuwapiga mawe.6Lakini
mitume walipopata habari hizi wakakimbilia
Listra na Derbe, miji ya Likaonia na sehemu
zilizopakana nayo. 7Huko wakaendelea kuhubiri
habari njema.

### *Paulo Na Barnaba Huko Listra*

8Katika mji wa Listra, alikuweko kiwete,
ambaye alikuwa amelemaa tangu kuzaliwa na
hakuwa ametembea kamwe. 9Alimsikiliza Paulo
alipokuwa akihubiri. Paulo alipomtazama
akaona ana imani ya kuponywa. 10 Paulo
akapaza sauti, "Simama kwa miguu yako!" Mara
yule mtu akasimama upesi akaanza kutembea!

11Ule umati wa watu ulipoona yale
yaliyokuwa yamefanywa na Paulo, wakapiga
kelele kwa lugha yao ya Kilikaonia wakasema,
"Miungu imetushukia katika umbo la binadamu!"
12Wakamwita Barnaba Zeu na Paulo
wakamwita Herme kwa kuwa ndiye aliyekuwa
msemaji mkuu. 13Kuhani wa Zeu, ambaye
hekalu lake lilikuwa nje kidogo tu ya mji, akaleta
mafahali na mashada ya maua penye lango la
mji kwa sababu yeye pamoja na ule umati wa
watu walitaka kuwatolea dhabihu.

14Lakini Mitume Paulo na Barnaba
waliposikia na kuona mambo haya waliyotaka
kufanya, wakararua nguo zao, wakawaendea
wale watu kwa haraka, wakawapigia kelele,
wakisema, 15"Enyi watu, kwa nini mnafanya
mambo haya? Sisi ni wanadamu tu kama ninyi!
Tunawaletea habari njema, tukiwaambia
kwamba mgeuke mtoke katika mambo haya
yasiyofaa mmwelekee Mungu aliye hai,
aliyeziumba mbingu na nchi na bahari na kila
kitu kilicho ndani yake. 16Zamani aliwaachia
watu waishi walivyotaka. 17Lakini hakuacha
kuwaonyesha watu uwepo wake: Ameonyesha
wema kwa kuwanyeshea mvua toka mbinguni
na kuwapa mazao kwa majira yake, naye
amewapatia chakula tele na kuijaza mioyo yenu
na furaha". 18Hata kwa maneno haya yote,
ilikuwa vigumu kuuzuia ule umati wa watu
kuwatolea dhabihu.

19Ndipo wakaja baadhi ya Wayahudi kutoka
Antiokia na Ikonio wakawashawishi wale watu,
wakampiga Paulo kwa mawe, wakamburuta
hadi nje ya mji, wakidhani amekufa. 20Lakini
baada ya wanafunzi kukusanyika akainuka na
kurudi mjini. Kesho yake yeye na Barnaba
wakaondoka kwenda Derbe.

### *Paulo Na Barbara Warudi Antiokia Huko Syria*

21Baada ya kuhubiri habari njema katika mji
huo wa Derbe na kupata wanafunzi wengi,
walirudi Listra, kisha wakaenda Ikonio na
Antiokia, 22wakiwaimarisha wanafunzi na
kuwatia moyo waendelee kudumu katika imani.
Wakawaonya wakisema, "Imetupasa kuingia
katika Ufalme wa Mungu kwa kupitia katika
taabu nyingi." 23Nao baada ya kuwawekea
wazee katika kila kanisa, kwa kufunga na
kuomba ambaye wamemwamini wakawakabidhi
kwa Bwana waliyemwamini kwa maombi na
kufunga. 24Kisha wakapitia Pisidia wakafika
Pamfilia. 25Baada ya kuhubiri neno la Mungu
huko Perga, wakateremkia Atalia.

26Kutoka Atalia huko wakasafiri baharini
kwa merikebu wakarudi mpaka Antiokia,
ambako walikuwa wamesifiwa kwa ajili ya
neema ya Mungu kutokana na ile kazi
waliokuwa wamekamilisha. 27Walipowasili
Antiokia wakaliita kanisa pamoja na kutoa
taarifa ya yale yote Mungu aliyokuwa ametenda
kwa kupitia kwao na jinsi alivyokuwa amefungua
mlango wa imani kwa ajili ya watu Mataifa.
28Nao wakakaa huko pamoja na wanafunzi kwa
muda mrefu.

### *Baraza Huko Yerusalemu*

**15** Baadhi ya watu wakashuka Antiokia
kutoka Uyahudi, nao wakawa
wanawafundisha ndugu waliomini kwamba,
"Isipokuwa mmetahiriwa kufuatana na desturi
aliyofundisha Mose, hamwezi kuokoka." 2Baada ya
Paulo na Barnaba kutokukubaliana kukawa
na mabishano makali na watu hawa, Paulo na

Barnaba na baadhi ya wengine miongoni mwao wakachaguliwa kuingia Yerusalemu ili kujadiliana jambo hili na mitume na wazee.
3Hivyo wakasafirishwa na kanisa, wakiwa njiani wakapitia Samaria wakawaeleza jinsi watu Mataifa walivyoongoka. Habari hizi zikaleta furaha kubwa kwa ndugu wote.
4Walipofika Yerusalemu, walipokelewa na kanisa na mitume pamoja na wazee ambao waliwaarifu kila kitu Mungu alichokuwa amefanya pamoja nao.

5Ndipo baadhi ya walioamini wa madhehebu ya Mafarisayo wakasimama na kusema, “Hao watu Mataifa lazima watahiriwe na waagizwe kuzitii sheria za Mose”.

6Mitume na wazee wakukutana pamoja ili kufikiri jambo hili.
7Baada ya majadiliano mengi, Petro akasimama na kusema, “Ndugu zangu, mnajua kwamba siku za kwanza Mungu alinichagua ili kwa midomo yangu watu Mataifa wapate kusikia ujumbe wa injili na kuamini.
8Mungu, yeye ajuae mioyo, alionyesha kwamba anawakubali kwa kuwapa Roho Mtakatifu kama vile alivyotupa sisi.
9Mungu hakutofautisha kati yetu na wao, bali alitakasa mioyo yao kwa imani.
10Sasa basi, mbona mnataka kumjaribu Mungu kwa kuweka kongwa shingoni mwa wanafunzi ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulibeba?
11Lakini sisi tunaamini ya kuwa tunaokolewa kwa neema ya Bwana Yesu Kristo, kama wao wanavyookolewa.”

12Kusanyiko lote likakaa kimya, wakawasikiliza Paulo na Barnaba wakieleza jinsi Mungu alivyowatumia kutenda ishara na maajabu kwa watu Mataifa.
13Walipomaliza kunena, Yakobo akasema, “Ndugu zangu, nisikilizeni.
14 Simoni amekwisha kutueleza jinsi Mungu, kwa mara ya kwanza alivyoonyesha kuhusika kwa kujichagulia watu kutoka katika watu Mataifa kwa ajili ya jina lake.
15Maneno ya manabii yanakubaliana na jambo hili, kama ilivyoandikwa:

16“ ‘Baada ya mambo haya nitarudi,
nami nitajenga upya nyumba ya
Daudi, iliyoanguka.
Nitajenga tena magofu yake
na kuisimamisha,
17ili wanadamu wengine wote wapate
kumtafuta Bwana,
hata wale watu Mataifa wote ambao
wanaitwa kwa jina langu,
asema Bwana, afanyaye mambo haya’
18tangu zamani.

19“Kwa hiyo uamuzi wangu ni kwamba, tusiwasumbue watu Mataifa wanaomgeukia Mungu kwa desturi zetu,
20badala yake, tuwaandikie kwamba wajiepushe tu na vitu vilivyotiwa unajisi na uasherati na wasile nyama za wanyama walionyongwa au kunywa damu.
21Kwa maana katika kila mji kwa vizazi vilivyopita, Mose amekuwa na wale wanaotangaza sheria yake kwa kuwa imekuwa ikisomwa kwa sauti kubwa katika masinagogi kila Sabato.”

### *Barua Kwa watu Mataifa Waaminio*

22Mitume na wazee pamoja na kanisa lote, wakaamua kuwachagua baadhi ya watu wao wenyewe na kuwatuma Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba. Wakamchagua Yuda aitwaye Barnaba na Sila, watu wawili ambao walikuwa viongozi miongoni mwa ndugu.
23Wakatumwa na barua ifuatayo:

Sisi Mitume na wazee, ndugu zenu,

Kwa wale ndugu Mataifa walioamini walioko Antiokia, Shamu na Kilikia :

Salamu.

24Tumesikia kwamba kuna baadhi ya watu waliokuja huko kutoka kwetu bila ruhusa yetu na kuwasumbua, wakiwataabisha mawazo yenu.
25Hivyo tumekubaliana wote kuwachagua baadhi ya watu na kuwatuma kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo,
26watu ambao wamehatarisha maisha yao kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo.
27Kwa hiyo tunawatuma Yuda na Sila, kuthibitisha maneno ya mdomo mambo haya tunayowaandikia.
28Kwa maana imempendeza Roho Mtakatifu na sisi tusiwatwike mzigo wo wote mkubwa zaidi ya mambo haya yafuatayo ambayo ni ya lazima:
29Kwamba mjiepushe na kitu cho chote kilichotolewa sadaka kwa sanamu, kunywa damu, nyama ya wanyama walionyongwa na mjiepushe na uasherati. Mkiyaepuka mambo haya mtakuwa mmefanya vyema.

Kwaherini.”

[30]Hivyo wakaagwa, wakashuka kwenda Antiokia. Baada ya kulikusanya kanisa pamoja, wakawapa ile barua. [31]Nao hao watu wakiisha kuisoma, wakafurahishwa sana kwa ujumbe wake wa kutia moyo. [32]Yuda na Sila, ambao wenyewe walikuwa manabii wakanena maneno mengi ya kuwatia moyo na kuwajenga katika imani wale ndugu walioamini. [33]Baada ya kukaa huko Antiokia kwa muda, wakaagwa kwa amani na wale ndugu ili waende kwa wale waliowatuma. ([34]Lakini Sila bado akaendelea kukaa huko.) [35]Lakini Paulo na Barnaba walibaki Antiokia ambako wao pamoja na wengine wengi waliwafundisha na kuhubiri neno la Bwana.

## *Safari Ya Pili ya Paulo ya Kitume (15:41 – 18:22)*

### *Paulo Na Barnaba Wagawanyika*

[36]Baada ya siku kadhaa, Paulo alimwambia Barnaba, "Turudi tukawatembelee ndugu katika miji yote ambamo tulihubiri neno la Bwana tuone jinsi wanavyoendelea." [37]Barnaba alitaka wamchukue Yohana aitwae Marko waende naye. [38]Lakini Paulo aliona si vyema kwa sababu aliwahi kuwaacha walipokuwa huko Pamfilia, hakutaka kuendelea kufanya kazi nao. [39]Pakatokea kutokukubaliana kati ya Paulo na Barnaba kuhusu jambo hili, hivyo wakagawanyika. Barnaba akamchukua Yohana Marko wakasafiri baharini kwenda Kipro. [40]Lakini Paulo akamchagua Sila na akaondoka baada ya ndugu kuwatakia neema ya Bwana. [41]Akapitia Shamu na Kilikia, akiimarisha makanisa ya huko.

## *Timotheo Aungana Na Paulo Na Sila*

**16** Paulo akafika Derbe na kisha Listra, ambako kulikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo, ambaye mama yake alikuwa Myahudi, aliyeamini, lakini baba yake alikuwa Myunani. [2]Alikuwa amesafiri sana na wale waliokuwa wameamini huko Listra na Ikonio. [3]Paulo alitaka Timotheo afuatane naye, akamchukua na akaamuru atahiriwe kwa sababu ya Wayahudi waliokuwa wanaishi eneo lile kwa maana wote walimjua baba yake ni Myunani. [4]Walipokuwa wakienda mji kwa mji, wakawa wanawapa yale maamuzi yaliyokuwa yametolewa. [5] Hivyo makanisa yakawa imara katika imani na kuongezeka kiidadi kila siku.

[6]Paulo pamoja na wenzake wakasafiri sehemu za Firigia na Galatia, wakiwa wamekatazwa na Roho Mtakatifu wasihubiri neno huko Asia. [7]Walipofika kwenye mpaka wa Misia, wakajaribu kuingia Bithinia lakini Roho wa Yesu hakuwaruhusu. [8]Kwa hiyo wakapita Misia, wakafika Troa. [9]Wakati wa usiku Paulo akaona maono, mtu wa Makedonia amesimama akimsihi, "Vuka uje huku Makedonia ukatusaidie." [10]Baada ya Paulo kuona maono haya, mara tulijiandaa kuondoka kwenda Makedonia tukiwa tumesadiki kwa sababu tuliona kwa hakika kwamba Mungu ametuita kuhubiri habari njema huko.

## *Kuongoka Kwa Lidia*

[11]Tukasafiri kwa njia ya bahari kutoka Troa na kwenda moja kwa moja kwa Samothrake, kesho yake tukafika Neapoli. [12]Kutoka huko tukasafiri hadi Filipi, mji mkuu wa Makedonia sehemu walipokuwa wanakaa Warumi, nasi tukakaa kwenye mji huo kwa siku kadhaa.

[13]Siku ya Sabato tukaenda nje ya lango la mji kando ya mto, mahali ambapo tulitarajia tungepata mahali pa kufanyia maombi. Tukaketi, tukaanza kuongea na baadhi ya wanawake waliokuwa wamekusanyika huko. [14]Mmoja wa wale wanawake waliotusikiliza aliitwa Lidia, mfanya biashara wa nguo za zambarau, mwenyeji wa mji wa Thiatira, aliyekuwa mcha Mungu. Bwana akaufungua moyo wake akaupokea ujumbe wa Paulo. [15]Basi alipokwisha kubatizwa yeye na watu wa nyumbani mwake, alitukaribisha nyumbani mwake akisema, "Kama mmeona kweli mimi nimemwamini Bwana, karibuni mkae nyumbani mwangu.'' Naye akatushawishi.

## *Paulo Na Sila Watiwa Gerezani*

[16]Siku moja, tulipokuwa tukienda mahali pa kusalia, tulikutana na mtumwa mmoja wa kike ambaye alikuwa na pepo wa uaguzi naye alikuwa amewapatia mabwana zake mapato makubwa ya fedha kwa ubashiri. [17]Huyu mtumwa wa kike alikuwa akimfuata Paulo na sisi akipiga kelele, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu Aliye Juu Sana, wao wanawatangazieni njia ya wokovu." [18]Akaendelea kufanya hivi kwa siku nyingi, lakini Paulo akiwa ameudhika sana, akageuka na kumwambia yule pepo, "Ninakuamuru katika jina la Yesu Kristo, umtoke!" Yule pepo akamtoka saa ile ile.

[19]Basi mabwana wa yule mtumwa wa kike walipoona kuwa tumaini lao la kuendelea kujipatia fedha limetoweka, wakawakamata Paulo na Sila wakawaburuta mpaka sokoni

mbele ya viongozi wa mji. 20Baada ya
kuwafikisha mbele ya mahakimu wakawashtaki
wakisema, “Hawa watu wanaleta ghasia katika
mji wetu, nao ni Wayahudi. 21Wanafundisha
desturi ambazo sisi raia wa Kirumi hatuwezi
kuzikubali au kuzitimiza.”

22Umati wa watu waliokuwepo wakajiunga
katika kuwashambulia na wale mahakimu
wakawaamuru wavuliwe nguo zao wakatoa amri
Paulo na Sila wachapwe viboko. 23Baada ya
kuchapwa sana wakatupwa gerezani na
kumwagiza mkuu wa gereza awalinde kikamilifu,
24kwa kufuata maelekezo haya, yule mkuu wa
gereza akawaweka katika chumba cha ndani
sana mle gerezani na akawafunga miguu yao
kwa minyororo.

25Ilipokaribia usiku wa manane, Paulo na
Sila walikuwa wakiomba na kuimba nyimbo za
kumsifu Mungu, nao wafungwa wengine
walikuwa wakiwasikiliza. 26Ghafla pakatokea
tetemeko kubwa la ardhi, hata msingi wa gereza
ukatikisika. Mara milango ya gereza ikafunguka
na ile minyororo iliyowafunga kila mmoja
ikafunguka. 27Yule mkuu wa gereza alipoamka
na kuona milango ya gereza iko wazi,
akachomoa upanga wake akataka kujiua,
akidhani ya kuwa wafungwa wote wametoroka.
28Lakini Paulo akapiga kelele kwa sauti kubwa,
akasema, “Usijidhuru kwa maana sisi sote tuko
hapa!”

29Yule askari wa gereza akaagiza taa
ziletwe, akaingia ndani ya kile chumba cha
gereza, akapiga magoti akitetemeka mbele ya
Paulo na Sila. 30Kisha akawaleta nje akisema,
“Bwana zangu, nifanye nini ili nipata kuokoka?”

31 Wakamjibu, “Mwamini Bwana Yesu
Kristo, nawe utaokoka, pamoja na wa nyumbani
mwako.” 32 Wakamwaambia neno la Bwana
yeye pamoja na wote waliokuwako nyumbani
mwake. 33Wakati ule ule yule mkuu wa gereza
akawachukua akawaosha majeraha yao, kisha
akabatizwa yeye pamoja na wote waliokuwa
nyumbani mwake bila kuchelewa.
34Akawapandisha nyumbani mwake
akawaandalia meza mbele yao, yeye pamoja na
wa nyumbani mwake wote wakafurahi sana kwa
kuwa amemwamini Mungu.

35Kulipopambazuka wale mahakimu
wakawatuma maafisa wao kwa mkuu wa gereza
wakiwa na agizo linalosema, “wafungue wale
watu, waache waende zao.” 36“Mahakimu
wametuma niwaache huru, kwa hiyo tokeni.”

37Lakini Paulo akawaambia wale maafisa,
“Wametupiga hadharani bila kutufanyia
mashtaka na kutuhoji, nao wakatutupa
gerezani, hata ingawa sisi ni raia wa Rumi. Nao
sasa wanataka kututoa gerezani kwa siri? Kweli
hapana! Wao na waje wenyewe watutoe humu
gerezani.”

38Wale maafisa wakarudi na kuwaambia
wale mahakimu maneno haya, wakaogopa sana
walipofahamu kuwa Paulo na Sila ni raia wa
Rumi. 39Kwa hiyo wakaja wakawaomba
msamaha, wakawatoa gerezani, wakawaomba
waondoke katika ule mji. 40Baada ya Paulo na
Sila kutoka gerezani walikwenda nyumbani kwa
Lidia, ambapo walikutana na wale ndugu
walioamini, wakawatia moyo, ndipo
wakaondoka.

### *Ghasia Huko Thesalonike*

**17** Wakasafiri kupitia Amfipoli na Apolonia wakafika
Thesalonike, ambako kulikuwa na sinagogi la
Wayahudi. 2Kama desturi yake
Paulo aliingia ndani ya sinagogi na kwa muda
wa majuma matatu akawa anahojiana nao
kutoka kwenye Maandiko 3akidhihirisha wazi na
kuthibitisha kwamba ilikuwa lazima Kristo
ateswe na afufuke kutoka kwa wafu, akasema,
“Huyu Yesu ninayewaambia habari zake, ndiye
Kristo.” 4Baadhi ya Wayahudi wakasadiki,
wakaungana na Paulo na Sila, wakiwepo idadi
kubwa ya Wayunani waliomcha Mungu na
wengi wa wanawake mashuhuri.

5Lakini Wayahudi ambao hawakuwa
wameamini wakawa na wivu, wakawakodi watu
ovyo, wafisadi kutoka sokoni, wakakutanisha
umati wa watu, wakaanzisha ghasia mjini.
Wakaenda mbio nyumbani kwa Yasoni
wakiwatafuta Pualo na Sila ili kuwaleta nje
penye ule umati wa watu. 6Lakini walipowakosa
wakamburuta Yasoni na ndugu wengine mbele
ya maafisa wa mji, wakipiga kelele: “Watu hawa
ni wale walioupindua ulimwengu wamekuja
huku nako, 7naye Yasoni amewakaribisha
nyumbani mwake. Hawa wote wanaasi amri za
Kaisari wakisema yuko mfalme mwingine
aitwaye Yesu. 8Waliposikia haya, ule umati wa
watu na maafisa wa mji wakaongeza ghasia.
9Nao baada ya kuchukua dhamana kwa ajili ya
Yasoni na wenzake wakawaacha waende zao.

### *Paulo Na Sila Huko Beroya*

10Usiku ule ule, wale ndugu walioamini
wakawapeleka Paulo na Sila waende zao
Beroya. Walipowasili huko wakaenda kwenye

sinagogi la Wayahudi. 11Hawa Wayahudi wa Beroya walikuwa waungwana zaidi kuliko wale wa Thesalonike, 12Wayahudi wengi wakaamini pamoja na wanawake na wanaume wa Kigiriki wa tabaka la juu.

13Lakini wale Wayahudi wa Thesalonike waliposikia kuwa Paulo anahubiri neno la Mungu huko Beroya, wakaenda huko nako wakishawishi watu na kuwachochea. 14Ndipo wale ndugu wa Beroya mara moja wakamsafirisha Paulo aende zake pwani, lakini Sila na Timotheo wakabaki Beroya. 15Wale waliomsindikiza Paulo wakaenda naye mpaka Athene, kisha wakarudi Beroya wakiwa na maagizo kutoka kwa Paulo kuhusu Sila na Timotheo kwamba wamfuate upesi iwezekanavyo.

### *Paulo Huko Athene*

16Wakati Paulo akiwasubiri huko Athene, alisumbuka sana moyoni mwake kuona kwamba mji umejaa sanamu. 17Hivyo akahojiana kila siku na Wayahudi pamoja na wacha Mungu kwenye sinagogi na pia sokoni kwa wale waliokutana naye huko. 18Kisha baadhi ya Waepikureo na Wastoiko wenye elimu ya juu sana wakakutana naye. Baadhi yao wakasema, "Je, huyu mpayukaji anajaribu kusema nini?" Wengine wakasema, "Inaonekana anasema habari za miungu ya kigeni." Walisema haya kwa sababu Paulo alikuwa anahubiri habari njema kuhusu Yesu na ufufuo wa wafu. 19Hivyo wakamchukua na kumleta kwenye mkutano wa Areopago, walikomwambia, "Je, tunaweza kujua mafundisho haya mapya unayofundisha ni nini? 20Wewe unaleta mambo mapya masikioni mwetu, hivyo tungetaka kujua maana yake ni nini?" 21(Waathene na wageni wote walioishi humo hawakutumia muda wao kufanya cho chote kingine isipokuwa kueleza au kusikia jambo jipya).

22Ndipo Paulo akasimama katikati ya Areopago akasema, "Enyi watu wa Athene! Ninaona kwamba katika kila jambo ninyi ni watu wa dini sana. 23Kwa kuwa nilipokuwa nikitembea mjini na kuangalia kwa bidii vitu vyenu vya kuabudiwa, niliona huko madhabahu moja iliyoandikwa: **KWA MUNGU ASIYEJULIKANA.** Basi sasa kile ambacho mmekuwa mkikiabudu kama kisichojulikana, ndicho ninachowahubiria.

24"Mungu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo ndani yake, Yeye ndiye Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu. 25Wala hatumikiwi na mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji cho chote, kwa sababu Yeye mwenyewe ndiye awapaye watu wote uhai na pumzi na vitu vyote. 26 Kutoka kwa mtu mmoja, yeye aliumba mataifa yote ya wanadamu ili waikalie dunia yote, naye akaweka nyakati za kuishi. 27Mungu alifanya hivyo ili wanadamu wamtafute na huenda wakamfikia ingawa kwa kupapasa – papasa ijapokuwa kwa kweli hakai mbali na kila mmoja wetu. 28'Kwa kuwa katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu'. Kama baadhi ya mashairi yenu yalivyosema, 'Sisi ni watoto wake'

29"Kwa kuwa sisi ni watoto wa Mungu, haitupasi kudhani kuwa Uungu ni kama sanamu ya dhahabu au ya fedha au ya jiwe iliyotengenezwa kwa ubunifu na ustadi wa mwanadamu. 30Zamani wakati wa ujinga, Mungu alijifanya kama haoni, lakini sasa anawaamuru watu wote kila mahali watubu. 31Kwa kuwa ameweka siku ambayo atauhukumu ulimwengu kwa haki akimtumia mtu aliyemchagua, kwake huyo amewahakikishia watu wote kwa kumfufua Yeye kutoka kwa wafu.''

32Waliposikia habari za ufufufo wa wafu, baadhi yao wakadhihaki, lakini wengine wakasema, "Tunataka kukusikia tena ukizungumza juu ya jambo hili." 33Kwa hiyo Paulo akaondoka katikati yao. 34Lakini baadhi yao wakaungana naye wakaamini. Kati yao alikuwepo Dionisio, Mwareopago na mwanamke mmoja aliyeitwa Damari na wengine wengi.

### *Paulo Huko Korintho*

**18** Baada ya haya, Paulo akaondoka Athene akaenda Korintho. 2Huko akakutana na Myahudi mmoja jina lake Akila, mwenyeji wa Ponto, ambaye alikuwa amewasili karibuni kutoka Italia pamoja na mkewe Prisila, kwa sababu Mfalme Klaudio alikuwa ameamuru Wayahudi wote waondoke Rumi. Paulo akaenda kuwaona. 3Naye kwa kuwa alikuwa mtengeneza mahema kama wao, akakaa na kufanya kazi pamoja nao. 4Kila Sabato Paulo alikuwa akihojiana nao akijitahidi kuwavuta Wayahudi na Wayunani.

5Sila na Timotheo walipowasili kutoka Mekodonia, walimkuta Paulo akiwa amejitolea muda wake wote katika kuhubiri, akiwashuhudia Wayahudi kwamba Yesu ndiye Kristo. 6Wayahudi walipompinga Paulo na kukufuru,

yeye aliyakung'uta mavazi yake, akawaambia,
"Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu! Mimi
sina hatia, nimetimiza wajibu wangu. Kuanzia
sasa nitawaendea watu Mataifa"

7Kisha akaondoka mle kwenye sinagogi,
akaenda nyumbani kwa mtu mmoja jina lake
Tito Yusto, aliyekuwa mcha Mungu. Nyumba
yake ilikuwa jirani na Sinagogi. 8Kiongozi wa
hilo sinagogi, aliyeitwa Krispo, akamwamini
Bwana pamoja na wote wa nyumbani mwake,
nao Wakorintho wengi waliomsikia Paulo
wakaamini na kubatizwa.

9Usiku mmoja Bwana akamwambia Paulo
katika maono, "Usiogope, lakini endelea kusema
wala usinyamaze, 10kwa maana mimi niko
pamoja nawe, wala hakuna mtu ye yote
atakayeweza kukushambulia ili kukudhuru, kwa
kuwa kuna wengi katika mji huu ambao ni watu
wangu.'' 11Hivyo Paulo akakaa huko kwa muda
wa mwaka mmoja na nusu, akifundisha neno la
Mungu miongoni mwao.

12Lakini wakati Galio alipokuwa msaidizi wa
mwakilishi wa mtawala huko Akaya, Wayahudi
waliungana kumshambulia Paulo,
wakamkamata na kumpeleka mahakamani.
13Wakamshitaki wakisema, "Mtu huyu
anawashawishi watu wamwabudu Mungu
kinyume cha sheria."

14Mara Paulo alipotaka kujitetea, Galio
akawaambia Wayahudi, "Kama ninyi Wayahudi
mlikuwa mkilalamika kuhusu makosa makubwa
ya uhalifu ingekuwa haki kwangu kuwasikiliza.
15Lakini kwa kuwa linahusu maneno, majina na
sheria yenu, amueni ninyi wenyewe. Mimi
sitakuwa mwamuzi wa mambo haya.''
16Akawafukuza kutoka mahakamani. 17Ndipo
wote wakamkamata Sosthene, kiongozi wa
sinagogi, wakampiga mbele ya mahakama,
lakini Galio hakujali hata mojawapo ya mambo
haya.

### *Paulo Arudi Antiokia*

18 Baada ya kukaa huko Korintho kwa
muda, Paulo akaagana na wale ndugu
walioamini akasafiri kwa njia ya bahari kwenda
Shamu akiwa amefuatana na Prisila na Akila.
Walipofika Kenkrea Paulo alinyoa nywele zake
kwa kuwa alikuwa ameweka nadhiri.
19Walipofika Efeso Paulo aliwaacha Prisila na
Akila huko, lakini kwanza yeye mwenyewe
akaingia kwenye sinagogi akawa anajadiliana
na Wayahudi. 20Walipomwomba akae nao kwa
muda mrefu zaidi hakukubali, 21lakini alipokuwa
akiondoka, akaahidi, "Nitarudi kama Mungu
akipenda." Kisha akasafiri kwa njia ya bahari
kutoka Efeso. 22Alitia nanga Kaisaria kwenda
Yerusalemu na kulisalimu kanisa, kisha
akaenda Antiokia.

23Baada ya kukaa huko kwa muda,
akaondoka na kwenda kutoka sehemu moja
hadi nyingine huko Galatia na Frigia,
akiwaimarisha wanafunzi wote.

### *Huduma Ya Apolo Huko Efeso Na Korintho*

24Basi akaja Efeso Myahudi mmoja, jina
lake Apolo, mwenyeji wa Aleksandria. Yeye
alikuwa mtu mwenye uwezo mkubwa wa
kunena, pia alikuwa hodari katika maandiko.
25Alikuwa amefundishwa katika njia ya Bwana,
naye alikuwa na bidii katika roho, naye
alifundisha kwa usahihi juu ya Yesu, ingawa
alijua tu ubatizo wa Yohana. 26Apolo alianza
kunena kwa ujasiri mkubwa katika sinagogi,
Lakini Prisila na Akila walipomsikia
walimchukua kando na kumweleza njia ya
Mungu kwa ufasaha zaidi.

27Naye Apolo alipotaka kwenda Akaya,
ndugu wa Efeso walimtia moyo wakampa barua
ya kumtambulisha kwa ndugu wa huko.
Alipofika huko aliwasaidia sana wale watu
ambao kwa neema ya Mungu walikuwa
wameamini, 28kwa maana kwa uwezo mkubwa
aliwakanusha hadharani Wayahudi, waliokuwa
wakipinga akionyesha kwa njia ya maandiko
kwamba Yesu ndiye Kristo.

### *Paulo Huko Efeso*

**19** Wakati Apolo akiwa huko Korintho, Paulo
alisafiri sehemu za bara, akafika Efeso. Huko
akawakuta wanafunzi kadhaa,
2akawauliza, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu
mlipoamini?"

Wakajibu, "Hapana, hata hatukusikia kuwa
kuna Roho Mtakatifu." 3Ndipo Paulo
akawauliza, "Je, mlibatizwa kwa ubatizo gani?"
Wakajibu, "Kwa ubatizo wa Yohana."

4Paulo akasema, "Ubatizo wa Yohana
ulikuwa wa toba, aliwaambia watu wamwamini
yeye atakayekuja baada yake, yaani, Yesu."
5Waliposikia haya, wakabatizwa katika jina la
Yesu. 6Paulo alipoweka mikono yake juu yao,
Roho Mtakatifu akawashukia, nao wakanena
kwa lugha mpya na kutabiri. 7Idadi yao ilikuwa
wapata wanaume kumi na wawili.

8Paulo akaingia katika sinagogi na kunena
humo kwa ujasiri kwa muda wa miezi mitatu,

akawa na majadiliano ya kuwafanya watu waamini mambo yanayohusu Ufalme wa Mungu. 9Lakini baadhi yao kwa ukaidi walipokataa kuamini na kukashifu ujumbe wake mbele ya umati wa watu, Paulo aliachana nao, akawachukua wanafunzi na kuhojiana nao kila siku katika darasa la mtu mmoja aitwaye Tirano. 10Jambo hili likaendelea kwa muda wa miaka miwili, kiasi kwamba Wayahudi na Wayunani wote walioishi huko Asia wakawa wamesikia neno la Bwana.

### *Wana Wa Skewa Wajaribu Kutoa Pepo Mchafu*

11Mungu akafanya miujiza mingi isiyo ya kawaida kwa mkono wa Paulo, 12kwamba leso au vitambaa vilivyokuwa vimegusa mwili wa Paulo viliwekwa juu ya wagonjwa, nao wakapona magonjwa yao na pepo wachafu wakawatoka.

13Basi baadhi ya Wayahudi wenye kutangatanga huku na huko wakitoa pepo wachafu wakajaribu kutumia jina la Yesu juu ya wale wenye pepo, walikuwa wakisema, “Kwa jina la Yesu, yule anayehubiriwa na Paulo, nakuamuru utoke.” 14 Palikuwa na wana saba wa mtu mmoja Myahudi jina lake Skewa, aliyekuwa kiongozi wa makuhani, ambao walikuwa wanafanya hivyo. 15Lakini pepo mchafu akawajibu, “Yesu namjua na Paulo pia namjua, lakini ninyi ni nani?” 16Kisha yule mtu aliyekuwa na pepo mchafu akawarukia, akawashambulia vikali, akawashinda nguvu wote, wakatoka ndani ya ile nyumba wakikimbia wakiwa uchi na wenye majeraha.

17Habari hii ikajulikana na Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu ikawajaa wote, nalo jina la Bwana Yesu likaheshimiwa sana. 18Wengi wa wale waliokuwa wameamini wakati huu wakaja na kutubu kuhusu matendo yao maovu waziwazi. 19Idadi kubwa ya wale waliofanya mambo ya uganga wakaleta vitabu vyao na kuviteketeza kwa moto hadharani. Walipofanya hesabu ya thamani ya vitabu vilivyoteketezwa ilikuwa drakamu 50,000[a] za fedha. 20 Hivyo neno la Bwana likaenea sana na kuwa na nguvu.

### *Ghasia Huko Efeso*

21Baada ya mambo haya kutukia, Paulo akakusudia rohoni kwenda Yerusalemu kwa kupitia Makedonia na Akaya. Akasema, “Baada ya kufika huko, yanipasa pia kwenda Rumi.” 22Hivyo akatuma wasaidizi wake wawili, Timotheo na Erasto, waende Makedonia, wakati yeye mwenyewe alibaki kwa muda kidogo huko Asia.

23Wakati huo huo pakatokea dhiki kubwa kwa sababu ya Njia ile ya Bwana. 24Mtu mmoja jina lake Demetrio mfua fedha aliyekuwa akitengeneza vihekalu vya fedha vya Artemi na kuwapatia mafundi wake biashara kubwa, 25aliwaita pamoja watu wengine waliofanya kazi ya ufundi kama yake na kusema, “Enyi watu, mnajua ya kuwa utajiri wetu unatokana na biashara hii? 26Pia ninyi mmeona na kusikia jinsi ambavyo si huku Efeso peke yake lakini ni karibu Asia yote huyu Paulo amewashawishi na kuvuta idadi kubwa ya watu kwa kusema kuwa miungu iliyotengenezwa na watu si miungu. 27Kwa hiyo kuna hatari si kwa kazi yetu kudharauliwa tu, bali pia hata hekalu la mungu mke Artemi, aliye mkuu, anayeabudiwa Asia yote na ulimwengu wote, litakuwa limepokonywa fahari yake ya kiungu.”

28Waliposikia maneno haya, wakaghadhabika wakaanza kupiga kelele, “Artemi wa Waefeso ni mkuu!” 29 Mara mji wote ukajaa ghasia, watu wakakimbilia katika ukumbi wa michezo kama mtu mmoja, wakawakamata Gayo na Aristarko, watu wa Makedonia waliokuwa wakisafiri pamoja na Paulo. 30 Paulo akataka kuingia katikati ya umati wa watu lakini wanafunzi hawakumruhusu. 31Hata baadhi ya viongozi wa sehemu ile, waliokuwa rafiki zake Paulo, wakatuma watu wakitamani asiingie katika ule ukumbi.

32Baadhi ya watu walikuwa wakilia hivi na wengine vile. Idadi kubwa ya watu hawakujua hata ni kwa nini walikuwa wamekusanyika huko. 33Wayahudi wakamsimamisha Aleksanda mbele na baadhi ya watu kwenye ule umati wakampa maelekezo. 34Lakini walitambua kwamba alikuwa Myahudi, wote wakapiga kelele kwa sauti moja kwa karibu muda wa saa mbili, wakisema, “Artemi wa Efeso ni mkuu!”

35Baadaye karani wa mji akaunyamazisha ule umati wa watu na kusema, “Enyi watu wa Efeso, je, ulimwengu wote haujui ya kuwa mji wa Efeso ndio unaotunza hekalu la Artemi aliye mkuu na ile sanamu yake iliyoanguka kutoka mbinguni? 36Kwa hiyo, kwa kuwa mambo haya hayakanushiki, inawapasa mnyamaze na wala msifanye lo lote kwa haraka. 37Kwa kuwa

[a]19 Drakamu ilikuwa ni sarafu ya fedha, thamani yake sawa na mshahara wa siku moja.

mmewaleta hawa watu hapa, ingawa hawajaiba
hekaluni wala kumkufuru huyu mungu wetu wa
kike. 38Basi, ikiwa Demetrio na mafundi
wenzake wana jambo zito dhidi ya mtu ye yote,
mahakama ziko wazi na wasaidizi wa mwakilishi
wa mtawala wapo. Wanaweza kufungua
mashtaka. 39Lakini kama kuna jambo jingine lo
lote zaidi mnalotaka kulileta, itabidi lisuluhishwe
katika kusanyiko halali. 40 Kama ilivyo sasa,
tuko hatarini kushtakiwa kwa kufanya ghasia
kwa sababu ya tukio la leo. Kwa kuwa hakuna
sababu tutakayoweza kutoa kuhalalisha
msukosuko huu." 41Baada ya kusema haya
akavunja mkutano.

### *Paulo Apita Makedonia Na Uyunani*

**20** Baada ya kumalizika kwa zile ghasia,
Paulo aliwaita wanafunzi pamoja akawatia
moyo, akawaaga, akaanza safari kwenda
Makedonia. 2Alipita katika sehemu zote,
akinena na watu maneno mengi ya kuwatia
moyo, ndipo hatimaye akawasili Uyunani,
3ambako alikaa kwa muda wa miezi mitatu.
Alipokuwa anakaribia kuanza safari kwa njia ya
bahari kwenda Shamu, kwa sababu Wayahudi
walikuwa wamefanya shauri baya dhidi yake,
hivyo aliamua kurudi kwa kupitia njia ya
Makedonia. 4Paulo alikuwa amefuatana na
Sopatro mwana wa Piro, Mberoya, Aristarko na
Sekundo kutoka Thesalonike na Gayo, mtu wa
Derbe, Timotheo pamoja na Tikiko na Trofimo
kutoka sehemu ya Asia. 5Hawa watu
walitutangulia wakaenda kutungojea Troa.
6Lakini sisi tukasafiri kwa njia ya bahari kwa siku
tano kutoka Filipi baada ya siku za Siku kuu ya
Mikate Isiyotiwa Chachu, nasi tukaungana na
wengine huko Troa, ambako tulikaa kwa siku
saba.

### *Eutiko Afufuliwa Huko Troa*

7Siku ya kwanza ya juma tulikutana pamoja
kwa ajili ya kumega mkate. Paulo akaongea na
watu, naye kwa kuwa alikuwa amekusudia
kuondoka kesho yake, aliendelea kuongea
mpaka usiku wa manane. 8Kwenye chumba cha
ghorofani walikokuwa wamekutania kilikuwa na
taa nyingi. 9Kijana mmoja jina lake Eutiko,
aliyekuwa amekaa dirishani, wakati Paulo
alipokuwa akiendelea kuhubiri kwa muda mrefu,
alipatwa na usingizi mzito, akaanguka kutoka
ghorofa ya tatu, wakamwinua akiwa amekufa.
10Paulo akashuka chini, akajitupa juu ya yule
kijana na kumkumbatia, akasema, "Msishtuke,
uzima wake bado umo ndani yake." 11Kisha
Paulo akapanda tena ghorofani, akamega
mkate na kula. Baada ya kuongea mpaka
mapambazuko, akaondoka. 12Watu
wakamrudisha yule kijana nyumbani akiwa hai
nao wakafarijika sana.

### *Paulo Awaaga Wazee Wa Efeso*

13Tuliingia melini tukasafiri kwa njia ya
bahari mpaka Aso ambako ndiko tungempakia
Paulo, ndivyo alivyopanga maana alitaka kufika
huko kupitia nchi kavu. 14 Alipotukuta huko Aso,
tulimpakia melini tukasafiri wote mpaka Mitilene.
15Kutoka huko tuliendelea kwa njia ya bahari na
kesho yake tukafika mahali panapokabili Kio.
Siku iliyofuata tukavuka kwenda Samo na kesho
yake tukawasili Mileto. 16Paulo alikuwa
ameamua tusipitie Efeso ili asitumie muda
mwingi huko sehemu za Asia, kwa sababu
alikuwa anatamani kufika Yerusalemu kama
ikiwezekana kabla ya siku ya Pentekoste.

17Paulo akiwa Mileto, akatuma ujumbe
kwenda Efeso kuwaita wazeee wa kanisa waje
wakutane naye. 18Walipofika akawaambia,
"Ninyi wenyewe mnajua jinsi nilivyoishi katikati
yenu muda wote tangu siku ya kwanza
nilipokanyaga hapa Asia. 19Nilimtumikia Bwana
kwa unyenyekevu wote na kwa machozi
nikivumilia taabu na mapingamizi yaliyonipata
kutokana na hila za Wayahudi. 20Mnajua
kwamba sikusita kuhubiri jambo lo lote ambalo
lingekuwa la kuwafaa ninyi lakini nilifundisha
hadharani na nyumba kwa nyumba. 21Kama
nilivyowashuhudia Wayahudi na Wayunani
kwamba inawapasa kumgeukia Mungu kwa
kutubu dhambi na kumwamini Bwana wetu
Yesu Kristo.

22"Nami sasa nimesukumwa na Roho
ninakwenda Yerusalemu wala sijui ni nini
kitakachonipata huko. 23Ila ninachojua tu ni
kwamba Roho Mtakatifu amenionya kuwa
vifungo na mateso vinaningoja. 24Lakini
siyahesabu maisha yangu kuwa ya thamani
kwangu, kama kuyamaliza mashindano na
kukamilisha ile kazi Bwana Yesu aliyonipa,
yaani, kazi ya kuishuhudia injili ya neema ya
Mungu.

25"Nami sasa najua ya kuwa hakuna hata
mmoja miongoni mwenu ninyi ambaye
nimemhubiria Ufalme wa Mungu katika kwenda
kwangu huko na huko, atakayeniona uso tena.
26Kwa hiyo nawaambieni leo hii kwamba sina
hatia ya damu ya mtu awaye yote. 27Kwa kuwa

sikusita kuwatangazia mapenzi yote ya Mungu. 28Jilindeni nafsi zenu na mlilinde lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake. Lichungeni kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe. 29Najua kwamba baada ya kuondoka, mbwa mwitu wakali watakuja katikati yenu ambao hawatalihurumia kundi. 30Hata kutoka miongoni mwenu wenyewe watainuka watu na kupotosha kweli ili wawavute wanafunzi wawafuate. 31Hivyo jilindeni! Kumbukeni kwamba kwa miaka mitatu sikuacha kamwe kuwaonya, kila mmoja kwa machozi usiku na mchana.

32“Sasa nawakabidhi kwa Mungu na kwa neno la neema yake, linaloweza kuwajenga na kuwapa ninyi urithi miongoni mwa wote ambao wametakaswa. 33Sikutamani fedha wala dhahabu wala nguo ya mtu ye yote. 34Ninyi wenyewe mnajua kwamba mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami. 35Katika kila jambo nililofanya, nimewaonyesha kwamba kwa njia hii ya kufanya kazi kwa bidii imetupasa kuwasaidia wadhaifu, mkikumbuka maneno ya Bwana Yesu mwenyewe jinsi alivyosema, ‘Ni baraka zaidi, kutoa kuliko kupokea.’ ”

36Paulo alipomaliza kusema haya akapiga magoti pamoja nao wote akaomba. 37Wote wakalia, wakamkumbatia Paulo na kumbusu, 38Kilichowahuzunisha zaidi ni kwa sababu ya yale maneno aliyosema kwamba kamwe hawatauona uso wake tena. Wakaenda naye mpaka kwenye meli.

### *Safari Ya Tatu Ya Paulo*

### *Paulo Aenda Yerusalemu*

**21** Tulipokwisha kujitenga nao na kuanza safari kwa njia ya bahari moja kwa moja mpaka Kosi. Siku ya pili yake tukafika Rodo na kutoka huko tukaenda Patara. 2Hapo tukapata meli iliyokuwa inavuka kwenda Foinike tukapanda tukasafiri nayo. 3Tulipokiona kisiwa cha Kipro, tukakizunguka tukakiacha upande weti wa kushoto, tukasafiri mpaka Shamu, tukatia nanga katika bandari ya Tiro ambapo meli yetu ilikuwa ipakue shehena yake. 4Baada ya kuwatafuta wanafunzi wa huko, tukakaa nao kwa siku saba. Wale wanafunzi wakiongozwa na Roho walimwambia Paulo asiende Yerusalemu. 5Lakini muda wetu ulipokwisha, tukaondoka tukaendelea na safari yetu. Wale wanafunzi pamoja na wake zao na watoto walitusindikiza hadi nje ya mji. Wote tukapiga magoti pale pwani tukaomba. 6 Baada ya kuagana, tulipanda melini, nao wakarudi majumbani mwao.

7Tukaendelea na safari yetu toka Tiro tukafika Tolemai, tukawasalimu wanafunzi wa huko tukakaa nao kwa siku moja. 8Siku iliyofuata tukaondoka, tukafika Kaisaria. Huko tukaenda nyumbani kwa Mwinjilisti mmoja jina lake Filipo, aliyekuwa mmoja wa wale watu saba waliochaguliwa kule Yerusalemu, tukakaa kwake. 9Filipo alikuwa na binti wanne mabikira ambao walikuwa wanatoa unabii.

10Baada ya kukaa kwa siku kadhaa, akatelemka nabii mmoja kutoka Uyahudi jina lake Agabo. 11Alipotufikia akachukua mshipi wa Paulo akajifunga, akautumia kufunga mikono na miguu yake mwenyewe akasema, “Roho Mtakatifu anasema: ‘Hivi ndivyo Wayahudi wa Yerusalemu watakavyomfunga mwenye mshipi huu na kumkabidhi kwa watu Mataifa.’ ”

12Tuliposikia maneno haya sisi na ndugu wengine tukamsihi Paulo asiende Yerusalemu. 13Lakini Paulo akajibu, “Kwa nini mnalia na kunivunja moyo? Mimi niko tayari si kufungwa tu, bali hata kufa huko Yerusalemu kwa ajili ya jina la Bwana Yesu.” 14Alipokuwa hashawishiki, tukaacha kumsihi, tukasema, “Mapenzi ya Bwana na yatendeke.”

15Baada ya haya, tukajiandaa, tukaondoka kwenda Yerusalemu. 16Baadhi ya wanafunzi kutoka Kaisaria wakafuatana nasi na kutupeleka nyumbani kwa Mnasoni, ambaye tungekaa kwake. Yeye alikuwa mtu wa Kipro, mmoja wa wanafunzi wa zamani.

### *Paulo Awasili Yerusalemu*

17Tulipofika Yerusalemu ndugu wakatukaribisha kwa furaha. 18Kesho yake Pualo pamoja na wengine wetu tulikwenda kumwona Yakobo na wazee wote wa kanisa walikuwepo. 19Baada ya kuwasalimu, Paulo akatoa taarifa kamili ya mambo yote ambayo Mungu alikuwa amefanya miongoni mwa watu Mataifa kwa kupitia huduma yake.

20Baada ya kusikia mambo haya wakamwadhimisha Mungu. Ndipo wakamwambia Paulo, “Ndugu, unaona, kuna elfu nyingi za Wayahudi walioamini, nao wote wana bidii kwa ajili ya sheria. 21Lakini wameambiwa habari zako kwamba unafundisha Wayahudi wote waishio miongoni mwa watu Mataifa kumkataa Mose na kwamba unawaambia wasiwatahiri watoto wao wala

kufuata desturi. [22]Sasa tufanyeje? Bila shaka watasikia kwamba umekuja Yerusalemu. [23]Kwa hiyo fanya lile tunalokuambia. Tunao watu wane hapa ambao wameweka nadhiri. [24]Jiunge na watu hawa, mfanye utaratibu wa ibada ya kujitakasa pamoja nao na ulipe gharama ili wanyoe nywele zao. Kwa njia hii kila mtu atafahamu ya kuwa mabo waliyosikia si ya kweli na kwamba wewe unaishika sheria. [25]Lakini kuhusu wale watu Mataifa waliomini tumewaandikia uamuzi wetu kwamba wajitenge na kitu cho chote kilichotolewa sadaka kwa sanamu na damu au kula nyama ya mnyama aliyeuawa kwa kunyongwa, tena wajitenge na uasherati."

[26]Ndipo kesho yake Paulo akawachukua wale watu na akajitakasa pamoja nao. Akaingia ndani ya hekalu ili akatoe taarifa ya tarehe ambayo siku zao za utakaso zingemalizika na sadaka ingetolewa kwa ajili ya kila mmoja wao.

### *Paulo Akamatwa*

[27]Zile siku saba zilipokaribia kumalizika, baadhi ya Wayahudi kutoka sehemu za Asia waliokuwa wamemwona Paulo ndani ya hekalu, wakachochea umati wote wa watu wakamkamata. [28]Wakapiga kelele wakasema, "Waisraeli wenzetu, tusaidieni! Huyu ndiye yule mtu anayefundisha kila mtu na kila mahali dhidi ya watu wetu, sheria zetu na hata hekalu hili. Zaidi ya hayo amewaleta Wayunani ndani ya hekalu na kupanajisi mahali hapa patakatifu." [29](Walikuwa wamemwona Trofimo, mwenyeji wa Efeso, akiwa mjini pamoja na Pualo wakadhani kuwa Paulo alikuwa amemwingiza Hekaluni.)

[30]Mji wote ukataharuki, watu wakaja wakikimbia kutoka pande zote wakamkamata Paulo, wakamburuta kutoka mle hekaluni. Milango ya hekalu ikafungwa. [31]Walipokuwa wakitaka kumwua, habari zikamfikia jemadari wa jeshi la askari wa Kirumi kwamba mji wa Yerusalemu wote ulikuwa katika machafuko. [32]Mara yule jemadari akachukua maafisa wengine wa jeshi pamoja na maaskari wakakimbilia kwenye ile ghasia, wale watu waliokuwa wakifanya ghasia walipomwona yule jemadari na askari wakija, wakaacha kumpiga Paulo.

[33]Yule jemadari akaja, kumkamata Paulo akaamuru afungwe kwa minyororo miwili. Akauliza yeye ni nani na alikuwa amefanya nini. [34]Baadhi ya watu katika ule umati wakapiga kelele, hawa wakisema hili na wengine wakisema lile. Yule jemadari alipoona kuwa hawezi kupata hakika ya habari kwa sababu ya zile kelele, akaamuru Paulo apelekwe katika ngome ya jeshi. [35]Paulo alipofika penye ngazi, ilibidi maaskari wambebe juu juu kwa sababu fujo za ule umati wa watu zilikuwa kubwa. [36]Ule umati ulikuwa ukifuata uliendelea kupiga kelele wakisema, "Mwondoe huyu!"

### *Paulo Anajitetea*

[37]Mara tu Paulo alipokaribia kuingizwa kwenye ngome ya jeshi, akamwambia yule jemadari, "Je, naweza kukuambia jambo moja?"

Yule jemadari akamjibu, "Je, unajua Kiyunani?"

[38]Je, wewe si yule Mmisri ambaye siku hizi za karibuni alianzisha uasi akaongoza kundi la magaidi elfu nne wenye silaha jangwani?"

[39]Paulo akajibu, "Mimi ni Myahudi, mzaliwa wa Tarso, huko Kilikia, raia wa mji usiokuwa wa kawaida. Tafadhali niruhusu nizungumze na hawa watu."

[40] Akiisha kupata ruhusa ya yule jemadari, Paulo akasimama penye ngazi akawapungia watu mkono ili wanyamaze. Wote waliponyamaza kimya, Paulo akazungumza nao kwa lugha ya Kiebrania, akasema:

### *Ushuhuda Wa Paulo Kwa Wayahudi Wa Yerusalemu*

**22** "Ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni utetezi wangu."

[2]Waliposikia akisema kwa lugha ya Kiebrania, wakanyamaza kimya kabisa.

Ndipo Paulo akasema, [3]"Mimi ni Myahudi, niliyezaliwa Tarso huko Kilikia, lakini nimelelewa hapa penye mji huu, miguuni mwa Gamalieli. Nilifundishwa kikamilifu katika sheria ya baba zetu, nikiwa mwenye juhudi kwa ajili ya Mungu kama kila mmoja wenu alivyo leo. [4]Niliwatesa watu wa Njia hii hadi kufa, nikiwakamata, waume kwa wake na kuwatupa gerezani. [5]Kama kuhani mkuu na baraza zima la wazee wanavyoweza kushuhudia kuhusu mimi. Hata nilipokea barua kutoka kwao kwenda kwa wale wa Dameski, nami nikaenda huko ili kuwaleta watu hawa Yerusalemu kama wafungwa ili waadhibiwe.

### *Paulo Aeleza Juu ya Kuongoka Kwake*

[6]"Nilipokuwa njiani kuelekea Dameski, yapata saa sita mchana, ghafula nuru kubwa kutoka mbinguni ikanimulika kote kote.

7Nikaanguka chini, nikasikia sauti ikiniambia,
'Sauli, Sauli, Mbona unanitesa?'
8Nikajibu, " 'Wewe ni nani Bwana?'
Naye akaniambia, " 'Mimi ni Yesu wa
Nazareti unayenitesa.' 9Basi wale watu
waliokuwa pamoja nami waliiona ile nuru, lakini
hawakuisikia ile sauti ya yule aliyekuwa akisema
nami.
10Nikauliza, " 'Nifanye nini Bwana?'
Naye Bwana akaniambia, " 'Inuka uingie
Dameski, huko utaambiwa mambo yote
yakupasayo kufanya.' 11 Kwa kuwa nilikuwa
siwezi kuona mng'ao wa ile nuru, wenzangu
wakanishika mkono wakaniongoza kuingia
Dameski.

12"Mtu mmoja Mcha Mungu, jina lake
Anania alikuja kuniona, aliyeshika sana sheria
zetu, na ambaye aliheshimiwa sana na
Wayahudi waliokuwa wakiishi huko Dameski,
13alisimama karibu nami akasema, 'Ndugu
Sauli, upate kuona tena!' saa ile ile nikapata
kuona tena, nami nikaweza kumwona.

14"Akasema, 'Mungu wa baba zetu
amekuchagua wewe ili ujue mapenzi yake,
umwone yeye Aliye Mwenye Haki na upate
kusikia maneno kutoka kinywani mwake. 15Kwa
kuwa utakuwa shahidi wake kwa watu kuhusu
kile ulichokiona na kukisikia. 16Sasa basi,
mbona unakawia? Inuka, ukabatizwe na dhambi
zako zikasafishwe, ukiliita jina lake.'

### *Paulo Atumwa Kwa Watu Mataifa*

17"Baada ya kurudi Yerusalemu, wakati
nikiwa ninaomba hekaluni, nilipatwa na usingizi
mzito 18nikamwona Yesu akiniambia,
'Harakisha utoke Yerusalemu upesi, maana
hawataukubali ushuhuda wako kunihusu mimi.'

19"Nami nikasema, 'Bwana, wao wenyewe
wanajua jinsi nilivyokwenda kwenye kila
sinagogi ili kuwatia gerezani na kuwapiga wale
waliokuamini. 20Wakati damu ya shahidi wako
Stefano ilipomwagwa, mimi mwenyewe nilikuwa
nimesimama kando, nikikubaliana na kitendo
hicho na kutunza mavazi ya wale waliomwua'.

21Ndipo Bwana akaniambia, 'Nenda, kwa
maana nitakutuma mbali, kwa watu Mataifa.' "

### *Paulo Na Jemadari Wa Kirumi*

22Ule umati wa watu wakamsikiliza Paulo
mpaka aliposema neno hilo, ndipo wakapaza
sauti zao na kupiga kelele wakisema,
"Mwondoeni duniani, hafai kuishi!"

23Wakati walipokuwa wakipiga na kutupa
mavazi yao huku wakirusha mavumbi juu
hewani, 24yule jemadari akaamuru Paulo
aingizwe kwenye ngome. Akaelekeza kwamba
achapwe viboko na aulizwe ili kujua kwa nini
watu walikuwa wanampigia kelele namna hiyo.
25Lakini walipokwisha kumfunga kwa kamba za
ngozi ili wamchape viboko, Paulo akamwambia
kiongozi wa maaskari aliyekuwa amesimama
pale karibu naye, "Je, ni halali kwenu kwa
mujibu wa sheria kumchapa mtu ambaye ni raia
wa Rumi hata kabla hajapatikana na hatia?"

26Yule askari aliposikia maneno haya,
alimwendea yule jemadari na kumwambia,
"Unataka kufanya nini? Kwa maana huyu mtu ni
raia wa Rumi."

27Yule jemadari akaja akamwuliza Pualo,
"Niambie, wewe ni raia wa Rumi?"
Paulo akajibu, "Naam, hakika ndiyo."
28Ndipo yule jemadari akasema, "Mimi
ilinigharimu kiasi kikubwa cha fedha kupata
uraia wangu."
Paulo akasema "Lakini mimi ni raia wa
Rumi kwa kuzaliwa."

29Mara wale waliokuwa wanataka kumhoji
wakajiondoa haraka na yule jemadari akaingiwa
na hofu, alipotambua ya kuwa amemfunga
Paulo, ambaye ni raia wa Rumi kwa minyororo.

### *Paulo Apelekwa Mbele Ya Baraza*

30Kesho yake, kwa kuwa yule Jemadari
alitaka kujua hakika kwa nini Paulo alikuwa
anashutumiwa na Wayahudi, alimfungua na
kuwaagiza viongozi wa makuhani na baraza
lote likutane. Kisha akamleta Paulo
akamsimamisha mbele yao.

**23** Paulo akawakazia macho wale wajumbe
wa baraza, akasema, "Ndugu zangu, nimetimiza
wajibu wangu kwa Mungu
kwa dhamiri safi kabisa hadi leo." 2Kwa ajili ya
jambo hili Kuhani Mkuu Anania akaamuru wale
waliokuwa karibu na Paulo wampige kofi
kinywani. 3Ndipo Paulo akamwambia, "Mungu
atakupiga wewe, ewe ukuta uliopakwa chokaa!
Wewe umeketi hapo ili kunihukumu kwa mujibu
wa sheria, lakini wewe mwenyewe unakiuka
sheria kwa kuamuru kwamba nipigwe kinyume
cha sheria!"

4Wale watu waliokuwa wamesimama karibu
na Paulo wakamwambia, "Je, wewe wathubutu
kumtukuna Kuhani Mkuu wa Mungu?"

5Paulo akajibu, "Ndugu zangu, sikujua
kwamba yeye alikuwa Kuhani Mkuu. Kwa
maana imeandikwa, 'Usimnene mabaya

kiongozi wa watu wako.' "

6Paulo alipotambua ya kuwa baadhi yao walikuwa Masadukayo na wengine ni Mafarisayo, akapaza sauti kwenye baraza, "Ndugu zangu, mimi ni Farisayo, mwana Farisayo. Hapa nimeshtakiwa kuhusu tumaini langu katika ufufuo wa wafu." 7Aliposema haya, farakano likaanza kati ya Mafarisayo na Masadukayo na baraza lote likagawanyika. 8(Kwa maana Masadukayo wanasema kwamba hakuna ufufuo, wala hakuna malaika au roho, lakini Mafarisayo wanaamini haya yote.)

9Kukawa na ghasia kubwa, nao baadhi ya walimu wa sheria ambao ni Mafarisayo, wakasimama wakapinga kwa nguvu wakisema, "Hatuoni kosa lo lote la mtu huyu! Huenda ikawa roho au malaika amezungumza naye" 10Ugomvi ukawa mkubwa kiasi kwamba yule jemadari akahofu kuwa wangemrarua Paulo vipande vipande, akaamuru vikosi vya askari vishuke na kumwondoa Paulo katikati yao kwa nguvu na kumleta ndani ya ngome ya jeshi.

11Usiku uliofuata, Bwana akasimama karibu naye akamwambia, "Jipe moyo! Kama vile ulivyonishuhudia hapa Yerusalemu, hivyo imekupasa kunishuhudia huko Rumi pia."

### *Hila Za Kumwua Paulo*

12Kulipopambazuka Wayahudi wakafanya shauri pamoja na kujifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala kunywa mpaka wamemwua Paulo. 13Waliofanya mpango huo walikuwa zaidi ya watu arobaini. 14Wakawaendea viongozi wa makuhani na wazee na kusema, "Tumejifunga pamoja kwa kiapo kwamba hatutakula wala kunywa mpaka tumemwua Paulo. 15Hivyo basi, wewe pamoja na baraza, inawapasa mumjulishe kwa jemadari ili amteremshe Paulo kwenu, mjifanye kama mnataka kufanya uchunguzi wa kina zaidi wa shauri lake. Nasi tuko tayari kumwua kabla hajafika hapa."

16Lakini mtoto wa dada yake Paulo aliposikia juu ya shauri hilo baya, alikwenda kule kwenye ngome ya askari na kumweleza Paulo.

17Ndipo Paulo akamwita mmoja wa wakuu wa maaskari akamwambia, "Mpeleke huyu kijana kwa jemadari, analo jambo la kumweleza." 18Hivyo yule mkuu wa maaskari akampeleka yule kijana kwa jemadari akamwambia, "Paulo, yule mfungwa aliniita na kuniomba nimlete huyu kijana kwako, kwa sababu ana neno la kukueleza."

19Yule jemadari akamshika yule kijana mkono, akampeleka kando na kumwuliza, "Unataka kuniambia nini?"

20Yule kijana akasema, "Wayahudi wamekubaliana wakuombe umpeleke Paulo kwenye baraza lao kesho kwa kisingizio kwamba wanataka kufanya uchunguzi wa kina wa shauri lake. 21 Lakini usishawishiwe nao kwa maana zaidi ya watu arobaini wanamvizia. Wamejifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala kunywa mpaka wamemwua Paulo. Sasa wako tayari, wanangoja idhini yako kwa ajili ya ombi lao."

22Yule jemadari akamruhusu yule kijana aende na akamwonya, akisema, "Usimwambie mtu ye yote kwamba umenieleza habari hizi.''

### *Paulo Ahamishiwa Kaisaria*

23Kisha yule jemadari akawaita wakuu wake wawili wa maaskari akawaambia, "Jiandaeni kuondoka saa tatu usiku huu kuelekea Kaisaria pamoja na askari 200, wapanda farasi 70 na watu 200 wenye mikuki. 24Pia tayarisheni na farasi watakaotumiwa na Paulo, mumpeleke salama mpaka kwa mtawala Feliksi."

25Kisha akaandika barua kwa Feliksi kama ifuatavyo:

26Klaudio Lisia,

Kwa Mtawala, Mtukufu Feliksi, Salaam.

27Mtu huyu alikamatwa na Wayahudi wakakaribia kumwua, lakini nikaja na vikosi vyangu vya maaskari nikamwokoa kwa kuwa nilipata habari kwamba yeye ni raia wa Rumi. 28Nilitaka kujua kwa nini walikuwa wanamshutumu, hivyo nikamleta mbele ya baraza lao. 29Ndipo nikaona kuwa alikuwa anashutumiwa kwa mambo yanayohusu sheria yao, lakini hakuwa ameshtakiwa kwa jambo lo lote linalostahili kifo au kifungo. 30Nilipoarifiwa kuwa kulikuwa na shauri baya dhidi ya mtu huyu, nilimtuma kwako mara, nikiwaagiza washtaki wake pia waeleze mbele yako mashtaka yao dhidi yake.

31Hivyo maaskari, kwa kufuata maelekezo waliyopewa, wakamchukua Paulo wakati wa usiku na kumleta mpaka Antipatri. 32 Kesho yake wakawaacha wale wapanda farasi waendelee na safari wakiwa na Paulo, wakati wao walirudi kwenye ngome ya maaskari. 33Walipofika

Kaisaria kumpa mtawala ile barua, walimkabidhi pia Paulo kwake. 34Mtawala alipokwisha kuisoma ile barua alimwuliza Paulo kwamba alikuwa mtu wa jimbo gani. Alipojua kuwa anatoka Kilikia, 35alisema, "Nitasikiliza shauri lako washtaki wako watakapofika hapa." Kisha akaamuru Paulo awekwe chini ya ulinzi kwenye jumba la kifalme la Herode.

### *Mbele Ya Feliksi Huko Kaisaria*

**24** Baada ya siku tano, Kuhani Mkuu Anania akashuka akiwa amefuatana na baadhi ya wazee pamoja na mwanasheria mmoja aitwaye Tertulo, nao wakaleta mashtaka yao dhidi ya Paulo mbele ya mtawala. 2Paulo alipoitwa aingie ndani, Tertulo akaanza kutoa mashtaka akisema, "Mtukufu Feliksi, kwa muda mrefu tumefurahia amani na matengenezo mengi mazuri yamefanywa kwa ajili ya watu hawa kwa sababu ya upeo wako wa kuona mambo ya mbele. 3Wakati wote na kila mahali, kwa namna yo yote, mtukufu sana Feliksi, tumeyapokea mambo haya yote kwa shukrani nyingi. 4Lakini nisije nikakuchosha zaidi, ningekuomba kwa hisani yako utusikilize kwa kifupi.

5"Tumemwona mtu huyu kuwa ni msumbufu, anayechochea ghasia miongoni mwa Wayahudi duniani pote. Yeye ndiye kiongozi wa dhehebu la Wanazareyo 6na hata amejaribu kulinajisi hekalu, hivyo tukamkamata tukataka kumhukumu kufuatana na sheria zetu. 7Lakini jemadari Lisia, alitujia na nguvu nyingi akamwondoa mikononi mwetu, 8akiwaamuru washtaki wake waje mbele yako: ili kwa kumchunguza wewe mwenyewe unaweza kujua kutoka kwake mambo yote yale tunayomshtaki kwayo."

9Pia wale Wayahudi wakaunga mkono wakithibitisha kuwa mashtaka yote haya ni kweli.

### *Paulo Ajitetea Mbele Ya Feliksi*

10Mtawala Feliksi alipompungia Paulo mkono ili ajitetee, yeye akajibu, "Najua kwamba wewe umekuwa hakimu katika taifa hili kwa miaka mingi, hivyo natoa utetezi wangu kwa furaha. 11Unaweza kuhakikisha kwa urahisi kuwa hazijapita zaidi ya siku kumi na mbili tangu nilipopanda kwenda Yerusalemu kuabudu. 12Hawa wanaonishtaki hawakunikuta nikibishana na mtu ye yote hekaluni au kuchochea umati wa watu katika sinagogi au mahali pengine po pote mjini. 13Wala hawawezi kabisa kukuthibitishia mashtaka haya wanayonishtaki kwayo. 14Lakini, ninakubali kwamba mimi namwabudu Mungu wa baba zetu mfuasi wa 'Njia' ile ambayo wao wanaiita dhehebu. Ninaamini kila kitu kinachokubaliana na Sheria na kile kilichoandikwa katika Manabii, 15nami ninalo tumaini kwa Mungu, ambalo hata wao wenyewe wanalikubali kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, kwa wote wenye haki na wasio na haki. 16Kwa hiyo ninajitahidi siku zote kuwa na dhamiri safi mbele za Mungu na mbele za wanadamu.

17 "Basi, baada ya kutokuwapo kwa miaka mingi nilikuja Yerusalemu ili kuwaletea watu wangu msaada kwa ajili ya maskini na kutoa dhabihu. 18Nilikuwa nimeshatakaswa kwa taratibu za kiibada waliponikuta hekaluni nikifanya mambo haya. Hapakuwa na umati wa watu, pamoja nami wala aliyehusika kwenye fujo yo yote. 19Lakini kulikuwa na baadhi ya Wayahudi kutoka Asia, ambao wangelazimika wawepo hapa mbele yako ili watoe mashtaka kama wanalo jambo lo lote dhidi yangu. 20Au, watu hawa walioko hapa waseme ni uhalifu gani walioniona nao waliponisimamisha mbele ya baraza, 21isipokuwa ni kuhusu jambo hili moja nililopiga kelele mbele yao kwamba, 'Mimi nashtakiwa mbele yako leo kwa sababu ya ufufuo wa wafu.' "

22 Basi Feliksi ambaye alikuwa anafahamu vizuri habari za Njia ile, akaahirisha shauri lile kwa maelezo yake akisema, "Wakati jemadari Lisia atakapoteremka huku, nitaamua shauri lako." 23 Ndipo akaamuru mkuu wa maaskari amweke chini ya ulinzi lakini ampe uhuru na kuwaruhusu rafiki zake wamhudumie.

24Baada ya siku kadhaa Feliksi alipokuja pamoja na Drusila mkewe, ambaye alikuwa Myahudi, alituma aitiwe Paulo na kumsikiliza alipokuwa akinena juu ya imani katika Yesu Kristo. 25Naye Paulo alipokuwa akinena juu ya haki kuwa na kiasi na juu ya hukumu ijayo, Feliksi aliingiwa na hofu na kusema, "Hiyo yatosha sasa! Waweza kuondoka. Nitakapokuwa na wasaa nitakuita." 26Wakati huo huo Feliksi alitazamia kwamba Paulo angempatia rushwa. Hivyo akawa anamwita mara kwa mara na kuzungumza naye.

27 Baada ya miaka miwili kupita, Porkio Festo akaingia kwenye utawala mahali pa Feliksi, lakini kwa kuwa Feliksi alitaka kuwapendeza Wayahudi, akamwacha Paulo

gerezani.

### *Paulo Mbele Ya Festo*

**25** Siku tatu baada ya Festo kuwasili Kaisaria kuchukua wajibu wake mpya, alipanda kwenda Yerusalemu, 2ambako viongozi wa makuhani na viongozi wa Wayahudi walikuja mbele yake na kuleta mashtaka yao dhidi ya Paulo. 3Wakamsihi sana Festo, kama upendeleo kwao, aamuru Paulo ahamishiwe Yerusalemu, kwa kuwa walikuwa wanaandaa kumvizia ili wamwue akiwa njiani. 4Festo akawajibu, "Paulo amezuiliwa huko Kaisaria, nami mwenyewe ninakwenda huko hivi karibuni. 5Baadhi ya viongozi wenu wafuatane nami na kutoa mashtaka dhidi ya mtu huyo huko, kama amekosa jambo lo lote."

6Baada ya Festo kukaa miongoni mwao kwa karibu siku nane au kumi, akashuka kwenda Kaisaria na siku iliyofuata akaitisha mahakama, akaketi penye kiti chake cha hukumu, akaamuru Paulo aletwe mbele yake. 7Paulo alipotokea, wale Wayahudi waliokuwa wameteremka toka Yerusalemu wakasimama wakiwa wamemzunguka, wakileta mashtaka mengi mazito dhidi yake ambayo hawakuweza kuyathibitisha.

8Ndipo Paulo akajitetea, akasema, "Mimi sikufanya jambo lo lote kinyumbe cha sheria ya Wayahudi au dhidi ya hekalu au kinyume cha Kaisari."

9Festo, akitaka kuwapendeza Wayahudi, akamwuliza Paulo, "Je, ungependa kwenda Yerusalemu na kukabili mashtaka mbele yangu huko?"

10Paulo akasema, "Mimi sasa nimesimama mbele ya mahakama ya Kaisari, ambako ndiko ninakostahili kushtakiwa. Kama vile wewe mwenyewe ujuavyo vema kabisa sijawatendea Wayahudi kosa lo lote. 11 Basi kama mimi nina hatia ya kutenda kosa lo lote linalostahili kifo, sikatai kufa. Lakini kama mashtaka yaliyoletwa dhidi yangu na hawa Wayahudi si kweli, hakuna ye yote aliye na haki ya kunikabidhi mikononi mwao. Naomba rufaa kwa Kaisari!"

12Baada ya Festo kufanya shauri pamoja na baraza lake, akatangaza, "Wewe umeomba rufaa kwa Kaisari, nako kwa Kaisari utakwenda!"

### *Festo Aomba Ushauri Kwa Agripa*

13Baada ya siku kadhaa Mfalme Agripa na Bernike wakapanda kuja Kaisaria kumsalimu Festo. 14Kwa kuwa walikuwa wakae huko Kaisaria kwa siku nyingi, Festo alijadili shauri la Paulo na mfalme, akisema, "Kuna mtu mmoja hapa ambaye Feliksi alimwacha gerezani. 15Nilipokuwa huko Yerusalemu, viongozi wa makuhani na wazee wa Wayahudi walinijulisha habari zake na wakaomba hukumu dhidi yake.

16"Lakini mimi nikawaambia kwamba si desturi ya Kirumi kumtoa mtu ye yote auwawe kabla mshtakiwa kuonana nao uso kwa uso na washtaki wake, naye awe amepewa nafasi ya kujitetea kuhusu mashtaka anayoshutumiwa. 17Hivyo walipokutana hapa, sikukawia, lakini kesho yake niliitisha baraza, nikaketi penye kiti changu cha hukumu, nikaagiza huyo mtu aletwe. 18Washtaki wake waliposimama, hawakushtaki kwa uhalifu wo wote niliokuwa ninatarajia. 19Badala yake walikuwa na vipengele fulani vya kutokukubaliana naye kuhusu dini yao na juu ya mtu mmoja aitwaye Yesu, ambaye alikufa, lakini yeye Paulo alidai kwamba yu hai. 20 Kwa kuwa sikujua jinsi ya kupeleleza jambo hili, nilimwuliza kama angependa kwenda Yerusalemu na kuhojiwa huko kuhusu mashtaka haya. 21Lakini Paulo alipoomba afadhiliwe ili rufaa yake isikilizwe na Mfalme Agusto, nilimwamuru alindwe mpaka nitakapoweza kumpeleka kwa Kaisaria."

22Ndipo Agripa akamwambia Festo, "Ningependa kumsikiliza mtu huyo mimi mwenyewe."

Yeye akajibu, "Kesho utamsikia."

### *Paulo Aletwa Mbele ya Agripa*

23Siku iliyofuata Agripa na Bernike walifika kwa fahari kubwa wakaingia katika ukumbi wa mahakama, pamoja na majemadari wa jeshi na watu mashuhuri wa mji. Ndipo kwa amri ya Festo, Paulo akaletwa ndani. 24Festo akasema, "Mfalme Agripa, nanyi nyote mlio hapa pamoja nasi, mnamwona mtu huyu! Jumuiya yote ya Kiyahudi wamenilalamikia kuhusu mtu huyu huko Yerusalemu na hapa Kaisaria, wakipiga kelele kwamba haimpasi kuendelea kuishi. 25Sikuona kwamba ametenda jambo lo lote linalostahili kifo, ila kwa kuwa alikuwa ameomba rufaa yake kwa Mfalme, niliamua kumpeleka Rumi. 26Lakini mimi sina kitu maalum cha kumwandikia mtukufu kumhusu mtu huyu. Kwa hiyo nimemleta mbele yenu ninyi nyote, hasa mbele yako, wewe Mfalme Agripa, ili kutokana na matokeo ya uchunguzi huu, niweze kupata kitu cha kuandika. 27Kwa kuwa naona hakuna

sababu ya kumpeleka mfungwa bila kuainisha
mashtaka dhidi yake.

### *Paulo Ajitetea Mbele ya Agripa*

**26** Ndipo Agripa akamwambia Paulo, "Unayo
ruhusa kujitetea."
Hivyo Paulo akawapungia kwa mkono
wake, akaanza kujitetea, akasema:- **2**"Mfalme
Agripa, najiona kuwa na heri kusimama mbele
yako leo ninapojitetea kuhusu mashtaka yote ya
Wayahudi, **3**hasa kwa sababu unajua vema
desturi zote za Kiyahudi na ya kuwa wewe
unajua kwa undani mila na maswala ya
mabishano. Kwa hiyo, nakusihi unisikilize kwa
uvumilivu.
**4**"Wayahudi wote wanajua jinsi nilivyoishi
tangu nilipokuwa mtoto, kuanzia mwanzo wa
maisha yangu katika nchi yangu na pia huko
Yerusalemu. **5**Wao wamefahamu kwa muda
mrefu na wanaweza kushuhudia kama
wakipenda, kutokana na misimamo mikali sana
ya dhehebu letu kwenye dini yetu niliishi nikiwa
Farisayo. **6**Nami sasa ni kwa sababu ya tumaini
langu katika kile ambacho Mungu aliwaahidi
baba zetu, ninashtakiwa leo. **7**Hii ndiyo ahadi
ambayo makabila yetu kumi na mawili
yanatarajia kuiona ikitimizwa wanapomtumikia
Mungu kwa bidii mchana na usiku. **8**Kwa nini ye
yote miongoni mwenu afikiri kwamba ni jambo
lisilosadikika Mungu kufufua watu?
**9**"Mimi pia nilikuwa nimeshawishika kwamba
imenipasa kufanya yote yale yaliyowezekana
kupinga jina la Yesu wa Nazareti. **10**Nami hayo
ndiyo nilivyofanya huko Yerusalemu. Kwa
mamlaka ya viongozi wa makuhani, niliwatia
wengi wa watakatifu gerezani na walipokuwa
wakiuawa, nilipiga kura yangu kuunga mkono.
**11**Mara nyingi nilikwenda kutoka sinagogi moja
hadi jingine nikiamuru waadhibiwe, nami
nilijaribu kuwalazimisha wakufuru. Katika
shauku yangu dhidi yao, hata nilikwenda miji ya
kigeni ili kuwatesa.

### *Paulo Aeleza Kuhusu Kuongoka Kwake*

**12** "Siku moja nilipokuwa katika mojawapo ya
safari hizi nikiwa ninakwenda Dameski, nilikiwa na
agizo kutoka kwa kiongozi wa makuhani. **13**Ilikuwa
yapata adhuhuri, Ee, Mfalme, nilipokuwa njiani,
niliona nuru kutoka mbinguni kali kuliko jua,
iking'aa kunizunguka pande zote mimi na wale
niliokuwa pamoja nao. **14**Wote tulipokuwa
tumeanguka chini, nikasikia sauti ikisema nami
kwa lugha ya Kiebrania, 'Sauli,
Sauli, mbona unanitesa? Ni vigumu kwako
kuupiga teke mchokoo.'
**15**"Nikauliza, 'Ni nani wewe, Bwana?'
Naye Bwana akajibu, " 'Ni Mimi Yesu
unayenitesa. **16**Lakini sasa inuka usimame, kwa
miguu yako, kwa sababu nimekutokea kwa
kusudi hili ili kukuweka utumike na kushuhudia
juu ya mambo ambayo umeyaona na yale
nitakayokutokea kwayo. **17**Nitakuokoa kutoka
kwa watu wako na watu Mataifa ambao
ninakutuma kwao, **18**uyafungue macho yao ili
wageuke kutoka gizani waingie nuruni na
kutoka kwenye nguvu za shetani, wamgeukie
Mungu ili wapate msamaha wa dhambi na
sehemu miongoni mwa wale waliotakaswa kwa
kuniamini Mimi.'
**19**"Hivyo basi, Mfalme Agripa, sikuacha
kuyatii yale maono yaliyotoka mbinguni, **20**bali
niliyatangaza kwanza kwa wale wa Dameski,
kisha Yerusalemu na katika vijiji vyote vya
Uyahudi na pia kwa watu Mataifa, kwamba
inawapasa kutubu na kumgeukia Mungu na
kuthibitisha toba yao kwa matendo yao. **21**Ni
kwa sababu hii Wayahudi walinikamata
nilipokuwa hekaluni, wakataka kuniua. **22**Hadi
leo nimepata msaada kutoka kwa Mungu na
hivyo nasimama hapa nikishuhudia wakubwa na
wadogo, bila kusema cho chote zaidi ya yale
ambayo manabii na Mose walisema yatatukia:
**23**kwamba Kristo atateswa na kwamba Yeye
atakuwa wa kwanza kufufuka kutoka kwa wafu,
atatangaza nuru kwa watu wake na kwa watu
Mataifa".

### *Paulo Aeleza Juu Ya Kuhubiri Kwake*

**24** Paulo alipokuwa akifanya utetezi huu,
Festo akasema kwa sauti kubwa, "Paulo, wewe
umerukwa na akili! Kusoma kwingi kunakufanya
uwe kichaa!"
**25**Lakini Paulo akajibu, "Mimi sijarukwa na
akili, mtukufu sana Festo, bali nanena kweli
nikiwa na akili zangu timamu. **26**Naam, Mfalme
anajua kuhusu mambo haya yote, nami nasema
naye kwa uhuru. Kwa sababu nina hakika
kwamba hakuna hata mojawapo ya mambo
haya asilolijua, kwa kuwa hayakufanyika
mafichoni. **27**Mfalme Agripa, Je, unaamimi
manabii? Najua kuwa unaamini."
**28**Agripa akamwambia Paulo, "Je,
unanishawishi kwa haraka namna hii niwe
Mkristo?"
**29**Paulo akasema, "Ikiwa ni kwa haraka au
la, namwomba Mungu, si wewe peke yako bali

pia wale wote wanaonisikiliza leo, wawe kama mimi nilivyo, isipokuwa minyororo hii."

30Baada ya kusema hayo, Mfalme akainuka pamoja na mtawala na Bernike nao wale waliokuwa wameketi pamoja nao, 31 wakati walipokuwa wakiondoka, wakaambiana "Mtu huyu hafanyi jambo lo lote linalostahili kufa au kufungwa."

32Agripa akamwambia Festo, "Mtu huyu angeweza kuachwa huru kama hangekuwa amekata rufaa kwa Kaisari."

### *Paulo Asafiri kwa Njia ya Bahari Kwenda Rumi*

27 Ilipoamuliwa kwamba tungesafiri kwa njia ya bahari twenda Italia, Paulo na wafungwa wengine wakakabidhiwa kwa askari mmoja jina lake Juliasi, ambaye alikuwa wa kikosi cha walinzi wa Kaisari Agusto. 2Tulipanda meli iliyotoka Adramitio, iliyokuwa inakaribia kusafiri kwenda kwenye bandari zilizopo pwani ya Asia, tukaanza safari yetu tukiwa pamoja na Aristarko, Mmakedonia kutoka Thesalonike.

3Kesho yake tukatia nanga Sidoni, naye Juliasi akamfanyia wema Paulo, akamruhusu aende kwa rafiki zake ili wampatie mahitaji yake. 4Kutoka huko tukaingia baharini tena na tukapita upande wa chini wa kisiwa cha Kipro kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho. 5 Baada ya sisi kuvuka bahari iliyoko upande wa Kilikia na Pamfilia, tukafika Mira huko Likia. 6Huko yule jemadari akapata meli ya Aleksandria ikielekea Italia, akatupandisha humo. 7Tukasafiri polepole kwa siku nyingi na kwa shida, hatimaye tukafika karibu na Nido. Kwa kuwa upepo wa mbisho, ulituzuia tusiweze kushika mwelekeo wa nia yetu, tukapita chini ya Krete mkabala na Salmone. 8Tukaambaa – ambaa na pwani, kwa shida tukafika sehemu moja iitwayo Bandari Nzuri, karibu na mji wa Lasea.

9Muda mwingi ulikuwa umepotea na kusafiri baharini kulikuwa hatari kwa sababu wakati huu ulikuwa baada ya siku za kufunga. Hivyo Paulo akawaonya, akasema, 10"Mabwana, naona kuwa hii safari ni yenye maafa na ya kuleta hasara kubwa kwa meli na shehena, pia kwa maisha yetu." 11Lakini badala ya yule askari kusikiliza yale Paulo aliyosema, akafuata zaidi ushauri wa nahodha na mwenye meli. 12Kwa kuwa ile bandari ilikuwa haifai kukaa wakati wa majira ya baridi, wengi wakashauri kwamba tuendelee na safari wakitarajia kufika Foinike na kukaa huko kwa majira ya baridi. Hii ilikuwa bandari iliyoko katika kisiwa cha Krete ikikabili upande wa kusini-magharibi na kaskazini-magharibi.

### *Dhoruba Baharini*

13Upepo mtulivu ulipoanza kuvuma toka kusini, wakadhani kuwa wangeweza kufikia lengo lao, hivyo wakang'oa nanga na kusafiri wakipita kando kando ya pwani ya kisiwa cha Krete. 14Lakini baada ya muda mfupi ikavuma tufani kubwa iitwayo "Eurakilo" toka kisiwa cha Krete. 15Meli ikapigwa na dhoruba na haikuweza kushindana na ule upepo, tukarudishwa baharini upepo ulikokuwa unaelekea. 16Hatimaye tukisafiri kupita chini ya kisiwa kidogo kiitwacho Kauda, ambapo kwa kuwa tulikuwa tumekingiwa upepo na hicho kisiwa, tuliweza kwa shida kuifunga mashua ya kuokolea watu. 17Watu walipokwisha kuivuta mashua hiyo na kuiingiza katika meli, waliifunga kwa kamba chini ya meli yenyewe ili kuzishikanisha pamoja. Wakiogopa kupelekwa kwenye mchanga karibu na pwani ya Sirti, wakashusha matanga wakaiacha meli isukumwe na huo upepo. 18Tulikuwa tunapigwa na dhoruba kwa nguvu kiasi kwamba kesho yake walianza kutupa shehena toka melini, 19siku ya tatu kwa mikono yao wenyewe, wakatupa vyombo vya meli baharini. 20Kulipokuwa hakuna kuonekana kwa jua wala nyota kwa siku nyingi, nayo dhoruba ikiwa inaendelea kuwa kali, hatimaye tulikata kabisa tamaa ya kuokoka.

21Baada ya watu kukaa siku nyingi bila kula chakula, Paulo akasimama katikati yao akasema, "Enyi watu, iliwapasa kunisikiliza na kuacha kusafiri baharini kutoka Krete, ndipo ninyi mngekuwa mmejinusuru na uharibifu huu na hasara hii. 23Jana usiku, malaika wa Mungu yule ambaye mimi ni wake na ambaye ninamwabudu alisimama karibu nami, 24naye akasema, 'Paulo usiogope, kwa kuwa ni lazima usimame mbele ya mfalme, naye Mungu amewapa salama wote wanaosafiri pamoja nawe. 25Hivyo jipeni moyo, enyi watu, kwa kuwa ninamwamini Mungu kwamba yatakuwa kama vile alivyoniambia.' 26Lakini hata hivyo meli yetu itakwama kwenye kisiwa fulani."

27Usiku wa kumi na nne, ulipofika, tulipokuwa bado tunasukumwa na upepo katika bahari ya Adria, ilipokuwa yapata usiku wa manane, mabaharia wakahisi kwamba walikuwa

wanakaribia nchi kavu. 28Kwa hiyo wakapima kina cha maji na kukuta kilikuwa pima ishirini[a], baada ya kuendelea mbele kidogo wakapima tena wakapata kina cha pima kumi na tano[b]. 29Wakiogopa kwamba meli yetu ingegonga kwenye miamba, wakashusha nanga nne za nyuma ya meli, wakawa wanaomba kupambazuke. 30Katika jaribio la kutoroka kutoka kwenye meli, mabaharia wakashusha mashua ya kuokolea watu baharini, wakijifanya kwamba wanakwenda kushusha nanga za omo[c]. 31Ndipo Paulo akamwambia yule jemadari na maaskari, "Hawa watu wasipobaki katika meli, hamtaweza kuokoka." 32Hivyo basi wale maaskari wakakata kamba zilizoshikilia ile mashua ya kuokolea watu kwenye meli wakaicha ianguke humo baharini.

33Kabla ya mapambazuko, Paulo akawasihi watu wote wale chakula akisema, "Leo ni siku ya kumi na nne mmekuwa katika wasiwasi mkiwa mmefunga na bila kula cho chote. 34Kwa hiyo nawasihi mle chakula, kwa maana itawasaidia ili mweze kuishi. Kwa kuwa hakuna hata mmoja wenu atakayepoteza unywele mmoja kutoka kichwani mwake." 35Baada ya kusema maneno haya, Paulo akachukua mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote, akaumega akaanza kula. 36Ndipo wote wakatiwa moyo, wakaanza kula chakula. 37Ndani ya meli tulikuwa jumla ya watu 276. 38Baada ya watu wote kula chakula cha kutosha, wakapunguza uzito wa meli kwa kutupa ngano baharini.

39Kulipopambazuka, mabaharia hawakuitambua ile nchi, lakini waliona ghuba yenye ufuko wa mchanga ambako waliamua kuipweleza meli kama ingewezekana. 40Kwa hiyo wakatupa nanga zote na kuziacha baharini, wakati huo huo wakalegeza kamba zilizokuwa zikishikilia usukani wa meli, kisha wakatweka tanga la mbele lishike upepo na kuisukuma meli kuelekea pwani. 41Lakini wakafika mahali ambapo bahari mbili zinakutana, wakaipweleza meli ufuoni, omo ikakwama sana, ikawa haiwezi kuondolewa, lakini sehemu ya shetri[d] ikavunjika vipande vipande kwa kule kupiga kwa mawimbi yenye nguvu.

42Wale maaskari wakapanga kuwaua wale wafungwa ili kuzuia hata mmoja wao asiogelee na kutoroka. 43Lakini yule jemadari akitaka kuokoa maisha ya Paulo, akawazuia maaskari wasitekeleze mpango wao. Akaamuru wale wanaoweza kuogelea wajitupe baharini kwanza, waogelee mpaka nchi kavu. 44Waliosalia wangefika nchi kavu kwa kutumia mbao au vipande vya meli iliyovunjika, hivyo ikatimia, kwamba wote wakaokoka na kufika nchi kavu salama.

### *Paulo Kisiwani Malta*

**28** Baada ya kufika nchi kavu salama, ndipo tukafahamu kwamba jina la kile kisiwa ni Malta.
2Wenyeji wa kile kisiwa hicho wakatufanyia ukarimu usio wa kawaida. Waliwasha moto na kutukaribisha sisi sote kwa sababu mvua ilikuwa inanyesha na ni baridi.
3Paulo alikuwa amekusanya mzigo wa kuni na alipokuwa anaweka kwenye moto, kwa ajili ya joto, nyoka mwenye sumu akatoka humo na kujisokotea mkononi mwake. 4Wale wenyeji wa kile kisiwa walipomwona yule nyoka akining'inia mkononi mwa Paulo, wakaambiana, "Huyu mtu lazima awe ni mwuaji, ingawa ameokoka kutoka baharini, haki haijamwacha aishi." 5Lakini Paulo akamkung'utia yule nyoka ndani ya moto wala yeye hakupata madhara yo yote. 6Watu walikuwa wanangoja avimbe au aanguke ghafula na kufa. Lakini baada ya kungoja kwa muda mrefu na kuona hakuna cho chote kisicho cha kawaida kilichomtokea, wakabadili mawazo yao na kuanza kusema kwamba yeye ni Mungu.

7Basi karibu na sehemu ile, palikuwa na shamba kubwa la mtu mmoja kiongozi wa kile kisiwa, aliyeitwa Publio, ambaye alitupokea akatuhudumia kwa ukarimu mkubwa kwa muda wa siku tatu. 8Baba yake Publio alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa anaumwa homa na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake na kumponya. 9Jambo hili lilipotukia, watu wote wa kisiwa kile waliokuwa wagonjwa wakaja, nao wakaponywa. 10Wakatupa heshima nyingi, nasi tulipokuwa tayari kusafiri kwa njia ya bahari, wakapakia melini vitu vyote tulivyokuwa tunavihitaji.

### *Paulo Anawasili Rumi*

11Miezi mitatu baadaye tukaanza safari kwa meli iliyokuwa imetia nanga kwenye kisiwa hicho kwa ajili ya majira ya baridi. Hii ilikuwa meli ya Aleksandria yenye alama ya miungu pacha waitwao Kasta na Poluksi.12Kituo chetu

---

a[28] Pima 20 ni kama mita 40.
b[28] Pima 15 ni kama mita 30
c[30] Omo hapa maana yake ni sehemu ya mbele ya meli ambayo pia huitwa gubeti.
d[41] Shetri – sehemu ya nyuma ya meli ambayo pia huitwa tezi.

cha kwanza kilikuwa Sirakusa na tukakaa huko
siku tatu, 13 Kisha tukang'oa nanga tukafika
Regio siku iliyofuata, upepo mkali wa kusi
ukavuma, na siku ya pili yake tukafika Puteoli.
14 Huko tukawakuta ndugu, nasi tukakaribishwa
tukae nao kwa siku saba. Hivyo tukaendelea na
safari mpaka Rumi. 15 Ndugu wa huko Rumi
waliposikia habari zetu, walikuja mpaka Soko la
Apio na mahali paitwapo 'Mikahawa Mitatu'
kutulaki. Paulo alipowaona, alimshukuru Mungu
akatiwa moyo. 16 Tulipofika Rumi, Paulo
aliruhusiwa kuishi peke yake akiwa na askari wa
kumlinda.

### *Paulo Ahubiri Rumi Chini Ya Ulinzi*

17 Siku tatu baadaye Paulo akawaita pamoja
viongozi wa Kiyahudi. Walipokwisha
kukusanyika akawaambia, "Ndugu zangu,
ingawa sikufanya jambo lo lote dhidi ya watu
wetu au dhidi ya desturi za baba zetu, lakini
nilikamatwa huko Yerusalemu nikakabidhiwa
kwa Warumi. 18 Wao walipokwisha kunihoji,
wakataka kuniachia huru kwa sababu
hawakuona kosa lo lote nililolifanya linalostahili
adhabu ya kifo. 19 Lakini Wayahudi walipopinga
uamuzi huo, nililazimika kukata rufaa kwa
Mfalme, ingawa sikuwa na lalamiko lo lote juu
ya taifa langu, 20 basi ili niseme nanyi, kwa kuwa
ni kwa ajili ya tumaini la Israeli nimefungwa kwa
minyororo."

21 Wakamjibu, "Hatujapokea barua zo zote
kutoka Uyahudi zinazokuhusu, wala hapana
ndugu ye yote aliyekuja hapa ambaye ametoa
taarifa au kuzungumza jambo lo lote baya juu
yako. 22 Lakini tungependa kusikia kutoka kwako
unalofikiri kwa sababu tunajua kwamba kila
mahali watu wanazungumza mabaya kuhusu
jamii hii."

23 Baada ya kupanga siku ya kuonana naye,
watu wengi wakaja kuanzia asubuhi hadi jioni
akawaeleza na kutangaza kuhusu Ufalme wa
Mungu akijaribu kuwahadithia juu ya Yesu
kutoka katika Sheria ya Mose na kutoka
Manabii. 24 Baadhi wakasadiki kwa yale
aliyosema, lakini wengine hawakuamini. 25 Hivyo
hawakukubaliana, nao walipokuwa
wanaondoka, Paulo akatoa kauli moja zaidi:
"Roho Mtakatifu alinena kweli na baba zenu
aliposema mambo yale yaliyomhusu Bwana
Yesu kwa kinywa cha Isaya kwamba,

26 " 'Nenda kwa watu hawa na useme,
''Kweli mtasikiliza lakini kamwe
hamtaelewa,
kweli mtatazama, lakini hamtaona,''
27 kwa kuwa mioyo ya watu hawa imekuwa
migumu,
na masikio yao ni mazito kusikia,
nao wamefumba macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
na kusikiliza kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao na kugeuka,
nami nikawaponya.'

28 "Basi na ijulikane kwenu kwamba, huu
wokovu wa Mungu umepelekwa kwa watu
Mataifa, nao watasikiliza." 29 Naye akiisha
kusema maneno haya, Wayahudi wakaondoka
wakiwa na hoja nyingi miongoni mwao.

30 Kwa miaka miwili mizima Paulo alikaa
huko kwenye nyumba yake mwenyewe
aliyokuwa amepanga. Akawakaribisha wote
waliokwenda kumwona. 31 Akihubiri Ufalme wa
Mungu na kufundisha mambo yale yaliyomhusu
Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri wote na bila
kizuizi cho chote.

## Warumi

### *Utangulizi*

Waraka huu Paulo aliwaandikia watakatifu huko Rumi. Huu ni mmoja wa nyaraka za kina sana katika Agano Jipya.

Kwa kuwa Paulo alikuwa amepanga kuzuru Rumi na kwenda mpaka Hispania *(15:24,28,32)*,akiwa amezuiliwa katika mipango yake ya awali *(1:13; 15:22)*, yawezekana aliandika waraka huu kwa kusudi la kujitambulisha kwa kanisa la Rumi kwa ajili ya maandalizi ya safari yake na pia ili kueleza kwa muhtasari msingi wa mafundisho yake.

Kwa sababu hii, waraka huu umepangwa vizuri kuliko nyaraka zake nyingine. Kwa njia hii anawahubiria Injili kama alivyo itambua. Anaanza kwa kueleza kwamba wanadamu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Kwa hiyo Wayahudi na hata watu Mataifa hawawezi kudai haki mbele za Mungu kwa sababu dhambi zao zinafuta haki hiyo. Lakini Mungu, kwa neema Yake, alituhesabia haki tuliyopoteza. Yeye alitupenda hata wakati tulipokuwa wenye dhambi *(5:8).* Kwa njia hii ya kuhesabiwa haki na Mungu katika Mwanawe, tunaweza kuwa washindi katika maisha ya Kikristo. Kisha Paulo anaeleza nafasi ya Wayahudi katika mpango wa Mungu *(9-11).* Anamalizia waraka wake kwa kutoa maonyo kadha wa kadha kuhusu maadili.

### *Wazo Kuu*

Haki aliyo nayo Mungu kuwahukumu wanadamu na mpango wa Mungu kuwapatia wanadamu haki ya wokovu inayopatikana bure kwa neema kwa njia ya imani, ambayo ndiyo kiini cha waraka huu. Mungu anadhihirishwa kuwa ni Mkuu, Mtakatifu na Mwenye haki, atawalaye ulimwengu wote na asiyeweza kulegeza amri Zake kwa sababu zinafuata asili Yake ya Kimungu. Lakini kwa kufuatana na sheria Yake, aliandaa mpango wa kuwaokoa Wayahudi pamoja na watu Mataifa. Ili kutimiza mpango Wake wa WOKOVU, alimtuma Mwanawe Yesu Kristo kutoka mbinguni, aje duniani kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Mtu ye yote anayemwamini Yesu ataokolewa *(10:9)* na kupewa uwezo wa kushinda dhambi maishani mwake. Hakuna kitu cho chote kiwezacho kumtenga Mungu na mtu anayemwamini Kristo na upendo wa Mungu*(8:38,39).*

### *Tarehe*

Paulo aliuandika waraka huu kama 57 B.K. wakati wa kumalizia safari yake ya tatu ya kueneza Injili alipokuwa anatazamia kuzuru Yerusalemu na hatimaye kwenda Rumi.

### *Mahali*

Korintho ambako alikaa miezi mitatu au Filipi*(Mdo.20:3 )*

### *Mgawanyo*

- Utangulizi (1:1-17)
- Watu wote hawana haki (1:18 – 3:20 )
- Haki ipatikanayo kwa kumwamini Kristo (3:21-5:21)
- Kushinda Dhambi kwa uwezo wa Kristo (6:1-8:39)
- Mpango wa Mungu kwa Israeli (9:1-11:36)
- Misingi ya Maisha ya Kikristo (12:1-15:13)
- Mawaidha ya Mwisho (15:14 -16:27).

**1** Paulo, mtumishi wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa
mtume na kutengwa kwa ajili ya Injili ya Mungu,
[2]Injili ambayo Mungu alitangulia
kuiahidi kwa vinywa vya manabii Wake katika
maandiko matakatifu, [3]yaani, Injili inayomhusu
Mwanawe, Yeye ambaye kwa uzao wa mwili
alikuwa mzao wa Daudi [4]na ambaye kwa uwezo
wa Roho wa utakatifu alidhihirishwa kuwa
Mwana wa Mungu kwa ufufuo Wake kutoka kwa
wafu, yaani, Yesu Kristo Bwana wetu. [5]Ambaye
kwa kupitia Kwake na kwa ajili ya Jina Lake,
tumepokea neema na utume ili kuwaita watu
miongoni mwa watu wote wasiomjua Mungu,
waje kwenye utii utokanao na imani. [6]Ninyi
nyote pia mko miongoni mwa watu walioitwa ili
mpate kuwa mali ya Kristo Yesu.

[7]Kwa wote walioko Rumi wapendwao na
Mungu na kuitwa kuwa watakatifu:

Neema na amani itokayo kwa Mungu Baba
yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Maombi Na Shukrani*

[8]Kwanza kabisa, namshukuru Mungu
wangu kwa njia ya Yesu Kristo kwa ajili yenu
nyote, kwa sababu imani yenu inatangazwa
duniani kote. [9]Kwa maana Mungu
ninayemtumikia kwa moyo wangu wote katika
kuhubiri Injili ya Mwanawe, ni shahidi Yangu
jinsi ninavyowakumbuka [10]katika maombi yangu
sikuzote, nami ninaomba kwamba hatimaye
sasa kwa mapenzi ya Mungu, njia ipate
kufunguliwa kwa ajili yangu ili nipate kuja
kwenu.

[11]Ninatamani sana kuwaona ili nipate
kuweka juu yenu karama za rohoni ili mwe
imara, [12]au zaidi, ninyi pamoja nami tuweze
kutiana moyo katika imani sisi kwa sisi. [13]
Ndugu zangu, napenda mfahamu kwamba mara
nyingi nimekusudia kuja kwenu, (ingawa mpaka
sasa nimezuiliwa), ili nipate kuvuna mavuno
miongoni mwenu kama nilivyovuna miongoni
mwa watu wengine wasiomjua Mungu.

[14]Mimi ni mdeni kwa Wayunani na wasio
Wayunani, kwa wenye hekima na wasio na
hekima. [15]Ndiyo sababu ninatamani sana
kuihubiri Injili kwenu pia ninyi mlioko Rumi.

[16]Mimi siionei haya Injili ya Kristo kwa
maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa
kila aaminiye, kwanza kwa Myahudi na kwa
Myunani pia. [17]Kwa maana katika Injili haki
itokayo kwa Mungu imedhihirishwa, haki ile iliyo
kwa njia ya imani hadi imani. Kama
ilivyoandikwa: "Mwenye haki ataishi kwa imani."

### *Ghadhabu Ya Mungu Kwa Wanadamu*

[18]Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa
kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa
wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu
wao, [19]kwa maana yote yanayoweza kujulikana
kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu
Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao.
[20]Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu,
asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani,
uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu,
umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana
na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na
udhuru.

[21]Kwa maana ingawa walimjua Mungu,
hawakumtukuza Yeye kama ndiye Mungu wala
hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili
na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza. [22]Ingawa
wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga
[23]na kubadili utukufu wa Mungu aishiye milele
kwa sanamu zilizofanywa zifanane na
mwanadamu ambaye hufa, ndege, wanyama na
viumbe vitambaavyo.

[24]Kwa hiyo, Mungu akawaacha wazifuate
tamaa mbaya za mioyo yao katika uasherati,
hata wakavunjiana heshima miili yao wao kwa
wao. [25]Kwa sababu waliibadili kweli ya Mungu
kuwa uongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe
badala ya Mwumba, ahimidiwaye milele! Amen.

[26]Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha
wavunjiane heshima kwa kufuata tamaa zao za
aibu. Hata wanawake wao wakabadili matumizi
ya asili ya miili yao wakaitumia isivyokusudiwa.
[27]Vivyo hivyo wanaume pia wakiacha matumizi
ya asili ya wanawake wakawakiana tamaa wao
kwa wao. Wanaume wakafanyiana matendo ya
aibu na wanaume wengine nao wakapata katika
maisha yao adhabu iliyowastahili kwa ajili ya
upotovu wao.

[28]Nao kwa kuwa walikataa kumkubali
Mungu, Yeye akawaacha wafuate akili zao za
upotovu, watende mambo yale yasiyostahili
kutendwa. [29] Wakiwa wamejawa na udhalimu
wa kila namna, uasherati, uovu, tamaa mbaya
na hila. Wamejawa na husuda, uuaji, ugomvi,
udanganyifu, hadaa na nia mbaya. Wao pia ni
wasengenyaji, [30]wasingiziaji, wanaomchukia
Mungu, wajeuri, wenye kiburi na majivuno,
wenye hila, wasiotii wazazi wao, [31]wajinga,

wasioamini, wasio na huruma na wakatili. 32Ingawa wanafahamu sheria ya haki ya Mungu kwamba watu wanaofanya mambo kama hayo wanastahili mauti, si kwamba wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia wanakubaliana na wale wanaoyatenda.

### *Hukumu Ya Mungu*

**2** Kwa hiyo huna udhuru wo wote, wewe mtu uwaye yote, utoaye hukumu kwa mwingine, kwa maana katika jambo lo lote unalowahukumu wengine, unajihukumu wewe mwenyewe kwa sababu wewe unayehukumu unafanya mambo yayo hayo. 2Basi tunajua kwamba hukumu ya Mungu dhidi ya wale wafanyao mambo kama hayo ni ya kweli. 3Hivyo wewe mwanadamu, utoapo hukumu juu yao na bado unafanya mambo yale yale, unadhani utaepuka hukumu ya Mungu? 4Au waudharau wingi wa wema, ustahimili na uvumilivu Wake, bila kujua kuwa wema wa Mungu wakuelekeza kwenye toba ?

5Lakini kwa sababu ya ukaidi wenu na mioyo yenu isiyotaka kutubu, unajiwekea akiba ya ghadhabu dhidi yenu wenyewe kwa siku ile ya ghadhabu ya Mungu, wakati hukumu Yake ya haki itakapodhihirishwa. 6Kwa maana Mungu atamlipa kila mtu sawasawa na matendo yake. 7Wale ambao kwa kuvumilia katika kutenda mema hutafuta utukufu, heshima na maisha yasiyoharibika, Mungu atawapa uzima wa milele. 8Lakini kwa wale watafutao mambo yao wenyewe na wale wanaokataa kweli na kuzifuata njia mbaya, kutakuwa na ghadhabu na hasira ya Mungu. 9Kutakuwa na taabu na dhiki kwa kila mmoja atendaye maovu, Myahudi kwanza na Myunani pia, 10bali utukufu, heshima na amani kwa ajili ya kila mmoja atendaye mema, kwa Myahudi kwanza, kisha kwa watu Mataifa. 11Kwa maana Mungu hana upendeleo.

12Watu wote waliotenda dhambi pasipo sheria wataangamia pasipo sheria, nao wote wale waliotenda dhambi chini ya sheria watahukumiwa kwa sheria. 13Kwa maana si wale wanaoisikia sheria ambao ni wenye haki mbele za Mungu, bali ni wale wanaoitii sheria ndio watakaohesabiwa haki. 14(Naam, wakati wa watu Mataifa, ambao hawana sheria, wanapofanya kwa asili mambo yatakiwayo na sheria, wao ni sheria kwa nafsi zao wenyewe, hata ingawa hawana sheria. 15 Wao wanaonyesha kwamba lile linalotakiwa na sheria limeandikwa kwenye mioyo yao, ambayo pia dhamiri zao zikiwashuhudia, nayo mawazo yao yenye kupingana yatawashtaki au kuwatetea). 16Hili litatukia siku hiyo Mungu atakapozihukumu siri za mioyo ya wanadamu kwa njia ya Yesu Kristo, kama isemavyo Injili yangu.

### *Wayahudi Na Torati*

17Tazama, wewe ukiwa unaitwa Myahudi na kuitegemea torati na kujisifia uhusiano wako na Mungu, 18kama unajua mapenzi ya Mungu na kukubali lililo bora kwa sababu umefundishwa na hiyo sheria, 19kama unatambua kuwa wewe ni kiongozi wa vipofu, na mwanga kwa wale walio gizani, 20mkufunzi wa wajinga na mwalimu wa watoto wachanga, kwa kuwa una maarifa ya kweli katika hiyo sheria, 21basi wewe, uwafundishaye wengine, mbona hujifunzi mwenyewe? Wewe uhubiriye kwamba mtu asiibe, wewe mwenyewe waiba? 22Wewe usemaye mtu asizini, wewe mwenyewe wazini? Wewe uchukiaye miungu ya sanamu, wafanya jambo la kumchukiza katika mahekalu? 23Wewe ujivuniaye sheria, wamwaibisha Mungu kwa kuvunja sheria? 24Kama ilivyoandikwa, ‘‘Kwa ajili yenu ninyi, Jina la Mungu linatukanwa miongoni mwa watu Mataifa.”

25Kutahiriwa kuna thamani ikiwa unatii sheria, lakini kama unavunja sheria, kutahiriwa kwako kumekuwa kutokutahiriwa. 26Hivyo, ikiwa wale wasiotahiriwa wanatimiza mambo ambayo sheria inataka, je, kutokutahiriwa kwao hakutahesabiwa kuwa sawa na kutahiriwa? 27Ndipo wale ambao kimwili hawakutahiriwa lakini wanaitii sheria watawahukumu ninyi Wayahudi, ambao mmetahiriwa na kuijua sana sheria ya Mungu lakini mwaivunja.

28 Kwa maana mtu si Myahudi kwa vile alivyo kwa nje, wala tohara ya kweli si kitu cha nje au cha kimwili. 29Lakini mtu ni Myahudi alivyo ndani na tohara ya kweli ni jambo la rohoni, ni la kiroho, wala si la kimwili. Mtu wa namna hiyo hapokei sifa kutoka kwa wanadamu bali kwa Mungu.

### *Uaminifu Wa Mungu*

**3** Basi kuna faida gani kuwa Myahudi? Au kuna thamani gani katika tohara? 2Kuna faida kubwa kwa kila njia maana wamekabidhiwa lile neno la Mungu hasa.

3Ingekuwaje kama wengine hawakuwa na

imani? Je, kutokuamini kwao kungebatilisha
uaminifu wa Mungu? 4La hasha! Mungu na
aonekane mwenye haki na kila mwanadamu
kuwa mwongo, kama ilivyoandikwa :

"Ili uweze kujulikana kuwa na haki katika
maneno yako,
nawe ukashinde katika hukumu."

5Ikiwa uovu wetu unathibitisha haki ya
Mungu waziwazi, tuseme nini basi? Je, Mungu
kuileta ghadhabu Yake juu yetu ni kwamba
Yeye si mwenye haki? (Nanena kibinadamu.)
6La hasha! Kama hivyo ndivyo ilivyo, Mungu
angehukumuje ulimwengu? 7Mtu aweza kuuliza,
"Kama uongo wangu unasaidia kuonyesha kweli
ya Mungu na kuzidisha utukufu Wake, kwa nini
basi mimi nahukumiwa kuwa mwenye dhambi?"
8Nasi kwa nini tusiseme, kama wengine
wanavyotusingizia kuwa tunasema, "Tutende
maovu ili mema yapate kuja?" Wao wanastahili
hukumu yao.

### *Wote Wametenda Dhambi*

9Tusemeje basi? Je, sisi ni bora kuliko wao?
La hasha! Kwa maana tumekwisha kuhakikisha
kwa vyo vyote kwamba Wayahudi na watu
Mataifa wote wako chini ya nguvu ya dhambi.
10Kama ilivyoandikwa:

"Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja.
11Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu,
hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu.
12Wote wamegeukia mbali,
wote kwa pamoja hawafai,
hakuna atendaye mema,
naam, hata mmoja."
13"Makoo yao ni makaburi wazi,
kwa ndimi zao hufanya udanganyifu."
Sumu ya nyoka iko midomoni mwao.
14"Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu."
15"Miguu yao ina haraka kumwaga damu,
16 maangamizi na taabu viko katika njia zao,
17wala njia ya amani hawaijui."
18 "Hakuna hofu ya Mungu machoni pao."

19Basi tunajua ya kwamba cho chote sheria
inachosema, inawaambia wale walio chini ya
sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na
ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu. 20Kwa
hiyo hakuna binadamu hata mmoja
atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa
matendo ya sheria, kwa maana sheria
hutufanya tuitambue dhambi.

### *Haki Kwa Njia Ya Imani*

21Lakini sasa, haki itokayo kwa Mungu
imedhihirishwa pasipo sheria, ambayo Torati na
Manabii wanaishuhudia. 22Haki hii itokayo kwa
Mungu hupatikana kwa Yesu Kristo kwa wote
wamwaminio. Kwa maana hapo hakuna tofauti,
23kwa kuwa wote wametenda dhambi na
kupungukiwa na utukufu wa Mungu,
24wanahesabiwa haki bure kwa neema Yake
kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.
25Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya
upatanisho kwa njia ya imani katika damu Yake.
Alifanya hivi ili kuonyesha haki Yake, kwa
sababu kwa ustahimili Wake aliziachilia zile
dhambi zilizotangulia kufanywa. 26Alifanya hivyo
ili kuonyesha haki Yake wakati huu, ili Yeye awe
mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule
anayemwamini Yesu.

### *Umuhimu Wa Kuwa Na Imani*

27Basi, kujivuna kuko wapi? Kumewekwa
mbali. Kwa sheria gani? Je, ni kwa ile ya
matendo? La hasha, bali kwa ile sheria ya
imani. 28Kwa maana twaona kwamba
mwanadamu huhesabiwa haki kwa njia ya imani
wala si kwa matendo ya sheria. 29 Je, Mungu ni
Mungu wa Wayahudi peke yao? Je, Yeye si
Mungu wa watu Mataifa pia? Naam, Yeye ni
Mungu wa watu Mataifa pia. 30Basi kwa kuwa
tuna Mungu mmoja tu, atawahesabia haki wale
waliotahiriwa kwa imani na wale wasiotahiriwa
kwa imani iyo hiyo. 31 Je, basi, ni kwamba
tunaibatilisha sheria kwa imani hii? La, hasha!
Badala yake tunaithibitisha sheria.

### *Abrahamu Ahesabiwa Haki Kwa Imani*

**4** Tuseme nini basi, kuhusu Abrahamu baba
yetu kwa jinsi ya mwili, yeye alipataje kujua jambo
hili ? 2Kwa maana ikiwa Abrahamu alihesabiwa
haki kwa matendo, basi, anacho kitu cha kujivunia,
lakini si mbele za Mungu. 3Kwa maana Maandiko
yasemaje? "Abrahamu alimwamini Mungu na
ikahesabiwa kwake
kuwa haki."

4Basi mtu afanyapo kazi, mshahara wake
hauhesabiwi kwake kuwa ni zawadi, bali ni haki
yake anayostahili. 5Lakini kwa mtu ambaye
hafanyi kazi na anamtumaini Mungu, Yeye
ambaye huwahesabia waovu haki, imani yake

inahesabiwa kuwa haki. 6 Daudi pia alisema
vivyo hivyo anenapo juu ya baraka za mtu
ambaye Mungu humhesabia haki pasipo
matendo:

7 “Wamebarikiwa wale ambao
uovu wao umesamehewa
na ambao dhambi zao zimefutwa.
8 Amebarikiwa mtu yule
ambaye Mungu hamhesabii dhambi zake.”

### *Haki Kabla Ya Tohara*

9 Je, huku kubarikiwa ni kwa wale
waliotahiriwa peke yao, au pia na kwa wale
wasiotahiriwa? Tunasema, “Imani ya Abrahamu
ilihesabiwa kwake kuwa haki.” 10 Je, ni lini basi
ilipohesabiwa kwake haki? Je, ilikuwa kabla au
baada ya kutahiriwa kwake? Haikuwa baada, ila
kabla hajatahiriwa. 11 Alipewa ishara ya tohara
kuwa muhuri wa haki aliyokuwa nayo kwa imani
hata alipokuwa bado hajatahiriwa. Kusudi
lilikuwa kumfanya baba wa wote wale waaminio
pasipo kutahiriwa na ambao wamehesabiwa
haki. 12 Vivyo hivyo awe baba wa wale
waliotahiriwa ambao si kwamba wametahiriwa
tu, bali pia wanafuata mfano wa imani ambayo
Baba yetu Abrahamu alikuwa nayo kabla ya
kutahiriwa.

### *Ahadi Ya Mungu Hufahamika Kwa Imani*

13 Kwa maana ile ahadi kwamba angeurithi
ulimwengu haikuja kwa Abrahamu au kwa
wazao wake kwa njia ya sheria bali kwa njia ya
haki ipatikanayo kwa imani. 14 Kwa maana ikiwa
wale waishio kwa sheria ndio warithi, imani
haina thamani na ahadi haifai kitu, 15 kwa
sababu sheria huleta ghadhabu. Mahali ambapo
hakuna sheria hakuna makosa.

16 Kwa hiyo, ahadi huja kwa njia ya imani, ili
iwe ni kwa neema na itolewe kwa wazao wa
Abrahamu, si kwa wale walio wa sheria peke
yao bali pia kwa wale walio wa imani ya
Abrahamu. Yeye ndiye baba yetu sisi sote.
17 Kama ilivyoandikwa: “Nimekufanya wewe
kuwa baba wa mataifa mengi.” Yeye ni baba
yetu mbele za Mungu ambaye alimwamini,
Mungu awapaye ahadi waliokufa na kuvitaja vile
vitu ambavyo haviko kana kwamba vimekwisha
kuwako.

### *Mfano Wa Imani Ya Abrahamu*

18 Akitarajia yasiyoweza kutarajiwa,
Abrahamu akaamini atakuwa, “Baba wa mataifa
mengi,” kama alivyoahidiwa kwamba, “Uzao
wako utakuwa mwingi mno.” 19 Abrahamu
hakuwa dhaifu katika imani hata alipofikiri juu ya
mwili wake, ambao ulikuwa kama uliokufa,
kwani umri wake ulikuwa unakaribia miaka mia
moja, au alipofikiiri juu ya ufu wa tumbo la Sara.
20 Lakini Abrahamu hakusitasita kwa
kutokuamini ahadi ya Mungu, bali alitiwa nguvu
katika imani yake na kumpa Mungu utukufu,
21 akiwa na hakika kabisa kwamba Mungu
alikuwa na uwezo wa kutimiza lile aliloahidi.
22 Hii ndio sababu, “ilihesabiwa kwake kuwa
haki.” 23 Maneno haya, “Ilihesabiwa kwake kuwa
haki,” hayakuandikwa kwa ajili yake peke yake,
24 bali kwa ajili yetu sisi pia, ambao Mungu
atatupa haki, kwa ajili yetu tunaomwamini Yeye
aliyemfufua Yesu Bwana wetu kutoka kwa wafu.
25 Alitolewa afe kwa ajili ya dhambi zetu, naye
alifufuka kwa ajili yetu ili tuhesabiwe haki.

### *Matokeo Ya Kuhesabiwa Haki*

**5** Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha
kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na
Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,
2 ambaye kwa kupitia Kwake tumepata kwa njia
ya imani kuifikia neema hii ambayo ndani yake
sasa tunasimama, nasi twafurahia katika
tumaini letu la kushiriki utukufu wa Mungu. 3 Si
hivyo tu, bali twafurahi pia katika mateso, kwa
sababu tunajua kuwa mateso huleta saburi,
4 nayo saburi huleta uthabiti wa moyo na uthabiti
wa moyo huleta tumaini, 5 wala tumaini
halitukatishi tamaa, kwa sababu Mungu
amekwisha kumimina pendo Lake mioyoni
mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye
ametupatia.

6 Kwa maana hata tulipokuwa dhaifu, wakati
ulipowadia, Kristo alikufa kwa ajili yetu sisi
wenye dhambi. 7 Hakika, ni vigumu mtu ye yote
kufa kwa ajili ya mwenye haki, ingawa
inawezekana mtu akathubutu kufa kwa ajili ya
mtu mwema. 8 Lakini Mungu anaudhihirisha
upendo Wake kwetu kwamba: Tulipokuwa
tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili
yetu.

9 Basi, kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki
kwa damu Yake, si zaidi sana tutaokolewa
kutoka katika ghadhabu ya Mungu kwa Yeye!
10 Kwa kuwa kama tulipokuwa adui wa Mungu
tulipatanishwa naye kwa njia ya kifo cha
Mwanawe, si zaidi sana tukiisha kupatanishwa,

tutaokolewa kwa uzima Wake. 11Lakini zaidi ya hayo, pia tunafurahi katika Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa kupitia Kwake tumepata upatanisho.

### *Adamu Alileta Kifo, Yesu Ameleta Uzima*

12Kwa hiyo kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja na kupitia dhambi hii, mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi. 13Kwa maana kabla sheria haijatolewa, dhambi ilikuwepo ulimwenguni. Lakini dhambi haihesabiwi wakati hakuna sheria. 14Hata hivyo, tangu wakati wa Adamu hadi wakati wa Mose, mauti ilitawala watu wote hata wale ambao hawakuvunja amri kama alivyofanya Adamu, ambaye alikuwa mfano wa yule atakayekuja.

15 Lakini ile karama iliyotolewa haikuwa kama lile kosa. Kwa maana ikiwa watu wengi walikufa kwa sababu ya kosa la mtu mmoja, zaidi sana neema ya Mungu na ile karama iliyokuja kwa neema ya mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo, imezidi kuwa nyingi kwa ajili ya wengi. 16Tena, ile karama ya Mungu si kama matokeo ya ile dhambi. Hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhabu, bali karama ya neema ya Mungu ilikuja kwa njia ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki. 17Kwa maana ikiwa kutokana na kosa la mtu mmoja, mauti ilitawala kupitia huyo mtu mmoja, zaidi sana wale wanaopokea wingi wa neema ya Mungu na karama Yake ya kuhesabiwa haki, watatawala katika uzima kwa njia ya huyo mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo.

18Kwa hiyo, kama vile kosa la mtu mmoja lilivyoleta hukumu kwa watu wote, vivyo hivyo pia kwa tendo la mtu mmoja la haki huleta kuhesabiwa haki kule kuletako uzima kwa wote. 19Kwa maana kama vile kwa kutokutii yule mtu mmoja wengi walifanywa wenye dhambi, vivyo hivyo kwa kutii kwa mtu mmoja wengi watafanywa wenye haki.

20Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi. 21Ili kwamba kama vile dhambi ilivyotawala kwa njia ya mauti, vivyo hivyo neema iweze kutawala kwa njia ya kuhesabiwa haki hata uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu.

### *Kufa Na Kufufuka Pamoja Na Kristo*

**6** Tuseme nini basi? Je, tuendelee kutenda dhambi ili neema ipate kuongezeka? 2La hasha! Sisi tuliyoifia dhambi, tutawezaje kuendelea kuishi tena katika dhambi? 3Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti Yake? 4Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti, ili kama vile Kristo alivyofufuka kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi nasi pia tupate kuenenda katika upya wa uzima.

5Kwa maana ikiwa tumeungana naye katika mauti Yake, bila shaka tutaungana naye katika ufufuo Wake. 6Kwa maana twajua kwamba utu wetu wa kale ulisulibiwa pamoja naye ili ule mwili wa dhambi upate kuangamizwa, nasi tusiendelee kuwa tena watumwa wa dhambi. 7Kwa maana mtu ye yote aliyekufa amewekwa huru mbali na dhambi.

8Basi ikiwa tulikufa pamoja na Kristo, tunaamini kwamba pia tutaishi pamoja naye. 9Kwa maana tunajua kwamba Kristo, akiisha kufufuka kutoka kwa wafu, hatakufa tena, mauti haina tena mamlaka juu Yake. 10Kifo alichokufa, aliifia dhambi mara moja tu, lakini uzima alio nao anamwishia Mungu.

11Vivyo hivyo, jihesabuni wafu katika dhambi lakini mlio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. 12 Kwa hiyo, msiruhusu dhambi itawale ndani ya miili yenu, ipatikanayo na kufa, ili kuwafanya mzitii tamaa mbaya. 13Wala msivitoe viungo vya miili yenu vitumike kama vyombo vya uovu vya kutenda dhambi, bali jitoeni kwa Mungu, kama watu waliotolewa kutoka mautini kuingia uzimani. Nanyi vitoeni viungo vya miili yenu Kwake kama vyombo vya haki. 14Kwa maana dhambi haitakuwa na mamlaka juu yenu, kwa sababu hampo chini ya sheria, bali chini ya neema.

### *Watumwa Wa Haki*

15Ni nini basi? Je, tutende dhambi kwa kuwa hatuko chini ya sheria bali chini ya neema? La, hasha! 16Je, hamjui kwamba mnapojitoa kwa mtu ye yote kama watumwa watiifu, ninyi ni watumwa wa yule mnayemtii, aidha watumwa wa dhambi, ambayo matokeo yake ni mauti, au wa utii ambao matokeo yake ni haki? 17Lakini Mungu ashukuriwe kwa kuwa ninyi ambao kwanza mlikuwa watumwa wa dhambi, mmekuwa watii kutoka moyoni kwa mafundisho mliyopewa, 18Nanyi, mkiisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mmekuwa watumwa wa haki.

19Ninasema kwa namna ya kibinadamu kwa

sababu ya mipaka yenu ya hali ya asili. Kama
vile kwanza mlivyokuwa mmevitoa viungo vya
miili yenu kama watumwa wa mambo machafu
na uovu uliokuwa ukiongezeka zaidi na zaidi,
hivyo sasa vitoeni viungo vya miili yenu vitumike
kwa ajili ya haki ambayo matokeo yake ni
utakatifu. 20Mlipokuwa watumwa wa dhambi,
mlikuwa hamtawaliwi na haki. 21Lakini mlipata
faida gani kwa mambo hayo ambayo sasa
mnayaonea aibu? Mwisho wa mambo hayo ni
mauti. 22Lakini sasa kwa kuwa mmewekwa huru
mbali na dhambi na mmekuwa watumwa wa
Mungu, faida mnayopata ni utakatifu, ambao
mwisho wake ni uzima wa milele. 23Kwa maana
mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya
Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu
Bwana wetu.

### *Hatufungwi Tena Na Sheria*

**7** Ndugu zangu, (sasa ninasema na wale
wanaoijua sheria.) Je, hamjui ya kwamba sheria
ina mamlaka tu juu ya mtu wakati akiwa hai?
2Kwa mfano, mwanamke aliyeolewa
amefungwa kwa mumewe wakati akiwa hai,
lakini yule mume akifa, yule mwanamke
amefunguliwa kutoka katika sheria ya ndoa.
3Hivyo basi, kama huyo mwanamke ataolewa
na mwanaume mwingine wakati mumewe akiwa
bado yuko hai, ataitwa mzinzi. Lakini kama
mumewe akifa, mwanamke huyo hafungwi tena
na sheria ya ndoa, naye akiolewa na mtu
mwingine haitwi mzinzi.

4Vivyo hivyo, ndugu zangu, ninyi mmeifia
sheria kwa njia ya mwili wa Kristo, ili mweze
kuwa mali ya mwingine, Yeye ambaye alifufuka
kutoka kwa wafu, ili kwamba tupate kuzaa
matunda kwa Mungu. 5Kwa maana tulipokuwa
tunatawaliwa na asili ya dhambi, tamaa za
dhambi zilizochochewa na sheria zilikuwa
zikitenda kazi katika miili yetu, hivyo tulizaa
matunda ya mauti. 6Lakini sasa, kwa kufia kile
kilichokuwa kimetufunga kwanza, tumewekwa
huru kutoka katika sheria ili tutumike katika njia
mpya ya Roho, wala si katika njia ya zamani ya
sheria iliyoandikwa.

### *Sheria Na Dhambi*

7Tuseme nini basi? Kwamba sheria ni
dhambi? La, hasha ! Lakini, ni kwa sababu ya
sheria nisingekuwa nimeijua dhambi.
Nisingekuwa nimejua kutamani ni nini kama
sheria haikusema, “Usitamani.” 8Lakini dhambi
kwa kupata nafasi katika amri, hii ikazaa ndani
yangu kila aina ya tamaa. Kwa maana pasipo
sheria, dhambi imekufa. 9Wakati fulani nilikuwa
hai pasipo sheria, lakini amri ilipokuja, dhambi
ikawa hai, nami nikafa. 10Nikaona kwamba ile
amri iliyokusudiwa kuleta uzima, ilileta mauti.
11Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi katika
amri, ilinidanganya na kwa kupitia hiyo amri,
ikaniua. 12 Hivyo basi, sheria yenyewe ni takatifu
na amri ni takatifu na ya haki, tena ni njema.

13Je, kile kilicho chema basi kilikuwa mauti
kwangu? La, hasha! Lakini ili dhambi itambuliwe
kuwa ni dhambi, ilileta mauti ndani yangu kupitia
kile kilichokuwa chema, ili kwa njia ya amri
dhambi izidi kuwa mbaya kupita kiasi.

### *Mgongano Wa Ndani*

14Kwa maana tunajua kwamba sheria ni ya
kiroho, lakini mimi ni wa kimwili nikiwa
nimeuzwa kwenye utumwa wa dhambi.
15Sielewi nitendalo, kwa maana lile ninalotaka
kulitenda, silitendi, lakini ninatenda lile
ninalolichukia. 16Basi kama ninatenda lile
nisilotaka kutenda, ni kwamba ninakubali kuwa
sheria ni njema. 17Lakini, kwa kweli si mimi tena
nitendaye lile nisilotaka bali ni ile dhambi ikaayo
ndani yangu. 18Kwa maana ninafahamu
kwamba hakuna jema lo lote likaalo ndani
yangu, yaani, katika asili yangu ya dhambi. Kwa
kuwa nina shauku ya kutenda lililo jema, lakini
siwezi kulitenda. 19Sitendi lile jema nitakalo
kutenda bali lile baya nisilolitaka, ndilo
nitendalo. 20Basi kama ninatenda lile nisilotaka
kutenda, si mimi tena nifanyaye hivyo, bali ni ile
dhambi ikaayo ndani yangu.

21Hivyo naiona sheria ikitenda kazi.
Ninapotaka kutenda jema, jambo baya liko papo
hapo. 22Kwa maana katika utu wangu wa ndani
naifurahia sheria ya Mungu. 23Lakini ninaona
kuna sheria nyingine inayotenda kazi katika
viungo vya mwili wangu inayopigana vita dhidi
ya ile sheria ya akili yangu.Sheria hii inanifanya
mateka wa ile sheria ya dhambi inayofanya kazi
katika viungo vya mwili wangu. 24Ole wangu,
mimi maskini! Ni nani atakayeniokoa na mwili
huu wa mauti? 25Ashukuriwe Mungu kwa njia ya
Yesu Kristo Bwana wetu!

Hivyo basi, mimi mwenyewe kwa akili zangu
ni mtumwa wa sheria ya Mungu, lakini katika asili
ya dhambi ni mtumwa wa sheria ya dhambi.

### *Maisha Katika Roho*

**8** Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya
adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu,
wale ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili
bali kwa kufuata Roho. 2Kwa sababu sheria
ya Roho wa uzima katika Kristo Yesu imeniweka
huru mbali na sheria ya dhambi na mauti. 3Kwa
maana kile ambacho sheria haikuwa na
uwezo wa kufanya, kwa vile ilivyokuwa
dhaifu katika mwili, Mungu kwa kumtuma
Mwanawe mwenyewe kwa mfano wa
mwanadamu mwenye mwili ulio wa dhambi na
kwa ajili ya dhambi, Yeye aliihukumu dhambi
katika mwili, 4ili kwamba haki ipatikanayo kwa
sheria itimizwe ndani yetu sisi, ambao
hatuenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuata
Roho.

5Kwa maana wale wanaoishi kwa kuufuata
mwili huziweka nia zao katika vitu vya mwili,
lakini wale wanaoishi kwa kufuata Roho,
huziweka nia zao katika mambo ya Roho. 6Kwa
maana kuwa na nia ya mwili ni mauti, bali kuwa
na nia inayoongozwa na Roho ni uzima na
amani. 7Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na
Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu,
wala haiwezi kuitii. 8Wale wanaotawaliwa na
mwili, hawawezi kumpendeza Mungu.

9Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na
Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani
yenu. Mtu ye yote ambaye hana Roho wa
Kristo, yeye si wa Kristo. 10Lakini kama Kristo
anakaa ndani yenu, miili yenu imekufa kwa
sababu ya dhambi, lakini roho zenu zi hai kwa
sababu ya haki. 11 Nanyi ikiwa Roho wa Mungu
aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu anakaa
ndani yenu, Yeye aliyemfufua Kristo Yesu
kutoka kwa wafu ataihuisha pia miili yenu
ambayo hufa, kwa njia ya Roho Wake akaaye
ndani yenu.

12Kwa hiyo ndugu zangu, sisi tu wadeni, si
wa mwili, ili tuishi kwa kuufuata mwili, 13kwa
maana mkiishi kwa kuufuata mwili, mtakufa,
lakini kama mkiyaua matendo ya mwili kwa
Roho, mtaishi. 14Kwa kuwa wote
wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ndio
watoto wa Mungu. 15Kwa maana hamkupokea
roho ya utumwa iwaleteayo tena hofu, bali
mlipokea roho ya kufanywa wana, ambaye kwa
Yeye twalia, ‘‘Abba,[a] yaani, Baba,’’ 16Roho
mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu ya
kwamba sisi tu watoto wa Mungu. 17Basi ikiwa
sisi ni watoto, basi tu warithi, warithi wa Mungu,
warithio pamoja na Kristo, naam, tukiteswa
pamoja Naye tupate pia kutukuzwa pamoja
Naye.

### *Utukufu Ujao*

18 Nayahesabu mateso yetu ya wakati huu
kuwa si kitu kulinganisha na utukufu
utakaodhihirishwa kwetu. 19Kwa maana viumbe
vyote vinangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa
watoto wa Mungu. 20Kwa kuwa viumbe vyote
viliwekwa chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali
kwa mapenzi Yake Yeye aliyevitiisha katika
tumaini, 21Ili kwamba viumbe vyote vipate
kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa
kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa
watoto wa Mungu.

22Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote
vimekuwa vikilia kwa uchungu kama utungu wa
wakati wa mwanamke kuzaa hata sasa. 23Wala
si hivyo viumbe peke yao, bali hata sisi ambao
ndio matunda ya kwanza ya Roho, kwa ndani
tunalia kwa uchungu tukisubiri kwa shauku
kufanywa wana wa Mungu, yaani, ukombozi wa
miili yetu. 24Kwa kuwa tuliokolewa kwa tumaini
hili. Lakini kama kinachotumainiwa kikionekana
hakiwi tumaini tena. Je, kuna mtu anayetumaini
kupata kitu alichonacho tayari? 25Lakini
tunapotumaini kupata kitu ambacho hatuna,
basi twakingojea kwa saburi.

26Vivyo hivyo, Roho hutusaidia katika
udhaifu wetu, kwa sababu hatujui kuomba
ipasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea
kwa uchungu kusikoweza kutamkwa. 27Naye
Mungu aichunguzaye mioyo, anaijua nia ya
Roho, kwa sababu Roho huwaombea
watakatifu sawasawa na mapenzi ya Mungu.

### *Tunashinda Na Zaidi Ya Kushinda*

28Nasi tunajua ya kuwa katika mambo yote
Mungu hutenda kazi pamoja na wote
wampendao, katika kuwapatia mema, yaani,
wale walioitwa kwa kusudi Lake. 29Maana wale
Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia
aliwachagua tangu mwanzo, wapate kufanana
na mfano wa Mwanawe, ili Yeye awe mzaliwa
wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. 30Nao
wale Mungu aliotangulia kuwachagua, akawaita,
wale aliowaita pia akawahesabia haki, nao wale
aliowahesabia haki, pia akawatukuza.

### *Upendo Wa Mungu*

[a]15 “Abba” ni neno la Kiaramu ambalo maana yake “Baba,” neno ambalo lingetumiwa na mtoto kwa yule aliyemzaa.

**31**Tuseme nini basi kuhusu haya? Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani awezaye kuwa kinyume chetu? **32**Ikiwa Mungu hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye? **33**Ni nani atakayewashtaki wale ambao Mungu amewachagua? Ni Mungu mwenyewe ndiye mwenye kuwahesabia haki. **34**Ni nani basi atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa, naam, zaidi ya hayo, ndiye aliyefufuka kutoka kwa wafu, yuko mkono wa kuume wa Mungu, naye ndiye anayetuombea. **35**Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je, ni shida au taabu au mateso au njaa au uchi au hatari au upanga? **36**Kama ilivyoandikwa :

‘‘Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa,
tumehesabiwa kama kondoo
wa kuchinjwa.’’

**37**Lakini katika mambo haya yote tunashinda, naam na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda. **38**Kwa maana nimekwisha kujua kwa hakika ya kuwa wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuja, wala wenye uwezo, **39**wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kingine cho chote kitakachoweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.

***Kuteuliwa Kwa Israeli Na Mungu.***

**9** Ninasema kweli katika Kristo, wala sisemi uongo, dhamiri yangu inanishuhudia katika Roho Mtakatifu. **2**Nina huzuni kuu na uchungu usiokoma moyoni mwangu. **3**Kwa maana ningetamani hata mimi nilaaniwe na kutengwa na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu hasa, wale walio wa kabila langu kwa jinsi ya mwili, **4**yaani, watu wa Israeli, ambao ndio wenye kule kufanywa wana, ule utukufu wa Mungu, yale maagano, kule kupokea sheria, ibada ya kwenye hekalu na zile ahadi. **5** Wao ni wa uzao wa mababa wakuu wa kwanza, ambao kutoka kwao Kristo alikuja kwa jinsi ya mwili kama mwanadamu,Yeye ambaye ni Mungu aliye juu ya vyote, mwenye kuhimidiwa milele! Amen.

**6** Si kwamba Neno la Mungu limeshindwa. Kwa maana si kila Mwisraeli ambaye ni wa uzao utokanao na Israeli ni Mwisraeli halisi. **7**Wala si tu kwamba kwa sababu wamezaliwa na wazao wa Abrahamu ni watoto wake, lakini ahadi ya Mungu kwa Abrahamu ilikuwa: “Watoto wako watahesabiwa katika uzao wa Isaki.’’ **8**Hii ina maana kwamba, si watoto waliozaliwa kimwili walio watoto wa Mungu, bali ni watoto wa ahadi wanaohesabiwa kuwa uzao wa Abrahamu. **9** Kwa maana ahadi yenyewe ilisema, “Nitakurudia tena wakati kama huu, naye Sara atapata mtoto wa kiume.’’

**10**Wala si hivyo tu, bali pia watoto aliowazaa Rebeka walikuwa na baba huyo huyo mmoja, yaani, baba yetu Isaki. **11**Lakini, hata kabla hao mapacha hawajazaliwa au kufanya jambo lo lote jema au baya, ili kwamba kusudi la Mungu la kuchagua lipate kusimama, **12**si kwa matendo, bali kwa Yeye mwenye kuita, Rebeka aliambiwa, “Mkubwa atamtumikia mdogo.’’ **13**Kama vile ilivyoandikwa, “Nimempenda Yakobo, lakini Esau nimemchukia.’’

***Mungu Hana Upendeleo***

**14**Tuseme nini basi? Je, Mungu ni dhalimu? La, hasha! **15**Kwa maana Mungu alimwambia Mose,

“Nitamrehemu yeye nimrehemuye,
nami nitamhurumia yeye
nimhurumiaye.’’

**16**Kwa hiyo haitegemei kutaka kwa mwanadamu au jitihada, bali hutegemea huruma ya Mungu. **17**Kwa maana Maandiko yamwambia Farao, “Nilikuinua kwa kusudi hili, ili kwamba nipate kuonyesha uweza Wangu juu yako na ili Jina Langu lipate kutangazwa duniani pote.’’

**18**Kwa hiyo basi, Mungu humhurumia yeye atakaye kumhurumia na humfanya mgumu Yeye atakayekumfanya mgumu.

**19**Basi mtaniambia, ‘‘Kama ni hivyo, kwa nini basi bado Mungu anatulaumu? Kwa maana ni nani awezaye kupinga mapenzi Yake?’’ **20**Lakini, Ewe mwanadamu, u nani wewe ushindane na Mungu? ‘‘Je, kilichoumbwa chaweza kumwambia yeye aliyekiumba, ‘Kwa nini umeniumba hivi?’ ’’ **21**Je, mfinyanzi hana haki ya kufinyanga kutoka katika bonge moja vyombo vya udongo vingine kwa matumizi ya heshima na vingine kwa matumizi ya kawaida?

**22**Iweje basi, kama Mungu kwa kutaka kuonyesha ghadhabu Yake na kufanya uweza Wake ujulikane, amevumilia kwa uvumilivu mwingi vile vyombo vya ghadhabu

vilivyoandaliwa kwa uharibifu? 23Iweje basi,
kama Yeye alitenda hivi ili kufanya wingi wa
utukufu Wake ujulikane kwa vile vyombo vya
rehema Yake, alivyotangulia kuvitengeneza kwa
ajili ya utukufu Wake, 24yaani pamoja na sisi,
ambao pia alituita, si kutoka kwa Wayahudi
peke yao, bali pia kutoka kwa watu Mataifa?

### *Yote Yalitabiriwa Katika Maandiko*

25Kama vile Mungu asemavyo katika
Hosea:

"Nitawaita 'watu Wangu' wale ambao si
watu Wangu,
nami nitamwita 'mpenzi Wangu' yeye
ambaye si mpenzi Wangu,"

26tena,
"Itakuwa hasa mahali
pale walipoambiwa,
'Ninyi si Watu wangu,'
wao wataitwa watoto wa Mungu aliye hai.' "

27Isaya anapiga kelele kuhusu Israeli:

"Ingawa idadi ya wana wa Israeli ni wengi
kama mchanga ulioko pwani ya bahari,
ni mabaki yao tu watakaookolewa.
28Kwa kuwa Bwana ataitekeleza
hukumu Yake duniani kwa haraka na kwa
ukamilifu."

29Ni kama vile alivyotabiri Isaya akisema:

"Kama Bwana wa majeshi[a]
asingetuachia uzao,
tungalikuwa kama Sodoma,
tungalikuwa kama Gomora."

### *Kutokuamini Kwa Israeli*

30Kwa hiyo tuseme nini basi? Kwamba watu
Mataifa ambao hawakutafuta haki, wamepata
haki ile iliyo kwa njia ya imani. 31Lakini Israeli,
ambao walijitahidi kupata haki kwa njia ya
sheria, hawakuipata. 32Kwa nini? Kwa sababu
hawakuitafuta kwa njia ya imani bali kwa njia ya
matendo. Wakajikwaa kwenye lile "jiwe la
kukwaza." 33Kama ilivyoandikwa,

"Tazama naweka katika Sayuni
jiwe la kukwaza
na mwamba wa kuwaangusha,
ye yote atakayemwamini hataaibika
kamwe."

**10** Ndugu zangu, shauku ya moyo wangu na
maombi yangu kwa Mungu ni kwa ajili ya
Waisraeli, kwamba waokolewe. 2Kwa
maana ninaweza nikashuhudia wazi kwamba
wao wanajuhudi kubwa kwa ajili ya Mungu,
lakini juhudi yao haina maarifa. 3 Kwa kuwa
hawakuijua haki itokayo kwa Mungu, wakatafuta
kuweka haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya
haki ya Mungu. 4Kwa maana Kristo ni ukomo
wa sheria ili kuwe na haki kwa kila mtu
aaminiye.

### *Wokovu Ni Kwa Ajili Ya Wote*

5Mose anaandika kuhusu haki ile itokanayo
na sheria, kwamba, "Mtu atendaye mambo
hayo ataishi kwa hayo." 6 Lakini ile haki
itokanayo na imani husema hivi : "Usiseme
moyoni mwako, 'Ni nani atakayepanda
mbinguni?' " (yaani, ili kumleta Kristo chini) 7"au
'Ni nani atashuka kwenda kuzimu?' " (yaani
kumleta Kristo kutoka kwa wafu.) 8Lakini andiko
lasemaje ? "Lile neno li karibu nawe, li kinywani
mwako na moyoni mwako," yaani, ni lile neno la
imani tunalolihubiri. 9Kwa sababu kama ukikiri
kwa kinywa chako kwamba "Yesu ni Bwana."
na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu
alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka. 10Kwa
maana kwa moyo mtu huamini na hivyo
kuhesabiwa haki, tena kwa kinywa mtu hukiri na
hivyo kupata wokovu. 11Kama yasemavyo
Maandiko, "Ye yote amwaminiye
hatatahayarika." 12 Kwa maana hakuna tofauti
kati ya Myahudi na Myunani, Yeye ni Bwana wa
wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao.
13Kwa maana, "Kila mtu atakayeliitia Jina la
Bwana, ataokoka."

14Lakini watamwitaje Yeye ambaye
hawajamwamini? Nao watawezaje kumwamini
Yeye ambaye hawajamsikia? Tena
watamsikiaje bila mtu kuwahubiria? 15Nao
watahubirije wasipopelekwa? Kama
ilivyyaoandikwa, "Ni mizuri mno miguu ya hao
wanaohubiri Injili ya amani na kuleta habari ya
mema!"

16Lakini si wote waliotii Habari Njema. Kwa
maana Isaya asema, "Bwana, ni nani aliyeamini

[a] 29 "Bwana wa majeshi hapa ni neno "Bwana wa Sabaothi" lililotafsiriwa kutoka kwenye lugha ya Kiebrania (pia Isa. 1:9 na Yakobo 5:4)

ujumbe wetu?'' 17Basi, imani chanzo chake ni
kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo.
18Lakini nauliza, Je, wao hawakusikia? Naam,
wamesikia, kwa maana :

''Sauti yao imeenea duniani kote,
nayo maneno yao yamefika hadi
miisho ya ulimwengu.''

19Nami nauliza tena, Je, Waisraeli
hawakuelewa?'' Kwanza, Mose asema,

''Nitawafanya mwe na wivu
kwa watu wale ambao si taifa.
Nitawakasirisha kwa taifa la watu
wasio na ufahamu.''

20Naye Isaya kwa ujasiri mwingi anasema,

''Watu wale waliokuwa hawanitafuti,
wamenipata,
nimejidhihirisha kwa watu wale
waliokuwa hawaniulizii.''

21Lakini kuhusu Israeli anasema,

"Mchana kutwa nimewanyoshea watu
wakaidi na wasiotii mikono Yangu.''

***Mabaki Ya Israeli***

**11** Basi nauliza, je, Mungu amewakataa
watu Wake? La, hasha! Mimi mwenyewe
ni Mwisraeli, tena uzao wa Abrahamu kutoka
kabila la Benyamini. 2Mungu hajawakataa watu
Wake, ambao Yeye aliwajua tangu mwanzo.
Je, hamjui yale maandiko yasemayo kuhusu
Eliya, jinsi alivyomlalamikia Mungu kuhusu
Israeli? 3Alisema, ''Bwana, wamewaua
manabii Wako na kuzibomoa madhabahu
Zako, nimebaki mimi peke yangu, nao wanataka
kuniua?'' 4Je, Mungu alimjibuje? ''Nimejibakizia
watu elfu saba ambao hawajapiga magoti
kumwabudu Baali.'' 5Vivyo hivyo pia, sasa wapo
mabaki waliochaguliwa kwa neema ya
Mungu. 6Lakini ikiwa wamechaguliwa kwa
neema, si tena kwa msingi wa matendo. Kama
ingekuwa kwa matendo,
neema isingekuwa neema tena.

7Tuseme nini basi? Kile kitu ambacho Israeli
alikitafuta kwa bidii hakukipata. Lakini
waliochaguliwa walikipata. Waliobaki walifanywa
wagumu, 8kama ilivyoandikwa:

"Mungu aliwapa bumbuazi la mioyo,
macho ili wasiweze kuona
na masikio ili wasiweze
kusikia, hadi leo.''

9Naye Daudi anasema:

"Karamu zao na ziwe tanzi na mtego
wa kuwanasa,
kitu cha kuwakwaza waanguke
na adhabu kwao.
10Macho yao yatiwe giza ili wasiweze kuona,
nayo migongo yao iinamishwe daima.''

***Matawi Yaliyopandikizwa***

11Hivyo nauliza tena, je, Waisraeli
walijikwaa ili waanguke na kuangamia kabisa?
La, hasha! Lakini kwa sababu ya makosa yao,
wokovu umewafikia watu Mataifa, ili kuwafanya
Waisraeli waone wivu. 12Basi ikiwa kujikwaa
kwao kumekuwa utajiri mkubwa kwa
ulimwengu, tena kama kuangamia kwao
kumeleta utajiri kwa watu Mataifa, kurudishwa
kwao kutaleta utajiri mkuu zaidi.

13Sasa ninasema nanyi watu Mataifa.
Maadam mimi ni mtume kwa watu Mataifa,
naitukuza huduma yangu 14ili kuwafanya watu
wangu waone wivu na hivyo kuwaokoa baadhi
yao. 15Kwa kuwa ikiwa kukataliwa kwao ni
kupatanishwa kwa ulimwengu, kukubaliwa kwao
si kutakuwa ni uhai baada ya kufa? 16Kama
sehemu ya donge la unga uliotolewa kuwa
limbuko ni mtakatifu, basi unga wote ni
mtakatifu, nalo shina kama ni takatifu, vivyo
hivyo na matawi nayo.

17 Lakini kama baadhi ya matawi yalikatwa,
nawe chipukizi la mzeituni mwitu ukapandikizwa
mahali pao ili kushiriki unono pamoja na matawi
mengine kutoka katika shina la mzeituni, 18 basi
usijivune juu ya hayo matawi. Kama ukijivuna,
kumbuka jambo hili. Si wewe unayelishikilia
shina, bali ni shina linalokushikilia wewe. 19Basi
utasema, ''Matawi yale yalikatwa ili nipate
kupandikizwa katika hilo shina.'' 20Hii ni kweli.
Matawi hayo yalikatwa kwa sababu ya
kutokuamini kwake, lakini wewe umesimama tu
kwa sababu ya imani. Kwa hiyo usijivune, bali
simama kwa kuogopa.21Kwa maana kama
Mungu hakuyahurumia matawi ya asili, wala
hatakuhurumia wewe.

22Angalia basi wema na ukali wa Mungu:

Kwa wale walioanguka, ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, kama utadumu katika wema Wake. La sivyo, nawe utakatiliwa mbali.
23Wao nao wasipodumu katika kutokuamini kwao, watapandikizwa tena kwenye shina, kwa maana Mungu anao uwezo wa kuwapandikiza tena kwenye hilo shina.
24 Ikiwa wewe ulikatwa kutoka katika kile ambacho kwa asili ni mzeituni mwitu na kupandikizwa kinyume cha asili kwenye mzeituni uliopandwa, si rahisi zaidi matawi haya ya asili kupandikizwa tena kwenye shina lake la mzeituni!

### *Israeli Wote Wataokolewa*

25Ndugu zangu, ili msije mkajidai kuwa wenye hekima kuliko mlivyo, nataka mfahamu siri hii: Ugumu umewapata Israeli kwa sehemu hadi idadi ya watu Mataifa watakaoingia itimie.
26Hivyo Israeli wote wataokolewa kama ilivyoandikwa:

"Mkombozi atakuja kutoka Sayuni,
ataondoa kutokumcha Mungu
katika Yakobo.
27Hili ndilo agano Langu
nao nitakapoziondoa dhambi zao."

28Kwa habari ya Injili, wao ni adui wa Mungu kwa ajili yenu, lakini kuhusu kule kuteuliwa kwao ni wapendwa, kwa ajili ya mababa zao wa zamani,
29 kwa maana akishawapa watu karama haziondoi, wala wito Wake.
30Kama vile ninyi wakati fulani mlivyokuwa waasi kwa Mungu lakini sasa mmepata rehema kwa sababu ya kutokutii kwao,
31hivyo nao Waisraeli wamekuwa waasi ili kwamba wao nao sasa waweze kupata rehema kwa ajili ya rehema za Mungu kwenu.
32Kwa maana Mungu amewafunga wanadamu wote kwenye kuasi ili apate kuwarehemu wote.

### *Wimbo Wa Shukrani*

33Tazama jinsi kilivyo kina cha utajiri wa hekima
na maarifa ya Mungu!
Tazama jinsi ambavyo hukumu Zake,
hazichunguziki na ambavyo njia Zake
zisivyotafutikana!
34"Ni nani aliyeijua nia ya Bwana?
Au ni nani ambaye amekuwa mshauri
Wake?"
35"Au ni nani aliyempa cho
chote ili arudishiwe?
36Kwa maana vitu vyote vyatoka Kwake,
viko Kwake na kwa ajili Yake.
Utukufu ni Wake milele. Amen.

### *Maisha Mapya Katika Kristo*

**12** Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana.
2Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni Pake na ukamilifu.
3Kwa ajili ya neema niliyopewa nawaambia kila mmoja miongoni mwenu, asijidhinie kuwa bora kuliko impasavyo, bali afikiri kwa busara kwa kulingana na kipimo cha imani Mungu aliyompa.
4Kama vile katika mwili mmoja tulivyo na viungo vingi, navyo viungo vyote havina kazi moja,
5vivyo hivyo na sisi tulio wengi, tu mwili mmoja katika Kristo, nasi kila mmoja ni kiungo cha mwenzake.
6Tuna karama zilizotofautiana kila mmoja kutokana na neema tuliyopewa. Kama ni unabii na tutoe unabii kwa kadiri ya imani.
7 Kama ni kuhudumu na tuhudumu, mwenye kufundisha na afundishe,
8kama ni kutia moyo na atie moyo, kama ni kuchangia kwa ajili ya mahitaji ya wengine na atoe kwa ukarimu, kama ni uongozi na aongoze kwa bidii, kama ni kuhurumia wengine na afanye hivyo kwa furaha.

### *Alama Za Mkristo Wa Kweli*

9Upendo lazima usiwe wa unafiki. Chukieni lililo ovu, shikamaneni na lililo jema.
10Pendaneni ninyi kwa ninyi kwa upendo wa kidugu. Waheshimuni na kuwatanguliza wengine.
11Msiwe wavivu, bali mwe na bidii katika roho mkimtumikia Bwana.
12Iweni na furaha katika tumaini, katika dhiki iweni na saburi, dumuni katika maombi.
13Changieni katika mahitaji ya watakatifu, wakaribisheni wageni.
14Wabarikini wale wanaowatesa, barikini wala msilaani.
15Furahini pamoja na wenye kufurahi, lieni pamoja na wale waliao.
16Kaeni kwa amani ninyi kwa ninyi. Msijivune, bali mwe tayari kushirikiana na wanyonge. Wala msiwe watu wenye kujivuna kwamba mnajua kila kitu.
17Msimlipe mtu ye yote ovu kwa ovu. Jitahidini ili mtende yaliyo mema machoni pa watu wote.
18Kama ikiwezekana, kwa upande

wenu kaeni kwa amani na watu wote.
19Wapendwa, msilipize kisasi, bali ipisheni
ghadhabu ya Mungu, maana imeandikwa:
"Kisasi ni juu Yangu, Mimi nitalipa, asema
Bwana." 20Badala yake:

"adui yako akiwa na njaa, mpe chakula,
akiwa na kiu, mnyweshe.
Maana ukifanya hivyo, utampalia makaa ya
moto yanayowaka kichwani pake.

21Usishindwe na ubaya, bali uushindeni ubaya
kwa wema.

### *Kutii Mamlaka*

**13** Kila mtu na atii mamlaka inayotawala, kwa
maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu,
nazo mamlaka zilizopo zimewekwa
na Mungu. 2Kwa hiyo yeye anayeasi dhidi ya
mamlaka inayotawala anaasi dhidi ya kile
kilichowekwa na Mungu, nao wale wafanyao
hivyo watajiletea hukumu juu yao wenyewe.
3Kwa kuwa watawala hawawatishi watu wale
wanaotenda mema bali wale wanaotenda
mabaya. Je, wataka usimwogope mwenye
mamlaka? Basi tenda lile lililo jema naye
atakusifu. 4Kwa maana mwenye mamlaka ni
mtumishi wa Mungu kwa ajili ya mema. Lakini
kama ukitenda mabaya, basi ogopa, kwa kuwa
hauinui upanga bila sababu. Yeye ni mtumishi
wa Mungu, mjumbe wa Mungu wa kutekeleza
adhabu juu ya watenda mabaya. 5Kwa hiyo ni
lazima kutii wenye mamlaka, si kwa sababu ya
kuogopa adhabu iwezayo kutolewa, bali pia kwa
ajili ya dhamiri.

6Kwa sababu hii mnalipa kodi, kwa maana
watawala ni watumishi wa Mungu, ambao
hutumia muda wao wote kutawala. 7Mlipeni kila
mtu kile mnachodaiwa. Kama mnadaiwa kodi
lipeni kodi, kama ni ushuru, lipeni ushuru,
astahiliye hofu, mhofu, astahiliye heshima,
mheshimu.

### *Kupendana Kila Mmoja Na Mwingine.*

8Msidaiwe kitu na mtu ye yote, isipokuwa
kupendana, kwa maana yeye ampendaye
mwenzake, ameitimiza sheria. 9Kwa kuwa amri
hizi zisemazo, "Usizini," "usiue," "usiibe,"
"usitamani" na amri nyingine zote, zinajumlishwa
katika amri hii moja: ''Mpende jirani yako kama
nafsi yako.'' 10 Upendo haumfanyii jirani jambo
baya. Kwa hiyo upendo
ndio utimilifu wa sheria.

11Nanyi fanyeni hivi, mkiuutambua wakati
tulio nao. Saa ya kuamka kutoka usingizini
imewadia, kwa maana sasa wokovu wetu
umekaribia zaidi kuliko hapo kwanza
tulipoamini. 12Usiku umeendelea sana,
mapambazuko yamekaribia. Kwa hiyo tuyaweke
kando matendo ya giza na tuvae silaha za nuru.
13Basi na tuenende kwa adabu kama
inavyopasa wakati wa mchana, si kwa kufanya
karamu za ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na
uasherati, si kwa ugomvi na wivu. 14Bali jivikeni
Bwana Yesu Kristo, wala msifikiri jinsi
mtakavyotimiza tamaa za miili yenu yenye asili
ya dhambi.

### *Msiwahukumu Wengine*

**14** Mkaribisheni yeye ambaye imani yake ni
dhaifu, lakini si kwa kugombana na kubishana
juu ya mawazo yake. 2Mtu mmoja imani yake
inamruhusu kula kila kitu, lakini mwingine
ambaye imani yake ni dhaifu, hula mboga tu.
3Yeye alaye kila kitu asimdharau yeye
asiyekula. Wala yeye asiyekula kila kitu
asimhukumu yule alaye kila kitu, kwa maana
Mungu amemkubali. 4Wewe ni nani hata
umhukumu mtumishi wa mtu mwingine? Kwa
bwana wake tu anasimama au kuanguka. Naye
atasimama kwa sababu Bwana anaweza
kumsimamisha.

5 Mtu mmoja anaitukuza siku fulani kuwa ni
bora kuliko nyingine na mwingine anaona kuwa
siku zote ni sawa. Basi kila mmoja awe na
hakika na yale anayoamini. 6Yeye anayehesabu
siku moja kuwa takatifu kuliko nyingine, hufanya
hivyo kwa kumheshimu Bwana. Naye alaye
nyama hula kwa Bwana, kwa maana
humshukuru Mungu, naye akataaye kula nyama
hufanya hivyo kwa Bwana na humshukuru
Mungu. 7 Kwa kuwa hakuna hata mmoja wetu
anayeishi kwa ajili yake mwenyewe, wala
hakuna hata mmoja wetu afaye kwa ajili yake
mwenyewe. 8Kama tunaishi, tunaishi kwa
Bwana, nasi pia tukifa twafa kwa Bwana. Kwa
hiyo basi, kama tukiishi au kama tukifa, sisi ni
mali ya Bwana.

9Kwani kwa sababu hii hasa, Kristo alikufa
na akawa hai tena kusudi apate kuwa Bwana
wa wote, yaani, waliokufa na walio hai. 10Basi
kwa nini wewe wamhukumu ndugu yako? Au
kwa nini wewe unamdharau ndugu yako? Kwa
kuwa sote tutasimama mbele ya kiti cha Mungu

cha hukumu. 11Kwa kuwa imeandikwa:

" 'Kama niishivyo,' asema Bwana,
'Kila goti litapigwa mbele Zangu
na kila ulimi utamkiri Mungu.' "

12Hivyo basi kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe kwa Mungu.

***Usimfanye Ndugu Yako Ajikwae***

13Kwa hiyo na tusiendelee kuhukumiana: Badala yake mtu asiweke kamwe kikwazo au
kizuizi katika njia ya mwingine. 14Ninajua tena nimehakikishiwa sana katika Bwana Yesu kwamba hakuna kitu cho chote ambacho ni najisi kwa asili yake. Lakini kama mtu anakiona kitu kuwa ni najisi, basi kwake huyo kitu hicho ni
najisi. 15Kama ndugu yako anahuzunishwa kwa sababu ya kile unachokula, basi huenendi tena katika upendo. Usiruhusu kile unachokula kiwe sababu ya kumwangamiza ndugu yako ambaye
Kristo alikufa kwa ajili yake. 16Usiruhusu kile ambacho unakiona kuwa chema kisemwe kuwa
ni kiovu. 17Kwa maana Ufalme wa Mungu si kula na kunywa, bali ni haki, amani na furaha
katika Roho Mtakatifu. 18Kwa sababu mtu ye yote anayemtumikia Kristo kwa jinsi hii, anampendeza Mungu na kukubaliwa na wanadamu.

19Kwa hiyo na tufanye bidii kutafuta yale yaletayo amani na kujengana sisi kwa sisi.
20Usiiharibu kazi ya Mungu kwa ajili ya chakula. Hakika vyakula vyote ni safi, lakini ni kosa kula kitu cho chote kinachomsababisha ndugu yako
ajikwae. 21Ni afadhali kutokula nyama wala kunywa divai au kufanya jambo lingine lo lote litakalomsababisha ndugu yako ajikwae.

22 Je, wewe unayo imani ? Ile imani uliyo nayo, uwe nayo nafsini mwako mbele za Mungu. Heri mtu yule asiye na sababu ya kujihukumu nafsi yake kwa ajili ya kile
anachokifanya. 23Lakini kama mtu ana shaka kuhusu kile anachokula, asile hicho kitu, kwa sababu hakula kwa imani. Kwa kuwa cho chote kinachofanywa pasipo imani ni dhambi.

***Usijipendeze Mwenyewe, Bali Wapendeze Wengine***

15 Sisi tulio na nguvu, hatuna budi kuchukuliana na kushindwa kwa wale walio dhaifu wala si kujipendeza nafsi zetu
wenyewe. 2Kila mmoja wetu inampasa kumpendeza jirani yake kwa mambo mema, ili
kumjenga katika imani. 3Kwa maana hata Kristo hakujipendeza mwenyewe, bali kama ilivyoandikwa: "Matukano yao wale
wanaokutukana wewe yalinipata mimi." 4Kwa maana kila kitu kilichoandikwa zamani, kiliandikwa kutufundisha, ili kwamba kwa saburi na faraja tunayopata katika Maandiko tuwe na tumaini.

5 Mungu atoaye saburi na faraja, awajalie ninyi roho ya umoja miongoni mwenu
mnapomfuata Kristo Yesu, 6ili kwa moyo mmoja mpate kumtukuza Mungu aliye Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.

***Injili Sawa Kwa Wayahudi Na Kwa watu Mataifa***

7Karibishaneni ninyi kwa ninyi kama Kristo alivyowakaribisha ninyi ili kumletea Mungu
utukufu. 8Kwa maana nawaambia kwamba, Kristo amekuwa mtumishi kwa wale waliotahiriwa ili kuonyesha kweli ya Mungu na kuthibitisha zile ahadi walizopewa baba zetu wa
zamani, 9pia ili watu Mataifa wamtukuze Mungu kwa rehema Zake. Kama ilivyoandikwa:

"Kwa hiyo nitakutukuza katikati ya
watu Mataifa,
nitaliimbia sifa Jina Lako."

10Tena yasema,

"Enyi watu Mataifa, furahini pamoja na watu
wa Mungu."

11Tena,

"Mhimidini Bwana, ninyi watu wote Mataifa
na kumwimbia sifa, enyi mataifa yote."

12Tena, Isaya anasema,

"Shina la Yese litachipuka,
Yeye atakayeinuka ili kutawala juu
ya mataifa,
watu Mataifa watamtumaini."

13Mungu wa tumaini awajaze ninyi furaha yote na amani katika kumwamini, ili mpate kujawa na tumaini tele kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

***Paulo Mhudumu Wa Watu Mataifa***

14Ndugu zangu, mimi mwenyewe ninasadiki

kwamba mmejaa wema, ufahamu wote, tena
mnaweza kufudishana ninyi kwa ninyi.
15Nimewaandikia kwa ujasiri vipengele kadha
wa kadha katika waraka huu kama
kuwakumbusha tena kwa habari ya ile neema
Mungu aliyonipa, 16ili kuwa mhudumu wa Kristo
Yesu kwa watu Mataifa nikiwa na huduma ya
kikuhani ya kutangaza Injili ya Mungu, ili watu
Mataifa wapate kuwa dhabihu inayokubaliwa na
Mungu, iliyotakaswa na Roho Mtakatifu.

17Kwa hiyo ninajisifu katika Kristo Yesu,
kwenye utumishi wangu kwa Mungu. 18Kwa
maana sitathubutu kusema kitu cho chote zaidi
ya kile ambacho Kristo amefanya kwa kunitumia
mimi katika kuwaongoza watu Mataifa wamtiii
Mungu kwa yale niliyosema na kufanya, 19 kwa
nguvu za ishara na miujiza, kwa uweza wa
Roho wa Mungu, ili kuanzia Yerusalemu hadi
maeneo yote ya kandokando yake, mpaka Iliriko
nimekwisha kuihubiri Injili ya Kristo kwa
ukamilifu. 20Hivyo ni nia yangu kuhubiri Habari
Njema, si pale ambapo Kristo amekwisha
kujulikana, ili nisije nikajenga juu ya msingi wa
mtu mwingine. 21Lakini kama ilivyoandikwa:

"Wale ambao hawajahubiriwa habari Zake
wataona,
nao wale ambao hawajazisikia
watafahamu.''

### *Paulo Apanga Kwenda Rumi*

22Hii ndiyo sababu nimezuiliwa mara nyingi
nisiweze kuja kwenu.

23Lakini sasa kwa kuwa hakuna nafasi zaidi
kwa ajili yangu katika sehemu hii, ninatamani
kuja kwenu kama ambavyo nimekuwa na
shauku kwa miaka mingi, 24nimekusudia
kufanya hivyo nitakapokuwa njiani kwenda
Hispania. Natarajia kuwaona katika safari yangu
na kusafirishwa nanyi mpaka huko, baada ya
kufurahia ushirika wenu kwa kitambo kidogo.
25Sasa, niko njiani kuelekea Yerusalemu kwa
ajili ya kuwahudumia watakatifu huko. 26Kwa
kuwa imewapendeza watu wa Makedonia na
Akaya kufanya changizo kwa ajili ya maskini
walioko miongoni mwa watakatifu huko
Yerusalemu. 27 Imewapendeza kufanya hivyo,
naam, kwani ni wadeni wao. Kwa maana ikiwa
watu Mataifa wameshiriki baraka za rohoni za
Wayahudi, wao ni wadeni wa Wayahudi, ili
Wayahudi nao washiriki baraka zao za mambo
ya mwilini. 28Kwa hiyo baada ya kukamilisha
kazi hii na kuhakikisha kuwa wamepokea kila
kitu kilichokusanywa, nitapitia kwenu nikiwa
njiani kwenda Hispania. 29Ninajua kwamba
nitakapokuja kwenu, nitakuja na wingi wa
baraka za Kristo.

30Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa Jina la
Bwana wetu Yesu Kristo na kwa upendo wa
Roho Mtakatifu, kujiunga nami katika taabu
zangu mkiniombea kwa Mungu. 31Ombeni ili
nipate kuokolewa mikononi mwa wale
wasioamini walioko Uyahudi na kwamba
utumishi wangu upate kukubaliwa na watakatifu
wa huko Yerusalemu, 32ili kwa mapenzi ya
Mungu niweze kuja kwenu kwa furaha, nami
niburudishwe pamoja nanyi. 33Mungu wa amani
na awe pamoja nanyi nyote. Amen.

### *Salamu Kwa Watu Binafsi*

**16** Napenda kumtambulisha kwenu dada yetu
Foibe, mtumishi katika kanisa la Kenkrea. 2Naomba
mpokeeni katika Bwana ipasavyo watakatifu na
kumpa msaada wo wote atakaohitaji kutoka kwenu,
kwa maana yeye amekuwa msaada kwa watu
wengi, mimi nikiwa
miongoni mwao.

3Wasalimuni Prisila[a] na Akila, watumishi
wenzangu katika Kristo Yesu. 4Wao
walihatirisha maisha yao kwa ajili yangu
wala si mimi tu ninayewashukuru bali pia
makanisa yote ya watu Mataifa.
5Lisalimuni pia kanisa linalokutana nyumbani
mwao.
Msalimuni rafiki yangu Epaineto, aliyekuwa mtu
wa kwanza kumwamini Kristo huko Asia.

6Msalimuni Maria, aliyefanya kazi kwa bidii kwa
ajili yenu.
7Wasalimuni Androniko na Yunia, jamaa zangu
ambao wamekuwa gerezani pamoja nami.
Wao ni maarufu miongoni mwa mitume,
nao walimjua Kristo kabla yangu.
8Msalimuni Ampliato, yeye nimpendaye katika
Bwana.
9Msalimuni Urbano, mtenda kazi mwenzetu
katika Kristo, pamoja na rafiki yangu
mpendwa Stakisi.
10Msalimuni Apele aliyejaribiwa na akaithibitisha
imani yake katika Kristo. Wasalimuni wote
walio nyumbani mwa Aristobulo.

---

a3 Prisila ni jina ambalo kwa Kiyunani ni Priska.Hivyo
tafsiri nyingine zimemwita Priska.

11Msalimuni ndugu yangu Herodioni na wote walio nyumbani mwa Narkisi walio katika Bwana.
12Wasalimuni Trifaina na Trifosa, wale wanawake wanaofanya kazi kwa bidii katika Bwana.
Msalimuni rafiki yangu mpendwa Persisi, mwanamke mwingine aliyefanya kazi kwa bidii katika Bwana.
13Msalimuni Rufo, mteule katika Bwana pamoja na mama yake, ambaye amekuwa mama kwangu pia.
14Wasalimuni Asinkrito, Flegoni, Herme, Patroba, Herma na ndugu wote walio pamoja nao.
15Wasalimuni Filologo, Yulia, Nerea na dada yake, Olimpa na watakatifu wote walio pamoja nao.
16Salimianeni ninyi kwa ninyi kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yanawasalimu.

letao matengano na kuweka vikwazo mbele yenu
dhidi ya mafundisho mliyojifunza. 18Kwa maana
watu kama hao hawamtumikii Bwana Kristo, bali wanatumikia tamaa zao wenyewe. Kwa kutumia mi nimejawa na furaha tele kwa ajili yenu. Lakini nataka mwe na hekima katika mambo mema na bila hatia katika mambo maovu.

20Mungu wa amani atamponda Shetani chini ya miguu yenu upesi.

Neema ya Bwana wetu Yesu iwe pamoja nanyi. Amen.

21Timotheo, mtenda kazi mwenzangu anawasalimu. Vivyo hivyo Lukio, Yasoni, Sosipatro na ndugu zangu.

22Mimi, Tertio, niliyemwandishi wa waraka huu nawasalimu katika Bwana.

23Gayo, ambaye ni mwenyeji wangu na wa kanisa lote anawasalimu.

Erasto, mweka hazina wa mji huu, pamoja na Kwarto ndugu yetu pia wanawasalimu.

24Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe pamoja nanyi nyote. Amen.

### *Maneno Ya Mwisho Ya Kumsifu Mungu*

25Sasa atukuzwe Yeye awezaye kuwafanya
ninyi imara kwa Injili yangu na kuhubiriwa kwa Yesu
Kristo, kutokana na kufunuliwa siri zilizofichika tangu
zamani za kale.
26Lakini siri ambayo sasa
imefunuliwa na kujulikana kupitia maandiko ya
kinabii kutokana na amri ya Mungu wa milele, ili
mataifa yote yaweze kumwamini na kumtii
27Mungu
aliye pekee mwenye hekima, ambaye kwa njia ya
Yesu Kristo utukufu una Yeye milele na milele. Amen.

# 1Wakorinto

### *Utangulizi*

Wakati wa huduma ya Paulo ya muda mrefu huko Efeso, Paulo alituma waraka huu kama itikio la habari alizopata kutoka vyanzo mbalimbali kuhusu hali iliyokuwa inaendelea katika kanisa la Korintho na pia kama kujibu barua ya kutoka katika kanisa hilo iliyokuwa inaomba ushauri.

Korintho ulikuwa mji uliojengwa pwani ya Bahari ya Mediterania. Huu mji ulikuwa umejengwa kando ya bahari na ulineemeka kwa kuwa na ukiritimba wa biashara. Kama kituo kikuu cha biashara cha wakati huo ulitajirika sana.Nyakati za Paulo ulikuwa koloni la Kirumi, ukiwavutia wakazi wa mataifa mbalimbali, wakiwemo Warumi, Wayunani na Wayahudi kutoka sehemu zinazoizunguka Bahari ya Mediterania. Mchanganyiko huu wa wakazi ulisababisha kuharibika na kumomonyoka kwa hali ya maadili. Hali hii iliwashangaza hata wapagani. Kutokana na hali kama hii si ajabu kwamba hata kanisa la Korintho lilikabiliwa na matatizo mengi.

Paulo alikuwa ameanzisha kanisa katika mji wa Korintho huko Uyunani katika safari yake ya pili ya kitume, yamkini ilikuwa wakati wa majira ya kipupwe mwaka 50 B.K. *(Mdo.18:11)* na kukaa huko kwa muda wa mwaka mmoja na nusu.Ni katika wakati huu ndipo alipoanzisha kanisa hili. Aliondoka Korintho huenda majira ya vuli ya 52 B.K., akifuatana na Prisila na Akila kwenda Efeso na kutoka huko alikwenda Palestina *(Mdo.18:22)*. Lakini mambo yalikuwa mabaya sana baada ya yeye kuondoka. Aliona ni muhimu awaandikie kuhusu matatizo mengi yaliyojitokeza kama haya yafuatayo: Walikataa kuwa yeye si mtume, walishiriki Meza ya Bwana isivyostahili, walibishana juu ya kula nyama zilizotolewa kafara kwa sanamu, walikuwa wakishtakiana mahakamani, walishiriki maisha ya uasherati, walikataa ukweli kuhusu ufufuo, walibishana juu ya ndoa na mengine mengi. Paulo aliona ana wajibu wa kushughulikia hali hiyo ili kanisa la Korintho lisije likaporomoka. Anaposhughulikia matatizo haya moja moja, Paulo anafafanua misingi ya mafundisho ya Kikristo juu ya imani.

### *Wazo Kuu*

Katika barua hii, kusudi kubwa la Paulo lilikuwa ni kusahihisha makosa dhahiri yaliyokuwamo katika kanisa la Korintho. Alionyesha umuhimu wa kuishi kama iwapasavyo watu wanaomwamini Kristo. Haitoshi kusema kwamba mtu ni mkristo tu, bali ni lazima mwenendo wa mkristo ufanane na ule wa Kristo. Kutokufanya hivyo ni kumwaibisha Kristo na kanisa Lake. Paulo pia anasisitiza kwamba Kristo anatosheleza haja zote za wale wanaomwamini. Mtu akiwa ndani ya Kristo anakuwa kiumbe kipya na anafanywa kuwa safi, yaani, mtakatifu.

### *Mwandishi*

Mwandishi ni Paulo.

### *Tarehe*

Waraka huu umeandikwa 55 B.K.

### *Mgawanyo:*

- Salamu za Paulo (*1:1-9*)
- Tatizo la mgawanyiko katika kanisa (*1:10 – 4:21*)
- Tatizo la zinaa katika kanisa (*5:1-13*)
- Tatizo la kushtakiana mahakamani (*6:1-11*)
- Tatizo la uasherati (*6:12-20*)
- Tatizo juu ya ndoa (*7:1-40*)
- Matatizo kuhusu ibada ya sanamu (*8:1-11:1*)
- Matatizo katika ibada (*11:2-14:40*)
- Matatizo kuhusu ufufuo wa wafu (*15:1-58*)
- Mawaidha ya mwisho (*16:1-24*)

### Salamu

**1** Paulo, aliyeitwa kwa mapenzi ya Mungu kuwa
mtume wa Yesu Kristo na Sosthene
ndugu yetu,

2 Kwa Kanisa la Mungu lililoko Korintho,
kwa wale waliotakaswa katika Kristo Yesu,
walioitwa kuwa watakatifu, pamoja na wale wote
ambao kila mahali wanaliitia Jina la Kristo Yesu
Bwana wetu, aliye Bwana wao na wetu pia:

3Neema na amani itokayo kwa Mungu Baba
yetu na kwa Bwana Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Shukrani*

4 Ninamshukuru Mungu sikuzote kwa ajili
yenu kwa sababu ya neema Yake mlioyopewa
katika Kristo Yesu. 5Kwa kuwa katika Kristo
mmetajirishwa kwa kila hali, katika kusema
kwenu na katika maarifa yenu yote, 6kwa
sababu ushuhuda wetu kumhusu Yesu
ulithibitishwa ndani yenu. 7Kwa hiyo
hamkupungukiwa na karama yo yote ya kiroho
wakati mnangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa
Bwana wetu Yesu Kristo. 8Yeye atawafanya
imara mpaka mwisho, ili msiwe na hatia siku ile
ya Bwana wetu Yesu Kristo. 9Mungu ni
mwaminifu ambaye mmeitwa naye ili mwe na
ushirika na Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu.

### *Mgawanyiko Ndani Ya Kanisa*

10Nawasihi ndugu zangu, katika Jina la
Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba mpatane nia
zenu ninyi kwa ninyi, ili pasiwepo na matengano
katikati yenu na kwamba mwe na umoja
kikamilifu katika nia na katika kusudi. 11Kwa
maana ndugu zangu, nimepata habari kutoka
kwa baadhi ya watu wa nyumbani mwa Kloe
kwamba kuna magomvi katikati yenu. 12Maana
yangu ni kwamba: Kila mmoja wenu husema,
“Mimi ni wa Paulo,” mwingine, “Mimi ni wa
Apolo,” mwingine “Mimi ni wa Kefa” na
mwingine “Mimi ni wa Kristo”.

13Je, Kristo amegawanyika? Je, Paulo
ndiye aliyesulibishwa kwa ajili yenu? Je,
mlibatizwa kwa jina la Paulo? 14Namshukuru
Mungu kwamba sikumbatiza mtu ye yote
miongoni mwenu isipokuwa Krispo na Gayo. 15
Kwa hiyo hakuna mtu ye yote miongoni mwenu
anayeweza kusema kwamba alibatizwa kwa jina
langu. 16 (Naam, niliwabatiza pia watu wa
nyumbani mwa Stefana. Lakini zaidi ya hao sijui
kama nilimbatiza mtu mwingine ye yote.) 17Kwa
maana Kristo hakunituma ili kubatiza bali
kuhubiri Injili na nifanye hivyo si kwa kutumia
maneno ya hekima ya kibinadamu ya
kushawishi, ili msalaba wa Kristo usije ukakosa
nguvu yake.

### *Kristo Hekima Na Nguvu Ya Mungu*

18Kwa maana ujumbe wa msalaba kwa wale
wanaopotea ni upuzi, lakini kwetu sisi
tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. 19Kwa maana
imeandikwa:

> “Nitaiharibu hekima ya wenye hekima na
> kuzibatilisha akili za wenye akili.”

20Yuko wapi mwenye hekima? Yuko wapi
msomi? Yuko wapi mwanafalsafa wa nyakati
hizi? Je, Mungu hakufanya hekima ya
ulimwengu huu kuwa umpumbavu? 21Kwa kuwa
katika hekima ya Mungu, ulimwengu kwa
hekima yake haukumjua Yeye, ilimpendeza
Mungu kuwaokoa wale waaminio kwa upuzi wa
lile neno lililohubiriwa. 22Wayahudi wanataka
miujiza na Wayunani wanatafuta hekima,
23lakini sisi tunamhubiri Kristo aliyesulibiwa,
ambaye kwa Wayahudi ni kitu cha kukwaza na
kwa Wayunani ni upuzi. 24Lakini kwa wale
ambao Mungu amewaita, yaani, Wayahudi na
Wayunani, Kristo ni nguvu na hekima ya
Mungu. 25Kwa maana upumbavu wa Mungu
una hekima zaidi kuliko hekima ya wanadamu,
nao udhaifu wa Mungu una nguvu kuliko nguvu
ya wanadamu.

26Ndugu zangu, kumbukeni mlivyokuwa
mlipoitwa. Kwa kipimo cha kibinadamu, si wengi
wenu mliokuwa na hekima. Si wengi waliokuwa
na nguvu, si wengi waliozaliwa katika jamaa
zenye vyeo. 27Lakini Mungu alichagua vitu
vipumbavu vya ulimwenguni ili aviaibishe
vyenye hekima, Mungu alichagua vitu dhaifu
vya ulimwengu ili aviaibishe vyenye nguvu.
28Alivichagua vitu vya chini na
vinavyodharauliwa vya dunia hii, vitu ambavyo
haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko, 29ili mtu ye
yote asijisifu mbele za Mungu. 30Mungu ndiye
chanzo cha uzima wenu katika Kristo Yesu,
aliyefanyika kwetu hekima itokayo kwa Mungu
na haki na utakaso na ukombozi, 31ili kama
ilivyoandikwa: “Yeye ajisifuye na ajisifu katika
Bwana.”

### *Kumtangaza Kristo Aliyesulibiwa*

**2** Ndugu zangu nilipokuja kwenu, sikuja na maneno ya ushawishi wala hekima ya hali ya juu nilipowahubiria siri za Mungu. 2Kwa kuwa niliamua kutokujua kitu cho chote wakati nikiwa nanyi isipokuwa Yesu Kristo, naye amesulibiwa msalabani. 3 Mimi nilikuja kwenu nikiwa dhaifu na mwenye hofu na kwa kutetemeka sana. 4Kuhubiri kwangu na ujumbe wangu haukuwa na hekima na maneno ya kuwashawishi watu, bali kwa madhihirisho ya nguvu za Roho Mtakatifu 5ili imani yenu isiwe imejengwa katika hekima ya wanadamu bali katika nguvu za Mungu.

### *Hekima Ya Kweli Itokayo Kwa Mungu*

6Lakini miongoni mwa watu waliokomaa twanena hekima, wala si hekima ya ulimwengu huu au ya watawala wa dunia hii wanaobatilika. 7Sisi tunanena hekima ya Mungu ambayo ni siri, tena iliyofichika kwa wanadamu, ambayo Mungu aliikusudia kabla ulimwengu kuwepo, kwa ajili ya utukufu wetu. 8Hakuna hata mtawala mmoja wa nyakati zetu aliyeelewa jambo hili. Kwa maana kama wangelielewa, wasingemsulibisha Bwana wa utukufu. 9Lakini ni kama ilivyoandikwa:

“Lile jambo ambalo jicho halijapata kuona,
sikio halijapata kusikia,
wala halikuingia moyoni
lile Mungu alilowaandalia wale
wampendao.”

10Lakini mambo haya Mungu ametufunulia kwa njia ya Roho Wake.

Roho huchunguza kila kitu, hata mambo ya ndani sana ya Mungu. 11 Kwa maana ni nani anayejua mawazo ya mtu isipokuwa roho iliyo ndani ya huyo mtu? Vivyo hivyo hakuna mtu ajuaye mawazo ya Mungu isipokuwa Roho wa Mungu. 12Basi hatukupokea roho ya dunia bali Roho yule atokaye kwa Mungu, ili tuweze kuelewa kile kipawa ambacho Mungu ametupatia bure. 13Haya ndiyo tusemayo, si kwa maneno tuliyofundishwa kwa hekima ya wanadamu bali kwa maneno tuliyofundishwa na Roho, tukifafanua kweli za kiroho kwa wale watu wa kiroho. 14Mtu ambaye hana Roho wa Mungu hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa jinsi ya rohoni. 15Mtu wa kiroho hutambua mambo yote, lakini yeye mwenyewe hatambuliwi na mtu ye yote.

16“Kwa maana ni nani aliyejua nia ya
Bwana ili apate kumfundisha?”

Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.

### *Kuhusu Mgawanyiko Katika Kanisa.*

**3** Ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama watu wa kiroho, bali kama watu wa mwilini, kama watoto wachanga katika Kristo. 2Naliwanywesha maziwa, wala si chakula kigumu, kwa kuwa hamkuwa tayari kwa hicho chakula kigumu. Naam, hata sasa hamkiwezi. 3Kwa maana ninyi bado ni watu wa mwilini. Kwa kuwa bado kuna wivu na magombano miongoni mwenu, je, ninyi si watu wa mwilini, nanyi mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu? 4Kwa maana mmoja anaposema, “Mimi ni wa Paulo,” mwingine, “Mimi ni wa Apolo”, je, ninyi si wanadamu wa kawaida?

5Kwani, Apolo ni nani? Naye Paulo ni nani? Ni watumishi tu ambao kwa kupitia wao mliamini. 6Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye aliyekuza. 7Hivyo mwenye kupanda mbegu na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke Yake ndiye akuzaye. 8Apandaye mbegu ni sawa na yule atiaye maji. Kila mmoja atalipwa kulingana na kazi yake. 9Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu, ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu.

10Kwa neema Mungu aliyonipa, niliweka msingi kama mjenzi stadi na mtu mwingine anajenga juu ya huo msingi. Lakini kila mmoja inampasa awe mwangalifu jinsi anavyojenga juu yake. 11 Kwa maana hakuna mtu ye yote awezaye kuweka msingi mwingine wo wote isipokuwa ule uliokwisha kuwekwa, ambao ni Yesu Kristo. 12Kama mtu ye yote akijenga juu ya msingi huu kwa kutumia dhahabu, fedha, mawe ya thamani, miti, majani au nyasi, 13 kazi yake itaonekana kuwa ikoje, kwa kuwa siku ile itaidhihirisha kazi yake. Itadhihirishwa kwa moto, nao moto utapima ubora wa kazi ya kila mtu. 14Kama kile alichojenga kitabaki, atapokea thawabu. 15Kama kazi ya mtu itateketea, atapata hasara, ila yeye mwenyewe ataokolewa, lakini kama mtu aliyenusurika kwenye moto.

16Je, hamjui ya kwamba ninyi ni hekalu la Mungu na kwamba Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? 17Kama mtu ye yote akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamwangamiza mtu huyo, Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu,

ambalo ndilo ninyi.

18Msijidanganye. Kama mtu ye yote miongoni mwenu akidhani kuwa ana hekima kwa viwango vya dunia hii, inampasa awe mjinga ili apate kuwa na hekima. 19Kwa maana hekima ya ulimwengu huu ni upuzi mbele za Mungu. Kama ilivyoandikwa: “Mungu huwanasa wenye hekima katika hila yao,” 20Tena, “Bwana anajua kwamba mawazo ya wenye hekima ni ubatili.” 21Hivyo basi, mtu asijivune kuhusu wanadamu! Kwa kuwa vitu vyote ni vyenu, 22ikiwa ni Paulo au Apolo au Kefa au dunia au uzima au mauti, au wakati uliopo au wakati ujao, haya yote ni yenu 23na ninyi ni wa Kristo, naye Kristo ni wa Mungu.

### *Mawakili Wa Siri Za Mungu*

**4** Basi, watu na watuhesabu sisi kuwa tu watumishi wa Kristo na mawakili wa siri za Mungu. 2Zaidi ya hayo, litakiwalo ni mawakili waonekane kuwa waaminifu. 3Lakini kwangu mimi ni jambo dogo sana kwamba nihukumiwe na ninyi au na mahakama yo yote ya kibinadamu. Hata mimi mwenyewe sijihukumu. 4Dhamiri yangu ni safi, lakini hilo halinifanyi nisiwe na hatia. Bwana ndiye anihukumuye. 5Kwa hiyo msihukumu jambo lo lote kabla ya wakati wake, ngojeni mpaka Bwana atakapokuja. Yeye atayaleta nuruni mambo yale yaliyofichwa gizani na kuweka wazi nia za mioyo ya wanadamu. Wakati huo kila mmoja atapokea sifa anayostahili kutoka kwa Mungu.

6Basi ndugu zangu, mambo haya nimeyafanya kuwa mfano wa mimi binafsi na Apolo kwa faida yenu, ili mweze kujifunza kutoka kwetu maana ya ule usemi usemao, “Msivuke zaidi ya yale yaliyoandikwa.” Hivyo hamtajivunia mtu fulani na kumdharau mwingine. 7 Kwa maana ni nani aliyekufanya wewe kuwa tofauti na mwingine? Ni nini ulicho nacho ambacho hukupokea? Nawe kama ulipokea, kwa nini unajivuna kama vile hukupokea?

8Sasa tayari mnayo yale yote mnayohitaji! Tayari mmekwisha kuwa matajiri! Mmekuwa wafalme, tena bila sisi! Laiti mngekuwa wafalme kweli ili na sisi tupate kuwa wafalme pamoja nanyi! 9Kwa maana ninaona kwamba Mungu ametuweka sisi mitume katika nafasi ya mwisho kabisa, kama watu waliohukumiwa kufa, kwa sababu tumefanywa kuwa maonyesho kwa ulimwengu wote, kwa malaika na kwa wanadamu pia. 10Kwa ajili ya Kristo sisi ni wajinga, lakini ninyi mna hekima ndani ya Kristo. Sisi tu dhaifu, lakini ninyi mna nguvu. Tunadharauliwa, lakini ninyi mnaheshimiwa. 11Mpaka saa hii tuna njaa na kiu, tu uchi, tumepigwa na hatuna makao. 12Tunafanya kazi kwa bidii kwa mikono yetu wenyewe. Tunapolaaniwa, tunabariki, tunapoteswa twastahimili, 13tunaposingiziwa, tunajibu kwa upole. Mpaka sasa tumekuwa kama takataka ya dunia na uchafu wa ulimwengu hadi leo.

14Siwaandikii mambo haya, ili kuwaaibisha, bali ili kuwaonya, kama wanangu wapendwa. 15Hata kama mnao walimu 10,000 katika Kristo, lakini hamna baba wengi. Mimi nilikuwa baba yenu katika Kristo Yesu kwa kuwaletea Injili. 16Basi nawasihi mwige mfano wangu. 17Kwa sababu hii ninamtuma Timotheo, mwanangu mpendwa na mwaminifu katika Bwana. Yeye atawakumbusha kuhusu maisha yangu katika Kristo ambayo yanakubaliana na mafundisho yangu ninayofundisha kila mahali kwenye kila kanisa.

18Baadhi yenu mmekuwa na majivuno mkidhani kuwa sitafika kwenu. 19Lakini kama Bwana akipenda, nitafika kwenu mapema, nami nitapenda kujua, si tu kile wanachosema hawa watu wenye kiburi, bali pia kujua nguvu yao. 20Kwa kuwa Ufalme wa Mungu si maneno matupu tu bali ni nguvu. 21Ninyi amueni. Je, nije kwenu na fimbo, au nije kwa upendo na kwa roho ya upole?

### *Mwasherati Atengwe*

**5** Kuna habari za kweli kwamba miongoni mwenu kuna uasherati ambao haujatokea hata miongoni mwa watu wasiomjua Mungu: kwamba mtu awe na mke wa baba yake. 2Nanyi mwajivuna! Je, haiwapasi kuhuzunika na kumtenga mtu huyo aliyefanya mambo hayo na ushirika wenu? 3Hata kama siko pamoja nanyi katika mwili, niko nanyi katika roho. Nami nimekwisha kumhukumu mtu huyo aliyetenda jambo hili, kama vile ningekuwapo. 4Mnapokutana katika Jina la Bwana wetu Yesu nami nikiwepo pamoja nanyi katika roho na uweza wa Bwana Yesu ukiwepo, 5mkabidhini mtu huyu kwa Shetani, ili asili ya dhambi iangamizwe lakini roho yake iokolewe katika siku ya Bwana.

6Majivuno yenu si mazuri. Je, hamjui ya kwamba chachu kidogo huchachusha donge zima la unga? 7Ondoeni chachu ya kale ili mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo

hamkutiwa chachu. Kwa maana Kristo, Mwana-Kondoo wetu wa Pasaka amekwisha tolewa kuwa dhabihu. 8Kwa hiyo, tusiiadhimishe sikukuu hii, kwa chachu ya zamani, chachu ya nia mbaya na uovu, bali kwa mkate usiotiwa chachu, mkate wa weupe wa moyo na kweli.

9Niliwaandikia katika waraka wangu kuwa msishirikiane na wazinzi. 10Sina maana kwamba msishirikiane na wazinzi wa ulimwengu huu, au wenye tamaa mbaya, wanyang'anyi au waabudu sanamu. Kwa kufanya hivyo ingewabidi mtoke humu ulimwenguni. 11Lakini sasa nawaandikia kwamba msishirikiane na mtu ye yote anayejiita ndugu lakini akiwa ni mzinzi, au mwenye tamaa mbaya, mwabudu sanamu au msingiziaji, mlevi au mdhalimu. Mtu kama huyo hata msile naye.

12Yanihusu nini kuwahukumu wale watu walio nje ya kanisa? Je, si mnapaswa kuwahumu hao walio ndani ya kanisa? 13 Mungu atawahukumu hao walio nje ya kanisa. "Ninyi mwondoeni huyo mtu mwovu miongoni mwenu."

### *Kushtakiana Miongoni Mwa Waamini.*

**6** Kama mtu ye yote wa kwenu ana ugomvi na mwenzake, anathubutuje kuupeleka kwa wasiomcha Mungu ili kuamuliwa badala ya kuupeleka kwa watakatifu? 2Je, hamjui kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu? Nanyi kama mtauhukumu ulimwengu, je, hamwezi kuamua mambo madogo madogo? 3Hamjui kwamba tutawahukumu malaika? Je, si zaidi mambo ya maisha haya? 4Kwa hiyo kama kuna ugomvi miongoni mwenu kuhusu mambo kama haya ninyi mwachagua watu ambao hata hawaheshimiwi katika kanisa kuwa waamuzi? 5Nasema hivi ili mwone aibu. Je, inawezekana kuwa miongoni mwenu hakuna mtu mwenye hekima ya kutosha kuamua ugomvi kati ya ndugu mmoja na mwenzake? 6Badala yake ndugu mmoja anampeleka mwenzake mahakamani, tena mbele ya watu wasioamini!

7 Ukweli ni kwamba huko kuwa na mashtaka dhidi ya mwingine miongoni mwenu tayari ni kushindwa. Kwa nini msikubali kutendewa mabaya? Kwa nini msikubali kunyang'anywa? 8Badala yake, ninyi wenyewe mwadanganya na kutenda mabaya, tena mwawatendea ndugu zenu.

### *Dhambi Za Zinaa*

12 ''Vitu vyote ni halali kwangu,'' lakini si vitu vyote vyenye faida, "Vitu vyote ni halali kwangu," lakini sitatawaliwa na kitu cho chote. 13"Chakula ni kwa ajili ya tumbo na tumbo ni kwa ajili ya chakula," lakini Mungu ataviangamiza vyote viwili. Mwili wa mwanadamu haukuumbwa kwa ajili ya zinaa bali kwa ajili ya Bwana na Bwana kwa ajili ya mwili. 14Naye Mungu aliyemfufua Bwana kutoka kwa wafu atatufufua sisi pia kwa uweza Wake. 15Je, hamjui kwamba miili yenu ni viungo vya Kristo? Je, nichukue viungo vya mwili wa Kristo na kuviunganisha na mwili wa kahaba? La hasha! 16 Hamjui kwamba aliyeungwa na kahaba anakuwa mwili mmoja naye? Kwa kuwa imenenwa, "Hao wawili watakuwa mwili mmoja." 17Lakini mtu uliyeungwa na Bwana anakuwa roho moja naye.

18Ikimbieni zinaa. Dhambi nyingine zote atendazo mtu ziko nje ya mwili wake, lakini yeye aziniye hutenda dhambi ndani ya mwili wake mwenyewe. 19Je, hamjui ya kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu, akaaye ndani yenu, ambaye mmepewa na Mungu? Ninyi si mali yenu wenyewe, 20kwa maana mmenunuliwa kwa gharama. Kwa hiyo mtukuzeni Mungu katika miili yenu na katika roho zenu ambazo ni mali ya Mungu.

### *Kuhusu Ndoa*

Basi kuhusu mambo yale mliyoniandikia: **7** Ni vema mwanaume asimguse mwanamke. 2Lakini ili kuepuka zinaa, kila mwanaume na awe na mke wake mwenyewe na kila mwanamke awe na mume wake mwenyewe. 3Mume atimize wajibu wake wa ndoa kwa mkewe,naye vivyo hivyo mke kwa mumewe. 4 Mwanamke hana mamlaka juu ya mwili wake bali mumewe, wala mume hana mamlaka juu ya mwili wake bali mkewe. 5Msinyimane, isipokuwa mmekubaliana kufanya hivyo kwa muda fulani ili mweze kujitoa kwa maombi, kisha mrudiane tena ili Shetani asije akapata nafasi ya kuwajaribu kwa sababu ya kutokuwa na kiasi. 6Nasema haya kama ushauri na si amri. 7Laiti watu wangekuwa kama mimi nilivyo. Lakini kila mtu amepewa kipawa chake kutoka kwa Mungu, mmoja ana kipawa cha namna hii na mwingine ana cha namna ile.

8Kwa wale wasiooa na kwa wajane, ingekuwa vizuri wabaki kama mimi nilivyo. 9Lakini kama hawawezi kujizuia, basi waoe na kuolewa, kwa maana ni afadhali kuoa au kuolewa kuliko kuwaka tamaa.

10Kwa wale waliooana nawapa amri, (si

mimi ila ni Bwana): Mke asimwache mumewe.
11Lakini kama akimwacha, ni lazima akae bila
kuolewa, ama sivyo apatane tena na mumewe.
Wala mume asimpe mkewe talaka.

12Lakini kwa wengine nasema, (si Bwana ila
ni mimi): Kama ndugu ana mke asiyeamini,
naye huyo mke anakubali kuishi pamoja naye,
basi asimwache. 13Naye mwanamke aaminiye
kama ameolewa na mwanaume asiyeamini na
huyo mume anakubali kuishi naye, basi huyo
mwanamke asimwache. 14Kwa maana huyo
mume asiyeamini anatakaswa kupitia mkewe,
naye mke asiyeamini anatakaswa kupitia
mumewe. Kama isingalikuwa hivyo watoto wenu
wangalikuwa si safi, lakini ilivyo sasa wao ni
watakafifu. 15Lakini kama yule asiyeamini
akijitenga, basi afanye hivyo. Katika hali kama
hiyo mwanamke au mwanaume aaminiye
hafungwi, kwa sababu Mungu ametuita tuishi
kwa amani. 16Wewe mke, unajuaje kama
utamwokoa mumeo? Au wewe mume unajuaje
kama utamwokoa mkeo?

### *Kuishi Kama Alivyoagiza Bwana*

17Lakini kila mtu na aishi maisha
aliyopangiwa na Bwana, yale Mungu aliyokuitia.
Hii ni sheria yangu kwa makanisa yote. 18Je,
mtu alikuwa ametahiriwa alipoitwa? Asijifanye
asiyetahiriwa. Je, mtu alikuwa hajatahiriwa
alipoitwa? Asitahiriwe. 19Kutahiriwa au
kutotahiriwa si kitu. Lakini kuzitii amri za Mungu
ndilo jambo muhimu. 20Basi kila mmoja wenu na
abaki katika hali aliyoitwa nayo. 21Je, wewe
ulipoitwa ulikuwa mtumwa? Jambo hilo
lisikusumbue. Hata kama unaweza kupata
uhuru, tumia nafasi uliyo nayo sasa kuliko
wakati mwingine wo wote. 22Kwa maana ye
yote aliyeitwa katika Bwana kama mtumwa yeye
ni mtu huru kwa Bwana, kama vile ye yote
aliyekuwa huru alipoitwa yeye ni mtumwa wa
Kristo. 23Mlinunuliwa kwa gharama, ili msiwe
watumwa wa wanadamu. 24 Ndugu zangu,
kama kila mtu alivyoitwa, akae katika wito wake
alioitiwa na Mungu.

### **Wajane na Wasiolewa.**

25Basi, kuhusu wale walio bikira, mimi sina
amri kutoka kwa Bwana, lakini mimi natoa
shauri kama mtu ambaye ni mwaminifu kwa
rehema za Bwana. 26Kwa sababu ya shida
iliyoko, naona ni vema mkibaki kama mlivyo.
27Je, umeolewa? Basi usitake talaka. Je,
hujaoa? Usitafute mke. 28Lakini kama ukioa,
hujatenda dhambi na kama bikira akiolewa,
hajatenda dhambi. Lakini wale wanaooa
watakabiliana na matatizo mengi katika maisha
haya, nami nataka kuwazuilia hayo.

29 Lakini ndugu zangu, nina maana
kwamba muda uliobaki ni mfupi. Tangu sasa
wale waliooa waishi kama wasio na wake 30nao
wanaoomboleza, kama ambao hawaombolezi,
wenye furaha kama wasiokuwa nayo, wale
wanaonunua, kama vile vitu walivyonunua si
mali yao, 31nao wale wanaoshughulika na vitu
vya dunia hii, kama ambao hawahusiki navyo.
Kwa maana dunia hii kama tunavyoiona sasa
inapita.

32Ningetaka msiwe na masumbufu.
Mwanaume ambaye hajaoa anajishughulisha na
mambo ya Bwana, yaani, jinsi ya kumpendeza
Bwana. 33Lakini mwanaume aliyeoa
anajishughulisha na mambo ya dunia, yaani,
jinsi ya kumfurahisha mkewe, 34Pia kuna tofauti
kati ya mwanamke aliyeolewa na msichana
bikira. Mwanamke asiyeolewa hujishughulisha
na mambo ya Bwana ili awe mtakatifu kimwili na
kiroho, lakini yule aliyeolewa hujishughulisha na
mambo ya dunia, jinsi atakavyoweza
kumfurahisha mumewe. 35Ninasema haya kwa
faida yenu, sio ili kuwawekea kizuizi cho chote,
bali mpate kuishi kwa jinsi ilivyo vema bila
kuvutwa pengine katika kujitoa kwenu kwa
Bwana.

36Kama mtu ye yote anadhani kwamba
hamtendei ilivyo sawa mwanamwali ambaye
amemposa, naye akiwa umri wake unazidi
kuendelea na mtu huyo anajisikia kwamba
inampasa kuoa, afanye kama atakavyo. Yeye
hatendi dhambi. Yawapasa waoane. 37Lakini
kama mwanaume ambaye ameshaamua
moyoni mwake kutokuoa bila kulazimishwa na
mtu ye yote, kama anaweza kujitawala kabisa,
basi anafanya vema kutokumwoa huyo
mwanamwali. 38 Hivyo basi, yeye mwanaume
amwoaye huyo mwanamwali afanya vema,
lakini yeye asiyemwoa afanya vema zaidi.

39Mwanamke aliyeolewa amefungwa na
sheria maadam mumewe yu hai. Lakini kama
mumewe akifa, basi mwanamke huyo yuko huru
kuolewa na mume mwingine ampendaye, lakini
lazima tu awe katika Bwana. 40Lakini kwa
uamuzi wangu, naona kuwa angekuwa na
furaha zaidi akibaki alivyo. Nami nadhani pia
nina Roho wa Mungu.

### ***Chakula Kilichotolewa Sadaka Kwa Sanamu.***

**8** Sasa kuhusu chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu, tunajua kwamba 'sisi sote tuna ujuzi.' Lakini 'ujuzi' hujivuna, bali upendo hujenga. 2Mtu ye yote anayedhani kwamba anajua kitu, hajui kama impasavyo kujua. 3Lakini mtu ampendaye Mungu, hujulikana Naye.

4Hivyo basi, kuhusu kula chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu, tunajua kwamba 'sanamu si kitu cho chote kabisa duniani na kwamba kuna Mungu mmoja tu.' 5Kwa maana hata kama wapo hao wanaoitwa 'miungu' kama ni mbinguni au duniani, (kama ilivyo kweli wapo 'miungu' wengi na 'mabwana' wengi). 6Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi.

7Lakini si wote wanaojua jambo hili. Baadhi ya watu bado wamezoea kufikiria kuwa sanamu ni halisi hivyo wanapokula chakula kama hicho wanadhani kimetolewa sadaka kwa sanamu na kwa kuwa dhamiri yao ni dhaifu, inatiwa unajisi. 8Lakini chakula hakituleti karibu na Mungu wala hatupotezi cho chote tusipokula, wala hatuongezi cho chote kama tukila.

9 Lakini angalieni jinsi tunavyotumia uhuru wetu usije ukawa kikwazo kwao walio dhaifu katika imani. 10Kwa maana kama mtu ye yote mwenye dhamiri dhaifu akiwaona ninyi wenye ujuzi mkila katika hekalu la sanamu, je, si atatiwa moyo kula chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu? 11Kwa njia hiyo, huyo ndugu mwenye dhamiri dhaifu, ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake, ataangamia kwa sababu ya ujuzi wenu. 12Mnapotenda dhambi dhidi ya ndugu zenu kwa njia hii na kujeruhi dhamiri zao zilizo dhaifu, mnamkosea Kristo. 13Kwa hiyo, kama kile ninachokula kitamfanya ndugu yangu aanguke katika dhambi, sitakula nyama kamwe nchi idumupo, nisije nikamfanya ndugu yangu aanguke.

### *Haki Za Mtume*

**9** Je, mimi si huru? Je, mimi si mtume? Je, mimi sikumwona Yesu, Bwana wetu? Je, ninyi si matunda ya kazi yangu katika Bwana? 2Hata kama mimi si mtume kwa wengine, hakika mimi ni mtume kwenu, kwa maana ninyi ni chapa ya utume wangu katika Bwana.

3Huu ndio utetezi wangu kwa hao wanaokaa kunihukumu. 4Je, hatuna haki ya kula na kunywa? 5Je, hatuna haki ya kusafiri na mke anayeamini, kama wanavyofanya mitume wengine na ndugu zake Bwana na Kefa? 6Au ni mimi na Barnaba tu ambao tunalazimika kufanya kazi ili tuweze kupata mahitaji yetu?

7 Ni askari yupi aendae vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni mkulima gani apandaye shamba la mizabibu na asile matunda yake? Ni nani achungaye kundi na asipate maziwa yake hata kidogo? 8Je, nasema mambo haya katika mtazamo wa kibinadamu tu? Je, sheria haisemi yayo hayo? 9Kwa maana imeandikwa katika sheria ya Mose? "Usimfunge ng'ombe kinywa apurapo nafaka." Je, Mungu hapa anahusika na ng'ombe? 10Je, Mungu hasemi haya hasa kwa ajili yetu? Hakika yameandikwa kwa ajili yetu, kwa sababu mtu anapolima na mwingine akapura nafaka, wote wanapaswa kufanya hivyo wakiwa na tumaini la kushiriki mavuno. 11Je, ikiwa sisi tulipanda mbegu ya kiroho miongoni mwenu, Je, itakuwa ni jambo kubwa iwapo tutavuna vitu vya mwili kutoka kwenu? 12Kama wengine wanahaki ya kupata msaada kutoka kwenu, sisi je, isingepasa tuwe na haki hiyo hata zaidi?

Lakini sisi hatukutumia haki hii. Kinyume chake, tunavumilia kila kitu ili tusije tukazuia injili ya Kristo. 13Je, hamjui kwamba, watu wafanyao kazi hekaluni hupata chakula chao kutoka hekaluni, nao wale wahudumiao madhabahuni hushiriki kile kitolewacho madhabahuni? 14Vivyo hivyo, Bwana ameagiza kwamba wale wanaohubiri injili wapate mahitaji yao kutokana na injili. 15Lakini sijatumia hata mojawapo ya haki hizi. Nami siandiki haya nikitumaini kwamba mtanifanyia mambo hayo. Heri nife kuliko mtu ye yote kuninyima huku kujisifu kwangu. 16Lakini ninapohubiri injili siwezi kujisifu maana ninalazimika kuhubiri. Ole wangu nisipoihubiri Injili! 17Nikihubiri kwa hiyari ninayo thawabu, lakini kama si kwa hiyari, ni kwamba ikiwa nalazimika kufanya hivyo, basi ninachofanya ni kutekeleza tu uwakili niliowekewa. 18Basi je, thawabu yangu ni nini? Twawabu yangu ni hii: ni kwamba katika kuhubiri Injili nitoe bila gharama, nisije nikatumia vibaya ule uwezo wangu nilio nao katika Injili.

19Ingawa mimi ni huru, wala si mtumwa wa mtu ye yote, nimejifanya kuwa mtumwa wa kila mtu, ili niweze kuwavuta wengi zaidi. 20Kwa Wayahudi, nilikuwa kama Myahudi, ili niwapate Wayahudi. Kwa watu wale walio chini ya sheria,

nilikuwa kama aliye chini ya sheria, (ingawa mimi siko chini ya sheria), ili niweze kuwapata wale walio chini ya sheria. 21Kwa watu wasio na sheria nilikuwa kama asiye na sheria, (ingawa siko huru mbali na sheria ya Mungu, bali niko chini ya sheria ya Kristo,) ili niweze kuwapata wale wasio na sheria. 22Kwa walio dhaifu nilikuwa dhaifu, ili niweze kuwapata walio dhaifu. Nimekuwa mtu wa hali zote kwa watu wote ili kwa njia ye yote niweze kuwaokoa baadhi yao. 23Nafanya haya yote kwa ajili ya Injili, ili nipate kushiriki baraka zake.

24Je, hamjui kwamba katika mashindano ya mbio wote wanaoshindana hukimbia, lakini ni mmoja wao tu apewaye tuzo? Kwa hiyo kimbieni katika mashindano kwa jinsi ambavyo mtapata tuzo. 25Kila mmoja anayeshiriki katika mashindano hufanya mazoezi makali. Wao hufanya hivyo ili wapokee taji isiyodumu, lakini sisi tunafanya hivyo ili kupata taji idumuyo milele. 26Kwa hiyo mimi sikimbii kama mtu akimbiaye bila lengo, sipigani kama mtu anayepiga hewa, 27la, bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha ili nikishawahubiria wengine, mimi nisiwe mtu wa kukataliwa.

### *Onyo Kutoka Historia Ya Waisraeli.*

**10** Zaidi ya hayo ndugu zangu, sitaki mkose kufahamu ukweli huu kwamba baba zetu walikuwa wote chini ya wingu na kwamba wote walipita katikati ya bahari. 2Wote wakabatizwa kuwa wa Mose ndani ya lile wingu na ndani ya ile bahari. 3Wote walikula chakula kile cha roho, 4na wote wakanywa kile kinywaji cha roho, kwa maana walikunywa kutoka katika ule mwamba wa roho uliofuatana nao, ule mwamba ulikuwa Kristo. 5Lakini Mungu hakupendezwa na wengi wao, kwa hiyo miili yao ilitapakaa jangwani.

6Basi mambo haya yalitokea kama mfano ili kutuonya tusiweke mioyo yetu katika mambo maovu kama wao walivyofanya. 7Msiwe waabudu sanamu, kama baadhi yao walivyokuwa, kama ilivyoandikwa, “Watu walikaa chini wakala na kunywa, kisha wakainuka kucheza na kufanya karamu za ulevi na ulafi.” 8Wala tusifanye uzinzi kama baadhi yao walivyofanya, wakafa watu 23,000 kwa siku moja. 9Wala tusimjaribu Bwana, kama baadhi yao walivyofanya, wakafa kwa kuumwa na nyoka. 10Msinung’unike kama baadhi yao walivyofanya, wakaangamizwa na mharabu.

11Mambo haya yote yaliwapata wao ili yawe mifano kwa wengine, nayo yaliandikwa ili yatuonye sisi ambao mwisho wa nyakati umetufikia. 12Hivyo, yeye ajidhaniaye amesimama, aangalie asianguke. 13Hakuna jaribu lo lote lililowapata ambalo si la kawaida kwa wanadamu. Naye Mungu ni mwaminifu ambaye hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza. Lakini mnapojaribiwa atawapa njia ya kutokea ili mweze kustahimili.

### *Karamu za Sanamu na Meza ya Bwana*

14Kwa hiyo wapenzi wangu, zikimbieni ibada za sanamu. 15Nasema nanyi kama na watu wenye ufahamu, amueni wenyewe kuhusu haya niyasemayo. 16Je, kikombe cha baraka ambacho tunakibariki, si ushirika katika damu ya Kristo? Mkate tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? 17(Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja, kwa kuwa wote twashiriki mkate mmoja)

18Waangalieni watu wa Israeli: Je, wale wote walao dhabihu si ni wale watendao kazi madhabahuni? 19Je, nina maana kwamba kafara iliyotolewa kwa sanamu ni kitu chenye maana yo yote? Au kwamba sanamu ni kitu chenye maana yo yote? 20La hasha! Lakini kafara za watu wasiomjua Mungu hutolewa kwa mashetani, wala si kwa Mungu. Nami sitaki ninyi mwe na ushirika na mashetani. 21 Hamwezi kunywa katika kikombe cha Bwana na cha mashetani pia. Hamwezi kuwa na sehemu katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani. 22Je, tunataka kuamsha wivu wa Bwana? Je, sisi tuna nguvu kuliko Yeye?

### *Fanyeni Yote Kwa Utukufu wa Mungu*

23“Vitu vyote ni halali,” lakini si vitu vyote vilivyo na faida. ‘‘Vitu vyote ni halali,’’ lakini si vyote vinavyojenga. 24Mtu ye yote asitafute yaliyo yake mwenyewe, bali kila mtu atafute yale yanayowafaa wengine.

25Kuleni cho chote kinachouzwa sokoni, bila kuuliza swali lo lote kwa ajili ya dhamiri. 26Kwa maana, “Dunia na vyote vilivyomo ni mali ya Bwana.”

27Kama ukikaribishwa chakula na mtu asiyeamini nawe ukikubali kwenda, kula kila kitu kitakachowekwa mbele yako bila kuuliza maswali kwa ajili ya dhamiri. 28Lakini kama mtu ye yote akikuambia, “Hiki kimetolewa kafara kwa sanamu,” basi usikile kwa ajili ya huyo aliyekuambia na kwa ajili ya dhamiri. 29Nina maana dhamiri ya huyo aliyekuambia, wala si

kwa ajili ya dhamiri yako. Lakini kwa nini uhuru
wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu
mwingine? 30Kama nikila kwa shukrani, kwa nini
nashutumiwa kwa kile ambacho kwa hicho
ninamshukuru Mungu?

31Basi, lo lote mfanyalo, kama ni kula au
kunywa, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.
32Msiwe kikwazo kwa mtu ye yote, kwa
Wayahudi au kwa Wayunani, au kwa Kanisa la
Mungu, 33kama mimi ninavyojaribu
kumpendeza kila mtu kwa kila namna. Kwa
maana sitafuti mema kwa ajili yangu mwenyewe
bali mema kwa ajili ya faida ya wengi, ili waweze
kuokolewa.

**11** NiigeniKristo. mimi kama nami ninavyomwiga

### *Utaratibu katika kuabudu*

2Ninawasifu kwa kuwa mnanikumbuka
katika kila jambo na kwa kushika mafundisho
niliyowapa.

3Lakini napenda mfahamu kwamba kichwa
cha kila mwanaume ni Kristo, na kichwa cha
mwanamke ni mwanaume, nacho kichwa cha
Kristo ni Mungu. 4Kila mwanaume anayeomba
au kutoa unabii akiwa amefunika kichwa chake,
anakiaibisha kichwa chake. 5Lakini kila
mwanamke anayeomba au kutoa unabii pasipo
kufunika kichwa chake, anakiaibisha kichwa
chake, kwani ni sawa na yeye aliyenyoa nywele.
6Kama mwanamke hatajifunika kichwa chake,
basi inampasa kunyoa nywele zake. Lakini
kama ni aibu kwa mwanamke kunyoa nywele
zake, basi afunike kichwa chake. 7Mwanaume
haimpasi kufunika kichwa chake kwa kuwa yeye
ni mfano wa Mungu na utukufu wa Mungu, lakini
mwanamke ni utukufu wa mwanaume. 8Kwa
maana mwanaume hakutoka katika mwanamke,
bali mwanamke alitoka kwa mwanaume. 9Wala
mwanaume hakuumbwa kwa ajili ya
mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya
mwanaume. 10Kwa sababu hii na kwa sababu
ya malaika, mwanamke inampasa awe na
ishara ya mamlaka iliyo juu yake.

11Lakini katika Bwana, mwanamke
hajitegemei pasipo mwanaume na mwanaume
hajitegemei pasipo mwanamke. 12Kama vile
mwanamke alivyoumbwa kutoka kwa
mwanaume, vivyo hivyo mwanaume huzaliwa
na mwanamke. Lakini vitu vyote vyatoka kwa
Mungu. 13Hukumuni ninyi wenyewe: Je, inafaa
kwa mwanamke kumwomba Mungu bila
kufunika kichwa chake? 14Je, maumbile ya asili
hayatufundishi kuwa ni aibu kwa mwanaume
kuwa na nywele ndefu? 15Lakini mwanamke
akiwa na nywele ndefu ni utukufu kwake. Kwa
maana mwanamke amepewa nywele ndefu ili
kumfunika. 16Kama mtu anataka kubishana juu
ya jambo hili, sisi wala makanisa ya Mungu
hatutambui desturi nyingine.

### *Matumizi Mabaya ya Meza ya Bwana*

17Basi katika maagizo yafuatayo, siwezi
kuwasifu, kwa sababu mkutanikapo si kwa ajili
ya faida bali kwa hasara. 18Kwanza,
mnapokutana kama kanisa, nasikia kwamba
kuna mgawanyiko miongoni mwenu, nami kwa
kiasi fulani nasadiki kuwa ndivyo ilivyo. 19Bila
shaka lazima pawe na tofauti miongoni mwenu
ili kuonyesha ni nani anayekubaliwa na Mungu.
20Mkutanikapo pamoja si chakula cha Bwana
mnachokula, 21kwa kuwa mnapokula, kila
mmoja wenu anakula bila kuwangoja wengine,
huyu hukaa njaa na mwingine analewa. 22Je,
hamna nyumbani kwenu ambako mnaweza kula
na kunywa? Au mnalidharau kanisa la Mungu
na kuwadhalilisha wale wasio na kitu?
Niwaambie nini? Je, niwasifu juu ya jambo hili?
La, hasha!

### *Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

23Kwa maana mimi nilipokea kutoka kwa
Bwana yale niliyowapa ninyi, kwamba Bwana
Yesu, usiku ule alipotolewa, alitwaa mkate,
24naye akiisha kushukuru, akaumega, akasema
“Huu ndio mwili Wangu, ambao ni kwa ajili
yenu. Fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu.”
25Vivi hivi baada ya kula, akakitwaa kikombe,
akisema, “Kikombe hiki ni agano jipya katika
damu Yangu. Fanyeni hivi kila mnywapo kwa
ukumbusho Wangu.” 26Maana kila mlapo mkate
huu na kunywea kikombe hiki, mnatangaza
mauti ya Bwana mpaka ajapo.

### *Kushiriki Meza Ya Bwana Isivyostahili*

27Kwa hiyo, mtu ye yote alaye mkate huo
au kukinywea kikombe hicho cha Bwana
isivyostahili, atakuwa na hatia ya dhambi juu ya
mwili na damu ya Bwana. 28Inampasa mtu
ajichunguze mwenyewe, kabla ya kula mkate na
kukinywea kikombe. 29Kwa maana mtu ye yote
alaye na kunywa pasipo kuutambua mwili wa
Bwana, anajiletea hukumu juu yake mwenyewe.
30Hii ndiyo sababu wengi miongoni mwenu ni
wagonjwa na dhaifu na wengine wenu hata

wamekufa. 31Lakini kama tungejipambanua
wenyewe tusingehukumiwa.
32Tunapohukumiwa na Bwana, tunaadabishwa
ili tusije tukahukumiwa pamoja na ulimwengu.

33Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo
pamoja ili kula, mngojane. 34 Kama mtu akiwa
na njaa, ale nyumbani kwake ili mkutanapo
pamoja msije mkahukumiwa.

Nami nitakapokuja nitawapa maelekezo zaidi.

### *Karama Za Rohoni*

12 Basi ndugu zangu, kuhusu karama za rohoni, sitaki mkose kufahamu.
2Mnajua kwamba mlipokuwa hammjui Mungu,
mlishawishika na kupotoshwa na sanamu
zisizonena. 3Kwa hiyo nataka mfahamu ya kuwa
hakuna mtu anayeongozwa na Roho wa Mungu
anayeweza kusema, “Yesu na alaaniwe.” Pia
hakuna mtu awezaye kusema, “Yesu ni Bwana,”
isipokuwa ameongozwa na Roho Mtakatifu.

4Basi kuna aina mbali mbali za karama,
lakini Roho ni yule yule. 5Pia kuna huduma za
aina mbali mbali, lakini Bwana ni yule yule.
6Kisha kuna tofauti za kutenda kazi, lakini ni
Mungu yule yule atendaye kazi zote kwa watu
wote.

7Basi kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho
kwa faida ya wote. 8Maana mtu mmoja kwa
Roho hupewa neno la hekima na mwingine
neno la maarifa kwa Roho huyo huyo. 9Mtu
mwingine imani kwa huyo Roho na mwingine
karama za kuponya. 10Kwa mwingine matendo
ya miujiza, kwa mwingine unabii kwa mwingine
kupambanua roho, kwa mwingine aina mbali
mbali za lugha, kwa mwingine tafsiri za lugha.
11Haya yote hufanywa na huyo huyo Roho
mmoja, Roho naye humgawia kila mtu, kama
apendavyo mwenyewe.

### *Mwili Mmoja, Wenye Viungo Vingi*

12Kama vile mwili ulivyo mmoja nao una
viungo vingi, navyo viungo vyote vya mwili
ingawa ni vingi, ni mwili mmoja, vivyo hivyo na
Kristo. 13Kwa maana katika Roho mmoja wote
tulibatizwa katika mwili mmoja, kama ni
Wayahudi au Wayunani, kama ni watumwa au
watu huru, nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.

14 Basi mwili si kiungo kimoja, bali ni viungo
vingi. 15Kama mguu ungesema, “Kwa kuwa
mimi si mkono basi mimi si wa mwili,” hiyo
isingefanya huo mguu usiwe sehemu ya mwili.
16Na kama sikio lingesema, “Kwa kuwa mimi si
jicho, basi mimi si la mwili,” hiyo isingefanya hilo
sikio lisiwe sehemu ya mwili. 17Kama mwili wote
ungelikuwa jicho, kusikia kungekuwa wapi? Au
kama mwili wote ungelikuwa sikio, kunusa
kungekuwa wapi? 18Lakini kama ilivyo, Mungu
ameweka viungo katika mwili, kila kimoja kama
alivyopenda. 19Kama vyote vingekuwa kiungo
kimoja, mwili ungekuwa wapi? 20Kama ulivyo,
kuna viungo vingi, lakini mwili ni mmoja.

21Jicho haliwezi kuuambia mkono, “Sina
haja nawe!” Wala kichwa hakiwezi kuiambia
miguu, “Sina haja na ninyi!” 22Lakini badala
yake, vile viungo vya mwili vinavyoonekana
kuwa dhaifu, ndivyo ambavyo ni vya muhimu
sana. 23Navyo vile viungo vya mwili
tunavyoviona havina heshima, ndivyo tunavipa
heshima maalum. Vile viungo vya mwili
ambavyo havina uzuri, tunavipa heshima ya
pekee. 24Wakati vile viungo vyenye uzuri
havihitaji utunzaji wa pekee. Lakini Mungu
ameviweka pamoja viungo vya mwili na akavipa
heshima zaidi vile vilivyopungukiwa, 25ili pasiwe
na mafarakano katika mwili, bali viungo vyote
vihudumiane usawa kila kimoja na mwenzake.
26Kama kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote
huumia pamoja nacho, kama kiungo kimoja
kikipewa heshima, viungo vyote hufurahi
pamoja nacho.

27Sasa ninyi ni mwili wa Kristo na kila
mmoja wenu ni kiungo. 28Mungu ameweka
katika kanisa, kwanza mitume, pili manabii, tatu
walimu, kisha watenda miujiza, pia karama za
kuponya, karama za masaidiano, karama za
maongozi, aina mbalimbali za lugha. 29 Je, wote
ni mitume? Je, wote ni manabii? Je, wote ni
walimu? Je, wote wanafanya miujiza? 30Je,
wote wana karama ya kuponya? Je, wote
hunena kwa lugha mpya? Je, wote wanatafsiri?
31Basi tamanini sana karama zilizo kuu.

Nami nitawaonyesha njia iliyo bora zaidi.

### *Karama ya Upendo*

13 Hata kama nitasema kwa lugha za
wanadamu na za malaika, kama sina upendo,
nimekuwa kengele inayolialia au toazi livumalo.
2Ningekuwa na karama ya unabii na kujua siri
zote na maarifa yote, hata kama nina imani kiasi
cha kuweza kuhamisha milima, kama sina
upendo, mimi si kitu. 3Kama nikitoa mali yote
niliyo nayo na kama nikijitolea mwili wangu
uchomwe moto, kama sina upendo,
hainifaidii kitu.

4Upendo huvumilia, upendo hufadhili,

upendo hauoni wivu, hauna majivuno. Upendo hauna kiburi. 5Haukosi kuwa na adabu. Upendo hautafuti mambo yake, haukasiriki upesi, hauweki kumbukumbu ya mabaya. 6Upendo haufurahii mabaya bali hufurahi pamoja na kweli. 7Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote.

8Upendo haushindwi kamwe. Lakini ukiwepo unabii, utakoma, zikiwepo lugha zitakoma, yakiwepo maarifa yatapita. 9Kwa maana tunafahamu kwa sehemu na tunatoa unabii kwa sehemu. 10Lakini ukamilifu utakapokuja, yale yasiyo kamili yatatoweka. 11Nilipokuwa mtoto, nilisema kama mtoto, niliwaza kama mtoto, nilifikiri kama mtoto. Nilipokuwa mtu mzima niliacha mambo ya kitoto. 12Kwa maana sasa tunaona taswira kama ya kwenye kioo, lakini wakati huo tutaona wazi. Sasa nafahamu kwa sehemu, wakati huo nitafahamu kikamilifu, kama vile mimi ninavyofahamika kikamilifu.

13Basi sasa, yanadumu mambo haya matatu: Imani, tumaini na upendo. Lakini lililo kuu miongoni mwa haya matatu ni upendo.

### *Karama Za Unabii Na Lugha*

**14** Fuateni upendo na kutaka sana karama za roho, hasa karama ya unabii. 2Kwa maana mtu ye yote anayesema kwa lugha, hasemi na wanadamu bali anasema na Mungu. Kwa kuwa hakuna mtu ye yote anayemwelewa, kwani anasema mambo ya siri kwa Roho. 3Lakini anayetoa unabii anasema na watu akiwajenga, kuwatia moyo na kuwafariji. 4Anenaye kwa lugha hujijenga mwenyewe, bali atoaye unabii hulijenga kanisa. 5Ningependa kila mmoja wenu anene kwa lugha mpya, lakini ningependa zaidi nyote mtoe unabii. Kwa kuwa yeye atoaye unabii ni mkuu kuliko anenaye kwa lugha, isipokuwa kama kuna mtu wa kutafsiri, ili kanisa zima lipate kujengwa.

6Sasa ndugu zangu, kama nikija kwenu nikasema kwa lugha mpya nitawafaidia nini kama sikuwaletea ufunuo au neno la maarifa au unabii au mafundisho? 7Hata vitu visivyo na uhai vitoapo sauti, kama vile filimbi au kinubi, mtu atajuaje ni wimbo gani unaoimbwa kusipokuwa na tofauti ya upigaji? 8Tena kama tarumbeta haitoi sauti inayoeleweka, ni nani atakayejiandaa kwa ajili ya vita? 9Vivyo hivyo na ninyi, kama mkinena maneno yasiyoeleweka katika akili, mtu atajuaje mnalosema? Kwa maana mtakuwa mnasema hewani tu. 10Bila shaka ziko sauti nyingi ulimwenguni, wala hakuna isiyo na maana. 11Basi kama sielewi maana ya hiyo sauti, nitakuwa mgeni kwa yule msemaji, naye atakuwa mgeni kwangu. 12Vivyo hivyo na ninyi. Kwa kuwa mnatamani kuwa na karama za rohoni, jitahidini kuzidi sana katika karama kwa ajili ya kulijenga kanisa.

13Kwa sababu hii, yeye anenaye kwa lugha na aombe kwamba apate kutafsiri kile anachonena. 14Kwa maana nikiomba kwa lugha, roho yangu inaomba, lakini akili yangu haina matunda. 15Nifanyeje basi? Nitaomba kwa roho, lakini nitaomba kwa akili yangu pia. Nitaimba kwa roho na nitaimba kwa akili yangu pia. 16Ikiwa unabariki kwa roho, mtu mwingine atakayejikuta katikati ya hao wasiojua, atawezaje kusema ‘amen’ katika kushukuru kwako, wakati haelewi unachosema? 17Mnaweza kuwa mnatoa shukrani kweli, sawa, lakini huyo mtu mwingine hajengeki.

18Namshukuru Mungu kwamba mimi nanena kwa lugha kuliko ninyi nyote. 19Lakini ndani ya kanisa ni afadhali niseme maneno matano ya kueleweka kwa akili ili niwafundishe wengine kuliko kusema maneno 10,000 kwa lugha.

20Ndugu zangu, msiwe kama watoto katika kufikiri kwenu, afadhali kuhusu uovu mwe kama watoto wachanga, lakini katika kufikiri kwenu, mwe watu wazima. 21Katika sheria imeandikwa kwamba:

‘‘Kwa kupitia watu wenye lugha ngeni na
kupitia midomo ya watu wageni,
nitasema na watu hawa,
lakini hata hivyo
hawatanisikiliza,” asema Bwana.

22Basi kunena lugha mpya, ni ishara si kwa watu waaminio, bali kwa ajili ya wasioamini, wakati unabii si kwa ajili ya wasioamini, bali kwa ajili ya waaminio. 23Kwa hiyo kama kanisa lote likikutana na kila mmoja akanena kwa lugha, kisha wakaingia wageni wasiomini, je, hawatasema kwamba wote mna wazimu? 24Lakini kama mtu asiyeamini au asiyeelewa wakati kila mtu anatoa unabii, ataaminishwa na watu wote kuwa yeye ni mwenye dhambi na kuhukumiwa na wote, 25nazo siri za moyo wake zitawekwa wazi. Kwa hiyo ataanguka chini na kumwabudu Mungu akikiri, “Kweli Mungu yuko katikati yenu!”

### *Kumwabudu Mungu Kwa Utaratibu*

26Basi tuseme nini, ndugu zangu?
Mnapokutana pamoja, mmoja atakuwa na
wimbo, mwingine neno la mafundisho, mwingine
ufunuo kutoka kwa Mungu, mwingine ataongea
lugha mpya na mwingine atatafsiri hiyo lugha.
Mambo yote yatendeke kwa ajili ya kujenga
kanisa. 27Kama mtu ye yote akinena kwa lugha,
basi waseme watu wawili au watatu si zaidi,
mmoja baada ya mwingine na lazima awepo
mtu wa kutafsiri. 28Lakini kama hakuna mtu ye
yote wa kutafsiri, hao watu na wanyamaze
kimya kanisani na wanene na nafsi zao
wenyewe na Mungu.

29Manabii wawili au watatu wanene na
wengine wapime yale yasemwayo. 30Kama mtu
ye yote aliyeketi karibu, akipata ufunuo, basi
yule wa kwanza na anyamaze. 31Kwa maana
wote mnaweza kutoa unabii mmoja baada ya
mwingine ili kila mtu apate kufundishwa na
kutiwa moyo. 32Roho za manabii zinawatii
manabii. 33 Kwa maana Mungu si Mungu wa
machafuko bali ni wa amani.

Kama ilivyo katika makusanyiko yote ya
watakatifu, 34wanawake wanapaswa kuwa
kimya kanisani. Hawaruhusiwi kusema, bali
wanyenyekee kama sheria isemavyo. 35Kama
wakitaka kuuliza kuhusu jambo lo lote,
wawaulize waume zao nyumbani. Kwa maana ni
aibu kwa mwanamke kuzungumza kanisani.

36Je, neno la Mungu lilianzia kwenu? Au ni
ninyi tu ambao neno la Mungu limewafikia?
37Kama mtu ye yote akidhani kwamba yeye ni
nabii, au ana karama za rohoni, basi na akubali
kwamba haya ninayoandika ni agizo kutoka kwa
Bwana. 38Kama mtu akipuuza jambo hili yeye
mwenyewe atapuuzwa.

39Kwa hiyo ndugu zangu, takeni sana kutoa
unabii na msikataze watu kusema kwa lugha.
40Lakini kila kitu kitendeke kwa heshima na kwa
utaratibu.

### *Kufufuka kwa Kristo*

**15** Basi ndugu zangu nataka
niwakumbushe kuhusu Injili niliyowahubiria,
mkaipokea na ambayo katika hiyo mmesimama.
2Kwa Injili hii mnaokolewa mkishikilia kwa uthabiti
neno nililowahubiria
ninyi. La sivyo, mmeamini katika ubatili.

3Kwa maana yale niliyopokea ndiyo
niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa
kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya
dhambi zetu, kama yasemayo Maandiko, 4ya
kuwa alizikwa na alifufuka siku ya tatu, 5na
kwamba alimtokea Kefa, kisha akawatokea
wale kumi na wawili. 6Baadaye akawatokea
wale ndugu waamini zaidi ya 500 kwa pamoja,
ambao wengi wao bado wako hai, ingawa
wengine wamelala. 7Ndipo akamtokea Yakobo
na kisha mitume wote. 8Mwisho wa wote,
akanitokea mimi pia, ambaye ni kama
aliyezaliwa si kwa wakati wake.

9Kwa maana mimi ndiye mdogo kuliko
mitume wote, nisiyestahili kuitwa mtume, kwa
sababu nililitesa kanisa la Mungu. 10Lakini kwa
neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo na
neema yake kwangu haikuwa kitu bure. Bali
nilizidi sana kufanya kazi kuliko mitume wote
lakini haikuwa mimi, bali ni ile neema ya Mungu
iliyokuwa pamoja nami. 11 Hivyo basi, kama
ilikuwa ni mimi au ni wao hili ndilo tulihubirilo na
hili ndilo mliaminilo.

### *Ufufuo wa Wafu*

12Basi kama tumehubiri ya kwamba Kristo
alifufuka kutoka kwa wafu, mbona baadhi yenu
mnasema hakuna ufufuo wa wafu? 13Lakini
kama hakuna ufufuo wa wafu, basi hata Kristo
hakufufuka. 14Tena ikiwa Kristo hakufufuka
kutoka kwa wafu, kuhuburi kwetu kumekuwa ni
bure na imani yenu ni batili. 15Zaidi ya hayo,
twaonekana basi kuwa mashahidi wa uongo wa
Mungu, kwa sababu tumeshuhudia kumhusu
Mungu kwamba alimfufua Kristo kutoka kwa
wafu, lakini hilo haliwezi kuwa kweli, kama wafu
hawafufuliwi. 16 Kwa kuwa kama wafu
hawafufuliwi, basi hata Kristo hajafufuka.
17Tena kama Kristo hajafufuka, imani yenu ni
batili, nanyi bado mko katika dhambi zenu.
18Hivyo basi wote waliolala katika Krito
wamepotea. 19Ikiwa tumaini letu ndani ya Kristo
ni kwa ajili ya maisha haya tu, sisi tunastahili
kuhurumiwa kuliko watu wengine wote duniani.

20 Lakini kweli Kristo amefufuka kutoka kwa
wafu, tunda la kwanza la wale wote waliolala.
21Kwa maana kama vile mauti ilivyokuja kwa
njia ya mtu mmoja, vivyo hivyo, ufufuo wa wafu
umekuja kwa njia ya mtu mmoja. 22Kwa maana
kama vile katika Adamu watu wote wanakufa,
vivyo hivyo katika Kristo wote watafanywa hai.
23Lakini kila mmoja kwa wakati wake: Kristo,
tunda la kwanza la ufufuo, kisha, wale walio
wake atakapokuja. 24Ndipo mwisho utafika,
wakati atakapomkabidhi Mungu Baba Ufalme,
akiisha angamiza kila utawala na kila mamlaka
na nguvu. 25Kwa maana lazima Kristo atawale

mpaka awe amewaweka adui zake wote chini
ya miguu yake. 26Adui wa mwisho
atakayeangamizwa ni mauti. 27”Kwa maana
Mungu ameweka vitu vyote chini ya miguu
yake.” Lakini isemapo kwamba, “Vitu vyote
vimewekwa chini Yake,” ni wazi kwamba Mungu
aliyetiisha vitu vyote chini ya Kristo hayumo
miongoni mwa hivyo vilivyotiishwa.
28Atakapokuwa amekwisha kutiisha vitu vyote
chini ya Mwana, ndipo Mwana mwenyewe
atatiishwa chini yake Yeye aliyetiisha vitu vyote,
ili Mungu awe yote katika yote.

29Basi kama hakuna ufufuo, watafanyaje
wale wabatizwao kwa ajili ya wafu? Kama wafu
hawafufuliwi kamwe, mbona watu wanabatizwa
kwa ajili yao? 30Nasi kwa upande wetu kwa nini
tunajitayarisha kila saa? 31Kama majivuno
yangu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu Bwana
wetu ni kweli, ndugu zangu, ninakufa kila siku.
32Kama kwa tumaini la kibinadamu tu nilipigana
na wanyama wakali huko Efeso, ningekuwa
nimepata faida gani kwa jambo hilo? Kama wafu
hawafufuliwi,

“Sisi na tule na kunywa,
wa kuwa kesho tutakufa.”

33Msidanganyike, “Ushirika na watu wabaya
huharibu tabia njema.” 34Zindukeni mwe na akili
kama iwapasavyo, msitende dhambi tena, kwa
maana watu wengine hawamjui Mungu.
Nasema mambo haya ili mwone aibu.

### *Mwili Wa Ufufuo*

35Lakini mtu anaweza kuuliza, “Wafu
wafufuliwaje? Watakuwa na mwili wa namna
gani?” 36Ninyi wapumbavu! Mpandacho hakiwi
hai kama hakikufa. 37Mpandapo, hampandi
mwili ule unaoutegemewa utakaokuwako, bali
mwapanda mbegu tupu, pengine ya ngano au
ya kitu kingine. 38Lakini Mungu huipa hiyo
mbegu umbo kama alivyokusudia mwenyewe na
kila aina ya mbegu huipa umbo lake. 39Kwa
maana nyama zote si za aina moja. Binadamu
wana nyama ya aina moja, wanyama wana aina
nyingine, kadhalika ndege na samaki wana
nyama tofauti. 40Pia kuna miili ya mbinguni na
miili ya duniani, lakini uzuri wa ile miili ya
mbinguni ni wa aina moja na uzuri wa ile miili ya
duniani ni wa aina nyingine. 41Jua lina fahari ya
aina moja, mwezi nao una fahari yake na nyota
pia, nazo nyota hutofautiana katika fahari.

42Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa
ufufuo wa wafu. Ule mwili wa kuharibika
uliopandwa utafufuliwa usioharibika,
43unapadwa katika aibu, unafufuliwa katika
utukufu, unapandwa katika udhaifu, unafufuliwa
katika nguvu, 44unapandwa mwili wa asili,
unafufuliwa mwili wa kiroho.

Kama kuna mwili wa asili, basi kuna mwili
wa kiroho pia. 45Kwa hiyo imeandikwa, “Mtu wa
kwanza Adamu alifanyika kiumbe hai,” Adamu
wa mwisho, Yeye ni roho iletayo uzima. 46Lakini
si ule wa kiroho uliotangulia, bali ni ule wa asili,
kisha ule wa kiroho. 47Mtu wa kwanza aliumbwa
kwa mavumbi ya ardhini, mtu wa pili alitoka
mbinguni. 48Kama vile alivyokuwa yule wa
ardhini, ndivyo walivyo wale walio wa ardhi na
kwa vile alivyo mtu yule aliyetoka mbinguni,
ndivyo walivyo wale walio wa mbinguni. 49Kama
vile tulivyochukua mfano wa mtu wa yule mtu
wa ardhini, ndivyo tutakavyochukua mfano wa
yule mtu aliyetoka mbinguni.

50 Ndugu zangu nisemalo ni hili: nyama na
damu haviwezi kuurithi Ufalme wa Mungu, wala
kuharibika kurithi kutokuharibika. 51Sikilizeni,
nawaambia siri: Sote hatutalala, lakini sote
tutabadilishwa 52ghafla, kufumba na kufumbua,
parapanda ya mwisho itakapolia. Kwa kuwa
parapanda italia, nao wafu watafufuliwa na miili
isiyoharibika, nasi tutabadilishwa. 53Kwa maana
mwili huu wa kuharibika lazima uvae
kutokuharibika, nao huu wa kufa lazima uvae
kutokufa. 54 Kwa hiyo, mwili huu wa kuharibika
utakapovaa kutokuharibika, nao huu mwili wa
kufa utakapovaa kutokufa, ndipo lile neno
lililoandikwa litakapotimia: “Mauti imemezwa
kwa kushinda.”

55“Kuko wapi Ewe mauti kushinda kwako?
Uko wapi Ewe mauti uchungu wako?”

56Uchungu wa mauti ni dhambi na nguvu ya
dhambi ni sheria. 57Lakini ashukuriwe Mungu,
Yeye atupaye ushindi kwa njia ya Bwana wetu
Yesu Kristo.

58Kwa hiyo, wapenzi, simameni imara,
msitikisike, mzidi sana katika kuitenda kazi ya
Bwana, kwa maana mnajua ya kuwa, juhudi
yenu si bure katika Bwana.

### *Changizo Kwa Ajili Ya Watakatifu*

**16** Basi kuhusu changizo kwa ajili ya watakatifu.
Kama nilivyoyaagiza makanisa ya Galatia, fanyeni
vivyo hivyo. 2Siku
ya kwanza ya kila juma, kila mmoja wenu

atenge kiasi cha fedha, kulingana na mapato
yake na fedha hizo aziweke akiba ili
nitakapokuja pasiwe na lazima ya kufanya
mchango. 3Kwa hiyo nitakapowasili, nitawapa
wale mtakaowachagua barua za
kuwatambulisha, ili kuwatuma wapeleke sadaka
zenu huko Yerusalemu. 4Kama ikionekana ni
vema na mimi niende, basi hao watu
watafuatana nami.

### *Mahitaji Binafsi*

5Baada ya kupitia Makedonia, nitakuja
kwenu; Maana ninakusudia kupitia Makedonia.
6Huenda nitakaa nanyi kwa muda, au hata
kukaa nanyi kipindi chote cha baridi, ili mweze
kunisaidia katika safari zangu, po pote
niendapo. 7Kwa maana sitaki niwaone sasa na
kupita tu, natarajia kuwa nanyi kwa muda wa
kutosha, kama Bwana akipenda. 8Lakini nitakaa
Efeso mpaka wakati wa Pentekoste, 9kwa
maana mlango mkubwa umefunguliwa kwangu
kufanya kazi yenye matunda, nako huko kuna
adui wengi.

10Ikiwa Timotheo atakuja kwenu,
mkaribisheni, hakikisheni kwamba hana hofu yo
yote akiwa nanyi, kwa sababu anafanya kazi ya
Bwana, kama mimi nifanyavyo. 11Basi asiwepo
mtu atakayekataa kumpokea. Msafirisheni kwa
amani ili aweze kunijia tena. Namtarajia yeye
pamoja na hao ndugu.

12Basi kwa habari za ndugu yetu Apolo,
nimemsihi kwa bidii aje kwenu pamoja na hao
ndugu. Kamwe alikuwa hapendi kuja sasa, lakini
atakuja apatapo nafasi.

### *Maneno Ya Mwisho*

13Kesheni, simameni imara katika imani,
iweni mashujaa na hodari. 14Fanyeni kila kitu
katika upendo.

15Ninyi mnajua kwamba watu wa nyumbani
mwa Stefana ndio waliokuwa wa kwanza
kuamini katika Akaya, nao wamejitoa kwa ajili ya
kuwahudumia watakatifu. 16Nawasihi mjitie
katika kuwahudumia watu kama hawa na kila
mmoja aingiaye kwenye kazi na kuifanya kwa
bidii. 17Nilifurahi Stefana, Fortunato na Akaiko
walipofika, kwa sababu hawa wamenipatia yale
niliyopungukiwa kutoka kwenu. 18Kwa kuwa
waliiburudisha roho yangu na yenu pia, watu
kama hawa, wanastahili kutambuliwa.

### Salamu za Mwisho

19Makanisa ya Asia wanawasalimu. Akila na
Prisila, pamoja na kanisa lililoko nyumbani kwao
wanawasalimu katika Bwana. 20Pia ndugu wote
walioko hapa wanawasalimu. Salimianeni kwa
busu takatifu.

21Mimi Paulo, naandika salamu hizi kwa
mkono wangu mwenyewe.

22 Kama mtu ye yote hampendi Bwana
Yesu Kristo na alaaniwe. "Maran-atha." Bwana
wetu, yu aja!

23Neema ya Bwana Yesu iwe nanyi.

24 Upendo wangu uwe nanyi nyote katika
Kristo Yesu. Amen.

**2Wakorinto**

### *Utangulizi*

Ingawa inaonekana kwamba waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wakorinthо uliwasaidia wakristo wa Korintho, lakini bado kulikuwa na mambo mengine ya kurekebisha kwani haukumaliza matatizo yote. Bado kulikuwa na mivutano na mashindano yaliyokuwa yakiendelea ndani ya kanisa la Korintho. Walimu wa uongo walikuwa wamejiingiza ndani ya kanisa wakiwa wanapinga na hata kushambulia uadilifu wa Paulo mwenyewe na mamlaka yake kama mtume.Wengine katika kanisa hawakutaka kutubu. Hivyo Paulo akisukumwa na upendo na kuhusika kwake, aliamua kutokurudi huko hadi tabia zao zibadilike.

Paulo akiwa na wasiwasi na kanisa la Korintho, alitoka Efeso akaenda Troa, ambapo alivunjika moyo kwa kutokupata habari zo zote kutoka Korintho*(2:12 – 13).* Paulo alipofika Makedonia aliburudishwa na Timotheo alipomletea habari nzuri kwamba uamsho ulikuwa umeanza katika kanisa la Korintho.

Huu ndio wakati Paulo alipoandika waraka wake wa pili. Katika waraka huu Paulo anaeleza hisia zake, wajibu, shauku na majukumu katika hali ya majadiliano katika ushirika wa Wakorintho wenyewe na mashambulizi yaliyokuwa yameelekezwa kwake binafsi kama mtume. Katika kushughulikia matatizo hayo, katika waraka huu wa pili Paulo alitaka kuthibitisha mamlaka yake. Kulikuwa na mashaka makubwa katika kanisa hilo kumhusu, japokuwa hatuelewi ni kwa nini. Lakini Paulo anaandika kwa uchungu mkubwa, kuthibitisha mamlaka yake kama mtume. Anajaribu pia kushughulikia masuala ya kiutekelezaji hasa kuhusu kusaidia waamini wasiojiweza walioko sehemu nyingine.

### *Wazo Kuu*

Katika barua hii Paulo anaonyesha jinsi tunavyoweza kupata ushindi katika mateso. Barua hii ni ya binafsi. Inaandikwa na mtu aliyekosewa sana na watu aliowapenda sana. Paulo anapoorodhesha mambo aliyoyapitia katika maisha yake kama mtumishi wa Kristo, tunaona jinsi neema ya Mungu inavyotenda kazi, ikileta mema kutoka katika mateso. Shetani anafanya bidii kujaribu kuiharibu kazi ya Mungu lakini Mungu ni mshindi na anawainua wale wanaomtegemea.

### *Mwandishi*

Paulo

### *Mahali*

Paulo aliandika waraka huu akiwa Makedonia baada ya kumaliza huduma yake ya miaka miwili huko Efeso.

### *Tarehe*

Waraka huu unaotambuliwa kama 2Wakorinthio inaonekana uliandikwa miezi michache tu baada ya ule wa kwanza, yamkini kabla tu ya kuanza kwa majira ya baridi katika mwaka 55 B.K.

### *Mgawanyo*

- Salamu na utambulisho (1:1-9)
- Mashindano ya makundi ndani ya kanisa (1:10 - 4::21)
- Uasherati, kushtakiana, usafi katika mwili (5:1- 6:20)
- Ndoa na useja ( 7:1- 40)
- Haki za Mkristo na wajibu wake (8:1-11:1)
- Mkristo katika ibada ya hadhara (11:2 - 34)
- Nafasi na umuhimu wa karama za Roho (12:1-14 :40).
- Ufufuo – msingi wa Imani ya Kikristo (15:1- 58)
- Hitimisho (16:1- 24)

### *Salamu*

**1** Barua hii ni kutoka kwangu mimi, Paulo,
mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya
Mungu na Timotheo ndugu yetu,

Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho,
pamoja na watakatifu wote walioko Akaya yote:

2Neema na amani kutoka kwa Mungu Baba
yetu na Bwana Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Mungu Wa Faraja Yote*

3Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu
Yesu Kristo, Baba wa huruma na Mungu wa
faraja yote. 4Yeye atufarijiye katika taabu zetu
zote, ili tuweze kuwafariji wale walio katika
taabu yo yote kwa faraja ambayo sisi wenyewe
tumepokea kutoka kwa Mungu. 5Kama vile
mateso ya Kristo yanavyotitirika ndani ya
maisha yetu, hivyo ndivyo faraja yetu
inavyofurika kwa njia ya Kristo. 6Kama
tunataabika, ni kwa ajili ya faraja na wokovu
wenu, kama tukifarijiwa, ni kwa ajili ya faraja
yenu, iwaleteayo saburi ya mateso yale yale
yanayotupata. 7Nalo tumaini letu kwenu ni
thabiti, kwa sababu tunajua kwamba kama vile
mnavyoshiriki mateso yetu, ndivyo pia
mnavyoshiriki katika faraja yetu.

8Ndugu wapendwa, hatutaki msijue kuhusu
zile taabu tulizopata huko Asia. Kwa maana
tulilemewa na mizigo sana kiasi cha kushindwa
kuvumilia, kwamba hata tulikata tamaa kuishi.
9Kwa kweli, mioyoni mwetu tulihisi tumekabiliwa
na hukumu ya kifo, ili tusijitegemee sisi
wenyenye bali tumtegemee Mungu afufuaye
wafu. 10 Yeye aliyetuokoa kwenye hatari kubwa
ya kifo ataendelea kutuokoa. Kwake Yeye
tumeweka tumaini letu kwamba atatuokoa tena.
11Kama vile mlivyoungana kusaidiana nasi
katika maombi, hivyo wengi watatoa shukrani
kwa niaba yetu kwa ajili ya baraka tulizopata
kwa maombi ya wengi.

### *Paulo Ahairisha Ziara*

12Basi haya ndiyo majivuno yetu: Dhamiri
yetu inatushuhudia kwamba tumeenenda katika
ulimwengu na hasa katika uhusiano wetu na ninyi,
katika utakatifu na uaminifu utokao kwa Mungu.
Hatukufanya hivyo kwa hekima ya kidunia bali kwa
neema ya Mungu. 13Kwa maana hatuwaandikii
mambo ambayo hamwezi kusoma au kuyaelewa.
Natumaini kwamba, 14kama vile mlivyotuelewa
kwa sehemu, mtakuja
kuelewa kwa ukamilifu ili mweze kujivuna kwa
ajili yetu, kama na sisi tutakavyojivuna kwa ajili
yenu katika siku ya Bwana Yesu.

15 Kwa kuwa nilikuwa na uhakika wa
mambo haya, nilitaka nije kwenu kwanza, ili
mpate upendeleo mara mbili. 16Nilipanga
kuwatembelea nikiwa safarini kwenda
Makedonia na kurudi tena kwenu nikitoka
Makedonia, ili mnisafirishe katika safari yangu
ya kwenda Uyahudi. 17Nilipopanga jambo hili,
je, nilikuwa kigeugeu ? Au ninafanya mipango
yangu kidunia, ili niseme, “Ndiyo, ndiyo’’ na
“Siyo, siyo’’ wakati huo huo ?

18Hakika kama Mungu alivyo mwaminifu,
maneno yetu kwenu hayajawa “Ndiyo na Siyo’’.
19Kwa kuwa Mwana wa Mungu Yesu Kristo,
ambaye tulimhubiri kwenu mimi, Silvano na
Timotheo, hakuwa ‘‘Ndiyo’’ na ‘‘Siyo’’, bali katika
Yeye sikuzote ni “Ndiyo’’. 20 Kwa maana ahadi
zote za Mungu zilizo katika Kristo ni “Ndiyo”.
Kwa sababu hii ni katika Yeye tunasema
“Amen” kwa utukufu wa Mungu. 21Basi ni
Mungu atufanyaye sisi pamoja nanyi kusimama
imara katika Kristo. Ametutia mafuta 22kwa
kututia muhuri Wake na kutupa Roho wake
mioyoni mwetu kuwa rehani kwa ajili ya
kututhibitishia kile kijacho.

23Mungu ni shahidi yangu kwamba ilikuwa
ni kwa kuwahurumia sikurudi Korintho. 24Si
kwamba tunatawala imani yenu, bali twatenda
kazi pamoja nanyi kwa ajili ya furaha yenu, kwa
sababu ni kwa imani mwasimama imara.

**2** Hivyo nilikusudia moyoni mwangu
nisifanye ziara nyingine yenye kuwaumiza ninyi.
2Kwa kuwa kama nikiwahuzunisha ninyi, ni nani
aliyebaki wa kunifurahisha isipokuwa ninyi
ambao nimewahuzunisha? 3Niliandika hivyo
kama nilivyofanya, ili nikija nisihuzunishwe na
wale watu ambao wangenifanya nifurahi. Nina
imani na ninyi nyote, kwamba wote
ningeshiriki furaha yangu. 4 Kwa maana
niliwaandikia katika dhiki kubwa na kutaabika
sana moyoni tena kwa machozi mengi, shabaha
yangu si ili niwasababishe mhuzunike bali
kuwaonyesha kina cha upendo wangu kwenu.

### *Msamaha Kwa Mwenye Dhambi*

5Basi ikiwa mtu ye yote amesababisha
huzuni, kwa kiasi fulani hakunihuzunisha mimi
kama alivyowahuzunisha ninyi nyote, ili
nisiifanye kali kupita kiasi. 6Adhabu hii
aliyopewa na wengi inamtosha. 7 Basi sasa
badala yake, inawapasa kumsamehe na

kumfariji, ili asigubikwe na huzuni kupita kiasi.
8Kwa hiyo, nawasihi, mpate kuuthibitisha tena
upendo wenu kwa ajili yake. 9Sababu ya
kuwaandikia ni kuona kama mngeweza
kushinda hilo jaribio na kutii katika kila jambo.
10Kama ninyi mkimsamehe mtu ye yote, mimi
pia nimemsamehe. Kile nilichosamehe, kama
kulikuwa na kitu cho chote cha kusamehe,
nimekwisha kusamehe mbele ya Kristo kwa ajili
yenu. 11 Ili Shetani asitushinde. Kwa maana
hatuachi kuzijua hila zake.

### *Wasiwasi Wa Paulo Huko Troa*

12Basi nilipofika Troa kuhubiri Injili ya Kristo
na kukuta kwamba Bwana alikuwa
amenifungulia mlango, 13bado nilikuwa sina
utulivu akilini mwangu kwa sababu sikumkuta
ndugu yangu Tito huko. Hivyo niliagana nao
nikaenda Makedonia.

14Lakini Mungu ashukuriwe, Yeye ambaye
sikuzote hutufanya tuandamane kwa ushindi
tukiwa ndani ya Kristo. Naye kwa kutupitia sisi
hueneza kila mahali kama harufu nzuri ya
kumjua Yeye. 15 Kwa maana sisi kwa Mungu ni
harufu nzuri ya manukato ya Kristo miongoni
mwa wale wanaookolewa. 16Kwa wale
wanaopotea sisi ni harufu ya mauti, lakini kwa
wale wanaookolewa sisi ni harufu nzuri iletayo
uzima. Ni nani basi awezaye kazi hiyo?
17Tofauti na watu wengine wengi, sisi
hatuchuuzi neno la Mungu kwa ajili ya kupata
faida. Kinyume chake, katika Kristo tunalisema
neno la Mungu kwa unyofu, kama watu
tuliotumwa kutoka kwa Mungu.

### *Wahudumu Wa Agano Jipya*

**3** Je, tunaanza kujisifu wenyewe tena? Au
tunahitaji kupata barua za utambulisho kwenu
au kutoka kwenu, kama watu wengine? 2Ninyi
wenyewe ndio barua yetu iliyoandikwa katika
mioyo yetu, inayojulikana na kusomwa na kila
mtu. 3Nanyi mwadhihirisha wazi kwamba ninyi
ni barua itokayo kwa Kristo, matokeo ya
huduma yetu, ambayo haikuandikwa kwa wino
bali kwa Roho wa Mungu aliye hai, si katika
vibao vya mawe, bali katika vibao ambavyo ni
mioyo ya wanadamu.

4Hili ndilo tumaini tulilo nalo mbele za
Mungu kwa njia ya Kristo. 5Si kwamba sisi
tunafikiri kuwa tunaweza kufanya jambo lo lote
wenyewe, lakini nguvu yetu inatoka kwa Mungu.
6Yeye ndiye aliyetufanya sisi kuwa wahudumu
wa Agano Jipya, si wa andiko bali wa Roho,
kwa kuwa andiko huua bali Roho hutia uzima.

### *Utukufu Wa Agano Jipya*

7Basi ikiwa ile huduma iliyoleta mauti, ile
iliyoandikwa kwa herufi juu ya jiwe ilikuja kwa
utukufu hata ikawa Waisraeli hawawezi
kuutazama uso wa Mose kwa sababu ya ule
utukufu wake, ingawa ulikuwa ni wa kufifia, 8je,
huduma ya Roho haitakuwa na utukufu zaidi?
9Ikiwa huduma ile iwahukumuyo wanadamu ina
utukufu, si itakuwa ya utukufu zaidi ile huduma
iletayo haki? 10Kwa maana kile kilichokuwa na
utukufu sasa hakina utukufu ukilinganisha na
huu utukufu uzidio sana wa Agano Jipya.
11Ikiwa kile kilichokuwa kinafifia kilikuja kwa
utukufu, si zaidi sana ya utukufu wa kile
kinachodumu?

12Kwa hiyo, kwa kuwa tunalo tumaini hili,
tuna ujasiri sana. 13Sisi si kama Mose, ambaye
ilimpasa kuweka utaji ili kufunika uso wake
Waisraeli wasiuone ule mng'ao ulivyokuwa juu
yake wakati ukififia na hatimaye kutoweka.
14Lakini akili zao zilitiwa upumbavu, kwa maana
mpaka leo utaji ule ule hufunika wakati Agano la
Kale lisomwapo.Huo utaji haujaondolewa kwa
maana ni katika Kristo peke Yake unaondolewa.
15Hata leo, torati ya Mose isomwapo, utaji
hufunika mioyo yao. 16 Lakini wakati wo wote
mtu anapomgeukia Bwana, "utaji
unaondolewa.'' 17Basi Bwana ndiye Roho.
Mahali alipo Roho wa Bwana hapo pana uhuru.
18Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji
tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye
kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka
utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa
Bwana, ambaye ndiye Roho.

### *Hazina Ya Mbinguni Kwenye Vyombo Vya Udongo*

**4** Kwa hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii kwa
rehema za Mungu, hatukati tamaa.
2Tumekataa mambo ya siri na ya aibu, wala
hatufuati njia za udanganyifu, tukichanganya
Neno la Mungu na uongo. Kinyume cha hayo
kwa kudhihirisha kweli waziwazi na
kujitambulisha wenyewe kwenye dhamiri ya kila
mtu mbele za Mungu. 3Hata nayo Injili yetu
kama imetiwa utaji, ni kwa wale tu wanaopotea.
4Kwa habari yao, mungu wa dunia hii
amepofusha akili za wasioamini, ili wasione
nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya
Mungu. 5Kwa maana hatujihubiri sisi wenyewe
ila tunamhubiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana na

sisi ni watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. 6Kwa
kuwa Mungu, Yeye aliyesema, ''Nuru na ing'ae
gizani,'' ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni
mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu
wa Mungu katika uso wa Kristo.

7Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya
udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa
ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu.
8Twataabika kila upande, lakini hatuangamizwi,
twaona wasiwasi lakini hatukati tamaa,
9twateswa lakini hatuachwi, twatupwa chini
lakini hatupondwi. 10Sikuzote twachukua katika
mwili kufa Kwake Yesu ili kwamba uzima wa
Yesu uweze kudhihirika katika miili yetu. 11Kwa
maana sisi tulio hai sikuzote tumetolewa tufe
kwa ajili ya Yesu, ili kwamba uzima wake upate
kudhihirishwa katika mwili wetu upatikanayo na
mauti. 12Hivyo basi, mauti inatenda kazi ndani
yetu, bali uzima unatenda kazi ndani yenu.

13Imeandikwa, ''Niliamini, kwa hiyo
nimesema.'' Kwa roho yule yule wa imani pia
tuliamini na hivyo tukasema, 14 kwa sababu
tunajua kwamba Yeye aliyemfufua Bwana Yesu
kutoka kwa wafu atatufufua pia na sisi pamoja
na Yesu na kutuleta sisi pamoja nanyi mbele
Zake. 15Haya yote ni kwa faida yenu, ili kwamba
neema ile inavyowafikia watu wengi zaidi na
zaidi, ipate kusababisha shukrani nyingi kwa
utukufu wa Mungu.

16Kwa hiyo, hatukati tamaa. Ingawa utu
wetu wa nje unachakaa, utu wetu wa ndani
unafanywa upya siku kwa siku. 17Kwa maana
dhiki yetu nyepesi iliyo ya kitambo
inatutayarisha kwa ajili ya utukufu wa milele
uzidio kuwa mwingi kupita kiasi, 18kwa sababu
hatuangalii yale yanayoweza kuonekana bali
yale yasiyoweza kuonekana, kwa maana yale
yanayoweza kuonekana ni ya kitambo tu, bali
yale yasiyoweza kuonekana ni ya milele.

### *Makao Yetu Ya Mbinguni*

**5** Kwa maana twajua kwamba kama hema
yetu ya dunia tunayoishi ikiharibiwa, tunalo
jengo kutoka kwa Mungu, nyumba
isiyojengwa kwa mikono ya wanadamu. 2Kwa
maana katika hema hii twalia kwa uchungu,
tukitamani kuvikwa makao yetu ya mbinguni,
3kwa kuwa tukiisha kuvikwa hatutaonekana tena
kuwa uchi. 4Kwa kuwa tukiwa bado katika hema
hii twalia kwa uchungu na kulemewa, kwa
sababu hatutaki kuvuliwa bali kuvikwa makao
yetu ya mbinguni ili kwamba kile kipatikanacho
na mauti kimezwe na uzima. 5Basi Mungu ndiye
aliyetufanya kwa ajili ya jambo ilo hilo naye
ametupa Roho Mtakatifu kuwa amana,
akituahidia kile kijacho.

6Kwa hiyo sikuzote tunalo tumaini, hata
ingawa tunajua kwamba wakati tukiwa katika
mwili huu, tuko mbali na Bwana, 7kwa maana
twaenenda kwa imani wala si kwa kuona.
8Naam, tunalo tumaini na ingekuwa bora zaidi
kuuacha mwili huu na kwenda kukaa na Bwana.
9Kwa hiyo, kama tuko katika mwili huu au tuko
mbali nao, lengo letu ni kumpendeza Bwana.
10Kwa kuwa sisi sote tutasimama mbele ya kiti
cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apate
kulipwa kwa ajili ya yale ambayo yametendwa
katika mwili wake, yakiwa mema au mabaya.

### *Huduma Ya Upatanisho*

11Basi, kwa kuwa tunajua kumcha Bwana,
tunajitahidi kuwavuta wengine, lakini Mungu
anatufahamu dhahiri, nami natumaini kwamba tu
dhahiri katika dhamiri zenu pia. 12Sio kwamba
tunajaribu kujistahilisha kwenu tena, lakini
tunataka kuwapa nafasi ili mwone fahari juu yetu
mweze kuwajibu hao wanaoona fahari juu ya
mambo yanayoonekana badala ya mambo yaliyo
moyoni. 13Kama tumerukwa na akili, ni kwa ajili ya
Mungu, kama tuna akili timamu ni kwa ajili yenu.
14Kwa kuwa upendo wa Kristo unatutia nguvu,
kwa sababu tunasadiki kuwa mmoja alikufa kwa
ajili ya wote, kwa hiyo wote walikufa. 15 Naye
alikufa kwa ajili ya watu wote, ili kwamba wote
wanaoishi wasiishi tena kwa ajili ya nafsi zao
wenyewe, bali kwa ajili Yake Yeye aliyekufa na
kufufuka tena kwa ajili yao.

16Hivyo tangu sasa hatumwangalii mtu ye
yote kwa mtazamo wa kibinadamu, ingawa wakati
fulani tulimwangalia Kristo kwa namna ya
kibinadamu, hatumwangalii tena kwa jinsi hiyo.
17Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo,
amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita,
tazama, yamekuwa mapya. 18Haya yote
yanatokana na Mungu, ambaye ametupatanisha
sisi na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo na
kutupatia sisi huduma ya upatanisho: 19Kwamba
Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha
ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe, akiwa
hawahesabii watu dhambi zao. Naye
ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho.
20Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo, kana
kwamba Mungu anawasihi kwa kupitia vinywa
vyetu, nasi twawaomba sana ninyi kwa niaba ya
Kristo, mpatanishwe na Mungu. 21Kwa maana
Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi

kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate
kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

6 Kama watenda kazi pamoja na Mungu,
tunawasihi msipokee neema ya Mungu
bure bila sababu . 2Kwa maana asema:

"Wakati uliokubalika nilikusikia,
siku ya wokovu nilikusaidia."

Tazama, wakati uliokubalika ndio huu, siku ya
wokovu ndiyo sasa."

### *Taabu Za Paulo*

3Hatuweki kitu cha kukwaza katika njia ya
mtu ye yote, ili huduma yetu isionekane kuwa na
lawama, 4bali kama watumishi wa Mungu
tuonyeshe kwa kila njia saburi nyingi katika
dhiki, katika misiba, katika shida, 5katika
kupigwa, katika kufungwa gerezani na katika
ghasia, katika kazi ngumu, katika kukesha na
katika njaa, 6katika utakatifu, katika ufahamu,
katika uvumilivu, katika utu wema, katika Roho
Mtakatifu na upendo wa kweli, 7katika maneno
ya kweli na katika nguvu za Mungu, kwa silaha
za haki za mkono wa kuume na za mkono za
kushoto, 8katika utukufu na katika kudharauliwa,
katika sifa mbaya na katika sifa nzuri, kama
wadanganyaji lakini tukiwa wakweli 9tukiwa
maarufu lakini tukihesabiwa kama tusiojulikana,
tukiwa kama wanaokufa lakini tunaishi,
tukipigwa lakini hatuuawi, 10kama wenye huzuni
lakini sikuzote tukifurahi, tukionekana maskini
lakini tukitajirisha wengi, tukiwa kama wasio na
kitu lakini tukiwa na vitu vyote.

11Tumesema nanyi wazi, enyi Wakorintho
na kuwafungulieni mioyo yetu wazi kabisa.
12Sisi hatujizuii kuwapenda, bali ninyi mmeuzuia
upendo wenu kwetu. 13Sasa nasema, kama na
watoto wangu: Ninyi pia
ifungueni mioyo yenu kabisa.

### *Msifungiwe Nira Pamoja Na Wasioamini*

14Msifungiwe nira pamoja na watu
wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa, kwa
maana pana uhusiano gani kati ya haki na
uovu? Au kuna ushirika gani kati ya nuru na
giza? 15Kuna mapatano gani kati ya Kristo na
Beliali[a]? Yeye aaminiye ana sehemu gani na
yeye asiyeamini? 16Kuna mapatano gani kati ya
hekalu la Mungu na sanamu? Kwa kuwa sisi tu
hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu
alivyosema : "Nitakaa pamoja nao na kutembea
katikati yao, nami nitakuwa Mungu wao, nao
watakuwa watu wangu."

17"Kwa hiyo tokeni miongoni
mwao, mkatengwe nao,
asema Bwana.
Msiguse kitu cho chote kilicho najisi,
Nami nitawakaribisha."
18"Mimi nitakuwa Baba kwenu,
nanyi mtakuwa wanangu na binti zangu,
asema Bwana Mwenyezi."

7 Wapenzi, kwa kuwa tunazo ahadi hizi, basi
na tujitakase nafsi zetu kutokana na kila kitu kitiacho
mwili na roho unajisi, tukitimiza
utakatifu kwa kumcha Mungu.

### *Furaha Ya Paulo*

2Tupatieni nafasi mioyoni mwenu.
Hatujamkosea mtu ye yote, hatujampotosha
mtu ye yote, wala hatujamdhulumu mtu ye yote.
3Sisemi haya ili kuwahukumu, kwa kuwa
nilisema mwanzo, kwamba ninyi mko mioyoni
mwetu hata kwa kufa pamoja au kuishi pamoja.
4Mara nyingi najivuna kwa ajili yenu, naona
fahari juu yenu, nimejawa na faraja, nina furaha
kupita kiasi katika mateso yetu yote.

5Kwa maana hata tulipoingia Makedonia,
miili yetu haikuwa na raha. Tulisumbuliwa kila
upande, kwa nje kulikuwa na mapigano na
mioyoni mwetu tulikuwa na hofu. 6Bali Mungu,
Yeye awafarijie wenye huzuni, alitufariji kwa
kufika kwake Tito, 7lakini si kule kuja kwa Tito
tu, bali pia kwa faraja mliyompa. Alitueleza jinsi
mlivyomwonea shauku, huzuni yenu kubwa na
juhudi yenu kwa ajili yangu, ili kwamba furaha
yangu ipate kuwa kubwa kuliko wakati wo wote.

8Hata kama niliwahuzunisha kwa barua
yangu, sijutii. Ingawa nilijuta kwa muda mfupi,
kwa kuwa najua kwamba barua yangu
iliwaumiza, lakini ni kwa kitambo tu, 9Lakini
sasa nina furaha, si kwa sababu mlihuzunika,
bali kwa kuwa huzuni hiyo iliwafanya mtubu.
Kwa maana mlihuzunishwa kama Mungu
alivyokusudia watu wahuzunike na hivyo sisi
hatukuwadhuru kwa njia yo yote. 10Kwa maana
huzuni ya kimungu huleta toba iletayo wokovu
na wala haina majuto. Lakini huzuni ya kidunia
husababisha mauti. 11Tazameni jinsi huzuni hii
ya kimungu ilivyoleta faida kutokana na huzuni
hii: bidii mliyo nayo, juhudi mliyofanya kujitetea,
uchungu wenu, hofu yenu, upendo wenu,
shauku yenu na jinsi mlivyokuwa tayari kutoa

a15 Beliali hapa ina maana ya "uovu", "kutokumcha Mungu"

adhabu inayostahili. Kwa kila njia mmethibitisha kuwa hamna hatia katika jambo hilo. 12Hivyo ingawa niliwaandikia, haikuwa kwa sababu ya huyo aliyekosa au huyo aliyekosewa. Lakini nilitaka ninyi wenyewe mwone, mbele za Mungu, jinsi mlivyojitoa kwa ajili yetu. 13Kwa ajili ya haya tumefarijika.

Zaidi ya kule sisi kutiwa moyo, tulifurahi sana kumwona Tito alivyo na furaha, kwa sababu roho yake imeburudishwa na ninyi nyote. 14Nilikuwa nimewasifu ninyi kwake, nanyi hamkuniaibisha. Lakini kila kitu tulichowaambia ninyi, kilikuwa kweli, hivyo kule kijisifu kwetu kwa Tito kuwahusu ninyi kumethibitishwa kuwa kweli pia. 15Upendo wake kwenu unaongezeka sana anapokumbuka jinsi mlivyokuwa watii na kumpokea kwa hofu na kutetemeka. 16Nafurahi kwamba ninaweza kuwatumaini ninyi kabisa.

### *Kutoa Kwa Ukarimu*

8 Basi sasa ndugu, nataka ninyi mjue kuhusu ile neema ambayo Mungu amewapa makanisa ya Makedonia. 2Pamoja na majaribu makali na taabu walizopata, furaha waliyokuwa nayo ilikuwa kubwa, ingawa walikuwa maskini kupindukia, kwa upande wao walifurika kwa wingi wa ukarimu. 3 Kwa maana nashuhudia kwamba wao walitoa kwa kadiri wawezavyo, hata na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe, 4wakitusihi kwa bidii wapewe fursa ya kushiriki katika huduma hii ya kuwasaidia watakatifu. 5Wala hawakufanya tulivyotazamia, bali walijitoa wao wenyewe kwa Bwana kwanza na ndipo wakajitoa kwa ajili yetu, kufuatana na mapenzi ya Mungu. 6Kwa hiyo tulimsihi Tito, kwa kuwa ndiye aliyeanzisha jambo hili, akamilishe tendo hili la neema kwa upande wenu. 7Lakini kama vile mlivyo mbele sana katika yote: Katika imani, katika usemi, katika maarifa, katika uaminifu wote na katika upendo wenu kwetu sisi, vivyo hivyo tunataka pia mzidi katika neema hii ya kutoa.

8Siwaamrishi, lakini nataka kujaribu unyofu wa upendo wenu kwa kuulinganisha na bidii ya wengine. 9Kwa maana mnajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba ingawa alikuwa tajiri, kwa ajili yenu alikubali kuwa maskini, ili kwa umaskini Wake ninyi mpate kuwa matajiri.

10Ushauri wangu kuhusu lile lililo bora kwenu juu ya jambo hili ni huu: Mwaka uliopita ninyi mlikuwa wa kwanza si tu kutoa lakini pia mlikuwa na shauku ya kufanya hivyo. 11Sasa ikamilisheni kazi hii kwa shauku kama mlivyoanza, jitoleeni kulingana na uwezo wenu. 12Kwa kuwa kama nia ya kutoa ipo, kitolewacho kinakubalika kulingana na kile mtu alicho nacho, wala si kwa kile ambacho hana.

13Nia yetu si kwamba wengine wasaidike wakati ninyi mnateseka, bali pawe na uwiano. 14Kwa wakati huu wingi wa vitu mlivyonavyo usaidie kutosheleza mahitaji yao, ili wakati wao wakiwa na wingi wa vitu, nao wapate kutosheleza mahitaji yenu. 15Ndipo patakuwa na usawa, kama maandiko yanavyosema, ‘‘Aliyekusanya kwa wingi, hakubakiza kitu, wala aliyekusanya kidogo hakupungukiwa.’’

### *Tito Atumwa Korintho*

16Ninamshukuru Mungu ambaye amemtia Tito moyo wa kuwajali ninyi kama mimi ninavyowajali. 17Si kwamba Tito amekubali tu ombi letu, bali anakuja kwenu akiwa na shauku kuliko wakati mwingine, tena kwa hiari yake mwenyewe. 18 Nasi tunamtuma pamoja naye ndugu ambaye anasifiwa na makanisa yote kwa huduma yake ya kuhubiri Injili. 19Zaidi ya hayo, alichaguliwa na makanisa ili asafiri pamoja nasi tulipokuwa tunatoa huduma hii ya ukarimu kwa ajili ya utukufu wa Bwana mwenyewe ili kuonyesha hisani yetu. 20Tunataka kuepuka lawana yo yote kuhusu jinsi tunavyosimamia matoleo haya ya ukarimu. 21Kwa kuwa tunakusudia kufanya kile kilicho haki si machoni mwa Bwana peke yake, bali pia machoni mwa watu wengine.

22Pamoja nao, tunamtuma ndugu yetu ambaye mara kwa mara ametuthibitishia kwa njia nyingi kwamba ana shauku, naam, zaidi sana sasa kwa sababu analo tumaini kuu kwenu. 23Kwa habari ya Tito, yeye ni mwenzangu na mtenda kazi pamoja nami miongoni mwenu. Kwa habari za ndugu zetu, wao ni wawakilishi wa makanisa, utukufu wa Kristo. 24Kwa hiyo waonyesheni wazi hawa ndugu uthibitisho wa upendo wenu na sababu inayotufanya tujivune kwa ajili yenu, mbele ya makanisa ,ili yapate kuona.

### *Wasaidieni Wakristo Wenzenu*

9 Hakuna sababu ya mimi kuwaandikia kuhusu huduma hii itolewayo kwa ajili ya watakatifu. 2Kwa kuwa ninajua mlivyo na shauku ya kusaidia, nami nimekuwa nikijivuna kwa ajili ya jambo hilo kwa watu wa Makedonia, nikiwaambia kuwa ninyi wa Akaya mmekuwa

tayari kutoa tangu mwaka jana na shauku yenu
imewachochea wengi wao katika kutoa. 3Lakini
sasa nawatuma hawa ndugu ili kujivuna kwetu
kuhusu mchango wenu kusiwe maneno matupu,
bali mpate kuwa tayari kama nilivyosema
mngekuwa tayari. 4Kwa maana kama nikija na
Mmakedonia ye yote na kuwakuta hamjawa
tayari, tutaona aibu kusema cho chote juu yenu
katika matoleo. 5 Kwa hivyo niliona ni muhimu
niwahimize hawa ndugu watangulie kuja huko
kwenu kabla yangu, wafanye mipango ya hayo
matoleo ya ukarimu mliyokuwa mmeahidi, ili
yawe tayari kama matoleo ya hiari wala si kama
ya kutozwa kwa nguvu.

### *Kupanda Kwa Ukarimu*

6Kumbukeni kwamba: Ye yote apandaye
kwa uchache pia atavuna kwa uchache, naye
apandaye kwa ukarimu pia atavuna kwa
ukarimu. 7Kila mtu atoe kama anavyokusudia
moyoni mwake, si kwa uchoyo au kwa
kulazimishwa, kwa maana Mungu humpenda
yeye atoaye kwa moyo mkunjufu. 8Naye Mungu
aweza kuwapa kila baraka kwa wingi, ili katika
mambo yote kila wakati, mwe na kila kitu
mnachohitaji, ili mweze kushiriki kwa wingi
katika kila kazi njema. 9Kama ilivyoandikwa:

"Ametawanya huwapa maskini,
haki yake yadumu milele."

10Yeye ampaye mpanzi mbegu kwa ajili ya
kupanda na mkate kuwa chakula, atawapa na
kuzidisha mbegu zenu za kupanda na kuongeza
mavuno ya haki yenu. 11Mtatajirishwa kwa kila
namna ili mpate kuwa wakarimu kila wakati,
ambako kwa kupitia kwetu, ukarimu wenu
utamletea Mungu shukrani.

12Huduma hii mnayofanya si tu kwa ajili ya
kukidhi mahitaji ya watakatifu, bali huzidi sana
kwa shukrani nyingi apewazo Mungu. 13Kwa
sababu ya huduma ambayo mmejithibitisha
wenyewe, watu watamtukuza Mungu kwa ajili ya
utii ufuatanao na ukiri wenu wa Injili ya Kristo na
kwa ukarimu wenu wa kushiriki pamoja nao na
pia wengine wote. 14Nao katika maombi yao
kwenu mioyo yao itawaonea shauku kwa
sababu ya neema ipitayo kiasi mliyopewa na
Mungu. 15Ashukuriwe Mungu kwa karama Yake
isiyoelezeka.

### *Paulo Atetea Huduma Yake*

Basi, mimi Paulo ninawasihi kwa unyenyekevu

**10** na upole wa Kristo, mimi niliye "mwoga"
ninapokuwa pamoja nanyi ana kwa ana, lakini mwenye
ujasiri nikiwa mbali nanyi!
2Nawaomba nitakapokuja kwenu nisiwe na
ujasiri dhidi ya watu fulani kama ninavyotazamia
kwa wale wanaodhani kwamba tunaishi kwa
kufuata namna ya ulimwengu huu. 3Ingawa
tunaishi duniani lakini hatupigani vita kama
ulimwengu ufanyavyo. 4Silaha za vita vyetu si
za mwili, Bali zina uwezo katika Mungu hata
kuangusha ngome. 5Tukiangusha mawazo na
kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya
Mungu na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii
Kristo, 6tena tukiwa tayari kuadhibu kila tendo la
kutokutii, kutii kwenu kutakapokamilika.

7Angalieni yale yaliyo machoni penu. Kama
mtu ye yote anaamini kuwa yeye ni mali ya
Kristo, basi kumbuka kuwa kama ulivyo wa
Kristo, vivyo hivyo na sisi ndivyo tulivyo. 8Basi
hata kama nikijisifu zaidi kidogo kuhusu
mamlaka tuliyo nayo, ambayo Mungu alitupa ili
kuwajenga wala si ya kuwabomoa, mimi
sitaionea haya. 9Sitaki nionekane kama
ninayejaribu kuwatisha kwa nyaraka zangu.
10Kwa maana wanasema, "Nyaraka zake ni
nzito na zenye nguvu, lakini akiwepo kwa mwili
ni dhaifu na kuzungumza kwake ni kwa
kudharauliwa." 11Watu kama hao wajue ya
kuwa, yale tusemayo kwa barua tukiwa hatupo
pamoja nanyi, ndivyo tulivyo na ndivyo
tutakavyofanya tutakapokuwa pamoja nanyi.

12Hatuthubutu kujiweka kwenye kundi moja
au kujilinganisha na hao wanaojitukuza
wenyewe kuwa wao ni wa maana sana.
Wanapojipima na kujilinganisha wenyewe kwa
wenyewe, wanaonyesha ya kuwa hawana
busara. 13Lakini sisi hatujajivuna kupita kiasi,
bali majivuno yetu yatakuwa katika mipaka ile
Mungu aliyotuwekea, mipaka ambayo inawafikia
hata nanyi. 14Kwa maana hatukuwa tunavuka
mipaka tunapowajumlisha katika mipaka yetu,
kwa sababu tulikuwa wa kwanza kuwaletea Injili
ya Kristo. 15Hatujivuni kupita kiasi, hii ina
maana katika taabu ya watu wengine, lakini
tumaini letu ni kwamba imani yenu inavyozidi
kukua, eneo letu la utendaji wetu miongoni
mwenu litapanuka sana, 16ili tuweze kuhubiri
Injili sehemu zilizo mbali nanyi na nchi yenu.
Kwa maana hatutaki kujisifu kwa ajili ya kazi
ambayo imekwisha kufanyika tayari katika eneo
la mtu mwingine. 17Lakini, "Yeye ajisifuye ajisifu
katika Bwana." 18Kwa maana si yeye ajisifuye

mwenyewe akubalïwaye, bali yeye ambaye
Bwana humsifu.

### *Paulo Na Mitume Wa Uongo*

**11** Laiti mngechukuliana nami kidogo
katika upumbuvu wangu! Naam,
chukulianeni nami. 2Ninawaonea wivu, wivu wa
kimungu, kwa kuwa mimi niliwaposea mume
mmoja, ili niwalete kwa Kristo kama mabikira
safi. 3Lakini nina hofu kuwa, kama vile Eva
alivyodanganywa kwa ujanja wa yule nyoka,
mawazo yenu yasije yakapotoshwa, mkauacha
unyofu na usafi wa upendo wenu kwa Kristo.
4Kwa sababu kama mtu akija na kuwahubiria
Yesu mwingine ambaye si yule tuliyemhubiri, au
kama mkipokea roho mwingine ambaye si yule
mliyempokea, au injili tofauti na ile mliyoikubali,
ninyi mnaitii kwa urahisi. 5Lakini sidhani ya kuwa
mimi ni dhalili sana kuliko hao ''mitume wakuu''.
6Inawezekana mimi nikawa si mnenaji hodari,
lakini ni hodari katika elimu. Jambo hili
tumelifanya liwe dhahiri kwenu kwa njia zote.
7Je, nilitenda dhambi kwa kujishusha ili
kuwainua ninyi kwa kuwahubiria Injili ya Mungu
pasipo malipo ? 8Niliyanyang'anya makanisa
mengine kwa kupokea misaada kutoka kwao ili
niweze kuwahudumia ninyi. 9 Nami nilipokuwa
pamoja nanyi, nikipungukiwa na cho chote,
sikuwa mzigo kwa mtu ye yote, kwa maana
ndugu waliotoka Makedonia walinipatia mahitaji
yangu. Kwa hiyo nilijizuia kuwa mzigo kwenu
kwa njia yo yote, nami nitaendelea kujizuia.
10Kwa hakika kama vile kweli ya Kristo ilivyo
ndani yangu, hakuna mtu ye yote katika Akaya
nzima atakayenizuia kujivunia jambo hili. 11Kwa
nini? Je, ni kwa sababu siwapendi? Mungu
anajua ya kuwa nawapenda! 12Nami
nitaendelea kufanya lile ninalofanya sasa ili
nisiwape nafasi wale ambao wanatafuta nafasi
ya kuhesabiwa kuwa sawa na sisi katika mambo
wanayojisifia.

13Watu kama hao ni mitume wa uongo, ni
wafanyikazi wadanganyifu, wanaojigeuza
waonekane kama mitume wa Kristo. 14Wala hii
si ajabu, kwa kuwa hata Shetani mwenyewe
hujigeuza aonekane kama malaika wa nuru.
15Kwa hiyo basi si ajabu, kama watumishi wa
Shetani nao hujigeuza ilil waonekane kama
watumishi wa haki. Mwisho wao utakuwa sawa
na matendo yao yanavyostahili.

### *Paulo Anajivunia Mateso Yake*

16Nasema tena, mtu ye yote asidhani
kwamba mimi ni mjinga. Lakini hata kama
mkinidhania hivyo, basi nipokeeni kama mjinga
ili nipate kujisifu kidogo. 17Ninayosema
kuhusiana na huku kujisifu kwa kujiamini, sisemi
kama vile ambavyo Bwana angesema, bali
kama mjinga. 18Kwa kuwa wengi wanajisifu
kama vile ulimwengu ufanyavyo, mimi nami
nitajisifu. 19Ninyi mwachukuliana na wajinga
kwa sababu mna hekima sana! 20Kweli ni
kwamba mnachukuliana na mtu akiwatia
utumwani au akiwatumia kwa ajili ya kupata
faida au akiwanyang'anya au akijitukuza
mwenyewe au akiwadanganya. 21Kwa aibu
inanipasa niseme kwamba sisi tulikuwa dhaifu
sana kwa jambo hilo!

Lakini cho chote ambacho mtu mwingine ye
yote angethubutu kujisifia, nanena kama mjinga,
nami nathubutu kujisifu juu ya hilo. 22Je, wao ni
Waebrania ? Mimi pia ni Mwebrania. Je, wao ni
Waisraeli ? Mimi pia ni Mwisraeli. Je, wao ni
wazao wa Abrahamu ? Mimi pia ni mzao wa
Abrahamu. 23Je, wao ni watumishi wa Kristo ?
Nanena kiwazimu, mimi ni zaidi yao: Nimefanya
kazi kwa bidii kuliko wao, nimefungwa gerezani
mara kwa mara, nimechapwa mijeledi sana,
nimekabiliwa na mauti mara nyingi. 24Mara tano
nimechapwa viboko arobaini kasoro kimoja na
Wayahudi. 25Mara tatu nalichapwa kwa fimbo,
mara moja nalipigwa kwa mawe, mara tatu
nimevunjikiwa na meli, nimekaa kilindini usiku
kucha na mchana kutwa. 26Katika safari za
mara kwa mara, hatari za kwenye mito, hatari
za wanyang'anyi, hatari kutoka kwa watu wangu
wenyewe, hatari kutoka kwa watu Mataifa,
hatari mijini, hatari nyikani, hatari baharini,
hatari kutoka kwa ndugu wa uongo.
27Nimekuwa katika kazi ngumu na taabu, katika
kukesha mara nyingi, ninajua kukaa njaa na
kuona kiu, nimekaa mara nyingi bila chakula,
nimesikia baridi na kuwa uchi. 28Zaidi ya hayo
yote, nakabiliwa na mzigo wa wajibu wangu kwa
makanisa yote. 29 Je, ni nani aliye dhaifu, nami
nisijisikie dhaifu? Je, nani aliyekwazwa, nami
nisiudhike?

30Kama ni lazima nijisifu, basi nitajisifia yale
mambo yanayoonyesha udhaifu wangu.
31Mungu na Baba wa Bwana Yesu, Yeye
ambaye anahimidiwa milele, anajua ya kuwa
mimi sisemi uongo. 32Huko Dameski, mtawala
aliyekuwa chini ya Mfalme Areta aliulinda mji wa
Dameski ili kunikamata. 33Lakini nilishushwa
kwa kapu kubwa kupitia katika dirisha ukutani
nikatoroka kutoka mikononi mwake.

### *Maono Ya Paulo Na Mwiba Aliokuwa Nao*

**12** Yanipasa nijisifu, ingawa haifaidii kitu. Nitaenda kwenye maono na ufunuo kutoka kwa Bwana.
2Namjua mtu mmoja katika Kristo ambaye miaka kumi na minne iliyopita alichukuliwa juu hadi mbingu ya tatu. Kama ni katika mwili au nje ya mwili, sijui, Mungu ajua.
3Nami najua ya kwamba mtu huyu, kwamba ni katika mwili au nje ya mwili mimi sijui, lakini Mungu ajua, 4alinyakuliwa hadi Paradiso[a]. Huko alisikia mambo yasiyoelezeka, mambo ambayo binadamu hana ruhusa ya kuyasimulia.
5Nitajisifu kwa ajili ya mtu kama huyo, lakini sitajisifu kuhusu mimi mwenyewe ila mimi nitajisifia udhaifu wangu. 6Hata kama ningependa kujisifu, sitakuwa mjinga, kwa maana nitakuwa nasema kweli. Lakini najizuia, ili mtu ye yote asije akaniona mimi kuwa bora zaidi kuliko ninavyoonekana katika yale ninayotenda na kusema.

7Ili kunizuia nisijivune kwa sababu ya ufunuo huu mkuu, nilipewa mwiba katika mwili wangu, mjumbe wa Shetani, ili anitese. 8 Kwa habari ya jambo hili nilimsihi Bwana mara tatu aniondolee mwiba huu. 9Lakini aliniambia, “Neema yangu inakutosha, kwa kuwa uweza wangu hukamilika katika udhaifu.” Kwa hiyo nitajisifu kwa furaha zaidi kuhusu udhaifu wangu, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. 10Hii ndiyo sababu, kwa ajili ya Kristo, nafurahia udhaifu, katika kutukanwa, katika taabu, katika mateso na katika shida, kwa maana ninapokuwa dhaifu, ndipo nina nguvu.

### *Wasiwasi Wa Paulo Kwa Wakorintho*

11Nimekuwa mjinga, lakini ninyi mmenilazimisha niwe hivyo. Kwa kuwa ilinipasa kusifiwa na ninyi, kwa sababu mimi si dhalili kuliko wale mitume “walio bora” ingawa mimi si kitu. 12Mambo yanayomtambulisha mtume wa kweli, yaani, ishara, miujiza na maajabu, yalifanywa miongoni mwenu kwa saburi nyingi.
13Je, ninyi ni kitu gani mlichopungukiwa kuliko makanisa mengine, ila tu kwamba mimi sikuwa mzigo kwenu? Nisameheni kwa kosa hili!

14Sasa niko tayari kuja kwenu kwa mara hii ya tatu, nami sitawalemea, kwa sababu sitahitaji cho chote chenu, ila ninawahitaji ninyi, kwa kuwa hata hivyo watoto hawaweki akiba kwa ajili ya wazazi wao, bali wazazi huweka akiba kwa ajili ya watoto wao. 15Hivyo nitafurahi kutumia kila kitu nilicho nacho kwa ajili yenu, hata mwili wangu pia. Hata ingawa inaonekana ninavyozidi kuwapenda, ndivyo upendo wenu kwangu unavyopungua.16Iwe iwavyo, kwa vyo vyote vile mimi sikuwalemea. Lakini kwa mimi kuwa mwerevu naliwapata. 17Je, nilijipatia faida kwa kumtumia mtu ye yote niliyemtuma kwenu?
18Nilimshawishi Tito aje kwenu, nami nilimtuma pamoja na ndugu yetu. Je, Tito aliwatumia ninyi ili kujipatia faida? Je, hatuenendi kwa Roho mmoja ? Je, hatuchukui hatua zile zile ?

19Je, mmekuwa mkifikiri kwamba sisi tunajaribu kujitetea mbele yenu ? Sisi tumekuwa tukinena mbele za Mungu kama wale walio katika Kristo na cho chote tufanyacho, ndugu wapendwa ni kwa ajili ya kuwatia nguvu. 20Kwa kuwa nina hofu ya kwamba nitakapokuja naweza kuwakuta nisivyotaka, nanyi mkanikuta msivyotaka, nina hofu kwamba panaweza kuwa na ugomvi, wivu, gadhabu, fitina, masingizio, masengenyo, majivuno na machafuko. 21Nina hofu kwamba nitakapokuja tena kwenu, Mungu wangu atanidhili mbele yenu, nami nitasikitishwa na wengi waliotenda dhambi huko nyuma na wala hawajatubia uchafu wao, yaani, uasherati na ufisadi walioufanya.

### *Maonyo Ya Mwisho Na Salamu*

**13** Hii ndiyo mara ya tatu nikija kwenu. “Shitaka lo lote lazima lithibitishwe na mashahidi wawili au watatu.” 2Nimekwisha kuwaonya nilipokuwa pamoja nanyi mara ya pili. Sasa narudia wakati sipo, kwamba nikija tena sitawahurumia wale waliokuwa wametenda dhambi hapo awali na wengine wote, 3kwa kuwa mnadai uthibitisho kwamba Kristo anazungumza kwa kunitumia mimi. Yeye si dhaifu katika kushughulika nanyi, bali ana nguvu katikati yenu. 4Kwa kuwa alisulibiwa katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za Mungu. Vivyo hivyo, sisi tu dhaifu katika Yeye, lakini katika kuwashughulikia ninyi tutaishi pamoja Naye kwa nguvu za Mungu.

5Jichunguzeni wenyewe mwone kama mnaishi katika imani. Jipimeni wenyewe. Je, hamtambui ya kuwa Yesu Kristo Yesu yumo ndani yenu? Kama sivyo, basi, mmeshindwa kufikia kipimo hicho! 6Natumaini mtaona kuwa sisi hatukushindwa. 7Lakini tunamwomba Mungu msije mkatenda kosa lo lote, si ili sisi tuonekane kuwa tumeshinda hilo jaribio, bali ili ninyi mtende lililo haki, hata kama tutaonekana kuwa tumeshindwa. 8Kwa maana hatuwezi

[a]4 Paradiso hapa ina maana Mbinguni

kufanya lo lote kinyume na kweli, bali kuithibitisha kweli tu. 9Tunafurahi wakati wo wote sisi tunapokuwa dhaifu, lakini ninyi mkawa na nguvu. Nayo maombi yetu ni kwamba mpate kuwa wakamilifu. 10Hii ndiyo sababu ninawaandikia mambo haya wakati sipo, ili nikija nisiwe mkali katika kutumia mamlaka yangu, mamlaka Bwana aliyonipa ya kuwajenga ninyi wala si ya kuwabomoa.

***Salamu Za Mwisho***

11Hatimaye, ndugu zangu, kwaherini. Iweni wakamilifu, mkafarijike, nieni pamoja, kaeni kwa amani, naye Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi.

12Salimianeni ninyi kwa ninyi kwa busu takatifu. 13Watakatifu wote wanawasalimu.

14Neema ya Bwana Yesu Kristo na upendo wa Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote. Amen.

### *Utangulizi*

Nadharia ya Galatia ya kaskazini inaeleza kuwa Paulo aliandika waraka huu kwa makanisa aliyoanzisha katika safari yake ya pili na ya tatu ya kitume*(Mdo.16:6 0; 18: 23).*

Paulo alikuwa amewahubiria watu wa Galatia katika safari yake ya kwanza ya kueneza Injili (*Matendo 13:14-14:23).* Baada ya yeye kuondoka, kikundi cha Wayahudi walioamini walifika, wakaanza kusisitiza kwamba ni lazima watu Mataifa walioamini watimize kwanza sheria za Mose ili wapate kuokoka. Paulo anaandika kupinga mafundisho hayo kwa kuonyesha jinsi ambavyo Abrahamu, ambaye aliishi miaka 400 kabla ya sheria ya Mose kutolewa, alivyookolewa kwa imani. Anaonyesha kwamba, kama vile ambavyo sheria haiwezi kumwokoa mtu, hakuna mtu anayeweza kuwa mkamilifu kwa kujitahidi kwa uwezo wake mwenyewe katika kutimiza sheria. Paulo anakazia hoja hiyo kwa kuthibitisha jinsi ambavyo yeye mwenyewe ni mtume wa Kristo na kwa kutoa mafundisho kuhusu jinsi mkristo anavyopaswa kuishi.

### *Wazo kuu*

Paulo anatetea kwa bidii kweli ya Injili ambayo kiini chake ni kwamba, 'Mtu anaokolewa kwa neema ya Mungu kwa kumwamini Kristo.' Mtu anayeongeza cho chote katika ukweli huu anapotosha kweli ya Mungu. *(1:7).* Tunahesabiwa haki mbele za Mungu kwa njia ya imani *(2:16)* na tunakuwa watoto wa Mungu (watoto wa Abrahamu) kwa njia iyo hiyo, yaani, kwa imani *(3:7)* . Kwa kuwa Kristo anatuweka huru, basi tusimruhusu mtu ye yote aturudishe kwenye mawazo ya kudhania kuwa matendo ya sheria yanatosha kutupatia wokovu. Kama watu waliookolewa kwa neema, tuna wajibu wa kuishi maisha yanayolingana na imani yetu. Hii ina maana kwamba inatupasa kumtii Roho Mtakatifu *(5:16)* na kumpenda jirani kama tunavyojipenda wenyewe *(* 5:14).Paulo anafanya masahihisho ya injili iliyohubiriwa na Wakristo wa Kiyahudi waliosisitiza kwamba ni lazima Wakristo wa watu Mataifa wafuate taratibu fulani fulani za Kiyahudi za Agano la Kale hasa kutahiriwa.Mtume Paulo anaonyesha kwamba kanuni ya mtu kuokolewa ni kwa njia ya imani katika Yesu Kristo.

### *Tarehe*

Tarehe ya makisio inaweza ikawa kati ya 53 na 57B.K., kufuatana na nadharia hiyo ya Galatia ya Kaskazini. Lakini nadharia ya Galatia ya Kusini inaufanya waraka huu uwe umeandikwa kati ya 48 na 49 B.K. mara tu baada ya lile baraza lililokaa Yerusalemu *(Mdo.15.)* Kufuatana na nadharia hii ya Galatia ya Kusini, makanisa Paulo anayosema nayo ni yale ya Antiokia ya Pisidia, Ikonio, Listra, na Deribe, ambayo ni makanisa katika sehemu ya kusini mwa Galatia Paulo aliyoyaanzisha katika safari yake ya kwanza ya *( Mdo.13 -14 )* kuitume.

Ikiwa nadharia hii ya Galatia ya Kusini itakubalika ,basi waraka huu utakuwa ndio wa awali kabisa kuandikwa na Paulo.Unaeleza juu ya upungufu wa rejea za baraza la Yerusalemu ambalo lilifanyika ili kushughulikia tatizo Paulo analokabiliana nalo katika waraka huu, yaani, uhusiano kati ya sheria za dini ya Kiyahudi na imani katika Kristo.

### *Mahali*

Waraka huu uliandikwa toka Rumi.

### *Mgawanyo*

- Paulo atetea Injili na mamlaka yake ya mtume (1:1-2:21)
- Kuwekwa huru kutokana na sheria (3:1-24)
- Ukuu wa Injili juu ya sheria (3:25-4:31)
- Uhuru wa Mkristo (5:1-26)
- Mawaidha kuhusu mwenendo wa Mkristo (6:1-18).

### *Salamu*

1 Paulo, mtume, si mtume wa wanadamu
aliyetumwa na mwanadamu, bali na Yesu Kristo
na Mungu Baba aliyemfufua Yesu kutoka kwa
wafu 2na ndugu wote walio pamoja nami,

Kwa makanisa ya Galatia:

3Neema iwe nanyi na amani kutoka kwa
Mungu Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu
Kristo, 4aliyejitoa kwa ajili ya dhambi zetu ili
apate kutuokoa kutoka katika ulimwengu huu
mbaya, sawasawa na
mapenzi yake Yeye aliye Mungu na Baba yetu.
5Utukufu una Yeye milele na milele. Amen.

### *Hakuna Injili Nyingine*

6Nashangaa kwamba mnamwacha upesi
hivyo Yeye aliyewaita kwa neema ya Kristo na
kuifuata injili nyingine, 7ambayo kwa kweli si injili
kamwe, ila kwa dhahiri kuna watu
wanaowachanganya na wanaotaka kuipotosha
Injili ya Kristo. 8Lakini hata ikiwa sisi au malaika
atokaye mbinguni akihubiri injili nyingine tofauti
na ile tuliyowahubiria sisi, basi huyo mtu na
alaaniwe! 9 Kama vile tulivyokwisha kusema
kabla, sasa nasema tena, ikiwa mtu ye yote
atawahubiria injili kinyume na ile mliyoipokea na
alaaniwe milele!

10Je, sasa mimi ninatafuta kukubaliwa na
wanadamu au kukubaliwa na Mungu? Au
nataka kuwapendeza wanadamu? Kama
ningekuwa najaribu kuwapendeza wanadamu,
nisingekuwa mtumishi wa Kristo.

### *Paulo Aitwa Na Mungu*

11Ndugu zangu, nataka mjue kwamba Injili
niliyowahubiria haikutokana na wanadamu.
12Kwa maana mimi sikuipokea hiyo Injili kutoka
kwa mwanadamu, wala sikufundishwa na mtu,
bali niliipata kwa ufunuo kutoka kwa Yesu
Kristo.

13Ninyi mmekwisha kusikia juu ya maisha
yangu ya zamani nilipokuwa katika dini ya
Kiyahudi, jinsi nilivyolitesa Kanisa la Mungu kwa
nguvu na kujaribu kuliangamiza. 14Nami
niliendelea sana katika dini ya Kiyahudi kuliko
Wayahudi wengi wa rika yangu maana nilikuwa
na bidii kubwa katika desturi za baba zangu.
15Lakini ilipompendeza Mungu, aliyenitenga
tangu tumboni mwa mama yangu na kuniita kwa
neema yake, 16alimdhihirisha Mwanawe
kwangu, ili nipate kumhubiri miongoni mwa
watu Mataifa. Mimi sikushauriana na
mwanadamu ye yote, 17wala sikupanda kwenda
Yerusalemu kwa hao waliokuwa mitume kabla
yangu, bali nilikwenda mara moja Arabuni na
kisha nikarudi Dameski.

18Kisha baada ya miaka mitatu nilipanda
kwenda Yerusalemu kuonana na Kefa na nilikaa
naye siku kumi na tano. 19Lakini sikuwaona
mitume wengine wo wote isipokuwa Yakobo,
ndugu yake Bwana. 20Nawahakikishia mbele za
Mungu kuwa ninayowaandikia si uongo.
21Baadaye nilikwenda sehemu za Syria [a] na
Kilikia. 22 Lakini mimi binafsi sikujulikana kwa
makanisa ya huko Uyahudi yaliyo katika Kristo.
23Wao walisikia habari tu kwamba, “Mtu yule
ambaye hapo kwanza alikuwa akitutesa sasa
anahubiri imani ile ile aliyokuwa akitaka
kuiangamiza.” 24Kwa hiyo wakamtukuza Mungu
kwa sababu yangu.

### *Paulo Akubaliwa Na Mitume*

2 Kisha, baada ya miaka kumi na minne,
nilipanda tena kwenda Yerusalemu pamoja
na Barnaba, nikamchukua na Tito ili awe
pamoja nami. 2Nilikwenda kwa sababu
nilikuwa nimefunuliwa na Mungu, kwamba
nikawaeleze kwa faragha wale walioonekana
kuwa viongozi, ile Injili ninayohubiri kwa watu
Mataifa. Nilifanya hivyo kwa kuhofia kwamba
nisije nikawa nilikuwa ninakimbia au nilikimbia
bure. 3Lakini hata Tito ambaye alikuwa
Myunani, hakulazimika kutahiriwa. 4 Lakini kwa
sababu ya ndugu wa uongo ambao walijiingiza
kwa siri katikati yetu ili kupepeleza uhuru wetu
tulio nao katika Kristo Yesu, wapate kututia
utumwani, 5hatukukubaliana nao hata dakika
moja, ili kwamba ukweli wa Injili ubaki nanyi.
6Kwa habari ya wale waliokuwa wakubaliwe
kuwa viongozi (kwangu mimi sikujali vyeo vyao,
maana Mungu hana upendeleo), wale watu
hawakuniongezea cho chote. 7Badala yake
walitambua kwamba nilikuwa nimekabidhiwa kazi
ya kuhubiri Iinjili kwa watu Mataifa kama vile Petro
alivyokabidhiwa kuhubiri Injili kwa Wayahudi.
8Kwa maana, Mungu aliyekuwa akitenda kazi
katika huduma ya Petro kama mtume kwa
Wayahudi, ndiye pia aliyekuwa anatenda kazi
katika huduma yangu kama mtume kwa watu
Mataifa. 9Basi, Yakobo, Kefa na Yohana,
walionekana kama nguzo za kanisa, walitupa
mkono wa shirika, mimi na Barnaba walipotambua
ile neema niliyopewa. Wakakubali

[a]21 Syria hapa ina maana ya Shamu

kwamba sisi tuende kwa watu Mataifa na wao waende kwa Wayahudi. 10 Walichotuomba ni kwamba tuendelee kuwakumbuka maskini, jambo ambalo ndilo nililokuwa na shauku ya kulifanya.

### *Paulo Ampinga Petro Huko Antiokia*

11 Lakini Petro alipofika Antiokia, mimi nilimpinga ana kwa ana kwa sababu alikuwa amekosea kwa wazi. 12 Kabla baadhi ya watu waliotoka kwa Yakobo hawajafika, alikuwa akila pamoja na watu Mataifa. Lakini hao watu walipofika alianza kujiondoa na kujitenga na watu Mataifa kwa sababu aliwaogopa wale wa kundi la tohara. 13 Pia Wayahudi wengine waliungana naye katika unafiki huu, hata Barnaba naye akapotoshwa na unafiki wao.

14 Nilipoona kwamba hawatendi sawasawa na kweli ya Injili, nilimwambia Petro mbele ya wote, "Wewe ni Myahudi, nawe unaishi kama mtu Mataifa na wala si kama Myahudi. Imekuwaje basi, mnawalazimisha watu Mataifa kufuata desturi za Kiyahudi?

### *Wayahudi Na Watu Mataifa Wanaokolewa Kwa Imani*

15 "Sisi wenyewe ni Wayahudi wa kuzaliwa na si watu wenye dhambi kama watu Mataifa, 16 lakini tunajua ya kwamba mtu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria bali kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Nasi tumemwamini Kristo Yesu ili tupate kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika Kristo, wala si kwa matendo ya sheria.

17 "Lakini ikiwa katika jitihada yetu ya kuhesabiwa haki katika Kristo, sisi tumeonekana dhahiri kwamba ni wenye dhambi, je, ina maana kwamba Kristo amekuwa mtumishi wa dhambi? La hasha! 18 Lakini ikiwa mimi ninajenga tena kile ambacho nimekwisha kukibomoa, basi ninaonyesha kwamba mimi ni mkosaji. 19 Kwa maana mimi kwa njia ya sheria, nimeifia sheria ili nipate kuishi kwa ajili ya Mungu. 20 Nimesulibiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu. 21 Siibatilishi neema ya Mungu, kwa maana kama haki ingeweza kupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure!''

### *Imani Au Kushika Sheria*

## 3

Ninyi Wagalatia wajinga! Ni nani aliyewaloga? Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele yenu kwamba amesulibiwa. 2 Nataka nijifunze neno moja kutoka kwenu: Je, mlipokea Roho wa Mungu kwa kushika sheria, au kwa kuyaamini yale mliyosikia? 3 Je, ninyi ni wajinga kiasi hicho? Baada ya kuanza kwa Roho, je, sasa mwataka kukamilishwa katika mwili? 4 Je, mlipata mateso kiasi hicho bure? Ni kama kweli yalikuwa bure? 5 Je, Mungu huwapa Roho Wake na kufanya miujiza katikati yenu kwa sababu mnatii sheria, au kwa sababu mnaamini kile mlichosikia?

6 Kama vile Abrahamu, ''Yeye alimwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa haki.'' 7 Hivyo basi mjue kwamba wale wanaomwamini Mungu hao ndio watoto wa Abrahamu. 8 Maandiko yakitabiri kwamba Mungu angewahesabia haki watu Mataifa kwa imani, alitangulia kumtangazia Abrahamu Injili akisema kwamba, "Kwa kupitia kwako mataifa yote yatabarikiwa." 9 Kwa sababu hii, wale wote wanaoamini wanabarikiwa pamoja na Abrahamu, mtu wa imani.

### *Sheria Na Laana*

10 Kwa maana wote wanaotumainia matendo ya sheria, wako chini ya laana, kwa kuwa imeandikwa, "Amelaani mtu yule asiyeshika na kutii mambo yote yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria.'' 11 Basi ni dhahiri kwamba hakuna mtu ye yote anayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa sheria, kwa maana, "Mwenye haki ataishi kwa imani". 12 Lakini sheria haitegemei imani, kinyume chake, "Ye yote atendaye matendo ya sheria ataishi kwa sheria." 13 Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana imeandikwa, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti." 14 Alitukomboa ili kwamba baraka aliyopewa Abrahamu ipate kuwafikia watu Mataifa kwa njia ya Kristo Yesu, ili kwa imani tupate kupokea ile ahadi ya Roho.

### *Sheria Na Ahadi*

15 Ndugu zangu, nataka nitoe mfano kutoka katika maisha ya kila siku. Kama vile hakuna mtu awezaye kutangua au kuongeza kitu katika agano la mtu ambalo limekwisha kuthibitishwa, vivyo hivyo kwa hali kama hii. 16 Ahadi zilinenwa kwa Abrahamu na kwa mzao wake. Maandiko hayasemi, "Kwa wazao," likimaanisha watu wengi, bali "Ni kwa mzao wako", yaani, mtu mmoja, ndiye Kristo. 17 Ninachotaka kusema ni

kwamba, sheria, ambayo ilitolewa miaka 430 baadaye, haitangui agano lililothibitishwa na Mungu ili kulibatilisha. 18 Kwa maana kama urithi hupatikana kwa sheria, basi hautegemei tena ahadi, lakini Mungu kwa neema Yake alimpa Abrahamu urithi kwa njia ya ahadi.

### *Kusudi La Sheria*

19 Kwa nini basi iwepo sheria? Sheria iliwekwa kwa sababu ya makosa mpaka atakapokuja yule mzao wa Abrahamu, ambaye alitajwa katika ile ahadi. Sheria iliamuriwa na malaika kwa mkono wa mpatanishi. 20 Basi mpatanishi huhusisha zaidi ya upande mmoja, lakini Mungu ni mmoja.

21 Je, basi, sheria inapingana na ahadi za Mungu? La hasha! Kwa maana kama sheria iliyotolewa ingeweza kuwapa watu uzima, basi haki ingepatikana kwa njia ya sheria. 22 Lakini Maandiko yamefanya vitu vyote vifungwe chini ya nguvu ya dhambi, ili yale yaliyoahidiwa kwa njia ya imani katika Yesu Kristo yapate kupewa wale wanaoamini.

23 Kabla imani haijaja tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ile imani ifunuliwe. 24 Hivyo, sheria ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Kristo, ili tupate tuhesabiwa haki kwa imani. 25 Lakini sasa kwa kuwa ile imani imekuja, hatusimamiwi tena na sheria.

### *Watoto Wa Mungu*

26 Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani. 27 Kwa maana wote mliobatizwa ndani ya Kristo, mmemvaa Kristo. 28 Wala hakuna tena Myahudi au Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume wala mwanamke, maana nyote mmekuwa wamoja ndani ya Kristo Yesu. 29 Nanyi mkiwa ni mali ya Kristo, basi ninyi ni wa uzao wa Abrahamu na warithi sawasawa na ile ahadi.

**4** Lile nisemalo ni kwamba wakati wote mrithi akiwa bado ni mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ndiye mmiliki wa mali yote. 2 Yeye huwa yuko chini ya uangalizi wa walezi na wadhamini mpaka ufike wakati uliowekwa na baba yake. 3 Vivyo hivyo na sisi, tulipokuwa bado watoto wadogo, tulikuwa utumwani chini ya taratibu za kawaida za ulimwengu. 4 Lakini ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe, ambaye alizaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, 5 kusudi awakomboe wale waliokuwa chini ya sheria, ili tupate kupokea zile haki kamili za kufanywa watoto wa Mungu. 6 Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, anayelia, "Abba[a]! Yaani, Baba." 7 Kwa hiyo, wewe si mtumwa tena, bali ni mtoto, nawe ikiwa ni mtoto, basi wewe pia ni mrithi, mrithi wa Mungu.

### *Paulo Awakemea Wagalatia*

8 Zamani, mlipokuwa hamumjui Mungu, mlikuwa mkitumikia viumbe ambavyo kwa asili si Mungu. 9 Lakini sasa kwa kuwa mmemjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, inakuwaje mnarejea tena katika zile kanuni za kwanza zenye udhaifu na upungufu ambazo mnataka ziwafanye tena watumwa? 10 Mnaadhimisha siku maalum, miezi, nyakati na miaka! 11 Nina hofu juu yenu, kwamba kazi niliyofanya kwa ajili yenu inaweza kuwa nimejitaabisha bure.

12 Ndugu zangu, nawasihi mwe kama mimi, kwa sababu mimi nimekuwa kama ninyi. Hamkunitendea jambo lo lote baya. 13 Ninyi mwajua kwamba ni kwa ajili ya udhaifu wangu niliwahubiria injili, 14 ingawa hali yangu iliwatia majaribuni, hamkunidharau wala kunidhihaki, bali mlinikaribisha kama malaika wa Mungu, kama vile Kristo Yesu. 15 Ile hali ya furaha mliyokuwa nayo imekwenda wapi ? Naweza kushuhudia kwamba, kama ingewezekana mngeng'oa macho yenu na kunipa mimi. 16 Je, sasa nimekuwa adui yenu kwa kuwaambia kweli?

17 Hao wana shauku ya kuwapata lakini si kwa kusudi zuri. Wanachotaka ni kuwatenga mbali nasi, ili ninyi mpate kuwaonea wao shauku. 18 Ni vizuri wakati wote kuwa na shauku kwa ajili ya kusudi nzuri, si wakati nikiwa pamoja nanyi tu. 19 Watoto wangu wapendwa, ambao kwa mara nyingine ninawaonea utungu, ninatamani kwamba Kristo aumbike ndani yenu. 20 Natamani kama ningekuwa pamoja nanyi sasa, pengine ningebadilisha sauti yangu. Kwa maana nina wasiwasi kwa ajili yenu.

### *Mfano Wa Hajiri Na Sara*

21 Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, je, hamjui sheria inavyosema? 22 Kwa maana imeandikwa kwamba Abrahamu alikuwa na wana wawili, mmoja wa mwanamke mtumwa na wa pili wa mwanamke huru. 23 Lakini, mtoto wa mwanamke mtumwa alizaliwa kwa mapenzi

---

[a] 6 "Abba" hapa ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni "baba"ambalo lingeweza kutumiwa tu na mtoto a kuzaa.

ya mwili na yule mwingine wa mwanamke huru
alizaliwa kutokana na ahadi ya Mungu.

24 Mambo haya yanaweza kuchukuliwa
kama mfano. Kwa maana hao wanawake wawili
ni mfano wa maagano mawili: Agano la kwanza,
ni lile lililofanyika katika mlima wa Sinai, lizaalo
watoto wa utumwa. Hili ndilo huyo Hajiri. 25Basi
Hajiri anawakilisha mlima Sinai ulioko Arabuni
na unafanana na Yerusalemu ya sasa ambayo
iko utumwani pamoja na watoto wake. 26Lakini
Yerusalemu wa juu ni huru, nayo ndiye mama
yetu. 27Kwa maana imeandikwa:

"Furahi, wewe uliyetasa
 wewe usiyezaa,
paza sauti, imba kwa furaha,
 wewe usiyepatwa na utungu,
kwa maana watoto wa mwanamke
  aliyeachwa ni wengi
 kuliko watoto wa yule aliye na mume.''

28Basi, sisi ndugu zangu, ni kama Isaki, tu
watoto wa ahadi. 29Lakini, kama vile ilivyokuwa
siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili
alivyomchokoza yule aliyezaliwa kwa Roho,
ndivyo ilivyo hata sasa. 30Lakini maandiko
yasemaje? "Mwondoe mwanamke mtumwa
pamoja na mwanawe, kwa sababu mwana wa
mtumwa kamwe hatarithi pamoja na mwana wa
aliye huru." 31Kwa hiyo ndugu zangu, sisi si
wana wa mwanamke mtumwa bali wa yule aliye
huru.

### *Uhuru Ndani Ya Kristo*

5 Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru. Hivyo
simameni imara wala msikubali
tena kulemewa na kongwa la utumwa.
2Sikilizeni! Mimi Paulo nawaambieni
kwamba kama mkikubali kutahiriwa, basi Kristo
hatawafaidia cho chote. 3Namshuhudia tena kila
mtu anayekubali kutahiriwa kwamba inampasa
kushika sheria yote. 4 Ninyi mnaotafuta
kuhesabiwa haki kwa njia ya sheria mmetengwa
na Kristo, mko mbali na neema ya Mungu. 5Kwa
maana, kwa njia ya Roho kwa imani, tunangojea
kwa shauku tumaini la haki. 6Kwa maana ndani
ya Kristo, kutahiriwa au kutotahiriwa hakuleti
tofauti, bali lililo muhimu ni imani itendayo kazi
kwa njia ya upendo.

7Mlikuwa mkipiga mbio vizuri, ni nani
aliyewazuia msiitii kweli? 8Ushawishi wa namna
hiyo hakutokani na yule anayewaita. 9 Chachu
kidogo kuchachua donge zima. 10Nina hakika
katika Bwana kwa habari yenu kwamba
hamtakuwa na msimamo mwingine. Mtu awaye
yote anayewachanganya anastahili adhabu.
11Lakini ndugu zangu, kama mimi bado
ninahubiri kuhusu kutahiriwa, kwa nini basi bado
niteswe na Wayahudi? Ukweli kwamba bado
wananitesa, ni ushahidi kwamba bado
ninahubiri wokovu kupitia msalaba wa Kristo
peke yake. 12Laiti hao wanaowavuruga
wangejihasi wao wenyewe!

13 Ndugu zangu, ninyi mliitwa ili mwe huru,
hivyo msitumie uhuru wenu kama fursa ya
kufuata tamaa za mwili, bali tumikianeni ninyi
kwa ninyi kwa upendo. 14Kwa maana sheria
yote hukamilika katika amri moja: "Mpende jirani
yako kama nafsi yako." 15Kama mkiumana na
kutafunana, angalieni, msije mkaangamizana.

### *Maisha Ya Kiroho*

16Kwa hiyo nasema, enendeni kwa Roho,
wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.
17Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo
kinyume na Roho, nayo Roho hutamani yale
yaliyo kinyume na mwili. Roho na mwili
hupingana na kwa sababu hiyo hamwezi
kufanya mnayotaka. 18Lakini kama mkiongozwa
na Roho, hamko chini ya sheria.

19 Basi matendo ya mwili ni dhahiri nayo ni
haya: Uasherati, uchafu, ufisadi, 20kuabudu
sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira,
fitina, faraka, uzushi, 21husuda, ulevi, ulafi na
mambo mengine yanayofanana na hayo.
Nawaonya, kama nilivyokwisha kuwaonya
kabla, kwamba watu watendao mambo kama
hayo, hawataurithi Ufalme wa Mungu.

22Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha,
amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu,
23upole, kiasi. Katika mambo kama haya
hakuna sheria. 24Wote walio wa Kristo Yesu
wameusulibisha mwili pamoja na tamaa zake.
25Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, basi na
tuenende kwa Roho. 26Tusijisifu bure,
tukichokozana na kuoneana wivu.

### *Chukulianeni Mizigo*

6 Ndugu zangu, kama mtu akipatikana na
dhambi fulani, basi ninyi mlio wa rohoni, mrejezeni
upya mtu huyo kwa roho ya upole. Lakini
jihadharini, ili ninyi wenyewe msije mkajaribiwa.
2Chukulianeni mizigo ninyi kwa ninyi, nanyi kwa
njia hii mtatimiza sheria ya Kristo. 3Kama mtu ye
yote akijiona kuwa yeye ni
bora na kumbe sivyo, basi mtu huyo

anajidanganya mwenyewe. 4 Lakini kila mtu na
aipime kazi yake mwenyewe, ndipo aweze
kujisifu, bila kujilinganisha na mtu mwingine.
5 Kwa maana, kila mtu atauchukua mzigo wake
mwenyewe. 6 Basi, yeye afundishwaye katika
neno na amshirikishe mwalimu wake mema
yote.

7 Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa
kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna.
8 Apandaye kwa mwili, katika mwili wake,
atavuna uharibifu, lakini yeye apandaye katika
Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.
9 Hivyo, tusichoke katika kutenda mema, kwa
kuwa tutavuna kwa wakati wake tusipokata
tamaa. 10 Kwa hiyo, kadiri tupatavyo nafasi na
tuwatendee watu wote mema, hasa wale wa
jamaa ya waaminio.

### *Si Kutahiriwa Bali Kiumbe Kipya*

11 Angalieni ni herufi gani kubwa nitumiazo
ninapowaandikia kwa mkono wangu
mwenyewe!

12 Wale wanaotaka kuonekana wazuri kwa
mambo ya mwili wanaotaka wawalazimishe
kutahiriwa, sababu pekee ya kufanya hivyo ni
kuepuka kuteswa kwa ajili ya msalaba wa
Kristo. 13 Hata wale waliotahiriwa wenyewe
hawaitii sheria, lakini wanataka ninyi mtahiriwe
ili wapate kujivuna kwa habari ya miili yenu.
14 Mungu apishie mbali nisije nikajivunia kitu cho
chote isipokuwa msalaba wa Bwana wetu Yesu
Kristo, ambaye kwa Yeye ulimwengu
umesulibiwa kwangu, nami nimesulibiwa kwa
ulimwengu. 15 Kwa maana katika Kristo Yesu
kutahiriwa au kutokutahiriwa si kitu, bali kule
kuwa kiumbe kipya ni kila kitu! 16 Amani na
rehema viwe na wote wanaofuata kanuni hii na
juu ya Israeli wa Mungu.

17 Hatimaye, tangu sasa mtu ye yote
asinitaabishe, kwa maana nachukua katika mwili
wangu chapa Zake Yesu.

18 Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu
Yesu Kristo ikae pamoja na roho zenu. Amen.

**WAEFESO**

### *Utangulizi*

Paulo aliandika waraka huu akiwa gerezani huko Rumi ili kuwatia moyo waamini wa Asia.Unaposoma kwa uangalifu waraka huu, ingawa Paulo alifungwa huko Kaisaria, utaona kwamba waraka huu uliandikwa kutoka Rumi ambako Paulo alikuwa na uhuru wa kuhubiri Injili *(Mdo.28)*.Waraka huu ulikuwa kama mwongozo uliokusudiwa kwa makanisa kadhaa.Katika maandiko mengine ya zamani neno "huko Efeso" halipo. Zaidi ya hayo, kwenye waraka huu hakuna salamu za watu binafsi, wala hakuna matatizo maalum au hali maalum ya kanisa la mahali pamoja inayotajwa. Pia mafundisho yaliyomo ni yenye upana mkubwa.Ingawa kanisa la Efeso ambako Paulo alihudumu kwa zaidi ya miaka miwili linajumuishwa humo, ni wazi kwamba waraka huu ulikusudiwa kwa makundi mengine ya kanisa kwa ujumla katika eneo hilo la kijeografia la Efeso, yaani, makanisa ya jirani.

Katika waraka huu, Paulo anapotaja "Kanisa" ana maana ya "Kanisa la po pote." Anaeleza kwamba Kanisa limeanzishwa na Mungu, akiwaelezea mpango wa Mungu wa tangu awali wa kuwaokoa watu Wake kwa njia ya Kristo. Mpango huu ulikuwako hata kabla ya ulimwengu kuumbwa. Kwa wakati huu, wote wanaomwamini Kristo wanaokolewa kwa neema. Mwenendo wa mwamini uko kinyume kabisa na ule wa maisha ya kale, akionyesha maisha ya kiroho kama "maisha katika ulimwengu wa roho". Ingawa inawapasa watu wa Mungu kupigana vita kali na nguvu za Shetani *(6:12),* kanisa linashinda na hatimaye uovu unashindwa.Sisi tunaomwamini Kristo ni viungo vya mwili Wake, yaani, Kanisa, kwa hiyo tunao uwezo wa kushinda.

Katika sehemu ya mwisho ya waraka huu, Paulo anaeleza juu ya maisha yanayowapasa wakristo kuhusu: Ndoa, tabia, mwenendo, wazazi na watoto wao pia watumishi na mabwana zao.

### *Wazo Kuu*

Kiini cha ujumbe wa waraka huu ni kwamba: Mpango wa Mungu wa milele wa kuuokoa ulimwengu unatimizwa kwa njia ya Kristo katika mwili Wake, yaani, Kanisa Lake. Mtu anapoamini, anakuwa ndani ya Kristo na anapata wokovu na kuwa salama. Mungu aliandaa wokovu huu tangu milele na amempa kila aaminiye mambo yote anayohitaji katika maisha yake ili aweze kusimama, ila ni wajibu wake kupokea mambo hayo aliyowekewa tayari. Paulo anamalizia kwa kufafanua mambo ambayo Mungu amewaandalia wale wamwaminio, kusudi waweze kumshinda Shetani anapowashambulia na baada ya mapambano wawe na ushindi wa kudumu.

### *Mwandishi*

Mwandishi wa waraka huu ni Paulo *(1:1).*

### *Tarehe*

Waraka huu uliandikwa 60 B.K.wakati wa kifungo cha Paulo cha miaka miwili.

### *Mahali*

Rumi.

### *Mgawanyo*

- Mpango wa Mungu na wokovu wa wote wamwaminio (1:1-2:22)
- Siri ya Injili (3:1-21)
- Maisha ya mkristo duniani (4:1-5:21)
- Jinsi wakristo wapaswavyo kuhusiana (5:22-6:9)
- Kupigana na uovu (6:10-24)

### *Salamu*

**1** Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu,

Kwa watakatifu walioko Efeso walio waaminifu katika Kristo Yesu.

2Neema na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Baraka Za Kiroho Zitokazo Kwa Kristo*

3Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyetubariki sisi kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo. 4 Kwa maana alituchagua katika Yeye kabla ya kuumbwa ulimwengu ili tuwe watakatifu na bila lawama mbele Zake. 5Kwa upendo alitangulia kutuchagua tuwe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo kwa furaha Yake na mapenzi Yake mwenyewe. 6Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. 7 Katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu Yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake 8aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na maarifa yote. 9Naye alitujulisha siri ya mapenzi Yake sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake, ambayo alikusudia katika Kristo, 10ili yapate kutimizwa katika wakati mkalimifu utakapowadia, yaani, kuvitia vitu vyote vya mbinguni na vya duniani pamoja chini ya kiongozi mmoja, ndiye Krsto.

11Katika Kristo sisi nasi tumepata urithi, tukiisha kuchaguliwa sawasawa na kusudi la Mungu, Yeye ambaye hufanya mambo yote kulingana na mapenzi Yake. 12 Ili kwamba, sisi tuliokuwa wa kwanza kuweka tumaini katika Kristo, tupate kuishi kwa sifa ya utukufu Wake. 13Ninyi pia mliingia ndani ya Kristo mliposikia Neno la kweli, Injili ya wokovu wenu. Mkiisha kuamini, ndani yake mlitiwa mhuri, kwa yule Roho Mtakatifu wa ahadi mliyeahidiwa, 14yeye ndiye amana ya urithi wetu hadi ukombozi wa milki yake kuwa sifa ya utukufu Wake.

### *Shukrani Na Maombi*

15 Kwa sababu hii tangu niliposikia juu ya imani yenu katika Bwana Yesu na upendo wenu kwa watakatifu wote, 16sijaacha kumshukuru Mungu kwa ajili yenu, nikiwakumbuka katika maombi yangu. 17Nazidi kumwomba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awajalieni ninyi roho ya hekima na ya ufunuo, ili mpate kumjua zaidi. 18 Ninaomba pia kwamba macho ya mioyo yenu yatiwe nuru ili mpate kujua tumaini mliloitiwa, utajiri wa urithi wa utukufu Wake kwa watakatifu 19na uweza Wake mkuu usiolinganishwa kwa ajili yetu sisi tuaminio. Uweza huo unaofanya kazi ndani yetu, ni sawa na ile nguvu kuu mno 20ambayo aliitumia alipomfufua Kristo kutoka kwa wafu, akamketisha mkono Wake wa kuume katika mbingu, 21juu sana kuliko falme zote na mamlaka, enzi na milki na juu ya kila jina litajwalo, si katika ulimwengu huu tu, bali na katika ule ujao pia. 22Naye Mungu ameweka vitu vyote viwe chini ya miguu Yake na amemfanya Yeye awe kichwa cha vitu vyote kwa ajili ya Kanisa, 23ambalo ndilo mwili Wake, ukamilifu Wake Yeye aliye yote katika yote.

### *Tumefanywa Kuwa Hai Ndani Ya Kristo*

**2** Kwa habari zenu, mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu, 2ambazo mlizitenda mlipofuatisha namna ya ulimwengu huu na za yule mtawala wa ufalme wa anga, yule roho atendaye kazi ndani ya wale wasiotii. 3Sisi sote pia tuliishi katikati yao hapo zamani, tukifuata tamaa za mwili na mawazo yake. Nasi kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu, kama mtu mwingine ye yote. 4Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, 5hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema. 6Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, 7ili katika ule ulimwengu ujao apate kuonyesha wingi wa neema Yake isiyopimika, iliyodhihirishwa kwetu kwa wema Wake ndani ya Kristo Yesu. 8Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, 9si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. 10 Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo.

### *Wamoja Katika Kristo*

11Kwa hiyo kumbukeni kwamba ninyi ambao hapo awali mlikuwa watu Mataifa kwa kuzaliwa mlioitwa, “Wasiotahiriwa” na wale wanaojiita “Waliotahiriwa,” yaani, tohara (ifanyikayo katika

mwili kwa mikono ya wanadamu), 12kumbukeni kwamba wakati ule mlikuwa hamna Kristo, mkiwa wageni katika jumuiya ya watu wa Mungu, yaani, Israeli na wageni katika lile agano la ahadi, mliishi duniani mkiwa hamna tumaini wala Mungu. 13Lakini sasa katika Kristo Yesu, ninyi ambao hapo kwanza mlikuwa mbali na Mungu, sasa mmeletwa karibu kwa njia ya damu ya Kristo.

14Kwa maana Yeye mwenyewe ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi tuliokuwa wawili, yaani, Wayahudi na watu Mataifa tuwe wamoja kwa kuvunja kizuizi na kubomoa ule ukuta wa uadui uliokuwa kati yetu. 15Kwa kuibatilisha ile sheria pamoja na amri zake na maagizo yake alipoutoa mwili wake, ili apate kufanya ndani yake mtu mmoja mpya badala ya hao wawili, hivyo akifanya amani, 16naye katika mwili huu mmoja awapatanishe wote wawili na Mungu kwa kupitia msalaba, ambao kwa huo aliangamiza uadui wao. 17Alikuja na kuhubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali na pia akahubiri amani kwao waliokuwa karibu. 18Kwa maana kwa kupitia Kwake, sisi sote tunaweza kumkaribia Baba katika Roho mmoja.

19Hivyo basi, ninyi sasa si wageni tena wala wapitaji, bali mmekuwa wenyeji pamoja na watakatifu na pia jamaa wa nyumbani Mwake Mungu. 20Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ndiye jiwe kuu la pembeni. 21Ndani Yake jengo lote limeshikamanishwa pamoja na kusimamishwa ili kuwa hekalu takatifu katika Bwana. 22Katika Yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja ili mpate kuwa makao ambayo Mungu anaishi ndani yake kwa njia ya Roho Wake.

### *Huduma ya Paulo kwa Watu Mataifa*

**3** Kwa sababu hii, mimi Paulo, nimekuwa mfungwa wa Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi watu Mataifa.

2Kwa hakika mmekwisha kusikia kuhusu ile huduma ya neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu 3na jinsi ile siri ilivyodhihirishwa kwangu kwa njia ya ufunuo, kama nilivyotangulia kuandika kwa kifupi. 4Kwa kusoma haya, basi mtaweza kuelewa ufahamu wangu katika siri ya Kristo. 5Siri hii haikudhihirishwa kwa wanadamu katika vizazi vingine kama vile sasa ilivyodhihirishwa na Roho kwa mitume na manabii watakatifu wa Mungu. 6Siri hii ni kwamba, kwa njia ya Injili, watu Mataifa ni warithi pamoja na Israeli, viungo vya mwili mmoja na washiriki pamoja wa ahadi katika Kristo Yesu.

7Nimekuwa mtumishi wa Injili hii kwa kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa nguvu Yake itendayo kazi. 8Ingawa mimi ni mdogo kuliko aliye mdogo kabisa miongoni mwa watakatifu wote, nilipewa neema hii ili niwahubirie watu Mataifa kuhusu utajiri usiopimika ulio ndani ya Kristo na 9kuweka wazi kwa kila mtu jinsi ile siri iliyokuwa imefichwa kwa nyakati zote katika Mungu aliyeumba vitu vyote. 10Ili kwa njia ya Kanisa, hekima yote ya Mungu ipate kujulikana kwa watawala na wenye mamlaka katika ulimwengu wa roho, 11sawasawa na kusudi Lake la milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. 12 Yeye ambaye ndani Yake na kwa njia ya imani katika Yeye tuweze kumkaribia Mungu kwa ujasiri na kwa uhuru. 13Kwa hiyo, nawaomba msikate tamaa kwa sababu ya mateso yangu kwa ajili yenu, hayo ni utukufu wenu.

### *Maombi Ya Paulo Kwa Waefeso*

14Kwa sababu hii nampigia Baba magoti, 15ambaye kwa Yeye ubaba wote wa kila jamaa za mbinguni na za duniani unaitwa. 16Namwomba Mungu awaimarishe kwa kuwatia nguvu mioyo yenu kwa njia ya Roho Wake kwa kadri ya utajiri wa utukufu Wake, 17ili kwamba, Kristo apate kukaa mioyoni mwenu kwa njia ya imani. Nami ninaomba kwamba ninyi mkiwa wenye mizizi tena imara katika upendo, 18mwe na uwezo wa kufahamu pamoja na watakatifu jinsi ulivyo upana na urefu na kimo na kina upendo wa Kristo 19na kujua upendo huu kwamba unapita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu wa Mungu.

20Basi kwa Yeye awezaye kutenda mambo ya ajabu yasiyopimika kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya uweza Wake ule utendao kazi ndani yetu, 21Yeye atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu kwa vizazi vyote, milele na milele. Amen.

### *Umoja Katika Mwili Wa Kristo*

**4** Basi, mimi niliye mfungwa wa Bwana, nawasihi mwenende kama inavyostahili wito wenu mlioitiwa. 2Iweni wanyenyekevu kabisa na wapole, mkiwa wavumilivu, mkichukuliana kwa upendo. 3Jitahidini kudumisha umoja wa Roho katika kifungo cha amani. 4Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama vile mlivyoitwa katika tumaini moja. 5Tena

kuna Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja,
[6]Mungu mmoja ambaye ni Baba wa wote, aliye
juu ya yote, katika yote na ndani ya yote.

[7]Lakini kila mmoja wetu amepewa neema
kwa kadiri ya kipimo cha kipawa cha Kristo.
[8]Kwa hiyo husema,

"Alipopaa juu,
aliteka mateka
akawapa wanadamu vipawa."

[9](Asemapo "Alipaa juu," maana yake nini
isipokuwa ni kusema pia kwamba Kristo
alishuka pande za chini sana za dunia[a]? [10]Yeye
aliyeshuka ndiye aliyepaa juu sana[b], kupita
mbingu zote, ili apate kuvijaza vitu vyote.
[11]Yeye ndiye aliyeweka wengine kuwa mitume,
wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti,
wengine kuwa wachungaji na wengine kuwa
walimu, [12]kwa kusudi la kuwakamilisha
watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma, ili
kwamba mwili wa Kristo upate kujengwa.
[13]mpaka sote tutakapoufikia umoja katika imani
na katika kumjua sana Mwana wa Mungu na
kuwa watu wazima kwa kufikia kipimo cha
ukamilifu wa Kristo.

[14]Ili tusiwe tena watoto wachanga,
tukitupwatupwa huku na huku na kuchukuliwa
na kila upepo wa mafundisho kwa hila za watu,
kwa ujanja, kwa kufuata njia zao za
udanganyifu. [15]Badala yake, tukiambiana kweli
kwa upendo, katika mambo yote tutakua, hata
tumfikie Yeye aliye kichwa, yaani, Kristo.
[16]Kutoka Kwake, mwili wote huunganishwa na
kushikamanishwa pamoja kwa msaada wa kila
kiungo, hukua na kujijenga wenyewe katika
upendo, wakati kila kiungo kinafanya kazi yake.

### *Maisha Ya Zamani Na Maisha Mapya*

[17]Hivyo nawaambia hivi, nami nasisitiza
katika Bwana kwamba, msiishi tena kama watu
Mataifa waishivyo, katika ubatili wa mawazo
yao. [18]Watu hao akili zao zimetiwa giza na
wametengwa mbali na uzima wa Mungu kwa
sababu ya ujinga wao na ugumu wa mioyo yao.
[19]Wakiisha kufa ganzi, wamejitia katika mambo
ya ufisadi na kupendelea kila aina ya uchafu,
wakiendelea kutamani zaidi.

[20]Lakini ninyi, hivyo sivyo mlivyomjifunza
Kristo. [21]Kama hivyo ndivyo ilivyo, ninyi
mmemsikia, tena mmefundishwa naye, vile
kweli ilivyo katika Yesu. [22]Mlifundishwa kuuvua
mwenendo wenu wa zamani, utu wenu wa kale,
ulioharibiwa na tamaa zake za udanganyifu.
[23]Mfanywe upya roho ya nia zenu, [24]mkajivike
utu mpya, ulioumbwa sawa sawa na mfano wa
Mungu katika haki yote na utakatifu.

### *Kanuni Za Maisha Mapya*

[25]Kwa hiyo kila mmoja wenu avue uongo na
kuambiana kweli mtu na jirani yake, kwa maana
sisi sote tu viungo vya mwili mmoja.
[26]Mkikasirika, msitende dhambi, wala jua
lisichwe mkiwa bado mmekasirika, [27]wala
msimpe ibilisi nafasi. [28]Yeye ambaye amekuwa
akiiba, asiibe tena, lakini mtu wa namna hiyo
lazima ajishughulishe, tena afanye kitu kifaacho
kwa mikono yake mwenyewe, ili awe na kitu cha
kuwagawia wahitaji.

[29]Maneno mabaya yasitoke vinywani
mwenu, bali yale yafaayo kwa ajili ya kuwajenga
wengine kulingana na mahitaji yao, ili yawafae
wale wasikiao. [30]Wala msimhuzunishe Roho
Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa huyo mlitiwa
muhuri kwa ajili ya siku ya ukombozi. [31]Ondoeni
kabisa uchungu, ghadhabu, hasira, makelele na
masingizio pamoja na kila aina ya uovu. [32]
Iweni wafadhili na wenye kuhurumiana ninyi
kwa ninyi, mkisameheana, kama vile naye
Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.

### *Kuenenda Nuruni*

**5** Kwa hiyo, mfuateni Mungu kama watoto
wapendwao, [2]Mkiishi maisha ya upendo, kama vile
Kristo alivyotupenda sisi akajitoa kwa ajili yetu kuwa
sadaka yenye harufu nzuri na
dhabihu kwa Mungu.

[3]Lakini uasherati, usitajwe miongoni
mwenu, wala uchafu wa aina yo yote, wala
tamaa, kwa sababu mambo haya hayastahili
miongoni mwa watakatifu. [4]Wala pasiwepo
mazungumzo machafu ya aibu, au maneno ya
upuzi au mzaha, ambayo hayafai, badala yake
mshukuruni Mungu. [5]Kwa habari ya mambo
haya mjue hakika kwamba: Mwasherati, wala
mtu mwovu, wala mwenye tamaa mbaya, mtu
kama huyo ni mwabudu sanamu, ambaye
kamwe hataurithi Ufalme wa Kristo na wa
Mungu. [6]Mtu ye yote na asiwadanganye kwa
maneno matupu, kwa kuwa hasira ya Mungu
huwaka kwa sababu ya mambo kama haya juu

---

[a]9 Pande za chini sana za dunia hapa maana yake ni sheol kwa Kiebrania, yaani, kuzimu

[b]10 Juu sana hapa ina maana mbingu za mbingu

ya wale wasiomtii. 7Kwa hiyo, msishirikiane nao.
8Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, lakini
sasa ninyi ni nuru katika Bwana. Enendeni kama
watoto wa nuru 9(kwa kuwa tunda la nuru
hupatikana katika wema wote, haki na kweli,)
10nanyi tafuteni yale yanayompendeza Bwana.
11Msishiriki matendo ya giza yasiyofaa, bali
yafichueni. 12 Kwa maana ni aibu hata kutaja
mambo yale ambayo wasiotii wanayafanya
sirini. 13Lakini kila kitu kilichowekwa nuruni,
huonekana, 14kwa kuwa nuru ndiyo hufanya kila
kitu kionekane. Hii ndiyo sababu imesemekana:

"Amka, wewe uliyelala,
ufufuke kutoka katika wafu,
naye Kristo atakuangazia."

15Kwa hiyo iweni waangalifu jinsi
mnavyoenenda, si kama watu wasio na hekima,
bali kama wenye hekima, 16mkiukomboa wakati,
kwa sababu nyakati hizi ni za uovu. 17Kwa hiyo
msiwe wajinga, bali mpate kujua nini yaliyo
mapenzi ya Bwana. 18Pia msilewe kwa mvivyo,
ambamo ndani yake mna upotovu, bali mjazwe
Roho. 19Msemezane ninyi kwa ninyi kwa zaburi,
nyimbo na tenzi za rohoni, mkimwimbia na
kumsifu Bwana mioyoni mwenu, 20sikuzote
mkimshukuru Mungu Baba katika Jina la Bwana
wetu Yesu Kristo kwa kila jambo.

21Nyenyekeaneni ninyi kwa ninyi kwa
heshima kwa ajili ya Kristo.

### *Mafundisho Kuhusu Wake Na Waume*

22Ninyi wake, watiini waume zenu kama
kumtii Bwana. 23Kwa maana mume ni kichwa
cha mkewe kama vile Kristo alivyo kichwa cha
Kanisa,ambalo ni mwili wake, naye Kristo ni
Mwokozi wake. 24Basi, kama vile Kanisa
linavyomtii Kristo, vivyo hivyo na wake nao
imewapasa kuwatii waume zao kwa kila jambo.

25 Ninyi waume, wapendeni wake zenu,
kama vile Kristo alivyolipenda Kanisa akajitoa
kwa ajili yake 26kusudi alifanye takatifu,
akilitakasa kwa kuliosha kwa maji katika Neno
lake, 27apate kujiletea Kanisa tukufu lisilo na
doa wala kunyanzi au waa lo lote, bali takatifu
lisilo na hatia. 28Vivyo hivyo imewapasa waume
kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe.
Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe.
29Hakuna mtu anayeuchukia mwili wake
mwenyewe, bali huulisha na kuutunza vizuri,
kama Kristo anavyolitunza Kanisa Lake. 30Sisi
tu viungo vya mwili Wake. 31"Kwa sababu hii,
mwanaume atamwacha baba yake na mama
yake, naye ataambatana na mkewe na hawa
wawili watakuwa mwili mmoja." 32Siri hii ni
kubwa, bali mimi nanena kuhusu Kristo na
Kanisa. 33Hata hivyo, kila mmoja wenu
ampende mkewe kama anavyoipenda nafsi
yake mwenyewe, naye mke lazima amheshimu
mumewe.

### *Mafundisho Kuhusu Watoto Na Wazazi*

6 Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana,
kwa kuwa hili ni jema.
2"Waheshimu baba yako na mama yako," hii
ndio amri ya kwanza yenye ahadi, 3"upate
baraka na uishi siku nyingi duniani."

4Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto
wenu, bali waleeni kwa nidhamu na mafundisho
ya Bwana.

### *Mafundisho Kuhusu Watumwa Na Mabwana*

5 Ninyi watumwa, watiini hao walio
mabwana zenu hapa duniani kwa heshima na
kwa kutetemeka na kwa moyo mmoja, kama
vile mnavyomtii Kristo. 6 Watiini, si tu wakati
wakiwaona ili mpate upendeleo wao, bali
mtumike kama watumwa wa Kristo, mkifanya
mapenzi ya Mungu kwa moyo. 7Tumikeni kwa
moyo wote, kama vile mnamtumikia Bwana na
si wanadamu. 8Mkijua kwamba Bwana atampa
kila mtu thawabu kwa lo lote jema alilotenda,
kama yeye ni mtumwa au ni mtu huru.

9Nanyi mabwana, watendeeni watumwa
wenu kwa jinsi iyo hiyo. Msiwatishe, kwa kuwa
mnajua ya kwamba Yeye aliye Bwana wenu na
Bwana wao yuko mbinguni, naye hana
upendeleo.

### *Silaha Za Mungu*

10Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika
Bwana na katika uweza wa nguvu Zake.
11Vaeni silaha zote za Mungu ili kwamba
mweze kuzipinga hila za Shetani. 12Kwa maana
kushindana kwetu si juu ya nyama na damu,
bali dhidi ya falme, mamlaka, dhidi ya wakuu wa
giza na majeshi ya pepo wabaya katika
ulimwengu wa roho. 13Kwa hiyo vaeni silaha
zote za Mungu ili mweze kushindana siku ya
uovu itakapokuja nanyi mkiisha kufanya yote,
simameni imara. 14Kwa hiyo simameni imara
mkiwa mmejifunga kweli kiunoni na kuvaa dirii
ya haki kifuani, 15nayo miguu yenu ifungiwe
utayari tuupatao kwa Injili ya amani. 16Zaidi ya
haya yote, twaeni ngao ya imani, ambayo kwa

hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto
ya yule mwovu. 17Vaeni chapeo ya wokovu na
mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la
Mungu. 18 Mkiomba kwa Roho sikuzote katika
sala zote na maombi, mkikesha kila wakati
mkiwaombea watakatifu wote.

19Niombeeni na mimi pia, ili kila
nifuanguapo kinywa changu, nipewe maneno ya
kusema, niweze kutangaza siri ya Injili kwa
ujasiri, 20ambayo mimi ni balozi wake katika
vifungo. Ombeni kwamba nipate kuhubiri kwa
ujasiri kama inipasavyo.

***Salamu Za Mwisho***

21Tikiko aliye ndugu mpendwa na mtumishi
mwaminifu katika Bwana, atawaambia kila kitu ili
pia mpate kujua hali yangu na kile ninachofanya
sasa. 22Ninamtuma kwenu kwa ajili ya kusudi
hili hasa, ili mpate kujua hali zetu na kuwatia
moyo.

23Amani iwe kwa ndugu na pendo pamoja
na imani kutoka kwa Mungu Baba na Bwana
Yesu Kristo. 24Neema iwe na wote wampendao
Bwana wetu Yesu Kristo kwa pendo wa dhati.
Amen.

## Wafilipi

### *Utangulizi*

Wafilipi umehesabiwa kama mojawapo ya zile nyaraka nne za Paulo za gerezani, ulioandikwa muda mfupi tu baada ya ule wa Waefeso ,Wakolosai na Filemoni.

Paulo aliandika waraka huu akiwa gerezani huko Rumi. Kwa kutambua kuzuiliwa kwa Paulo kanisa la Filipi lilimpelekea Paulo msaada kwa mkono wa Epafrodito *(4:18).* Akitaka kuwashukuru rafiki zake wapendwa waliokuwa wamempelekea msaada huo kwa ajili ya mahitaji yake, anaanza kwa kuwashukuru kwa msaada wao, pia anatumia nafasi hiyo kueleza juu ya hali yake, kuwatia Wafilipi moyo na kuwataka kusimama imara, akiwahimiza wawe na unyenyekevu kama aliokuwa nao Kristo na wawe na umoja.Paulo anawasifu Timotheo na Epafrodito kwa kanisa la Filipi. Paulo haachi kueleza jinsi alivyokuwa na imani nao, Kisha anawaeleza juu ya matatizo anayopata huko Rumi.

Hajui mwisho wa shauri lake utakavyokuwa. Lakini hata kama atauawa yeye atafurahi akiwa na Kristo. Kama ataendelea kuishi, atazidi kumtumikia Mungu kwa uwezo wake wote. Anawaagiza wakatae kabisa mafundisho ya uongo. Waamini wote wanaambiwa wawe na malengo ya juu kabisa katika maisha yao ya Kikristo kwa maana Mungu atawapa mahitaji yao yote katika maisha haya. Paulo anawakazia kufurahi nyakati zote.

### *Wazo Kuu*

Katika waraka huu wa binafsi, Paulo anasisitiza juu ya furaha. Kila mtu aliyempokea Kristo anapaswa kuwa na furaha kwa sababu anapendwa na Mungu, Kristo amekufa kwa ajili yake na Mungu anamtimizia mahitaji yake yote katika maisha haya. Paulo anasisitiza kuwa wasijisumbue kwa ajili ya jambo lo lote ila katika kila jambo kwa kusali, kuomba na kushukuru. Haja zote zijulikane na Mungu *(4:16).* Hatimaye anamalizia kuwakumbusha kuwa Mungu atawajaza na kila wanachohitaji kwa kadiri ya utajiri Wake *(4:19)*. Hii haina maana kwamba wakristo hawatapata shida. Kama ikibidi, hatuna budi kufuata mfano wa unyenyekevu wa Kristo ambaye alimtii Mungu, akakubali hata kufa msalabani. Sisi ni raia wa mbinguni (*3:20)* na hatuna budi kuishi kwa kutambua jambo hili.

### *Mahali*

Gerezani huko Rumi

### *Tarehe*

Waraka huu uliandikwa 61 B.K.

### *Mwandishi*

Mwandishi wa waraka huu ni Mtume Paulo.

### *Mgawanyo*

- Paulo na matatizo yake huko Rumi (1:1-30)
- Mfano wa utii wa Yesu (2:1- 30)
- Mafundisho kuhusu mwenendo wa mkristo (3:1-21)
- Amani ya Mungu na jinsi Mungu anavyowatimizia waamini mahitaji yao (4:1-23).

### *Salamu*

**1** Paulo na Timotheo, watumishi wa Kristo Yesu,

Kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu
walioko Filipi, pamoja na maaskofu na
mashemasi:

2Neema na amani itokayo kwa Mungu Baba
yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Shukrani Na Maombi*

3Ninamshukuru Mungu wangu kila
niwakumbukapo ninyi. 4Katika maombi yangu
yote daima nimekuwa nikiwaombea ninyi nyote
kwa furaha, 5kwa sababu ya kushiriki kwenu
katika kueneza Injili, tangu siku ya kwanza hadi
leo, 6nina hakika kwamba, Yeye aliyeianza kazi
njema mioyoni mwenu, ataiendeleza na
kuikamilisha hata siku ya Kristo Yesu.

7 Ni haki na ni wajibu wangu kufikiri hivi juu
yenu nyote, kwa sababu ninyi mko moyoni
mwangu, ikiwa nimefungwa au nikiwa ninaitetea
na kuithibitisha Injili, ninyi nyote mnashiriki
neema ya Mungu pamoja nami. 8Mungu ni
shahidi yangu, jinsi ninavyowaonea shauku ninyi
nyote kwa huruma ya Kristo Yesu.

9Haya ndiyo maombi yangu kwamba
upendo wenu uongezeke zaidi na zaidi katika
maarifa na ufahamu wote, 10ili mpate kutambua
yale yaliyo mema, mkawe safi, wasio na hatia
hadi siku ya Kristo, 11mkiwa mmejawa na
matunda ya haki yapatikanayo kwa njia ya Yesu
Kristo, kwa utukufu na sifa za Mungu.

### *Kufungwa Kwa Paulo Kwaieneza Injili*

12Basi, ndugu zangu, nataka mjue kwamba
mambo yale yaliyonipata kwa kweli yamesaidia
sana kueneza Injili. 13Matokeo yake ni kwamba
imejulikana wazi kwa walinzi wote wa jumba la
kifalme na kwa wengine wote kuwa nimefungwa
kwa ajili ya Kristo. 14Kwa sababu ya vifungo
vyangu, ndugu wengi katika Bwana wametiwa
moyo kuhubiri neno la Mungu kwa ujasiri zaidi
na bila woga.

15 Ni kweli kwamba wengine wanaomhubiri
Kristo kutokana na wivu na kwa kutaka
kushindana, lakini wengine wanamhubiri Kristo
kwa nia njema. 16Hawa wa mwisho wanamhubiri
Kristo kwa moyo wa upendo, wakifahamu kwamba
nimo humu gerezani kwa ajili ya kuitetea Injili.
17Hao wa kwanza wanamtangaza
Kristo kutokana na tamaa zao wenyewe wala si
kwa moyo mweupe bali wanakusudia kuongeza
mateso yangu katika huku kufungwa kwangu.
18Lakini inadhuru nini? Jambo la muhimu ni
kwamba kwa kila njia, ikiwa ni kwa nia mbaya
au njema Kristo anahubiriwa. Nami kwa ajili ya
jambo hilo ninafurahi.

Naam, nami nitaendelea kufurahi, 19kwa
maana ninajua kwamba kwa maombi yenu na
kwa msaada unaotolewa na Roho wa Yesu
Kristo, yale yaliyonipata mimi yatageuka kuwa
wokovu wangu. 20Ninatarajia kwa shauku
kubwa na kutumaini kwamba sitaaibika kwa njia
yo yote, bali nitakuwa na ujasiri wa kutosha ili
sasa kama wakati mwingine wo wote, Kristo
atatukuzwa katika mwili wangu, ikiwa ni kwa
kuishi au kwa kufa. 21 Kwa maana kwangu
mimi, kuishi ni Kristo na kufa ni faida. 22Kama
nitaendelea kuishi katika mwili, hii ni kwa ajili ya
matunda ya kazi. Lakini sijui nichague lipi? Mimi
sijui! 23Ninavutwa kati ya mambo mawili:
Ninatamani kuondoka nikakae pamoja na
Kristo, jambo hilo ni bora zaidi. 24Lakini kwa
sababu yenu ni muhimu zaidi mimi nikiendelea
kuishi katika mwili. 25Kwa kuwa nina matumaini
haya, ninajua kwamba nitaendelea kuwapo na
kuwa pamoja nanyi nyote, ili mpate kukua na
kuwa na furaha katika imani. 26Ili kwamba
furaha yenu iwe nyingi katika Kristo Yesu kwa
ajili yangu kwa kule kuja kwangu kwenu tena.

### *Kuenenda Ipasavyo Injili*

27 Lakini lo lote litakalotukia, mwenende
kama ipasavyo Injili ya Kristo, ili kwamba nikija
na kuwaona au nikiwa sipo, nipate kusikia haya
juu yenu: Kuwa mnasimama imara katika roho
moja, mkiishindania imani ya Injili kwa umoja,
28wala msitishwe na wale wanaowapinga. Hii ni
ishara kwao kuwa wataangamia, lakini ninyi
mtaokolewa na hii ni kazi ya Mungu. 29Kwa
maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si
kumwamini tu, bali pia kuteswa kwa ajili yake,
30kwa kuwa mnashiriki mashindano yale yale
mliyoyaona nikiwa nayo na ambayo hata sasa
mnasikia kuwa bado ninayo .

### *Kuiga Unyenyekevu Wa Kristo*

**2** Kama kukiwa na jambo lo lote la kutia moyo,
kukiwako faraja yo yote katika upendo, kukiwa
na ushirika wo wote katika Roho, kukiwa na
wema wo wote na huruma, 2basi ikamilisheni
furaha yangu kwa kuwa na nia
kama hiyo, mkiwa na upendo huo huo, wenye

roho moja na kusudi moja. [3]Msitende jambo lo
lote kwa nia ya kujitukuza, bali kwa
unyenyekevu, kila mtu akimhesabu mwingine
bora kuliko nafsi yake. [4]Kila mmoja wenu
asiangalie mambo yake mwenyewe tu, bali pia
ajishughulishe kwa faida ya wengine.

[5]Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo
Yesu.

[6]Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu,
hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu
cha kushikamana nacho,
[7]bali alijifanya si kitu,
akajifanya sawa na mtumwa,
akazaliwa katika umbo la mwanadamu.
[8]Naye akiwa na umbo la mwanadamu,
alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya
msalaba!
[9]Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana
na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina,
[10]ili kwa Jina la Yesu, kila goti lipigwe,
la vitu vya mbinguni, vya duniani na vya
chini ya nchi
[11]na kila ulimi ukiri ya kwamba **YESU
KRISTO NI BWANA**,
kwa utukufu wa Mungu Baba.

### *Ng'aeni Kama Mianga Katika Ulimwengu*

[12] Kwa hiyo, wapenzi wangu, kama vile
ambavyo mmekuwa mkitii sikuzote, si tu wakati
nikiwa pamoja nanyi, bali sasa zaidi sana
nisipokuwapo. Utimizeni wokovu wenu kwa
kuogopa na kutetemeka, [13]kwa maana Mungu
ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu
na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi Lake
jema.

[14]Fanyeni mambo yote bila kunung'unika
wala kushindana, [15]ili msiwe na lawama wala
hatia, bali mwe wana wa Mungu wasio na
kasoro katika kizazi chenye ukaidi na
kilichopotoka, ambacho ndani yake ninyi
mnang'aa kama mianga ulimwenguni.
[16]Mkilishika neno la uzima, ili nipate kuona
fahari siku ya Kristo kwamba sikupiga mbio wala
kujitaabisha bure. [17]Lakini hata kama
nikimiminwa kama sadaka ya kinywaji kwenye
dhabihu na huduma itokayo katika imani yenu,
mimi ninafurahi na kushangilia pamoja nanyi
nyote. [18]Vivyo hivyo, ninyi nanyi imewapasa
kufurahi na kushangilia pamoja nami.

### *Paulo Amsifu Timotheo*

[19]Nina tumaini katika Bwana Yesu kumtuma
Timotheo hivi karibuni aje kwenu, ili nipate
kufarijika moyo nitakapopata habari zenu.
[20]Sina mtu mwingine kama yeye ambaye
ataangalia hali yenu kwa halisi. [21] Kwa maana
kila mmoja anajishughulisha zaidi na mambo
yake mwenyewe wala si yale ya Yesu Kristo.
[22]Lakini ninyi wenyewe mnajua jinsi Timotheo
alivyojithibitisha mwenyewe, kwa maana
amefanya kazi ya Injili pamoja nami kama vile
mwana kwa baba yake. [23]Kwa hiyo, ninatumaini
kumtuma kwenu upesi mara nitakapojua
mambo yangu yatakavyokuwa. [24]Nami
mwenyewe ninatumaini katika Bwana kwamba
nitakuja kwenu hivi karibuni.

### *Paulo Amsifu Epafrodito*

[25]Lakini nadhani ni muhimu kumtuma tena
kwenu Epafrodito, ndugu yangu na mtenda kazi
pamoja nami, aliye askari mwenzangu, ambaye
pia ni mjumbe wenu mliyemtuma ili ashughulike
na mahitaji yangu. [26]Kwa maana amekuwa
akiwaonea sana shauku ninyi nyote, akiwa na
wasiwasi kwa kuwa mlisikia kwamba alikuwa
mgonjwa. [27]Kweli alikuwa mgonjwa, tena karibu
ya kufa. Lakini Mungu alimhurumia, wala si
yeye tu, bali hata na mimi alinihurumia,
nisipatwe na huzuni juu ya huzuni. [28]Kwa hiyo
mimi ninafanya bidii kumtuma kwenu ili
mtakapomwona kwa mara nyingine, mpate
kufurahi, nami wasiwasi wangu upungue. [29]Kwa
hiyo mpokeeni katika Bwana kwa furaha kubwa,
nanyi wapeni heshima watu kama hawa, [30]kwa
sababu alikaribia kufa kwa ajili ya kazi ya Kristo,
akihatirisha maisha yake ili aweze kunipa
msaada ambao ninyi hamkuweza kunipa.

### *Hakuna Tumaini Katika Mwili*

**3** Hatimaye, ndugu zangu, furahini katika Bwana!
Mimi kuwaandikia mambo yale yale hakuniudhi, kwa
maana ni kinga kwa ajili
yenu.

[2]Jihadharini na mbwa, wale watenda
maovu, jihadharini na wale wajikatao miili yao,
wasemao ili kuokoka ni lazima kutahiriwa. [3]Kwa
maana sisi ndio tulio tohara, sisi tumwabuduo
Mungu katika Roho, tunaona fahari katika Kristo
Yesu, ambao hatuweki tumaini letu katika mwili,
[4]ingawa mimi mwenyewe ninazo sababu za
kuutumainia mwili.

Kama mtu ye yote akidhani anazo sababu
za kuutumainia mwili, mimi zaidi. [5]Nilitahiriwa
siku ya nane, mimi ni Mwisraeli wa kabila la
Benyamini, Mwebrania wa Waebrania. Kwa

habari ya sheria, ni Farisayo, 6kwa habari za
juhudi, nilikuwa nalitesa kanisa, kuhusu haki
ipatikanayo kwa sheria, mimi nilikuwa sina hatia.
7Lakini mambo yale yaliyokuwa faida
kwangu, sasa nayahesabu kuwa hasara kwa
ajili ya Kristo. 8Zaidi ya hayo, nayahesabu
mambo yote kuwa hasara tupu nikiyangalinisha
na faida kubwa ipitayo kiasi ya kumjua Kristo
Yesu Bwana wangu, ambaye kwa ajili Yake
nimepata hasara ya mambo yote, nikiyahesabu
kuwa kama mavi ili nimpate Kristo, 9nami
nionekane mbele Zake nisiwe na haki yangu
mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile
ipatikanayo kwa imani katika Kristo, haki ile
itokayo kwa Mungu kwa njia ya imani. 10Nataka
nimjue Kristo na uweza wa kufufuka Kwake na
ushirika wa mateso Yake, ili nifanane naye
katika mauti Yake, 11ili kwa njia yo yote niweze
kufikia ufufuo wa wafu.

### *Kukaza Mwendo Ili Kufikia Lengo*

12Si kwamba nimekwisha kufikia, au
kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu, la hasha!
Bali nakaza mwendo ili nipate kile ambacho kwa
ajili yake, nimeshikwa na Kristo Yesu. 13Ndugu
zangu, sijihesabu kuwa nimekwisha kushika.
Lakini ninafanya jambo moja: Ninasahau
mambo yale yaliyopita, nakaza mwendo kufikia
yale yaliyo mbele. 14Nakaza mwendo nifikie ile
alama ya ushindi iliyowekwa ili nipate tuzo ya
mwito mkuu wa Mungu ambao nimeitiwa huko
juu mbinugni katika Kristo Yesu.
15Hivyo sisi sote tuliokuwa kiroho tuwaze
jambo hili, hata mkiwaza mengine katika jambo
lo lote, Mungu ataliweka wazi hilo nalo. 16Lakini
na tushike sana lile ambalo tumekwisha kulifikia.
17Ndugu zangu, kwa pamoja fuateni mfano
wangu na kuwatazama wale wanaofuata
kielelezo tulichowawekea. 18Kwa maana, kama
nilivyokwisha kuwaambia mara nyingi kabla,
nami sasa nasema tena hata kwa machozi,
watu wengi wanaishi kama adui wa msalaba wa
Kristo. 19Mwisho wa watu hao ni uangamivu,
Mungu wao ni tumbo na utukufu wao ni aibu na
mawazo yao yamo katika mambo ya dunia.
20Lakini wenyeji wetu uko mbinguni. Nasi
tunamngoja kwa shauku Mwokozi kutoka huko,
yaani, Bwana Yesu Kristo, 21atakayebadili mwili
wetu wa unyonge, ili upate kufanana na mwili
Wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa
huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote chini Yake.

**4** Kwa hiyo, ndugu zangu, ninaowapenda
na ambao ninawaonea shauku, ninyi mlio
furaha yangu na taji yangu, hivi ndivyo
iwapasavyo kusimama imara katika Bwana,
ninyi wapenzi wangu.

### *Mausia*

2 Nawasihi Euodia na Sintike wawe na nia
moja katika Bwana. 3Naam, nawasihi ninyi pia,
wenzi wangu waaminifu, wasaidieni hawa
wanawake, kwa sababu walijitaabisha katika
kazi ya Injili pamoja nami bega kwa bega,
wakiwa pamoja na Klementi na watenda kazi
wenzangu ambao majina yao yameandikwa
katika kitabu cha uzima.
4Furahini katika Bwana sikuzote, tena
nasema furahini! 5 Upole wenu na ujulikane na
watu wote. Bwana yu karibu. 6Msijisumbue kwa
jambo lo lote, bali katika kila jambo kwa kuomba
na kusihi pamoja na kushukuru, haja zenu na
zijulikane na Mungu. 7Nayo amani ya Mungu,
inayopita fahamu zote, itawalinda mioyo yenu
na nia zenu katika Kristo Yesu.
8Hatimaye, ndugu zangu, mambo yote
yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo na sifa njema, yo
yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote
ya kupendeza, yo yote yenye staha, ukiwako
uzuri wo wote, pakiwepo cho chote
kinachostahili kusifiwa, tafakarini mambo hayo.
9Mambo yote mliyojifunza au kuyapokea au
kuyasikia kutoka kwangu, au kuyaona kwangu,
yatendeni hayo. Naye Mungu wa amani
atakuwa pamoja nanyi.

### *Shukrani Kwa Matoleo Yenu*

10Nina furaha kubwa katika Bwana kwamba
hatimaye mmeanza upya kushughulika tena na
maisha yangu. Kweli mmekuwa mkinifikiria
lakini mlikuwa hamjapata nafasi ya kufanya
hivyo. 11Sisemi hivyo kwa vile nina mahitaji, la!
Kwa maana nimejifunza kuridhika katika hali yo
yote. 12Ninajua kupungukiwa, pia ninajua kuwa
na vingi. Nimejifunza siri ya kuridhika katika kila
hali, wakati wa kushiba na wakati wa kuona
njaa, wakati wa kuwa na vingi na wakati wa
kupungukiwa. 13Naweza kuyafanya mambo
yote katika Yeye anitiaye nguvu.
14 Lakini, mlifanya vema kushiriki nami katika
taabu zangu. 15Zaidi ya hayo, ninyi Wafilipi
mnajua kwamba siku za kwanza nilipoanza
kuhubiri Injili, nilipoondoka Makedonia, hakuna
kanisa jingine lililoshiriki nami katika masuala ya
kutoa na kupokea isipokuwa ninyi. 16Kwa maana
hata nilipokuwa huko Thesalonike, mliniletea
msaada kwa ajili ya mahitaji yangu

zaidi ya mara moja. 17Si kwamba natafuta sana
yale matoleo, bali natafuta sana ile faida
itakayozidi sana kwa upande wenu. 18Nimelipwa
kikamilfu hata na zaidi, nimetoshelezwa kabisa,
sasa kwa kuwa nimepokea kutoka kwa Epafrodito
vile vitu mlivyonitumia, sadaka yenye harufu nzuri,
dhabihu inayokubalika na ya kumpendeza Mungu.
19Naye Mungu wangu atawajaza ninyi kila
mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri Wake katika
utukufu ndani ya Kristo Yesu.

20Mungu wetu aliye Baba yetu apewe
utukufu milele na milele. Amen.

### *Salamu Za Mwisho*

21 Msalamuni kila mtakatifu katika Kristo
Yesu. Ndugu walioko pamoja nami
wanawasalimu. 22Watakatifu wote
wanawasalimu, hasa wale watu wa nyumbani
mwa Kaisari wanawasalimu.

23Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja
na roho zenu. Amen.

## WAKOLOSAI

### *Utangulizi*

Wakolosai umeitwa waraka pacha wa Waefeso.Zikiwa zimendikwa wakati mmoja, yale yaliyomo yanafanana sana.Timotheo alishirikiana na Paulo huko Rumi katika kuandika nyaraka hizi mbili wakati Paulo akiwa mfungwa.Hivyo Wakolosai ni mojawapo ya nyaraka za gerezani. Tikiko ndiye aliyepeleka waraka huu huko Kolosai.

Mji wa Kolosai ulikuwa umejengwa kama kilomita 160 *(maili 100 )* kutoka Efeso kwenye bonde la Lika karibu na Hierapoli na Laodikia *(4:13).* Kwa kadiri ionekanavyo Paulo alikuwa hajautembelea mji huo wa Kolosai *(2:1) ,* ila mji huu ulihubiriwa Injili wakati Paulo akiwa Efeso *(Mdo. 19:10*) na Epafra *(1:7),*Timotheo au watu wengine. Hivyo Paulo alipata kuwafahamu waamini hawa akiwa Efeso katika safari yake ya pili ya kueneza Injili na sasa alikuwa na wasiwasi kwa sababu alisikia kuwa mafundisho ya Unostiki yaliyokuwa yanasema kwamba kila kitu ni kibaya lakini roho ni njema, yalikuwa yameingia katika kanisa hilo. Mafundisho haya yalikuwa yanaufanya ujumbe wa Injili kuelekea mahali pa hatari. Mambo yaliyokuwa yakiwasumbua Wakolosai yalikuwa ni mchanganyiko wa elimu ya nyota, uchawi na mafundisho hayo ya Unostiki ambayo yalisema kuwa Kristo alikuwa sawasawa na malaika. Paulo aliwaandikia kuwathibitishia kuwa Kristo ni Mungu na kwamba anao ukamilifu wa Mungu wa milele *(2:9).* Ndipo anawapa mafundisho kuhusu maisha yampasayo mkristo.

### *Wazo kuu*

Katika barua hii muhimu ya Paulo tunapewa maelezo kamili yaliyoandikwa kwa ufasaha na kwa uangalifu kuhusu Uungu wa Kristo na utukufu Wake. Kristo ni Mungu wa vyote na mtu ye yote anayemwamini Kristo anakuwa na vitu vyote ndani Yake. Paulo anawaonya waamini wasiyumbishwe na elimu wala hekima kwa kufuata mapokeo ya wanadamu *(2:8).* Anatoa mafundisho kuhusu maisha yampasayo mkristo, akisisitiza kuwa wakristo kama mwili mmoja wanaomtegemea Kristo aliye Kichwa wanapewa nguvu, amani na furaha na Mungu.

### *Mahali*

Waraka huu uliandikwa kutoka Rumi.

### *Tarehe*

Uliandikwa kama 60 B.K.

### *Mwandishi*

Paulo

### *Mgawanyo*

- Salamu na shukrani za Paulo (1:1- 8)
- Yesu Kristo na waamini (1:9 - 2:7)
- Hatari kuhusu mafundisho ya uongo (2:8 - 23)
- Mafundisho kuhusu maisha ya kikristo (3:1- 4:1)
- Maagizo kuhusu kuomba na mausia ya mwisho (4:2-18).

### *Salamu*

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu na Timotheo ndugu yetu.

2Kwa ndugu watakatifu na waaminifu katika Kristo, waishio Kolosai:

Neema iwe nanyi na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu.

### *Shukrani Na Maombi*

3Sikuzote tunamshukuru Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, tunapowaombea ninyi, 4kwa sababu tumesikia juu ya imani yenu katika Kristo Yesu na juu ya upendo wenu mlio nao kwa watakatifu wote, 5 imani na upendo ule utokao katika tumaini mlilowekewa akiba mbinguni na ambalo mmesikia habari zake katika neno la kweli, yaani, ile Injili iliyowafikia ninyi. 6Duniani kote Injili hii inazaa matunda na kuenea kama ilivyokuwa kwenu tangu siku ile mlipoisikia na kuielewa neema ya Mungu katika kweli yote. 7Mlijifunza habari zake kutoka kwa Epafra, mtumishi mwenzenu mpendwa, yeye aliye mhudumu mwaminifu wa Kristo kwa ajili yetu, 8ambaye pia ametuambia kuhusu upendo wenu katika Roho.

9Kwa sababu hii, tangu siku ile tuliposikia habari zenu, hatukukoma kuomba kwa ajili yenu na kumsihi Mungu awajaze ninyi na maarifa ya mapenzi Yake katika hekima yote ya kiroho na ufahamu. 10Nasi tunaomba haya ili mpate kuishi maisha yanayostahili mbele za Bwana ili mpate kumpendeza kwa kila namna: Mkizaa matunda kwa kila kazi njema, mkikuwa katika kumjua Bwana. 11Mkiwa mmetiwa nguvu kwa uwezo wote kwa kadiri ya nguvu ya utukufu Wake, ili mpate kuwa na wingi wa saburi na uvumilivu, nanyi kwa furaha 12mkimshukuru Baba, ambaye amewastahilisha kushiriki katika urithi wa watakatifu katika ufalme wa nuru. 13Kwa maana alituokoa kutoka katika ufalme wa giza na kutuingiza katika ufalme wa Mwana Wake mpendwa, 14ambaye katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa dhambi.

### *Ukuu Wa Kristo*

15Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. 16Kwa Yeye vitu vyote vilivyoko mbinguni na juu ya nchi viliumbwa, vile vitu vinavyoonekana na vile visivyoonekana, kama ni viti vya enzi au falme, au wenye mamlaka au watawala, vitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake. 17Yeye alikuwapo kabla ya vitu vyote na katika Yeye vitu vyote vinashikamana pamoja. 18Yeye ndiye kichwa cha mwili, yaani, Kanisa, naye ni wa mwanzo na mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, ili Yeye awe mkuu katika vitu vyote. 19Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba ukamilifu Wake wote wa kimungu uwe ndani Yake 20na kwa njia ya Mwanawe aweze kuvipatanisha vitu vyote na Yeye mwenyewe, ikiwa ni vitu vilivyoko duniani au vilivyoko mbinguni, kwa kufanya amani kwa damu Yake iliyomwagika msalabani.

21Hapo kwanza ninyi mlikuwa mmetengana na Mungu na mlikuwa adui Zake katika nia zenu kwa sababu ya mwenendo wenu mbaya. 22Lakini sasa Mungu amewapatanisha ninyi kwa njia ya mwili wa Kristo kwa kupitia mauti, ili awalete mbele Zake mkiwa watakatifu, bila dosari wala lawama, 23mradi tu kwamba mtaendelea kuwa waaminifu, mkiwa mmefanywa imara na thabiti katika imani, pasipo kuliacha tumaini lililoahidiwa na Injili ile mliyosikia, hii ndiyo ile Injili mliyoisikia na ambayo imehubiriwa kwa kila kiumbe chini ya mbingu na ambayo mimi Paulo, nimekuwa mtumwa wake.

### *Taabu Ya Paulo Kwa Ajili ya Kanisa*

24Sasa nafurahia kule kuteseka kwangu kwa ajili yenu na katika mwili wangu ninatimiliza yale yaliyopungua katika mateso ya Kristo kwa ajili ya mwili wake, ambao ni Kanisa. 25Mimi nimekuwa mtumishi wa Kanisa kwa wajibu alionipa Mungu ili kuwaletea ninyi neno la Mungu kwa ukamilifu. 26Siri hii ilikuwa imefichika kwa karne nyingi na vizazi vingi, lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu. 27Kwao, Mungu amechagua kujulisha miongoni mwa watu Mataifa utukufu wa utajiri wa siri hii, ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.

28Yeye Kristo ndiye tunayemtangaza, tukimwonya kila mtu na kumfundisha kila mtu kwa hekima yote ili tuweze kumleta kila mmoja akiwa amekamilika katika Kristo. 29Kwa ajili ya jambo hili, ninajitaabisha, nikijitahidi kwa kadiri ya nguvu zile ambazo kwa uwezo mwingi hutenda kazi ndani yangu.

2 Kwa kuwa nataka mjue jinsi ninavyojitaabisha kwa ajili yenu na kwa ajili ya wale walioko Laodikia na kwa ajili ya wote

wale ambao hawajapata kuniona mimi binafsi. 2Kusudi langu ni kuwa watiwe moyo na kuunganishwa katika upendo, ili wapate kujua ulivyo utajiri wa ufahamu kamili, waijue siri ya Mungu, yaani, Kristo mwenyewe, 3 ambaye ndani Yake kumefichwa hazina yote ya hekima na maarifa. 4Nawaambia mambo haya ili mtu ye yote asiwadanganye kwa maneno ya kuwashawishi. 5Kwa maana ingawa mimi siko pamoja nanyi kimwili, lakini niko pamoja nanyi kiroho, nami nafurahi kuuona utaratibu wenu na uthabiti wa imani yenu katika Kristo.

### *Ukamilifu Wa Maisha Katika Kristo*

6Hivyo basi, kama vile mlivyompokea Kristo Yesu kuwa Bwana, endeleeni kukaa ndani Yake. 7Mwe na mizizi, mkiwa mmejengwa ndani Yake, mkiimarishwa katika imani kama mlivyofundishwa na kufurika kwa wingi wa shukrani.

8Angalieni mtu ye yote asiwafanye ninyi mateka kwa elimu batili na madanganyo matupu yanayotegemea mapokeo ya wanadamu na mafundisho ya ulimwengu ambayo siyo ya Kristo.

9Maana ukamilifu wote wa uungu umo ndani ya Kristo katika umbile la mwili wa kibinadamu, 10nanyi mmepewa ukamilifu ndani ya Kristo, ambaye Yeye ndiye mkuu juu ya kila enzi na kila mamlaka. 11Katika Kristo pia mlitahiriwa kwa kutengwa mbali na asili ya dhambi, si kwa tohara inayofanywa kwa mikono ya wanadamu bali kwa ile tohara iliyofanywa na Kristo, 12mkiwa mmezikwa pamoja naye katika ubatizo na kufufuliwa pamoja naye kwa kuuamini uweza wa Mungu aliyemfufua kutoka kwa wafu.

13Mlipokuwa wafu katika dhambi zenu na kutokutahiriwa katika asili yenu ya dhambi, Mungu aliwafanya mwe hai pamoja na Kristo. Alitusamehe dhambi zetu zote, 14akiisha kuifuta ile hati yenye mashtaka yaliyokuwa yanatukabili pamoja na amri zake, aliiondoa isiwepo tena, akiigongomea kwenye msalaba Wake. 15Mungu akiisha kuzivua enzi na mamlaka, alizifanya kuwa kitu cha fedheha hadharani kwa kuziburuta kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba wa Kristo.

16Kwa hiyo mtu asiwahukumu ninyi kuhusu vyakula au vinywaji, au kuhusu kuadhimisha sikukuu za dini, au Sikukuu za Mwandamo wa mwezi au Siku ya Sabato. 17Hizi zilikuwa kivuli cha mambo ambayo yangekuja, lakini ile iliyo halisi imo ndani ya Kristo. 18Mtu ye yote asiwaondolee thawabu yenu, akisisitiza kumnyenyekea yeye na kuabudu malaika, akidumu katika maono yake, akijivuna bila sababu katika mawazo ya kibinadamu, 19wala hakishiki kwa uthabiti Kichwa, ambaye kutoka Kwake mwili wote unalishwa na kushikamanishwa pamoja kwa viungo na mishipa, ambao hukua kwa ukuaji utokao kwa Mungu.

### *Maonyo Dhidi Ya Walimu Wa Uongo*

20Kwa kuwa mlikufa pamoja na Kristo, mkayaacha yale mafundisho ya msingi ya ulimwengu huu, kwa nini bado mnaishi kama vile ninyi ni wa ulimwengu? Kwa nini mnajitia chini ya amri? 21"Msishike! Msionje! Msiguse?" 22Haya yote mwisho wake ni kuharibika yanapotumiwa, kwa sababu hayo msingi wake ni katika maagizo na mafundisho ya wanadamu. 23Kwa kweli amri kama hizo huonekana kama zina hekima, katika namna za ibada walizojitungia wenyewe, unyenyekevu wa uongo na kuutawala mwili kwa ukali, lakini hayafai kitu katika kuzuia tamaa za mwili.

### *Kanuni Za Kuishi Maisha Matakatifu*

**3** Basi, kwa kuwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. 2Yafikirini mambo yaliyo juu, wala si ya duniani. 3Kwa maana ninyi mlikufa, nao uhai wenu sasa umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. 4Wakati Kristo atakapotokea Yeye aliye na uzima wenu ndipo nanyi mtakapotokea pamoja naye katika utukufu.

5Kwa hiyo, kiueni kabisa cho chote kilicho ndani yenu cha asili ya kidunia: Yaani, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya na kutamani, ambayo ndiyo ibada ya sanamu. 6Kwa sababu ya mambo haya, ghadhabu ya Mungu inakuja. 7 Ninyi pia zamani mlienenda katika mambo haya mlipoishi maisha hayo. 8Lakini sasa yawekeni mbali nanyi mambo kama haya yote, yaani : Hasira, ghadhabu, uovu, masingizio na lugha chafu kutoka midomoni mwenu. 9Msiambiane uongo kwa maana mmevua kabisa utu wenu wa kale pamoja na matendo yake 10nanyi mmevaa utu mpya unaofanywa upya katika ufahamu sawasawa na mfano wa Mwumba wake. 11Hapa hakuna Myunani wala Myahudi, aliyetahiriwa wala asiyetahiriwa, asiyestaarabika wala aliyestaarabika, mtumwa wala mtu huru, bali

Kristo ni yote na ndani ya wote.

12Kwa hiyo, kwa kuwa ninyi mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu, wapendwa, jivikeni moyo wa huruma, utu wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu. 13Vumilianeni na kusameheana. Mtu akiwa na lalamiko lo lote dhidi ya mwenzake, sameheaneni kama vile Bwana alivyowasamehe ninyi. 14 Zaidi ya maadili haya yote jivikeni upendo, ambao ndio unaofunga kila kitu pamoja katika amani kamilifu.

15Amani ya Kristo na itawale mioyoni mwenu, kwa kuwa ninyi kama viungo vya mwili mmoja mmeitiwa amani. Tena iweni watu wa shukrani. 16Neno la Kristo na lidumu kwa wingi ndani yenu, mkifundishana na kuonyana katika hekima yote, mkimwimbia Mungu zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni huku mkiwa na shukrani mioyoni mwenu. 17Lo lote mfanyalo, ikiwa ni kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba katika Yeye.

### *Kanuni Katika Madaraka Ya Nyumbani*

18Ninyi wake, watiini waume zenu, kama inavyostahili katika Bwana.

19Ninyi waume, wapendeni wake zenu, wala msiwe na uchungu dhidi yao.

20Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote, kwa maana hivi ndivyo inavyompendeza Bwana.

21Ninyi akina baba msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa.

22Ninyi watumwa, watiini mabwana zenu wa hapa duniani katika mambo yote. Fanyeni hivyo si wakiwepo tu, bali mkimwogopa Mungu, wala si kwa kutafuta upendeleo wao wakati wanapowaonaa. 23Lo lote mfanyalo, fanyeni kwa moyo kama watu wanaomtumikia Bwana na si wanadamu. 24Kwa kuwa mnajua kwamba mtapokea urithi wenu kutoka kwa Bwana kuwa thawabu yenu. 25Ye yote atendaye mabaya atalipwa kwa ajili ya mabaya yake, wala hakuna upendeleo.

**4** Ninyi mabwana, watendeeni watumwa wenu yaliyo haki na yanayostahili mkitambua ya kwamba ninyi pia mnaye Bwana mbinguni.

### Maagizo Zaidi.

2Dumuni sana katika maombi, mkikesha katika hayo pamoja na kushukuru. 3Pia tuombeeni na sisi ili Mungu atufungulie mlango wa kunena, ili tupate kuitangaza siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake pia mimi nimefungwa. 4Ombeni ili nipate kuitangaza Injili kwa udhahiri kama ipasavyo kunena. 5Iweni na hekima jinsi mnavyoenenda mbele yao wale walio nje, mkiutumia vizuri wakati wenu. 6 Maneno yenu yawe yamejaa neema siku zote, yanayofaa, ili mjue jinsi iwapasavyo na inavyofaa kumjibu kila mtu.

### *Salamu Za Mwisho*

7Tikiko atawaambia habari zangu zote. Yeye ni ndugu mpendwa, mtenda kazi mwaminifu na mtumishi mwenzangu katika Bwana. 8Nimemtuma kwenu kwa madhumuni haya ili kwamba mpate kufahamu hali yetu na pia awatie moyo. 9Anakuja pamoja na Onesmo, ndugu yetu mpendwa na mwaminifu, ambaye ni mmoja wenu. Watawaambia mambo yote yanayotendeka hapa kwetu.

10Aristarko aliye mfungwa pamoja nami anawasalimu, vivyo hivyo Marko, binamu yake Barnaba. (Mmeshapata maagizo yanayomhusu, akija kwenu, mpokeeni). 11Yesu, yeye aitwaye Yusto, pia anawasalimu. Hawa peke yao, ndio Wayahudi miongoni mwa watenda kazi wenzangu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, nao wamekuwa faraja kwangu. 12Epafra, ambaye ni mmoja wenu na mtumishi wa Kristo Yesu, anawasalimu. Yeye sikuzote anawaombea kwa bidii kwamba msimame imara katika mapenzi yote ya Mungu mkiwa wakamilifu na thabiti. 13Ninashuhudia kwa ajili yake kwamba anafanya kazi kwa bidii kwa ajili yenu na kwa ajili ya ndugu wa Laodikia na Hierapoli. 14Rafiki yetu mpenzi Luka, yaani, yule tabibu, pamoja na Dema, wanawasalimu. 15 Wasalimuni ndugu wote wa Laodikia na pia Nimfa pamoja na kanisa linalokutana katika nyumba yake.

16Baada ya barua hii kusomwa kwenu, hakikisheni kwamba inasomwa pia katika kanisa la Walaodikia. Nanyi pia msome barua inayotoka Laodikia.

17Mwambieni Arkipo hivi: "Hakikisha kuwa unakamilisha ile huduma uliyopokea katika Bwana."

18Mimi, Paulo, naandika salamu hizi kwa mkono wangu mwenyewe. Kumbukeni minyororo yangu. Neema iwe nanyi. Amen.

## 1WATHESALONIKE

### *Utangulizi*

Waraka huu ni mojawapo ya nyaraka za awali kabisa za Paulo. Kutoka Filipi, Paulo katika safari yake ya pili ya kitume, alitembelea mji wa Thesalonike, ambao ulikuwa bandari iliyokuwa kituo cha biashara. Hapa kwenye mji huu Paulo alihudumu kwa majuma matatu, akihudumu katika sinagogi la Wayahudi, akithibitisha Maandiko (Agano la Kale), kwamba Yesu ndiye Kristo. Baadhi ya Wayahudi na Wayunani wakaamini, lakini akalazimika kuondoka huko haraka kwa sababu ya mateso yaliyozuka humo *(Matendo 17:1-9)* kwa kuwa upinzani ulikuwa mkubwa. Akiwa njiani akaelekea Athene na Korintho alitembelea Beroya (*Mdo. 17).*

Timotheo, ambaye alikuwa ametumwa kurudi Thesalonike *(3:1–5)*, baadaye alimletea Pauo taarifa kuhusu hali ilivyo huko Thesalonike. Paulo anawasifu Wathesalonike kwa tabia yao ya ujasiri nyakati za mateso. Pia anaongezea mafundisho yake ya kwanza kuhusu matatizo ya waamini, hasa watu Mataifa ambao hawakuwa na msingi wa Kiyahudi, uliokuwa unakabili maisha ya Ukristo.

Baada ya kufika Athene na hatimaye Korintho, Paulo alipata habari kutoka kwa Timotheo kuwa pamoja na mateso yaliyokuwepo, waamini wa Thesalonike walikuwa wamesimama imara. Kwa hiyo Paulo aliandika barua hii ili kuwatia moyo na kuwafariji waamini ambao walikuwa wachanga katika Kristo. Aliwaandikia pia kuiimarisha imani yao katika misingi ya mafundisho ya kanisa kuhusu Mungu, Roho Mtakatifu na Kristo, maisha yampasayo mkristo na pia kuhusu kurudi kwa Yesu mara ya pili. Yaelekea waamini hawa walikuwa na wasiwasi kwamba wakristo wenzao waliokwisha kufa, wasingeweza kuufikia ufufuo wa wafu. Hivyo Paulo anawaandikia kuwahakikishia kwamba waliokufa wakiwa wanamwamini Kristo watafufuka kwanza *(4:16).*

### *Wazo Kuu*

Paulo anaandika ili kuwathibitishia waamini wachanga katika mafundisho ya msingi aliyokuwa amewafundisha, anawatia moyo kudumu katika utakatifu, nao wale wanaoteswa kuwahakikishia kwamba Mungu yu pamoja nasi na ametuahidi ushindi. Ushindi wa mwisho utapatikana Kristo atakaporudi, wakati Bwana mwenyewe atakaposhuka kutoka mbinguni na kutukusanya Kwake tuwe naye milele *(4:17) .* Tukitambua haya, inatupasa kuvumilia mateso na kuishi maisha yasiyo na lawama, yaani, maisha matakatifu ya kumcha Mungu.

### *Tarehe*

Waraka huu uliandikwa 51 B.K. wakati wa safari yake ya pili.

### *Mahali*

Korintho.

### *Mgawanyo*

- Shukrani za Paulo kwa ajili ya Wathesalonike (1:1-10)
- Huduma ya Paulo katika kanisa (2:1-16)
- Maelezo ya matukio tangu kuondoka Thesalonike (2:7-3:13)
- Mahusia kuhusu mwenendo na maisha ya kumcha Mungu (4:1-12)
- Kurudi kwa Yesu mara ya pili (4:13-5:11)
- Maagizo ya mwisho (5:12-22)
- Hitimisho(5:23-28)

### *Salamu*

**1** Paulo, Silvano na Timotheo,

kwa kanisa la Wathesalonike, ninyi mlio
ndani ya Mungu Baba yetu na ndani ya Bwana
Yesu Kristo:

Neema iwe kwenu na amani itokayo kwa
Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

### *Shukrani Kwa Ajili Ya Imani Ya Wathesalonike*

2 Sikuzote tunamshukuru Mungu kwa ajili
yenu ninyi nyote, tukiwataja kwenye maombi
yetu daima. 3 Tunaikumbuka daima kazi yenu ya
imani mbele za Mungu aliye Baba yetu, taabu
yenu katika upendo na saburi yenu ya tumaini
katika Bwana wetu Yesu Kristo.

4 Ndugu zetu mpendwao na Mungu, kwa
kuwa tunajua kwamba Mungu amewachagua,
5 kwa maana ujumbe wetu wa Injili haukuja
kwenu kwa maneno matupu bali pia
ulidhihirishwa katika nguvu, katika Roho
Mtakatifu, tena ukiwa na uthibitisho kamili, kama
vile ninyi wenyewe mnavyojua jinsi
tulivyoenenda katikati yenu kwa ajili yenu. 6 Ninyi
mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, ingawa
mlipata mateso mengi, mlilipokea lile Neno kwa
furaha katika Roho Mtakatifu. 7 Hivyo ninyi
mkawa kielelezo kwa waamini wote katika
Makedonia na Akaya. 8 Kwa maana kutoka
kwenu Neno la Mungu limesikika, si katika
Makedonia na Akaya tu, bali pia imani yenu
katika Mungu imejulikana kila mahali kiasi
kwamba hatuna haja ya kusema lo lote kwa
habari yake. 9 Kwa maana watu wa maeneo
hayo wenyewe wanaeleza jinsi mlivyotupokea
na jinsi mlivyomgeukia Mungu mkaacha
sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai na wa
kweli 10 na ili kumngojea Mwanawe kutoka
mbinguni, ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa
wafu, yaani, Yesu, Yeye aliyetuokoa kutoka
katika ghadhabu inayokuja.

### *Huduma Ya Paulo Huko Thesalonike*

**2** Ndugu zangu, kwa kuwa ninyi wenyewe
mnajua ya kwamba kuja kwetu kwenu
hakukuwa bure, 2 kama vile mjuavyo, tulikuwa
tumeteswa na kutukanwa huko Filipi, lakini hata
hivyo, kwa msaada wa Mungu wetu, tulikuwa na
ujasiri wa kuwaambia Injili ya Mungu ingawa
kulikuwa na upinzani mkubwa. 3 Kwa maana
maonyo yetu hayakutokana na hila wala nia
mbaya au udanganyifu. 4 Kinyume chake,
tulinena kama watu tuliokubaliwa na Mungu
tukakabidhiwa Injili. Sisi hatujaribu
kuwapendeza wanadamu bali kumpendeza
Mungu, Yeye ayachunguzaye mawazo ya ndani
sana ya mioyo yetu. 5 Kama mjuavyo na Mungu
akiwa shahidi yetu hatukuja kwenu kwa maneno
ya kujipendekeza au maneno yasiyo ya kweli
kwa ajili ya kuficha tamaa mbaya. 6 Wala
hatukuwa tunatafuta sifa kutoka kwa
wanadamu, si kutoka kwenu au kwa mtu
mwingine awaye yote.

Kama mitume wa Kristo tungaliweza kuwa
mzigo kwenu, 7 lakini tulikuwa wapole katikati
yenu kama mama anayewatunza watoto wake
wadogo. 8 Tuliwapenda sana kiasi kwamba
tulifurahia kushirikiana nanyi, si Injili ya Mungu
tu, bali hata maisha yetu, kwa sababu mlikuwa
wa thamani mno kwetu. 9 Ndugu zetu,
mnakumbuka juhudi yetu na taabu yetu,
tulifanya kazi usiku na mchana, ili tusimlemee
mtu ye yote wa kwenu wakati tulipokuwa
tunawahubiria Injili ya Mungu.

10 Ninyi wenyewe ni mashahidi na Mungu
pia, jinsi tulivyokuwa watakatifu, wenye haki na
wasio na lawama miongoni mwenu ninyi
mlioamini. 11 Maana mnajua kwamba
tuliwatendea kila mmoja wenu kama vile baba
awatendeavyo watoto wake mwenyewe:
12 tuliwatia moyo, tuliwafariji na kuwahimiza
kuishi maisha yampendezayo Mungu,
anayewaita katika Ufalme na utukufu Wake.

13 Nasi pia tunamshukuru Mungu bila
kukoma kwa sababu mlipolipokea neno la
Mungu mlilosikia kutoka kwetu, hamkulipokea
kama neno la wanadamu, bali mlilipokea kama
lilivyo hasa, neno la Mungu, litendalo kazi ndani
yenu ninyi mnaoamini. 14 Kwa maana ninyi
ndugu zetu, mlifanyika wafuasi wa makanisa ya
Mungu yaliyoko ndani ya Kristo Yesu katika
Uyahudi. Mlipata mateso yale yale kutoka kwa
watu wenu wenyewe kama vile makanisa hayo
yalivyoteswa na Wayahudi, 15 wale waliomwua
Bwana Yesu na manabii, nasi wakatufukuza
pia. Watu hao walimchukiza Mungu na tena ni
adui wa watu wote, 16 wakijitahidi kutuzuia
tusizungumze na watu Mataifa ili kwamba
wapate kuokolewa. Kwa njia hii wanazidi
kujilundikia dhambi zao ili kufikia upeo. Lakini
hatimaye ghadhabu ya Mungu imewafikia.

### *Paulo Atamani Kuwaona Wathesalonike*

17 Lakini ndugu zetu, tulipotenganishwa nanyi kwa kitambo kidogo, (ingawa kutengana huko kulikuwa kwa mwili tu, si kwa moyo), tulizidi kuwa na shauku kubwa kuwaona uso kwa uso. 18 Maana tulitaka kuja kwenu, hasa mimi Paulo, nilitaka kuja tena na tena, lakini Shetani akatuzuia. 19Kwa maana tumaini letu ni nini, au furaha yetu au taji yetu ya kujisifia mbele za Bwana Yesu Kristo wakati wa kuja Kwake? Je, si ninyi? 20Naam, Ninyi ndio fahari yetu na furaha yetu.

### *Timotheo Atumwa Kwenda Thesalonike*

**3** Kwa hivyo tulipokuwa hatuwezi kuvumilia zaidi, tuliamua tubaki Athene peke yetu, 2tukamtuma Timotheo ambaye ni ndugu yetu na mtumishi mwezetu wa Mungu katika kuieneza Injili ya Kristo, aje kuwaimarisha na kuwatia moyo katika imani yenu, 3ili mtu ye yote asifadhaishwe na mateso haya. Mnajua vema kwamba tumewekewa hayo mateso. 4Kwa kweli, tulipokuwa pamoja nanyi tuliwaambia mara kwa mara kwamba tutateswa na imekuwa hivyo kama mjuavyo: 5Kwa sababu hii nilipokuwa siwezi kuvumilia zaidi, nilimtuma mtu ili nipate habari za imani yenu. Niliogopa kwamba kwa njia fulani yule mjaribu asiwe amewajaribu, nasi tukawa tumejitaabisha bure.

### *Taarifa Ya Timotheo Ya Kutia Moyo*

6Lakini sasa Timotheo ndiyo tu amerejea kwetu kutoka kwenu na ameleta habari njema kuhusu imani yenu na upendo wenu. Ametuambia kwamba sikuzote mnatukumbuka kwa wema na kwamba mna shauku ya kutuona kama vile sisi tulivyo na shauku ya kuwaona ninyi. 7Kwa hiyo, ndugu zetu, katika dhiki na mateso yetu yote tumefarijika kwa sababu ya imani yenu. 8Kwa maana sasa kwa hakika tunaishi kwa kuwa ninyi mmesimama imara katika Bwana. 9Je, tutawezaje kumshukuru Mungu kiasi cha kutosha kwa ajili yenu, kutokana na furaha tuliyo nayo mbele za Mungu wetu kwa sababu yenu? 10Usiku na mchana tunaomba kwa bidii ili tupate kuwaona tena na kujaliza kile kilichopungua katika imani yenu.

11Basi Mungu wetu na Baba yetu Mwenyewe na Bwana wetu Yesu atengeneze njia ya sisi kuja kwenu. 12Bwana na auongeze upendo wenu na kuuzidisha kati ya ninyi kwa ninyi na kwa wengine wote, kama vile tulivyo na upendo mwingi kwenu. 13Tunamwomba Mungu awaimarishe mioyo yenu katika utakatifu ili msiwe na lawama, mbele za Mungu wetu aliye Baba yetu wakati wa kuja kwake Bwana Yesu pamoja na watakatifu wote.

### *Maisha Yanayompendeza Mungu*

**4** Hatimaye, ndugu, tuliwaomba na kuwasihi katika Bwana Yesu kwamba, kama mlivyojifunza kutoka kwetu jinsi iwapasavyo kuishi ili kumpendeza Mungu, kama vile mnavyoishi, imewapasa mzidi sana kufanya hivyo. 2Kwa kuwa mnajua ni maagizo gani tuliyowapa kwa mamlaka ya Bwana Yesu.

3 Kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu ninyi mwe watakatifu, ili kwamba mjiepushe na uasherati, 4ili kwamba kila mmoja wenu ajifunze kuutawala mwili wake mwenyewe katika utakatifu na heshima, 5si kwa tamaa mbaya kama watu Mataifa wasiomjua Mungu. 6Katika jambo hili mtu asimkosee ndugu yake wala kumlaghai. Kwa kuwa Bwana ni mlipiza kisasi katika mambo haya yote, kama vile tulivyokwisha kuwaambia mapema na kuwaonya vikali. 7Kwa maana Mungu hakutuitia uchafu, bali utakatifu. 8Kwa hiyo, mtu ye yote anayekataa mafundisho haya hamkatai mwanadamu, bali anamkataa Mungu anayewapa ninyi Roho Wake Mtakatifu.

9Sasa kuhusu upendano wa ndugu hamna haja mtu ye yote kuwaandikia, kwa maana ninyi wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana. 10Nanyi kwa kweli mnawapenda ndugu wote katika Makedonia nzima. Lakini ndugu, tunawasihi mzidi sana kuwapenda.

11Jitahidini kuishi maisha ya utulivu, kila mtu akijishughulisha na mambo yake mwenyewe na kufanya kazi kwa mikono yake, kama vile tulivyowaagiza, 12ili maisha yenu ya kila siku yajipatie heshima kutoka kwa watu walio nje, ili msimtegemee mtu ye yote.

### *Kuja Kwake Bwana*

13Lakini ndugu, hatutaki msijue kuhusu wale waliolala mauti, ili msihuzunike kama watu wengine wasiokuwa na tumaini. 14Kwa kuwa tunaamini kwamba Yesu alikufa na kufufuka, hata hivyo, Mungu kwa njia ya Yesu atawafufua pamoja naye wale waliolala mauti. 15Kulingana na neno la Mungu mwenyewe tunawaambia kwamba, sisi ambao bado tuko hai, tutakaobaki hadi kuja Kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wale waliolala mauti. 16Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka toka

mbinguni, akitoa amri kwa sauti kuu pamoja na
sauti ya malaika mkuu na sauti ya tarumbeta ya
Mungu, nao wale waliolala mauti wakiwa
wanamwamini Kristo watafufuka kwanza.
17Baada ya hilo sisi tulio hai bado, tuliosalia,
tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili
kumlaki Bwana hewani, hivyo tutakuwa pamoja
na Bwana milele. 18Kwa hiyo farijianeni kwa
maneno haya.

### *Mwe Tayari Kwa Siku Ya Bwana*

**5** Basi, ndugu, kwa habari ya nyakati na
majira hatuna haja ya kuwaandikia, 2kwa kuwa
mnajua vema kwamba siku ya Bwana itakuja
kama mwivi ajapo usiku. 3Wakati watu
wanaposema, “Kuna amani na salama,”
maangamizi huwajia ghafla kama vile utungu
umjiavyo mwanamke mwenye mimba wala
hawatatoroka.

4Bali ninyi, ndugu, hamko gizani hata
kwamba siku ile iwakute ghafula kama mwivi.
5Ninyi nyote ni wana wa nuru na wana wa
mchana. Sisi si wana wa giza wala wa usiku.
6Kwa hiyo basi, tusilale kama watu wengine
walalavyo, bali tukeshe na kuwa na kiasi. 7Kwa
kuwa wote walalao hulala usiku na wale
walewao hulewa usiku. 8Lakini kwa kuwa sisi ni
wana wa mchana, basi tuwe na kiasi, tukijivika
imani na upendo kama dirii kifuani na tumaini
letu la wokovu kama chapeo. 9Kwa maana
Mungu hakutuita ili tupate ghadhabu bali tupate
wokovu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.
10Yeye alikufa kwa ajili yetu ili kwamba kama
tuko macho au tukiwa tumelala tupate kuishi
pamoja Naye. 11Kwa hiyo farijianeni na
kujengana, kama vile mnavyofanya sasa.

### *Maagizo Ya Mwisho, Salamu Na Kuwatakia Heri*

12Sasa tunawaomba, ndugu, waheshimuni
wale wanaofanya kazi kwa bidii miongoni
mwenu, wale ambao wana mamlaka juu yenu
katika Bwana na ambao wanawaonya.
13Mkawajali sana katika upendo kwa ajili ya kazi
yao. Iweni na amani ninyi kwa ninyi. 14Nasi
twawasihi, ndugu, waonyeni wale wavivu,
watieni moyo waoga, wasaidieni wanyonge na
iweni na uvumilivu na kila mtu. 15Angalieni kuwa
mtu asilipe ovu kwa ovu, bali sikuzote tafuteni
kutendeana mema
ninyi kwa ninyi na kwa watu wote.

16Furahini siku zote, 17ombeni pasipo
kukoma, 18shukuruni kwa kila jambo, kwa
maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwa ajili
yenu katika Kristo Yesu.

19Msiuzime moto wa Roho Mtakatifu,
20msiyadharau maneno ya nabii. 21Jaribuni kila
kitu. Yashikeni yaliyo mema. 22Jiepusheni na
uovu wa kila namna.

23Mungu mwenyewe, Mungu wa amani,
awatakase ninyi kabisa, roho zenu, nafsi zenu na miili
yenu, nanyi mhifadhiwe kikamilifu bila kuwa na lawama
katika Bwana wetu Yesu Kristo. 24Yeye aliyewaita ni
mwaminifu naye
atafanya hayo.

25Ndugu, tuombeeni. 26Wasalimuni ndugu
wote kwa busu takatifu.27Nawaagizeni mbele
za Bwana mhakikishe kuwa ndugu wote
wanasomewa barua hii.

28Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe
nanyi. Amen.

### *Utangulizi*

Waraka huu wa pili wa Paulo uliandikwa miezi michache tu baada ya ule wa kwanza. Baadhi ya watu walikuwa wamemwelewa vibaya Paulo au waraka mwingine wa bandia uliosemekana kuwa ulitoka kwa Paulo ulikuwa umewafadhaisha Wathesalonike kuhusu kuja kwa Yesu mara ya pili. Yawezekana kwamba mateso waliyoendelea kuyapata pia yaliwafadhaisha.

Paulo anaandika waraka huu ili kuwakumbusha yale aliyokuwa ametangulia kuwafundisha akiwahakikishia waamini kuwa Kristo atarudi kuwafariji wamwaminio na kuwaadhibu wale wanaowatesa wao *(1:7,8).* Anawaambia kwamba siku ya Bwana, yaani, siku ya hukumu, haitawafikia mara moja, bali itatanguliwa na matukio mbalimbali *(2:3).* Wakifahamu kuwa hakika Kristo atarudi, waamini inawapasa kuishi maisha matakatifu yasiyo na lawama.

### *Wazo Kuu*

Katika waraka huu mfupi, ushindi wa Mungu juu ya uovu unasisitizwa. Ingawa waamini wanaweza kupata mateso sasa, lakini Mungu amewaandalia faraja na thawabu. Lakini wale wanaomkataa Mungu watapata dhiki na watahukumiwa. Paulo pia anasisitiza umuhimu wa kuishi maisha yanayomtukuza Mungu. Baadhi ya watu wa Thesalonike walikuwa wameacha kufanya kazi kwa kuamini kwamba Kristo angerudi upesi. Jambo hili halimtukuzi Mungu na Paulo alisema kuwa mtu ye yote asiyefanya kazi, wala asile. *(3:10).*

### *Mgawanyo*

- Faraja kutokana na kurudi kwa Kristo (1:1-12)
- Matukio kabla ya kuja kwa siku ya Bwana (2:1-12)
- Maagizo zaidi na maonyo (2:13-3:5)
- Mausia ya kikristo na salamu kuwatakia heri (3:6-18).

**1** Paulo, Silvano na Timotheo,

Kwa kanisa la Wathesalonike mlio katika Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo:

2Neema na amani itokayo kwa Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Shukrani Na Maombi*

3Ndugu, imetubidi kumshukuru Mungu kwa ajili yenu sikuzote, kama ulivyo wajibu wetu, kwa sababu imani yenu inakua zaidi na zaidi na upendo wa kila mmoja wenu alio nao kwa mwenzake unazidi kuongezeka. 4Ndiyo sababu miongoni mwa makanisa ya Mungu, tunajivuna kuhusu saburi yenu na imani mliyo nayo katika mateso yote na dhiki mnazostahimili.

5Haya yote ni uthibitisho kwamba hukumu ya Mungu ni ya haki na kwa sababu hiyo ninyi mtahesabiwa kwamba mtastahili Ufalme wa Mungu, ambao ninyi mnateswa kwa ajili Yake. 6Mungu ni mwenye haki: Yeye atawalipa mateso wale wawatesao ninyi 7na kuwapa ninyi mnaoteseka raha pamoja na sisi, wakati Bwana Yesu atakapodhihirishwa kutoka mbinguni katika mwali wa moto pamoja na malaika wake wenye nguvu. 8Atawaadhibu wale wasiomjua Mungu na ambao hawakuitii Injili ya Bwana wetu Yesu. 9Wataadhibiwa kwa uangamivu wa milele na kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa uweza Wake, 10siku hiyo atakapokuja kutukuzwa katika watakatifu wake na kustaajabiwa miongoni mwa wote walioamini. Ninyi pia mtakuwa miongoni mwa hawa kwa sababu mliamini ushuhuda wetu kwenu.

11Kwa sababu hii, tunawaombea ninyi bila kukoma, ili kwamba Mungu apate kuwahesabu kuwa mnastahili wito Wake na kwamba kwa uwezo Wake apate kutimiza kila kusudi lenu jema na kila tendo linaloongozwa na imani yenu. 12Tunaomba hivi ili Jina la Bwana wetu Yesu lipate kutukuzwa ndani yenu, nanyi ndani Yake, kulingana na neema ya Mungu wetu na Bwana Yesu Kristo.

### *Yule Mtu Wa Kuasi*

**2** Ndugu, kuhusu kuja Kwake Bwana wetu Yesu Kristo na kukusanyika kwetu pamoja mbele Zake, tunawasihi, 2msiyumbishwe kwa urahisi wala msitiwe wasiwasi na roho wala neno au barua inayosemekana kuwa imetoka kwetu, isemayo kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwako. 3Mtu ye yote na asiwadanganye kwa namna yo yote kwa maana siku ile haitakuja mpaka uasi utokee kwanza na yule mtu wa kuasi adhihirishwe, yule ambaye amehukumiwa kuangamizwa kabisa. 4 Yeye atapingana na kujitukuza juu ya kila kitu kiitwacho Mungu au kinachoabudiwa, ili kujiweka juu katika hekalu la Mungu, akijitangaza mwenyewe kuwa ndiye Mungu.

5Je, hamkumbuki ya kwamba nilipokuwa pamoja nanyi niliwaambia mambo haya? 6Nanyi sasa mnajua kinachomzuia, ili kwamba apate kudhihirishwa wakati wake utakapowadia. 7Maana ile nguvu ya siri ya uasi tayari inatenda kazi, lakini yule anayeizuia ataendelea kufanya hivyo mpaka atakapoondolewa. 8Hapo ndipo yule mwasi atafunuliwa, ambaye Bwana Yesu atamteketeza kwa pumzi ya kinywa Chake na kumwangamiza kabisa kwa ufunuo wa kuja Kwake. 9Kuja kwa yule mwasi kutaonekana kana kwamba ni kutenda kazi kwake Shetani ambaye hutumia nguvu zote, ishara, maajabu ya uongo 10na kila aina ya udanganyifu kwa wale wanaoangamia kwa sababu walikataa kuipenda kweli wapate kuokolewa. 11Kwa sababu hii, Mungu ameruhusu watawaliwe na nguvu ya udanganyifu, ili waendelee kuamini uongo 12na hivyo wote wahukumiwe ambao hawakuamini ule ukweli bali wamefurahia uovu.

### *Simameni Imara*

13Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu daima kwa ajili yenu, ndugu mpendwao na Bwana, kwa sababu Mungu aliwachagua ninyi tangu mwanzo ili mwokolewe kwa kutakaswa na Roho na kwa kuiamini katika kweli. 14Kwa kusudi hili Mungu aliwaita kwa njia ya kuhubiri kwetu Injili, ili kwamba mpate kushiriki katika utukufu wa Bwana Yesu Kristo. 15Hivyo basi, ndugu wapendwa, simameni imara na myashike sana yale mafundisho tuliyowapa ikiwa ni kwa maneno ya kinywa au kwa barua.

16Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe na Mungu Baba yetu, aliyetupenda na kwa neema Yake akatupatia faraja ya milele na tumaini jema, 17awafariji mioyo yenu na kuwaimarisha katika kila neno na tendo jema.

### *Ombi La Kuhitaji Maombi*

**3** Hatimaye, ndugu, tuombeeni ili kwamba Neno la Bwana lipate kuenea kwa haraka na kuheshimiwa kila mahali, kama vile

ilivyokuwa kwa upande wenu. 2Ombeni pia ili
kwamba tupate kuokolewa kutokana na watu
waovu na wabaya, kwa maana si kila mmoja
ana imani. 3Lakini Bwana ni mwaminifu, naye
atawaimarisha ninyi na kuwalinda kutokana na
yule mwovu. 4Nasi tuna tumaini katika Bwana
ya kuwa mnafanya na mtaendelea kufanya yale
tuliyowaagiza. 5Bwana aiongoze mioyo yenu
katika upendo wa Mungu na katika saburi ya
Kristo.

### *Onyo Dhidi Ya Uvivu*

6Ndugu, tunawaagiza katika Jina la Bwana
Yesu Kristo, jitengeni na kila ndugu ambaye ni
mvivu na ambaye haishi kufuatana na maagizo
tuliyowapa. 7Maana ninyi wenyewe mnajua jinsi
iwapasavyo kufuata mfano wetu. Sisi hatukuwa
wavivu tulipokuwa pamoja nanyi, 8wala hatukula
chakula cha mtu ye yote pasipo kukilipia. Badala
yake tulifanya kazi kwa bidii usiku na mchana, ili
tusimlemee mtu ye yote miongoni mwenu.
9Tulifanya hivi, si kwa sababu hatukuwa na haki
ya kupata msaada kama huo, lakini ili kusudi
tujifanye sisi wenyewe kuwa kielelezo.” 10Kwa
maana hata tulipokuwa pamoja nanyi, tuliwapa
amri ili kwamba: ‘‘Mtu ye yote asiyetaka kufanya
kazi, wala asile.’’

11Kwa kuwa tunasikia kwamba baadhi ya
watu miongoni mwenu ni wavivu. Hawafanyi
kazi bali hujishughulisha na mambo ya wengine.
12Basi watu kama hao tunawaagiza na
kuwaonya katika Jina la Bwana Yesu Kristo
wafanye kazi kwa utulivu na kujipatia mahitaji ya
maisha yao wao wenyewe. 13Kwa upande
wenu, ndugu, ninyi kamwe msichoke katika
kutenda mema.

14Ikiwa mtu ye yote hayatii maagizo yetu
yaliyoko katika barua hii, mwangalieni sana mtu
huyo. Msishirikiane naye, ili kwamba apate
kuona aibu. 15Lakini msimhesabu kuwa adui,
bali mwonyeni kama ndugu.

### *Salamu Za Mwisho*

16Basi, Bwana wa amani mwenyewe
awapeni amani nyakati zote na kwa kila njia.
Bwana awe nanyi nyote.

17Mimi, Paulo, ninaandika salamu hizi kwa
mkono wangu mwenyewe. Hii ndio alama ya
utambulisho katika barua zangu zote. Hivi
ndivyo niandikavyo.

18 Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe
nanyi nyote. Amen.

**1TIMOTHEO**

### *Utangulizi*

Waraka wa Kwanza, wa Pili kwa Timotheo na wa Tito kwa kawaida hutambuliwa kama nyaraka za Kichungaji zilizoandikwa na Paulo. Paulo aliandika waraka huu karibu na kufa kwake. Alimwandikia Timotheo msaidizi wake, ambaye alikuwa amemwacha huko Efeso kusahihisha matatizo kadhaa katika kanisa hilo. Wakati huu kulikuwa na matatizo kuhusu mafundisho ya Kikristo, mwenendo wa kanisa, uongozi wa kanisa na mambo kadha wa kadha kuhusu mwenendo uwapasao waamini. Paulo aliandika ili kumpa Timotheo maagizo kuhusu mambo haya kusudi kanisa lifanye kazi yake vema. Aliandika pia kumtia moyo Timotheo asichoke katika maisha yake ya kikristo, bali aishi maisha ya ukamilifu kwa utukufu wa Mungu. Pia anatoa masharti maalumu kuhusu viongozi wa kanisa. Muda mfupi tu baada ya hili alikamatwa na kurudishwa tena Rumi kama mfungwa, ambako ndiko alikoandikia Waraka wa pili kwa Timotheo.

Timotheo alizaliwa huko Listra akiwa na baba Myunani na mama Myahudi (ambaye alimfundisha Maandiko tangu utoto). Paulo alipofika Listra katika safari yake ya pili ya kitume *(Mdo.16:1-3)*, alimchagua Timotheo ambaye alishirikiana na Paulo hadi mwisho wa huduma yake. Timotheo mwenyewe alifungwa lakini hatimaye aliachiwa huru *(Ebr.13:23).*

Waraka wa kwanza kwa Timotheo uko katika mfumo wa mazungumzo ambayo ni ya kibinafsi sana. Paulo anamwelekeza Timotheo kuhusu sifa na wajibu wa viongozi mbalimbali katika kanisa.Pia anatoa mwongozo kwa Timotheo katika wajibu wake wa kichungaji, akimwagaliza majukumu, pamoja na yale yampasayo kama “ mtu wa Mungu*”(6:11)*

### *Wazo kuu*

Jambo kuu katika waraka huu ni umuhimu wa kuwa na imani sahihi, mwenendo mnyofu na uadilifu. Paulo anakazia kwamba waamini inawapasa kuifahamu kweli na kuitetea dhidi ya mafundisho ya uongo yanayojitokeza. Pia hawana budi kuishi maisha yanayofanana ya mafundisho hayo ili Shetani asipate nafasi kuwateka watu wa Mungu. Kadhalika anatia mkazo umuhimu wa kuwa na viongozi wa kanisa waliojitoa, wenye sifa zote na pia wenye moyo safi.

### *Tarehe*

Nyaraka hizi ziliandikwa baada ya kifungo cha kwanza cha Paulo huko Rumi ambacho kinandikwa kwenye kitabu cha Matendo *(Mdo.28),* huenda kati ya 63 – 65 B.K. Kwa kuwa vitabu vya Agano Jipya havitoi habari za mfululizo za muendelezo wa Ukristo baada ya wakati huu, nukuu za Nyaraka hizi za Kichungaji zinatoa msingi kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa Paulo. Huenda Paulo aliachiwa kati ya 60 au 61 B.K. na kuyatembelea tena makanisa ya Asia. Akiwa njiani kwenda Makedonia, Paulo alimwacha Timotheo huko Efeso *(1:3)*. Paulo alielekea Krete, ambako alihudumu kwa muda mfupi, kisha akawaacha waamini chini ya uongozi wa Tito *(Tit.1:5)* wakati yeye akielekea Dalmatia.

### *Mahali*

Waraka wa kwanza kwa Timotheo huko Efeso na ule wa Tito huko Krete zimeandikwa na Paulo akiwa safarini, huenda akiwa Makedonia.

### *Mgawanyo*

- Maonyo kuhusu mafundisho ya uongo (1:1-20)
- Mafundisho kuhusu maombi (2:1-15)
- Sifa zinazowapasa waangalizi na wazee wa kanisa (3:1-16)
- Maonyo na huduma (4:1- 5:25)
- Huduma ya kikristo na maagizo kwa Timotheo (6:1-21)

### *Salamu*

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na ya Kristo Yesu tumaini letu.

2Kwa Timotheo, mwanangu mwaminifu katika imani:

Neema, rehema na amani kutoka kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.

### *Maonyo Dhidi Ya Walimu Wa Uongo*

3Kama nilivyokusihi kuendelea kubaki Efeso, wakati nilipokwenda Makedonia, ili kwamba upate kuwaagiza watu wasiendelee kufundisha mafundisho ya uongo 4wala wasitoe muda wao kwa hadithi za kubuniwa na orodha zisizo na mwisho za majina ya vizazi ambazo huchochea mabishano badala ya mpango wa kimungu utokanao na imani. 5Kusudi la maagizo haya ni upendo, utokao katika moyo safi, dhamiri njema na imani ya kweli. 6Watu wengine wamepotoka kutoka katika haya na kugeukia majadiliano yasiyo na maana kwa kuwa, 7wanataka kuwa walimu wa sheria, lakini hawajui mambo yale wanayosema wala hayo wanayoyatumainia kwa uthabiti.

8Tunajua kwamba sheria ni njema ikiwa inatumika kwa halali kama ilivyokusudiwa. 9Lakini tunajua ya kuwa sheria si kwa ajili ya wenye haki, bali kwa ajili ya wavunja sheria na waasi, kwa ajili ya wasiomcha Mungu na wenye dhambi, wasio watakatifu na wanaokufuru, kwa wale wawauao baba zao au mama zao, kwa wauaji, 10kwa wazinzi, walawiti, wauza watu, kwa waongo, waapao kwa uongo na cho chote kingine kilicho kinyume na mafundisho ya kweli, 11ambayo yanakubaliana na Injili ya utukufu wa Mungu anayehimidiwa, ambayo mimi Paulo nimewekea amana.

### *Neema Ya Mungu Kwa Paulo*

12Namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu, kwa sababu aliniona mwaminifu, akaniteua kwa kazi yake. 13 Ingawa wakati fulani nilikuwa mwenye kukufuru, mtesaji na mwenye jeuri. Lakini nilipata rehema kwa sababu nilitenda hivyo kwa kutokujua na kutokuamini kwangu. 14Neema ya Bwana wetu ilimiminwa juu yangu kwa wingi, ikiambatana na imani na upendo ulio katika Kristo Yesu.

15Msemo huu ni wa kweli na unaostahili kukubalika, usemao kwamba: Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi, ambao mimi ndiye niliye mbaya kuliko wote. 16Lakini kwa sababu hiyo nilipata rehema, ili kwamba katika mimi niliyekuwa mwenye dhambi kuliko wote, Kristo Yesu apate kuonyesha uvumilivu wake usio na kikomo, niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini wapate uzima wa milele. 17Basi, Mfalme wa milele, asiye na mwisho, asiyeonekana, aliye Mungu pekee, apewe heshima na utukufu milele na milele. Amen.

18Mwanangu Timotheo, ninakupa agizo hili, kwa kadiri ya maneno ya unabii yaliyosemwa kukuhusu, ili kwa kuyafuata upate kupigana vile vita vizuri, 19ukiishikilia imani na dhamiri njema ambayo wengine wamevikataa na hivyo, wakaangamia kwa habari ya imani yao. 20Miongoni mwao wako Himenayo na Aleksanda, ambao nimemkabidhi Shetani ili wafundishwe wasije wakakufuru.

### *Maagizo Kuhusu Kuabudu*

2 Awali ya yote, nasihi, kwanza kabisa, naagiza kwamba dua, sala, maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote: 2kwa ajili ya wafalme na wale wote wenye mamlaka, ili tupate kuishi kwa amani na utulivu, katika uchaji wote wa Mungu na utakatifu. 3Jambo hili ni jema tena linapendeza machoni pa Mungu Mwokozi wetu 4anayetaka watu wote waokolewe na wafikie kuijua kweli. 5 Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani, mwanadamu Kristo Yesu, 6aliyejitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wanadamu wote, jambo hili lilishuhudiwa kwa wakati wake. 7Nami kwa kusudi hili nimewekwa niwe mhubiri na mtume, (nasema kweli katika Kristo wala sisemi uwongo,) mwalimu wa watu Mataifa katika imani na kweli.

8Nataka kila mahali wanaume wasali wakiinua mikono mitakatifu pasipo hasira wala kugombana.

9Vivyo hivyo nataka wanawake wajipambe kwa adabu na kwa heshima katika mavazi yanayostahili, si kwa kusuka nywele, kuvalia dhahabu, lulu au mavazi ya gharama kubwa, 10bali kwa matendo mazuri kama iwapasavyo wanawake wanaokiri kuwa wanamcha Mungu.

11Mwanamke na ajifunze kwa utulivu na kwa utii wote. 12Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha au kuwa na mamlaka juu ya

mwanaume. Mwanamke inampasa kukaa kimya. 13Kwa maana Adamu aliumbwa kwanza, kisha Eva. 14Wala si Adamu aliyedanganywa, bali ni mwanamke aliyedanganywa akawa mkosaji. 15Lakini mwanamke ataokolewa kwa kuzaa kwake kama wakiendelea kudumu katika imani, upendo na utakatifu, pamoja na kuwa na kiasi.

### *Sifa Za Waangalizi*

**3** Hili ni neno kweli, kwamba mtu akitamani kazi ya askofu, atamani kazi nzuri. 2Basi, imempasa askofu awe mtu asiye na lawama, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi, anayejitawala, anayeheshimika, mkarimu, ajuaye kufundisha. 3Asiwe mlevi, wala mkali bali awe mpole, asiwe mgomvi wala mpenda fedha. 4Lazima aweze kuisimamia nyumba yake mwenyewe vizuri na kuhakikisha kwamba watoto wake wanamtii na kuwa na heshima kwa kila njia. 5 (Kwa maana kama mtu hajui jinsi ya kusimamia nyumba yake mwenyewe atawezaje kuliangalia kanisa la Mungu?) 6Asiwe mtu aliyeongoka karibuni asije akajivuna na kuangukia kwenye hukumu ile ile ya Shetani. 7Inampasa pia awe na sifa njema kwa watu walio nje, ili asije akalaumiwa na kuanguka kwenye mtego wa ibilisi.

### *Sifa Za Mashemasi*

8Vivyo hivyo, mashemasi nao wawe watu wanaostahili heshima, wasiwe wenye kauli mbili au wenye kujifurahisha kwa mvinyo, wala wanaotamani faida isiyo halali. 9Inawapasa kushikamana sana na ile siri ya imani kwa dhamiri safi. 10Ni lazima wapimwe kwanza, kisha kama hakuna neno dhidi yao, basi na waruhusiwe kuhudumu kama mashemasi.

11Vivyo hivyo wake zao wawe wanawake wanaostahili heshima, wasiozungumza maneno ya kuwadhuru wengine, bali wawe na kiasi na waaminifu katika kila jambo.

12Shemasi awe mume wa mke mmoja na inampasa aweze kusimamia watoto wake na watu wa nyumbani mwake vema. 13Wale ambao wamehudumu vema katika huduma ya ushemasi hujipatia msimamo bora na ujasiri mkubwa katika imani yao ndani ya Kristo Yesu.

14Ingawa ninatarajia kuja kwako hivi karibuni, ninakuandikia maagizo haya sasa ili kwamba, 15kama nikikawia, utajua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, ambayo ndiyo kanisa la Mungu aliye hai, lililo nguzo na msingi wa kweli. 16Bila shaka yo yote, siri ya utauwa ni kubwa:

Alidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu,
alithibitishwa kuwa na haki katika Roho,
akaonekana na malaika,
akahubiriwa miongoni mwa
mataifa, akaaminiwa ulimwenguni,
akachukuliwa juu katika utukufu.

### *Maagizo Kwa Timotheo*

**4** Roho asema waziwazi kwamba katika siku za mwisho baadhi ya watu wataiacha imani na kufuata roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani. 2Mafundisho kama hayo huja kwa kupitia kwa waongo ambao ni wanafiki hali dhamiri zao zikiungua kwa kuchomwa na moto. 3Wao huwakataza watu wasioe na kuwaagiza wajiepushe na vyakula fulani, ambavyo Mungu aliviumba ili vipokewe kwa shukrani na wale wanaoamini na kuijua kweli. 4Kwa maana kila kitu alichokiumba Mungu ni chema, wala hakuna kitu cho chote cha kukataliwa kama kikipokewa kwa shukrani, 5kwa sababu kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba.

### *Mtumishi Mwema Wa Yesu Kristo*

6Kama ukiwakumbusha ndugu mambo haya, utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, uliyelelewa katika kweli ya imani na yale mafundisho mazuri uliyoyafuata. 7Usijishughulishe kamwe na hadithi za kipagani na masimulizi ya uongo ya wanawake wazee, badala yake, jizoeze kuwa mtauwa. 8Kwa maana mazoezi ya mwili yanafaida kwa sehemu, lakini utauwa una faida katika mambo yote, yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa na ya ule ujao.

9Hili ni neno la kuaminiwa tena lastahili kukubaliwa kabisa, 10(nasi kwa ajili ya hili tunajitaabisha na kujitahidi), kwamba tumeweka tumaini letu kwa Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote, hasa wale waaminio.

11Mambo haya yaagize na kuyafundisha. 12Mtu ye yote asikudharau kwa kuwa wewe ni kijana, bali uwe kielelezo kizuri kwa waaminio katika usemi, mwenendo, upendo, imani na usafi. 13Fanya bidii kusoma Maandiko hadharani, kuhubiri na kufundisha, mpaka nitakapokuja. 14Usiache kutumia kipawa kilicho ndani yako, ambacho ulipewa kwa neno la unabii wakati wazee walipokuwekea mikono.

15Uwe na bidii katika mambo haya, jitolee kwa ajili ya mambo hayo kikamilifu, ili kila mtu aone kuendelea kwako. 16Jilinde sana nafsi yako na mafundisho yako. Dumu katika hayo, kwa maana kwa kufanya hivyo utajiokoa wewe mwenyewe pamoja na wale wanaokusikia.

### *Maagizo Kuhusu Wajane, Wazee Na Watumwa*

**5** Usimkemee mzee kwa ukali bali umwonye kama vile angekuwa ni baba yako.
Uwatendee vijana kama vile ndugu zako,
2wanawake wazee uwatendee kama mama zako na wanawake vijana kama dada zako, katika usafi wote.

3Waheshimu wanawake wajane ambao ni
wajane kweli kweli. 4Kama mjane ana watoto ama wajukuu, hawa inawapasa awali ya yote wajifunze kutimiza wajibu wao wa kumcha Mungu katika matendo, kuwatunza wale wa jamaa zao wenyewe ili wawarudishie wema ule wazazi wao waliowatendea, kwa kuwa hivi
ndivyo impendazavyo Mungu. 5Mwanamke ambaye ni mjane kweli kweli, yaani, yeye aliyebaki peke yake huweka tumaini lake kwa Mungu naye hudumu katika maombi usiku na
mchana akimwomba Mungu ili amsaidie. 6Lakini mjane aishiye kwa anasa, amekufa, ingawa
anaishi. 7Wape watu maagizo haya pia, ili
asiwepo ye yote wa kulaumiwa. 8Kama mtu hawatunzi wale wa jamaa yake, hasa wale wa nyumbani mwake mwenyewe, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko yeye asiyeamini.

9Mjane ye yote asiwekwe kwenye orodha ya wajane isipokuwa awe ametimiza umri wa miaka sitini na ambaye alikuwa mke wa mume mmoja,
10awe ameshuhudiwa kwa matendo yake mema, aliyewalea watoto wake vizuri, aliye mkarimu, aliyewanawisha watakatifu miguu, aliyewasaidia wenye shida na aliyejitolea kwa ajili ya matendo mema ya kila namna.

11Lakini kwa habari za wajane vijana usiwaweke kwenye orodha hiyo, maana tamaa zao za kimaumbile zikizidi kule kujitoa kwao kwa
Kristo, watataka kuolewa tena. 12Nao kwa njia hiyo watajiletea hukumu kwa kukiuka ahadi yao
ya kwanza. 13 Zaidi ya hayo, wajane kama hao huwa na tabia ya uvivu wakizurura nyumba kwa nyumba, wala hawawi wavivu tu, bali pia huwa wasengenyaji, wajiingizao katika mambo yasiyowahusu na kusema mambo
yasiyowapasa kusema. 14Hivyo nawashauri wajane vijana waolewe, wazae watoto na wasimamie nyumba zao, wasije wakampa adui
nafasi ya kutushutumu. 15Kwa maana kwa kweli wajane wengine wamepotoka ili kumfuata Shetani.

16Lakini kama mwanamke ye yote aaminiye anao wajane katika jamaa yake, inampasa awasaidie wala si kuwaacha wakililemea kanisa, ili kanisa liweze kuwasaidia wale ambao ni wajane kweli kweli.

### *Wazee Wa Kanisa*

17Wazee wa kanisa wanaoongoza shughuli za kanisa vizuri wanastahili heshima mara mbili, hasa wale ambao kazi yao ni kuhubiri na
kufundisha. 18Kwa maana Maandiko husema, "Usimfunge ng'ombe kinywa apurapo nafaka," tena, "Mfanyakazi anastahili mshahara wake."
19Usiendekeze mashtaka dhidi ya mzee ila yawe
yameletwa na mashahidi wawili au watatu. 20Wale wanaodumu katika dhambi uwakemee hadharani, ili wengine wapate kuogopa.

21 Ninakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu na mbele za malaika wateule, shika maagizo haya pasipo ubaguzi wala upendeleo.

22Usiwe na haraka kumwekea mtu mikono wala usishiriki dhambi za watu wengine. Jilinde nafsi yako uwe safi.

23Acha kunywa maji peke yake, tumia divai kidogo kwa sababu ya tumbo lako na maumivu yako ya mara kwa mara.

24Dhambi za watu wengine ni dhahiri nazo zinawatangulia kwenda hukumuni na dhambi za
watu wengine zinawafuata nyuma yao. 25Vivyo hivyo, matendo mema yako dhahiri na hata yale ambayo si mema hayawezi kufichika.

### *Watumwa*

**6** Wale wote walio chini ya kongwa la utumwa inawapasa kuwahesabu mabwana zao kuwa wanastahili heshima yote, ili jina la
Mungu lisitukanwe wala mafundisho yetu. 2Wale watumwa ambao wana mabwana waaminio, haiwapasi kupunguza heshima yao kwa sababu wao ni ndugu, badala yake, wawatumikie hata vizuri zaidi, kwa sababu wale wanaonufaika na huduma yao ni waaminio, ambao ni wapenzi wao.

### *Mafundisho Ya Uongo Na Utajiri Wa Kweli*

3Ikiwa mtu ye yote atafundisha mafundisho mapotofu wala hakubaliani na mafundisho manyofu ya Bwana wetu Yesu Kristo na yale ya utauwa, huyo amejivuna wala hajui kitu cho

chote. 4Yeye ni mgonjwa aliyejaa tamaa ya
mabishano na ugomvi ambayo matokeo yake ni
wivu na mapigano, maneno ya ukorofi, shuku
mbaya 5na kuzozana kusikokoma kati ya watu
walioharibika akili zao, walioikosa kweli na
ambao hudhani kwamba utauwa ni njia ya
kupata faida.
6Lakini utauwa na kuridhika ni faida kubwa.
7Kwa kuwa hatukuja humu duniani na kitu cho
chote, wala hatuwezi kutoka humu na kitu.
8Lakini kama tuna chakula na mavazi,
tutaridhika navyo. 9Lakini wale watu
wanaotamani kuwa na mali kwa haraka haraka
huanguka kwenye majaribu na wamenaswa na
tamaa nyingi za kipumbavu, zenye kudhuru,
zinazowazamisha watu katika uharibifu na
maangamizi. 10Kwa maana kupenda fedha
ndiyo shina moja la maovu ya kila namna.
Baadhi ya watu wakitamani fedha, wameiacha
amani na kujichoma wenyewe kwa maumivu
mengi.

### *Vitu Vizuri Vya Imani*

11Lakini wewe, mtu wa Mungu, yakimbie
mambo haya yote. Fuata haki, utauwa, imani,
upendo, saburi na upole. 12Pigana vile vita
vizuri vya imani. Shika uzima wa milele ambao
ndio ulioitiwa ulipokiri ule ukiri mzuri mbele ya
mashahidi wengi. 13Nakuagiza mbele za Mungu
avipaye vitu vyote uhai na mbele za Kristo Yesu
ambaye alipokuwa anashuhudia mbele ya
Pontio Pilato alikiri ukiri mzuri, 14uishike amri hii
bila dosari wala lawama mpaka kuja kwake
Bwana wetu Yesu Kristo, 15ambaye Mungu
atamleta kwa wakati wake mwenyewe, Yeye
ahimidiwaye, aliye peke yake Mtawala, Mfalme
wa wafalme na Bwana wa mabwana. 16Yeye
peke yake hapatikani na mauti, ambaye anakaa
katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye
hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye
kumwona. Heshima na uweza una Yeye milele.
Amen.

17Waagize wale ambao ni matajiri wa
ulimwengu huu waache kujivuna, wala
wasiweke tumaini lao katika mali ambayo si ya
hakika, bali waweke tumaini lao katika Mungu
ambaye hutupatia vitu vyote kwa wingi ili
tuvifurahie. 18Waagize watende mema, wawe
matajiri katika matendo mema, pia wawe
wakarimu na walio tayari kushiriki mali zao na
wengine. 19 Kwa njia hii watajiwekea hazina
kama msingi kwa ajili ya wakati ujao na hivyo
watajipatia uzima, yaani, ule uzima ambao ni wa
kweli.

### *Maelekezo Ya Binafsi Na Maombi Ya Baraka*

20Timotheo, linda kile kilichowekwa amana
kwako. Epuka majadiliano yasiyo ya utauwa na
mabishano ambayo kwa uongo huitwa elimu,
21ambayo wengine kwa kujidai kuwa nayo
wameiacha imani.

Neema iwe nanyi. Amen.

## 2Timotheo

### *Utangulizi*

Paulo alikuwa amefungwa tena huko Rumi chini ya utawala wa Nero. Pengine huu ulikuwa waraka wa mwisho kabisa wa Paulo. Baada ya kuandika waraka wake wa kwanza kwa Timotheo msaidizi wake, huenda akiwa Makedonia, inaelekea Paulo alikamatwa aidha akiwa Troa au Nikopili *(Tit.3:12)* na kurudishwa gerezani huko Rumi.

Katika waraka huu inakuwa kama vile Paulo anahisi fursa zake za kuhubiri Injili zinakaribia kikomo *(4:6 – 8).* Ndani ya waraka huu wa binafsi Paulo anaeleza hisia zake za ndani kabisa. Anamkumbusha Timotheo kwamba hata kama maisha yake hapa duniani yatakoma, Mungu alikuwa amemwandalia maisha ya milele *(1:10-12).* Paulo pia anakumbusha juu ya uaminifu wa Mungu ambaye amemwongoza katika maisha yake yote. Anagusia juu ya nyakati za hatari ambazo zingekuja, siku za taabu ambazo watu wataiacha kweli na kupenda anasa kuliko kummpenda Mungu*(3:1-8).*

Wakati huu Paulo alikuwa mpweke na alitamani sana Timotheo aje aungane naye *(4:9, 21).* Anajitahidi kumtia Timotheo moyo na kumwimarisha kwa ajili ya kazi kubwa aliyokabidhiwa. Paulo anatamani kumwona Timotheo tena, akimwomba amletee vile vitabu vya ngozi alivyokuwa ameviacha Troa.

Anamwagiza Timotheo asimame imara katika mateso yajayo na kuilinda imani iliyo nyofu.

### *Wazo kuu*

Barua hii inazungumzia hasa kuhusu uweza wa Mungu juu ya vitu vyote. Ingawa mateso yanakuja na yataendelea kuongezeka, Mungu anatawala. Kwa hiyo wote wamwaminio haiwapasi kuogopa kitu cho chote. Paulo anatoa ushuhuda wa imani yake, akieleza jinsi alivyopigana vita kwa ajili ya kweli na jinsi atakavyopewa thawabu siku ya mwisho *(4:6-8).*

### *Tarehe*

Waraka huu uliandikwa kati ya 66 – 67 B.K. wakati wa utawala wa Nero.

### *Mahali*

Rumi.

### *Mgawanyo*

- Shukrani za Paulo kwa ajili ya Timotheo (1:1-5)
- Maagizo ya Paulo kwa Timotheo (1:6-2:2)
- Sifa za mtumishi mwaminifu (2:3-26 )
- Mateso yajayo (3:1-17)
- Maneno ya mwisho(4:1-22).

### *Salamu*

**1** Paulo mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya
Mungu, kulingana na ile ahadi
ya uzima uliomo ndani ya Kristo Yesu.

2Kwa Timotheo, mwanangu mpendwa:

Neema, rehema na amani kutoka kwa
Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.

### *Shukrani Na Kutiwa Moyo*

3Ninamshukuru Mungu, ninayemtumikia
kwa dhamiri safi, kama walivyofanya baba
zangu, ninapokukumbuka usiku na mchana
katika maombi yangu. 4Nikiyakumbuka machozi
yako, ninatamani sana kukuona ili nipate kujawa
na furaha. 5Nimekuwa nikiikumbuka imani yako
ya kweli, waliokuwa nayo bibi yako Loisi na
mama yako Eunike na ambayo mimi nina sadiki
sasa wewe nawe unayo. 6Kwa sababu hii
nakukumbusha uchochee ile karama ya Mungu,
iliyowekwa ndani yako nilipokuwekea mikono
yangu. 7Maana Mungu hakutupa roho ya woga,
bali roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa
kiasi.

8Kwa hiyo usione haya kushuhudia kuhusu
Bwana wetu, wala usinionee haya mimi niliye
mfungwa kwa ajili Yake, bali uishiriki pamoja
nami taabu ya Injili kwa kadiri ya nguvu ya
Mungu, 9ambaye alituokoa na kutuita katika
mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu
mema bali kwa sababu ya kusudi Lake
mwenyewe na neema Yake. Neema hii tulipewa
katika Kristo Yesu kabla ya kuwako kwa
ulimwengu. 10Lakini sasa imefunuliwa kwa
kudhihirishwa Kwake Mwokozi wetu, Kristo
Yesu, ambaye amebatilisha mauti na kuleta
uzima na kutokufa kwa njia ya Injili. 11Nami
nimewekwa kuwa mhubiri, mtume na mwalimu
wa Injili hii. 12Hii ndiyo sababu ninateseka
namna hii, lakini sioni haya kwa maana
ninamjua Yeye niliyemwamini na kusadiki ya
kuwa anaweza kukilinda kile nilichokiweka
amana Kwake hadi siku ile.

13Shika kwa uthabiti kielelezo cha
mafundisho yenye uzima yale uliyoyasikia
kwangu pamoja na imani na upendo katika
Kristo Yesu. 14Ilinde ile amana uliyokabidhiwa
kwa Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu.

15Unajua ya kuwa watu wote katika Asia
wameniacha, miongoni mwao wamo Filego na
Hermogene.

16Bwana akawahurumie watu wa nyumbani
mwa Onesiforo, kwa sababu aliniburudisha
mara kwa mara wala hakuonea aibu minyororo
yangu. 17Badala yake, alipokuwa Rumi,
alinitafuta kwa bidii mpaka akanipata. 18Bwana
na amjalie kupata rehema kutoka kwa Bwana
siku ile! Nawe unajua vema jinsi alivyonisaidia
huko Efeso.

### *Askari Mwema Wa Kristo Yesu*

**2** Basi, wewe mwanangu, uwe hodari katika
neema iliyo ndani ya Kristo Yesu. 2Nayo
mambo yale uliyonisikia nikiyasema mbele ya
mashahidi wengi, uwakabidhi watu waaminifu
watakaoweza kuwafundisha watu wengine vile
vile. 3Vumilia taabu pamoja nasi kama askari
mwema wa Kristo Yesu. 4Hakuna askari ye yote
ambaye akiwa vitani hujishughulisha na mambo
ya kawaida ya maisha haya kwa sababu nia
yake ni kumpendeza yule aliyemwandika awe
askari. 5 Vivyo hivyo, yeye ashindanaye katika
michezo hawezi kupewa tuzo ya ushindi
asiposhindana kulingana na kanuni za
mashindano.6Mkulima mwenye bidii ya kazi
ndiye anayestahili kuwa wa kwanza kupata
fungu la mavuno.7Fikiri sana kuhusu haya
nisemayo, kwa maana Mungu atakupa ufahamu
katika mambo hayo yote.

8Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuka kutoka
kwa wafu, Yeye aliye wa uzao wa Daudi. Hii
ndiyo Injili yangu, 9ambayo kwayo ninateseka
hata kufikia hatua ya kufungwa minyororo kama
mhalifu. Lakini neno la Mungu halifungwi. 10Kwa
hiyo ninavumilia mambo yote kwa ajili ya
wateule wa Mungu, kusudi wao nao wapate
wokovu ulio katika Kristo Yesu, pamoja na
utukufu wa milele.

11Hili ni neno la kuaminiwa:

Kwa maana kama tumekufa pamoja naye,
tutaishi pia pamoja naye.
12Kama tukistahimili,
pia tutatawala pamoja
naye. Kama tukimkana Yeye,
naye atatukana sisi.
13Kama tusipoamini,
Yeye hudumu kuwa mwaminifu, kwa
maana hawezi kujikana mwenyewe.

### *Mfanyakazi Aliyekubaliwa na Mungu*

14Endelea kuwakumbusha mambo haya
ukiwaonya mbele za Bwana waache
kushindana kwa maneno ambayo hayana faida

yo yote bali huwaangamiza tu wale wanaoyasikia. **15**Jitahidi kujionyesha kwa Mungu kuwa umekubaliwa na Yeye, mtenda kazi asiye na sababu ya kuona aibu, ukilitumia kwa usahihi neno la kweli. **16**Jiepushe na maneno mabaya, yasiyo na maana, yasiyo ya utauwa, kwa maana hayo huzidi kuwatosa watu katika kukosa heshima kwa Mungu. **17**Mafundisho yao yataenea kama kidonda kinachooza. Miongoni mwao wamo Himenayo na Fileto **18**ambao wameiacha kweli, wakisema kwamba ufufuo wa wafu umekwisha kuwako na kupotosha baadhi ya watu. **19**Lakini msingi wa Mungu ulio mathubuti umesimama ukiwa na muhuri wenye maandishi haya: ‘‘Bwana anawajua walio wake’’ tena, ‘‘Kila alitajaye jina la Bwana auche uovu.’’

**20**Katika nyumba kubwa kuna vyombo si vya dhahabu na fedha tu, bali pia vimo vyombo vya miti na vya udongo, vingine kwa matumizi maalum na vingine kwa matumizi ya kawaida. **21**Basi ikiwa mtu amejitakasa na kujitenga na hayo niliyoyataja, atakuwa chombo maalum, kilichotengwa na ambacho kinamfaa mwenye nyumba, kikiwa tayari kwa kila kazi njema.

**22**Zikimbie tamaa mbaya za ujana, ufuate haki, imani, upendo na amani pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi. **23**Jiepushe na mabishano ya kipumbavu na yasiyo na maana, kwa kuwa wajua ya kwamba hayo huzaa magomvi. **24**Tena haimpasi mtumishi wa Bwana kuwa mgomvi, bali inampasa awe mwema kwa kila mtu, awezaye kufundisha, tena mvumilivu. **25**Inampasa kuwaonya kwa upole wale wanaopingana naye, kwa matumaini kwamba Mungu atawajalia kutubu na kuijua kweli, **26**ili fahamu zao ziwarudie tena, nao waponyoke katika mtego wa Shetani ambaye amewateka wapate kufanya mapenzi yake.

### *Hatari Za Siku Za Mwisho*

**3** Lakini yakupasa ufahamu jambo hili, kwamba siku za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari. **2**Kwa maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kumkufuru Mungu, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio watakatifu, **3**wasio na upendo, wasiopenda kupatanishwa, wasingiziaji, wasiozuia tamaa zao, wakatili, wasiopenda mema, **4**wasaliti, wakaidi, waliojaa majivuno, wapendao anasa zaidi kuliko kumpenda Mungu. **5**Wakiwa na mfano wa utauwa kwa nje lakini wakizikana nguvu za Mungu. Jiepushe na watu wa namna hiyo.

**6**Miongoni mwao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu na kuwachukua mateka wanawake wajinga, waliolemewa na dhambi zao na kuyumbishwa na aina zote za tamaa mbaya. **7** Wakijifunza sikuzote lakini kamwe wasiweze kufikia ujuzi wa kweli. **8**Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Mose, vivyo hivyo watu hawa hupingana na ile kweli. Hawa ni watu wenye akili zilizopotoka, ambao wamekataliwa kwa mambo ya imani. **9**Lakini hawataendelea sana, kwa sababu upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote, kama ulivyokuwa dhahiri upumbavu wa hao watu wawili.

### *Paulo Amwagiza Timotheo*

**10**Lakini wewe umeyajua mafundisho yangu, mwenendo, makusudi, imani, uvumilivu, upendo, ustahimilivu, **11**mateso na taabu. Yaani, yale mambo yote yaliyonipata huko Antiokia, Ikonio na Listra, mateso yote niliyostahimili, lakini Bwana aliniokoa katika hayo yote. **12**Naam, ye yote anayetaka kuishi maisha ya utauwa ndani ya Kristo Yesu atateswa. **13**Lakini watu waovu na wadanganyaji watazidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. **14**Bali wewe, udumu katika yale uliyojifunza na kuyaamini kwa uthabiti, ukitambua ya kuwa ulijifunza hayo kutoka kwa nani **15**na jinsi ambavyo tangu utoto umeyajua Maandiko matakatifu, ambayo yanaweza kukuhekimisha upate wokovu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. **16**Kila andiko, lililovuviwa na Mungu lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwafundisha katika haki **17**ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila kazi njema.

### *Maagizo Ya Mwisho*

**4** Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu watu walio hai na waliokufa wakati wa kuja Kwake na ufalme Wake kwamba: **2**Uhubiri Neno, uwe tayari wakati ufaao na wakati usiofaa, karipia, kemea na kuonya kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho mazuri.**3**Maana wakati utakuja watu watakapokataa kuyakubali mafundisho yenye uzima, badala yake, ili kutimiza tamaa zao wenyewe watajikusanyia idadi kubwa ya walimu wapate kuwaambia yale ambayo masikio yao yanayowasha yanatamani kuyasikia.

**4**Watakataa kusikiliza kweli na kuzigeukia

hadithi za uongo. 5Kwa habari yako wewe,
vumilia mateso, fanya kazi ya mhubiri wa Injili,
timiza wajibu wote wa huduma yako.

6Kwa maana mimi sasa ni tayari kumiminwa
kama sadaka ya kinywaji, nayo saa yangu ya
kuondoka imetimia. 7Nimevipiga vita vizuri,
mashindano nimeyamaliza, imani nimelinda.
8Sasa nimewekewa taji ya haki ambayo Bwana,
mwamuzi wa haki, atanitunukia siku ile, wala si
mimi tu, bali pia wote ambao wamengoja kwa
shauku kuja Kwake.

***Maombi Ya Binafsi***

9Jitahidi kuja kwangu upesi 10kwa sababu
Dema, kwa kuupenda ulimwengu, ameniacha
na amekwenda Thesalonike. Kreske
amekwenda Galatia na Tito amekwenda
Dalmatia. 11Ni Luka peke yake ndiye aliye hapa
pamoja nami. Mtafute Marko uje naye kwa
sababu ananifaa sana katika huduma yangu.
12Nimemtuma Tikiko Efeso. 13Utakapokuja,
niletee lile joho nililoliacha kwa Karpo huko Troa
na vile vitabu vyangu, hasa vile vya ngozi.

14Aleksanda, yule mfua chuma alinitendea
ubaya mkubwa. Mungu atamlipa kwa ajili ya
yale aliyotenda. 15Wewe pia ujihadhari naye
kwa sababu aliyapinga sana maneno yetu.

16Katika utetezi wangu wa mara ya kwanza,
hakuna hata mmoja aliyeniunga mkono, bali kila
mmoja aliniacha. Namwomba Mungu
wasihesabiwe hatia kwa jambo hilo. 17Lakini
Bwana alisimama upande wangu akanitia
nguvu, ili kwa kunipitia mimi lile Neno lihubiriwe
kwa ukamilifu, watu wote Mataifa wapate
kulisikia. Mimi niliokolewa kutoka katika kinywa
cha simba. 18Bwana ataniokoa katika kila
shambulio baya na kunileta salama katika
Ufalme Wake wa mbinguni. Atukuzwe Yeye
milele na milele. Amen.

***Salamu Za Mwisho***

19Wasalimu Prisila, Akila na wote wa
nyumbani kwa Onesiforo. 20Erasto alibaki
Korintho. Nami nikamwacha Trofimo huko Mileto
akiwa mgonjwa. 21Jitahidi ufike huku kabla ya
majira ya baridi. Eubulo anakusalimu, vivyo
hivyo Pude, Lino, Klaudia na ndugu wote.

22Bwana awe pamoja na roho yako. Neema
iwe pamoja nanyi. Amen.

**Tito**

### *Utangulizi*

Waraka huu aliandikiwa Tito mmoja wa wafuasi wa Paulo muda mfupi tu baada ya Paulo kumwachia wajibu wa kuangalia na kuimarisha kanisa huko Krete. Tito alikuwa na wajibu wa kuwaweka wazee wa kanisa, kuwasimika na kuwafundisha kushika misingi ya imani ya Kikristo. Inaonekana kwamba Paulo alikuwa Korintho akiwa njiani kwenda Nikopoli huko Akaya *(3:12).*Waraka huu umeandikwa baada ya kuachiwa kutoka gerezani Rumi mara ya kwanza, huenda kati ya 63B.K. na 65 B.K.

Waraka huu unaonyesha kuwa kanisa huko Krete halikuwa na mpangilio na kwamba lilikuwa na washirika waliohitaji maelekezo mahsusi. Ilimbidi Paulo aeleze kwa kina kuhusu sifa za wazee wa kanisa na pia kutoa mafundisho kadha wa kadha kwa waamini wengine pia. Katika mafundisho hayo, Paulo anagusia juu ya matatizo yanayowapata watumishi wa Mungu na jinsi matatizo hayo yanavyoweza kutatuliwa.

Tito alikuwa mshirika wa Paulo kwa karibu muda wa miaka kumi na mitano.Akiwa mwongofu Mmataifa kutoka Antiokia na kama mwamini asiyetahiriwa, alifuatana na Paulo na Barnaba kwenda kwenye baraza la Yerusalemu *(Gal.2:1-3 ).* Aliendelea kusafiri na Paulo *( ona 2Kor.2:12 – 13:7;5 – 7:13-14; 8:3,16-17),*hivyo Paulo akawa amemwacha huko Krete.

## *Wazo Kuu*

Mkazo wa barua hii ni kuhusu umuhimu wa kuishi maisha matakatifu katika Kristo katikati ya uovu ulioko duniani. Ingawa katika maisha yetu duniani tunazungukwa na uovu na chuki, hatuna budi maisha yetu kuwa kielelezo jinsi neema ya Mungu inavyotupatia ushindi. Maisha kama hayo yataleta matokeo mema. Paulo anarudia mara kwa mara kusisitiza juu ya kudumisha matendo mema. Maneno matupu hayawezi kufanya lo lote, inatubidi tuishi maisha yenye matendo mema.

Katika waraka huu, Mtume Paulo anakaribia sana kuweka ukiri wa imani katika uandishi wake wote.Vidokezo muhimu vya *MAFUNDISHO (THEOLOGIA*) ya Agano Jipya vinaonekana katika waraka huu.

## *Mgawanyo*

- Salamu (1:1-4)2
- Sifa za wazee wa kanisa (1:5-16) 3
- Maelezo ya jumla kuhusu waamini (2:1-15)4
- Maagizo kuhusu maisha yawapasayo wakristo (3:1-15).

**Salamu**

**1** Paulo, mtumishi wa Mungu na mtume wa Yesu
Kristo kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu na
ujuzi wa kweli ile iletayo uchaji wa
Mungu, 2imani na ujuzi ulioko katika tumaini la
uzima wa milele ambao Mungu,asiyesema
uongo, aliahidi hata kabla ya kuwekwa misingi
ya ulimwengu, 3Naye kwa wakati Wake
aliouweka alilidhihirisha neno Lake kwa njia ya
mahubiri ambayo mimi nimewekewa amana kwa
amri ya Mungu Mwokozi wetu.

4Kwa Tito, mwanangu mwaminifu katika
imani tunayoshiriki sote.

Neema iwe kwako na amani itokayo kwa
Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Mwokozi wetu.

### *Kazi Ya Tito Huko Krete*

5Sababu ya mimi kukuacha huko Krete ni ili
uweke kwenye utaratibu mambo yale yaliyosalia
na kuwaweka wazee wa kanisa katika kila mji,
kama nilivyokuagiza. 6Mzee wa kanisa asiwe na
lawama, awe mume wa mke mmoja, mtu
ambaye watoto wake ni waaminio na wala
hawashtakiwi kwa ufisadi. 7Kwa kuwa askofu,
kama wakili wa Mungu, imempasa kuwa mtu
asiye na lawama, asiwe mwenye majivuno au
mwepesi wa hasira, wala mlevi, wala asiwe mtu
mwenye tamaa ya mapato yasiyo ya halali. 8Bali
awe mkarimu, anayependa mema, mwenye
kiasi, mwenye haki, mwadilifu, mnyofu,
mtakatifu na mwenye kuitawala nafsi yake.
9Inampasa alishike kwa uthabiti lile neno la
imani kama lilivyofundishwa, kusudi aweze
kuwafundisha wengine kwa mafundisho
manyofu na kuwakanusha wale wanaopingana
nayo.

### *Walimu Wa Uongo*

10Kwa maana wako wengi wasiotii, wenye
maneno yasiyo na maana, hasa wale wa kikundi
cha tohara. 11Hao ni lazima wanyamazishwe,
kwa sababu wanaharibu watu wa nyumba nzima
wakifundisha mambo yasiyowapasa kufundisha.
Wanafanya hivyo kwa ajili ya kujipatia mapato
ya udanganyifu. 12Hata mmojawapo wa manabii
wao mwenyewe amesema: "Wakrete ni waongo
sikuzote, wanyama wabaya, walafi, wavivu."
13Ushuhuda huu ni kweli. Kwa hiyo, uwakemee
kwa ukali
wapate kuwa wazima katika imani, 14ili
wasiendelee kuangalia hadithi za Kiyahudi au
maagizo ya wale watu wanaoikataa kweli.
15Kwa wale walio safi, kila kitu ni safi kwao.
Lakini kwa wale waliopotoka na wasioamini,
hakuna cho chote kilicho safi. Kwa kweli nia zao
na dhamiri zao zimepotoka. 16Wanadai kumjua
Mungu, lakini kwa matendo yao wanamkana.
Hao watu ni chukizo, wasiotii, wasiofaa kwa
jambo lo lote jema.

### *Fundisha Mafundisho Manyofu*

Lakini kwa habari yako wewe, inakupasa
**2** kufundisha kulingana na mafundisho
yenye uzima. 2Wafundishe wazee kuwa na
kiasi, wastahivu, wenye busara na wanyofu
katika imani, upendo na saburi.

3Vivyo hivyo wafundishe wanawake wazee
kuwa na mwenendo wa unyenyekevu
unaostahili utakatifu, wala wasiwe wasingiziaji
au walevi, bali wafundishe yale yaliyo mema, 4ili
waweze kuwafundisha wanawake vijana kuwa
na kiasi, wawapende waume zao na
kuwapenda watoto wao, 5wawe waaminifu,
watakatifu, wakitunza vema nyumba zao,
wema, watiifu kwa waume zao, ili mtu ye yote
asije akalikufuru neno la Mungu.

6Vivyo hivyo, sisitiza vijana kuwa na kiasi.
7Katika kila jambo wewe mwenyewe uwe
kielelezo cha matendo mema na katika
mafundisho yako uonyeshe unyofu, utaratibu,
ukweli 8 na maneno yenye uzima, yale ambayo
hayawezi kulaumiwa, hata wale wenye
kukupinga watahayari, wakose neno lo lote
baya la kusema juu yetu.

9Wafundishe watumwa kuwatii mabwana
zao katika kila jambo, wakijitahidi kuwapendeza
wala wasijibizane nao, 10wala wasiwaibie, bali
watumwa waonyeshe kuwa wanaweza
kuaminika kabisa, ili kwamba kwa kila namna
wayafanye mafundisho ya Mungu Mwokozi
wetu kuwa ya kupendeza.

11Kwa maana neema ya Mungu iwaokoayo
wanadamu wote imefunuliwa. 12Nayo
yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za
kidunia, ili tupate kuishi maisha ya kiasi, ya haki
na ya kumcha Mungu, katika ulimwengu huu wa
sasa, huku 13tukilitazamia tumaini lenye baraka
na ufunuo wa utukufu wa Mungu wetu Mkuu na
Mwokozi wetu Yesu Kristo, 14Yeye ndiye
aliyejitoa nafsi Yake kwa ajili yetu ili atukomboe
kutoka katika uovu wote na kujisafishia watu
kuwa mali Yake Mwenyewe, yaani, wale walio

na bidii katika kutenda mema.

15Basi wewe fundisha mambo haya, onya na karipia kwa mamlaka yote. Mtu ye yote asikudharau.

### *Kutenda Mema*

3 Wakumbushe watu kuwanyenyekea watawala na kuwatii wenye mamlaka, wawe tayari kutenda kila lililo jema.
2Wasimnenee mtu ye yote mabaya, wasiwe wagomvi, bali wawe wapole, wakionyesha unyenyekevu kwa watu wote.

3Maana sisi wenyewe wakati fulani tulikuwa wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa wa tamaa mbaya na anasa za kila aina. Tuliishi katika uovu na wivu, tukichukiwa na kuchukiana sisi kwa sisi.
4Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa,
5 alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu,
6ambaye Mungu alitumiminia kwa wingi kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu,
7ili kwamba, tukiisha kuhesabiwa haki kwa neema Yake, tupate kuwa warithi tukiwa na tumaini la uzima wa milele.
8 Hili ni neno la kuaminiwa. Nami nataka uyasisitize mambo haya, ili wale ambao wamemwamini Mungu wapate kuwa waangalifu kujitoa kwa ajili ya kutenda mema wakati wote. Mambo haya ni mazuri tena ya manufaa kwa kila mtu.

9Lakini jiepushe na maswali ya kipuzi, mambo ya koo, mabishano na ugomvi kuhusu sheria, kwa sababu haya hayana faida tena ni ubatili.
10Mtu anayesababisha mafarakano, mwonye mara ya kwanza, kisha mwonye mara ya pili. Baada ya hapo, usihusike naye tena.
11Kwa kuwa unajua kwamba mtu kama huyo amepotoka na tena ni mwenye dhambi. Yeye amejihukumu mwenyewe.

### *Maneno Ya Mwisho Na Kumtamkia Baraka*

12Mara nitakapomtuma Artema au Tikiko kwako, jitahidi kuja unione huko Nikopoli, kwa sababu nimeamua kukaa huko wakati wa majira ya baridi.
13 Fanya kila uwezalo uwasafirishe Zena, yule mwanasheria na Apolo na uhakikishe kwamba wana kila kitu wanachohitaji.
14Watu wetu hawana budi kujifunza kujitoa kutenda mema, ili waweze kuwasaidia watu wenye mahitaji ya lazima ya kila siku, wasije wakaishi maisha yasiyokuwa na matunda.

15Wote walio pamoja nami wanakusalimu. Wasalimu wale wanaotupenda katika imani. Neema iwe nanyi nyote. Amen.

# Filemoni

### *Utangulizi*

Waraka huu mfupi uliandikwa na Paulo kutoka Rumi nao umeainishwa na ule wa Waefeso, Wakolosai na Wafilipi kama mojawapo ya nyaraka zake za gerezani. Ameandikiwa Filemoni, kwa Afia mwanamke mkristo, ( huenda alikuwa mkewe Filemoni ), kwa Arkipo *(Kol.4:17)* na kwa kanisa lililokuwa likikusanyika nyumbani kwa Filemoni.

Bila shaka Onesmo alikuwa ametoroka kutoka kwa Filemoni huko Kolosai kwenda Rumi, ambako aliongoka na kushirikiana na Paulo. Kama mtumwa, alikuwa mali ya Filemoni kisheria. Zaidi ya hayo inawezekana Onesmo alikuwa anadaiwa vitu fulani fulani na Filemoni.

Kwa barua hii Paulo anamtuma Onesmo kwa Filemoni, akisisitiza kwamba mwenendo wa kikristo ungepaswa utawale katika uhusiano wao. Paulo anaomba msamaha kwa ajili ya Onesmo, akiomba akubaliwe kama ndugu mkristo. Ombi hilo limeandikwa kwa maarifa na waraka huu umepangwa kwa namna ambayo ungejenga kusikilizana, kushawishi nia na kuamsha hisia.

### *Mwandishi*

Mwandishi waraka huu ni Mtume Paulo.

### *Tarehe*

*Huu ni mojawapo wa waraka wa gerezani*

### *Mgawanyo*

- Salamu (1:1- 3)
- Kuhusika kwa Paulo na upendo (1:4 – 7)
- Paulo kumwombea Onesmo (1:8 – 22)
- Kuagana (1:23 – 25)

### *Salamu*

1Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, pamoja
na Timotheo ndugu yetu,

Kwa Filemoni rafiki yetu mpendwa na
mtenda kazi mwenzetu, 2kwa dada yetu
mpendwa Afia, kwa Arkipo askari mwenzetu na
kwa kanisa lile likutanalo nyumbani mwako:

3Neema iwe nanyi na amani itokayo kwa
Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

### *Shukrani Na Maombi*

4Sikuzote ninamshukuru Mungu
ninapokukumbuka katika maombi yangu, 5kwa
sababu ninasikia juu ya imani yako katika
Bwana Yesu na upendo wako kwa watakatifu
wote. 6Naomba utiwe nguvu katika kuishuhudia
imani yako, ili upate kuwa na ufahamu mkamilifu
juu ya kila kitu chema tulicho nacho ndani ya
Kristo. 7Upendo wako umenifurahisha mno na
kunitia moyo, kwa sababu wewe ndugu,
umeiburudisha mioyo ya watakatifu.

### *Maombi Ya Paulo Ya Kumtetea Onesmo*

8Hata hivyo, ingawa katika Kristo ningeweza
kuwa na ujasiri na kukuagiza yale yakupasayo
kutenda, 9lakini ninakuomba kwa upendo, mimi
Paulo, mzee na pia sasa nikiwa mfungwa wa
Kristo Yesu, 10nakuomba kwa ajili ya mwanangu
Onesmo, aliyefanyika mwanangu nilipokuwa
kwenye minyororo. 11Mwanzoni alikuwa hakufai,
lakini sasa anakufaa sana wewe na mimi pia.

12Namtuma kwako, yeye aliye moyo wangu
hasa.13Ningependa nikae naye ili ashike nafasi
yako ya kunisaidia wakati huu nikiwa kifungoni
kwa ajili ya Injili. 14Lakini sikutaka kufanya lo
lote bila idhini yako, ili wema wo wote uufanyao
usiwe wa lazima, bali wa hiari. 15Huenda
sababu ya yeye kutengwa nawe kwa kitambo
kidogo ni ili uwe naye daima. 16Si kama
mtumwa, bali bora kuliko mtumwa, kama ndugu
mpendwa. Yeye ni mpendwa sana kwangu na
hata kwako zaidi, yeye kama mwanadamu na
kama ndugu katika Bwana.

17Hivyo kama unanihesabu mimi kuwa
mshirika wako, mkaribishe kama vile
ungenikaribisha mimi mwenyewe. 18Kama
amekukosea lo lote au kama unamdai cho
chote, nidai mimi. 19Mimi Paulo, ninaandika
waraka huu kwa mkono wangu mwenyewe,
mimi nitalipa. Si kwamba ninakudai hata nafsi
yako mwenyewe. 20Ndugu yangu, natamani
nipate faida kwako katika Bwana, uuburudisha
moyo wangu katika Kristo. 21Nikiwa na hakika
ya utii wako, nakuandikia, nikijua kwamba
utafanya hata zaidi ya yale nisemayo.

22Jambo moja zaidi: Niandalie chumba cha
wageni, kwa kuwa nataraji kurudishwa kwenu
kama jibu la maombi yenu.

### *Salamu Za Mwisho Na Dua Ya Kuwatakia Heri*

23 Epafra, aliye mfungwa mwenzangu
katika Kristo Yesu, anakusalimu. 24Vivyo hivyo
Marko, Aristarko, Dema na Luka, watenda kazi
wenzangu wanakusalimu.

25Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja
na roho zenu. Amen.

## WAEBRANIA

### *Utangulizi*

Mwandishi wa waraka huu hajitambulishi lakini bila shaka alikuwa anajulikana vema na wale walioupokea. Kumekuwa na mawazo mbalilmbali aidha wengine wakimhusisha Paulo, Barnaba au Apolo, lakini uandishi wake unafanana sana na ule wa Mtume Paulo. Ingawa mwandishi hafahamiki wazi, bila shaka alikuwa mtu mwenye ufahamu mkubwa katika Agano la Kale, ambaye ni Myahudi na aliyekuwa rafiki wa Timotheo. Anaonyesha umahiri mkubwa wa usomi na uandishi kama ule wa waandishi wengine wa Agano Jipya.Mwandishi anamwonyesha Yesu kuwa ndiye ukamilifu wa ufunuo wa Mungu kupitia kwa manabii.Ufunuo huu wa ki- Uungu katika ubinadamu wa Yesu Kristo ni wa hali ya juu kwa viwango vyote katika hali zote.

### *Wazo kuu*

Kiini cha Waebrania ni mamlaka ya juu kabisa na uwezo wa Yesu Kristo kama Mdhihirishaji na Mjumbe wa neema ya Mungu. Katika kitabu hiki majina ya heshima zaidi ya ishirini yametumika yakimtaja Yesu Kristo.
Neno kuu la ufunguo ni pale mwandishi anapomwonyesha Yesu kuwa ndiye ukamilifu wa ufunuo ulionenwa kwanza na Mungu kisha na manabii Wake. Ufunuo huu wa Mungu katika mwanadamu Yesu Kristo ndio wa juu kabisa unaomwonyesha Yesu Kristo kuwa ndiye amfunuaye Mungu, tena Yeye ndiye Mjumbe wa Neema ya Mungu.Yesu anaonekana katika huduma ya Kuhani-Mfalme.

Mara nyingi onyo limetolewa kwamba msomaji asiudharau wala kuukataa Wokovu Mkuu uliotolewa kwa njia ya Yesu Kristo. Uwezekano mkubwa ni kwamba waraka huu ulielekezwa kwa wakristo Wayahudi huko Palestina au Rumi, ambao walikuwa wanajaribiwa kugeukia dini ya Kiyahudi au kuifanya Injili iwe yenye mfumo wa dini hiyo ya Kiyahudi.

### *Mwandishi*

Kumekuwako na mawazo yanayotofautiana miongoni mwa viongozi wa Kanisa la kwanza.
Wengine wanamhusisha Paulo, wengine Barnaba au Apolona uandishi wa waraka huu, lakini wazo lililo bora sana ni lile la Origen, ambaye alisema kwamba, "Iwe ni nani aliyeandika waraka huu, Mungu peke Yake ndiye anayemjua." Ingawa waraka hauna jina la mwandishi, una ushahidi mwingi kwamba ni mtu kwenye kizazi pili cha Wakristo, aliyekuwa na ujuzi mkubwa wa Agano la Kale.

### *Tarehe*

Inaelekea ni kwenye mwisho wa miaka ya 60 B.K. katika karne ya kwanza, yaani, muda mfupi tu kabla ya kuharibiwa kwa Yerusalemu 70 B.K. Katika kipindi hiki hofu ya mateso ilikuwa kubwa kwa kanisa huko Rumi.Wakati huo hali ya mateso ilikuwa ya kutia hofu kwa kanisa huko Rumi.

### *Mahali*

Waraka huu uliandikwa kutoka Rumi.

### *Mgawanyo:*

- Mnenaji bora kwa ajili ya Mungu (1:1 - 4:13)
- Mwombezi au Kuhani aliye bora (4:14 - 7:28)
- Agano na Dhabihu iliyo bora (8:1- 10: 18)
- Agizo la kuitunza na kuilinda imani (11:1-12:29)
- Mwisho :Kanuni za maisha ya Kikristo (13:1-17)
- Kuhitaji maombi (13:18-19)
- Hitimisho (13:20–21)
- Maelezo ya binafsi (13:22-23)
- Salamu(13:24-25) -

### *Mwana Ni Mkuu Kuliko Malaika*

**1** Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa
njia ya manabii mara nyingi na kwa njia
mbalimbali, 2lakini katika siku hizi za mwisho
amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye
amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye
kwa Yeye aliuumba ulimwengu. 3Mwana ni
mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi
wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno
Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa
ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu
huko mbinguni. 4Kwa hiyo alifanyika bora kuliko
malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko
lao.

5Kwa maana ni malaika yupi ambaye wakati
wo wote Mungu alipata kumwambia,

"Wewe ni Mwanangu,
leo Mimi nimekuzaa?"

Au tena,

"Mimi nitakuwa Baba Yake,
naye atakuwa Mwanangu?"

6Tena, Mungu amletapo mzaliwa Wake wa
kwanza ulimwenguni, husema,

"Malaika wote wa Mungu na wamsujudu"

7Anenapo kuhusu malaika husema,

"Huwafanya malaika Zake kuwa upepo,
watumishi Wake kuwa miali ya moto."

8Lakini kwa habari za Mwana asema,

"Kiti chako cha enzi, Ee Mungu,
kitadumu milele na milele,
nayo haki itakuwa fimbo ya utawala ya
Ufalme Wako.
9Umependa haki na kuchukia uovu,
kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekuweka
juu ya wenzako
kwa kukupaka mafuta ya furaha."

10Pia asema,

"Hapo mwanzo, Ee Bwana, uliweka misingi
ya dunia,
nazo mbingu ni kazi ya mikono Yako.
11Hizo zitaangamia, lakini Wewe utadumu,
zote zitachakaa kama vazi.
12Utazikunja-kunja kama joho,
kama vazi zitachakaa.
Bali Wewe hubadiliki,
wala miaka Yako kamwe haitakoma."

13Je, ni kwa malaika yupi ambaye Mungu
amepata kumwambia wakati wo wote,

"Wewe keti mkono Wangu wa kuume
mpaka nitakapowaweka adui Zako
chini ya nyayo Zako? "

14Je, malaika wote si roho watumikao
waliotumwa kuwahudumia wale watakaorithi
wokovu?

### *Wokovu Mkuu*

**2** Kwa hiyo, imetupasa kuwa waangalifu
sana kuhusu kile tulichosikia, ili tusije
tukakiacha. 2Kwa kuwa ujumbe ulionenwa na
malaika ulikuwa imara na kila uasi na kutokutii
kulipata adhabu ya haki, 3je, sisi tutapajе
kutapona kama tusipojali wokovu mkuu namna
hii? Wokovu huu, ambao mwanzo ulitangazwa
na Bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale
waliomsikia. 4Pia Mungu aliushuhudia kwa
ishara, maajabu na kwa miujiza mbalimbali na
karama za Roho Mtakatifu alizozigawa
kulingana na mapenzi Yake.

### *Yesu Alifananishwa Na Ndugu Zake*

5Mungu hakuuweka ulimwengu ujao ambao
tunanena habari zake chini ya malaika. 6Lakini
kuna mahali mtu fulani ameshuhudia akisema:

"Mwanadamu ni kitu gani hata umfikirie,
mwana wa adamu ni nani hata umjali?
7Umemfanya kuwa chini kidogo kuliko malaika.
Umemvika taji ya utukufu na heshima,
8nawe umeweka vitu vyote chini ya
miguu yake."

Kwa kuweka vitu vyote chini yake, Mungu
hakuacha kitu cho chote ambacho hakukiweka
chini ya mwanadamu. Lakini kwa sasa, hatuoni
kwamba kila kitu kiko chini yake. 9Lakini
twamwona Yesu, aliyefanywa chini kidogo
kuliko malaika, sasa akiwa amevikwa taji ya
utukufu na heshima kwa sababu alistahimili
mauti, ili kwamba kwa neema ya Mungu apate
kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu.

10Ili kuwaleta wana wengi katika utukufu,
ilimpendeza Mungu, kwa ajili Yake na kwa

kupitia Yeye kila kitu kilichopo, kumkamilisha
mwanzilishi wa wokovu wao kwa njia ya mateso.
11Yeye awafanyaye watu kuwa watakatifu na
wale ambao hufanywa watakatifu, wote hutoka
katika jamaa moja. Hivyo Yesu haoni aibu
kuwaita ndugu Zake. 12Yeye husema,

“Nitalitangaza Jina Lako kwa ndugu Zangu,
mbele ya kusanyiko nitaimba sifa Zako.”

13Tena,

“Nitaweka tumaini langu Kwake.’’

Tena anasema,

“Niko hapa, mimi pamoja na watoto Mungu
alionipa”

14Basi kwa kuwa watoto wana nyama na
damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao,
ili kwa kifo chake, apate kumwangamiza huyo
mwenye nguvu za mauti, yaani, Shetani, 15na
kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani
maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti.
16Kwa kuwa ni dhahiri kwamba hakuja kusaidia
malaika, bali uzao wa Abrahamu. 17Kwa sababu
hii ilibidi afanane na ndugu Zake kwa kila hali, ili
apate kuwa Kuhani Mkuu mwenye huruma na
mwaminifu katika kumtumikia Mungu, ili pia
apate kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za
watu. 18Kwa kuwa Yeye mwenyewe aliteswa
alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wale
wanaojaribiwa.

### *Yesu Ni Mkuu Kuliko Mose.*

3 Kwa hiyo ndugu watakatifu, mnaoshiriki
mwito wa mbinguni, mtafakarini Yesu, mtume
na Kuhani Mkuu wa ukiri wetu. 2Alikuwa
mwaminifu kwa Yeye aliyemweka, kama vile
Mose alivyokuwa mwaminifu katika nyumba
yote ya Mungu. 3Yesu ameonekana anastahili
heshima kubwa kuliko Mose, kama vile mjenzi
wa nyumba alivyo wa heshima kubwa kuliko
nyumba yenyewe. 4Kwa kuwa kila nyumba
hujengwa na mtu fulani, lakini Mungu ni mjenzi
wa kila kitu. 5Basi Mose kama mtumishi alikuwa
mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu,
akishuhudia kwa yale ambayo yangetamkwa
baadaye. 6Lakini Kristo Yeye ni mwaminifu
kama Mwana katika nyumba ya Mungu, sisi ndio
nyumba Yake, kama tutashikamana sana
na ujasiri wetu na katika tumaini tunalojivunia.

### *Onyo Dhidi Ya Kutokuamini.*

7Kwa hiyo, kama Roho Mtakatifu asemavyo,

“Leo, kama mkiisikia sauti yake,
8msifanye mioyo yenu migumu,
kama mlivyofanya katika uasi,
wakati ule wa kujaribiwa jangwani,
9pale baba zenu waliponijaribu na kunipima
ingawa kwa miaka arobaini walikuwa
wameona matendo Yangu.
10Hiyo ndiyo sababu nilikasirikia kizazi kile,
nami nikasema, ‘Siku zote mioyo yao
hupotoka,
nao hawajazijua njia Zangu’.
11Hivyo nikaapa kwa hasira Yangu,
‘kamwe hawataininga rahani Mwangu.’ ”

12Ndugu zangu, angalieni, asiwepo
miongoni mwenu mtu mwenye moyo mwovu
usioamini, unaojitenga na Mungu aliye hai.
13Lakini mtiane moyo kila siku mtu na
mwenzake, maadam iitwapo ‘leo’, ili asiwepo
hata mmoja wenu mwenye kufanywa mgumu
kwa udanganyifu wa dhambi. 14Kwa kuwa
tumekuwa washiriki wa Kristo, kama
tukishikamana tu kwa uthabiti na tumaini letu la
kwanza hadi mwisho. 15Kama ilivyonenwa:

“Leo, kama mtaisikia sauti Yake,
msifanye mioyo yenu migumu
kama mlivyofanya wakati wa kuasi.”

16Basi ni nani wale waliosikia lakini bado
wakaasi? Je, si wale wote waliotoka Misri
wakiongozwa na Mose? 17Lakini ni nani
aliowakasirikia miaka arobaini? Je, si wale
waliofanya dhambi ambao miili yao ilianguka
jangwani? 18Nao ni nani ambao Mungu aliapa
kuwa kamwe hawataingia rahani Mwake
isipokuwa ni wale waliokataa kutii? 19 Hivyo
tunaona kwamba hawakuweza kuingia kwa
sababu ya kutokuamini kwao.

### *Pumziko Lile Mungu Aliloahidi*

4 Kwa hiyo, kwa kuwa bado ahadi ya kuingia
rahani iko wazi, tujihadhari ili hata mmoja wenu
asije akaikosa. 2Kwa maana sisi pia tumesikia
Injili iliyohubiriwa kwetu, kama nao walivyosikia,
lakini ujumbe ule waliousikia haukuwa na
maana kwao, kwa sababu wale waliousikia
hawakuuchanganya na imani. 3Sasa

sisi ambao tumeamini tunaingia katika ile raha, kama vile Mungu alivyosema,

“Hivyo natangaza kwa kiapo katika
hasira Yangu,
‘Kamwe hawataingia rahani Mwangu.’ ”

Lakini kazi Yake ilikamilika tangu kuumbwa kwa
ulimwengu. 4Kwa maana mahali fulani
amezungumza kuhusu siku ya saba, akisema: “Katika siku ya saba Mungu alipumzika katika
kazi Zake zote” 5Tena hapo juu asema, “Kamwe
hawataingia rahani Mwangu.”

6Kwa hiyo kwa kuwa inabaki kuwa wazi kwa ajili ya wengine kuingia, nao wale wa kwanza waliopokea Injili walishindwa kuingia kwa
sababu ya kutokutii, 7kwa hiyo Mungu ameweka
siku nyingine akisema, “Leo,” akisema kwa kinywa cha Daudi baadaye sana, kwa maneno yalitangulia kunenwa:

“Leo, kama mkiisikia sauti Yake,
msifanye migumu mioyo yenu.”

8Kwa maana kama Yoshua alikuwa amewapa raha, Mungu hangelisema tena baadaye kuhusu
siku nyingine. 9Kwa hiyo basi, imebaki raha ya
Sabato kwa ajili ya watu wa Mungu, 10kwa kuwa
kila mmoja aingiaye katika raha ya Mungu pia hupumzika kutoka kazi zake mwenyewe, kama vile naye Mungu alivyopumzika kutoka katika
kazi Zake. 11Basi na tufanye bidii kuingia katika
raha hiyo, ili kwamba asiwepo ye yote atakayeanguka kwa kufuata mfano wao wa kutokutii.

12Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua
mawazo na makusudi ya moyo. 13Wala hakuna
kiumbe cho chote kilichofichika machoni pa Mungu. Kila kitu kimefunuliwa na kiko wazi machoni pake Yeye ambaye Kwake tutatoa hesabu.

### *Yesu Kristo Kuhani Mkuu Kuliko Wote*

14Kwa kuwa tunaye Kuhani Mkuu kuliko wote ambaye ameingia mbinguni, Yesu Mwana wa Mungu, basi na tushikamane sana kwa
uthabiti na ule ukiri wa imani yetu. 15Kwa kuwa
hatuna Kuhani Mkuu anaweza kuchukuliana na sisi katika udhaifu wetu, kwani Yeye mwenyewe alijaribiwa kwa kila namna, kama vile sisi
tujaribiwavyo, lakini Yeye hakutenda dhambi. 16
Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

**5** Kwa maana kila Kuhani Mkuu anayechaguliwa miongoni mwa wanadamu anawekwa kuwawakilisha kwa mambo yanayomhusu Mungu, ili apate kutoa matoleo
na dhabihu kwa ajili ya dhambi. 2Kwa kuwa
yeye mwenyewe ni dhaifu, aweza kuwachukulia kwa upole wale wasiojua na
kupotoka. 3Hii ndiyo sababu inawapasa kutoa
dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe na vivyo hivyo kwa ajili ya dhambi za watu.
4Hakuna anayejitwalia heshima hii mwenyewe, ni lazima aitwe na Mungu, kama
vile Aroni alivyoitwa. 5Pia Kristo hakujitwalia
utukufu Yeye mwenyewe wa kuwa Kuhani Mkuu, bali Mungu alimwambia,

“Wewe ni Mwanangu,
Mimi leo nimekuzaa.

6Pia mahali pengine asema,

“Wewe ndiwe kuhani milele,
kwa mfano wa Melkzedeki”

7Katika siku za maisha ya Yesu hapa duniani, alimtolea maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, Yeye awezaye kumwokoa na mauti, naye Mungu akamsikia kwa sababu ya kutii Kwake kwa unyenyekevu.
8Ingawa alikuwa Mwana, alijifunza utii kutokana
na mateso aliyoyapata, 9akiisha kukamilishwa,
akawa chanzo cha wokovu wa milele kwa wote
wanaomtii, 10 naye amewekwa na Mungu kuwa
Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki.

### *Onyo Kuhusu Kuanguka.*

11Tunayo mengi ya kusema kuhusu habari ukuhani huu, lakini ni vigumu kuyaeleza, kwa
sababu ninyi ni wazito wa kuelewa. 12Kwa
hakika, ingawa mpaka wakati huu ingewapasa kuwa walimu, lakini bado mnahitaji mtu wa kuwafundisha, tena hatua za awali za kweli ya Neno la Mungu. Mnahitaji maziwa, wala si
chakula kigumu, 13kwa maana ye yote aishiye
kwa kunywa maziwa bado yeye ni mtoto mchanga, hana ujuzi katika mafundisho kuhusu
neno la haki. 14Lakini chakula kigumu ni kwa
ajili ya watu wazima, ambao kwa kujizoeza

wamejifunza kupambanua kati ya mema na mabaya.

**Hatari Ya Kuanguka**

**6** Kwa hiyo, tukiachana na mafundisho yale ya awali kuhusu Kristo na tusonge mbele ili tufikie utimilifu, si kuweka tena msingi wa mafundisho ya kuzitubia kazi zisizo na uhai na imani katika Mungu, yaani, 2mafundisho kuhusu mabatizo, kuwekea watu mikono, ufufuo wa wafu na hukumu ya milele. 3Mungu akitujalia tutafanya hivyo.

4Kwa kuwa ni vigumu kuwarejeza tena katika toba wale ambao wakati fulani walishapata nuru, ambao walishaonja kipawa cha mbinguni, ambao wamekwisha kushiriki katika Roho Mtakatifu. 5wale ambao wameonja uzuri wa Neno la Mungu na nguvu za wakati ujao, 6kisha wakaanguka, kwa kuwa kwa nafsi zao wanamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili na kumfedhehi hadharani.

7 Ardhi ile ipokeayo mvua inyeshayo juu yake mara kwa mara hutoa mazao yanayowanufaisha wale ambao kwa ajili yao yalimwa, nayo nchi hiyo hupokea baraka kutoka kwa Mungu. 8Lakini ardhi ile ikizaa miiba na mibaruti haina thamani na iko hatarini kulaaniwa. Mwisho wake ni kuchomwa moto.

9Ingawa tunasema hivi, ndugu zangu wapendwa, kwa upande wenu tuna hakika ya mambo mema zaidi, mambo yale yahusuyo wokovu. 10Mungu si dhalimu, hataisahau kazi yenu na upendo ule mlioonyesha kwa ajili Yake katika kuwahudumia watakatifu na kama vile mnavyoendelea kuwahudumia. 11Nasi twataka kila mmoja wenu aonyeshe bidii iyo hiyo ili mpate kujua uhakika kamili wa lile tumaini mpaka mwisho, 12ili msije mkawa wavivu, bali mpate kuwaiga wale ambao kwa imani na saburi hurithi zile ahadi.

***Uhakika Wa Ahadi Ya Mungu***

13Mungu alipompa Abrahamu ahadi Yake, kwa kuwa hakuwepo mwingine aliyekuwa mkuu kuliko Yeye ambaye angeweza kuapa kwa jina lake, aliapa kwa nafsi Yake, 14akisema, “Hakika nitakubariki na kukupa wazao wengi.” 15Naye baada ya kungoja kwa saburi, Abrahamu alipokea kile kilichoahidiwa.

16 Wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao, nacho kiapo hicho huthibitisha kile kilichosemwa na kumaliza mabishano yote. 17Kwa njia hii, Mungu alipotaka kuonyesha kwa udhahiri zaidi kwa warithi wa ile ahadi ile asili ya kutokubadilika kwa ahadi Yake, aliithitibisha kwa kiapo. 18Mungu alifanya hivyo, ili kwa vitu viwili visivyobadilika, yaani ahadi Yake na kiapo Chake, ambavyo kwa hivyo Mungu hawezi kusema uongo, sisi ambao tumemkimbilia, tuwe na moyo mkuu kulishika lile tumaini lililowekwa mbele yetu. 19Tunalo tumaini hili lililo kama nanga ya roho, lililo imara na thabiti. Tumaini hili huingia katika patakatifu palipo nyuma ya pazia, 20mahali ambapo, Yesu mtangulizi wetu aliingia kwa niaba yetu. Yeye amekuwa Kuhani Mkuu milele, kwa mfano wa Melkizedeki.

***Kuhani Melkizedeki***

**7** Kwa kuwa huyu Melkizedeki alikuwa mfalme wa Salemu na Kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Abrahamu akirudi katika kuwashinda hao wafalme, naye Melkizedeki akambariki, 2ambaye Abrahamu alimpa “sehemu moja ya kumi [a]” ya kila kitu. Kwanza, jina hilo Melkizedeki maana yake, “Mfalme wa haki,” pia “Mfalme wa Salemu” maana yake “Mfalme wa amani.” 3Hana Baba wala mama, hana ukoo, hana mwanzo wala mwisho wa siku zake, kama Mwana wa Mungu, yeye adumu kuhani milele.

4Tazama jinsi alivyokuwa mkuu! Hata Abrahamu, baba yetu mkuu, alimpa moja ya kumi ya nyara zake. 5Basi sheria inawaagiza wana wa Lawi wale ambao hufanyika makuhani hupokea sehemu moja ya kumi kutoka watu ambao ni ndugu zao, ingawa wao ni wazao wa Abrahamu. 6Huyu Melkizedeki, ingawa hakufuatia ukoo wake kutoka kwa Lawi, lakini alipokea moja ya kumi kutoka kwa Abrahamu na kumbariki yeye aliyekuwa na zile ahadi. 7Wala hakuna shaka kwamba mdogo hubarikiwa na aliye mkuu kuliko yeye. 8Kwa upande mmoja, sehemu moja ya kumi hupokelewa na wale ambao hupatikana na kufa, lakini kwa upande mwingine hupokelewa na Yeye ambaye hushuhudiwa kuwa yu hai. 9Mtu anaweza hata kusema kwamba Lawi, ambaye hupokea sehemu moja ya kumi alitoa hiyo sehemu moja ya kumi kupitia kwa Abrahamu, 10kwa sababu Melkizedeki alipokutana na Abrahamu, Lawi alikuwa bado katika viuno vya baba yake wa zamani, yaani, alikuwa hajazaliwa.

***Yesu Mfano Wa Melkizedeki.***

---

[a]2 Sehemu moja ya kumi mahali pengine huitwa fungu la kumi au zaka. Hii moja ya kumi ya pato hutolewa kwa Mungu

11Kama ukamilifu ungeweza kupatikana kwa
njia ya ukuhani wa Walawi (kwa kuwa katika
msingi huo sheria ilitolewa kwa watu) kwa nini basi
imekuwapo haja ya kuja kuhani mwingine, kwa
mfano wa Melkizedeki, wala si kwa mfano wa
Aroni? 12 Kwa kuwa yanapotokea mabadiliko ya
ukuhani, pia lazima yawepo mabadiliko ya sheria.
13Yeye ambaye ndiye anayesemwa katika mambo
haya, alikuwa wa kabila jingine na hakuna mtu wa
kabila hilo aliyekuwa amehudumu katika
madhabahu. 14Kwa maana ni dhahiri kwamba
Bwana wetu alitoka katika uzao wa Yuda, tena
kuhusu kabila hilo Mose hakusema lo lote kwa
habari za ukuhani. 15Tena hayo tuliyosema yako
wazi zaidi kama akitokea kuhani mwingine kama
Melkizedeki, 16Yeye ambaye amefanyika kuhani si
kwa misingi ya sheria kama ilivyokuwa kwa baba
zake, bali kwa misingi ya uwezo wa uzima
usioharibika. 17Kwa maana imeshuhudiwa
kwamba:

"Wewe ndiye kuhani milele, kwa
mfano wa melkizedeki."

18Kwa upande mmoja, kubatilishwa kwa ile
amri ya mwanzo isiyofaa. 19(kwa maana sheria
haikufanya kitu cho chote kuwa kikamilifu), kwa
upande mwingine, tumeletewa tumaini lililo bora
zaidi ambalo kwalo linatuleta karibu na Mungu.

20Nalo tumaini hilo halikutolewa pasipo
kiapo. Wengine walikuwa makuhani pasipo
kiapo cho chote, 21lakini Yesu alikuwa Kuhani
kwa kiapo wakati Mungu alipomwambia:

"Bwana ameapa
naye hatabadili nia Yake:
'Wewe ndiwe Kuhani milele.' "

22Kwa ajili ya kiapo hiki, Yesu amekuwa
mdhamini wa agano lililo bora zaidi.

23Basi pamekuwepo na makuhani wengi wa
aina hiyo, kwa kuwa kifo kiliwazuia kuendelea
na huduma yao ya ukuhani, 24lakini kwa sababu
Yesu aishi milele, anao ukuhani wa kudumu.
25Kwa hiyo anaweza kuwaokoa kabisa wale
wanaomjia Mungu kupitia Kwake, kwa sababu
Yeye adumu daima kuomba kwa ajili yao.

26Kwa kuwa ilitupasa tuwe na Kuhani Mkuu
wa namna hii, yaani, aliye mtakatifu, asiye na
lawama, asiye na dosari, aliyetengwa na wenye
dhambi na kuinuliwa juu ya mbingu. 27Yeye
hahitaji kutoa dhabihu siku kwa siku kwa ajili ya
dhambi, kwanza kwa ajili ya dhambi Zake
mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za watu
wengine kama wale makuhani wakuu wengine.
Yeye alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zao
mara moja tu, alipojitoa Mwenyewe. 28Kwa
kuwa sheria huwaweka makuhani wakuu watu
ambao ni dhaifu, lakini lile neno la kiapo,
lililokuja baada ya sheria, lilimweka Mwana,
ambaye amefanywa kuwa mkamilifu milele.

### *Kuhani Mkuu Wa Agano Jipya*

Basi jambo tunalotaka kulisema ni hili:
8 Tunaye Kuhani Mkuu ambaye ameketi
mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu
mbinguni, 2 Yeye ahudumuye katika patakatifu,
pa hema la kweli lililowekwa na Bwana, wala si
mwanadamu.

3Kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe sadaka
na dhabihu. Vivyo hivyo ilikuwa jambo muhimu
kwa huyu Kuhani naye awe na kitu cha kutoa.
4Kama angelikuwa duniani, hangelikuwa kuhani,
kwa sababu tayari wapo watu watoao sadaka
kama ilivyoelekezwa na sheria. 5Wanahudumu
katika patakatifu palipo mfano na kivuli cha ile
iliyoko mbinguni. Hii ndiyo sababu Mose alionywa
alipokaribia kujenga hema, akiambiwa: "Hakikisha
kuwa unafanya kila kitu sawasawa na kile
kielelezo ulichoonyeshwa kule mlimani." 6Lakini
huduma Yesu aliyopewa ni bora zaidi kuliko yao
kama vile lile agano ambalo Yeye ni mjumbe
wake lilivyo bora zaidi kuliko lile la zamani, nalo
limewekewa misingi juu ya ahadi zilizo bora zaidi.

7Kwa maana kama hapakuwa na kasoro
katika lile agano la kwanza, pasingekuwa na
haja ya kutafuta nafasi kwa ajili ya jingine.
8Lakini Mungu aliona kosa kwa watu naye
akasema:

"Siku zinakuja, asema Bwana,
nitakapofanya agano jipya
na nyumba ya Israeli
na nyumba ya Yuda.
9Agano hili halitakuwa kama lile
nililofanya na baba
zao nilipowashika mkono
ili kuwatoa katika nchi ya Misri,
kwa kuwa hawakuendelea kuwa
waaminifu katika agano Langu,
nami nikawaacha,
asema
Bwana. 10Baada ya siku zile, hili ndilo agano
nitakalofanya na nyumba ya Israeli,
asema Bwana,

'Nitaweka sheria zangu katika nia zao
na kuziandika katika mioyo yao.
Nitakuwa Mungu wao,
nao watakuwa watu Wangu.
11Mtu hatamfundisha tena jirani yake,
wala mtu hatamfundisha ndugu
yake, akisema, 'Mjue Bwana,'
kwa sababu wote watanijua Mimi,
tangu aliye mdogo wa wote hadi aliye
mkuu sana.
12Kwa kuwa nitasamehe uovu wao,
wala sitazikumbuka dhambi zao tena!"

13Kwa kuliita agano hili "Jipya" Mungu
amefanya lile agano la kwanza kuwa kuukuu,
nacho kitu kinachoanza kuchakaa na kuwa
kikuukuu kiko karibu kitatoweka.

### *Ibada Katika Hema La Kidunia*

**9** Basi agano lile la kwanza lilikuwa na kanuni
zake za kuabudu na pia patakatifu pake pa kidunia.
2Hema lilitengenezwa, katika
sehemu yake ya kwanza kulikuwa na kinara cha
taa, meza na mikate iliyowekwa wakfu, hii
sehemu iliitwa Mahali Patakatifu. 3Nyuma ya
pazia la pili, palikuwa na sehemu iliyoitwa
Patakatifu pa Patakatifu, 4ambako ndiko
kulikokuwa na ile madhabahu ya dhahabu ya
kufukizia uvumba na lile sanduku la agano
lililofunikwa dhahabu. Sanduku hili lilikuwa na
gudulia la dhahabu lenye ile mana, ile fimbo ya
Aroni iliyochipuka na vile vibao vya mawe vya
agano. 5 Juu ya lile sanduku kulikuwa na
makerubi ya utukufu yakitilia kivuli kile kifuniko
ambacho ndicho kiti cha rehema. Lakini
hatuwezi kueleza vitu hivi kwa undani sasa.

6Basi viti hivi vilikuwa vimepangwa, kwamba
makuhani wakiingia daima katika sehemu ya
kwanza ya hema ili kufanya taratibu zao za
ibada, 7lakini ni kuhani mkuu peke yake ndiye
aliyeingia ndani ya sehemu ya pili ya hema, tena
hii alikuwa mara moja tu kwa mwaka, lakini si
bila kuchukua damu ambayo angetoa kwa ajili
yake mwenyewe na kwa ajili ya watu waliotenda
dhambi bila kukusudia. 8Kwa njia hii, Roho
Mtakatifu alikuwa anaonyesha kwamba
maadam ile hema ya kwanza ilikuwa bado
imesimama, njia ya kuingia Patakatifu pa
Patakafifu ilikuwa bado haijafunguliwa. 9Huu
ulikuwa mfano kwa ajili ya wakati wa sasa,
kuonyesha kwamba sadaka na dhabihu
zilizokuwa zikitolewa hazikuweza kusafisha
dhamiri ya mtu anayeabudu. 10Lakini hizi
zilishughulika tu na vyakula na vinywaji pamoja
na taratibu mbalimbali za kunawa kwa nje,
kanuni kwa ajili mwili zilizowekwa hadi wakati
utimie wa matengenezo mapya.

### *Damu Ya Kristo.*

11Kristo alipokuja akiwa Kuhani Mkuu wa
mambo mema ambayo tayari yameshawasili,
alipitia kwenye hema iliyo kuu zaidi na bora
zaidi, ambayo haikujengwa kwa mikono ya
binadamu, hii ni kusema, ambayo si sehemu ya
uumbaji huu. 12Hakuingia kwa njia ya damu ya
mbuzi na ya ndama, lakini aliingia Patakatifu pa
Patakatifu mara moja tu kwa damu yake
mwenyewe, akiisha kupata ukombozi wa milele.
13Damu ya mbuzi na ya mafahali na majivu ya
mitamba vilivyonyunyiziwa wale waliokuwa
najisi kwa taratibu za kiibada viliiwatakasa hata
kuwaondolea uchafu wa nje. 14 Basi si zaidi
sana damu ya Kristo, ambaye kwa Roho wa
milele alijitoa nafsi Yake kwa Mungu kuwa
sadaka isiyo na waa kutusafisha dhamiri zetu,
kutokana na matendo yaletayo mauti, ili tupate
kumtumikia Mungu aliye hai!

15Kwa sababu hii Kristo ni mjumbe wa
agano jipya, ili kwamba wale walioitwa waweze
kupokea ile ahadi ya urithi wa milele, Yeye
alikufa awe ukombozi wao kutoka katika dhambi
walizozitenda chini ya agano la kwanza.

16Kwa habari ya wosia, ni muhimu
kuthibitisha kifo cha yule aliyeufanya, 17kwa
sababu wosia huwa na nguvu tu wakati mtu
akishakufa, kamwe hauwezi kutumika wakati
yule aliyeuandika akiwa bado yuko hai. 18Hii
ndiyo sababu hata lile agano la kwanza
halikuweza kutekelezwa pasipo damu. 19Wakati
Mose alipotangaza kila amri kwa watu wote,
alichukua damu ya ndama na ya mbuzi, pamoja
na maji, sufu nyekundu na matawi ya mti wa
hisopo, akanyunyuzia kile kitabu na watu wote.
20Akisema, "Hii ndiyo damu ya agano, ambalo
Mungu amewaamuru kulitii." 21Vivyo hivyo
alinyunyizia damu hiyo kwenye lile hema
pamoja na kila kifaa kilichotumika ndani yake
kwa taratibu za ibada. 22Kwa kweli sheria hudai
kwamba, karibu kila kitu kitakaswe kwa damu,
wala pasipo kumwaga damu, hakuna msamaha
wa dhambi.

23Kwa hiyo, ilikuwa muhimu kwa nakala za
vitu vile vya mbinguni vitakaswe kwa dhabihu
hizi, lakini vitu halisi vya mbinguni vilihitaji
dhabihu bora kuliko hizi. 24 Kwa maana Kristo
hakuingia kwenye patakatifu palipofanywa kwa

mikono ya mwanadamu, ambao ni mfano wa
kile kilicho halisi. Yeye aliingia mbinguni
penyewe, ili sasa aonekane mbele za Mungu
kwa ajili yetu. 25Wala hakuingia mbinguni ili
apate kujitoa Mwenyewe mara kwa mara, kama
vile kuhani mkuu aingiavyo Patakatifu pa
Patakatifu kila mwaka kwa damu ambayo si
yake mwenyewe. 26Ingelikuwa hivyo,
ingelimpasa Kristo kuteswa mara nyingi tangu
kuumbwa kwa ulimwengu. Lakini sasa
ametokea mara moja tu katika mwisho wa
nyakati aindoe dhambi kwa kujitoa mwenyewe
kuwa dhabihu. 27Kama vile mwandamu
alivyowekewa kufa mara moja tu na baada ya
kufa akabili hukumu, 28 vivyo hivyo Kristo
alitolewa mara moja tu kuwa dhabihu ili
azichukue dhambi za watu wengi, naye atakuja
mara ya pili, si ili kuchukua dhambi, bali
kuwaletea wokovu wale wanaomngoja kwa
shauku.

### *Dhabihu Ya Kristo Ni Mara Moja Tu*

**10** Kwa kuwa Torati ni kivuli tu cha mambo mema
yajayo, wala si uhalisi wa mambo yenyewe. Kwa
sababu hii, haiwezekani
kamwe kwa njia ya dhabihu zitolewazo mwaka
hadi mwaka, kuwakamilisha wale wanaokaribia
ili kuabudu. 2Kama dhabihu hizo zingeweza
kuwakamilisha, hazingeendelea kutolewa tena,
kwa kuwa hao waabuduo wangekuwa
wametakaswa mara moja tu, wala wasingejiona
tena kuwa na dhambi. 3Lakini zile dhabihu
zilikuwa ukumbusho wa dhambi kila mwaka,
4kwa sababu haiwezekani damu ya mafahali na
mbuzi kuondoa dhambi.

5Kwa hiyo, Kristo alipokuja duniani alisema,

“Dhabihu na sadaka hukuzitaka,
bali mwili uliniandalia,
6sadaka za kuteketezwa na za
dhambi hukupendezwa nazo.
7Ndipo niliposema, ‘Tazama niko hapa,
kama nilivyoandikiwa katika kitabu,
Nimekuja kufanya mapenzi
Yako, Ee Mungu.’ ”

8Kwanza alisema, “Dhabihu na sadaka, sadaka
za kuteketezwa na za dhambi hukuzitaka, wala
hukupendezwa nazo” (ingawa sheria iliagiza
zitolewe). 9Kisha akasema “Tazama niko hapa,
nimekuja kuyafanya mapenzi Yako.” Aondoa lile
agano la kwanza ili kuimarisha la pili. 10Katika
mapenzi hayo sisi tumetakaswa na kufanywa
watakatifu kwa njia ya sadaka ya mwili wa Yesu
Kristo alioutoa mara moja tu.

11Kila kuhani husimama siku kwa siku
akifanya huduma yake ya ibada na kutoa tena
na tena dhabihu zile zile ambazo haziwezi
kamwe kuondoa dhambi. 12Lakini huyu kuhani
akiisha kutoa dhabihu moja kwa ajili ya dhambi
kwa wakati wote, aliketi mkono wa kuume wa
Mungu. 13Tangu wakati huo anangoja mpaka
adui zake wawekwe chini ya miguu yake, 14kwa
sababu kwa dhabihu moja amewafanya kuwa
wakamilifu milele wale wote wanaotakaswa.

15Pia Roho Mtakatifu anatushuhudia
kuhusu jambo hili. Kwanza anasema,

16“Hili ndilo agano nitakalofanya nao baada
ya siku hizo, asema Bwana.
Nitaziweka sheria zangu mioyoni mwao,
na kuziandika katika nia zao.”

17Kisha aongeza kusema:

“Dhambi zao na kutokutii
kwao sitakumbuka tena.”

18Basi haya yakiisha kusamehewa, hakuna tena
dhabihu yo yote inayotolewa kwa ajili ya
dhambi.

### *Wito Wa Kuvumilia*

19Kwa hiyo, ndugu zangu, kwa kuwa tunao
ujasiri wa kupaingia Patakatifu pa Patakatifu
kwa damu ya Yesu, 20 kwa njia mpya iliyo hai
tuliyofunguliwa kwa ajili yetu kupitia kwenye lile
pazia, yaani, mwili Wake, 21basi kwa kuwa
tunaye kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu,
22sisi na tumkaribie Mungu kwa moyo mnyofu
kwa imani timilifu, mioyo yetu ikiwa
imenyunyizwa damu ya Kisto na kuwa safi
kutokana na dhamiri mbaya nayo miili yetu ikiwa
imeoshwa kwa maji safi. 23Tushike kwa uthabiti
lile tumaini la ukiri wetu bila kuyumba–yumba,
kwa maana Yeye aliyeahidi ni mwaminifu.
24Tuangaliane na kuhimizana sisi kwa sisi
katika upendo na katika kutenda mema. 25Wala
tusiache kukutana pamoja, kama wengine
walivyo na desturi ya kukutana, tuhimizane sisi
kwa sisi kadri tuonavyo siku ile inakaribia.

26Kama tukiendelea kutenda dhambi kwa
makusudi baada ya kupokea ufahamu wa ile
kweli, hakubaki tena dhabihu kwa ajili ya
dhambi. 27Lakini kinachobaki ni kungoja kwa
hofu hukumu ya moto uwakao

utakaowaangamiza adui za Mungu. 28 Ye yote aliyeikataa sheria ya Mose alikufa pasipo huruma kwa ushahidi wa watu wawili au watatu.
29Je, mnadhani ni adhabu kali kiasi gani anayostahili kupewa mtu aliyemkanyaga Mwana wa Mungu chini ya nyao zake, yeye aliyeifanya damu ya agano iliyomtakasa kuwa kitu najisi na kumtendea maovu Roho wa neema? 30Kwa kuwa tunamjua Yeye aliyesema, "Kulipiza kisasi ni juu Yangu, Mimi nitalipiza." Tena asema, "Bwana atawahukumu watu Wake." 31Ni jambo la kutisha kuanguka mikononi mwa Mungu aliye hai.

32Kumbukeni siku zile za kwanza, ambazo mkiisha kutiwa nuru mlistahimili mashindano makali ya maumivu. 33Wakati mwingine mlitukanwa na kuteswa hadharani, wakati mwingine mlikuwa radhi kuungana na wale waliofanyiwa hivyo. 34Mliwahurumia wale waliokuwa kifungoni, mkikubali kwa furaha kunyang'anganywa mali zenu kwa maana mlijua kwamba mnayo mali iliyo bora zaidi idumuyo.

35Kwa hiyo msilitupe tumaini lenu, kwa maana lina thawabu kubwa mno. 36Inawapasa kuvumilia ili mkiisha kufanya mapenzi ya Mungu mpate kile alichoahidi. 37Kwa kuwa bado kitambo kidogo tu,

"Yeye ajaye atakuja wala hatakawia, 38Lakini mwenye haki Wangu ataishi kwa imani.
Lakini kama akisita-sita sina furaha naye."

39Lakini sisi hatumo miongoni mwa hao wanaosita na kuangamia, bali tuko miongoni mwa hao wenye imani na hivyo tunaokolewa.

### *Maana Ya Imani*

**11** Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni udhahiri wa mambo yasiyoonekana. 2Naam, kwa imani baba zetu wa kale walishuhudiwa.

3Kwa imani tunafahamu kwamba ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, vitu vyote vinavyoonekana viliumbwa kwa vitu visivyoonekana.

### *Mfano Wa Abeli, Enoki Na Noa*

4 Kwa imani Abeli alimtolea Mungu dhabihu bora zaidi kuliko Kaini. Kwa imani alishuhudiwa kuwa mwenye haki, Mungu mwenyewe akazishuhudia sadaka zake. Kwa imani bado ananena ingawa amekufa.

5Kwa imani Enoki alitwaliwa kutoka katika maisha haya, kiasi kwamba hakuonja mauti. Hakuonekana, kwa sababu Mungu alikuwa amemchukua. Kwa kuwa kabla hajatwaliwa alikuwa ameshuhudiwa kuwa ni mtu aliyempendeza Mungu. 6Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana ye yote anayemjia Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko na ya kuwa huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.

7Kwa imani, Noa alipoonywa na Mungu kuhusu mambo ambayo hayajaonekana bado, kwa kumcha Mungu alitengeneza safina ili kuokoa jamaa yake. Kwa imani yake aliuhukumu ulimwengu na akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.

### *Imani Ya Abrahamu*

8Kwa imani Abrahamu, alipoitwa aende mahali ambapo Mungu angempa baadaye kuwa urithi, alitii na akaenda, ingawa hakujua anakokwenda. 9 Kwa imani alifanya maskani yake katika nchi ya ahadi kama mgeni katika nchi ya kigeni, akaishi katika mahema, kama Isaki na Yakobo walivyofanya, waliokuwa pia warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. 10Kwa maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi ya kudumu ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.

11 Kwa imani Abrahamu, ingawa alikuwa mzee wa umri, naye Sara mwenyewe aliyekuwa tasa, alipokea uwezo wa kuwa baba kwa sababu alimhesabu Mungu aliyemwahidi kuwa mwaminifu na kwamba angelitimiza ahadi Yake.
12Hivyo kutokana na huyu huyu ambaye alikuwa sawa na mfu, wakazaliwa wazao wengi kama nyota za mbinguni na kama mchanga wa pwani usiohesabika.

13Watu hawa wote wakafa katika imani bila kuzipokea zile ahadi, lakini waliziona kwa mbali na kuzishangilia. Nao walikubali kwamba walikuwa wageni na wasiokuwa na maskani hapa duniani. 14Watu wasemao mambo kama haya, wanaonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe. 15Kwa kweli kama wangekuwa wanafikiri kuhusu nchi waliyoiacha, wangalipata nafasi ya kurudi huko. 16 Lakini badala yake wanatamani nchi iliyo bora zaidi, yaani, nchi ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao, kwa kuwa amekwisha kuandalia mji kwa ajili yao.

17Kwa imani Abrahamu, alipojaribiwa na Mungu, alimtoa Isaki kuwa dhabihu. Yeye

aliyekuwa amezipokea ahadi za Mungu alikuwa tayari kumtoa mwanawe, aliyekuwa mwanawe pekee awe dhabihu. 18Ingawa Mungu alikuwa amemwambia Abrahamu, "Uzao wako utahesabiwa kwa njia ya Isaki,'' 19 Abrahamu alihesabu kuwa Mungu angaliweza kumfufua Isaki kutoka kwa wafu na kwa kusema kwa mfano alimpata tena Isaki kutoka kwa wafu.

20Kwa imani Isaki alimbariki Yakobo na Esau kuhusu maisha yao ya baadaye.

21Kwa imani Yakobo alipokuwa anakufa, alimbariki kila mmoja wa mtoto wa Yosefu, akamwabudu Mungu akiwa ameegemea juu ya kichwa cha fimbo yake.

22Kwa imani, Yosefu alipokaribia mwisho wa maisha yake, alinena habari za kutoka kwa wana wa Israeli huko Misri na akatoa maagizo kuhusu mifupa yake.

### *Imani Ya Mose*

23Kwa imani, wazazi wa Mose walimficha kwa miezi mitatu baada ya kuzaliwa, kwa sababu waliona kuwa si mtoto wa kawaida, wala hawakuiogopa amri ya mfalme.

24Kwa imani, Mose alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa mwana wa binti Farao. 25Akachagua kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha kwa anasa za dhambi kwa kitambo kidogo tu. 26Aliona kushutumiwa kwa ajili ya Kristo ni utajiri mkubwa zaidi kuliko hazina za Misri, maana alikuwa anatazamia kupata thawabu baadaye. 27Kwa imani Mose aliondoka Misri bila kuogopa ghadhabu ya mfalme, alivumilia kwa sababu alimwona Yeye asiyeonekana kwa macho. 28Kwa imani akaadhimisha Pasaka na kunyunyiza damu, ili yule mwenye kuwaangamiza wazaliwa wa kwanza asiwaguse wazaliwa wa Israeli.

### *Imani Ya Mashujaa Wengine Wa Israeli*

29Kwa imani, watu walivuka Bahari ya Shamu kama vile juu ya nchi kavu, lakini Wamisri walipojaribu kufanya hivyo, walitoswa ndani ya maji.

30Kwa imani kuta za Yeriko zilianguka, baada ya watu kuzizunguka kwa siku saba.

31Kwa imani, Rahabu, yule kahaba, hakuangamizwa pamoja na wale waliomwasi Mungu, kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi.

32Basi niseme nini zaidi? Sina wakati wa kusema habari za Gideoni, Baraka, Samsoni, Yeftha, Daudi, Samweli na manabii, 33ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitekeleza haki, walipokea ahadi za Mungu, walifunga vinywa vya simba, 34walizima makali ya miali ya moto, waliepuka kuuawa kwa upanga, udhaifu wao ukageuka kuwa nguvu, walikuwa hodari vitani wakayashinda majeshi ya wageni na kuyafukuza. 35Wanawake walipokea watu wao waliokuwa wamekufa wakafufuliwa. Lakini wengine waliteswa nao wakakataa kufunguliwa, ili wapate ufufuo ulio bora zaidi. 36Wengine walidhihakiwa na kupigwa, hata walifungwa minyonyoro na kutiwa gerezani. 37Walipigwa kwa mawe, walipasuliwa vipande viwili kwa msumemo, waliuawa kwa upanga, walizunguka-zunguka wakiwa wamevaa ngozi za kondoo na mbuzi, wakiwa maskini, waliteswa na kutendwa mabaya, 38watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao. Walizunguka majangwani na milimani, katika mapango na katika mahandaki ardhini.

39Hawa wote walishuhudiwa vema kwa sababu ya imani yao, lakini hakuna hata mmoja wao aliyepokea yale yaliyoahidiwa. 40Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea kitu kilicho bora zaidi ili tu kwamba wao wasikamilishwe pasipo sisi.

### *Mungu Huwaadibisha Wanawe*

**12** Kwa sababu hii, kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa namna hii la mashahidi, basi na tuweke kando kila kitu kinachotuzuia na ile dhambi inayotuzinga kwa urahisi, nasi tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa kwa ajili yetu. 2 Basi na tumtazame sana Yesu mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu, Yeye ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake alistahimili msalaba, bila kujali aibu ya huo msalaba, naye ameketi mkono wa kuume wa Mungu. 3Mtafakarini sana Yeye aliyestahimili upinzani mkuu namna hii kutoka kwa watu wenye dhambi, ili kwamba msije mkachoka na kukata tamaa.

4Katika kushindana kwenu dhidi ya dhambi, bado hamjapigana kiasi cha kumwaga damu yenu. 5Nanyi mmesahau yale maneno ya kuwaonya yanayowataja ninyi kuwa wana, yakisema,

"Mwanangu, usidharau kuadibishwa
na Bwana
wala usikate tamaa,

6kwa sababu Bwana huwaadibisha
wale awapendao
na humwadhibu kila mmoja anayemkubali
kuwa mtoto Wake."

7Vumilieni taabu kwa ajili ya kufunzwa adabu. Mungu anawatendea ninyi kama watoto Wake, kwa maana ni mtoto yupi asiyeadibishwa
na mzazi wake? 8Kama hakuna kuadibishwa (ambalo ni fungu la watoto wote), basi ninyi ni
watoto wa haramu wala si watoto halali. 9Tena, sisi sote tunao baba wa kimwili, waliotuadibisha nasi tukawaheshimu kwa ajili ya hilo. Je, si inatupasa kujinyenyekeza zaidi kwa Baba wa
roho zetu ili tuishi? 10Baba zetu walituadibisha kwa kitambo kidogo kama wao wenyewe walivyoona vema, lakini Mungu hutuadibisha kwa faida yetu ili tupate kushiriki utakatifu Wake.
11Kuadibishwa wakati wo wote hakuonekani kuwa kitu cha kufurahisha bali chenye maumivu kinapotekelezwa. Lakini baadaye huzaa matunda ya haki na amani kwa wale waliofunzwa nayo.

12Kwa hiyo itieni nguvu mikono yenu iliyo dhaifu na magoti yenu yaliyolegea.
13Sawazisheni mapito ya miguu yenu, ili kitu kilicho kiwete kisidhoofishwe bali kiponywe.

***Onyo Dhidi Ya Kuikataa Neema Ya Mungu*.**

14Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote na huo utakatifu, ambao bila kuwa nao,
hakuna mtu atakayemwona Bwana. 15Angalieni sana mtu ye yote asiikose neema ya Mungu na kwamba shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua na watu wengi wakatiwa unajisi
kwa hilo. 16 Angalieni miongoni mwenu asiwepo mwasherati au mtu asiyemcha Mungu kama Esau, ambaye kwa ajili ya mlo mmoja aliuza
haki ya uzaliwa wake wa kwanza. 17Mnajua kwamba baadaye kama mnavyofahamu, alipotaka kurithi ile baraka, alikataliwa, maana hakupata nafasi ya kutubu, ingawa aliitafuta kwa machozi.

18Hamjaufikia mlima ule uwezao kuguswa na ambao unawaka moto, wala kwenye giza,
utusitusi na dhoruba, 19kwenye mlio wa tarumbeta, au kwenye sauti isemayo maneno ya kutisha kiasi ambacho wale walioisikia waliomba
wasiambiwe neno jingine zaidi, 20kwa sababu wasingeliweza kustahimili neno lile lililoamriwa: "Hata kama mnyama atagusa mlima huu,
atapigwa mawe." 21Waliyoyaona yalikuwa ya kutisha kiasi kwamba Mose alisema, "Ninatetemeka kwa hofu."

22Lakini ninyi mmeufikia Mlima wa Sayuni, Yerusalemu ya mbinguni, mji wa Mungu aliye hai. Mmefika penye kusanyiko kubwa la malaika maelfu kwa maelfu wasiohesabika
wanaoshangilia, 23kwenye kanisa la wazaliwa wa kwanza wa Mungu, ambao majina yao yameandikwa mbinguni. Mmekuja kwa Mungu, mhukumu wa watu wote, kwenye roho za wenye
haki waliokamilishwa, 24kwa Yesu mjumbe wa agano jipya na kwa damu iliyonyunyuzwa ile inenayo mambo mema kuliko damu ya Abeli.

25Angalieni, msije mkamkataa yeye anenaye. Ikiwa wao hawakuepuka adhabu walipomkataa yeye aliyewaonya hapa duniani, sisi je, tutaokokaje tusimpomsikiliza Yeye
anayetuonya kutoka mbinguni? 26Wakati ule sauti Yake ilitetemesha dunia, lakini sasa ameahidi, "Kwa mara moja tena nitatetemesha si nchi tu bali na mbingu pia."

27Maneno haya, "Kwa mara moja tena" yanaonyesha kuondoshwa kwa vile vitu vinavyoweza kuondoshwa, yaani, vile vitu vilivyoumbwa ili kusudi vibaki vile tu visivyoweza kutetemeshwa.

28Kwa hiyo, kwa kuwa tunapokea ufalme ule
ambao hauwezi kutetemeshwa, basi na tuwe na shukrani na hivyo tumwabudu Mungu kwa namna inavyompendeza, kwa unyenyekevu na uchaji,
29kwa kuwa "Mungu wetu ni moto ulao."

***Huduma Inayompendeza Mungu***

**13** Upendo wa kidugu na udumu.

2Msisahau kuwakaribisha wageni, kwa kuwa kwa kufanya hivyo, watu wengine waliwakaribisha malaika pasipo kujua.
3Wakumbukeni wale waliofungwa gerezani kama vile nanyi mmefungwa pamoja nao, pia wakumbukeni wale wanaotendwa vibaya, kama vile ni ninyi wenyewe mnateswa.

4Ndoa na iheshimiwe na watu wote, nayo malazi yawe safi, kwa kuwa Mungu atawahukumu wazinzi na waasherati wote.
5Yalindeni maisha yenu msiwe na tabia ya kupenda fedha, bali mridhike na vile mlivyo navyo, kwa sababu Mungu amesema,

"Kamwe sitakuacha
wala sitakupungukia."

6Kwa hiyo tunaweza kusema kwa ujasiri,

"Bwana ni msaada wangu, sitaogopa,
mwanadamu atanitenda nini?"

7 Wakumbukeni viongozi wenu, wale
waliowaambia neno la Mungu. Angalieni
matokeo ya mwenendo wa maisha yao mkaiige
imani yao. 8 Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo
na hata milele.

9 Msichukuliwe na kila aina ya mafundisho ya
kigeni. Ni vema mioyo yenu iimarishwe kwa
neema, wala si kwa sheria kuhusu utaratibu wa
vyakula, ambavyo havina faida kwa wale
wanaozishika. 10 Sisi tunayo madhabahu ambayo
wale wanaohudumu katika hema hawana haki ya
kula vile vitu vilivyowekwa juu yake.

11 Kuhani mkuu huchukua damu ya
wanyama na kuiingiza Patakatifu pa Patakatifu,
kama sadaka ya dhambi, lakini miili ya hao
wanyama huteketezwa nje ya kambi. 12 Vivyo
hivyo Yesu naye aliteswa nje ya lango la mji ili
awatakase watu kwa damu Yake mwenyewe.
13 Kwa hiyo basi na tumwendee nje ya kambi,
tukiichukua aibu aliyobeba. 14 Kwa kuwa hapa
hatuna mji udumuo, bali tunautafuta ule ujao.

15 Basi kwa njia Yake, tuzidi kumtolea
Mungu dhabihu ya sifa, yaani, matunda ya
midomo inayolikiri Jina Lake. 16 Msiache kutenda
mema na kushirikiana vile mlivyo navyo, kwa
kuwa dhabihu kama hizo ndizo zinazompendeza
Mungu.

17 Watiini viongozi wenu na kujinyenyekeza
chini ya mamlaka yao. Kwa maana wao
wanakesha kwa ajili yenu kama watu
watakaopaswa kutoa hesabu. Watiini ili kwamba
wafanye kazi yao kwa furaha, wala si kama
mzigo, maana hiyo haitakuwa na faida kwenu.

18 Tuombeeni. Tuna hakika kuwa tunayo
dhamiri safi na shauku ya kuishi kwa uadilifu
kwa kila njia. 19 Ninawasihi zaidi mniombee ili
nipate kurudishwa kwenu upesi.

### *Maombi Ya Kuwatakia Baraka*

20 Basi Mungu wa amani, ambaye kwa damu
ya agano la milele alimleta tena kutoka kwa
wafu Bwana wetu Yesu, yule Mchungaji Mkuu
wa kondoo, 21 awafanye ninyi wakamilifu mkiwa
mmekamilishwa katika kila jambo jema ili mpate
kutenda mapenzi Yake, ili atende ndani yetu kile
kinachompendeza machoni Pake, kwa njia ya
Yesu Kristo, ambaye utukufu una Yeye milele na
milele. Amen.

### *Maneno Ya Mwisho Na Salamu*

22 Ndugu zangu, nawasihi mchukuliane na
maneno yangu ya maonyo, kwa kuwa
nimewaandikia waraka mfupi tu.

23 Nataka ninyi mjue kwamba ndugu yetu
Timotheo amefunguliwa kutoka gerezani. Akifika
mapema, nitakuja pamoja naye kuwaona.

24 Wasalimuni viongozi wenu wote na
watakatifu wote. Wale wa kutoka Italia
wanawasalimu.

25 Neema iwe nanyi nyote. Amen.

## Yakobo

### *Utangulizi*

Waraka wa Yakobo unaweza ukawa mojawapo ya nyaraka za kwanza kabisa katika Agano Jipya, huenda wakati mmoja na ule wa Paulo kwa Wagalatia. Waraka huu uliandikiwa kwa Wakristo wa Kiyahudi wa Utawanyiko waliokuwa katika hali ya ugeni huko Ponto, Galatia, Kapadokia, Asia na Bithinia ili kuwapatia mawaidha kuhusu jinsi inavyopasa kuishi kama waamini wakidhihirishwa na matendo mema na imani itendayo kazi.. Barua hii ina methali nyingi fupi fupi zinazosaidia kuweka wazi yale mafundisho ya Bwana Yesu ya Mlimani. Matatizo yanayozungumziwa ni matatizo yaliyokuwa yakiwasumbua waamini.

Tunasoma juu ya kiburi, ubaguzi, choyo, tamaa, unafiki, kupenda anasa na kusengenya. Yakobo anaandika kusahihisha makosa haya kwa kuonyesha kwamba imani pasipo matendo imekufa *(2:26).* Hii ina maana kuwa kusema tu kwamba unaamini hakutoshi. Imani halisi huambatana na matendo.

### *Wazo kuu*

Yakobo anasisitiza umuhimu wa mkristo kuishi maisha yanayodhihirisha hali yake ya ndani. Hapo ndipo ulimwengu utapata kujua jinsi Injili iwezavyo kubadili maisha ya watu. Kama mtu anajiita mkristo lakini maisha yake ni sawasawa na ya mtu asiyeamini, atakuwa hajapata faida yo yote, nao watu wanaomwona pia watakuwa hawajasaidika cho chote. Ukweli ni kwamba Injili hubadilisha maisha. Kama tukijitoa kwa Kristo tutaona kwamba, kwa sababu ya imani yetu, matendo hai yaliyo mema na yenye upendo yatatiririka na kuwabariki wengine.

### *Tarehe*

Waraka huu unawezekana ukawa umeandikwa wakati mmoja na ule wa Wagalatia kama 48 B.K.

### *Mwandishi*

Yakobo ambaye kwenye Injili ametambuliwa kuwa ndugu wa kunyonya wa Yesu *(Mk.6:3)*

### *Mgawanyo*

- Maisha ya imani ya kweli (1:1-27)
- Matarajio ya watu wasioamini kwa Wakristo (2:1-13)
- Imani ya kweli na matendo (2:14-26)
- Kuhusu kuutawala ulimi (3:1-18)
- Mwenendo upasao (4:1-17)
- Matajiri wakemewa (5:1-6)
- Mawaidha ya mwisho (5:7-20).

**1** Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu
Kristo,

Kwa makabila kumi na mawili
yaliyotawanyika ulimwenguni, salamu.

### *Imani Na Hekima*

2 Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha
tupu mnapopatwa na majaribu mbalimbali, 3kwa
sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa imani
yenu huleta saburi. 4Saburi na iwe na kazi
timilifu, ili mpate kuwa wakamilifu,
mmekamilishwa, bila kupungukiwa na kitu cho
chote. 5Kama mtu ye yote miongoni mwenu
amepungukiwa na hekima na amwombe Mungu,
Yeye awapaye watu wote kwa ukarimu wala
hana kinyongo, naye atapewa. 6Lakini
anapoomba, lazima aamini wala asiwe na
shaka, kwa sababu mtu aliye na shaka ni kama
wimbi la bahari, lililochukuliwa na upepo na
kutupwa huku na huku. 7Mtu kama huyo
asidhani ya kuwa atapata kitu cho chote kutoka
kwa Bwana. 8Yeye ni mtu mwenye nia mbili,
mwenye kusitasita katika njia zake zote.

### *Umaskini Na Utajiri*

9Ndugu asiye na cheo kikubwa yampasa
ajivunie hali hiyo maana ametukuzwa. 10Lakini
yeye aliye tajiri yampasa asijivunie hali hiyo
maana ameshushwa, kwa sababu atatoweka
kama ua la shambani. 11Kwa maana jua kali
lenye kuchoma huchomoza na kuliuunguza,
likayakausha majani na ua lake likapukutika nao
uzuri wake huharibika. Vivyo hivyo tajiri naye
atanyauka akiwa anaendelea na shughuli zake.

### *Kujaribiwa*

12Heri mtu anayevumilia wakati wa
majaribu, kwa sababu akiisha kushinda hilo
jaribio atapewa taji ya uzima Mungu
aliyowaahidia wale wampendao.

13Mtu anapojaribiwa asiseme, ‘‘Ninajaribiwa
na Mungu’’ kwa maana Mungu hawezi
kujaribiwa na maovu wala Yeye hamjaribu mtu
ye yote. 14 Lakini kila mtu hujaribiwa wakati
anapovutwa na kudanganywa na tamaa zake
mwenyewe. 15Basi ile tamaa akiisha kuchukua
mimba, huzaa dhambi, ile dhambi ikikomaa,
huzaa mauti.

16Ndugu zangu, msidanganyike. 17Kila
kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili,
hutoka juu, hushuka kutoka kwa Baba wa
mianga, ambaye Kwake hakuna kubadilika,
wala kivuli cha kugeuka-geuka. 18Kwa mapenzi
Yake mwenyewe alituzaa kwa Neno la kweli,
kusudi tuwe kama mazao ya kwanza katika
viumbe Vyake vyote.

### *Kusikia Na Kutenda*

19Ndugu zangu wapendwa, fahamuni jambo
hili: Kila mtu awe mwepesi wa kusikia, lakini
asiwe mwepesi wa kusema wala wa kukasirika.
20Kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi
haki ya Mungu. 21Kwa hiyo, ondoleeni mbali
uchafu wote na uovu ambao umezidi kuwa
mwingi, mkalipokee kwa unyenyekevu lile Neno
lililopandwa ndani yenu ambalo laweza kuokoa
nafsi zenu.

22Basi iweni watendaji wa Neno wala msiwe
wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu.
23Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno
wala hatendi kile linachosema, yeye ni kama
mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo 24na
baada ya kujiona alivyo, huenda zake na mara
husahau jinsi alivyo. 25Lakini yeye anayeangalia
kwa bidii katika sheria kamilifu, ile iletayo uhuru,
naye akaendelea kufanya hivyo bila kusahau
alichosikia, bali akalitenda, atabarikiwa katika
kile anachofanya.

26Kama mtu akidhani ya kuwa anayo dini
lakini hauzuii ulimi wake kwa hatamu, bali
hujidanganya moyoni mwake, dini yake mtu
huyo haifai kitu. 27Dini iliyo safi, isiyo na uchafu,
inayokubalika mbele za Mungu Baba yetu,
ndiyo hii: Kuwasaidia yatima na wajane katika
dhiki zao na kujilinda usitiwe madoa na dunia.

### *Onyo Kuhusu Upendeleo*

**2** Ndugu zangu, kama waaminio katika imani
ya Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu,
msiwe na upendeleo kwa watu.
2Kwa maana kama akija mtu katika kusanyiko
lenu akiwa amevaa pete ya dhahabu na mavazi
mazuri, pia akaingia mtu maskini mwenye
mavazi yaliyochakaa, 3nanyi mkampa heshima
yule aliyevaa mavazi mazuri na kumwambia,
‘‘Keti hapa mahali pazuri,’’ lakini yule maskini
mkamwambia, ‘‘Wewe simama pale,’’ au ‘‘Keti
hapa sakafuni, karibu na miguu yangu,’’ 4je,
hamjawabagua na kuwa mahakimu mioyoni
mwenu mkihukumu kwa mawazo yenu maovu?

5Ndugu zangu, sikilizeni: Je, Mungu
hakuwachagua wale walio maskini machoni pa
ulimwengu kuwa matajiri katika imani na kuurithi
Ufalme aliowaahidi wale wampendao? 6Lakini
ninyi mmemdharau yule aliye maskini. Je, hao

matajiri si ndio wanaowadhulumu na kuwapeleka mahakamani? [7]Je, si wao wanaolikufuru Jina lile lililo bora sana mliloitiwa?

[8]Kama kweli mnaitimiza ile sheria ya kifalme inayopatikana katika Maandiko isemayo, ‘‘Mpende jirani yako kama unavyoipenda nafsi yako,’’ mnafanya vema. [9] Lakini kama mnakuwa na upendeleo kwa watu, mnatenda dhambi na sheria inawahukumu kuwa ninyi ni wakosaji. [10]Kwa maana mtu ye yote anayeishika sheria yote lakini akajikwaa katika kipengele kimoja tu, ana hatia ya kuivunja sheria yote. [11]Kwa sababu Yeye aliyesema, ‘‘Usizini,’’ alisema pia, ‘‘Usiue.’’ Basi kama huzini lakini unaua, umekuwa mvunjaji wa sheria yote.

[12]Hivyo semeni na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo uhuru. [13]Kwa kuwa hukumu itakuwa haina huruma kwa mtu ye yote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda hukumu.

### *Imani Na Matendo*

[14] Ndugu zangu, yafaa nini ikiwa mtu atadai kuwa anayo imani lakini hana matendo? Je, imani kama hiyo yaweza kumwokoa? [15]Ikiwa ndugu yako au dada hana mavazi wala chakula, [16]mmoja wenu akamwambia, ‘‘Enenda zako kwa amani, ukaote moto na kushiba,’’ pasipo kumpatia yale mahitaji ya mwili aliyopungukiwa, yafaa nini ? [17]Vivyo hivyo, imani peke yake kama haikuimbatana na matendo, imekufa.

[18]Lakini mtu mwingine atasema, ‘‘Wewe unayo imani, mimi ninayo matendo.’’

Nionyeshe imani yako pasipo matendo nami nitakuonyesha imani yangu kwa matendo. [19]Unaamini kwamba kuna Mungu mmoja. Vema! Hata mashetani yanaamini hivyo na kutetemeka.

[20] Je, wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani bila matendo haifai kitu? [21]Je, Abrahamu baba yetu hakuhesabiwa haki kwa kile alichotenda, alipomtoa mwanawe Isaki madhabahuni? [22]Unaona jinsi ambavyo imani yake na matendo yake vilikuwa vinatenda kazi pamoja, nayo imani yake ikakamilishwa na kile alichotenda. [23]Kwa njia hiyo yakatimizwa yale Maandiko yasemayo, ‘‘Abrahamu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki,’’ naye akaitwa rafiki wa Mungu. [24]Mnaona ya kwamba mtu huhesabiwa haki kwa yale anayotenda wala si kwa imani peke yake.

[25]Vivyo hivyo, hata Rahabu, yule kahaba, hakuhesabiwa haki kwa yale aliyotenda alipowapokea wale wapelelezi na kuwaambia waende njia nyingine? [26]Kama vile ambavyo mwili pasipo roho umekufa, kadhalika nayo imani pasipo matendo imekufa.

### *Kuufuga Ulimi*

**3** Ndugu zangu, msiwe walimu wengi, kwa maana mnafahamu kwamba sisi tufundishao tutahukumiwa vikali zaidi. [2]Sisi sote tunajikwaa katika mambo mengi. Ikiwa mtu ye yote hakosei kamwe katika yale anayosema, yeye ni mkamilifu, naye anaweza kuuzuia pia na mwili wake wote.

[3]Tunapotia lijamu kwenye vinywa vya farasi ni ili kuwafanya watutii, hivyo tunaweza kuigeuza miili yao yote. [4]Au angalia pia meli, ingawa ni kubwa sana, nazo huchukuliwa na upepo mkali, lakini hugeuzwa kwa usukani mdogo sana, ko kote anakotaka nahodha. [5]Vivyo hivyo ulimi ni kiungo kidogo sana katika mwili, lakini hujivuna majivuno makuu. Fikirini jinsi moto mdogo unavyoweza kuteketeza msitu mkubwa! [6]Ulimi pia ni moto, ndio ulimwengu wa uovu katika ya viungo vya mwili wetu. Ulimi huutia mwili wote wa mtu unajisi na kuuwasha moto mfumo mzima wa maisha yake, nao wenyewe huchomwa moto wa jehanam.

[7]Kwa maana kila aina ya mnyama na ndege, wanyama watambaao na wanyama wa kila aina, ndege, nyoka na viumbe vya baharini wanaweza kufugwa na vimekwisha kufugwa na binadamu, [8]lakini hakuna mtu awezaye kuufuga ulimi. Ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti.

[9]Kwa ulimi tunamhimidi Bwana, yaani, Baba yetu na kwa huo twawalaani watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu. [10]Katika kinywa hicho hicho hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, haistahili kuwa hivyo. [11] Je, chemchemi yaweza kutoa katika tundu moja maji matamu na maji ya chumvi? [12]Je, ndugu zangu, mtini waweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa tini? Wala chemchemi ya maji ya chumvi haiwezi kutoa maji matamu.

### *Aina Mbili Za Hekima*

[13]Ni nani aliye na hekima na ufahamu miongoni mwenu? Basi na aionyeshe hiyo kwa maisha yake mema na kwa matendo yake yaliyotendwa kwa unyenyekevu utokanao na hekima. [14]Lakini ikiwa mna wivu na ni wenye chuki na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu kwa ajili ya hayo wala msiikatae kweli. [15]Hekima ya

namna hiyo haishuki kutoka mbinguni bali ni ya kidunia, ya tabia ya kibinadamu wala si ya kiroho bali ni ya Shetani. 16 Kwa maana panapokuwa na wivu na ugomvi ndipo penye machafuko na uovu wa kila namna.

17Lakini hekima itokayo mbinguni kwanza ni safi, kisha inapenda amani, ya upole, iliyo tayari kusikiliza maneno ya watu wengine, yenye unyenyekevu, iliyojaa huruma na matunda mema, isiyopendelea mtu, tena ya kweli.
18Mavuno ya haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani.

### *Jinyenyekezeni Kwa Mungu*

**4** Ni kitu gani kinachosababisha mapigano na ugomvi miongoni mwenu? Je, haya hayatokani na tamaa zenu zinazoshindana ndani yenu?
2Mnatamani lakini hampati, kwa hiyo mwaua. Mwatamani kupata lakini hampati vile mnavyotaka, kwa hiyo mnajitia katika magomvi na mapigano. Mmepungukiwa kwa sababu hamumwombi Mungu. 3Mnapoomba hampati kwa sababu mnaomba kwa nia mbaya, ili mpate kuvitumia hivyo mtakavyopata kwa tamaa zenu.

4Ninyi wanaume na wanawake wanzinzi, hamjui ya kwamba urafiki na dunia ni uadui na Mungu? Kwa hiyo mtu ye yote anayetaka kuwa rafiki wa dunia hufanyika adui wa Mungu. 5Au mwadhani kwamba maandiko yanasema bure kuwa, huyo Roho ambaye Mungu amemweka ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu?
6Lakini Yeye hutupatia neema zaidi. Hii ndiyo sababu Maandiko husema:

> "Mungu huwapinga wenye kiburi,
> lakini huwapa wanyenyekevu neema."

7Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. 8Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, ninyi wenye dhambi na kuisafisha mioyo yenu, ninyi wenye nia mbili. 9Huzunikeni, ombolezeni na kulia. Kicheko chenu na kigeuzwe kuwa kuombeleza na furaha yenu kuwa huzuni.
10Jinyenyekezeni mbele za Bwana, naye atawainua.

### *Onyo Kuhusu Kuhukumu Wengine*

11 Ndugu, msineneane mabaya ninyi kwa ninyi. Mtu ye yote anayesema mabaya dhidi ya ndugu yake au kumhukumu anasema dhidi ya sheria na kuihukumu. Unapoihukumu sheria, basi huishiki sheria bali umekuwa hakimu wa kuihukumu hiyo sheria. 12Yuko Mtoa–Sheria mmoja tu na Yeye peke Yake ndiye Hakimu. Yeye awezaye kuokoa na kuangamiza. Lakini wewe ni nani hata umhukumu jirani yako?

### *Kujivuna Kwa Ajili Ya Kesho*

13Basi sikilizeni ninyi msemao, "Leo au kesho tutakwenda katika mji huu ama ule tukae humo mwaka mmoja, tufanye biashara na kupata faida." 14Lakini hamjui hata litakalotukia kesho. Maisha yenu ni nini? Ninyi ni ukungu ambao huonekana kwa kitambo kidogo kisha hutoweka. 15Badala yake, inawapasa kusema, "Kama Bwana akipenda, tutaishi na kufanya hili ama lile." 16Kama ilivyo sasa, mnajisifu na kujigamba. Kujisifu kwa namna hiyo ni kubaya.
17Basi mtu ye yote anayejua jema limpasalo kutenda, lakini asilitende, mtu huyo anatenda dhambi.

### *Onyo Kwa Matajiri*

**5** Basi sikilizeni, ninyi matajiri, lieni na kuomboleza kwa ajili ya hali mbaya sana inayowajia. 2Utajiri wenu umeoza na mavazi yenu yameliwa na nondo. 3Dhahabu yenu na fedha yenu vimeliwa na kutu. Kutu yake itashuhudia dhidi yenu nayo itaila miili yenu kama vile moto. Mmejiwekea hazina kwa ajili ya siku za mwisho. 4Angalieni! Ule ujira wa vibarua waliolima mashamba yenu mliouzuia kwa hila unapiga kelele dhidi yenu na vilio vya wavunaji vimefika masikioni mwa Bwana wa majeshi[a].
5Mmeishi duniani kwa anasa na kwa starehe, mmejinenepesha kama vile katika siku ya karamu. 6Mmewahukumu na kuwauwa watu wenye haki , ambao walikuwa hawapingani nanyi.

### *Uvumilivu Katika Mateso*

7Kwa hiyo, ndugu zangu, vumilieni hadi kuja Kwake Bwana. Angalieni jinsi mkulima angojavyo ardhi itoe mavuno yake yaliyo ya thamani na jinsi anavyovumilia kwa ajili ya kupata mvua za kwanza na za mwisho. 8Ninyi nanyi vumilieni tena simameni imara, kwa sababu kuja kwa Bwana kumekaribia. 9Ndugu zangu, msinung'unikiane msije mkahukumiwa. Hakimu amesimama mlangoni!

---

a4 Bwana wa majeshi hapa ni neno la Kiebrania, Bwana wa Sabaoth pia kwenye *(Rum. 9:29, Isa. 1:9)*

10Ndugu zangu, waangalieni manabii
walionena kwa Jina la Bwana, ili kuwa mfano wa
uvumilivu katika kukabiliana na mateso. 11Kama
mnavyojua, tunawahesabu kuwa wamebarikiwa
wale waliovumilia. Mmesikia habari za uvumilivu
wake Ayubu na mmeona kile ambacho hatimaye
Bwana alimtendea. Bwana ni mwingi wa huruma
naye aliyejaa rehema.

12Zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, ama
kwa mbingu, au kwa dunia au kwa kitu kingine
cho chote. ‘‘Ndiyo’’ yenu na iwe ndiyo na
‘‘Hapana’’ yenu, iwe hapana, la sivyo
mtahukumiwa.

***Maombi Ya Imani***

13Je, mtu ye yote miongoni mwenu
amepatwa na taabu? Basi inampasa aombe. Je,
kuna ye yote mwenye furaha? Basi na aimbe
nyimbo za kusifu. 14Je, kuna ye yote miongoni
mwenu aliye mgonjwa? Basi inampasa awaite
wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka
mafuta kwa Jina la Bwana. 15Kule kuomba kwa
imani kutamwokoa huyo mgonjwa, naye Bwana
atamwinua na kama ametenda dhambi,
atasamehewa. 16Kwa hiyo ungamianeni
makosa yenu ninyi kwa ninyi na kuombeana ili
mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki
yana nguvu tena yanafaa sana.

17Eliya alikuwa mwanadamu kama sisi.
Akaomba kwa bidii kwamba mvua isinyeshe
nayo haikunyesha juu ya nchi kwa muda wa
miaka mitatu na miezi sita. 18Kisha akaomba
tena, mbingu zikatoa mvua nayo ardhi ikatoa
mazao yake.

19Ndugu zangu, ye yote miongoni mwenu
akipotoka na kuicha kweli, naye akarejezwa na
mtu mwingine, 20hamna budi kujua kwamba ye
yote amrejezaye mwenye dhambi kutoka katika
upotovu wake, ataiokoa roho ya huyo mwenye
dhambi kutoka katika mauti na kusitiri wingi wa
dhambi.

# 1Petro

### *Utangulizi*

Petro ni mmoja wa wale wanafunzi kumi na wawili wa Yesu ambaye aliyaandikia makanisa ya sehemu ya kaskazini ya Asia Ndogo waraka huu muda mfupi kabla ya kufa kwake. Petro anapotumia neno "Babeli" *(5:3)*, alikuwa akimaanisha Rumi, maadam hatuna ushahidi wo wote unaoonyesha kwamba alikuwa Babeli huko Eufrati. Ule ukweli kwamba Yohana Marko *(1Petro 5:14)* alikuwa huko Rumi pamoja na Paulo wakati kama huu unatoa uwezekano mkubwa zaidi kuwa mwandishi alikuwa Rumi wakati anauandika waraka huu.

Waraka huu unaonyesha kwamba waamini walikuwa wanakabiliwa na dhiki na mateso. Shabaha yake ilikuwa kuwafariji waamini waliokuwa wakiishi Asia, kwani ni katika kipindi hiki cha miaka ya sitini utawala wa Rumi chini ya Nero ulipobadili hali yake ya uvumilivu na kuanza mateso huko Rumi. Kutokana na mapokeo, Petro na Paulo waliuawa huko Rumi mnamo mwishoni mwa miaka hiyo ya sitini kwa sababu ya kukataa kuikana imani. Petro anaonyesha kwamba mateso ni sehemu ya maisha ya Kikristo na kwamba Mungu ameandaa thawabu zisizoharibika kwa wote wamwaminio. Kwa kuwa kuenea kwa mateso kutoka kwa serikali ya Rumi hayakuenea pote hadi mwishoni mwa karne ya kwanza chini ya utawala wa Domitia, inaonekana kwamba mateso ya waamini waliyokuwa wanapata ni kutoka kwenye mazingira yao ya kipagani. Kwa wale waliokuwa wanafikiria kurudia imani yao ya Kiyahudi ili kuepuka mateso, anawaambia kuwa sasa kanisa ndilo ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu ambao ni milki Yake Mungu *(2:9)*. Kwa hiyo mawazo ya kurejea imani ya Kiyahudi yalikuwa hayana faida yo yote. Kisha Petro anatoa mfano wa Kristo na jinsi alivyopata mateso na kuwakumbusha waamini kuwa wao pia hawana budi kupata mateso. Mwisho, Petro anatoa maagizo kwa vikundi mbalimbali vya wakristo.

### *Wazo Kuu*

Kiini kikuu cha waraka huu ni mateso, neno ambalo limetajwa mara kumi na sita na ushindi utakaopatikana baada ya mateso. Wakristo wa kwanza walipata mateso mengi. Wengi wao waliuawa kwa ajili ya imani yao. Lakini waraka huu unatuonyesha kwamba hata kama tutauawa kwa ajili ya imani, tushikilie imani yetu. Mungu anafahamu yote yanayotendeka na katika mpango Wake wa milele hatimaye mambo yote yatakamilika kwa utukufu Wake.Katika elimu kumhusu Kristo, mateso ya Kristo yamerudiwa mara kwa mara. Mwandishi anaonyesha tumaini la wakati wa mwisho kama kitu cha kumtia moyo mwamini katika mateso. Wakristo wanaoishi katika ulimwengu wenye uadui hawana budi kuteswa kama Kristo alivyo teswa na kuruhusu neema ya Mungu kukuzwa maishani mwao. Wajibu wetu ni kumtegemea Mungu sikuzote, tukitambua kwamba hapa duniani sisi ni wapitaji na wasafiri na yakwamba maskani yetu ni mbinguni.

### *Mwandishi*

Petro.

### *Tarehe*

Waraka huu uliandikwa kama 63 B.K.

### *Mahali*

Inaonekana Petro alikuwa Rumi wakati anaandika waraka huu.

### *Mgawanyo*

- Utukufu wa wokovu wa Kristo (1:1-25)
- Utii wa mkristo (2:1-10) Mfano wa mateso ya Kristo (2:11-25)
- Maisha yampasayo mkristo nyumbani kwake na hapa duniani (3:1-17)
- Mateso na mfano wa Kristo (3:18-4:19)
- Huduma ya kikristo na mawaidha ya mwisho (5:1-14)

### *Salamu*

**1** Petro, mtume wa Yesu Kristo,

Kwa wateule wa Mungu, wageni katika
ulimwengu, waliotawanyika kote katika Ponto,
Galatia, Kapadokia, Asia na Bithinia.
2Ninawaandikia ninyi ambao mlichaguliwa tangu
mwanzo na Mungu Baba kulingana na
alivyotangulia kuwajua, kwa kazi ya utakaso wa
Roho, katika utii na kunyunyizwa damu ya Yesu
Kristo:

Neema iwe nanyi na amani iongezwe
kwenu.

### *Tumaini Lenye Uzima*

3Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu
Yesu Kristo! Kwa rehema zake kuu ametufzaa
sisi mara ya pili katika tumaini lenye uzima kwa
kufufuka kwa Yesu Kristo kutoka kwa wafu 4ili
tuupate urithi usioharibika, usio na uchafu, ule
usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.
5Nanyi, mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia
ya imani hadi uje ule wokovu ulio tayari
kufunuliwa nyakati za mwisho. 6Katika hili
mnafurahi sana, ingawa sasa kwa kitambo
kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa
majaribu ya namna nyingi, 7ili kwamba uhalisi
wa imani yenu, yenye thamani kuliko dhahabu,
ingwa hupotea, yenyewe hujaribiwa kw moto, ili
ionekane kuwa katika sifa, heshima na utukufu,
Yesu Kristo atakapodhihirishwa. 8Ambaye
ingawa hamjamwona, mnampenda, tena ingawa
sasa hamumwoni, mnamwani na kujawa na
furaha isiyoneneka yenye utukufu usioelezeka.
9Maana mnaupokea wokovu wa roho zenu,
ambao ndio lengo la imani yenu.

10Kwa habari ya wokovu huu, wale manabii
walosema kuhusu neema ambayo ingewajia
ninyi, walitafuta kwa bidii na kwa uangalifu
mkubwa, 11wakijaribu kujua ni wakati upi na
katika mazingira gani ambayo ndani yao Roho
wa Kristo aliyokuwa akionyesha alipotabiri
kuhusu mateso ya Kristo na utukufu ule ambao
ungefuata. 12Mitume walidhihirishiwa kwamba
walikuwa hawajihudumii wao wenyewe, bali
walihudumu kwa ajili yenu katika mambo hayo
ambayo sasa yamehubiriwa kwenu na wale
waliowahubiri ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu
aliyetumwa kutoka mbinguni. Mambo ambayo
hata malaika wanatamani kuyafahamu.

### *Mwito Wa Kuishi Maisha Matakatifu*

13Kwa hiyo, vifungeni viuno vya nia zenu, mwe na
kiasi, mkitumainia kikamilifu ile neema mtakayopewa,
Yesu Kristo atakapodhihirishwa. 14Kama watoto
watiifu, msifuate tamaa zenu mbaya za kwanza za
wakati wa ujinga. 15Bali kama Yeye aliyewaita alivyo
mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika
mwenendo wenu wote, 16kwa maana imeandikwa:
“Mtakuwa watakatifu, kwa kuwa Mimi ni mtakatifu.”

17Nanyi kama mnamwita “Baba,” Yeye
ahukumuye kila mtu kulingana na matendo yake
pasipo upendeleo, enendeni kwa hofu ya kumcha
Mungu wakati wenu wa kukaa hapa duniani kama
wageni. 18Kwa maana mnafahamu kwamba
mlikombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa
ambao mliurithi kutoka kwa baba zenu, si kwa vitu
viharibikavyo, yaani, kwa fedha na dhahabu, 19bali
kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ile ya Mwana-
Kondoo asiye na dosari wala doa. 20Yeye aliwekewa
hayo kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu,
lakini akadhihirishwa katika siku hizi za mwisho kwa
ajili yenu, 21ambaye kwa Yeye mmemwamini Mungu
aliyemfufua kutoka kwa wafu akampa utukufu, ili imani
yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu.

22Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa
kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu
zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati
kutoka moyoni. 23Kwa maana mmezaliwa upya, si
kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika,
kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele.
24Maana,

“Mwili wote ni kama majani
na utukufu wote wa binadamu ni kama ua
la majani, kama ua la majani,
majani hunyauka na ua lake
hupukutika, 25 lakini neno la Mungu ladumu
milele.”

Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu.

### *Jiwe Lililo Hai Na Watu Waliochaguliwa*

**2** Kwa hiyo, wekeni mbali nanyi uovu wote na udanganyifu
wote, unafiki, wivu na masingizio ya kila namna. 2Kama
watoto wachanga, waliozaliwa
sasa, yatamanini maziwa ya kiroho yasiyoghoshiwa, ili
kwa hayo mpate kuukulia wokovu, 3ikiwa kweli
mmeonja ya kwamba Bwana ni mwema.

4Mwendeeni Yeye aliye Jiwe lililo hai, lililokataliwa
na wanadamu bali kwa Mungu ni teule na la thamani
Kwake. 5Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai,
mmejengwa kuwa nyumba ya Roho, mpate kuwa
ukuhani mtakatifu, mkitoa dhabihu za kiroho

zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. 6Kwa maana Maandiko yasema:

“Tazama, naweka katika Sayuni,
jiwe la pembeni, teule lenye thamani
na kila amwaminiye hataaibika.”

7Kwenu ninyi mnaoamini, Yeye ni wa thamani. Lakini kwao wasioamini,

“Jiwe lile walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni,”

8tena,

“Jiwe lenye kuwafanya watu wajikwae,
mwamba wa kuwafanya waanguke.”

Wanajikwaa kwa sababu hawakutii lile neno, kama walivyowekewa tangu zamani.

9Lakini ninyi ni taifa teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu la Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu. 10Mwanzo ninyi mlikuwa si taifa, lakini sasa ninyi ni taifa la Mungu. Mwanzo mlikuwa hamkupata rehema, lakini sansa mmepata rehema.

11Wapenzi, ninawasihi, mkiwa kama wageni na wapitaji hapa ulimwenguni, epukeni tamaa mbaya za mwili ambazo hupigana vita na roho zenu. 12Mwe na mwenendo mzuri mbele ya watu wasiomjua Mungu, ili kama wanawasema kuwa ninyi ni watenda mabaya, wayaone matenddo yenu mema wamtukuze Mungu siku atakapokuja kuhukumu.

### *Kuwatii Wenye Mamlaka*

13Tiini kila mamlaka iliyowekwa na wanadamu kwa ajili ya Bwana: Mfalme akiwa ndiye aliye na mamlaka ya juu zaidi, 14pamoja na maafisa aliowaweka.Kwa kuwa mfalme amewatuma ili kuwaadhibu wale wanaokosa na kuwasifu wale watendao mema. 15Kwa maana ni mapenzi ya Mungu kwamba kwa kutenda mema mnyamazishe maneno ya kijinga ya watu wapumbavu. 16Mkiishi kama watu huru, lakini msitumie uhuru wenu kama kisingizio cha kutenda uovu, bali ishini kama watumishi wa Mungu. 17Mheshimuni kila mtu. Wapendeni jamaa ya waaminio. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme.

### *Mfano Wa Mateso Ya Kristo*

18Ninyi watumwa, watiini mabwana zenu kwa heshima yote, si wale mabwana walio wema na wapole peke yao, bali pia wale walio wakali. 19Kwa maana ni jambo la sifa kama mtu akivumilia anapoteswa kwa uonevu kwa ajili ya kumkumbuka Mungu. 20Kwani ni faida gani kwa mtu kustahimili anapopigwa kwa sababu ya makosa yake? Lakini kama mkiteswa kwa sababu ya kutenda mema, nanyi mkastahimili, hili ni jambo la sifa mbele za Mungu. 21Kwa kuwa ninyi mliitwa kwa ajili ya hayo, kwa sababu Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake.

22“Yeye hakutenda dhambi,
wala udanganyifu haukuonekana kinywani mwake.

23Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano, alipoteswa, hakutishia, bali alijikabidhi kwa Yeye ahukumuye kwa haki. 24Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba,tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa. 25Kwa maana mlikuwa mmepotea kama kondoo, lakini sasa mmerudi kwa Mchungaji na Mlinzi wa roho zenu.

### *Mafundisho Kwa Wake Na Waume*

**3** Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu, ili kama wako wasioamini lile Neno, wapate kuvutwa na mwenendo wa wake zao pasipo neno, 2kwa kuuona utakatifu na uchaji wa Mungu katika maisha yenu.
3Kujipamba kwenu kusiwe kwa nje tu, kama vile kusuka nywele, kuvalia vitu vilivyofanyizwa kwa dhahabu na kwa mavazi. 4Badala yake kujipamba kwenu kuwe katika utu wenu wa ndani, kwa uzuri usioharibika, wa roho ya upole na utulivu, ambako ni kwa thamani sana machoni pa Mungu. 5 Kwa kuwa hivi ndivyo walivyokuwa wakijipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu. Wao walikuwa ni watiifu kwa waume zao, 6kama Sara alivyomtii mumewe Abrahamu, akamwita ‘bwana.’ Ninyi ni watoto wa Sara kama mkitenda yaliyo mema na bila kuogopa jambo lo lote.

7Vivyo hivyo ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili, nanyi wapeni heshima mkitambua ya kuwa wao ni wenzi walio dhaifu na kama warithi pamoja nanyi wa kipawa cha thamani cha uzima, ili kusiwepo na cho chote cha kuzuia maombi yenu.

### *Kuteseka Kwa Kutenda Mema*

8Hatimaye, ninyi nyote iweni na nia moja, wenye kuhurumiana, mkipendana kama ndugu, wasikitivu na wanyenyekevu. 9Msilipe ovu kwa ovu, au jeuri kwa jeuri, bali barikini, kwa maana hili ndilo mliloitiwa ili mpate kurithi baraka. 10Kwa maana,

“Ye yote apendaye uzima
na kuona siku njema,
basi auzuie ulimi wake usinene mabaya
na midomo yake isiseme hila.
11Mtu huyo lazima aache ubaya,
akatende mema,
atafute amani na kuifuatilia sana. 12Kwa
maana macho ya Bwana huwaelekea
wenye haki,
na masikio yake husikiliza maombi yao,
bali uso wa Bwana ni dhidi yao watendao
maovu.”

### *Kuvumilia Mateso*

13Basi, ni nani atakayewadhuru mkiwa wenye bidii katika kutenda mema? 14Lakini mmebarikiwa nata kama ikiwalazimu kuteseka kwa ajili ya haki. Msiogope vitisho vyao wala msiwe na wasiwasi, 15bali mtakaseni Kristo kuwa Bwana mioyoni mwenu. Sikuzote mwe tayari kumjibu mtu ye yote atakayewauliza kuhusu tumaini lililomo ndani yenu. Lakini fanyeni hivyo kwa upole na kwa heshima. 16Mkizitunza dhamiri zenu ziwe safi, ili wale wasemao mabaya dhidi ya mwenendo wenu mzuri katika Kristo, waaibike wa ajili ya masingizio yao. 17Kwa maana ni afadhali kupata mateso kwa ajili ya kutenda mema kama kuteseka huko ndiyo mapenzi ya Mungu, kuliko kuteseka kwa kutenda maovu. 18Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja tu, mwenye haki kwa ajili ya wasio na haki, ili awalete ninyi kwa Mungu. Mwili wake ukauawa, lakini akafanywa hai katika Roho, 19 ambayo kwa hiyo alikwenda na kuzihubiria roho zilizokuwa kifungoni. 20 Roho hizo ambazo zamani hazikutii, wakati ule uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja katika siku za Noa, wakati wa kujenga safina, ambako watu wachache tu, yaani, watu wanane waliokolewa wasiangamie kwa gharika. 21 Nayo maji hayo ni kielelezo cha ubatizo ambao sasa unawaokoa ninyi pia, si kwa kuondoa uchafu kwenye mwili, bali kama ahadi ya dhamiri safi kwa Mungu, kwa njia ya ufufuo wa Yesu Kristo, 22ambaye ameingia mbinguni na amekaa mkono wa kuume wa Mungu pamoja na malaika, mamlaka na nguvu zote vikiwa vimetiishwa chini yake.

### *Kuishi Kwa Ajili Ya Mungu*

**4** Kwa hiyo, kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili Wake, ninyi nanyi jivikeni nia iyo hiyo kwa maana mtu aliyekwisha kuteswa katiaka mwili ameachana na dhambi. 2Matokeo yake, maisha yake yaliyobaki ya kuishi hapa duniani, haishi tena kwa kufuata tamaa mbaya za wanadamu, bali anaishi kwa kufuata mapenzi ya Mungu. 3Maana wakati uliopita mmekwisha kutumia muda wa kutosha katika maisha yenu mkifanya yale ambayo watu wasiomjua Mungu hupenda kutenda, wakiishi katika uasherati, tamaa mbaya, ulevi, karamu a ulafi, za ulevi na ngoma mbaya na ibada za sanamu ambazo ni chukizo. 4Wao huona kuwa ni ajabu ninyi kutokujiingiza tena pamoja nao katika huo wingi wa ufisadi, nao huwatukana ninyi. 5Lakini itawapasa wao kutoa hesabu mbele Zake Yeye aliye tayari kuwahukumu walio hai na waliokufa. 6Kwa kuwa hii ndiyo sababu Injili ilihubiriwa hata kwa wale waliokufa, ili kwamba wahukumiwe sawasawa na wanadamu wengine katika mwili, lakini katika roho waishi sawasawa na Mungu aishivyo.

### *Kuja Kwa Kristo Kumekaribia*

7Mwisho wa mambo yote umekaribia. Kwa hiyo iweni na akili pia mwe na kiasi mkikesha katika kuomba.8Zaidi ya yote, dumuni katika upendo kwa maana upendo husitiri wingi wa dhambi. 9Iweni wakarimu kila mtu na mwenzake pasipo manung’uniko. 10Kila mmoja na atumie kipawa cho chote alichopewa kuwahudumia wengine, kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za Mungu. 11Ye yote asemaye hana budi kusema kama mtu asemaye maneno ya Mungu mwenyewe. Ye yote ahudumuye maneno hana budi kuhudumu kwa nguvu zile apewazo na Mungu, ili Mungu apate kutukuzwa katika mambo yote kwa njia ya Yesu Kristo. Utukufu na uweza una Yeye milele na milele. Amen.

### *Kuteseka Kwa Kuwa Ni Mkristo*

12Wapenzi, msione ajabu katika yale mateso yanayotukia miongoni mwenu, kana kwamba ni kitu kigeni kinachowapata. 13Bali furahini kuwa mnashiriki katika mateso ya Kristo, ili kwamba mpate kufurahi zaidi na kushangilia wakati utukufu wake utakapofunuliwa. 14Kama mkilaumiwa kwa ajili ya Jina la Kristo, mmebarikiwa, kwa sababu Roho wa utukufu, yaani, Roho wa utukufu, ambaye ndiye Roho wa Mungu, anakaa juu yenu. 15Lakini asiwepo mtu ye yote miongoni mwenu anayeteswa kwa kuwa ni mwuaji, au mwivi, au mhalifu au anayejishughulisha

na mambo ya watu wengine, ili kuwagombanisha. 16Lakini kama mtu ye yote akiteseka kwa kuwa ni Mkristo, asihesabu jambo hilo kuwa ni aibu, bali amtukuze Mungu kwa sababu ameitwa kwa Jina hilo. 17Kwa maana wakati umewadia wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu. Basi kama ikianza kwetu sisi, mwisho wa hao wasiotii Injili ya Mungu utakuwaje? 18Basi,

"Ikiwa ni vigumu kwa mwenye haki kuokoka,
itakuwaje kwa mtu asiyemcha Mungu
na mwenye dhambi?"

19Kwa hiyo, wale wanaoteswa sawasawa na mapenzi ya Mungu, wajikabidhi kwa Mwumba wao aliye mwaminifu huku wakizidi kutenda mema.

### *Kulichunga Kundi La Mungu*

**5** Kwa wazee waliomo miongoni mwenu, nawasihi mimi nikiwa mzee mwenzenu, shahidi wa mateso ya Kristo na mshiriki katika utukufu utakaofunuliwa, 2lichungeni kundi la Mungu mlilokabidhiwa, mkitumika kama waangalizi, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari, kama Mungu anavyowataka mwe, si kwa tamaa ya fedha, bali mlio na bidii katika kutumika. 3Msijifanye mabwana juu ya wale walio chini ya uangalizi wenu, bali iweni vielelezo kwa hilo kundi. 4Naye Mchungaji Mkuu atakapodhihirishwa mtapokea taji ya utukufu isiyoharibika.

5Vivyo hivyo ninyi mlio vijana hamna budi kuwatii wazee. Nanyi nyote imewapasa kujivika unyenyekevu katika kuhudumiana, kila mtu na mwenzake, kwa kuwa,

"Mungu huwapinga wenye kiburi
bali huwapa wanyenyekevu neema."

6Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati Wake. 7Mtwikeni Yeye fadhaa zenu zote kwa maana hujishughulisha sana na mambo yenu.

8 Mwe na kiasi na kukesha, maana adui yenu Ibilisi, kama simba angurumaye huzungukazunguka akitafuta mtu ili apate kummeza. 9Mpingeni huyo mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kwamba mateso yayo hayo yanawapata ndugu zenu pote duniani.

10Nanyi mkiisha kuteswa kwa kitambo kidogo, Mungu wa neema yote aliyewaita kuingia katika utukufu Wake wa milele ndani ya Kristo, Yeye mwenyewe atawatengeneza upya, atawasaidia, atawatia nguvu na kuwathibitisha. 11Uweza una Yeye milele na milele. Amen.

### *Salamu Za Mwisho*

12Kwa msaada wa Silvano, yeye ambaye ninamhesabu kuwa ndugu mwaminifu, nimewaandikia waraka huu mfupi ili kuwatia moyo na kushuhudia kwamba hii ni neema halisi ya Mungu. Simameni imara katika neema hiyo.

13 Kanisa lililoko Babeli, lililochaguliwa pamoja nanyi wanawasalimu, vivyo hivyo mwanangu Marko anawasalimu. 14Salimianeni kwa busu la upendo.

Amani iwe nanyi nyote mlio katika Kristo. Amen.

## 2Petro

### *Utangulizi*

Barua hii iliandikwa muda mfupi tu kabla ya kifo cha Petro na inagusia matatizo ambayo aliona yangebaki baada ya kifo chake. Anawahimiza waamini waendelee kukua kiroho wakiitambua kweli iliyomo katika Injili ya Kristo. Kweli hii haitokani na hadithi za kale bali inatokana na mambo yaliyoonekana kwa macho. Anawaonya kuhusu walimu wa uongo ambao wangetukuza mawazo yao wenyewe badala ya mafundisho ya kweli ya Neno la Mungu. Hatimaye anakumbusha kwamba Kristo atakuja siku moja kuangamiza hali ya asili ya ulimwengu huu na kwa sababu hii hatuna sababu ya kuung'ang'ania sana.

### *Wazo Kuu*

Waraka wa Pili wa Petro unakaza juu ya umuhimu wa kusimama imara wakati ambapo kuna mafundisho mengi ya kupotosha. Kiini kikuu cha waraka huu ni "maarifa", yaani, kupata ujuzi na "kujua", neno ambalo limetajwa mara kumi na sita. Hatari inayowakabili hawa wasomaji sasa haikuwa mateso kama ilivyokuwa wakati waraka wa kwanza ulipoandikwa, bali upotovu kuhusu tumaini la mambo ya mwisho, uliokuwa ukitangazwa na walimu wa uongo na watenda maovu waliokuwa wamejiingiza ndani ya kanisa. Watu wa dunia wanajitahidi kuiharibu kazi ya Mungu lakini sisi tunaoamini hatuna budi kuepuka majaribu yote, tuishi maisha ya kumcha Mungu, tuamini la kweli, tuvumilie mateso, tumwamini Mungu na kungojea kurudi Kwake Kristo.

### *Mwandishi*

Yale maneno ya ufunguzi yenyewe yanamtambulisha kuwa mwandishi wa waraka huu ni "Simoni Petro, mtumishi na mtume wa Yesu Kristo." Maadam kuna ushahidi kutoka nje ya kanisa la kwanza kuuhesabia waraka huu kuwa umeandikwa na Mtume Petro, wasomi wengine wametia shaka uhalisi wa uandishi kuwa wa Petro kwa msingi kwamba ile tofauti ya mtindo wa uandishi wa nyaraka hizi mbili, kutajwa kwa Paulo *(3:15–16)* na ule mfafanuo kati ya *2Petro* na Yuda.

Lakini, hata hivyo, kuna ushahidi wa ndani unaoashiria kuwa Petro ndiye mwandishi. Kule kutambulisha mwandishi kama "Simoni Petro" kunaelekea kuwa halisi kwa kuwa kama angekuwa ni mtu anyejifanya angetumia "Petro" ili aweze kufuata mtriririko wa waraka wa kwanza.Ule uandishi wa kibinafsi na msamiati unalinganishwa na maisha na mahubiri ya Petro.Ile jinsi ya kusema na yale mawazo yaliyomo vina mfanano mkubwa kati ya hizi nyaraka mbili zinazohesabiwa kuwa za Petro.

### *Tarehe*

Waraka huu uliandikwa kati ya 65 na 68 B.K., muda mfupi tu kabla ya kifo cha Petro, nao unaandikiwa wasomaji wale wale ambao Petro alikuwa akiwatia moyo katika waraka wa kwanza.

### *Mahali*

Uwezekano mkubwa ni kwamba waraka huu mwandishi alikuwa Rumi wakati wa kuuandika.

### *Mgawanyo*

- Namna ya kukua kiroho (1:1-21)
- Maonyo kuhusu walimu wa uongo (2:1-22)
- Maagizo juu ya kuja kwake Kristo mara ya pili (3:1-18).

### *Salamu*

**1** Simoni Petro mtumishi na mtume wa Yesu Kristo,

Kwa wale ambao kwa njia ya haki ya Mungu wetu na Yesu Kristo mmepokea imani iliyo na thamani kama yetu:

[2]neema na amani iwe kwenu kwa wingi katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu.

### *Wito Wa Mkristo Na Uteule*

[3]Uweza Wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake mwenyewe.
[4]Kwa sababu hiyo, ametukirimia ahadi Zake kuu na za thamani kupitia mambo haya, ili kwa kupitia hayo mpate kuokoka na upotovu ulioko duniani kwa sababu ya tamaa mbaya.

[5] Kwa sababu hii, jitahidini sana katika imani yenu kuongeza wema na katika wema wenu
maarifa, [6]katika maarifa yenu kiasi; katika kiasi,
saburi, katika saburi yenu, utauwa, [7]katika utauwa wenu upendano wa kidugu, katika
upendano wa kidugu, upendo. [8]Kwa maana haya yakiwa kwenu kwa wingi, nayo yakizidi kuongezeka yanawafanya kuwa wenye bidii na wenye kuzaa matunda katika kumjua Bwana
wetu Yesu Kristo. [9] Kwa kuwa mtu asiyekuwa na mambo haya haoni mbali, pia ni kipofu, naye amesahau kule kutakaswa kwa dhambi zake za zamani.

[10]Kwa hiyo, ndugu zangu, fanyeni bidii zaidi kuuthibitisha wito wenu na uteule wenu, kwa maana mkifanya hivyo, hamtajikwaa kamwe.
[11]Kwa njia hii, mtajaliwa kwa ukarimu mwingi kuingia katika Ufalme wa milele wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.

### *Unabii Wa Maandiko*

[12]Hivyo nitawakumbusha mambo haya sikuzote, hata ingawa mnayajua na yamethibitishwa katika kweli mliyo nayo.
[13]Naona ni vema kuwaamsha kwa kuwakumbusha mambo haya wakati wote niwapo katika hema hili ambalo ni mwili wangu.
[14]Kwa sababu najua ya kwamba karibuni nitaliweka kando, kama vile Bwana wetu Yesu
Kristo alivyoliweka wazi kwangu. [15]Nami nitafanya kila juhudi kuona kwamba baada ya kuondoka kwangu mtaweza kuyakumbuka mambo haya sikuzote.

[16]Tulipowafundisha juu ya uweza na kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo, hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, bali tulishuhudia kwa macho yetu utukufu wake.
[17]Maana alipewa heshima na utukufu kutoka kwa Mungu Baba sauti ilipomjia katika Utukufu Mkuu ikisema, ‘‘Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa naye",
[18]Sisi wenyewe tuliisikia sauti hii ambayo ilitoka mbinguni, wakati tulipokuwa pamoja Naye kwenye ule mlima mtakatifu.

[19]Nasi tunalo pia neno la hakika zaidi la unabii, ambalo mtafanya vema mkiliangalia kwa bidii, kama vile nuru inayong’aa gizani, hadi kupambazuka na nyota ya asubuhi itokee
mioyoni mwenu. [20]Awali ya yote, yawapasa mjue kwamba hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa kama apendavyo mtu mwenyewe.
[21]Kwa maana unabii haukuja kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali watu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

### Manabii Wa Uongo Na Adhabu Yao

**2** Lakini pia waliinuka manabii wa uongo miongoni mwa watu, kama vile watakavyokuwako walimu wa uongo miongoni mwenu, ambao kwa siri, wataingiza mafundisho yasiyopatana na kweli hata kumkana Bwana wa pekee aliyewanunua na kujiletea juu yao
maangamizi ya haraka. [2]Hata hivyo, wengi watafuata njia zao za ufisadi ambao kwa ajili
yao njia ya kweli itatukanwa. [3]Nao katika tamaa yao watajipatia faida kwenu kwa maneno ya madanganyo waliyotunga wenyewe. Lakini hukumu imekwisha kutangazwa dhidi yao tangu zamani, ambayo haikawii wala ungamivu wao haujalala usingizi.

[4]Kwa maana kama Mungu hakuwasamehe malaika walipotenda dhambi, bali aliwatupa
kuzimu [a], katika vifungo vya giza wakae humo
mpaka ije hukumu, [5]kama hakuusamehe ulimwengu wa kale alipoleta gharika juu ya watu wale wasiomcha Mungu, akamhifadhi Noa, mhubiri wa haki, pamoja na watu wengine saba,
[6]kama aliihukumu miji ya Sodoma na Gomora kwa kuiteketeza kwa moto ikawa majivu na kuifanya kuwa kielelezo kwa wote ambao

---

a[4] “Kuzimu” linatokana na neno la Kiyunani “Tartarus” ambalo maana yake “chini sana, mahali pa mateso kwa watu waliopotea”

hawatamcha Mungu 7na kama alimwokoa Loti,
mtu mwenye haki, ambaye alihuzunishwa na
maisha machafu ya watu wapotovu 8(kwa
sababu yale matendo mapotovu aliyoyaona na
kuyasikia huyo mtu mwenye haki alipoishi
miongoni mwao yalimhuzunisha siku baada ya
siku), 9 ikiwa hivyo ndivyo, basi Bwana anajua
jinsi ya kuwaokoa wacha Mungu kutoka katika
majaribu na kuwaweka waasi katika adhabu
hadi siku ya hukumu. 10Hii ni hakika hasa kwa
wale wanaofuata tamaa mbaya za mwili na
kudharau mamlaka.

Kwa ushupavu na kwa kiburi watu hawa
hawaogopi kunena mabaya dhidi ya viumbe vya
mbinguni, 11lakini hata malaika, ingawa wana
nguvu na uwezo zaidi, hawaleti mashtaka dhidi
ya viumbe kama hao mbele za Bwana. 12Lakini
watu hawa hukufuru katika mambo
wasiyoyafahamu. Wao ni kama wanyama wasio
na akili, viumbe wanaotawaliwa na hisia za
mwili, waliozaliwa ili wakamatwe na kuchinjwa.
Wao husingizia wasiyoyafahamu na wanyama
hao watakapoangamizwa, hawa nao
wataangamizwa pia.

13Watalipwa madhara kwa ajili ya madhara
waliyowatendea wengine. Huhesabu kuwa ni
anasa kufanya karamu za ulevi na ulafi wakati
wa mchana. Wao ni mawaa na dosari katika
karamu zenu wakijifurahisha kwa ulevi na ulafi
katika anasa zao wanaposhiriki katika karamu
zenu. 14Wakiwa na macho yaliyojaa uzinzi,
hawaachi kutenda dhambi. Huwashawishi wale
wasio imara, wao ni hodari kwa kutamani, wana
wa laana! 15Wameiacha njia iliyonyoka,
wakapotoka na kuifuata njia ya Balaamu mwana
wa Beori aliyependa mshahara wa uovu.
16Lakini Balaamu kwa ajili ya uovu wake,
alikemewa na punda, mnyama asiyejua
kusema, akaongea akitumia sauti ya
mwanadamu na kuzuia wazimu wa huyo nabii.

17Watu hawa ni chemchemi zisizo na maji
na ukungu upeperushwao na tufani, ambao giza
nene limewekwa tayari kwa ajili yao. 18Kwa
maana wao hunena maneno makuu mno ya
upumbavu na kwa tamaa mbaya za uasherati
huwashawishi watu ambao ndipo tu
wamejiondoa miongoni mwa wale wanaoishi
katika ufisadi. 19Huwaahidi uhuru hao
waliowanasa, wakati wao wenyewe ni watumwa
wa ufisadi. Kwa maana mtu ni mtumwa wa kitu
cho chote kinachomtawala. 20Kwa kuwa kama
wameukimbia upotovu wa dunia kwa kumjua
Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo, kisha
wakanaswa tena na kushindwa, hali yao ya
mwisho ni mbaya zaidi kuliko ile ya kwanza.
21Ingelikuwa afadhali kwao kama wasingelijua
kamwe njia ya haki, kuliko kuijua kisha
wakaiacha ile amri takatifu waliyokabidhiwa.
22Imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya
kweli isemayo, “Mbwa ameyarudia matapishi
yake mwenyewe,” tena nyingine yasema,
“Nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa
matopeni.”

### *Ahadi Ya Kuja Kwa Bwana*

3 Wapenzi, huu ndio waraka wa pili
ninaowaandikia. Katika nyaraka hizi mbili
ninajaribu kuziamsha nia zenu safi kwa
kuwakumbusha kwamba, 2nataka ninyi
mkumbuke maneno yaliyosemwa zamani na
manabii watakatifu na ile amri ya Bwana na
Mwokozi mliyopewa kwa kupitia kwa mitume
wenu.

3Kwanza kabisa ni lazima mfahamu ya
kwamba siku za mwisho watakuja watu wenye
dhihaka wakidhihaki na kuzifuata tamaa zao
mbaya. 4na kusema, “Iko wapi ile ahadi ya kuja
Kwake? Tangu baba zetu walipokufa, kila kitu
kinaendelea kama kilivyokuwa tangu mwanzo
wa kuumbwa.” 5Wao kwa makusudi hupuza
ukweli huu, ya kwamba kwa neno la Mungu
mbingu zilikuwepo tangu zamani nayo dunia
ilifanyizwa kutoka ndani ya maji na kwa hayo
maji, 6ulimwengu wa wakati ule uligharikishwa
na kuangamia. 7Lakini kwa neno lilo hilo mbingu
za sasa na dunia, zimewekwa akiba kwa ajili ya
moto, zikihifadhiwa hadi siku ile ya hukumu na
ya kuangamizwa kwa watu wasiomcha Mungu.

8Lakini wapenzi, msisahau neno hili,
kwamba kwa Bwana, siku moja ni kama miaka
elfu na miaka elfu ni kama siku moja. 9 Bwana
hakawii kuitimiza ahadi Yake kama watu
wengine wanavyodhani kukawia, bali Yeye
anawavumilia, maana hataki mtu ye yote
aangamie, bali kila mmoja afikilie toba.

10Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi.
Ndipo mbingu zitatoweka kwa kishindo kikuu na
vitu vya asili vitateketezwa kwa moto, nayo
dunia na kila kitu kilichomo ndani yake
kitaunguzwa.

11Kwa kuwa vitu vyote vitayeyuka hivyo,
ninyi je, imewapasa kuwa watu wa namna gani?
Inawapasa kuishi maisha matakatifu na ya
kumcha Mungu, 12 mkingojea na kuhimiza kuja
kwa hiyo siku ya Mungu, ambayo siku hiyo
mbingu zitachomwa moto na kutoweka na vitu

vya asili vitayeyuka kwa moto. 13Lakini
kufuatana na ahadi Yake, sisi tunatazamia kwa
furaha mbingu mpya na dunia mpya, ambayo
haki hukaa ndani yake.

14Kwa sababu hii, wapenzi, kwa kuwa
mnatazamia kwa furaha mambo haya, fanyeni
bidii ili awakute katika amani, bila mawaa wala
dosari. 15Nanyi hesabuni uvumilivu wa Bwana
kuwa ni wokovu, kama vile ndugu yetu mpenzi
Paulo alivyowaandikia kwa hekima ile aliyopewa
na Mungu. 16Huandika vivyo hivyo katika
nyaraka zake zote akizungumzia ndani yake
mambo haya. Katika nyaraka zake kuna mambo
mengine ambayo ni vigumu kuyaelewa, ambayo
watu wajinga na wasio thabiti huyapotosha kwa
maangamizi yao wenyewe, kama wapotoshavyo
pia Maandiko mengine.

17Basi, ninyi wapenzi, kwa kuwa
mmekwisha kujua mambo haya, jilindeni msije
mkachukuliwa na kosa la watu hao waasi na
kuanguka kutoka kwenye uthabiti wenu. 18Bali
kueni katika neema na katika kumjua Bwana na
Mwokozi wetu Yesu Kristo. Utukufu una Yeye
sasa na milele! Amen.

## 1Yohana

### *Utangulizi*

Yale yaliyomo katika waraka huu, mfano uandishi wake na ile misamiati iliyotumika vinakubaliana na lile hitimisho kwamba nyaraka hizi ziliandikiwa wasomaji wale wale wa Injili ya Yohana. Waraka huu wa Kwanza unakuwa kama ufupisho unaowawazia wasomaji kwamba tayari wanaijua Injili ya Yohana na unawahakikishia juu ya imani yao katika Kristo. Waraka huu unaonyesha kuwa wasomaji walikuwa wanakabiliwa na upotovu wa imani ya Unostiki, ambao ulikuja kuwa tatizo kubwa zaidi katika karne ya pili. Unostiki ulikuwa na mafundisho yasemayo kwamba vitu vyote ni viovu lakini roho tu ndiyo nzuri.

### *Wazo Kuu*

Katika ujumbe wa Injili, Yohana anaonyesha wazi kuwa Yesu ni Mungu aliyefanyika mwili na hivyo kupinga kabisa ile dhana kwamba Kristo aliwaziwa tu kama aliyekuwa na mwili, eti kwamba Yeye alikuwa roho. Pia iliondolea mbali yale mafundisho yaliyomwelezea Yesu kama vitu viwili, kwamba wakati fulani alikuwa anafanyika mwanadamu na wakati mwingine anakuwa Mungu.

### *Mwandishi*

Waraka wa Kwanza, wa Pili na wa Tatu wa Yohana tangu mwanzo kabisa zimeonekana kuwa mwandishi ni mtume Yohana ambaye pia ndiye mwandishi wa Injili ya Yohana ,yaani, mojawapo ya zile Injili nne. Huyu ndiye yule mwanafunzi aliyekuwa anapendwa ambaye aliegama kifuani mwa Yesu wakati wa chakula cha mwisho na wanafunzi Wake.

### *Tarehe*

Vitabu vyote hivi vinne, yawezekana vimeandikwa wakati mmoja, huenda kati ya *85-96 BK.*

### *Mgawanyo*

- Utangulizi (1:1-4)
- Umuhimu wa nuru katika ushirika (1:5-2:29)
- Upendo sharti uenee katika maisha (3:1-4:21)
- Imani na kuona kwa hakika (5:1-21)

***Neno La Uzima***

**1** Tunawajulisha lile lilokuwako tangu mwanzo,
lile tulilosikia,ambalo tumeliona kwa macho yetu,
ambalo tumelitazama na
kuligusa kwa mikono yetu, kuhusu Neno la
Uzima, [2]Uzima huo ulidhihirishwa, nasi
tumeuona na kuushuhudia, nasi
twawatangazieni uzima wa milele, ambao
ulikuwa pamoja na Baba, nao ukadhihirishwa
kwetu. [3]Twawatangazia lile tulililoliona na
kulisikia ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi
na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na
Mwanawe Yesu Kristo. [4]Tunaandika mambo
haya ili furaha yetu ipate kuwa timilifu.

***Kutembea Nuruni***

[5]Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka Kwake
na kuwatangazia ninyi, kwamba Mungi ni nuru
na ndani yake hamna giza lo lote. [6]Kama
tukisema kwamba twashirikiana naye huku
tukienda gizani, wasema uongo,wala hatutendi
lililo kweli. [7]Lakini tikienenda nuruni, kama Yeye
alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na
damu yake Yesu, Mwana Wake yatusafisha
dhambi yote.

[8]Kama tukisema kwamba hatuna dhambi,
twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani
yetu. [9]Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni
mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi
zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote.
[10]Kama tukisema hatukutenda dhambi,
twamfanya Yeye kuwa mwongo na Neno Lake
halimo ndani yetu.

***Kristo Mwombezi Wetu***

**2** Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya
ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote
akitenda dhambi, tunaye Mwombezi
kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki. [2]Yeye
ndiye dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi
zetu, wala si kwa ajili ya dhambi zetu tu, bali pia
kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote.

[3]Basi katika hili twajua ya kuwa tumemjua
kama tunazishika amri Zake. [4]Mtu ye yote
asemaye kuwa, "Ninamjua" lakini hazishiki amri
Zake, ni mwongo, wala ndani ya mtu huyo
hamna kweli. [5]Lakini kama mtu ye yote analitii
Neno Lake, upendo wa Mungu umekamilika
ndani yake kweli kweli .Katika hili twajua kuwa
tumo ndani yake. [6]Ye yote anayesema anakaa
ndani Yake hana budi kuenenda kama Yesu
alivyoenenda.

***Amri Mpya***

[7]Wapenzi, siwaandikii ninyi amri mpya bali
ile ya zamani, ambayo mmekuwa nayo tangu
mwanzo. Amri hii ya zamani ni lile neno
mlilosikia. [8]Lakini ninawaandikia amri mpya,
yaani, lile neno lililo kweli ndani yake na ndani
yenu, kwa sababu giza linapita na ile nuru ya
kweli tayari inang'aa.

[9]Ye yote anayesema yumo nuruni lakini
anamchukia ndugu yake bado yuko gizani.
[10]Yeye ampendaye ndugu yake anakaa nuruni,
wala hakuna kitu cho chote ndani yake cha
kumkwaza. [11]Lakini ye yote amchukiaye ndugu
yake yuko gizani na anaenenda gizani, wala
hajui anakokwenda, kwa sababu giza
limempofusha macho.

[12]Nawaandikia ninyi, watoto wadogo,
kwa sababu dhambi zenu zimesamehewa
kwa ajili ya Jina Lake.
[13]Nawaandikika ninyi, akina baba,
kwa sababu mmemjua Yeye aliye tangu
mwanzo.
Nawaandikia ninyi vijana
kwa sababu mmemshinda yule
mwovu. Nawaandikia ninyi watoto wadogo,
kwa sababu mmejua Baba.
[14]Nawaandikia ninyi akina baba,
kwa sababu mmejua Yeye aliye
tangu mwanzo.
Nawaandikia ninyi, vijana,
kwa sababu mna nguvu na neno
la Mungu linakaa ndani yenu,
nanyi mmeshinda yule mwovu.

***Msiupende Ulimwengu***

[15]Msiupende ulimwengu wala mambo
yaliyoko ulimwenguni. Kama mtu ye yote
akiupenda ulimwengu, kumpenda Baba hakumo
ndani yake. [16]Kwa maana kila kitu kilichomo
ulimwenguni, yaani, tamaa ya mwili, tamaa ya
macho na kiburi cha uzima, havitokani na Baba
bali hutokana na ulimwengu. [17]Nao ulimwengu
unapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye
afanyaye mapenzi ya Mungu adumu milele.

***Onyo Dhidi Ya Mpinga Kristo.***

[18]Watoto wadogo, huu ni wakati wa
mwisho! Kama mlivyosikia kwamba mpinga
Kristo anakuja, hivyo basi wapinga Kristo wengi
wamekwisha kuja. Kutokana na hili twajua
kwamba huu ni wakati wa mwisho. [19]Walitoka

kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu hasa. Kwa maana kama wangelikuwa wa kwetu, wangelikaa pamoja nasi, lakini kutoka kwao kulionyesha kwamba hakuna hata mmoja wao aliyekuwa wa kwetu.

[20]Lakini ninyi mmetiwa mafuta na Yeye Aliye Mtakatifu, nanyi nyote mnaijua kweli. [21]Siwaandikii kwa sababu hamjui kweli, bali kwa sababu mnaijua, nanyi mnajua hakuna uongo utokao katika kweli. [22]Je, mwongo ni nani? Mwongo ni mtu yule asemaye kwamba Yesu si Kristo. Mtu wa namna hiyo ndiye mpinga Kristo, yaani, yeye humkana Baba na Mwana. [23]Hakuna ye yote amkanaye Mwana aliye na Baba. Ye yote anayemkubali Mwana anaye na Baba pia.

[24]Hakikisheni kwamba lile mlilosikia tangu mwanzo linakaa ndani yenu. Kama lile mlilosikia tangu mwanzo linakaa ndani yenu, ninyi ninyi mtakaa ndani ya Mwana na ndani ya Baba. [25]Hii ndiyo ahadi yake kwetu, yaani, uzima wa milele.

[26]Ninawaandikia mambo haya kuhusu wale watu ambao wanajaribu kuwapotosha. [27]Kwa habari yenu ninyi, upako ule mlioupata kutoka Kwake unakaa ndani yenu, wala ninyi hamna haja ya mtu ye yote kuwafundisha. Lakini kama vile upako Wake unavyowafundisha kuhusu mambo yote nayo ni kweli wala si uongo, basi kama ulivyowafundisha kaeni ndani Yake.

### *Watoto Wa Mungu*

[28]Sasa basi, watoto wadogo, kaeni ndani Yake, ili atakapofunuliwa, tuwe na ujasiri, wala tusiaibike mbele zake wakati wa kuja kwake. [29]Kama mkijua kuwa Yeye ni mwenye haki, mwajua kwamba kila atendaye haki amezaliwa na Yeye.

**3** Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu! Nasi ndivyo tulivyo. Sababu kwa nini ulimwengu haututambui, ni kwa kuwa haukumtambua Yeye. [2]Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. [3]Kila mmoja mwenye matumaini haya katika Yeye hujitakasa, kama vile Yeye alivyo mtakatifu.

[4]Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. [5]Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala ndani Yake hamna dhambi. [6]Kila mtu akaaye ndani yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi hakumwona Yeye wala hakumtambua.

[7]Watoto wadogo, mtu ye yote na asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki. [8]Yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi. [9]Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu. [10]Kwa jinsi hii tunaweza kujua dhahiri watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi nao. Ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake.

### *Mpendane Ninyi Kwa Ninyi.*

[11]Hili ndilo neno mlilolisikia tangu mwanzo, kwamba imetupasa tupendane sisi kwa sisi. [12]Msiwe kama Kaini aliyekuwa wa yule mwovu akamwua ndugu yake. Basi kwa nini alimwua? Ni kwa sababu matendo yake Kaini yalikuwa mabaya na ya ndugu yake yalikuwa ya haki. [13]Ndugu zangu, ninyi msistaajabu kama ulimwengu ukiwachukia. [14]Sisi tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda ndugu. Kila asiyempenda ndugu yake akaa mautini. [15]Ye yote amchukiaye ndugu yake ni mwuaji, nanyi mwajua ya kwamba mwuaji hana uzima wa milele ndani yake.

[16]Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu, kwa sababu Yesu Kristo aliutoa uhai Wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu. [17]Ikiwa mtu anavyo vitu vya ulimwengu huu na akamwona ndugu yake ni mhitaji lakini asimhurumie, upendo wa Mungu wakaaje ndani ya mtu huyo? [18]Watoto wangu wadogo, tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali kwa tendo na katika kweli. [19]Basi hivi ndivyo tutakavyoweza kujua ya kuwa sisi tu wa kweli na hivyo twaithibitisha mioyo yetu mbele za Mungu [20]kila mara mioyo yetu inapotuhukumu. Kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu, naye anajua kila kitu.

[21] Wapenzi, kama mioyo yetu haituhukumu, tunao ujasiri mbele za Mungu. [22]Lo lote tuombalo, twalipokea kutoka Kwake, kwa sababu tumezitii amri Zake na kutenda yale yanayompendeza. [23] Hii ndiyo amri Yake, kwamba tuliamini Jina la Mwanawe, Yesu Kristo na kupendana sisi kwa sisi kama Yeye

alivyotuamuru. 24Wale wote wanaozishika amri
Zake hukaa ndani Yake na Yeye ndani yao. Hivi
ndivyo tunavyojua kwamba anakaa ndani yetu.
Nasi twajua hili kwa njia ya Roho yule
aliyetupatia.

### *Zijaribuni Hizo Roho*

Wapenzi, msiamini kila roho,bali zijaribuni
4 hizo roho mwone kama zimetoka kwa
Mungu, kwa sababu manabii wengi wa uongo
wametokea ulimwenguni. 2Hivi ndivyo
mnavyoweza kutambua Roho wa Mungu: Kila
roho inayokubali kwamba Yesu Kristo amekuja
katika mwili yatoka kwa Mungu. 3Lakini kila roho
ambayo haimkubali Yesu haitoki kwa Mungu. Hii
ndiyo roho ya mpinga Kristo, ambayo mmesikia
kwamba inakuja na sasa tayari iko ulimwenguni.

4Watoto wadogo, ninyi mmetokana na
Mungu, nanyi mmewashinda kwa sababu Yeye
aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika
ulimwengu. 5Wao wanatokana na ulimwengu na
kwa hiyo hunena yaliyo ya ulimwengu, hivyo
ulimwengu huwasikia.6 Sisi twatokana na
Mungu na ye yote anayemjua Mungu
hutusikiliza, lakini asiyetokana na Mungu
hatusikilizi. Hivi ndivyo tunavyoweza kutambua
Roho wa Kweli na roho ya upotovu.

### *Mungu Ni Upendo*

7Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo
watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa
na Mungu naye anamjua Mungu.8Yeye
asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu
ni upendo. 9Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha
upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu
alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili
tupate uzima kwa Yeye. 10Huu ndio upendo, si
kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye
alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe
dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu.
11Wapenzi, kama Mungu alitupenda sisi hivi,
imetupasa na sisi kupendana. 12Hakuna mtu ye
yote aliyemwona Mungu wakati wo wote. Kama
tukipendana, Mungu anakaa ndani yetu na
upendo Wake umekamilika ndani yetu.

13Tunajua kwamba twakaa ndani Yake na
Yeye ndani yetu, kwa sababu ametupatia sisi
sehemu ya Roho Wake. 14Nasi tumeona na
kushuhudia kwamba Baba amemtuma
Mwanawe ili awe Mwokozi wa ulimwengu. 15Kila
akiriye kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu,
Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya
Mungu. 16Hivyo nasi twajua na kuutumainia
upendo wa Mungu alio nao kwa ajili yetu.
Mungu ni Upendo. Kila akaaye katika upendo
hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani
yake. 17Kwa njia hii, upendo hukamilishwa
miongoni mwetu ili tupate kuwa na ujasiri katika
siku ya hukumu, kwa sababu kama alivyo
ndivyo tulivyo sisi katika ulimwengu huu.
18Katika upendo hakuna hofu. Lakini upendo
ulio kamili huitupa nje hofu, kwa sababu hofu
inahusika na adhabu. Kila mwenye hofu
hakukamilika katika upendo. 19Twampenda
Yeye kwa sababu Yeye alitupenda kwanza.
20Ikiwa mtu atasema,"Nampenda Mungu", lakini
anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo. Kwa
maana kila mtu asiyempenda ndugu yake
ambaye amemwona, atampendaje Mungu
ambaye hajamwona? Naye ametupa amri hii:
Ye yote anayempenda Mungu lazima pia
ampende ndugu yake.

### *Imani Katika Mwana Wa Mungu Huushinda Ulimwengu*

5 Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye
Kristo amezaliwa na Mungu na ye yote
ampendaye Baba humpenda pia mtoto
aliyezaliwa naye. 2Hivi ndivyo tunavyojua
kwamba tunawapenda watoto wa Mungu, kwa
kumpenda Mungu na kuzitii amri Zake. 3Kwa
kuwa huu ndio upendo wa Mungu, kwamba
tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito. 4Kwa
maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda
ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako
ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu. 5Ni nani yule
aushindaye ulimwengu? Ni yule aaminiye
kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

### *Ushuhuda Kuhusu Mwana Wa Mungu*

6Huyu ndiye aliyekuja kwa maji na damu,
yaani, Yesu Kristo. Hakuja kwa maji peke yake,
bali kwa maji na damu. Naye Roho ndiye
ashuhudiaye, kwa sababu Roho ndiye kweli. 7Kwa
maana wako watatu washuhudiao mbinguni:Hao
ni Baba, Neno na Roho Mtakatifu, nao hawa
watatu ni wamoja. 8Pia wako mashahidi watatu
duniani, yaani, Roho, Maji na Damu, wote hawa
watatu wanakubaliana katilka umoja. 9Kama
tunaukubali ushuhuda wa wanadamu, basi
ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi, kwa kuwa huu
ndio ushuhuda wa Mungu kwamba
amemshuhudia Mwanawe. 10Kila mtu
amwaminiye Mwana wa Mungu anao ushuhuda
ndani mwake.Kila mtu asiyemwamini Mungu
amemfanya Yeye kuwa mwongo, kwa sababu

hakuamini ushuhuda Mungu alioutoa kuhusu
Mwanawe. 11Huu ndio ushuhuda kwamba,
Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo
uzima umo katika Mwanawe. 12Aliye naye
Mwana wa Mungu anao uzima,yeye asiye na
Mwana wa Mungu hana uzima.

### Maneno Ya Mwisho

13Nawaandikia mambo haya ninyi
mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu ili mpate
kujua ya kuwa mnao uzima wa milele. 14Huu
ndio ujasiri tulio nao ndani Yake, kama tukiomba
kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia.
15Nasi kama tunajua ya kuwa atusikia, lo lote
tuombalo, tunajua ya kwamba tumekwisha
kupata zile haja tulizomwomba.

16Kama mtu akimwona ndugu yake
anatenda dhambi isiyo ya mauti, inampasa
aombe, naye Mungu atampa uzima mtu
huyo,yaani, kwa wale ambao dhambi yao si ya
mauti. Iko dhambi ya mauti, sisemi kwamba
utaomba kwa ajili ya hiyo. 17Jambo lo lote lisilo
la haki ni dhambi, lakini iko dhambi isiyo ya
mauti.

18Tunajua ya kuwa yeye aliyezaliwa na
Mungu hatendi dhambi, bali aliyezaliwa na
Mungu hujilinda wala yule mwovu hawezi
kumdhuru. 19Sisi twajua kuwa tu watoto wa
Mungu na ya kwamba ulimwengu wote uko chini
ya utawala wa yule mwovu.20Nasi twajua ya
kwamba Mwana wa Mungu amekuja, naye
ametupa sisi akili ili tupate kumjua Yeye aliye
Kweli. Nasi tumo ndani Yake Yeye aliye Kweli,
yaani, ndani ya Yesu Kristo Mwanawe. Yeye
ndiye Mungu wa kweli na uzima wa milele.

21Watoto wadogo,jilindeni na sanamu.
Amen.

## 2Yohana

***Utangulizi***

Waraka wa pili wa Yohana umeandikwa kwa "Bibi mteule (Siria na watoto wake)", ambao unaweza kuwa unamhusu mtu binafsi na jamaa yake, au kuna uwezekano kabisa kwamba unalihusu kanisa. Msisitizo umewekwa katika umuhimu wa imani kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu katika umbo la mwanadamu na kwamba waamini wanaosoma inawapasa kudumu katika pendo la Mungu na kukataa mafundisho potofu ya imani.

Yohana pia aliandika kuwaonya ili waweze kutambua walimu wa uongo wanaosafiri huku na huko, wao wasije wakakawaunga mkono na kuwasaidia. Yaani mtu ye yote asije akachangia kwenye kueneza mafundisho ya uongo badala ya yale ya kweli.

***Wazo Kuu***

Mwenendo wa waamini na kuwaonya hao waamini dhidi ya wadanganyaji jinsi wanavyodanganya.

***Mwandishi***

Yohana, yule mwanafunzi mpenzi aliyeegama kifuani mwa Yesu wakati wa chakula cha mwisho na wanafunzi Wake.

***Tarehe***

*Waraka huu uliandikwa 90 B.K.*

***Mahali***

Efeso.

**Mgawanyo**

- Salamu (1:1 - 3)
- Ushauri na maonyo (1:4 - 11)
- Hitimisho (1:12 - 13)

### *Salamu*

1Mzee,

Kwa bibi mteule na watoto wake,
niwapendao katika kweli, wala si mimi tu, bali na
wale wote waijuao kweli, 2kwa sababu ya ile
kweli ikaayo ndani yetu na ambayo itaendelea
kukaa nasi milele.

3Neema, rehema na amani itokayo kwa
Mungu Baba na kwa Yesu Kristo, Mwanawe
Baba, itakuwa pamoja nasi katika kweli na
upendo.

### *Kweli Na Upendo*

4Imenipa furaha kuu kuona baadhi ya
watoto wako wanaenenda katika kweli, kama
vile Baba alivyotuagiza.5 Sasa, bibi mpendwa,
nakuomba, si kwamba ninakuandikia amri
mpya, bali ile tuliyokuwa nayo tangu mwanzo.
Sisi na tupendane kila mmoja na mwenzake.
6Hili ndilo pendo, kwamba tuenende sawasawa
na amri Zake. Hii ndiyo amri Yake kama vile
mlivyosikia tangu mwanzo, kwamba mwenende
katika upendo.

7Wadanganyifu wengi, wasiokubali kwamba
Yesu Kristo amekuja katika mwili, wametokea
ulimwenguni. Mtu wa namna hiyo ni
mdanganyifu na mpinga Kristo. 8Jiangalieni
msije mkapoteza kile mlichokitenda, bali mpate
kupewa thawabu kamilifu. 9Mtu ye yote
asiyedumu katika mafundisho ya Kristo, bali
akayaacha, yeye hana Mungu. Ye yote
anayedumu katika mafundisho ana Baba na
Mwana pia. 10Msimpokee mtu ye yote
anayewajia ambaye hawaletei mafundisho
haya, wala msimkaribishe nyumbani kwenu.
11Ye yote amkaribishaye mtu wa namna hiyo
anashiriki katika matendo maovu ya mtu huyo.

### *Salamu Za Mwisho*

12Ingawa ninayo mengi ya kuwaandikia,
lakini sitaki kutumia karatasi na wino. Badala
yake, nataraji kuja kwenu na kuongea nanyi ana
kwa ana, ili furaha yetu ipate kuwa timilifu.

13Watoto wa dada yako mteule
wanakusalimu. Amen.

## 3Yohana

***Utangulizi***

Waraka wa tatu wa Yohana anaandikiwa Gayo, ambaye yawezekana alikuwa na wajibu wa kichungaji au inawezekana alikuwa kiongozi muhimu katika kanisa. Anaelekezwa kuwasaidia na kuwahudumia wale wanaokuja kama wajumbe wa Mungu. Pia anapewa onyo kuhusu Deotrefe, juu ya tabia yake ya kukosa ushirikiano. Yohana anaeleza tarajio lake la kuja na kushughulikia tatizo hili yeye mwenyewe.

***Wazo Kuu***

Wajibu wa binafsi kuhusu watumishi wa kweli na wa uongo.

***Tarehe***

Waraka huu uliandikwa 90 B.K.

***Mahali***

Efeso.

***Mgawanyiko***

- Salamu (1:1- 4)
- Kutiwa moyo kwa Gayo (1: 5 – 8)
- Kukemewa kwa Deotrefe (1: 9 – 10)
- Kusifiwa kwa Demetrio (1: 11 – 12)
- Hitimisho (1:13 – 15)

**Salamu**

1Mzee,

Kwa Gayo mpenzi, nimpendaye katika kweli.

***Gayo Anasifiwa Kwa Ajili Ya Ukarimu Wake***

2Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo
yote na kuwa na afya yako kama vile roho yako
ifanikiwavyo. 3Ilinifurahisha sana baadhi ya
ndugu walipokuja na kutueleza juu ya uaminifu
wako katika kweli na jinsi unavyoendelea
kuenenda katika hiyo kweli. 4Sina furaha kubwa
kuliko hii, kusikia kwamba watoto wangu
wanaenenda katika kweli.

5Mpenzi, wewe ni mwaminifu kwa yale
unayowatendea ndugu, ingawa wao ni wageni
kwako. 6Wameshuhudia kuhusu upendo wako
mbele ya kanisa. Utafanya vema ukiwasafirisha
kama inavyostahili kwa Mungu. 7Ilikuwa ni kwa
ajili ya hilo Jina waliondoka, bila kukubali
kupokea msaada wo wote kutoka kwa watu
wasioamini. 8Kwa hiyo imetupasa sisi
kuonyesha ukarimu kwa watu kama hao ili
tuweze kutenda kazi pamoja kwa ajili ya kweli.

***Deotrefe Na Demetrio***

9Nililiandikia kanisa, lakini Deotrefe yeye
apendaye kujifanya wa kwanza, hakubali
mamlaka yetu. 10Hivyo kama nikija,
nitakumbuka matendo yake atendayo,
akitusingizia kwa maneno ya hila. Wala
hatosheki na hayo anayotusingizia,bali pia
hukataa kuwakaribisha ndugu na hata huwazuia
wale walio tayari kufanya hivyo na kuwafukuza
watoke kanisani.

11 Mpenzi, usiige lile lililo baya bali lile lililo
jema. Ye yote atendaye mema atoka kwa
Mungu, atendaye mabaya hakumwona Mungu.

***Salamu Za Mwisho***

12Kila mtu ameshuhudia mema kuhusu
Demetrio, vivyo hivyo hata na hiyo kweli
yenyewe. Sisi pia twashuhudia mema juu yake,
nanyi mwajua kwamba ushuhuda wetu ni kweli.

13Ninayo mambo mengi ya kukuandikia,
lakini sipendi kuandika kwa kalamu na wino.
14Badala yake, nataraji kukuona upesi, nasi
tutaongea pamoja ana kwa ana.

Amani iwe kwako. Rafiki zetu walioko hapa wanakusalimu. Wasalimu hao rafiki zetu walioko huko, kila mmoja kwa jina lake.

## Yuda

### *Utangulizi*

Mwandishi wa waraka huu ametambuliwa kuwa ni Yuda, ambaye alikuwa nduguye Yakobo. Yakobo aliyekuwa msimamizi wa baraza la Yerusalemu na ambaye ndiye mwandishi wa waraka wa Yakobo. Yeye alikuwa ndugu wa Yesu wa kuzaliwa na Maria *(Mk.6:3).* Mfanano wa yaliyomo na yale yaliyomo kwenye Waraka wa pili wa Petro yanaashiria kuwa Yuda alikuwa amehamasishwa na ujumbe wa Petro. Katika *(Yuda 1:3)* anaonyesha kuwa alikusudia kuandika kuhusu wokovu wao lakini sasa anabadili nasaha zake kuelekea kwenye mwelekeo wa kukemea mtazamo wa watu fulani wenye tabia mbaya waliokuwa wanazunguka miongoni mwao wakiwa wanapotosha neema ya Mungu.

### *Tarehe*

Tarehe ya kuandikwa kwa waraka huu inaweza ikawa kati ya mwaka 65 - 70 B.K., au kama miaka kumi baadaye. Kama waraka huu uliandikiwa Wakristo wa Kiyahudi huko Palestina, tarehe ya awali inakubalika zaidi.

### *Wazo Kuu*

Yuda anasisitiza umuhimu wa kuishindania imani. Upotovu, yaani, uzushi, ni lazima uonyeshwe wazi kwamba si kweli. Anaonya kwamba hukumu ya Mungu itakuja juu ya wale wanaopotoka katika imani kama vile ilivyokuja juu ya Kaini, Kora na Balaamu.

### *Mgawanyo*

- Utangulizi (1:1- 4)
- Maonyo dhidi ya uongo (1: 5 -16)
- Marudi na hitimisho (1:17- 25)

***Salamu***

1Yuda, mtumwa wa Yesu Kisto nduguye Yakobo,

Kwa wale walioitwa, wapendwa katika Mungu Baba na kuhifadhiwa salama
ndani ya Yesu Kristo:

2Rehema, amani na upendo viwe kwenu kwa wingi.

***Dhambi Na Hukumu Ya Watu Wasiomcha Mungu***

3Wapenzi, ingawa nilikuwa ninatamani sana kuwaandikia kuhusu wokovu ambao tunaushiriki sisi sote, niliona imenipasa kuwaandikia na kuwasihi kwamba mwishindanie imani
iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. 4Kwa
kuwa kuna watu waliojipenyeza kwa siri katikati yenu, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, waovu, wapotoshao neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi wakimkana Yeye aliye Bwana wetu wa pekee, Bwana Yesu Kristo.

## *Hukumu Kwa Walimu Wa Uongo*

5Ingawa mmekwisha kujua haya yote, nataka niwakumbushe kuwa Bwana akiisha kuwaokoa watu Wake kutoka Misri, baadaye
aliwaangamiza wale ambao hawakuamini. 6Nao
malaika ambao hawakulinda nafasi zao, lakini wakayaacha makao yaliyokuwa yao hasa, hawa amewaweka katika giza, wakiwa wamefungwa kwa minyororo ya milele kwa ajili ya hukumu
siku ile kuu. 7Vivyo hivyo, Sodoma na Gomora
na pia ile miji iliyokuwa kando-kando, ambayo kwa jinsi moja na hao, walijifurahisha kwa uasherati na kufuata tamaa za mwili zisizo za asili, waliwekwa wawe mfano kwa kuadhibiwa katika moto wa milele.

8Vivyo hivyo hawa waotao ndoto huutia mwili unajisi, hukataa kuwa chini ya mamlaka na
kunena mabaya juu ya wenye mamlaka. 9Lakini
hata Malaika Mkuu Mikaeli alipokuwa anashindana na ibilisi juu ya mwili wa Mose, hakuthubutu kumlaumu, bali alimwambia,
“Bwana na akukemee!” 10 Lakini watu hawa
hunena mabaya dhidi ya mambo wasiyoyafahamu na katika mambo yale wanayoyafahamu kwa hisia kama wanyama wasio na akili, hayo ndiyo hasa yanayowaharibu.

11Ole wao! Kwa kuwa wanaifuata njia ya Kaini, wamekimbilia faida katika kosa la Baalamu na kuangamia katika uasi wa Kora.

12Watu hawa ni dosari katika karamu zenu za upendo, wakila pamoja nanyi bila hofu, wakijilisha pasipo hofu. Wao ni mawingu yasiyokuwa na maji, yakichukuliwa na upepo, miti isiyo na matunda wakati wa mapuputiko ambayo hunyauka iliyokufa mara mbili na
kung’olewa kabisa. 13 Wao ni mawimbi makali
ya bahari, yakitoa povu la aibu yao wenyewe, ni nyota zipoteazo, ambao weusi wa giza ndio akiba yao waliowekewa milele.

14Enoki, mtu wa saba kuanzia Adamu alitoa unabii kuhusu watu hawa, akisema, “Tazama, Bwana anakuja pamoja na maelfu kwa maelfu ya watakatifu Wake, ili kumhukumu kila mmoja na kuwapatiliza wote wasiomcha Mungu kwa matendo yao yote ya uasi waliyoyatenda, pamoja na maneno yote ya kuchukiza ambayo
wenye dhambi wamesema dhidi Yake.” 16Watu
hawa ni wenye kunung’unika na wenye kutafuta makosa, wao hufuata tamaa zao mbaya, hujisifu kwa maneno makuu kuhusu wao wenyewe na kuwasifu mno watu wenye vyeo kwa ajili ya kujipatia faida.

***Maonyo Na Mausia***

17Lakini ninyi wapenzi, kumbukeni yale Mitume wa Bwana Yesu Kristo waliyotangulia
kusema. 18Kwa kuwa waliwaambia, “Siku za
mwisho kutakuwa na watu wenye kudhihaki watakaofuata tamaa zao wenyewe za upotovu.”
19Hawa ndio watu wanaowagawa ninyi, wafuatao tamaa zao za asili wala hawana Roho.

20Lakini ninyi wapenzi, jijengeni katika imani yenu iliyo takatifu sana tena ombeni katika Roho
Mtakatifu. 21Jilindeni katika upendo wa Mungu
mkitazamia kwa furaha rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo ili awalete katika uzima wa milele.

22Wahurumieni wengine wale wenye shaka,
23wengine waokoeni kwa kuwanyakua kutoka kwenye moto, nao wengine wahurumieni mkiwa na hofu mkichukia hata vazi lenye mawaa na kutiwa unajisi na mwili.

***Dua Ya Kutakia Heri***

24Kwake Yeye awezaye kuwalinda msianguke na kuwaleta ninyi mbele za utukufu Wake mkuu bila dosari kwa furaha ipitayo kiasi,
25Yeye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu, ukuu, uweza na mamlaka vina Yeye tangu milele, sasa na hata milele! Amen.

## Ufunuo wa Yohana

### *Utangulizi:*

Kitabu hiki kinaanza, *"Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa na Mungu… "* kikionyesha kuwa Yesu Kristo ndiye mhusika mkuu katika kitabu hiki. Tangu mwanzo kuonekana kwa Kristo ndiko kunakotawala. Hivyo Ufunuo huu ni wa Yesu Kristo aliopewa na Mungu, japo kitabu kimechukua jina la mwandishi, "Ufunuo wa Yohana", ukweli ni kwamba haumzungumzii Yohana kwa undani wala haumfunui yeye, bali Yesu Kristo. Yesu ndiye Mwana Kondoo ambaye ameleta ukombozi. Yeye ndiye atakayehukumu na hatimaye atashinda kabisa uovu, ili ufalme wa milele ulio bora kabisa usimamishwe.

Kuna sehemu kubwa tatu katika kitabu hiki chenye mambo mengi muhimu. Sehemu ya kwanza ni maono ya Yesu Kristo, (*sura ya 1).* Sehemu ya pili inahusu habari za makanisa, yaani, barua zinazoandikwa kwa makanisa saba yaliyoko Asia *(sura ya 2-3).* Sehemu ya tatu inahusu maono mbalimbali juu ya maisha na mateso ya watu wa Mungu, kushindwa kwa uovu, kuja kwa Kristo mara ya pili, hukumu ya mwisho, utawala wa miaka elfu moja na maisha ya mbinguni *( sura ya 4-22).* Sehemu kubwa ya maono hayo inahusu maafa yatakayoipata dunia ambapo ghadhabu ya Mwana- Kondoo, yaani, Yesu, inaonyeshwa. Katika maono haya yamo pia maono kuhusu watu wa Mungu walioteswa na kuuawa ambao sasa wako mbinguni. Maono yanafikia kilele kwenye vita baina ya yule kahaba Babeli na ushindi wa Neno la Mungu ambaye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana *(19:16).* Yeye amekuja kuangamiza kazi za Shetani (uovu) na kuandaa karamu kwa wale wamwaminio. Ndipo yanafuata maono kuhusu hukumu na utukufu na maneno ya mwisho, 'Amen, na uje Bwana Yesu' *(22:20).*

Mstari wa ufunguo wa kitabu hiki ni *(1:19 "Basi andika mambo uliyoyaona, yaliyoko na yale yatakayotukia baada ya haya."* Kikiwa na lugha ya kiufunuo, yaani, matumizi ya mifano na majina ya kubuniwa ambayo si halisi, lugha ya mfano, ndoto, maono, matumizi makubwa ya tarakimu na viumbe vya mbinguni. Tumaini kwa wale wanaoteswa katika nyakati zile za kukata tamaa.

### *Wazo Kuu*

Kitabu hiki chenye utukufu kinamwonyesha Yesu ambaye mwanzo alidharauliwa, Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, akichukua utawala wa historia nyakati za mwisho na akileta ushindi wa milele kwa kuangamiza uovu na kuleta utawala wa haki milele na milele. Mkristo katika kitabu hiki anapata uhakika wa tumaini lake kwamba: siku moja mambo yote yatakuwa mema na Mungu atatawala juu ya yote. Machozi yatafutwa, kifo, huzuni, majonzi na uchungu vitakoma milele'' *(21:4)*. Huu ni ujumbe wa kutia moyo kwa waamini wote, wakati wote.

### *Mwandishi*

Yale yaliyomo kwenye kitabu hiki na ushahidi wa nje unaonyesha kwamba mwandishi ni mtu aliyekuwa na nafasi muhimu ya uongozi katika makanisa ya Asia. Mwandishi wa kitabu hiki ni Yohana*, ''Mimi Yohana, ndugu yenu ninayeshiriki pamoja nanyi mateso katika Yesu… '', (1:9-10),* ambaye ametajwa mahali pengi *(1:1, 4, 9: 21:2 na 22:8)*. Huyu ndiye aliyeandika pia Injili pamoja na nyaraka zote tatu, ambaye ndiye yule anayetajwa kama mwanafunzi aliyependwa na ambaye aliegama kifuani mwa Yesu wakati wa chakula cha mwisho kati ya Yesu na wanafunzi Wake.

### *Tarehe*

Kitabu hiki kimeandikwa 96 B.K.

### *Mahali*

Kisiwa cha Patmo karibu na pwani ya Uyunani (Greece).

### *Mgawanyo*

- Mwanzo wa maono (1:1-20)
- Barua saba kwa Makanisa (2:1-3:22)
- Maono kuhusu Mungu na Mwana-Kondoo (4:1-5:14)
- Lakiri saba za hukumu (6:1-8:5)
- Tarumbeta saba za hukumu (8:6-11:19)
- Maono kuhusu vita ya duniani na mbinguni (12:1-14:20)
- Mabakuli saba ya hukumu (15:1-16:21)
- Hukumu juu ya Kahaba Babeli ( 17:1-19:21)
- Mwisho wa nyakati na wakati ujao ( 20:1-22:21)

### *Utangulizi Na Salamu*

1 Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa na
Mungu ili awaonyeshe watumishi Wake mambo
yatakayotukia karibuni. Alijulisha mambo
haya kwa kumtuma malaika Wake kwa Yohana
mtumishi Wake, 2ambaye ameshuhudia kuhusu
kila kitu alichoona, yaani, Neno la Mungu na
ushuhuda wa Yesu Kristo. 3Amebarikiwa
yeye asomaye maneno ya unabii huu na pia
wamebarikiwa wale wanaoyasikia na kuyatia
moyoni yale yaliyoandikwa humo, kwa
sababu wakati umekaribia.

### *Salamu Kwa Makanisa Saba*

4Yohana,

kwa makanisa saba yaliyoko Asia:

Neema na amani kutoka kwa Yeye aliyeko,
aliyekuwako na atakayekuja na kutoka kwa wale
Roho saba walioko mbele ya kiti Chake cha enzi
5na kwa Yesu Kristo ambaye ni shahidi
mwaminifu, aliye mzaliwa wa kwanza kutoka
kwa wafu, ambaye Yeye ndiye mtawala wa
wafalme wa dunia.

Kwake Yeye aliyetupenda na ambaye
ametuweka huru kutoka katika dhambi zetu kwa
damu Yake, 6akatufanya sisi kuwa ufalme na
makuhani, tumtumikie Mungu Wake ambaye ni
Baba yake. Utukufu na uwezo vina Yeye milele
na milele! Amen.

7Tazama! Anakuja na mawingu
na kila jicho litamwona,
hata wale waliomchoma mkuki,
na mataifa yote ulimwenguni
yataomboleza kwa sababu yake.
Naam ndivyo itakavyokuwa! Amen.

8‘‘Mimi ni Alfa na Omega,’’ asema Bwana
Mungu, ‘‘Aliyeko, aliyekuwako na atakayekuja,
Mwenyezi.’’

### *Maono Ya Kristo*

9Mimi Yohana, ndugu yenu ninayeshiriki
pamoja nanyi mateso katika Yesu na katika
ufalme na uvumilivu katika saburi, nilikuwa
katika kisiwa kiitwacho Patmo kwa ajili ya neno
la Mungu na ushuhuda wa Yesu. 10Nilikuwa
katika Roho siku ya Bwana, nikasikia sauti
kubwa kama ya tarumbeta nyuma yangu
11ikisema, “Andika kwenye kitabu haya yote
unayoyaona, kisha ukipeleke kwa makanisa
saba, yaani: Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira,
Sardi, Filadelfia na Laodikia.’’

12Ndipo nikageuka ili nione ni sauti ya nani
iliyokuwa ikisema nami. Nami nilipogeuka,
nikaona vinara saba vya taa vya dhahabu,
13katikati ya vile vinara vya taa, nikaona mtu
kama Mwana wa Adamu, amevaa joho refu na
mkanda wa dhahabu umefungwa kifuani
mwake. 14Kichwa chake na nywele zake
zilikuwa nyeupe kama sufu, nyeupe kama
theluji, nayo macho yake yalikuwa kama mwali
wa moto. 15 Nyayo zake zilikuwa kama shaba
iliyosuguliwa sana, kama vile imesafishwa
katika tanuru ya moto, nayo sauti yake ilikuwa
kama sauti ya maji mengi. 16 Katika mkono
wake wa kuume alishikilia nyota saba na
kinywani mwake ulitoka upanga wenye makali
kuwili. Uso wake kama jua kali linalong’aa kwa
nguvu zake zote.

17 Nilipomwona, nilianguka miguuni pake
kama aliyekufa. Ndipo akaweka mkono wake
wa kuume juu yangu na kusema, “Usiogope,
Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho. 18Mimi ni
Yeye aliye hai, niliyekuwa nimekufa na tazama,
ni hai milele na milele! Nami ninazo funguo za
mauti na kuzimu[a]. 19Basi andika mambo
uliyoyaona, yaliyopo na yale yatakayotukia
baada ya haya. 20Kuhusu siri ya zile nyota saba
ulizoziona katika mkono Wangu wa kuume na
vile vinara saba vya taa vya dhahabu ni hii: zile
nyota saba ni malaika wa yale makanisa saba,
navyo vile vinara saba ni hayo makanisa saba.

### *Kwa Kanisa Lililoko Efeso*

2 ‘‘Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika:

Haya ndiyo maneno ya yule aliyezishika
zile nyota saba katika mkono wake wa
kuume, na ambaye hutembea katikati ya
vile vinara saba vya taa vya dhahabu.
2‘‘Nayajua matendo yako, bidii yako na
saburi yako. Najua kuwa huwezi
kuvumiliana na watu waovu na ya kwamba
umewajaribu wale wanaojifanya kuwa
mitume na kumbe sio, nawe umewatambua

---

a18 “Kuzimu” hapa linatokana na neno la Kiyunani “Hades” au “Tartarus”, yaani, mahali pa mateso kwa ajili ya waliopotea.

kuwa ni waongo. 3Nami najua umevumilia na kustahimili taabu kwa ajili ya Jina langu, wala hukuchoka.

4Lakini nina neno juu yako: umeuacha upendo wako wa kwanza. 5Kumbuka basi ni wapi ulikoanguka! Tubu na ukafanye matendo yale ya kwanza. Kama usipotubu, nitakuja kwako na kukiondoa kinara chako cha taa kutoka mahali pake. 6Lakini una jambo hili kwa upande wako: unayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo nami nayachukia.

7Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho ayaambia makanisa. Yeye atakayeshinda, nitampa haki ya kula matunda ya mti wa uzima, ambao uko katika paradiso[a] ya Mungu.

### *Kwa Kanisa Liliko Smirna*

8"Kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika:

Haya ndiyo maneno yake Yeye aliye wa Kwanza na wa Mwisho, aliyekufa kisha akafufuka. 9Naijua dhiki yako na umaskini wako, lakini wewe ni tajiri! Nayajua masingizio ya wale wasemao kuwa ni Wayahudi lakini sio, wao ni sinagogi la Shetani. 10Usiogope mateso yatakayokupata. Nakuambia Shetani atawatia baadhi yenu gerezani ili kuwajaribu, nanyi mtapata dhiki kwa muda wa siku kumi. Uwe mwaminifu, hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.

11Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho anayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatadhuriwa na mauti ya pili.

### *Kwa Kanisa Lililoko Pergamo*

12"Kwa malaika wa Kanisa lililoko Pergamo andika:

Haya ndiyo maneno yake Yeye aliye na upanga wenye makali kuwili. 13Ninajua unakoishi, ni kule ambako Shetani ana kiti chake cha enzi. Lakini umelishika jina langu. Wala hukuikana imani yako kwangu hata katika siku za shahidi wangu mwaminifu Antipa, ambaye aliuawa katika mji wenu, ambako ndiko anakokaa Shetani.

14 Lakini nina mambo machache dhidi yako: unao watu wafuatao mafundisho ya Balaamu, yule aliyemfundisha Balaki kuwashawishi Waisraeli watende dhambi kwa kula vitu vilivyotolewa dhabihu kwa sanamu na kufanya uasherati. 15Vivyo hivyo unao wale wayashikao mafundisho ya Wanikolai. 16Basi tubuni! ama sivyo, nitakuja kwako upesi na kupigana na watu hao kwa upanga wa kinywa changu.

17Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho anayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa yeye jiwe jeupe ambalo juu yake limeandikwa jina jipya asilolijua mtu, isipokuwa yule anayelipokea.

### *Kwa Kanisa Lililoko Thiatira*

18"Kwa malaika wa kanisa lililoko Thiatira andika :

Haya ndiyo maneno ya Mwana wa Mungu, ambaye macho yake ni kama mwali wa moto na ambaye miguu yake ni kama shaba iliyosuguliwa sana. 19Nayajua matendo yako, upendo wako, imani yako, huduma na saburi yako na kwamba matendo yako ya sasa yamezidi yale ya kwanza.

20Lakini nina neno dhidi yako: unamvumilia yule mwanamke Yezebeli ambaye anajiita nabii, lakini anawafundisha na kuwapotosha watumishi wangu ili wafanye uasherati na kula vyakula vilivyotolewa kafara kwa sanamu.
21Nimempa muda ili atubie uasherati wake, lakini hataki. 22Kwa hiyo nitamtupa kwenye kitanda cha mateso, nami nitawafanya hao wanaozini naye kupata mateso makali wasipotubia njia zake. 23Nami nitawaua watoto wake. Nayo makanisa yote yatajua kwamba Mimi ndiye nichunguzaye mioyo na nia za watu na kwamba nitamlipa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake.
24Basi nawaambia ninyi wengine mlioko Thiatira, ninyi ambao hamyafuati mafundisho ya Yezebeli, wala hamkujifunza hayo wengine wanayoyaita mambo ya ndani sana ya Shetani (sitaweka mzigo mwingine wo wote juu yenu): 25Lakini shikeni sana mlicho nacho, mpaka nitakapokuja.

26Atakayeshinda na kutenda mapenzi Yangu mpaka mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa.

---

a[7] Paradiso hapa ina maana ya bustani, yaani,shamba dogo la miti izaayo matunda.

27'Atawatawala kwa fimbo ya chuma,
atawavunja vipande vipande kama
chombo cha udongo,

kama vile mimi nilivyopokea mamlaka
kutoka kwa Baba yangu. 28Yeye ashindaye
nitampa ile nyota ya asubuhi. 29Yeye aliye
na sikio na asikie yale ambayo Roho
anayaambia makanisa.

### *Kwa Kanisa Lililoko Sardi*

**3** "Kwa malaika wa Kanisa lililoko Sardi andika:

Haya ndiyo maneno Yake Yeye aliye na
zile Roho saba za Mungu na zile nyota
saba. Nayajua matendo yako, kwamba una
sifa ya kuwa hai, lakini umekufa. 2Amka!
Nawe uyaimarishe yale yaliyo karibu kufa,
kwa maana sikuona kwamba kazi zako
zimekamilika machoni pa Mungu wangu.
3Kumbuka basi yale uliyoyapokea na
kuyasikia, yatii na ukatubu. Lakini
usipoamka, nitakuja kama mwivi wala
hutajua saa nitakayokuja kwako.

4Lakini bado una watu wachache katika
Sardi ambao hawajayachafua mavazi yao.
Wao wataenda pamoja nami, wakiwa
wamevaa mavazi meupe, kwa maana
wanastahili. 5Yeye ashindaye atavikwa vazi
jeupe kama wao, nami sitafuta jina lake
kutoka katika kitabu cha uzima, bali nitalikiri
jina lake mbele za Baba yangu na mbele za
malaika Wake. 6Yeye aliye na sikio na asikie
yale ambayo Roho anayaambia makanisa.

### *Kwa Kanisa Lililoko Filadelfia*

7"Kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia
andika :

Haya ndiyo maneno Yake Yeye aliye
mtakatifu na wa kweli, Yeye aliye na
ufunguo wa Daudi. Anachokifungua hakuna
awezaye kukifunga, wala anachokifunga
hakuna awezaye kukifungua. 8Nayajua
matendo yako. Tazama, nimeweka mbele
yako mlango uliofunguliwa, wala hakuna
awezaye kuufunga. Ninajua kwamba una
nguvu kidogo lakini umelishika neno Langu
wala hukulikana Jina langu. 9Nitawafanya
wale wa sinagogi la Shetani, wale ambao
husema kuwa ni Wayahudi lakini sio, bali ni
waongo, waje wapige magoti miguuni pako,
nao watajua ya kwamba nimekupenda.
10Kwa kuwa umelishika neno la saburi
Yangu nitakulinda hata utoke katika saa ya
kujaribiwa inayokuja ulimwenguni pote ili
kuwajaribu wote wakaao duniani.

11Ninakuja upesi. Shika sana ulicho
nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako.
12Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo
katika hekalu la Mungu wangu, wala
hatatoka humo kamwe. Nitaandika juu yake
Jina la Mungu wangu na jina la mji wa
Mungu wangu, yaani, Yerusalemu mpya,
ambao unashuka kutoka mbinguni kwa
Mungu wangu. Nami pia nitaandika juu
yake Jina langu jipya. 13Yeye aliye na sikio
na asikie yale ambayo Roho anayaambia
makanisa.

### *Kwa Kanisa Lililoko Laodikia*

14"Kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia
andika :

Haya ndiyo maneno Yake Yeye aliye
Amen, shahidi mwaminifu na wa kweli,
mtawala wa uumbaji wote wa Mungu. 15
Nayajua matendo yako, ya kwamba wewe
si baridi wala si moto. Afadhali ungelikuwa
baridi au moto. 16 Hivyo kwa kuwa u
uvuguvugu, kwamba wewe si baridi wala si
moto, nitakutapika utoke kinywani Mwangu.
17Kwa maana unasema, 'Mimi ni tajiri,
nimefanikiwa, wala sihitaji kitu cho chote.'
Hujui ya kwamba wewe ni mnyonge, wa
kuhurumiwa, masikini, kipofu, tena uliye
uchi. 18Kwa hiyo nakushauri ununue kutoka
Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili
upate kuwa tajiri na mavazi meupe ili
uyavae, upate kuficha aibu ya uchi wako na
mafuta ya kupaka macho yako ili upate
kuona .

19Wale niwapendao, ninawakemea na
kuwaadibisha. Hivyo uwe na bidii ukatubu.
20Tazama, nasimama mlangoni nabisha.
Kama mtu ye yote akisikia sauti Yangu na
kufungua mlango, nitaingia ndani na kula
pamoja naye,naye pamoja nami.

21Yeye ashindaye nitampa haki ya kuketi
pamoja Nami kwenye kiti Changu cha enzi,
kama vile Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja
na Baba Yangu kwenye kiti Chake cha enzi.
22Yeya aliye na sikio na asikie yale ambayo
Roho anayaambia makanisa."

### *Kiti Cha Enzi Kilichoko Mbinguni*

**4** Baada ya mambo hayo nilitazama, nami
nikaona mbele yangu mlango uliowazi
mbinguni. Nayo ile sauti niliyokuwa nimeisikia
hapo kwanza ikisema nami kama tarumbeta
ikasema, “Njoo panda huku nami nitakuonyesha
yale ambayo hayana budi kutokea baada ya
haya.’’ 2Ghafula nilikuwa katika Roho, hapo
mbele yangu kilikuwapo kiti cha enzi mbinguni,
kikiwa kimekaliwa na mtu mmoja. 3Yeye
aliyekuwa amekikalia alikuwa anaonekana
kama yaspi na akiki. Kukizunguka kile kiti cha
enzi palikuwa na upinde wa mvua ulioonekana
kama zumaridi. 4 Pia kukizunguka hicho kiti cha
enzi palikuwa na viti ishirini na vinne na juu ya
hivyo viti walikuwa wameketi wazee ishirini na
wanne, waliovaa majoho meupe, wakiwa na taji
za dhahabu vichwani mwao. 5Kwenye kile kiti
cha enzi palikuwa panatoka miali ya umeme wa
radi, ngurumo na sauti za radi. Mbele ya hicho
kiti cha enzi, palikuwa na taa saba zilizokuwa
zinawaka. Hizi ndizo Roho saba za Mungu. 6Pia
mbele ya hicho kiti cha enzi palikuwa na kile
kilichoonekana kama bahari ya kioo, iliyokuwa
angavu kama jiwe lisilo na rangi yo yote
ling’aalo sana.

Katikati, kukizunguka kile kiti cha enzi,
kulikuwa na viumbe wanne wenye uhai, wakiwa
wamejawa na macho mbele na nyuma. 7Huyo
kiumbe wa kwanza mwenye uhai alikuwa kama
simba, wa pili alikuwa kama ng'ombe dume, wa
tatu alikuwa na uso kama wa mwanadamu na
wa nne alikuwa kama tai anayeruka. 8Kila
mmoja wa hawa viumbe wenye uhai wanne,
alikuwa na mabawa sita na kujawa na macho
pande zote, hadi chini ya mabawa. Usiku na
mchana hawakuacha kusema:

“Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu,
ni Bwana Mungu Mwenyezi,
aliyekuwako, aliyeko na atakayekuja.’’

9Kila mara viumbe hao wenye uhai wanne
walipomtukuza, kumheshimu na kumshukuru
Yeye aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi, tena
aishie milele na milele, 10 wale wazee ishirini na
wanne huanguka mbele Zake Yeye aliyeketi
kwenye kile kiti cha enzi na kumwabudu Yeye
aliye hai milele na milele. Wao huziweka taji zao
mbele ya hicho kiti cha enzi wakisema,

11“Bwana wetu na Mungu wetu,
Wewe umestahili kupokea utukufu
na heshima na uweza,
kwa maana ndiwe uliyeviumba vitu vyote
na kwa mapenzi Yako viliumbwa
na vimekuwako.’’

### *Kitabu Na Mwana-Kondoo*

**5** Kisha nikaona katika mkono Wake wa
kuume yule aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi,
kitabu kilichoandikwa ndani na upande wa
nyuma kikiwa kimefungwa kwa lakiri saba.
2Nami nikamwona malaika mwenye nguvu
akitangaza kwa sauti kuu, akisema, “Ni nani
anayestahili kuzivunja hizo lakiri na kukifungua
hicho kitabu?” 3Lakini hapakuwa na ye yote
mbinguni wala duniani au chini ya dunia
aliyeweza kukifungua hicho kitabu wala hata
kutazama ndani yake. 4Nikalia sana sana kwa
sababu hakuonekana ye yote aliyestashili
kukifungua hicho kitabu wala kutazama ndani
yake. 5Kisha, mmoja wa wale wazee
akaniambia, “Usilie! Tazama, Simba wa kabila la
Yuda, wa uzao wa Daudi, ameshinda, ili
kwamba aweze kukifungua hicho kitabu na
kuvunja hizo lakiri zake saba.’’

6 Ndipo nikaona kati ya kile kiti cha enzi na
wale viumbe wenye uhai wanne na miongoni
mwa wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama,
akiwa kama amechinjwa. Alikuwa na pembe
saba na macho saba, ambazo ndizo zile Roho
saba za Mungu zilizotumwa duniani pote. 7Huyo
Mwana-Kondoo akaja na kukitwaa kile kitabu
kutoka kwenye mkono wa kuume wa yule
aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi. 8Alipokwisha
kukitwaa kile kitabu, wale viumbe wenye uhai
wanne pamoja na wale wazee ishirini na wanne
wakaanguka mbele ya yule Mwana-Kondoo.
Kila mmoja wao alikuwa na kinubi, nao
walikuwa wameshika mabakuli ya dhahabu
yaliyojaa uvumba, ambayo ni maombi ya
watakatifu. 9Nao wakaimba wimbo mpya
wakisema:

“Wewe unastahili kukitwaa kitabu
na kuzivunja lakiri zake,
kwa sababu ulichinjwa
na kwa damu Yako ukamnunulia
Mungu watu
kutoka katika kila kabila, kila lugha,
kila jamaa na kila taifa.
10Wewe umewafanya hawa wawe ufalme na
makuhani wa kumtumikia Mungu wetu,
nao watamiliki katika dunia.’’

11Nami nikatazama, nikasikia sauti za
malaika wengi wakiwa wamekizunguka kile kiti
cha enzi, pamoja na wale viumbe wenye uhai
wanne na wale wazee ishirini na wanne, idadi
yao ilikuwa kumi elfu mara kumi elfu na maelfu
ya maelfu. 12Nao wakiimba kwa sauti kuu,
wakisema:

“Anastahili Mwana-Kondoo, Yeye
aliyechinjwa,
kupokea uweza na utajiri na hekima
na nguvu
na heshima na utukufu na sifa!”

13Kisha nikasikia kila kiumbe mbinguni na
duniani, chini ya nchi na baharini na vyote
vilivyomo ndani yake vikiimba:

“Sifa na heshima na utukufu na uweza ni
vyake Yeye aketiye juu ya hicho kiti
cha enzi na kwa Mwana-Kondoo,
milele na milele!”

14Wale viumbe wenye uhai wanne wakasema,
“Amen!” Nao wale wazee ishirini na wanne
wakaanguka kifudifudi wakaabudu.

### *Mwana- Kondoo Avunja Lakiri Saba*

6 Kisha nikamwona Mwana-Kondoo
akivunja ile lakiri ya kwanza miongoni
mwa zile saba. Ndipo nikasikia mmoja wa wale
viumbe wenye uhai wanne akisema kwa sauti
kama ya radi: “Njoo!” 2Nikatazama na hapo
mbele yangu alikuwepo farasi mweupe! Yeye
aliyempanda alikuwa na upindi, naye akapewa
taji, akampanda akatoka akishinda ili apate
kushinda.

3Alipoivunja ile lakiri ya pili, nikamsikia yule
kiumbe mwenye uhai wa pili akisema, “Njoo!”
4Ndipo akatokea farasi mwingine wa rangi
nyekundu. Yeye aliyempanda akapewa uwezo
wa kuondoa amani duniani na kuwafanya watu
wauane. Yeye akapewa upanga mkubwa.

5Alipoivunja ile lakiri ya tatu, nikamsikia yule
kiumbe wa tatu mwenye uhai akisema, “Njoo!”
Nikatazama na mbele yangu alikuwepo farasi
mweusi! Yeye aliyempanda alikuwa na mizani
mkononi mwake. 6 Ndipo nikasikia kile
kilichokuwa kama sauti katikati ya wale viumbe
wanne wenye uhai ikisema, “Kipimo kimoja cha
ngano kwa mshahara wa kibarua wa siku moja.
Vipimo vitatu vya shayiri kwa mshahara wa
kibarua wa siku moja [a]. Lakini usiharibu mafuta
ya zeituni wala divai!”

7Alipovunja ile lakiri ya nne, nikasikia sauti
ya yule kiumbe wa nne mwenye uhai ikisema,
“Njoo!” 8Nikatazama na hapo mbele yangu
alikuwepo farasi mwenye rangi ya kijivujivu!
Yeye aliyempanda huyo farasi aliitwa Mauti,
naye Kuzimu[b] alikuwa akifuatana naye, nao
wakapewa mamlaka juu ya robo ya dunia, kuua
kwa upanga, njaa, tauni na kwa wanyama
wakali wa dunia.

9Alipoivunja ile lakiri ya tano, nikaona chini
ya madhabahu, roho za wale waliouawa kwa
ajili ya Neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda
walioutunza. 10Wakalia kwa sauti kuu,
wakisema, “Hata lini, Ee Bwana Mwenyezi,
uliye Mtakatifu na Mwaminifu, kutokuwahukumu
na kulipiza kisasi juu ya watu waishio duniani
kwa ajili ya damu yetu?” 11Kisha kila mmoja
wao akapewa joho jeupe, nao wakaambiwa
wangoje kwa muda kidogo zaidi, mpaka idadi ya
ndugu zao na watumishi wenzao watakaouawa
kama wao walivyouawa, itakapotimia.

12Nikaangalia, Naye alipokuwa akiivunja ile
lakiri ya sita, pakatokea tetemeko kuu la nchi na
jua likawa jeusi kama nguo ya gunia
iliyotengenezwa kwa singa za mbuzi, mwezi
wote ukawa mwekundu kama damu. 13Nyota
zilizo angani zikaanguka ardhini kama vile
matunda ya mtini yasiyokomaa yaangukavyo
wakati mti wake unapotikiswa na upepo mkali.
14Anga ikatoweka kama vile karatasi
isokotwavyo na kila mlima na kila kisiwa
kikaondolewa mahali pake.

15Ndipo wafalme wa duniani, wakuu wote,
majemadari, matajiri, wenye nguvu na kila mtu,
mtumwa na mtu huru, wakajificha katika
mapango na kwenye miamba ya milima.
16Wakaiita milima na miamba wakisema,
“Tuangukieni, mkatufiche na uso Wake Yeye
aketiye kwenye kiti cha enzi na mkatuepushe na
ghadhabu ya Mwana-Kondoo, 17kwa maana
siku ile kuu ya ghadhabu yao imewadia.Je, ni
nani awezaye kusimama?”

### *Wale Wasraeli 144,000 Watiwa Muhuri*

7 Baada ya haya nikaona malaika wanne wakiwa
wamesimama katika pembe nne
za dunia, wakizuia hizo pepo nne za dunia, ili

---

[a]6 Mshahara wa kibarua wa siku moja ulikuwa sawa na dinari moja.

[b]7 Kuzimu hapa ni neno linalotokana na neno la Kiyunani “Hades” au kwa Kiebrania “Sheol”

kwamba pasiwe na upepo utakaovuma juu ya nchi au juu ya bahari au juu ya mti wo wote.
2Nikaona malaika mwingine akipanda kutoka maawio ya jua akiwa na muhuri wa Mungu aliye hai. Akawaita kwa sauti kubwa wale malaika wanne waliokuwa wamepewa mamlaka ya kuidhuru nchi na bahari, akisema, 3"Msiidhuru nchi wala bahari, wala miti, hadi tuwe tumetia alama kwenye vipaji vya nyuso za watumishi wa Mungu wetu." 4Ndipo nikasikia idadi ya wale waliowekewa alama, yaani, watu 144,000 kutoka katika makabila yote ya Israeli.

5Kutoka kabila la Yuda 12,000,
kabila la Reubeni 12,000,
kabila la Gadi 12,000,
6kabila la Asheri 12,000,
kabila la Naftali 12,000,
kabila la Manase 12,000,
7kabila la Simeoni 12,000,
kabila la Lawi 12,000,
kabila la Isakari 12,000,
8kabila la Zabuloni 12,000,
kabila la Yosefu 12,000
na kabila la Benyamini 12,000.

### *Umati Mkubwa Wa Watu Kutoka Mataifa yote*

9Baada ya haya nikatazama na hapo mbele yangu palikuwa na umati mkubwa wa watu ambao hakuna ye yote awezaye kuuhesabu. Kutoka kila taifa, kila kabila, kila jamaa na kila lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi na mbele ya Mwana-Kondoo. Walikuwa wamevaa mavazi meupe na wakiwa wameshika matawi ya mitende mikononi mwao. 10Nao walikuwa wakipiga kelele kwa sauti kubwa wakisema:

"Wokovu una Mungu wetu,
Yeye aketiye kwenye kiti cha enzi
na Mwana-Kondoo!"

11Nao malaika wote walikuwa wamesimama kukizunguka kile kiti cha enzi na wale wazee ishirini na wanne na wale viumbe wanne wenye uhai. Wakaanguka kifudifudi mbele ya hicho kiti cha enzi na kumwabudu Mungu, 12wakisema:

"Amen!
Sifa na utukufu
na hekima na shukrani na heshima
na uweza na nguvu
viwe kwa Mungu wetu milele na milele,
Amen!"

13Kisha mmoja wa wale wazee ishirini na wanne akaniuliza, "Ni nani hawa waliovaa mavazi meupe, nao wametoka wapi?"
14Nikamjibu, "Bwana, wewe wajua."
Naye akasema, "Hawa ni wale waliotoka katika ile dhiki kuu, nao wamefua mavazi yao katika damu ya Mwana-Kondoo na kuyafanya meupe kabisa. 15Kwa hiyo,

"wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu
na kumtumikia usiku na mchana katika
Hekalu Lake,
naye aketiye katika kile kiti cha enzi
atakaa pamoja nao na kuwalinda.
16Kamwe hawataona njaa wala kiu
tena. Jua halitawapiga
wala joto lo lote liunguzalo.
17Kwa maana Mwana-Kondoo aliyeko katikati
ya kile kiti cha enzi atakuwa Mchungaji
wao,
naye atawaongoza kwenda kwenye
chemchemi za maji yaliyo hai.
Naye Mungu atafuta kila chozi kutoka
katika macho yao."

### *Lakiri Ya Saba Na Chetezo Cha Dhahabu*

**8** Mwana-Kondoo alipoivunja ile lakiri ya saba, pakawa kimya mbinguni kwa muda wa nusu saa.

2Nami nikawaona wale malaika saba wanaosimama mbele za Mungu, nao wakapewa tarumbeta saba.

3Malaika mwingine aliyekuwa na chetezo cha dhahabu, akaja na kusimama mbele ya madhabahu. Akapewa uvumba mwingi ili autoe pamoja na maombi ya Watakatifu wote, juu ya ile madhabahu ya dhahabu iliyoko mbele ya kile kiti cha enzi. 4 Ule moshi wa uvumba pamoja na yale maombi ya watakatifu, vikapanda juu mbele za Mungu, kutoka mkononi mwa huyo malaika. 5Kisha yule malaika akachukua kile chetezo, akakijaza moto kutoka kwenye ile madhabahu, akautupa juu ya dunia. Pakatokea sauti za radi, ngurumo, umeme wa radi na tetemeko la nchi.

### *TARUMBETA SABA*

### *Tarumbeta Ya Kwanza*

6Basi wale malaika saba waliokuwa na zile tarumbeta saba wakajiandaa kuzipiga.

7Malaika wa kwanza akaipiga tarumbeta

yake, pakatokea mvua ya mawe na moto uliochanganyika na damu, vikatupwa kwa nguvu juu ya nchi na theluthi ya dunia ikateketea, theluthi ya miti ikateketea na majani yote mabichi yakateketea.

### *Tarumbeta Ya Pili*

8Malaika wa pili akaipiga tarumbeta yake na kitu kama mlima mkubwa unaowaka moto kikatupwa baharini. Theluthi ya bahari ikawa
damu, 9theluthi ya viumbe vyenye uhai viishivyo baharini vikafa na theluthi ya meli zikaharibiwa.

### *Tarumbeta Ya Tatu*

10Malaika wa tatu akaipiga tarumbeta yake na nyota kubwa iliyokuwa ikiwaka kama taa, ikaanguka toka angani, ikaangukia theluthi ya
mito na chemchemi za maji. 11Nyota hiyo inaitwa "Uchungu.'' Theluthi ya maji yakawa machungu na watu wengi wakafa kutokana na maji hayo kwa maana yalikuwa machungu.

### *Tarumbeta Ya Nne*

12Kisha malaika wa nne akaipiga tarumbeta yake na theluthi ya jua, theluthi ya mwezi na theluthi ya nyota, zikapigwa. Kwa hiyo theluthi moja ya mwanga ikawa giza. Theluthi ya mchana ikawa haina mwanga na pia theluthi ya usiku.

13Nilipokuwa tena nikitazama, nikamsikia tai mmoja akipiga kelele kwa sauti kuu wakati akiruka katikati ya mbingu, akisema, "Ole, Ole, Ole, wa watu waishio duniani, kwa sababu ya tarumbeta ambazo malaika wengine watatu wanakaribia kuzipiga.''

### *Tarumbeta Ya Tano*

**9** Malaika wa tano akaipiga tarumbeta yake, nami nikaona nyota iliyokuwa imeanguka toka angani hadi ardhini. Nyota hiyo ilipewa ufunguo wa shimo lisilo na mwisho[a].
2Alipolifungua hilo shimo lisilo na mwisho, moshi ukapanda kutoka humo kama moshi wa tanuru kubwa sana. Jua na anga vikatiwa giza na ule moshi uliotoka katika hilo shimo lisilokuwa na
mwisho. 3Ndipo katika ule moshi wakatoka nzige wakaenda juu ya nchi, nao wakapewa nguvu kama zile za nge wa duniani.
4Wakaambiwa wasidhuru majani ya nchi, wala mmea wala mti wo wote, bali wawadhuru tu wale watu ambao hawana alama ya Mungu
kwenye vipaji vya nyuso zao. 5 Wakaruhusiwa kuwatesa kwa muda wa miezi mitano, lakini wasiwaue. Uchungu wa kuuma kwao ulikuwa
kama ule wa mtu aumwapo na nge. 6Katika siku hizo watu watatafuta kifo lakini hawatakiona, watatamani kufa, lakini kifo kitawakimbia.

7Wale nzige walikuwa na umbo kama la farasi waliotayarishwa kwa ajili ya vita. Kwenye vichwa vyao kulikuwa na kitu kama taji za dhahabu na nyuso zao zilikuwa kama za
binadamu. 8Walikuwa na nywele kama za wanawake na meno yao yalikuwa kama ya
simba. 9Walikuwa na dirii kama za chuma na sauti za mabawa yao zilikuwa kama ngurumo za magari mengi ya farasi wanaokimbilia vitani.
10Walikuwa na mikia yenye miiba ya kuumia kama nge. Nguvu yao ya kutesa watu kwa huo muda wa miezi mitano ilikuwa katika hiyo mikia
yao. 11Walikuwa na malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho kama mfalme wao, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni[b] na kwa Kiyunani ni Apolioni.

12Ole ya kwanza imepita, bado nyingine mbili zinakuja.

### *Tarumbeta Ya Sita*

13Malaika wa sita akaipiga tarumbeta yake, nami nikasikia sauti ikitoka katika zile pembe nne za madhabahu ya dhahabu iliyoko mbele
za Mungu. 14Ile sauti ikamwambia yule malaika wa sita mwenye tarumbeta, "Wafungulie wale malaika wanne waliofungwa kwenye ule mto
mkubwa Eufrati.'' 15Basi wale malaika wanne wakafunguliwa ambao walikuwa wamewekwa tayari kwa ajili ya saa hiyo na siku hiyo na mwezi huo na mwaka huo ili wawaue theluthi ya
wanadamu. 16Idadi ya majeshi wapandao farasi ilikuwa 200,000,000.

17Hivi ndivyo nilivyowaona hao farasi na wapanda farasi katika maono yangu: Wapanda farasi walivaa dirii vifuani zenye rangi ya moto na yakuti samawi na kiberiti. Vichwa vya hao farasi vilikuwa kama vichwa vya simba. Moto, moshi na kiberiti vilitoka vinywani mwao.
18Theluthi ya wanadamu wakauawa kwa maafa hayo matatu, yaani, huo moto, moshi na kiberiti, vilivyotoka kwenye vinywa vya hao farasi.
19Nguvu za hao farasi zilikuwa katika vinywa vyao na kwenye mikia yao, kwa sababu mikia

---

a1 Shimo lisilo na mwisho, yaani, "Abyss"maana yake kuzimu (makao ya pepo wachafu.)

b11 Kiebrania Abadoni na kwa Kiyunani Apolioni maana yake "Mharabu," yaani, yeye aharibuye.

yao ilikuwa kama nyoka. yenye vichwa ambayo waliitumia kuwadhuru watu.

20Wanadamu waliosalia, ambao hawakuuawa katika maafa hayo, bado walikataa kutubu na kuacha kumwabudu shetani na vitu walivyotengeneza kwa mikono yao wenyewe, yaani, sanamu za dhahabu, za fedha, za shaba, za mawe na za miti, ambazo haziwezi kuona, kusikia wala kutembea. 21Wala hawakutubu na kuacha matendo yao ya uuaji, uchawi, uasherati wala wizi wao.

### *Malaika Mwenye Kitabu Kidogo*

**10** Kisha nikamwona malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni. Alikuwa amevikwa wingu na upinde wa mvua juu ya kichwa chake. Uso wake uling'aa kama jua na miguu yake ilikuwa kama nguzo za moto. 2Mkononi mwake alikuwa ameshika kitabu kidogo kilichokuwa kimefunguliwa. Akauweka mguu wake wa kuume juu ya bahari na mguu wake wa kushoto akauweka juu ya nchi kavu. 3Naye akapiga kelele kwa sauti kuu kama simba anayenguruma. Alipopiga kelele, zile radi saba zikatoa ngurumo zake. 4Nazo zile radi saba zilipotoa ngurumo, nilitaka kuanza kuandika, lakini nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, “Yatie muhuri hayo yaliyosemwa na hizo radi saba na usiyaandike.’’

5Kisha yule malaika niliyekuwa nimemwona akiwa amesimama juu ya bahari na juu ya nchi kavu akainua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni. 6Naye akaapa kwa Jina la Mungu aishiye milele na milele, aliyeumba mbingu na vyote vilivyomo, dunia na vyote viijazavyo, pamoja na bahari na vyote vilivyomo ndani yake, akasema, ‘‘Hakuna kungoja tena. 7Lakini katika siku zile ambazo huyo malaika wa saba atakapokaribia kuipiga hiyo tarumbeta yake, siri ya Mungu itatimizwa, kama vile alivyowatangazia watumishi wake manabii.’’

8Ndipo ile sauti niliyokuwa nimeisikia kutoka mbinguni ikasema nami tena ikaniambia, ‘‘Nenda, chukua kile kitabu kilichofunguliwa kilichoko mkononi mwa yule malaika aliyesimama juu ya bahari na juu ya nchi kavu.’’

9Basi nikamwendea nikamwomba yule malaika anipe kile kitabu kidogo. Akaniambia, ‘‘Chukua na ukile. Kitakuwa kichungu tumboni mwako, lakini kinywani mwako kitakuwa kitamu kama asali.’’ 10Hivyo nikakichukua kile kitabu kidogo kutoka mkononi mwa yule malaika nikakila. Kilikuwa kitamu kama asali kinywani mwangu, lakini baada ya kukila, tumbo langu likatiwa uchungu. 11Kisha nikaambiwa, “Imekupasa kutoa unabii tena kuhusu makabila mengi, mataifa, lugha na wafalme.’’

### *Mashahidi Wawili*

**11** Ndipo nikapewa mwanzi wa kupimia ulio kama fimbo, nikaambiwa, “Nenda ukapime Hekalu la Mungu pamoja na madhabahu, nawe uwahesabu wale waabuduo humo. 2Lakini usiupime ua wa nje wa Hekalu, uache, kwa sababu ua huo wamepewa watu Mataifa. Hao wataukanyagakanyaga mji mtakatifu kwa muda wa miezi arobaini na miwili. 3Nami nitawapa mashahidi wangu wawili uwezo, nao watoe unabii kwa muda wa siku 1,260, wakiwa wamevaa nguo za gunia.’’ 4Hawa ndio ile mizeituni miwili na vile vinara viwili vya taa visimamavyo mbele za Bwana wa dunia yote. 5Kama mtu ye yote akitaka kuwadhuru, moto hutoka vinywani mwao na kuwateketeza adui zao. Hivi ndivyo mtu ye yote atakayetaka kuwadhuru atakavyokufa. 6Watu hawa wanao uwezo wa kufunga anga ili mvua isinyeshe wakati wote watakapokuwa wanatoa unabii wao. Nao watakuwa na uwezo wa kuyabadili maji kuwa damu na kuipiga dunia kwa kila aina ya mapigo mara kwa mara kama watakavyo.

7Basi watakapokuwa wamemaliza ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika lile shimo lisilo na mwisho atapigana nao vita, atawashinda na kuwaua. 8 Maiti zao zitabaki katika barabara ya mji mkubwa, ambao kwa fumbo unaitwa Sodoma na Misri, ambapo pia Bwana wao alisulibiwa. 9Kwa muda wa siku tatu na nusu, watu wa kila kabila, jamaa, lugha na taifa wataziangalia hizo maiti zao na hawataruhusu wazikwe. 10Watu waishio duniani watazitazama kwa furaha maiti za hao manabii wawili na kushangilia kwa kupeana zawadi kwa sababu hao manabii waliwatesa watu waishio duniani.

11Lakini baada ya zile siku tatu na nusu, pumzi ya uhai kutoka kwa Mungu ikawaingia, nao wakasimama kwa miguu yao na wote waliowaona wakaingiwa na hofu kuu. 12Kisha wale manabii wawili wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, ‘‘Njoni huku juu!’’ Nao wakapaa mbinguni katika wingu, wakati adui zao wakiwa wanawatazama.

13Saa iyo hiyo, kukatokea tetemeko kubwa la nchi na sehemu moja ya kumi ya mji

ikaanguka. Watu elfu saba wakauawa katika tetemeko hilo, nao walionusurika wakaogopa sana, wakamtukuza Mungu wa mbinguni.

14Ole ya pili imekwisha kupita, tazama ole ya tatu inakuja upesi.

### *Tarumbeta Ya Saba*

15 Yule malaika wa saba akaipiga tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa mbinguni iliyosema :

''Ufalme wa ulimwengu umekuwa
ufalme wa Bwana wetu na wa
Kristo wake,
naye atatawala milele na milele.''

16Nao wale wazee ishirini na wanne, waliokuwa wameketi mbele za Mungu, kwenye viti vyao vya enzi wakaanguka kifudifudi wakamwabudu
Mungu, 17wakisema,

''Tunakushukuru, Bwana Mungu Mwenyezi,
uliyeko na uliyekuwako,
kwa kuwa umetwaa uweza Wako mkuu
na ukaanza kutawala.
18Mataifa walikasirika
kwa kuwa wakati wa ghadhabu Yako
umewadia.
Wakati umewadia wa kuwahukumu
waliokufa na kuwapa thawabu
watumishi
wako manabii na watakatifu wako
pamoja
na wale wote wanaoliheshimu Jina Lako,
wakubwa kwa wadogo na
kuwaangamiza
wale wanaoiangamiza dunia.''

19Ndipo Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa na sanduku la agano lake likaonekana humo ndani. Kukatokea mianga ya umeme wa radi, ngurumo, sauti za radi, tetemeko la nchi na mvua kubwa ya mawe.

### *Mwanamke Na Joka*

**12** Kukaonekana ishara kuu mbinguni: Palikuwa na mwanamke aliyevikwa jua na mwezi ukiwa chini ya miguu yake na taji ya nyota kumi na mbili ilikuwa kichwani mwake.
2Alikuwa na mimba naye akilia kwa uchungu
kwa kuwa alikuwa anakaribia kuzaa. 3Kisha
ishara nyingine ikaonekana mbinguni: Likaonekana joka kubwa jekundu lenye vichwa saba na pembe kumi na taji saba katika vichwa
vyake. 4Mkia wake ukakokota theluthi ya nyota zote angani na kuziangusha katika nchi. Ndipo lile joka likasimama mbele ya yule mwanamke aliyekuwa karibu kuzaa ili lipate kumla huyo
mtoto mara tu atakapozaliwa. 5Yule mwanamke
akazaa mtoto mwanamume, atakayeyatawala mataifa yote kwa fimbo yake ya utawala ya chuma. Lakini huyo mtoto akanyakuliwa na kupelekwa kwa Mungu kwenye kiti Chake cha
enzi. 6Yule mwanamke akakimbilia nyikani,
ambako Mungu alikuwa amemtayarishia mahali ili apate kutunzwa huko kwa muda wa siku 1,260.

### *Malaika Mikaeli Amshinda Yule Joka*

7 Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka
pamoja na malaika zake likapigana nao. 8Lakini
joka na malaika zake wakashindwa na hapakuwa tena na nafasi kwa ajili yao mbinguni.
9Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake.

### *Ushindi Mbinguni Watangazwa*

10Kisha nikasikia sauti kuu mbinguni ikisema,

"Sasa Wokovu na uweza na Ufalme wa
Mungu wetu umekuja na mamlaka ya
Kristo wake.
Kwa kuwa ametupwa chini mshtaki wa
ndugu zetu,
anayewashtaki mbele za Mungu
usiku na mchana.
11Nao wakamshinda
kwa damu ya Mwana-Kondoo
na kwa neno la ushuhuda wao.
Wala wao hawakuyapenda maisha
yao hata kufa.
12Kwa hiyo, furahini ninyi mbingu na
wote wakaao humo!
Lakini ole wenu nchi na bahari,
kwa maana huyo Shetani
ameshuka kwenu,
akiwa amejaa ghadhabu, kwa sababu
anajua ya kuwa muda wake ni mfupi!'

13Lile joka lilipoona kuwa limetupwa chini duniani, lilimfuatilia yule mwanamke aliyekuwa
amezaa mtoto mwanamume. 14Lakini huyo
mwanamke akapewa mabawa mawili ya tai

mkubwa, kusudi aweze kuruka mpaka mahali
palipotayarishwa kwa ajili yake huko nyikani,
ambako atatunzwa kwa wakati na nyakati na
nusu wakati [a] ambako yule joka hawezi kufika.
15Ndipo lile joka likamwaga maji kama mto
kutoka kinywani mwake, ili kumfikia huyo
mwanamke na kumkumba kama mafuriko.
16Lakini nchi ikamsaidia huyo mwanamke kwa
kufungua kinywa na kuumeza huo mto ambao
huyo joka alikuwa ameutoa kinywani mwake.
17Kisha lile joka likapatwa na hasira kali kwa ajili
ya huyo mwanamke, likaondoka ili kupigana vita
na watoto waliosalia wa huyo mwanamke,
yaani, wale wanaozitii amri za Mungu na
kuushika ushuhuda wa Yesu Kristo. Lile joka
likasimama kwenye mchanga wa bahari. 18Yule
joka akajikita katika mchanga ulioko ufuoni mwa
bahari.

***Mnyama Kutoka Baharini***

**13** Nami nikamwona mnyama akitoka ndani
ya bahari. Mnyama huyo alikuwa na pembe kumi
na vichwa saba, akiwa na taji
kumi kwenye hizo pembe zake na juu ya kila
kichwa kulikuwa na jina la kukufuru. 2Mnyama
yule niliyemwona alikuwa kama chui, miguu
yake ilikuwa kama ya dubu na kichwa chake
kama cha simba. Lile joka likampa huyo
mnyama nguvu zake, kiti chake cha enzi na
mamlaka makubwa. 3Kimojawapo ya vichwa
vya huyo mnyama kilikuwa kama kilichokwisha
kupata jeraha la mauti, lakini jeraha hilo la mauti
likapona. Ulimwengu wote ukashangaa
ukamfuata huyo mnyama. 4Watu wakaliabudu
lile joka kwa sababu lilikuwa limempa huyo
mnyama mamlaka yake, pia wakamwabudu
huyo mnyama na kuuliza, “Ni nani aliye kama
huyu mnyama? Ni nani awezaye kupigana vita
naye?’’

5Huyo mnyama akapewa kusema maneno
ya kujisifu na kukufuru na kutumia mamlaka
yake kwa muda wa miezi arobaini na miwili.
6Akafungua kinywa chake ili kumkukufuru
Mungu, akilitukana Jina lake na mahali aishipo
na wale wakaao mbinguni. 7Pia akaruhusiwa
kufanya vita na watakatifu na kuwashinda.
Akapewa uwezo juu ya watu wa kila kabila,
jamaa, lugha na taifa. 8Nao watu wote waishio
duniani watamwabudu huyo mnyama, yaani,
wale wote ambao majina yao hayakuandikwa
kwenye kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo
aliyechinjwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu.

9“Yeye aliye na sikio na asikie.

10Ikiwa mtu ni wa kuchukuliwa mateka,
atachukuliwa mateka.
Ikiwa mtu ni wa kuuawa kwa
upanga, atauawa kwa upanga.

Hapa ndipo penye wito kwa ajili ya saburi na
imani ya watakatifu.

***Mnyama Kutoka Katika Dunia***

11Kisha nikamwona mnyama mwingine,
akipanda juu kutoka katika dunia. Alikuwa na
pembe mbili kama mwana-kondoo, lakini
akanena kama joka. 12Akatumia mamlaka yote
ya yule mnyama wa kwanza kwa niaba yake,
naye akawafanya wote wakaao duniani
kumwabudu yule mnyama wa kwanza, ambaye
jeraha lake la mauti lilipona. 13Huyu mnyama
wa pili akafanya ishara kuu na za ajabu, hata
kusababisha moto kushuka toka mbinguni kuja
duniani watu wakiona waziwazi. 14Kwa sababu
ya zile ishara alizokuwa amepewa uwezo wa
kufanya kwa niaba ya yule mnyama wa kwanza,
akawadanganya wakaao duniani. Akawaamuru
wasimamishe sanamu kwa heshima ya yule
mnyama aliyekuwa amejeruhiwa kwa upanga
lakini akaishi. 15 Akapewa uwezo wa kuipa
pumzi ile sanamu ya yule mnyama wa kwanza,
ili iweze kusema na kuwasababisha wale wote
waliokataa kuiabudu hiyo sanamu kuuawa.
16Pia alimlazimisha kila mmoja, mdogo na
mkubwa, tajiri na maskini, mtu huru na mtumwa,
atiwe chapa kwenye mkono wake wa kuume au
kwenye kipaji chake cha uso, 17ili kwamba mtu
ye yote asiweze kununua wala kuuza isipokuwa
amekuwa na hiyo chapa, ambayo ni jina la huyo
mnyama au tarakimu za jina lake.

18Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na
akili na ahesabu tarakimu za huyo mnyama,
kwa maana ni tarakimu za kibinadamu.
Tarakimu zake ni 666.

***Mwana-Kondoo Na Wale 144,000***

**14** Kisha nikatazama na hapo mbele yangu
alikuwepo Mwana-Kondoo, akiwa amesimama
juu ya Mlima Sayuni. Pamoja
naye walikuwa wale watu 144,000 wenye Jina
la Mwana-Kondoo na Jina la Baba Yake likiwa
limeandikwa kwenye vipaji vya nyuso zao.
2Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni kama

---

[a] 14 “Wakati na nyakati na nusu wakati” hapa maana yake ni miaka mitatu na nusu.

sauti ya maji mengi yaendayo kasi na sauti
kama ngurumo ya radi. Sauti hiyo niliyoisikia
ilikuwa kama sauti ya wapiga vinubi wakipiga
vinubi vyao. 3 Nao wakaimba wimbo mpya mbele
ya hicho kiti cha enzi na mbele ya wale viumbe
wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na
wanne. Hakuna mtu ye yote aliyeweza kujifunza
wimbo huo isipokuwa hao watu 144,000
waliokuwa wamekombolewa kutoka duniani.
4 Hawa ndio wale ambao hawakujitia unajisi kwa
wanawake, kwa kuwa wao ni mabikira. Wao
humfuata Mwana -Kondoo kila aendako. Hawa
wamekombolewa kutoka miongoni mwa
wanadamu wakawa malimbuko kwa Mungu na
kwa Mwana-Kondoo. 5 Vinywani mwao
hapakuonekana uongo, wala hawakuwa na
hatia yo yote.

### *Malaika Watatu*

6 Kisha nikamwona malaika mwingine
akiruka juu angani, naye alikuwa na Injili ya
milele ya kuwatangazia wale waishio duniani,
yaani, kwa kila taifa, kabila, lugha na jamaa.
7 Akasema kwa sauti kubwa, ‘‘Mcheni Mungu na
kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake
imewadia. Mwabuduni Yeye aliyeziumba
mbingu, dunia, bahari na chemchemi za maji.’’

8 Malaika wa pili akafuata akisema,
“Ameanguka! Ameanguka Babeli aliye mkuu,
yeye aliyeyafanya mataifa yote kulewa kwa
mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake.’’

9 Malaika wa tatu akawafuata hao wawili
akisema kwa sauti kubwa, “Kama mtu ye yote
anamwabudu huyo mnyama na sanamu yake
na kutiwa chapa yake kwenye kipaji chake cha
uso au kwenye mkono wake, 10 yeye naye,
atakunywa mvinyo wa hasira kali ya Mungu
ambayo imemiminwa katika kikombe cha
ghadhabu yake pasipo kuchanganywa na maji.
Naye atateswa kwa moto uwakao na kiberiti
mbele ya malaika watakatifu na mbele za
Mwana-Kondoo. 11 Nao Moshi wa mateso yao
hupanda juu milele na milele. Hakuna
mapumziko, mchana wala usiku, kwa wale
wamwabuduo huyo mnyama na sanamu yake,
au kwa ye yote anayepokea chapa ya jina lake.’’
12 Hapa ndipo penye subira na uvumilivu wa
watakatifu, yaani, wale wanaozishika amri za
Mungu na kudumu kuwa waaminifu kwa Yesu.

13 Kisha nikasikia sauti kutoka mbinguni
ikisema, “Andika: Wamebarikiwa wale wafao
katika Bwana tangu sasa.”

“Naam,’’ asema Roho, “watapumzika kutoka
katika taabu zao, kwa kuwa matendo yao
yatawafuata.’’

### *Kuvuna Mavuno Ya Dunia*

14 Nikatazama, hapo mbele yangu palikuwa
na wingu jeupe na aliyekuwa ameketi juu ya hilo
wingu alikuwa kama Mwana wa Adamu,
mwenye taji ya dhahabu kichwani mwake na
mundu mkali mkononi mwake. 15 Kisha malaika
mwingine akaja kutoka Hekaluni naye akamwita
kwa sauti kubwa yule aliyekuwa ameketi juu ya
lile wingu akasema, “Chukua mundu wako
ukavune kwa kuwa wakati wa mavuno
umewadia, kwa maana mavuno ya dunia
yamekomaa.’’ 16 Hivyo yule aliyekuwa ameketi
juu ya lile wingu akauzungusha mundu wake
duniani, nayo dunia ikavunwa.

17 Malaika mwingine akatoka katika Hekalu
lililoko mbinguni, naye pia alikuwa na mundu
mkali.

18 Kisha malaika mwingine, aliyekuwa na
mamlaka juu ya moto, akatoka kwenye
madhabahu, naye akamwita yule malaika
mwenye mundu mkali kwa sauti kubwa,
akisema, “Chukua mundu wako mkali
ukakusanye vichala vya mizabibu ya dunia,
maana zabibu zake zimeiva.’’ 19 Hivyo yule
malaika akauzungusha mundu wake duniani na
kukusanya vichala vya zabibu za dunia na
kuzitupa kwenye shinikizo kubwa la ghadhabu
ya Mungu. 20 Lile shinikizo likakanyagwa nje ya
mji, nayo damu ikatiririka kama mafuriko kutoka
katika hilo shinikizo kufikia kimo cha hatamu za
farasi[a], kwa umbali wa maili mia mbili.[b]

### *Malaika Saba Na Mapigo Saba*

15 Ndipo nikaona ishara nyingine kubwa
ya ajabu mbinguni, malaika saba
wenye yale mapigo saba ya mwisho, kwa
sababu kwa mapigo hayo ghadhabu ya Mungu
ilikuwa imekamilika. 2 Nikaona kile
kilichoonekana kama bahari ya kioo
iliyochanganyikana na moto. Kando ya hiyo
bahari, walikuwa wamesimama wale watu
waliomshinda yule mnyama na sanamu yake
pamoja na tarakimu ya jina lake. Mikononi
mwao walikuwa wameshika vinubi walivyopewa
na Mungu. 3 Nao wakaimba wimbo wa Mose,
mtumishi wa Mungu na wimbo wa Mwana-
Kondoo wakisema:

---

a20 Kimo cha hatamu za farasi hapa ni kama mita moja na nusu (1.5m)

b20 Maili 200 hapa ni sawa na kilomita 320

"Bwana Mungu Mwenyezi, matendo Yako ni
makuu na ya ajabu Mfalme wa zamani
zote,
njia Zako Wewe ni za haki na za kweli!
4Ni nani ambaye hatakuogopa Wewe Bwana na
kulitukuza Jina Lako?
Kwa kuwa Wewe peke yako ndiwe
mtakatifu.
Mataifa yote yatakuja na kuabudu mbele
zako,
kwa kuwa matendo yako ya haki
yamedhihirishwa.''

5Baada ya haya nikatazama, nalo hekalu la
hema la ushuhuda lilikuwa limefunguliwa
mbinguni, 6ndani ya lile hekalu wakatoka
malaika saba wakiwa na mapigo saba.
Walikuwa wamevaa nguo safi za kitani ing'aayo
na kufungwa mikanda ya dhahabu vifuani
mwao. 7Ndipo mmoja wa wale wenye uhai
wanne akawapa wale malaika saba mabakuli
saba ya dhahabu yaliyojaa ghadhabu ya Mungu,
Yeye aishiye milele na milele. 8 Nalo lile hekalu
lilijawa na moshi uliotokana na utukufu wa
Mungu na uweza wake, wala hakuna ye yote
aliyeweza kuingia mle hekaluni mpaka yale
mapigo saba ya wale malaika saba
yalipomalizika.

### *Mabakuli Saba Ya Ghadhabu Ya Mungu*

**16** Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka mle hekaluni
ikiwaambia wale malaika saba, "Nendeni,
mkayamwage duniani hayo
mabakuli saba ya ghadhabu ya Mungu.''
2Malaika wa kwanza akaenda akalimwaga
hilo bakuli lake juu ya nchi. Majipu mabaya
yenye maumivu makali yakawapata wale watu
wote waliokuwa na chapa ya yule mnyama na
kuiabudu sanamu yake.
3Malaika wa pili akalimwaga bakuli lake
baharini, nayo ikabadilika kuwa damu kama ya
mtu aliyekufa na kila kiumbe hai kilichokuwa
ndani ya bahari kikafa.
4Malaika wa tatu akalimwaga bakuli lake
katika mito na chemchemi za maji, nazo zikawa
damu. 5Ndipo nikamsikia malaika msimamizi wa
maji akisema,

"Wewe una haki katika hukumu hizi
ulizotoa,
wewe uliyeko, uliyekuwako, uliye
Mtakatifu,
kwa sababu umehukumu hivyo,
6kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu
Wako na manabii Wako,
nawe umewapa damu wanywe
kama walivyostahili.''
7Nikasikia madhabahu ikiitikia,

"Naam, Bwana Mungu Mwenyezi,
hukumu Zako ni kweli na haki."

8Malaika wa nne akamimina bakuli lake
kwenye jua, nalo likapewa nguvu za
kuwaunguza watu kwa moto. 9Watu
wakaunguzwa na hilo joto kali, lakini wakalaani
Jina la Mungu, aliyekuwa na uwezo juu ya
mapigo haya, wala hawakutubu na kumtukuza
Mungu.
10Malaika wa tano akamimina bakuli lake
kwenye kiti cha enzi cha yule mnyama, nao
ufalme wake ukagubikwa na giza. Watu
wakatafuna ndimi zao kwa ajili ya maumivu
11wakamlaani Mungu wa mbinguni kwa sababu
ya maumivu na majeraha yao, wala hawakutubu
kwa ajili ya matendo yao maovu.
12Malaika wa sita akamimina bakuli lake
kwenye mto mkubwa Eufrati, maji yake
yakakauka ili kutayarisha njia kwa ajili ya
wafalme watokao mashariki. 13Kisha nikaona
roho wachafu watatu waliofanana na vyura
wakitoka katika kinywa cha lile joka na katika
kinywa cha yule mnyama na katika kinywa cha
yule nabii wa uongo. 14Hizo ndizo roho za pepo
wachafu zitendazo miujiza. Nazo huwaendea
wafalme wa ulimwengu wote na kuwakusanya
tayari kwa ajili ya vita katika siku ile kuu ya
Mungu Mwenyezi.
15"Tazama, naja kama mwivi! Amebarikiwa
yeye akeshaye na kuziweka tayari nguo zake ili
asiende uchi na kuoenekana aibu yake".
16Ndipo wakawakusanya wafalme pamoja
mahali paitwapo "Armagedoni"[a] kwa Kiebrania.
17Malaika wa saba akamimina bakuli lake
angani na sauti kubwa ikatoka mle hekaluni
katika kile kiti cha enzi, ikisema, ''Imekwisha
kuwa!'' 18Kukawa na mianga ya umeme wa
radi, ngurumo, radi na tetemeko kubwa la ardhi.
Hapajawa kamwe na tetemeko la ardhi kama
hilo tangu mwanadamu awepo duniani, hivyo
lilikuwa tetemeko kubwa ajabu. 19Ule mji
mkubwa ukagawanyika katika sehemu tatu,
nayo miji ya mataifa ikaanguka. Mungu

[a] 16 Armagedoni au Har-magedoni hapa ina maana mlima Magido mahali pa kinabii ambapo wafalme wote wa dunia watakusanyika kwa vita katika siku ya Mungu Mwenyezi.

akaukumbuka Babeli ule uliokuwa mkuu na kuupa kikombe cha hasira na ghadhabu Yake.
20Kila kisiwa kikatoweka wala milima haikuonekana. 21Mvua kubwa ya mawe, mawe yenye uzito wa talanta moja[b] yakaanguka kutoka mbinguni, yakawaangukia wanadamu. Nao wanadamu wakamlaani Mungu kwa ajili ya hayo mapigo ya mvua ya mawe, kwa sababu pigo hilo lilikuwa la kutisha.

### *Kahaba Mkuu Na Mnyama*

**17** Mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na yale mabakuli saba akaja akaniambia, ‘‘Njoo, nitakuonyesha adhabu ya yule kahaba mkuu, aketiye juu ya maji mengi. 2Yule ambaye wafalme wa dunia walizini naye na watu wakaao duniani walilewa kwa mvinyo wa uzinzi wake.’’

3Kisha yule malaika akanichukua katika Roho akanipeleka nyikani. Huko nikamwona mwanamke mmoja ameketi juu ya mnyama mwekundu aliyejaa majina ya kumkufuru Mungu mwili mzima. Mnyama huyo alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. 4Huyo mwanamke alikuwa amevaa mavazi ya rangi ya zambarau na nyekundu, akimetameta kwa dhahabu, vito vya thamani na lulu. Mkononi mwake alikuwa ameshika kikombe cha dhahabu kilichojaa mambo ya machukizo na uchafu wa uzinzi wake. 5Kwenye kipaji chake cha uso palikuwa pameandikwa jina:

“SIRI,
BABELI MKUU,
MAMA WA MAKAHABA
NA MACHUKIZO YA DUNIA.’’

6Nikaona kuwa huyo mwanamke alikuwa amelewa kwa damu ya watakatifu, yaani, damu ya wale watu waliouawa kwa ushuhuda wa Yesu.

Nilipomwona huyo mwanamke, nilistaajabu sana. 7Ndipo yule malaika akaniambia, ‘‘Kwa nini unastaajabu? Nitakufafanulia siri ya huyo mwanamke na huyo mnyama aliyempanda, mwenye vichwa saba na pembe kumi. 8Huyo mnyama, ambaye ulimwona, wakati fulani alikuwepo, lakini sasa hayupo, naye atapanda kutoka katika lile shimo lisilo na mwisho na kwenda kwenye maangamizo. Watu waishio duniani ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha uzima tangu kuumbwa kwa ulimwengu watastaajabu kumwona huyo mnyama, kwa maana alikuwepo, wakati fulani na sasa hayupo, lakini atakuja.

9‘‘Hapa ndipo penye akili pamoja na hekima. Vile vichwa saba ni vilima saba ambavyo huyo mwanamke amevikalia. 10Pia hivyo vichwa saba ni wafalme saba ambao miongoni mwao watano wamekwisha kuanguka, mwingine hajaja bado, lakini atakapokuja, atalazimika kukaa kwa muda mfupi. 11Yule mnyama aliyekuwepo wakati fulani na ambaye sasa hayupo, yeye ni mfalme wa nane. Ni miongoni mwa wale saba, naye anakwenda kwenye maangamizi.

12‘‘Zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi ambao bado hawajapokea ufalme, lakini ambao watapokea mamlaka kuwa wafalme kwa wakati mmoja pamoja na yule mnyama. 13Hawa wana nia moja, nao watamwachia yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao. 14Watafanya vita na Mwana-Kondoo, lakini Mwana-Kondoo atawashinda kwa sababu Yeye ni Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme. Yeye atakuwa pamoja na watu wake walioitwa ambao ni wateule wake na wafuasi wake waaminifu.’’

15Kisha yule malaika akaniambia, ‘‘Yale maji uliyoyaona, yule kahaba akiwa ameketi juu yake ni jamaa za watu, makutano, mataifa na lugha. 16Zile pembe kumi ulizoziona, pamoja na huyo mnyama, watamchukia huyo kahaba, watamfilisi na kumwacha uchi, watamla nyama yake na kumteketeza kwa moto. 17Kwa maana Mungu ataweka mioyoni mwao kutimiza kusudi lake kwa kukubali kumpa yule mnyama mamlaka yao ya utawala mpaka maneno ya Mungu yatakapotimia. 18Yule mwanamke uliyemwona ni ule mji mkubwa unaotawala juu ya wafalme wa dunia.’’

### *Kuanguka Kwa Babeli*

**18** Baada ya haya nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, akiwa na mamlaka makuu na dunia ikamulikiwa na mng’ao wake. 2Naye akalia kwa nguvu kwa sauti kubwa, akisema:

‘‘Umeanguka! Umeanguka Babeli
ulio mkuu!
Umekuwa makao ya mashetani
na makazi ya kila pepo mchafu,
makazi ya kila ndege na kila
mnyama achukizaye.

3Kwa maana mataifa yote yamekunywa mvinyo

[b]21 Talanta moja ni kama kilo 34

wa uasherati wake,
nao wafalme wa dunia wamefanya uzinzi
naye,
nao wafanyi biashara wa
dunia wametajirika
kutokana na wingi wa utajiri wake.''

4Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka
mbinguni ikisema:

"Tokeni katikati yake, enyi watu wangu,
ili msije mkashiriki dhambi zake,
ili usije ukapatwa na pigo lake lo lote,
5kwa kuwa dhambi zake zimelundikana hadi
mbinguni,
naye Mungu ameukumbuka uhalifu wake.
6Mtendee kama yeye alivyotenda,
umlipe mara mbili kwa ajili ya yale
aliyotenda.
Katika kikombe chake mchanganyie mara
mbili ya kile alichochanganya.
7Mpatie mateso na huzuni nyingi sawa
na utukufu na anasa alizojipatia.
Kwa kuwa moyoni mwake hujivuna
akisema,
'Mimi ninatawala kama malkia,
mimi si mjane wala sitaona huzuni
kamwe.'
8Kwa hiyo mapigo yatampata kwa siku
moja: mauti, maombolezo na njaa.
Naye atateketezwa kwa moto, kwa maana
amhukumuye ni Bwana Mungu
Mwenyezi.

9"Wafalme wa dunia waliozini naye na
kushiriki anasa zake watakapoona moshi wa
kuungua kwake, watamlilia na kumwombolezea.
10Watasimama mbali na kulia kwa hofu
kutokana na mateso yake na kusema:

" 'Ole! Ole Ee mji mkuu,
Ee Babeli mji wenye nguvu!
Hukumu yako imekuja katika saa moja!'

11"Na wafanyi biashara wa duniani wanalia
na kuomboleza kwa sababu hakuna anunuaye
bidhaa zao tena. 12Bidhaa za dhahabu, za
fedha, za vito vya thamani na vya lulu, kitani
safi, nguo za rangi ya zambarau, hariri, nguo
nyekundu, aina zote za miti ya manukato, vifaa
vyote vya pembe za ndovu, vifaa vyote vya miti
yenye thamani kuliko yote, shaba nyeusi, chuma
na marmar, 13mdalasini, vikolezi,
uvumba, manemane, uvumba wenye harufu
nzuri, divai, mafuta ya zeituni, unga mzuri na
ngano, ng'ombe na kondoo, farasi na magari,
watumwa, pia na roho za wanadamu.

14"Watasema, 'Yale matunda ambayo roho
yako iliyatamani yamekoma. Utajiri wako wote
na fahari yako vimetoweka, wala haviwezi
kupatikana tena kamwe!' 15Wale
wafanyibiashara wauzao bidhaa hizo na kupata
utajiri wao kutoka kwake watasimama mbali
naye kwa hofu ya mateso yanayompata.
Watalia na kuomboleza wakipiga kelele
wakisema:

16" 'Ole! Ole, Ee, mji mkubwa,
uliyekuwa umevikwa mavazi ya
kitani safi, ya rangi ya zambarau na
nyekundu,
ukimetameta kwa dhahabu, vito
vya thamani na lulu!
17Katika muda wa saa moja utajiri wote
mkubwa kama huu umeangamia!'

''Kila nahodha, mabaharia wote wasafirio
baharini na wote wafanyao kazi melini
watasimama mbali naye. 18Watakapoona moshi
wa kuungua kwake watalia wakisema, 'Je,
ulipata kuwako mji mkuu kama huu?' 19Nao
watajirushia mavumbi vichwani mwao huku
wakilia na kuomboleza wakisema:

" 'Ole, Ole, Ee mji mkubwa,
mji ambao wote wenye meli baharini
walitajirika kwa kupitia mali zako!
Katika saa moja tu umeangamizwa!
20Furahia uharibifu wake, Ee mbingu!
Furahini ninyi watakatifu na mitume na
manabii!
Kwa kuwa Mungu ameutendea kama
vile ulivyowatendea ninyi.' "

21Kisha malaika mmoja mwenye nguvu
akainua jiwe kubwa kama la kusagia akalitupa
baharini akisema:

"Hivyo ndivyo mji mkubwa Babeli
utakavyotupwa chini
kwa nguvu wala hautaonekana tena.
22Nyimbo za wapiga vinubi na waimbaji, wapiga
filimbi na sauti za wapiga
tarumbeta hazitasikika ndani yako tena.
Ndani yako kamwe hataonekana fundi
mwenye ujuzi wa aina yo yote.

Wala sauti ya jiwe la kusagia
kamwe haitaisikika.
23Mwanga wa taa
hautaangaza tena ndani yako.
Wala sauti ya bwana arusi na bibi arusi
kamwe haitasikiwa ndani yako.
Kwa kuwa wafanyi biashara wako walikuwa
watu maarufu wa dunia
na mataifa yote yalidanganyika kwa
uchawi wako.
24Ndani yako ilionekana damu ya manabii na
ya watakatifu
na watu wote waliouawa duniani.''

***Shangwe Huko Mbinguni***

**19** Baada ya haya nikasikia sauti kama sauti ya umati mkubwa wa watu
mbinguni ikisema kwa nguvu :

"Haleluya!
Wokovu na utukufu na uweza
ni vya Mungu wetu,
2kwa maana hukumu Zake ni za kweli na
za haki.
Amemhukumu yule kahaba mkuu
aliyeuharibu ulimwengu kwa uzinzi
wake.
Mungu amemlipiza kisasi kwa ajili ya damu
ya watumishi wake.''

3Wakasema tena kwa nguvu:

"Haleluya!
Moshi wake huyo kahaba unapanda juu
milele na milele.''

4 Wale wazee ishirini na wanne pamoja na wale viumbe wenye uhai wanne wakaanguka kifudifudi, wakamwabudu Mungu, aliyekuwa ameketi kwenye kile kiti cha enzi. Wakasema kwa sauti kuu:

''Amen! Haleluya!''

5Kisha sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi, ikisema:

''Msifuni Mungu wetu,
ninyi watumishi wake wote,
ninyi nyote mnaomcha,
wadogo kwa wakubwa!''

6Kisha nikasikia sauti kama sauti ya umati mkubwa wa watu, kama sauti ya maji mengi yaendayo kasi na kama ngurumo kubwa ya radi ikisema:

''Haleluya!
Kwa maana Bwana Mungu
wetu Mwenyezi anamiliki.
7Tufurahi, tushangilie
na kumpa utukufu!
Kwa maana arusi ya Mwana-
Kondoo Imewadia,
na bibi arusi wake amejiweka tayari.
8Akapewa kitani safi, nyeupe inayong'aa
ili avae.''

(Hiyo kitani safi inawakilisha matendo ya haki ya watakatifu.)

9Ndipo yule malaika akaniambia, "Andika haya: 'Wamebarikiwa wale walioalikwa kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo !' " Naye akaongeza kusema, "Haya ndiyo maneno ya kweli ya Mungu.''

10Ndipo nikaanguka kifudifudi miguuni pake ili kumwabudu, lakini yeye akaniambia, "Usifanye hivyo! Mimi pia ni mtumishi mwenzako pamoja na ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Mwabudu Mungu! Maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii.''

***Aliyepanda Farasi Mweupe***

11Kisha nikaona mbingu imefunguka na hapo
mbele yangu akiwepo farasi mweupe, ambaye
Yeye aliyempanda huyo farasi aliitwa Mwaminifu
na wa Kweli. Yeye ahukumu kwa haki na
kupigana vita. 12Macho yake ni kama miali ya
moto na juu ya kichwa Chake kuna taji nyingi.
Alikuwa na jina lililoandikwa ambalo hakuna mtu
ye yote anayelijua isipokuwa Yeye mwenyewe. 13
Alikuwa amevaa vazi lililochovywa kwenye damu
na Jina lake ni ''Neno la Mungu.'' 14Majeshi ya
mbinguni walikuwa wakimfuata, wakiwa
wamepanda farasi weupe, hali wamevaa mavazi
ya kitani nzuri, nyeupe safi. 15Kinywani mwake
mlitoka upanga mkali ambao kwa huo
atayaangusha mataifa. Atayatawala kwa ''fimbo
yake ya utawala ya chuma.'' Atalikanyaga
shinikizo la mvinyo wa ghadhabu ya Mungu
Mwenyezi. 16Kwenye vazi lake na paja lake
liliandikwa jina hili:

MFALME WA WAFALME NA BWANA WA
MABWANA.

### *Mnyama Na Majeshi Yake Yashindwa*

17 Nami nikamwona malaika amesimama ndani kwenye jua, akaita ndege wote warukao angani kwa sauti kuu, ‘‘Njoni, kusanyikeni kwa ajili ya karamu kubwa ya Mungu, 18 ili mpate kula nyama ya wafalme na ya majemadari, ya mashujaa, ya farasi na ya wapanda farasi, nyama ya wanadamu wote walio huru na watumwa, wadogo na wakubwa.’’

19 Kisha nikamwona yule mnyama na wafalme wa dunia pamoja na majeshi yao wakiwa wamekusanyika pamoja ili kupigana vita dhidi ya yulealiyempanda huyo farasi mweupe pamoja na jeshi Lake. 20 Lakini yule mnyama akakamatwa pamoja na huyo nabii wa uongo ambaye alikuwa amefanya ishara kwa niaba ya huyo mnyama, ambaye kwa ishara hizi aliwadanganya wale waliopokea chapa ya huyo mnyama na kuiabudu sanamu yake. Hawa wawili wakatupwa wakiwa hai ndani ya ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti. 21 Wale waliosalia waliuawa kwa upanga uliotoka kinywani mwa yule aliyekuwa amempanda huyo farasi mweupe, nao ndege wote wakajishibisha kwa nyama yao.

### *Utawala Wa Miaka Elfu Moja*

**20** Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, akiwa ameshika ufunguo wa lile shimo lisilo na mwisho na mnyororo mkubwa mkononi mwake. 2 Akalishika lile joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ndiye Ibilisi na Shetani, naye akamfunga kwa muda wa miaka 1,000. 3 Akamtupa katika lile shimo lisilo na mwisho, akamfunga humo na kulitia lakiri, ili kumzuia asiendelee kudanganya mataifa mpaka hiyo miaka 1,000 itimie. Baada ya hayo atafunguliwa kwa muda mfupi.

4 Kisha nikaona viti vya enzi vilivyokuwa vimekaliwa na hao waliopewa mamlaka ya kuhukumu. Nami nikaona roho za wale waliokatwa vichwa kwa sababu ya ushuhuda wa Yesu na kwa sababu ya neno la Mungu. Hawakuwa wamemsujudia huyo mnyama wala sanamu yake wala hawakupokea ile chapa yake kwenye vipaji vya nyuso zao au kwenye mikono yao. Wakawa hai na kutawala pamoja na Kristo miaka 1,000. 5 (Wafu waliosalia hawakufufuka mpaka ilipotimia hiyo miaka 1,000.) Huu ndio ufufuo wa kwanza. 6 Wamebarikiwa tena ni watakatifu wale walio na sehemu katika huo ufufuo wa kwanza.Hao mauti ya pili haina nguvu juu yao, bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye kwa muda wa miaka 1,000.

### *Kuhukumiwa Kwa Shetani*

7 Hiyo miaka 1,000 itakapotimia, Shetani atafunguliwa kutoka kifungoni mwake, 8 naye atatoka ili kuyadanganya mataifa yaliyopo katika pembe nne za dunia, yaani, Gogu na Magogu apate kuwakusanya tayari kwa vita. Idadi yao ni kama mchanga ulioko Pwani. 9 Nao walitembea katika eneo lote la dunia, wakaizunguka kambi ya watakatifu na ule mji uliopendwa. Lakini moto ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza. 10 Naye Ibilisi aliyewadanganya akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti alipo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao wakateswa huko mchana na usiku, milele na milele.

### *Wafu Wanahukumiwa*

11 Kisha nikaona kiti kikubwa cha enzi cheupe, dunia na mbingu zikaukimbia uso wake Yeye aliyeketi juu yake, wala mahali pao hapakuonekana. 12 Nami nikawaona wafu wakubwa na wadogo, wakiwa wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi na vitabu vikafunguliwa. Pia kitabu kingine kikafunguliwa ambacho ni cha uzima. Hao wafu wakahukumiwa sawasawa na matendo yao kama yaliyoandikwa ndani ya hivyo vitabu. 13 Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake, nayo mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Kila mtu akahukumiwa kulingana na yale aliyotenda. 14 Kisha Mauti na Kuzimu zikatupwa katika ziwa la moto. Hii ndio Mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. 15 Iwapo mtu jina lake halikuonekana katika kile kitabu cha uzima, alitupwa ndani ya lile ziwa la moto.

### *Mbingu Mpya Na Nchi Mpya*

**21** Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya, maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapakuwepo na bahari tena. 2 Nikaona Mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa umeandaliwa kama bibi arusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. 3 Nami nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, ‘‘Tazama, makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe

atakuwa pamoja nao. 4Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita.''

5Naye yule aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi akasema, ''Tazama, nayafanya mambo yote kuwa mapya.'' Pia akasema, "Andika haya, maana maneno haya ni ya kuaminika tena ni kweli.''

6Akaniambia, "Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Yeye aonaye kiu nitampa kunywa kutoka katika chemchemi ya maji ya uzima bila gharama yo yote. 7Yeye atakayeshinda atayarithi haya yote, Nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. 8Lakini waoga, wasioamini, wachafu, wauaji, wazinzi, wachawi, waabudu sanamu, pamoja na waongo wote, mahali pao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.''

9Kisha mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na yale mabakuli saba ya hayo mapigo saba ya mwisho akaja akaniambia, ''Njoo, nami nitakuonyesha bibi arusi, yaani, mke wa Mwana-Kondoo.'' 10Naye akanichukua katika Roho hadi kwenye mlima mkubwa na mrefu, akanionyesha ule Mji Mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu. 11Ulikuwa uking'aa kwa utukufu wa Mungu kama kito chenye thamani sana, kama yaspi, safi kama kioo. 12Ulikuwa na ukuta mkubwa, mrefu wenye malango kumi na mawili, pakiwa na malaika kumi na wawili kwenye hayo malango. Kwenye malango hayo yaliandikwa majina ya yale makabila kumi na mawili ya Israeli. 13Kulikuwa na malango matatu upande wa mashariki, matatu upande wa kaskazini, matatu upande wa kusini na matatu upande wa magharibi. 14Ukuta wa huo mji ulikuwa na misingi kumi na miwili na juu yake yaliandikwa majina ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana-Kondoo.

15Huyo malaika aliyesema nami alikuwa na ufito wa dhahabu wa kupimia huo mji, malango yake na kuta zake. 16Mji huo ulikuwa mraba, urefu wake ulikuwa sawa na upana. Akaupima huo mji kwa huo ufito akaukuta una kama kilometa 2,400[a] urefu wake na upana wake na kwenda juu kwake vilikuwa sawa. 17Akaupima ukuta wake, ulikuwa na unene wa dhiraa 144[b] kwa kipimo cha kibinadamu ambacho huyo malaika alikuwa akikitumia. 18Ukuta huo ulijengwa kwa yaspi hali mji wenyewe ulijengwa kwa dhahabu safi, iking'aa kama kioo. 19Misingi ya mji huo ilipambwa kwa kila aina ya kito cha thamani. Msingi wa kwanza ulikuwa wa yaspi, wa pili yakuti samawi, wa tatu kalkedoni, wa nne zamaridi, 20wa tano sardoniki, wa sita akiki, wa saba krisolitho, wa nane zabarajadi, wa tisa yakuti manjano, wa kumi krisopraso, wa kumi na moja hiakintho, wa kumi na mbili amethisto. 21Yale malango kumi na mbili yalikuwa ni lulu kumi na mbili, kila lango lilikuwa limetengenezwa kwa lulu moja. Barabara za mji huo zilikuwa za dhahabu safi ing'aayo kama kioo.

22Sikuona Hekalu ndani ya huo mji kwa sababu Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo ndio Hekalu lake. 23Ule mji hauhitaji jua wala mwezi kuuangazia kwa sababu utukufu wa Mungu ndio nuru yake na Mwana-Kondoo ndiye taa yake. 24Mataifa yatatembea yakiangaziwa na nuru yake na wafalme wa duniani wataleta fahari yao ndani yake. 25Malango yake hayatafungwa kamwe mchana, kwa maana hakutakuwa na usiku humo. 26 Utukufu na heshima za mataifa zitaletwa humo. 27Lakini kitu kichafu hakitaingia humo kamwe, wala mtu ye yote atendaye mambo ya aibu au ya udanganyifu. Bali watakaoingia humo ni wale tu ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.

### *Mto Wa Maji Ya Uzima*

**22** Kisha yule malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima, maangavu kama kioo yakitiririka kutoka kwenye kile kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo, 2kupitia katikati ya barabara kuu ya huo mji. Kwenye kila upande wa huo mto kulikuwa na mti wa uzima utoao matunda ya aina kumi na mbili, ukizaa matunda yake kila mwezi. Nayo majani ya mti huo ni kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. 3Katika mji huo hakutakuwa tena na kitu cho chote kilicholaaniwa, bali kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo humo na watumishi wake watamtumikia, 4nao watamwona uso Wake na Jina lake litakuwa kwenye vipaji vya nyuso zao. 5Usiku hautakuwako tena, wala hawatahitaji mwanga wa taa au wa jua, kwa maana Bwana Mungu atakuwa nuru yao, nao watatawala milele na milele.

---

[a]16 Kilomita 2,400 hapa ni sawa na maili 1,500

[b]17 Dhiraa 144 ni sawa na mita 64.8 yaani karibu Km. 65.

6 Kisha yule malaika akaniambia, "Maneno haya ni ya kuaminika na kweli. Bwana, Mungu wa roho za manabii, amemtuma malaika wake kuwaonyesha watumishi wake yale ambayo hayana budi kutukia upesi.

***Bwana Yesu Anakuja***

7"Tazama, naja upesi! Amebarikiwa yeye ayashikaye maneno ya unabii wa kitabu hiki."

8Mimi Yohana, ndiye niliyesikia na kuyaona mambo haya. Nami nilipokwisha kuyasikia na kuyaona, nilianguka chini nikasujudu miguuni pa yule malaika aliyekuwa akinionyesha mambo
hayo. 9Lakini yeye akaniambia, "Usifanye hivyo! Mimi ni mtumishi pamoja nawe na ndugu zako manabii na wote wanaoyashika maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu!"

10Kisha akaniambia, "Usiyafunge maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu hiki, kwa
sababu wakati umekaribia. 11Atendaye mabaya na aendelee kutenda mabaya, aliye mchafu na aendelee kuwa mchafu, yeye atendaye haki na aendelee kutenda haki na yeye aliye mtakatifu na aendelee kuwa mtakatifu."

12"Tazama, naja upesi! nikiwa na mshahara wangu, nami nitamlipa kila mtu sawasawa na
alivyotenda. 13Mimi ni Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho, Mwanzo na Mwisho.

14"Wamebarikiwa wale wafuao nguo zao, ili wapate haki ya kuuendea huo mti wa uzima na kuuingia huo mji kwa kupitia kwenye malango
yake. 15Huko nje wako mbwa, wachawi, wazinzi, wauaji, waabuduo sanamu na kila mtu apendaye udanganyifu na kuufanya.

16"Mimi Yesu, nimemtuma malaika wangu kushuhudia mambo haya kwa ajili ya makanisa. Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya asubuhi ing'aayo."

17 Roho na bibi arusi wanasema, "Njoo!" Naye asikiaye na aseme, "Njoo!" Ye yote mwenye kiu na aje na kila anayetaka na anywe maji ya uzima bure.

18Namwonya kila mtu asikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki: Mtu ye yote akiongeza cho chote, Mungu atamwongezea mapigo
yaliyoandikwa katika kitabu hiki. 19Kama mtu ye yote akipunguza cho chote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.

20Yeye anayeshuhudia mambo haya asema, "Naam, naja upesi!"

Amen. Njoo Bwana Yesu.

21Neema ya Bwana Yesu iwe na watakatifu wote. Amen.